# KITABU CHA TAARIFA ZA WIZARA KWENYE MIKUTANO YA SERIKALI NA WAANDISHI WA HABARI KUADHIMISHA MIAKA 60 YA UHURU: TULIPOTOKA, TULIPO NA TUNAPOELEKEA - 1961-2021

2021

MIAKA 60
YA UHURU
**1961-2021**

Disemba, 2021. maelezo.go.tz

1961-2021

MIAKA 60 YA UHURU;
Tanzania imara, Kazi iendelee.

Idara ya Habari-MAELEZO | maelezo.go.tz

# Utangulizi

Tarehe 9 Disemba 2021 nchi yetu imeadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza uliopatikana Disemba 9 mwaka 1961.

Miongoni mwa shughuli zilizofanywa na Serikali wakati wa kuelekea maadhimisho hayo ni pamoja na mikutano ya Vyombo vya Habari kuelezea maendeleo ya sekta zote kwa kipindi Cha miaka 60 ya Uhuru.

Idara ya Habari - MAELEZO iliratibu mikutano iliyohusisha Wizara zote 23 na Vyombo vya Habari, iliyofanyika Dodoma kuanzia Novemba 2 - 30, 2021.

Mawaziri 20 walishiriki mikutanon hiyo huku Manaibu Waziri wawili na Kamishna wa Nishati waliwawakilisha Mawaziri wao katika kutoa taarifa.

Mikutano yote ilirushwa mubashara (live) kwenye Televisheni na Redio. Waandishi wa Habari na Wapiga Picha takriban 50 kutoka kwenye magazeti, Redio, Televisheni na mitandao ya kijamii walialikwa na kushiriki mikutano hiyo. Wizara zilipata fursa ya kuwasilisha taarifa zao na baada ya zoezi hilo waandishi wa Habari walipewa nafasi ya kuuliza maswali na kujibiwa.

Tathmini inaonyesha nchi yetu imepiga hatua kubwa ya maendeleo kwenye sekta zote ukilinganisha na tulipokuwa wakati tunapata Uhuru. Hii imejidhihirisha kwenye taarifa za Wizara zilizoelezea sekta zilipotoka yaani historia ya maendeleo ya sekta hizo, tulipo na tunapoelekea.

Idara ya Habari - MAELEZO imechapisha taarifa hizo zilizoandaliwa na Wizara zote kwa lengo la kuweka kumbukumbu ya historia ya maendeleo ya nchi yetu kwa ajili ya faida ya vizazi vya sasa na baadaye.

Hivyo, nawakaribisha kusoma kitabu hiki cha taarifa za Wizara zote zinazoelezea tulipotoka, tulipo na tunapoelekea wakati tunaadhimisha miaka 60 ya nchi yetu.

Gerson Msigwa
Mkurugenzi
Idara ya Habari-MAELEZO

## Yaliyomo


001 **Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

006 **Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji)**

018 **Wizara ya Madini**

024 **Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

038 **Wizara ya Nishati**

045 **Wizara ya Maji**

050 **Wizara ya Fedha na Mipango**

054 **Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi**

064 **Wizara Utamaduni, Sanaa na Michezo**

070 **Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)**

076 **Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

081 **Wizara ya Viwanda na Biashara**


## Yaliyomo


097 **Wizara ya Katiba na Sheria**

108 **Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

117 **Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

122 **Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)**

133 **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

140 **Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

151 **Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

164 **Wizara ya Kilimo**

175 **Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

182 **Wizara ya Maliasili na Utalii**

189 **Ofisi ya Rais - TAMISEMI**







# MAFANIKIO YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KATIKA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

Ndugu wanahabari, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuwezesha kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Pia napenda kuchukua fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake kwa nchi hii ambayo ameijalia tunu za amani, utulivu, mshikamano, umoja na mtangamano katika kipindi chote cha miaka 60 ya Uhuru wa nchi yetu. Tunu hizo zimetuwezesha kuendelea na shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa na pia kutoa fursa kwa wananchi kuweza kujifanyia shughuli zao za maendeleo.

Ndugu wanahabari, Ofisi yangu inatambua mchango wenu katika kuwaelimisha na kuwafikishia wananchi taarifa muhimu zinazohusu masuala ya kiutumishi na utawala bora ili umma wa Watanzania uweze kuhabarishwa. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa mchango wenu huu mkubwa kwa Taifa.

Ndugu wanahabari, kama tunavyofahamu sasa hivi tuko katika kipindi cha maandalizi ya kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara itakapofika tarehe 9 Desemba, 2021. Sote tunafahamu kuwa katika kipindi hicho cha miaka 60 ya Uhuru, Utumishi wa Umma umeendelea kuwa uliotukuka katika kuchangia ustawi wa Taifa.

Ndugu wanahabari, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni moja ya Ofisi mtambuka katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Utawala wa Utumishi wa Umma na usimamizi wa rasilimaliwatu pamoja na taratibu za uendeshaji wa Utumishi wa Umma. Kutokana na umuhimu wa rasilimawatu katika maendeleo ya nchi, majukumu ya Ofisi hii yamekuwepo toka tulipopata uhuru mpaka sasa.

Ndugu wanahabari, wakati Tanganyika (Tanzania Bara) ikipata uhuru mwaka 1961, ilirithi Utumishi wa Umma ambao jukumu lake kubwa lilikuwa ni kuihudumia Serikali ya kikoloni na kulinda masilahi yake. Katika kipindi hicho, nchi yetu ilikuwa inakabiliwa na upungufu wa watumishi wazawa wenye sifa na taaluma mbalimbali za kuwawezesha kutekeleza majukumu ya taasisi mpya zilizoanzishwa. Pia hawakuwepo watumishi wazawa wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi na maafisa wa kikoloni ambao walilazimika kuacha kazi baada ya uhuru. Changomoto nyingine ni kuwepo kwa mifumo ya utawala na mitizamo ya Watumishi ya kikoloni, na huduma nyingi za kijamii kama vile afya, makazi bora, barabara na elimu zilielekezwa katika maeneo waliyokuwa wakiishi wakoloni. Mwelekeo na mtazamo wa Utumishi huo ulichangia kusababisha changamoto kubwa tatu ambazo ni ujinga, umaskini na maradhi miongoni mwa wananchi.

Ndugu Wanahabari, Hatuwezi kutambua na kuthamini hatua kubwa tuliyopiga kama Taifa katika kujijengea uwezo wetu wa kukabiliana na changamoto mbalimbali kwa kuendeleza taaluma mbalimbali ndani ya miaka 60 bila kujua tulikotoka. Wengi wetu hatujui kwamba, Tanganyika ilipopata Uhuru, tulikuwa na Madaktari 12 tu nchi nzima na Wahandisi wawili, wakati asilimia 85 ya wananchi walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Ndani ya miaka 60 hatujafika tunakotaka kufika, lakini tumepiga hatua kubwa sana kwenye nyanja zote za kujenga nguvu kazi.

Ndugu wanahabari, Hata Mwalimu Nyerere aliulizwa na Benki ya Dunia alipowatembelea baada ya kustaafu, How did he fail? Na jibu la Mwalimu Nyerere ni jibu fikirishi kwetu sote kwa tulikotoka kama Taifa.

**“Why have you failed?”** The World Bank Experts asked him, Nyerere answered: “The British Empire left us a country with 85 percent illiterates, two Engineers and 12 Doctors. When I left office, we had 9 percent illiterates and thousands of Engineers and Doctors. I left office 13 years ago. Then our income per capita was twice what it is today; now we have one-third less children in our schools and public health and social services are in ruins. During these 13 years, Tanzania has done everything that the World Bank and the International Monetary Fund have demanded.” And Nyerere passed the question back to the World Bank Experts; **“Why you have failed?”**

Ndugu wanahabari, Katika kukabiliana na changamoto hizo za ujinga, umaskini na maradhi zilizotokana na mfumo wa utawala wa kikoloni, ajenda kubwa ya Serikali huru ya Tanganyika ilikuwa ni kujenga Utumishi wa Umma utakaoshughulikia changamoto hizo kwa kufanyia kazi ongezeko la majukumu ya Serikali kutokana na mfumo mpya ya kiutawala.

Ndugu wanahabari, tangu nchi yetu ipate uhuru, historia inabainisha uwepo wa vipindi mbalimbali ambavyo vimekuwa na uhitaji tofauti wa namna ya uendeshaji wa Serikali, sambamba na utatuzi wa changamoto za usimamizi wa Utumishi wa Serikali kuu na baadaye utumishi wa umma.

Kipindi kinachoanzia mwaka 1961 hadi mwaka 1990, nchi yetu imechukua hatua mbalimbali ili kujenga Utumishi wa Umma imara ambao unalenga kuwatumikia wananchi na kuwaletea maendeleo na kuwezesha kuendesha nchi kama Taifa huru. Hatua zilizochuliwa ni pamoja na: kutekeleza Sera ya Wazawa mwaka 1961, kuandaa mipango ya rasilimaliwatu mwaka 1963, kuanzisha Jeshi la Kujenga Taifa mwaka 1963, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, kuanzisha mfumo wa chama kimoja cha siasa mwaka 1965, Azimio la Arusha mwaka 1967 ambalo pamoja na masuala mengine liliweka miiko ya Viongozi, na Madaraka Mikoani mwaka 1972.

Ndugu wanahabari, pamoja na maamuzi yaliyolenga kuleta tija katika uendeshaji wa Serikali, kuimarisha usimamizi wa Watumishi Serikalini, na kuimarisha utoaji huduma za kijamii na kiuchumi, mafanikio yaliyopatikana hayakukidhi matarajio kwa wakati wote. Hiyo ilitokana na changamoto za kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia mwaka 1974, kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, vita vya Kagera mwaka 1978, ongezeko kubwa la watumishi na taasisi za Umma kulikozidi uwezo wa Serikali kujiendesha, watumishi na taasisi za Umma kutoa huduma za kijamii na kiuchumi chini ya viwango, na pia utumishi wa Serikali kushindwa kuendana na kasi ya mageuzi ya kiuchumi na kisiasa.

Ndugu wanahabari, ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kurejeshwa kwa mfumo wa Serikali za Mitaa mwaka 1984, kuanzisha mageuzi ya kiuchumi na soko huria katika miaka ya 1980, kurejesha mfumo wa vyama vingi vya Siasa mwaka 1992 na kutekeleza programu ya Mabadiliko ya Utendaji kazi Serikalini kuanzia mwaka 1991 hadi mwaka 1999.

Ndugu wanahabari, Mabadiliko ya Utendaji kazi Serikalini yalilenga kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali, kupunguza ukubwa wa Serikali ili kuwa na Serikali inayojimudu na kuboresha utoaji huduma kwa Umma. Vile vile katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2014, Serikali ilitekeleza programu mpya ya mabadiliko katika Utumishi wa Umma ambayo ilijikita katika kuweka mifumo ya utendaji kazi katika taasisi za Umma na kujenga utamaduni wa utendaji kazi kwa kutumia mifumo ya kimenejimenti na utendaji kazi ili kuimarisha utoaji huduma wa taasisi za Umma.

Ndugu wanahabari, hatua nyingine zilizochukuliwa ni kuanzisha programu za mabadiliko katika Serikali za Mitaa ambayo ilijikita katika kuimarisha mfumo wa utendaji kazi na utoaji huduma katika Serikali za Mitaa, kufanya marekebisho katika muundo katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kutunga Sheria Na. 10 ya mwaka 1982 inayohusu Utumishi katika Serikali za Mitaa; na Sheria Na. 11 ya mwaka 1982 inayohusu Usuluhishi katika Serikali za Mitaa.

Ndugu wanahabari, Hatua nyingine ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa maadili ya Viongozi kwa kutunga Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa lengo la kuhakikisha nchi inaongozwa na Viongozi waadilifu, wenye kuzingatia misingi ya utu, uhuru, maendeleo, usawa, haki, kufanya kazi kwa bidii, kujitegemea, utaifa, umoja, uzalendo na mshikamano.

Ndugu wanahabari, Serikali katika miaka 60 ya uhuru, imeanzisha na kuimarisha vyombo mbalimbali vya kusimamia menejimenti ya utumishi wa Umma na Utawala Bora ambavyo ni: Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Chuo cha Utumishi wa Umma, Taasisi ya UONGOZI, Wakala ya Ndege za Serikali, Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira, Watumishi Housing, na Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Ndugu wanahabari, sasa naomba kuchukua fursa hii kuelezea mafanikio yaliyopatikana katika miaka 60 tangu uhuru kupitia vyombo na taasisi nilizozitaja. Kwa kweli mafanikio ni mengi sana, lakini kutokana na ufinyu wa muda nitaelezea baadhi kama ifuatavyo: -

a) Kuongezeka kwa ajira katika Utumishi wa Umma kutoka watumishi 17,565 mwaka 1961 hadi 528,290 mwezi Oktoba, 2021. Kati ya hao, watumishi wa sekta ya Afya wamefikia 72,961 sawa na asilimia 13.8 na walimu wamefikia 281,729 sawa na asilimia 53.3;

b) Kuboreshwa kwa Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) na kujengewa uwezo wa Watumishi kutoka Taasisi za Serikali 427 kutumia Mfumo huo. Mfumo huu umesaidia kuingiza watumishi wapya kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara kwa wakati na kuwawezesha kupata mishahara yao ndani ya kipindi cha mwezi mmoja. Mfumo huu umeongeza wigo wa taarifa na watumiaji na hivyo basi kuboresha usimamizi wa masuala ya rasilimaliwatu katika taasisi za Umma;

c) Kuwaondoa kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Payroll) watumishi 15,578 waliobainika kughushi vyeti vya kufaulu mtihani wa Kidato cha Nne, cha Sita na Ualimu kati ya watumishi 535,770 waliohakikiwa. Pia, kuwaondoa katika Orodha ya Malipo ya Mishahara Watumishi 5,335 walioajiriwa katika Utumishi wa Umma kinyume na Sifa za Miundo ya maendeleo ya kiutumishi, hivyo kubakia na watumishi wenye sifa stahiki;

d) Kuwaondoa katika Orodha ya Malipo ya Mishahara watumishi hewa 19,708 na kuiwezesha Serikali kuokoa jumla ya Shilingi Bilioni 19.84;

e) Kuimarika kwa Mfumo wa Kitaasisi wa Usimamizi wa Serikali Mtandao kwa kuanzisha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019 na Kanuni zake za mwaka 2020 zinazoweka utaratibu na masharti ya kisheria kuhusu utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa Serikali Mtandao nchini;

f) Kurahisishwa kwa mawasiliano na upatikanaji wa huduma zitolewazo na Serikali kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Utumishi wa Umma. Vile vile, kuanzisha Vitengo vya Usimamizi wa TEHAMA katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

g) Kurahisisha upatikanaji wa taarifa za ajira kwa kuanzisha kanzidata ya waombaji na waliofaulu usaili ambayo hutumika kuwapangia vituo moja kwa moja wasailiwa waliofaulu usaili hivyo kupunguza gharama za usaili;
h) Kuongezewa uwezo, ujuzi na maarifa Viongozi na watumishi wa Umma kwa kuanzisha Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) na kuimarishwa kwa Chuo cha Utumishi wa Umma;
i) Kuongezeka kwa uwezo na weledi wa watumishi wa Umma na sekta binafsi kupitia Chuo cha Utumishi wa Umma kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu;
j) Kusogeza huduma kwa umma kwa kuanzisha matawi ya Chuo cha Utumishi wa Umma Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga, Mbeya pamoja na kuanzisha Kituo cha Mafunzo kwa njia ya Mtandao;
k) Kuimarika kwa mahusiano kazini kati ya Viongozi na watendaji wengine kupitia mafunzo ya Taasisi ya UONGOZI ambapo yameongeza uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi. Pia, mafunzo hayo yamewaongezea uwezo wa kuchambua changamoto kwa kina, kuzitafutia ufumbuzi na kuboresha usimamizi wa rasilimali za Serikali ikiwa ni pamoja na rasilimaliwatu na rasilimali fedha;
l) Kukusanywa, kuchambuliwa na kutunzwa kwa taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali kuhusu historia ya nchi kwa ajili ya vizazi vijavyo. Vile vile, kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu vilikusanywa na kuhifadhiwa kwa lengo la kuhifadhi historia ya Waasisi wa Taifa letu;
m) Kuhifadhi nyaraka kidijitali ili zidumu, kurahisisha upatikanaji wake, kuwa na hifadhi mbadala na kulinda nakala halisi. Aidha, hadi kufikia mwaka 2021 jumla ya Majalada 2,843 yamehifadhiwa kwenye mfumo wa kidijitali;
n) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya masikini ili kuziwezesha kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu na kujenga rasilimaliwatu hususan watoto kwa kugharamia elimu na huduma za afya, ambapo kiasi cha shilingi Trilioni 1.646 kilitumika katika utekelezaji wa Kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Tatu;
o) Kuanzishwa kwa miradi ya kutoa ajira ya muda kwa walengwa na miradi ya kuendeleza miundombinu ya huduma za jamii. Katika Awamu ya I na II, jumla ya miradi 14,051 ya kutoa huduma za jamii yenye thamani ya shilingi bilioni 502.0 ilitekelezwa kwa kutoa huduma zilizokusudiwa kwa jamii husika katika Sekta mbalimbali;
p) Kuimarika kwa Maadili ya Viongozi wa Umma kutokana na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ikiwa ni pamoja na kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa maadili, kujaza Fomu za Tamko la Mali na Madeni na kufanya uhakiki wa Matamko ya Rasilimali, Maslahi na Madeni ya Viongozi wa Umma. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni kutoa elimu kwa Viongozi wa Umma, Watumishi wa Umma na Wananchi kuhusu maadili ya viongozi wa umma ili kuimarisha utawala bora nchini;
q) Kuimarika kwa nidhamu, uadilifu na uwajibikaji kufuatia mapambano dhidi ya Rushwa katika nyanja mbalimbali zikiwemo za Utumishi wa Umma, biashara, ukusanyaji mapato, matumizi ya madaraka na fedha za umma. Hatua hizo, zimeijengea Serikali msingi imara wa kukuza uchumi na kuongeza kasi ya utoaji huduma za kijamii na kiuchumi kwa wananchi;
r) Kuongezeka kwa wigo na kujenga miundombinu ya kukuza utawala bora, kuzuia na kupambana na rushwa kwa kuanzisha Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji "National Anti-Corruption Strategy and Action Plan" (NACSAP) Awamu ya I hadi ya III;
s) Kuongeza mapato ya Serikali kutokana ununuzi wa ndege 11 za kibiashara ambazo zimekodishwa kwa ATCL na kuchangia upatikanaji wa huduma za usafiri wa anga nchini. Ndege hizo ni tano (5) za masafa mafupi aina ya De havilland Q400-8, ndege nne (4) za masafa ya kati aina ya Airbus A220-300 na ndege mbili aina ya Boeing 787-8 Dreamliner;
t) Kupungua na kutatuliwa kwa migogoro ya ardhi kwa wananchi waliorasimisha maeneo yao, kuongeza usalama wa miliki na uhakika wa miliki za ardhi;
u) Wananchi kuongezewa uwezo wa kiuchumi kwa kuwezeshwa kupata mikopo kwa kutumia Hatimiliki ya ardhi walizorasimisha kama dhamana;
v) Kuimarika kwa usimamizi wa rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma kwa kuwawezesha Watumishi, Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za nidhamu katika Utumishi wa Umma kutekeleza na kusimamia rasilimaliwatu kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake;
w) Kuongezeka kwa uwajibikaji katika eneo la usimamizi wa rasilimaliwatu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo katika usimamizi wa rasilimaliwatu kutokana na ukaguzi wa rasilimaliwatu kwa waajiri;
x) Kuboresha makazi ya watumishi wa Umma kwa kuanzisha kampuni ya Ujenzi na Ushauri kupitia Watumishi Housing kwa kujenga nyumba za bei nafuu ili kupunguza gharama za ujenzi ukilinganisha na bei ya nyumba katika soko; na
y) Kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa umma wanaofanya kazi maeneo yenye mazingira magumu hususan walimu kwa kujenga nyumba katika mikoa 19 yenye mazingira magumu.

Ndugu wanahabari, mafanikio haya katika eneo la Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yanadhihirisha kuwa Awamu zote sita za uongozi, zimefanya kazi kubwa katika kuboresha utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi ili kuwaletea maendeleo watanzania. Hii inadhihirisha kuwa safari na historia ya Utumishi wa Umma uliotukuka ambao ndiyo umekuwa msingi wa ustawi wa Taifa tunaouona sasa na tunu za amani, utulivu, mshikamano, umoja na mtangamano katika kipindi chote cha miaka 60 ya Uhuru wa nchi yetu.

Ndugu wanahabari, kwa niaba ya Ofisi yangu niwashukuru tena kwa ushirikiano wenu ambao mmekuwa mkiutoa pindi tunapowahitaji, na niwahakikishie kuwa Ofisi yangu itaendelea kufanya kazi nanyi bega kwa bega katika masuala ya kiutumishi na utawala Bora ambayo wananchi wana haki ya kupatiwa taarifa.




MAFANIKIO YA OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI) KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

## UTANGULIZI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu ipate Uhuru mwaka 1961 kupitia Awamu ya Kwanza hadi ya Sita ya uongozi imefanya juhudi mbalimbali ili kukuza uwekezaji, maendeleo ya sekta binafsi, ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi pamoja na miradi ya kimkakati na uwekezaji kama inavyoonesha katika sehemu namba 2.0 hadi 6.0. Shabaha kubwa ya uwekezaji imejikita katika kupiga vita umasikini, ujinga na maradhi. Kupitia uwekezaji nchi yetu imeweza kukuza ajira zenye kipato kupanua wigo wa kodi, kukuza teknolojia na kuhamasisha matumizi ya rasilimali zatu.

## 2.0 UWEKEZAJI

Uwekezaji wa mitaji binafsi kutoka nje ni chanzo muhimu cha uwekezaji na umesaidia katika maendeleo ya nchi. Kuhusu uwekezaji miaka takriban 20 baada ya Uhuru, Serikali ilikuwa ndiyo nguzo kuu ya uchumi na Mwekezaji Mkuu kupitia Mashirika ya Umma. Kufuatia mageuzi makubwa ya uchumi yaliyofanyika mwaka 1988, Tanzania imefanya jitihada kubwa kukuza uwekezaji kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia uwekezaji.

### 2.1 Uwekezaji Katika Kipindi cha Mwaka 1961 hadi Mwaka 1996

Baada ya Tanzania kupata Uhuru Mwaka 1961, Sera za Uwekezaji za Tanzania Bara zilihamasisha uwekezaji wa sekta binafsi ikiwa ni ni pamoja na kutunga Sheria ya Kuhamasisha Uwekezaji wa Kutoka Nje ya nchi (Foreign Investment Protection Act) ya Mwaka 1963 hadi ilipofika mwaka 1967 ilipotangaza Azimio la Arusha ambapo Serikali ilisimamia na kuendesha shughuli kuu za uzalishaji na kusababisha mvuto mdogo wa uwekezaji binafsi ikiwemo ule wa kutoka nje. Katika kipindi hicho, ilitaifisha kampuni, biashara na huduma binafsi ikiwemo shule za huduma za afya na kujikita zaidi katika uanzishaji wa mashirika mapya ya umma, ikiwemo Viwanda, mashamba, huduma za kiuchumi na kijamii na kadhalika. Shughuli za uzalishaji zilizotaifishwa ziliendeshwa na Watanzania wenyewe ambapo katika miaka ya awali ilionesha mafanikio lakini baadaye mashirika mengi yalishindwa kujiendesha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mapungufu ya usimamizi.

Katika Kitabu chake cha “Safari ya Maisha Yangu” Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili anaeleza kuwa mfano mmojawapo wa matokeo hasi ya utaifishaji ni kilimo cha mkonge ambacho baada ya utaifishaji na kukabidhiwa kwa Mamlaka ya Mkonge Tanzania baada ya miaka michache kilikumbwa na matatizo ya kiuongozi na menejimenti. Moja ya sababbu waliyotoa watu wetu ikawa uhaba wa wakata mkonge wazoefu kwa vile waliokuwepo walikuwa wanazeeka. Kwa maneno mengine hawakuwa wametambua tatizo hilo mapema na kuandaa vijana wakata mkonge. Lakini mashamba haya yalipokuwa kwenye mikono ya sekta binafsi tatizo hilo halikuwepo. Kwa hiyo tatizo hilo japo ni la kweli, linaashiria upungufu wa uwezo na uzoefu wa kuendesha mashamba hayo kama mashirika ya umma.

Rais Mwinyi anatoa takwimu kuwa, kwa ulinganisho tu, wakati uamuzi wa kuyataifisha haya mashamba unafanywa mwaka 1967, yalikuwa yanazalisha tani 220,000 za katani kwa mwaka na kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji mkubwa wa katani kuliko wote duniani. Kufikia mwaka 1970 tulikuwa tunazalisha tani 202,000, mwaka 1974 tani 174,000 na mwaka 1984 tani 47,000 tu. Baadaye ikaamriwa mashamba 12 yaliyokuwa na hali mbaya zaidi yauzwe kwa watu binafsi na wasipopatikana wanunuzi yagawiwe kwa wananchi. Kwa maneno mengine, hata Mwalimu Nyerere mwenyewe aliona umuhimu wa kubinafsisha baadhi ya mashirika ya umma wakati bado ni Rais wa nchi yetu.

Kutokana na matatizo ya kiuchumi yaliyotokea kati ya miaka ya 1970 hadi miaka ya 1980, Serikali iliamua kurejesha Sera zinazohamasisha uwekezaji binafsi kuanzia Mwaka 1986. Tija halisi ya uwekezaji (Net Investment Productivity) iliyofikia asilimia 48.6 miaka ya 1996 – 1970 ikaanza kushuka na kuwa asilimia 31.6 (1971 – 1975), 1.8 (1976 – 1980) na 18.4 (1981 – 1983). Baadhi ya sababu ya kushuka huko kwa tija ilikuwa uhaba wa fedha za kigeni na matumizi haba ya uwezo wa uzalishaji (low capacity utilisation) hasa kuanzia katikati ya miaka ya 1970. Vipo Viwanda vipya vilivyowahi kujengwa ambavyo havikuzalisha kabisa, au vilivhelewa sana kuanza kuzalisha na hatimaye pia vikazalisha chini ya kiwango cha uwezo kilichowekezwa. Uamuzi wa kusambaza Viwanda nchini ili kusawazisha maendeleo ulisababisha mara nyingine Viwanda kujengwa mahali ambapo hakuna maji, au umeme, au vyote viwili, bila kusahau hali duni ya miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

Kutokana na maamuzi hayo ya kurudisha uendeshaji wa shughuli za kiuchumi kwa sekta binafsi, yalichangia ukuaji mzuri wa uchumi ambao ulifikia asilimia 4 kwa mwaka katika kipindi cha mwaka 1986 – 1995 ukilinganisha na ukuaji wa asilimia 2 kwa mwaka katika kipindi cha mwaka 1981 – 1985.

### 2.2 Uwekezaji kuanzia Miaka ya 1990

Tanzania imefanya jitihada kubwa katika kipindi cha miongo mitatu iliyopita kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa lengo la kuvutia uwekezaji binafsi wa ndani na kutoka nje. Mabadiliko makubwa ya kisera na kimiundo yalifanyika tangu miaka ya 1980. Maboresho hayo yanajumuisha kutungwa kwa Sheria ya Kuhamasisha na Kulinda Uwekezaji ya Mwaka 1990 (National Investment Promotion and Protection) Act 1990, ambayo ilianzisha Taasisi iliyokuwa ikishughulika na suala la kuhamasisha uwekezaji iliyojulikana kama Investment Promotion Centre (IPC). Sheria hii ilifuta Sheria ya Kuhamasisha uwekezaji wa kutoka Nje ya Nchi (Foreign Investment Protection Act of 1963).

Aidha, mwaka 1996 Serikali ilitunga Sera ya kuhamasisha Uwekezaji (National Investment Policy of

1996) na Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997 ambayo ilianzisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC). Sheria hii ilifuta Sheria ya Kuhamasisha na Kulinda Uwekezaji ya mwaka 1990. Serikali iliamua kutunga Sera ya Taifa ya Kuhamasisha Uwekezaji kwa lengo la kuvutia uwekezaji zaidi wa ndani na wa kutoka nje kwa kuongeza imani kwa wawekezaji na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji. Malengo ya Sera hii ni: -

(i) Kuimarisha matumizi ya uwezo wa nchi yetu katika kuvutia uwekezaji ikiwa ni pamoja na kushirikiana na nchi mbalimbali zilizoendelea na zinazoendelea. Hapa Wizara ya Mambo ya Nje na Mabalozi wana majukumu yanayosaidia moja kwa moja katika kuhamasisha uwekezaji;

(ii) Kuhamasisha uzalishaji unaolenga kuchochea mauzo nje ya nchi (Export promotion) na kuhakikisha kuwa sekta ya nje inakuwa shindani na inayobadilika kulingana na mahitaji. Hapa ni taasisi za uwekezaji pamoja na wadau wengine katika biashara za ndani na nje;

(iii) Uhamasishaji wa uwekezaji kutoka nje ili kusaidia maeneo ambayo kama nchi hatuna uwezo nayo. Jukumu hili linategemea taasisi ya Uwekezaji pamoja na mabalozi;

(iv) Kuhamasisha na kuwezesha maendeleo ya teknolojojia mpya kupitia uwekezaji hususan katika maeneo ya kuongeza tija, ubora na kuongeza ushindani wa uchumi wetu. Jukumu hili linategemea sekta zote zinazohamashisha uzalishaji pamoja na uwekezaji;

(v) Kuimarisha uwazi katika mfumo wa kisheria na ulinzi wa mitaji ya uwekezaji; na

(vi) Kuimarisha mfumo wa kutoa vibali vya uwekezaji.

Sheria ya Uwekezaji Tanzania ilitungwa Mwaka 1997 kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kitaasisi za uhamasishaji, uwezeshaji na uratibu wa uwekezaji nchini na kuhakikisha uwepo wa mazingira wezeshi ya uwekezaji. Majukumu ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania ni: -

(i) Kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye sekta muhimu zitakazokuza uchumi kwa haraka;

(ii) Kuandaa na kusambaza taarifa sahihi kwa wawekezaji kuhusu fursa za uwekezaji pamoja na upatikanaji wa mitaji na wabia;
(iii) Kuwasaidia wawekezaji kupata vibali na hati mbalimbali za kisheria ili waweze kuwekeza hapa nchini;

(iv) Kubuni mbinu za kujenga mazingira bora ya uwekezaji nchini kwa lengo la kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje;

(v) Kushirikiana na Serikali kutafuta maeneo yenye ardhi kwa ajili ya uwekezaji;

(vi) Kuwasaidia wajasiriamali wadogo na wa kati katika kuibua fursa za uwekezaji kwa lengo la kukuza biashara zao na kuongeza kipato;

(vii) Kufanya tafiti za uwekezaji ili kuwezesha kushauri maboresho ya mazingira ya uwekezaji; na

(viii) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kituo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**2.3 Mafanikio katika Sekta ya Uwekezaji**
Kutokana na jitihada za Serikali za kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji, uwekezaji wa ndani (Domestic Direct Investment - DDI) na ule wa kutoka nje (Foreign Direct Investment - FDI) umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Mafanikio hayo yanaweza kupimwa kwa vigezo vitatu vinavyotumika kupima kiwango cha uwekezaji kwa nchi ambavyo ni Uwiano wa Uwekezaji na Pato la Taifa (Gross Capital Formation to GDP ratio) pamoja na Kiwango cha Uwekezaji Kutoka Nje (Foreign Direct Investment inflows) na kiwango cha Ukuzaji Rasilimali kwa kila mwaka (Fixed Capital Formation).

**2.4 Uwiano wa Uwekezaji kwa Pato la Taifa**
Tangu Serikali ilipoanza kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwekezaji na Sheria ya Uwekezaji Tanzania, wastani wa uwekezaji unaopimwa kwa kuangalia uwiano wa uwekezaji yaani Ukuzaji Rasilimali kwa Pato la Taifa (Gross Capital Formation to GDP ratio), umekuwa ukiongezeka. Takwimu zinaonesha uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa umekua kutoka asilimia 14.7 mwaka 1997 hadi asilimia 39.7 mwaka 2019. Hivi ni viwango vikubwa ukilinganisha na wastani wa nchi za Afrika wa asilimia 21 – 22 na nchi zilizoendelea wa asilimia 23 hadi 25.

**2.5 Uwekezaji kutoka Nje ya Nchi**
Uwekezaji wa mitaji kutoka nje umekuwa ukiongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 0.73 mwaka 1996 hadi Dola za Marekani bilioni 2.18 mwaka 2013 na hadi Dola za Marekani bilioni 1.01 mwaka 2020.

**2.6 Uanzishwaji wa Kituo cha Utoaji Huduma za Uwekezaji**
Uanzishwaji wa Kituo cha Utoaji Huduma za Uwekezaji Mahali Pamoja - One Stop Facilitation Centre (OSFC). Serikali imefanikiwa kuanzisha Kituo cha Utoaji Huduma za Uwekezaji Mahali Pamoja kwa kuleta pamoja Wizara na Taasisi 12 ambazo ni Wizara ya Kazi (masuala ya vibali vya kazi), Wizara ya Ardhi (masuala ya Ardhi-Derivative rights), Idara ya Uhamiaji (Masuala ya vibali vya ukaazi, TIC (kuratibu na kutoa Cheti cha Vivutio), BRELA (Usajiri wa Kampuni), NIDA, TBS, NEMC, OSHA, TRA, TMDA na TANESCO,

Tangu Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997 ilipoanza kutekelezwa kuna ushahidi wa miradi ya uwekezaji takriban kwa kila sekta. Mifano ifuatayo inatoa ushahidi huo:-

(i) Utalii: Kuanzishwa kwa hoteli mpya za kisasa kwa mfano Hyatt Regency, Serena, Giraffe, Protea, Holiday Inn, Sleep Inn, Ngurdoto, n.k. Pia, kuibuka kwa Uwekezaji mkubwa katika kutoa huduma kwa watalii (Tour operators) kama Leopard Tours, Kearsely, Choice Motors, Savannah Tours, Takims Holidays, Walji's Travel Agency, National Tours Ltd n.k.

(ii) Viwanda–Cello Industries, Jambo Plastics, Princewares, Viwanda vya Saruji, Sukari, Vinywaji na Viwanda vya kusindika matunda na vyakula, Viwanda vya vifaa vya ujenzi na Chuma vikiwepo Kamal Steels, Lotus Steel, M.M. Steel, Kiboko Steel, Insignia – Coral Paint, Kiboko Paint n.k.

(iii) Kilimo- Kuanzishwa kwa mashamba makubwa ya Mazao ya Chakula na Biashara kama Kilombero Plantations, Kagera Sugar, Mtibwa Sugar, Kiliflora, Enzazadem, Qsem, Dekker Bruins na Mount Meru Flowers,

(iv) Majengo ya Biashara (Real Estate) – Miradi ya majengo ya biashara na makazi kwa mfano PPF Tower, Mlimani City, Quality Centre, Victoria Plaza, Virgin Plaza, n.k

(v) Huduma za Utangazaji: ITV, TBC/Star Media, Agape TV, Clouds Radio & Televisions, Tumaini Radio & Televisions, CTV, Uhuru Radio, Sahara Communications, n.k

(vi) Miundombinu: Daraja la Mwl. Nyerere, Mwanza Airport Ground Handling, KIA Ground Handling, n. k.

(vii) Huduma za Elimu: Kujengwa kwa vyuo vikuu kama vile Eckenford, Bagamoyo na Kampala; na Shule za Tusiime, St. Mary's, Feza Schools, Bakili Muluzi, Consolata, Filbert Bayi, Neema Trust, Mbutano, n.k.

(viii) Sekta ya Fedha: Kuanzishwa na Kupanuliwa huduma kwa mabenki kama NMB, NBC, CRBD, Bank of Baroda, Bank of India, Diamond Trust Bank, Standard Chartered Bank, CBA, United Bank of Africa, Bank of Africa, n.k.

(ix) Usafirishaji wa Mizigo na Anga: Kuanzishwa kwa miradi kama Precision Air, Fly 540, TRH, Koru freight, Panone, Dalbit, Ruby Roadways, Inara, Road Force, Efficient, Swift Motors, Simba Truck, Sunvic Express, Nas Hauliers, Dhandho Haulage, Prime Fuels, n.k.

2.7 Uanzishwaji wa Kamati mbalimbali za Kitaifa kuhusu masuala ya Uwekezaji nchini.

(i) National Investment Steering Committee (NISC)
Katika jitihada za kuhamasisha uwekezaji wa kimkakati, TIC imesajiri jumla ya miradi mikubwa ya kimkakati (kwa kupewa hadhi ya Miradi mahiri) ipatayo 43. Miradi hiyo inatarajia kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani milioni 12,278.00 na inatarajiwa kutoa ajira zipatazo 130,720 Miradi hiyo inahusisha sekta mbalimbali, ambazo ni Kilimo, Uzalishaji Viwandani, Majengo ya Biashara/Ujenzi na Madini. Baadhi ya miradi iliyofanikishwa kupata hadhi ya uwekezaji kupitia NISC ni pamoja na Mradi wa Mount Meru Millers, Mlimani City, Dangote Industries Limited, Mtibwa Sugar Estates Ltd, Kagera Sugar Estate, Kilombero Sugar Company, Kilombero Plantations Limited (KPL), Tanga Cement Company Limited, TANCOAL Energy Limited, Goodwil Ceramics (Tz) Limited;

(ii) Uanzishwaji wa Kamati ya Uwezeshaji Uwekezaji (National Investment Facilitation Committee - NIFC)
NIFC inayoundwa na Wakuu wa Taasisi zinazotoa vibali na leseni mbalimbali kwa wawekezaji. Kamati hiyo ina jukumu la kusaidia kuondoa changamoto mbalimbali zinazowakabili wawekezaji kwenye maeneo yanayosimamiwa na taasisi za Serikali.

(iii) Kuanzishwa kwa Kamati ya Taifa ya Uhamasishaji Uwekezaji (National Investment Promotion Committee – NIPC)
NIPC ambayo inaundwa na Tasisi za serikali ambazo zinahusika na uhamasishaji Uwekezaji na Biashara. Lengo la Kamati hiyo ni kuwa na mkakati wa pamoja na kushirikiana katika shughuli zote za uhamasishaji Uwekezaji na Biashara. Wajumbe wa kamati hiyo ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Viwanda na Biashara, TIC, ZIPA, TANTRADE, EPZA, TTB, TANAPA, NDC,

(iv) Uboreshwaji wa Mifumo ya kuhudumia wawekezaji

Mifumo ya kielektroniki imeboreshwa kwa kwa upande wa Cheti cha Uwekezaji, Usajili wa Kampuni, Kibali cha Kazi na Ukaazi maombi yote yanachakatwa katika mfumo wa kielektroniki. Pia, taasisi zote zilizopo katika Kitengo cha Huduma za Mahali pamoja zinapokea malipo ya huduma zao kwa mfumo wa GePG hivyo kurahisisha malipo. Taratibu na kanuni za kuanzisha biashara na uwekezaji zimeainishwa waziwazi katika tovuti za kila taasisi na pia katika tovuti ya TIC kwa kutumia mfumo wa eRegulations.

(v) Kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya Uwekezaji ikiwemo uanzishwaji wa Kamati ya Kitaifa ya Ardhi (National Land Committee – NLC).

Ardhi ni msingi wa uwekezaji hivyo TIC katika kutekeleza majukumu yake katika eneo hili kwa kushirikiana na wadau kama Halmashauri, Taasisi za Serikali mfano Mifuko ya Pensheni, Shirika la Nyumba

Taasisi binafsi na wananchi binafsi imeweza kutafuta, kutenga na kuandaa kanzidata ya ardhi ya uwekezaji kwa sekta mbalimbali yenye vitalu na mashamba 157. Wawekezaji wanaohitaji kuwekeza maeneo mbalimbali ya Nchi wanakaribishwa kutembelea tovuti ya TIC (www.tic.go.tz) kisha ingia Zonal Offices kwa taarifa zaidi kuhusu akiba ya ardhi ya uwekezaji.

2.8 Mafanikio ya Uwekezaji Serikali ya Awamu ya Sita
Kutokana na Jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suhuhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuweka mazingira wezeshi ya Uwekezaji kwa kipindi cha miezi sita ya uongozi wake, kumekuwa na mafanikio makubwa katika uwekezaji. Mafanikio hayo ni pamoja na :-

(i) Kuongezeka kwa Usajili wa miradi ya uwekezaji yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.5 (sawa na shilingi trilioni 8.050. Miradi hii itatoa ajira za moja kwa moja elfu 38). Taarifa ya ulinganifu kwa kuzingatia miradi iliyoandikishwa TIC peke yake katika kipindi cha miezi sita ni 164 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.158 sawa na Shilingi za Tanzania trilioni 7.267. Usajili wa miradi hii ni sawa na ongezeko la takriban asilimia 500 ikilinganishwa na usajili kwa kipindi kama hiki mwaka jana ambapo miradi iliyosajiliwa ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 647.43;

(ii) Kuongezeka kwa idadi ya ajira zinazotarajiwa kutokana na Miradi iliyoandikishwa ambapo ajira elfu 38 zitapatikana kwa ujumla. Taarifa za ulinganifu kwa kipindi kama hicho mwaka jana zinapatikana kutoka TIC ambapo kwa kipindi cha awamu hii miradi ya TIC itatoa ajira 32,715 ikilinganishwa na ajira elfu 10 kwa kipindi kama hicho mwaka jana. Ongezeko hili ni zaidi ya asilimia 300 na kielelezo cha hatua kubwa kwa serikali ya mafanikio kwa serikali ya awamu ya sita;

(iii) Kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu uandaaji wa Land Bank, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Kituo cha Uwekezaji imekamilisha zoezi la kubainisha ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji nchi nzima. Ofisi imeanzisha kanzidata ya ardhi ambapo hadi sasa jumla ya hekta 1,606,193.40 zimepatikana. Kwa sasa Kituo cha Uwekezaji kinaendelea na ujenzi wa Mfumo ambao utatumika kuhifadhi taarifa za ardhi hiyo ili kurahisisha upatikanaje wake kwa wawekezaji. Uanzishaji wa Mfumo (Portal) utawezesha wawekezaji kujua maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na upatikanaji wake utakuwa kwa njia ya mtadao. Ardhi, iliyobanishwa ni kwa ajili ya kilimo, biashara, makazi, viwanda, Hoteli, Hospitali, Shule za Sekondari, kumbi za mikutano;

(iv) Kupungua muda wa upatikanaji vibali vya kazi. Katika kutekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuondoa urasimu wa upatikanaji vibali vya kazi hivi sasa hata ndani ya siku moja mwombaji anaweza kupatiwa kibali kupitia mfumo wa ki elektriniki (e-permit). Mfumo huu unaruhusu pia upatikanaji wa kibali cha ukaazi (residency and work permit) katika kadi moja. Kabla ya hapo kibali kilichukua hadi miezi sita na maombi mengi yalikuwa yanakataliwa baada ya mwombaji kulipa a non-refundable fee;

(v) Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni ambapo kwa sasa sheria inaruhusu sheria inaruhusu mwekezaji kuingiza wataalamu 10 kutoka watano (5) ilivyokuwa kabla ya Oktoba 2021;

(vi) Uanzishaji Kituo cha Mawasiliano kwa Uwekezaji katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (Tanzania Investment Call Centre) kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha uundwaji wa mfumo wa ufuatiliaji malalamiko ya wawekezaji na kuwapatia taarifa sahihi kituo hiki kimeanzishwa na kinafanya kazi kwa ufanisi;

(vii) Wizara iliratibu ubainishaji wa changamoto za uwekezaji kwa kuwataka wawekezaji kuwasilisha changamoto zao ambapo Ofisi ilipokea changamoto 112 kutoka katika kampuni 92. Kati ya Changamoto hizo tayari changamoto 19 zimepatiwa ufumbuzi na zilizobakia zinaendelea kufanyiwa kazi na wizara za kisekta chini ufuatiliaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu; na

(viii) Serikali imewezesha upatikanaji wa Uwekezaji wa Miradi yenye manufaa makubwa kiuchumi ikiwemo ya Kampuni ya Elsewedy wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni tatu ($3bn); mradi wa Uzalishaji Sukari wa Kampuni ya SJ Sugar; na mradi wa Kiwanda cha Mbolea ya asili wa Kampuni ya ITRACOM FERTILIZERS LIMITED ambao ulizinduliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Evariste Ndayishimiye, Rais wa Burundi;

(ix) Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kukuza Uwekezaji

Serikali ilikamilisha tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 ambapo tathmini hiyo imeonesha mafanikio mbalimbali yaliyopatikana pamoja na changamoto mbalimbali za kisera, kisheria na kiutendaji. Kutokana na tathmini hiyo, Serikali imeendelea na maandalizi ya Sera ya Maendeleo ya Uwekezaji ikiwa ni pamoja na Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Uwekezaji na utungaji wa Sheria mpya ya Uwekezaji ili kuimarisha uratibu, usimamizi, uhamasishaji na ufuatiliaji wa masuala ya uwekezaji nchini.

Pia, Serikali imeendelea kutekeleza programu mbalimbali za kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji ikiwemo Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (The Government Roadmap) wa Mwaka 2010, Mpango wa kuboresha mifumo ya udhibiti wa biashara (Blue print) wa Mwaka 2019 na kuandaa Mfumo wa Kielektroniki wa kupokea na kushughulikia malala-

miko ya wawekezaji (Online Investors Feedback Platform);

(x) Vilevile, Serikali ilifanya maboresho ya utoaji wa vibali vya kazi ambapo kwa sasa maombi yanaweza kutolewa hata ndani ya siku moja kama nyaraka zote zinakuwapo na wahusika pia. Hivi sasa vibali hivyo vinaweza kupatikana kwa njia ya mtandao na vinaunganishwa na vibali vya ukaazi yaani e permit;

(xi) Serikali imeanza maandalizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Utoaji wa Huduma za Upatikanaji wa Vibali vya Uwekezaji (Tanzania Electronic Investment Window) utakaotoa huduma za Taasisi zote zilizo katika Kituo cha Utoaji wa Huduma kwa Pamoja TIC;

(xii) Kuendeleza Kongani za Kiuchumi
Katika kuendeleza kongani za kiuchumi ikiwemo za viwanda, teknolojia, bandari za kisasa, na uendelezaji vituo vya biashara mipakani, Serikali ilitekeleza mikatati ya kuvutia uwekezaji katika eneo hili. Serikali kwa kushirikiana na wadau imeweza kuhamasisha uanzishaji wa kongani kwa wawekezaji wa ndani katika eneo la Kitaraka Manyoni na Dumila, Morogoro ambazo zitakuwa mahususi kwa ajili ya uendelezaji kilimo cha kisasa cha alizeti na uzalishaji mafuta ya kisasa ya alizeti (double refined) pamoja na sukari. Serikali imeendelea na utekelezaji wa Kanda za Manyoni, Singida na Dumila, Morogoro pamoja na kuanza majadiliano ya uendelezaji wa Mradi wa Eneo Maalum la Kiuchumi Bagamoyo (BSEZ), ujenzi wa kongani ya viwanda eneo la Kwala Mkoa wa Pwani na kongani ya Viwanda eneo la Kigamboni, Dar es Salaam.

(xiii) Benki ya Ardhi kwa ajili ya Uwekezaji (Land Bank)
Serikali imeanza maandalizi ya kuweka Benki ya Ardhi kwa kubainisha ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji nchi nzima ambapo jumla ya hekta 1,606,193.40 zimeainishwa. Serikali imeendelea na ujenzi wa Mfumo ambao utatumika kuhifadhi taarifa za ardhi hiyo ili kurahisisha upatikanaje wake kwa wawekezaji. Uanzishaji wa Mfumo (Portal) utawezesha wawekezaji kujua maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na upatikanaji wake utakuwa kwa njia ya mtadao. Ardhi, iliyobanishwa ni kwa ajili ya kilimo, biashara, makazi, viwanda, hoteli, hospitali, Shule za Sekondari, kumbi za mikutano, n.k.
(xiv) Uhamasishaji Uwekezaji

Ili kuhakikisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wanapata taarifa za fursa za uwekezaji zinazotokana na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kiliratibu utafiti wa kuibua na kuchambua fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali zitakazotokana na mradi wa Reli ya kisasa (SGR) ili kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi. Vilevile, Serikali iliandaa mikutano ya uwekezaji iliyojumuisha nchi 14 iliyofanyika nchini, mikutano 14 iliyofanyika nje ya nchi na mikutano 20 kwa njia ya mtandao. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa, TIC iliwezesha uandaaji wa makongamano ya uwekezaji 4 yaliyofanyika katika mikoa ya Mara, Tabora, Katavi, Pwani, Singida na Tanga.

## 3.0 KUIMARISHA MAJADILIANO KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI

Serikali imendelea kuimarisha majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kutafutia ufumbuzi changamoto zinazoikabili sekta binafsi ili kukuza uchumi na kuiwezesha sekta binafsi kuwa injini ya uchumi.

### 3.1 Baraza la Taifa la Biashara

Kufanya majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kupitia Baraza la Taifa la Biashara na kufikia maazimio mbalimbali ya kuboresha sera, sheria, kanuni na taratibu zinazoathiri shughuli za sekta binafsi. Tangu kuanzishwa, Baraza la Taifa la Biashara mwaka 2001 mikutano 12 ya Baraza la Taifa la Biashara ilifanyika chini ya Uenyekiti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matokeo ya utekelezaji wa maazimio ya Mikutano ya Baraza la Taifa la Biashara ni yafuatayo: -

(i) Kufanya mapitio ya sheria zinazosimamiwa na mamlaka za udhibiti ili kuona uwezekano wa Mamlaka moja kutambua matokeo ya Mamlaka nyingine au kuweka utaratibu wa ukaguzi kufanyika kwa pamoja. Kazi hii ilipelekea kuanzishwa kwa Mpango wa kuboresha Mazingira ya Biashara nchini (BLUEPRINT) for regulatory reform mwaka 2019 ikiwa na lengo la kuondoa kero ya wawekezaji kwenda kutafuta huduma katika kila mamlaka;

(ii) Kuanzishwa kwa mfumo unganishi wa taarifa za ardhi (Integrated Land Management Information System). Serikali imeboresha taarifa za ardhi nchini na maboresho katika ramani kijiografia. Mfumo wa kuunganisha taarifa za ardhi (Integrated Land Management Information System – ILMIS) umeunganisha Makao Makuu, Ofisi za ardhi za Kanda ya Dar es Salaam na Ofisi za Ardhi za Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa kituo cha kutunza taarifa za ardhi; Kuanzishwa kwa Mifumo ya Usajili wa Makampuni kwa njia ya Mtandao (Online Registration System) na Mfumo wa Kutoa Leseni za Biashara Kielektroniki na matumizi ya National Business Portal kwa kutoa taarifa za kibiashara;

(iii) Kurahisisha upatikanaji wa vibali vya kazi na ukaazi kupitia mfumo wa pamoja wa kutoa vibali hivyo (Single Window System) bila usumbufu na kwa wakati kwa wawekezaji;

(iv) Kuanzishwa kwa utaratibu wa kutoa huduma za Bandari ya Dar es Salaam kwa saa 24 kwa siku 7 za wiki kuanzia tarehe 8 Mei, 2017;

(v) Kuanzishwa utaratibu wa pamoja wa kutambua malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Mamlaka za Mapato za Zanzibar na Tanzania Bara;

(vi) Kuondolewa na kupunguzwa kwa kodi, ushuru na tozo mbalimbali zilizokuwa kero kwa wafanyabiashara na wawekezaji kupitia sheria za fedha (finance Act) kwa vipindi tofauti. Mifano ni kodi ya sukari ya viwandani kupunguzwa kutoka 15% hadi 5%; kupunguzwa kwa tozo ya ujuzi kutoka 4.5% hadi 4%; na kuwekwa kwa tozo za kulinda viwanda vya Tanzania pamoja na Kodi ya Forodha ya mafuta ghafi ya chakula imeongezwa maradufu ili kuimari-

sha ushindani na kuongeza uzalishaji wa mafuta nchini;

(vii) Kutolewa kwa msamaha wa adhabu za kikodi kwa wafanyabiashara (Tax Amnesty on Fines and Penalties) wa asilimia 100 kwa kipindi cha miezi sita, Julai, 2018 hadi Disemba, 2018;

(viii) Kuwatambua wajasiriamali wasio rasmi baada ya kupitisha maamuzi ya kuanzisha mfumo wa kuwatambua wajasiriamali 1,527,323 katika sekta isiyo rasmi kupitia vitambulisho vya wajasiriamali;

(ix) Kuanzishwa kwa masoko ya madini ili kuhakikisha kuwa wachimbaji wanapata thamani halisi ya madini yao kupitia masoko rasmi;

(x) Kupitiwa na kugatua baadhi ya majukumu ya taasisi za umma kwa lengo la kupunguza muingiliano wa majukumu unaosababisha kero na kuongeza gharama kwa sekta binafsi (kati ya TFDA iliyobadilishwa na kuwa TMDA na TBS);

(xi) Kuandaliwa kwa Sera ya Maendeleo ya Sekta ya Utalii sambamba na Mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo;

(xii) Kupitisha mapendekezo ya mageuzi ya Sekta ya Utalii yanayolenga kufungua Ukanda wa Utalii wa Kusini mwa Tanzania kwa kuboresha miundombinu kama viwanja vya Ndege;

(xiii) Kuimarisha mfumo wa usajili na utoaji leseni katika sekta ya utalii (Tourism Registration and Licensing System – TORLIS) ili kusajili na kutoa leseni kwa wadau waliokidhi vigezo na masharti ya kufanya biashara za utalii;

(xiv) Kupungua kwa muda wa usajili wa pembejeo (mbegu na mbolea) toka miaka 3 hadi kuwa mwaka mmoja (1). Utekelezaji wa azimio la Baraza la Taifa la Biashara umewezesha Serikali kufanya marekebisho katika Kanuni za Mbolea za mwaka 2011 kwa kurekebisha muda wa usajili wa mbolea kutoka misimu mitatu kwa gharama za USD 10,000 kila msimu ambapo misimu mitatu ilikuwa USD 30,000 hadi msimu mmoja katika Kanda mbili za mazao kwa gharama ya USD 10,000 tu;

(xv) Kupungua kwa Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (Skills Development Levy) kutoka asilimia 4.5 hadi asilimia 4;

(xvi) Kuanzisha Programu ya Kuimarisha Mazingira ya Biashara (Business Environment Strenghterning Program for Tanzania - BEST) kwa ajili ya kuboresha mazingira ya biashara nchini Tanzania;

(xvii) Kuanzishwa kwa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF). Serikali kupitia mikutano ya majadiliano imepelekea kuanzishwa kwa TSPF ili kuratibu sekta binafsi nchini katika majadiliano na Serikali. TPSF imewezesha kuishauri Serikali hatua mbalimbali za kuimarisha mazingira ya biashara, uwekezaji na uchumi;

(xviii) Kuongezeka kwa hali ya kuaminiana kati Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Kwa sasa sekta ya umma na sekta binafsi zinaaminiana na kushirikiana na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kwa manufaa ya Taifa; na

(xix) Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi yametoa fursa kwa sekta binafsi kuweza kushiriki katika mipango ya Serikali na kutoa maoni na mapendekezo ya kuwezesha kufikia malengo ya kitaifa ya muda mfupi na muda mrefu.

### 3.2 Mabaraza ya Biashara ya Wilaya na Mikoa

Serikali imeanzisha na kujengea uwezo Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya kwa ajili ya kuwezesha majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika ngazi ya Mikoa na Wilaya. Tangu kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Biashara, Mikoa 26 ya Tanzania Bara imewezeshwa kuratibu Mikutano ya Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya (Regional Business Councils - RBSs na District Business Councils - DBCs) kwa ajili ya kuibua na kutatua changamoto mbalimbali na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji katika ngazi za mikoa na wilaya. Mikutano Saba (7) ya RBCs imefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mtwara, Kigoma, Geita na Mwanza ambapo mikutano hiyo ilitanguliwa na mikutano ya Wilaya za mikoa husika. Wilaya hizo ni pamoja na Mkuranga, Kigamboni, Sengerema, Magu, Ilemela, Kwimba, Misungwi, Ukerewe, Nyamagana, Tabora Mjini, Igunga, Kaliua, Nzega, Sikonge, Uyui na Urambo. Matokeo ya utekelezaji wa maazimio ya mikutano ya RBCs na DBCs ni yafuatayo: -

(i) Kuanzishwa kwa miradi inayochochea uwepo wa mazingira rafiki kwa shughuli za biashara na uwekezaji kama vile Vituo vya kutoa Huduma Biashara ya Pamoja (One Stop Business Centres - OSBC);

(ii) Ujenzi wa miundombinu ya masoko na umwagiliaji katika ngazi za Mikoa na Wilaya;

(iii) Kupungua au kufutwa kwa ushuru na tozo zilizowekwa kwa sheria ndogondogo za Halmashauri ambazo ni kero na zinazoongeza gharama kwa sekta binafsi; na

(iv) Kufanyika kwa majadiliano yaliyoongozwa na Mawaziri wanaosimamia sekta za kibiashara na kiuchumi katika ngazi ya Mikoa kwenye Mikoa sita (6) kwa lengo la kutathmini utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji nchini.

### 3.3 Vikundi Kazi vya Kisekta

Serikali imeendelea kuratibu na kufanya majadiliano ya kitaalamu kupitia Vikundi Kazi vya Kisekta (Tech-

nical Working Groups) kwa sekta za Kilimo, Uwezeshaji (Economic Empowerment), Miundombinu, Ardhi, Maendeleo ya Rasilimali watu, Fedha, Biashara ya Kimataifa, Viwanda, Misitu, Utalii na Mazingira ya Biashara. Katika kipindi cha miaka 20, Vikundi Kazi vya Kisekta vimewezesha mafanikio yafuatayo: -

(i) Kuwezesha kufanyika kwa utafiti kuhusu bidhaa za mbao zilizohandisiwa (Engineered Wood Products–EWP) na fursa zake na Kuandaa Mpango Kazi wa Kutekeleza Mfumo/Mwongozo wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Bidhaa za Mbao Zilizohandisiwa (National Engineered Wood Sector Development Framework 2021-2030);

(ii) Kuandaa mkakati wa kitaifa kuhusu bidhaa za mbao zilizohandisiwa (engineered wood products) na kuwasilishwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ajili ya utekelezaji;

(iii) Kuandaa mapendekezo ya kuimarisha mfumo wa usimamizi na kupanua wigo wa kodi nchini ikiwemo kuanzisha utaratibu wa kurasimisha wafanyabiashara/ wajasiriamali kwa njia ya kuboresha vitambulisho vyao, kutoza kodi katika "data" za kidijitali na makampuni yanayomiliki mitandao ya kijamii kama vile google, facebook, tweeter, YouTube, Amazon n.k;

(iv) Kutoa mapendekezo ya kuimarisha miundombinu mbalimbali ikiwemo bandari, mawasiliano kama vile kuanzishwa kwa mkongo wa taifa (fibre optical cable) pamoja na kutenganisha huduma za shirika ta simu Tanzania (TTCL);

(v) Kuanzisha Kitengo cha Local Content katika taasisi ya NEEC kwa ajili ya kusimamia na kuratibu ushiriki wa Watanzania katika uchumi;

(vi) Kuondolewa mapendekezo ya namna ya kuimarisha uwekezaji katika mnyororo wa thamani wa sekta ndogo za mafuta ya kula, Horticulture, uvuvi na maziwa; na

(vii) Kutathmini utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa ya kuboresha mazingira ya biashara, hususan kupitia mpango wa BLUEPRINT.

## 4.0 KUFANYA TAFITI NA TATHMINI ZA MAZINGIRA YA BIASHARA NA UWEKEZAJI

Serikali imeendelea kuratibu na kufanya tafiti na tathmini za mazingira ya biashara, uwekezaji na uchumi ambazo hutumika kuwezesha maamuzi katika mikutano ya majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta bianfsi. Katika kipindi cha miaka 20, tafiti na tathmini zifuatazo zimefanyika: -

### 4.1 Economic Empowernment – Kilimo Kwanza

Serikali liliendesha midahalo kuanzia ngazi ya Wilaya, Mikoa na Taifa kwa lengo la kutathmini namna ya kuwawezesha wananchi washiriki kikamilifu katika nyanja za uchumi na kuimarisha usawa katika uchangiaji na ugawanywaji wa rasilimali. Tathmini hii imewezesha Serikali kubuni Kilimo Kwanza ukiwa ni mkakati wa uwezeshaji wananchi kiuchumi baada ya kubainisha kuwa kilimo ndiyo njia kuu ya kumkomboa mwananchi kutoka kwenye umaskini. Madhumuni ya Kilimo Kwanza ni kufanya kilimo kiwe cha kisasa na kibiashara ili kuleta Mapinduzi ya Kijani na kuchangia katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025.

Aidha, Mkutano wa Maendeleo wa Africa (World Economic Forum for Africa) uliofanyika mwezi Mei, 2010 hapa Dar es Salaam, uliamua kukifanya kilimo kuwa agenda ya uchumi ya kimataifa (World Economic Agenda) kwa lengo la kuzalisha chakula cha kutosha na uhifadhi wake (food security). Mkutano huu ulitilia mkazo ushiriki wa kikamilifu wa sekta binafsi katika kilimo kupitia mpango wa Southern Agriculture Growth Corridor for Tanzania (SAGCOT). Vilevile, mkakati wa kilimo kwanza umewezesha kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) mwaka 2013.

### 4.2 Tafiti kuhusu Gharama za Kufanya Biashara Kitaifa (Sub National Cost of Doing Business Survey)

TNBC ilifanya tafiti mwaka 2007 ili kuainisha vyanzo vikuu vinavyochangia kupandisha gharama za biashara nchini na kupendekeza hatua muafaka za kuchukua ili kuboresha mazingira ya biashara, uwekezaji na uchumi nchini. Tafiti hiyo ilifanywa Tanzania Bara katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Mwanza na Dar es Salaam pamoja na Zanzibar. Mafanikio yaliyoambata na tafiti hii ni kuainisha changamoto za kufanyabiashara na uwekezaji sambamba na kuwezesha mikoa husika kuchua hatua mahsusi za kukabiliana na changamoto hizo. Pia, Mikoa ilipata fursa ya kujifunza namna bora ya kukabiliana na changamoto za kufanyaja biashara na uwekezaji toka katika Mikoa ambayo imekua ikifanya vizuri katika kupunguza gharama za kufanya biashara.

4.3 Utafiti kuhusu Bidhaa za Mbao Zilizohandisiwa (Engineered Wood Products–EWP)

Serikali imeratibu na kufanya tafiti kuhusu bidhaa za mbao zilizohandisiwa (Engineered Wood Products–EWP), fursa zake na kuandaa mapendekezo ya maboresho yanayohitajika ili kuchochea uwekazaji katika sekta ya Misitu. Aidha, Serikali imeratibu na kuandaa andiko kuhusu changamoto za MSMEs kwa sekta ndogo ya misitu ya kibiashara na bidhaa za misitu. Mafanikio yaliyotokana na tafiti hizi ni kuandaliwa kwa Mfumo/ Mwongozo wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Bidhaa za Mbao Zilizohandisiwa (National Engineered Wood Sector Development Framework 2021-2030) pamoja na Mwongozo wa Taifa wa Engineered Wood Products–EWP pamoja na Mpango wake.

**4.4 Kuboresha Mazingira ya Biashara kupitia utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN for Improvement of Business Environment)**

Serikali iliunda Kikosi Kazi ambacho kilishirikisha sekta binafsi na sekta ya umma kwa ajili ya kuainisha matatizo ya msingi yanayoathiri uwekezaji na uendeshaji biashara hapa nchini na kupendekeza vipaumbele vya ufumbuzi wa matatizo ili yaingizwe kwenye Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Maeneo yaliyoainishwa na Kikosi Kazi ni:-

(i) Kuboresha Kanuni na Taratibu za biashara na Taasisi zinazosimamia biashara;
(ii) Upatikanaji wa Ardhi na haki za umiliki wake;
(iii) Kuimarisha ukusanyaji wa kodi na kupunguza wingi wa kodi na tozo mbalimbali;
(iv) Kuzuia na kupambana na rushwa;
(v) Kuboresha sheria za kazi na kuimarisha mafunzo na stadi za kazi; na
(vi) Kusimamia utekelezaji wa Mikataba na utawala wa sheria.

**5. KUKUZA USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**

Uwezeshaji wananchi kiuchumi ni juhudi za makusudi za kumtoa mtu katika ngazi fulani ya maisha au uchumi na kumpeleka kwenye ngazi ya juu zaidi kutoka pale alipokuwa. Inaweza kuwa ni mtu wa chini sana kumpeleka ngazi ya kati au kumtoa mtu ngazi ya kati kwenda ya juu. Chimbuko la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi lilitokana na sababu za kihistoria wakati wa ukoloni ambapo wananchi hawakushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi kwa kuwa walinyimwa fursa. Wananchi wengi waliwekewa vikwazo vya kushiriki shughuli rasmi za kiuchumi hivyo wengi wao walijishughulisha na uchumi wa sekta isiyo rasmi. Mbinu zilizotumika kubagua watanzania ni pamoja na utoaji wa mikopo, elimu, ardhi na leseni za biashara ambavyo vilipewa kipaumbele kwa wazungu na wananchi wachache.

Tangu Uhuru ulipopatikana mwaka 1961, wananchi walipata madaraka ya kisiasa lakini sehemu kubwa ya uchumi bado ilibaki mikononi mwa wageni na baadhi ya Watanzania. Katika kukuza ushiriki wa wananchi kwenye uchumi, mafanikio yafuatayo yamepatikana: -

(i) Kutangazwa kwa Azimio la Arusha, mwaka wa 1967. Azimio hilo lilikuwa ni mkakati muhimu wa kuhakikisha kwamba wananchi kwa pamoja kupitia dola wanashika njia kuu za uchumi. Aidha, shughuli zote za uzalishaji na utoaji wa huduma ziliundiwa mashirika ya umma;
(ii) Kuanzishwa kwa Mamlaka na Taasisi mbalimbali ili kusaidia wananchi katika kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi ikiwemo: Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) kwa ajili ya kuendeleza viwanda vidogo nchini (1973); kuunda upya Serikali za Mitaa (1982); kurudisha Vyama vya Ushirika mikononi mwa wananchi mwaka 1984; Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (2004); Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (2012);
(iii) Kuweka mazingira ya upatikanaji wa mitaji kwa kuimarisha vyanzo vya mikopo ili kuinua hali na hadhi ya wananchi ili wakopesheke kwa kuanzisha mifuko na programu 52. Kati ya Mifuko na Programu 52, Mifuko 21 inatoa mikopo moja kwa moja, mifuko 9 inatoa dhamana ya mikopo, mifuko 17 inatoa ruzuku na programu 5 za uwezeshaji. Mifuko ya uwezeshaji inayotoa mikopo moja kwa moja kwa kushirikiana na ile inayotoa dhamana imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi Trilioni 4.97 kwa wajasiriamali 7,231,617 wakiwemo wanawake 3,795,598 sawa na asilimia 52.5 na wanaume 3,436,019 sawa na asilimia 47.5. Aidha, Mifuko hii imetengeneza jumla ya ajira 13,591,146 ambapo kati ya hizi, ajira 8,018,775 sawa na asilimia 59 zilikuwa ajira za moja kwa moja na ajira 5,572,371 sawa na asilimia 41 zilikuwa zisizo za moja kwa moja. Kati ya jumla ya ajira 13,591,146; ajira kwa wanawake zilikuwa 5,708,281 sawa na asilimia 42 na ajira kwa wanaume ni 7,882,865 sawa na asilimia 58;

(iv) Kuimarisha utendaji wa mifuko na progeamu za uwezeshaji wananchi kwa kufanya tathmini ya utendaji wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi kwa Lengo la kuongeza ufanisi na tija. Tathmini hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyoyatoa tarehe 13 Novemba, 2020 wakati akifungua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita alipokutana na Bunge tarehe 22 Aprili, 2021 na alipokutana na wanawake tarehe 8 Juni, 2021 Mkoani Dodoma. Taarifa ya tathmini imekamilika na imetoa mapendekezo ya baadhi ya mifuko kuunganishwa ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza tija;

(v) Kuwahimiza wananchi kuanzisha shughuli za kiuchumi kwa kuanzisha miavuli ambayo inahusika na uanzishwaji na uendelezaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii ambayo ni VICOBA- Federation of Tanzania (VICOBA-FETA, Tanzania Informal Microfinance Association of Practitioners (TIMAP) na Inter-Religious VICOBA (IR VICOBA). Hadi June, 2021 jumla ya vikundi 30,484 vimeanzishwa vyenye wanachama 914,520. Kati ya wananchama waliopo kwenye miavuli, wanawake 731,616 na wanaume 182,904. Jumla ya mitaji iliyokusanywa kupitia miavuli hiyo ni shilingi 1,736,930,313,669;

(vi) Kuimarisha na kukuza ushirika nchini. Hadi Juni, 2021 kuna Vyama vya Ushirika 9,185 vyenye jumla ya wanachama 6,050,324 ambapo wanaume 3,932,711 na wanawake 2,117,613. Kati ya vyama, Vyama vya Ushirika wa Masoko ya Mazao (AMCOS) vilikuwa 4,039 vyenye jumla ya wanachama 2,660,562, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) vilikuwa 3,831 vyenye jumla ya wanachama 2,523,548, Vyama vya Msingi (Union) vilikuwa 58 vyenye jumla ya wanachama 38,206, Vyama vya Joint enterprises vilikuwa 42 vyenye jumla ya wanachama 27,666 na Vyama vingine

(katika sekta mbalimbali) vilikuwa 1,215 vyenye jumla ya wanachama 800,342;

(vii) Kuanzisha Vituo vya Uwezeshaji 17 katika Mikoa ya Singida (1), Shinyanga (1) Kigoma (6), Dodoma (7), Rukwa (1) na Geita (1) kama iliyoelekezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025 katika Ibara ya 26 (K). Vituo vya uwezeshaji vinatoa huduma mbalimbali ikiwemo usajili na uendelezaji wa biashara na mikopo kwa wananchi 10,893 wakiwemo wanawake 5,781 sawa na asilimia 53 na wanaume 5,112 sawa na asilimia 47. Aidha, vituo hivi vimetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 44.5 kwa wananchi 4,474 ambapo wanawake 1,903 na wanaume 2,571. Vilevile, vituo vimewezesha urasimishaji wa biashara 5,721 na kutoa mafunzo ya ujuzi na ujasiriamali kwa wananchi 6,339 wakiwemo wanawake 4,16 na wanaume 2,113;

(viii) Kuwezesha wananchi kununua hisa kwenye mashirika yaliyobinafsishwa. Hadi kufikia Juni, 2021 jumla ya Kampuni 29 zimesajiriwa na soko la Hisa. Kati ya Makampuni hayo 23 ni ya ndani na sita (6) ni ya nje;

(ix) Kuanzisha majukwaa ya wanawake katika mikoa yote ili kukuza shughuli za kiuchumi za wajasiriamali wanawake. Katika kuimarisha Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi jumla ya majukwaa 927 yaliyopo katika ngazi za mikoa (24), halmashauri (123), kata (280) na vijiji (500). Aidha, Serikali imeanzisha Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (Presidential Trust Fund) ili utumike kulea wanawake wajasiriamali kupitia majukwaa ya wanawake. Aidha, Serikali imeendelea kutenga maeneo wezeshi ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogo wakiwemo wanawake ili kuwawezesha wanawake kufanya biashara zenye ubora na kiwango cha kitaifa na kimataifa;

(x) Kuwajegea uwezo vijana ili kuongeza ujuzi, kupata uzoefu pamoja na kuwawezesha kuhimili ushindani katika masoko ya ndani na nje kwa kukuza ujuzi. Serikali imekuza ujuzi kwa vijana 18,956 wakiwemo wanaume 10,878 na wanawake 8,078 wa kuwawezesha kujiajiri au kuajiriwa. Kati yao, vijana 5,538 walipata mafunzo ya uanagenzi katika fani ya ufundi stadi na vijana 10,178 walipata mafunzo ya kurasimishiwa ujuzi kupitia mfumo usio rasmi ambapo kati ya wanufaika hao, 28 ni watu wenye ulemavu na vijana 3,240 waliwezeshwa kupata mafunzo ya uzoefu kazini;

(xi) Kuwajengea uwezo vijana ili waweze kujiajiri au kuajirika kwa kutekeleza Mpango wa Kuwajengea Uwezo Vijana (2JIAJIRI Youth Entrepreneurship Training Program) katika mikoa sita ya Dar es Salaam, Morogoro, Zanzibar, Arusha, Kilimanjaro na Mwanza. Mpango umewezesha mafunzo kwa vijana 303 wakiwemo wanawake 172 na wanaume 131. Mafunzo yalitolewa katika mikoa yote ambapo: Dar es Salaam (89), Morogoro (33), Zanzibar (44), Arusha (51), Kilimanjaro (40) na Mwanza (46). Mafunzo hayo ni kuhusu: sifa za mjasiriamali; mjasiriamali na familia; vyanzo vya mitaji; masoko; utunzaji kumbukumbu; kumjali mteja; urasimishaji biashara; kupanga bajeti; namna ya kutunza muda, umuhimu wa uwekaji akiba; na mtandao wa biashara;

(xii) Kuwezesha mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa baishara kwa vijana 430 kupitia Programu ya Kijana Jiajiri. Kati ya vijana hao, vijana 85 wamefungua kampuni (mpya) na biashara 100 za vijana zimerasimishwa kutokana na kushiriki kwao kwenye mafunzo hayo na vijana 97 kupitia Programu hii wamepata mikopo nafuu. Aidha, kupitia Programu ya Jiandalie Ajira Serikali imewezesha vijana 800 kupata mafunzo ya ujasiriamali ambapo vijana 20 wameanzisha kampuni mpya. Serikali kupitia Programu ya Ajira Yangu, vijana wajasiriamali 49 wenye umri kati ya miaka 15-35 walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali kuhusu stadi za kuanzisha na kusimamia biashara na kutengeneza maandiko ya biashara ambayo yalishindanishwa;

(xiii) Kutekeleza Mpango wa Uanzishaji Mafunzo ya Ujasiriamali kwa vitendo kwa wanafunzi wa shule 12 za Sekondari katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha. Mpango huu umelenga shule za Sekondari ambazo ziko katika Halmashauri za Mwanga DC, Siha DC, Moshi DC, Arusha CC, Meru DC, Monduli DC, Ubungo DC, Kinondoni MC na Ilala MC. Aidha, jumla ya miradi 12 imeibuliwa na wanafunzi wajasiriamali 493 kati ya hao wasichana 305 na wavulana 188. Kuibuliwa kwa miradi hii kumetokana na wanafunzi hao kupata mafunzo ya jinsi ya kupata wazo la biashara, mpango wa biashara, kujiamini, vyanzo vya mitaji, na utafutaji wa masoko;

(xiv) Kutoa uelewa kwa wananchi kupitia  maonesho ya mifuko na Programu za Uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo yalifanyika kwa madhumuni ya Kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kuweka akiba na kuwekeza katika miradi yenye kuleta faida, Kukuza uelewa wa wananchi juu ya uwepo, majukumu na vigezo vinavyotumika katika kutoa huduma za mifuko na program za uwezeshaji, Kuhamasisha kuanzishwa na kuimarishwa kwa vikundi vya kifedha vya kijamii kwa ajili ya kujiwekea akiba na kukopeshana ili kupata mitaji ya kuwekeza katika miradi ya kiuchumi, Kuwakutanisha wajasiriamali na watoa huduma mbalimbali wa Serikali na binafsi watakaosaidia kuongeza thamani na kukuza biashara zao, Kutengeneza mtandao wa wajasiriamali na wadau mbalimbali kwa ajili ya kubadilishana uzoefu. Aidha, maonesho haya yamefanyika katika Mikoa ya Dodoma (2017), Mbeya (2018), Simiyu (2019) na Arusha 2021). Wananchi 13,616 walifanikiwa kutembelea maonesho hayo na jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.3 ilitolewa kupitia maonesho hayo;

(xv) Baraza kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine limeratibu mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake na vijana katika halmashauri za wilaya 117. Dhumuni kuu la mafunzo lilikuwa ni kuwakutanisha wajasiriamali wanawake na vijana na wadau mbalimbali kwa ajili ya kutatua changamoto za mitaji, urasimishaji,

elimu ya biashara, masoko, namna ya kuandika maandiko ya miradi yenye sifa za kukopesheka katika benki za biashara. Jumla ya wananchi 75,894 walipata mafunzo miongoni mwao wanawake walikuwa ni 47,813 ambao ni sawa na asilimia 63 na vijana ni 28,081 sawa na asilimia 37; na

(xvi) Kuwajengea uwezo Waratibu wa Uwezeshaji kuhusu usimamizi na uratibu wa masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Mikoa 26 Tanzania Bara (Kanda za Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Mashariki na Kanda ya Kati). Mafunzo hayo yaliwashirikisha viongozi na waratibu wa uwezeshaji wa mikoa na Halmashauri 673 pamoja na maafisa kutoka katika Halmashauri zilizoshiriki.

### 6. KUKUZA USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA MIRADI YA KIMKAKATI NA UWEKEZAJI

Ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji ni thamani ya ziada inayochangia kwenye uchumi wa Taifa kutokana na uwekezaji kupitia ushiriki wa Watanzania. Ushiriki wa Watanzania huhakikisha nchi inaongeza ushiriki wa watu wake ili wananufaike kwenye sekta zote za kiuchumi kupitia miradi ya kimkakati, Uwekezaji wa Nje (FDIs), Mikataba ya Kimataifa na Uwekezaji Mkubwa wa Ndani. Serikali imeendelea kuhakikisha wazawa wanapata fursa kushiriki katika miradi ya kimkakati na miradi mingine ya uwekezaji ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana: -

(i) Kuweka mazingira wezeshi kwa watanzania kushiriki katika uwekezaji na miradi ya kimkakati kwa kufanya mapitio ya Sera na marekebisho ya Sheria za kisekta. Baadhi ya Sera na Sheria zenye masuala ya ushiriki wa watanzania ni pamoja na: Sera ya Nishati, 2015, Sheria ya Mafuta, 2015, Kanuni za Ushiriki wa Watanzania katika Sekta ya Mafuta 2017, Sheria ya Madini, 2010 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2017), Kanuni za Ushiriki wa Watanzania katika Sekta ya Madini, 2018, Sheria ya Bima 2009 na Kanuni zake, Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (Watoa Huduma Ndogo za Fedha Wasiopokea Amana) 2019, Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016), Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Kama ilivyorekebishwa mwaka 2018) na Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania, 2017. Mfano katika Sekta ya Madini, marekebisho ya sera na sheria hizi yamewezesha kuweka mfumo thabiti wa kukagua shughuli za migodi, kukusanya takwimu na kufuatilia maduhuli yatokanayo na madini; kuvutia uwekezaji; kuhamasisha uzalishaji na masoko ya madini viwandani; kuweka miundombinu muhimu kwenye maeneo yenye uwezekano wa kuanzishwa kwa migodi mikubwa mipya; kuwawezesha wachimbaji wadogo kujiajiri kupitia sekta hii; na kuhakikisha migodi yote mikubwa nchini inaendelea kununua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini kwa kiwango cha kuridhisha kwa kadri ya upatikanaji wake;

(ii) Kutengeneza na kuzindua Kanzidata ya Uwezeshaji kiuchumi ili kuwaunganisha wajasiriamali na wawekezaji, wakandarasi au kampuni za nje kwa lengo la kuwawezesha watanzania wakiwemo wazalishaji na watoa huduma kutambulika na nchi mbalimbali hasa wawekezaji kwa lengo la kukuza ushiriki wa watanzania kwenye uchumi;

(iii) Kukuza ajira na ujuzi kwa watanzania kwa kuwawezesha watanzania kupata ajira, uzoefu na ujuzi katika uwekezaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Ushiriki wa watanzania kupitia ajira umeendelea kupewa kipaumbele na kuzingatiwa ipasavyo katika miradi mbalimbali ya kimkakati na uwekezaji nchini. Katika miradi mingi kwa sasa, ajira za ujuzi wa kati na zisizohitaji ujuzi kwa zaidi ya asilimia 90 zinafanywa na watanzania na wageni wameajiriwa zaidi kwenye ajira za ujuzi wa juu. Mfano katika mradi wa treni ya mwendo kasi (SGR) umeajiri wafanyakazi wa kitanzania 18,000 (82%) ya wafanyakazi wote. Mradi wa uboreshaji wa Reli ya Kati watanzania 3,487 (91%) ya wafanyakazi wote wameajiriwa. Mradi wa Uwanja wa Ndege wa Mwl. J.K. Nyerere umeajiri watanzania 997 (95%) ya wafanyakazi wote. Barabara ya juu ya ubungo (ubungo interchange) umeajiri watanzania 1,845 (95%) ya wafanyakazi wote, mradi wa matengenezo ya daraja la salander umeajiri watanzania 405 (91%) ya wafanyakazi wote.

Pia, mradi wa kufua umeme wa Mwl. J.K. Nyerere umeajiri watanzania 4,783 (88%) ya wafanyakazi wote kwa sasa. Miradi ya kuchimba gesi ya Moren and Prome imejiri watanzania 170 (96%) ya wafanyakazi wote, mradi wa Songas umeajiri watanzania 70 (96%) ya wafanyakazi wote na mradi wa PAN AFRICAN umeajiri watanzania 98 (98%) ya wafanyakazi wote. Kwa kipindi cha mwaka 2019/20, jumla ya watu 35,718 waliajiriwa kufanya kazi kwenye miradi ya kimkakati wakiwemo wageni 6,529 sawa na asilimia 18 na watanzania 29,189 sawa na asilimia 82. Miradi hiyo ni pamoja na: mradi wa kufua umeme, ujenzi wa reli ya kisasa, Ubungo Interchange, New Salender Bridge, uwanja wa Ndege wa Kimataifa (JNIA TB III), miradi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami mfano Urambo-Kaliua, miradi ya umeme wa nishati vijijini, miradi ya maji mijini na vijijini, sekta ya uziduaji na bima.

Serikali pia, imekuza ajira katika migodi ambapo watanzania wameendelea kupewa kipaumbele kutokana na maboresho katika sekta ya madini ikiwemo marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na Kanuni za Ushiriki wa Watanzania katika Sekta ya Madini, 2018. Katika kipindi cha mwaka 2018, ajira za watanzania katika migodi zilikuwa 6,623 ikilinganishwa na ajira za wageni 140. Aidha, ajira za watanzania kwenye migodi kwa mwaka 2019 na 2020 zilikuwa 7,967;

(iv) Kuzingatia masuala ya ushiriki wa watanzania kwenye zabuni kwa kuziwezesha kampuni za ndani kupata zabuni kwenye miradi ya kimkakati na kuweza kuuza bidhaa na kutoa huduma. Katika mwaka 2019/20 kwenye utekelezaji wa miradi ya kimkakati

13, jumla ya kampuni 358 zilipata zabuni ikiwemo kampuni za ndani 304 na kampuni za nje 54. Aidha, kiasi cha shilingi 3,337,444,819,288.15 kilitumika katika ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati na uwekezaji ikiwemo Mgodi wa Dhahabu wa North Mara, Mbeya Cement LTD, CMS LTD, Dangote Cement, TCL Service LTD na Ruvuma Coal LTD pamoja na miradi ya sekta ya ujenzi na uchukuzi.

Kati ya fedha hizo, shilingi 2,039,232,597,120.97 zilienda kwa kampuni za ndani na shilingi 1,298,212,222,167.18 kampuni za nje;

(v) Kutekeleza dhana ya ushiriki wa watanzania katika uwekezaji na miradi ya kimkakati kwa kusajili makampuni ya makandarasi 769 yakiwemo makampuni ya kigeni 6 na makampuni ya kitanzania 761. Aidha, kampuni mbalimbali za kitanzania zinatoa huduma na bidhaa kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji. Mfano katika mwaka 2020/21 kampuni 612 zilitoa huduma na bidhaa kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji ikiwemo mradi wa Kufua Umeme – JNHP ni kampuni 45, sekta ya mafuta na gesi ambapo kampuni 108, sekta ya madini ni kampuni 40, Reli ya SGR ni kampuni 412;

(vi) Kuongeza ushiriki wa watanzania kwenye uwekezaji na miradi ya kimkakati kwenye sekta ya uziduaji na ujenzi kwa kuwezesha mafunzo na ujengaji uwezo kwa watanzania 57,192;

(vii) Kusimamia suala la ujuzi na uhaulishaji wa teknolojia kwa watanzania. Mfano katika mwaka 2019/20, kupitia miradi 9 ya kimkakati kwa kuhaulisha teknolojia na ukuzaji ujuzi kwa watanzania 7,177. Hatua hii imewezesha wawekezaji na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya kimkakati kukuza ujuzi na kuhaulisha teknolojia kwa watanzania. Mfano kampuni ya PanAfrican Energy mwezi Februari, 2020 ilimteua mtanzania kuwa Naibu Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo. Aidha, mwezi Februari, 2020 kampuni ya Songas pia ilimteua mtanzania kuwa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo kama sehemu ya urithishaji wa ujuzi;

(viii) Kuhimiza wawekezaji, wamiliki wa leseni, wakandarasi wakubwa na watoa huduma kuhusu dhana ya uwajibikaji kwa jamii inayoizunguka maeneo ya uwekezaji ili watanzania wanufaike na fursa za huduma za kijamii. Hatua hii imewezesha wawekezaji, wakandarasi na watoa huduma kuzingatia dhana ya uwajibikaji kwa jamii kwa kuwezesha huduma za jamii katika maeneo husika kwa kujenga barabara, zahanati, shule na visima vya maji. Kwa mwaka 2019/20, kupitia utekelezaji wa miradi ya kimkakati 9, iliwezesha huduma za jamii maeneo mbalimbali ikiwemo uchongaji barabara (vijiji vya Nsenda, Ushokola, Vumilia na Kaliua – Tabora); ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu na ukarabati wa barabara (Kilosa, Kondoa na Tabora mjini); na ujenzi wa shule na ujenzi wa zahanati (Mbinga). Aidha, katika mwaka 2020 kupitia uwekezaji mfano Mgodi wa Dhahabu wa North Mara, Mbeya Cement LTD, CMS LTD na Dangote Cement, kiasi cha shilingi 20,394,414,718 kimetolewa kama uwajibikaji kwa jamii; na

(ix) Kuwajegea uwezo wadau 573 kuhusu masuala ya ushiriki wa watanzania katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati na uwekezaji ili kuongeza uelewa katika sekta hii. Washiriki 573 walijengewa uwezo kuhusu masuala ya local content. Lengo ni kuwawezesha wafanyakazi kuongeza maarifa na ujuzi katika masuala ya ushiriki wa watanzania kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji na kujifunza kutoka nchi nyingine kwa jitihada zao nzuri katika kuongeza ushiriki wa wazawa kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji.

## 7.0 HITIMISHO

Kutoka Tanzania ipate uhuru, Serikali imechukua hatua ya makusudi ya kukuza uchumi wa Taifa na kuboresha hali ya maisha ya wananchi wake kwa kuhamasisha uwekezaji na ushiriki wa wananchi katika uchumi. Kutokana na juhudi hizo, Serikali imepata mafanikio ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta mbalimbali nchini, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, utoaji wa mikopo kwa wajasiliamali, ujenzi wa miundombinu (umeme, reli, barabara, madaraja, n.k), utaoaji wa elimu kwa wajasiriamali, utoaji wa huduma za kijamii (afya, elimu, n.k) na ujenzi wa vituo vya uwezeshaji.

Serikali inaendelea kuchukua hatua nyingine za kuandaa, kusimamia na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ikiwemo Sheria, Kanuni na Maelekezo yote yanayohusu uwekezaji ili kuhakikisha kuwa vikwazo vyote katika uwekezaji vinatambulika na kuondolewa pamoja na kuwa na mazingira rafiki na sawa katika uwekezaji. Serikali pia itaendelea kujenga mazingira wezeshi ambayo yatasaidia wananchi na sekta binafsi kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa Taifa pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, kuimarisha miundombinu (barabara, reli, madaraja, umeme, viwanja vya ndege) ili kupunguza gharama za uzalishaji, kutengwa kwa maeneo ya biashara, kuongeza ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati na miradi mikubwa ya uwekezaji, kuboresha utoaji wa mikopo kwa kupunguza riba na masharti mengine, kutoa elimu kwa wajasiriamali na kudhamini mikopo kwa wajasiriamali.




# MAFANIKIO NA MAENDELEO YA SEKTA YA MADINI KABLA NA BAADA YA UHURU

Ndugu Wanahabari, Sekta ya Madini ina historia ndefu kuanzia kipindi cha kabla ya uhuru hadi kufikia kipindi hiki cha kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Taifa letu. Sekta hii imepitia katika hatua na miundo mbalimbali ya Serikali katika awamu tofauti tokea kipindi cha Ukoloni hadi sasa. Miongoni mwa muundo wa Serikali ambako Sekta ya Madini imepitia ni pamoja na kuwa sehemu ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Maji, Wizara ya Nishati na Madini, na hatimaye mwaka 2017 baada ya kugawanywa kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini na kuundwa kwa Wizara ya Madini ambayo ina dhamana ya kusimamia sekta ya Madini peke yake. Pamoja na majukumu mengine, jukumu la msingi la Wizara hii ni kusimamia na kuboresha Sera Sheria na Kanuni za Madini nchini.

Ndugu Wanahabari, shughuli za uchimbaji na biashara ya madini nchini Tanzania zimekuwepo kabla na baada ya Uhuru wa Tanzania Bara Mwaka 1961. Kabla ya Uhuru, shughuli za madini na biashara ya madini hazikuwa kubwa, wakati huo uchimbaji wa madini ulisimamiwa na Sheria ya Madini ya Mwaka 1920 (The Mining Ordinance 1920), ambapo biashara zilizofanyika zilikuwa za kufua vito chini ya Sheria ya Goldsmiths na Silversmiths Ordinace 1937 ambayo ilihusu usimamizi na udhibiti wa biashara ya dhahabu. Kuanzia miaka ya 1965 mpaka 1975 Bunge lilipitisha Sheria ya "The National Investment Promotion and Protection Act" ambayo ilisimamiwa na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) kwa kuendeleza shughuli chache za uchimbaji na biashara ya madini. Uchache wa shughuli za uchimbaji madini ulitokana na uliokuwa uamuzi wa Serikali wa kuhifadhi rasilimali za madini hadi muda ambao Taifa litakuwa limepata utaalamu na kujenga kada ya wataalamu watakaohudumu katika Sekta ya Madini wakiwemo, wanajiosayansi, wahandisi na wataalam wengine muhimu wa kusimamia na kuendesha shughuli za uchimbaji na uchakataji madini kwa ufanisi.

Ndugu Wanahabari, tangu wakati huo, nyenzo za usimamizi sekta ikiwa ni pamoja na Sera na Sheria ya Madini zimekuwa zikifanyiwa marekebisho na maboresho ya mara kwa mara kulingana na uhitaji wa kufanya hivyo, kwa mfano, mwaka 2009 Serikali ilitunga upya Sera ya Taifa ya Madini na kufuatiwa na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Baada ya kuonekana kuwepo kwa changamoto kadhaa, Serikali ilifanya mapitio ya Sheria ya Madini 2010 kwa lengo la siyo tu kuimarisha uwezo wa Serikali kuisimamia Sekta ili iweze kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa, bali pia kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa wachimbaji wadogo kwenye shughuli za madini, kuinua sekta ndogo ya uchakataji madini na vilevile kwa lengo la kufungamanisha Sekta ya Madini na Sekta nyingine za uchumi kwa maendeleo ya Taifa.

Ndugu Wanahabari, mtakumbuka kuwa, Mwaka 2017 yalifanyika marekebisho makubwa katika Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.7 ya mwaka 2017. Pamoja na malengo mengine ya Marekebisho hayo kuliwekwa masharti yatakayowezesha wananchi na Taifa kunufaika zaidi na maliasili ya madini kupitia dhana ya "Permanent Sovereinty over Natural Resources".

Ili kuwezesha kupatikana kwa manufaa hayo, masharti kadhaa yaliingizwa kwenye Sheria ya Madini ya Mwaka 2010; ikiwa ni pamoja na kutambua na kuweka umiliki wa rasilimali madini kwa wananchi chini ya usimamizi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa niaba ya Wananchi na kuweka umiliki wa rasilimali madini kwa Serikali bila kuathiri masharti ya Mikataba iliyoingiwa na makampuni ya uwekezaji.

Mabadiliko hayo pia yalilenga kutambua haki ya ushiriki wa Serikali (Government participation) katika shughuli zote za uchimbaji, uchakataji na uchenjuaji wa madini na umiliki wa hisa kwa asilimia 16 (16% non dilutable free carried interest) katika makampuni ya uchimbaji na Serikali kuwa na Uwezo wa kuongeza ushiriki (Umiliki) mpaka kufikia asilimia 50 kupitia thamani ya vivutio vya uwekezaji na kikodi alivyopewa mwekezaji.

Ndugu Wanahabari, kwa kuzingatia historia hii ya Kisera na Kisheria ambayo nimeileza kwa kifupi sana, utaona kuwa mapinduzi makubwa yamefanyika katika kipindi tangu uhuru mpaka sasa ambapo Serikali imefanya jitihada kubwa za kuhakikisha watanzania wananufaika na rasilimali madini, huku tukishuhudia ongezeko la kasi ya ukuaji wa Sekta. Kwa mfano, sekta ilikua kwa asilimia 17.7% mwaka 2019 na kuwa ya kwanza kwa ukuaji nchini ikilinganishwa na kipindi cha nyuma kabla na baada ya Uhuru. Kwa upande wa mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 5.2 mwaka 2019. Kabla ya kipindi hicho wastani wa mchango wa Sekta kwenye Pato la Taifa ulikuwa takribani asilimia 3. Aidha, mchango wa sekta katika Pato la Taifa uliongezeka hadi kufikia 6.7% mwaka 2020 kutoka 4.8% mwaka 2017. Wakati Mchango wa wachimbaji wadogo wa dhahabu (ASM-Dhahabu) kwenye makusanyo ya maduhuli ya Serikali umeongezeka kutoka 10% mwaka 2017/18 hadi 27% mwaka 2020/21. Wakati katika mwaka 2020 Sekta ya Madini ilichangia asilimia 6.7 kwenye Pato la Taifa, hivi karibuni mchango wa sekta umeongezeka hadi kufikia asilimia 7.7 katika robo ya pili mwaka 2021 (Aprili - Juni). Kwa mwenendo huo huku jitihada za kuifungua Sekta zikiendelea, hakuna shaka kuwa, ifikapo mwaka 2025 mchango wa Sekta ya Madini utafikia asilimia 10 ya Pato la Taifa kama inavyotarajiwa.

Ndugu Wanahabari, Tofauti na miaka iliyopita kabla ya kufanyika kwa mabadiliko ya Sheria ya Madini mwaka 2017, ushiriki wa watanzania katika uchumi wa madini umeongezeka, mathalan, katika kipindi cha Mwaka 2020/2021 jumla ya kampuni za watoa huduma kwenye migodi 961 sawa na 66% zilikuwa ni za kitanzania na idadi ya kampuni za kigeni zilikuwa 506 sawa na asilimia 34. Uwepo wa idadi kubwa ya watoa huduma wa kitanzania umechochewa kwa kiasi kikubwa na usimamizi wa Sheria ya Madini na Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania. Tume ya Madini imekuwa ikisisitiza wamiliki wa leseni za madini kutoa kipaumbele kwa bidhaa au huduma zinazotolewa na watanzania na kuhakikisha kuwa bidhaa au huduma pekee zinazotole

wa na kampuni za kigeni ni zile ambazo hazipatikani nchini.

Aidha, kama bidhaa na huduma zinazohitajika migodini hazipatikani nchini, Kanuni za Ushirikishwaji wa watanzania zimeelekeza kuundwa kwa kampuni ya ubia kati ya kampuni ya Kigeni na Kampuni ya Kitanzania kwa ajili ya kutoa huduma hiyo. Katika ubia huo kampuni ya kitanzania inatakiwa kuwa na walau asilimia 20 ya hisa. Vilevile, katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2021 kumekuwepo na ongezeko la kampuni zenye kuonesha Ushirikishwaji wa Watanzania katika kutoa huduma migodini.

Ndugu Wanahabari, ikilinganishwa na tulipotoka, hivi sasa Taifa letu lina migodi mikubwa 9; (6 ya dhahabu, 1 wa almasi, 1 wa tanzanite na 1 wa makaa ya mawe). Pia ipo migodi takribani 28 ya uchimbaji wa kati na mingine mingi ya uchimbaji mdogo wa dhahabu, almasi, madini ujenzi, madini ya viwandani na ya vito vya thamani.

Kwa upande wa Madini adimu ya Tanzanite ambayo yanapatikana nchini kwetu tu, hivi sasa baada ya kuweka udhibiti mzuri wa madini haya ikiwemo ujenzi wa ukuta wenye urefu wa kilomita 24.5 kuzunguka eneo la migodi ya Mirerani ambao umekuwa na manufaa makubwa kwa Serikali kwa kuongeza mapato ya serikali kutoka shilingi millioni 166 kwa mwaka kabla ya kuwepo ukuta hadi kufikia shilingi bilioni 3.9 baada ya ujenzi wa ukuta. Hivi sasa kama Taifa tunashuhudia uchimbaji na upatikanaji wa madini haya ya kipekee yenye uzito mkubwa na thamani kubwa ambayo haijawahi kutokea katika historia ya uchimbaji wa madini haya. Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uchimbaji na biashara kwa madini haya ili kuhakikisha yanabaki kuwa tunu ya Taifa letu duniani.

Ndugu Wanahabari, yapo mengi ambayo kama Taifa tumefanikiwa kupitia Sekta ya Madini ikiwemo; kupandisha uchumi wa Taifa letu, kuongeza ufanisi wa sekta kupitia maboresho ya sheria, kuanzishwa kwa masoko ya madini, kuongeza uwazi na ushiriki wa watanzania katika sekta ya madini nikitaja kwa uchache. Hivi karibuni ikiwa ni ndani ya kipindi hicho hicho cha miaka 60 ya Uhuru Serikali ilisaini Mikataba ya Ubia na Kampuni ya LZ Nickel ya nchini Uingereza na kuanzisha Kampuni ya Tembo Nickel Corporation Limited yenye Kampuni tanzu mbili ambazo ni Kampuni ya Uchimbaji wa Madini ya Tembo Nickel Mining Company Ltd na Kampuni ya Usafishaji wa Madini ya Tembo Nickel Refinery Company Ltd. Kama mtakumbuka, Leseni hii tuliikabidhi rasmi kwa Kampuni hii tarehe 27 Oktoba, 2021 jijini Dodoma. Mradi huu unatarajia kutengeneza ajira zipatazo 978 na mapato ya Dola za Marekani bilioni 7.54 sawa na shilingi Trilioni 17.35 za kitanzania kwa kipindi chote cha uhai wa mgodi. Mapato hayo yatatokana na gawio la hisa huru za Serikali, tozo na kodi. Sambamba na hilo, pia kutakuwa na ujenzi wa kiwanda cha ubia cha usafishaji Madini ya metali kitakachojengwa Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga ambacho kitakuwa na uwezo wa kusafisha Madini ya metali aina mbalimbali.

Bila ya kusahau, makubaliano kama haya yameipatia nafasi Serikali ya kumiliki Hisa asilimia 16 kupitia Kampuni ya Twiga Minerals baada ya kuwepo makubaliano kati ya Serikali na Kampuni ya Barrick. Mbali na kupata mapato hayo, pia Serikali itanufaika kwa kupata asilimia 50 kwa 50 kama faida itakayopatikana katika kipindi cha uhai wa mgodi. Aidha, Serikali itaendelea kupata umiliki kama huu wa asilimia 16 katika Migodi yote Mikubwa na Kati itakayoanzishwa nchini. Hii ni kwa mujibu wa Sheria kufuatia marekebisho yalifanyika.

Aidha, kupitia Baraza lake la Mawaziri Serikali imetoa ridhaa ya kutolewa kwa Leseni za uanzishwaji wa Mgodi Mpya Mkubwa wa Uchimbaji Dhahabu wa Nyanzanga utakaojengwa kijiji cha Sotta Wilayani Sengerema Mkoani Mwanza na Mgodi Mkubwa wa uchimbaji madini ya Rare Earth Elements utakaojengwa katika kijiji cha Ngwala Mkoani Songwe. Vilevile, ikumbukwe kwamba, muda si mrefu mradi mkubwa wa uchimbaji wa Madini ya Graphite utaanza mkoani Lindi huku tayari Kampuni ya Shanta Gold ikiendelea na ujenzi wa Mgodi wa Kati wa uchimbaji Madini ya Dhahabu wa Singida. Haya ni mapinduzi makubwa na mafanikio kwa Serikali katika kipindi hiki cha miaka 60 ikizingatiwa na historia ya mahali tulipotoka.

Ndugu Wanahabari, kwa ufupi tu nipende kuwaeleza kuwa, nchi yetu inaendelea kufungua shughuli hizi za uchimbaji na biashara ya madini kwani hadi kufikia Septemba 2021, Leseni hai ambazo zimeshatolewa ni za utafutaji wa madini ni 1,044 ni za utafutaji wa madini, leseni 15 za uchimbaji mkubwa, leseni 161 za uchimbaji wa kati, leseni 34,000 za uchimbaji mdogo na leseni 1561 za biashara ya madini. Kutolewa kwa leseni hizi kunamaanisha kwamba, Serikali inaweza kuongeza mapato zaidi kupitia sekta hii ya madini. Mfano halisi ni Mwaka wa Fedha tulioumaliza mwezi Juni mwaka 2021 ambapo Wizara ilikusanya shilingi Bilioni 584.8 sawa na asilimia 111.03 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 524 ambazo Wizara ilipangiwa na Serikali izikusanye.

Ndugu Wanahabari, kufuatia kuanzishwa kwa Masoko ya Madini, Wizara kupitia Tume ya Madini imeendelea kufungua biashara ya madini kwa kuweka mazingira wezeshi na miundombinu rahisi ya kufanya biashara kwa uwazi na ufanisi. Tangu kuanzishwa kwa masoko hayo mwezi Machi, 2019, hivi sasa nchi yetu ina jumla ya masoko ya Madini 42 na Vituo vya Ununuzi wa Madini 59 yaliyoenea katika mikoa mbalimbali. Aidha, kupitia uwepo wa masoko hayo na vituo vya ununuzi, madini yenye thamani ya shilingi trilioni 3.19 yameuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya shilingi bilioni 222.07 kama mrabaha na ada ya ukaguzi tangu kuanzishwa kwake. Ndugu Wanahabari, haya ni Mafanikio makubwa ikilinganishwa na tulipotoka. Ndugu wanahabari, uwepo wa masoko haya na namna yanavyofanya kazi umeifanya Tanzania kuwa mfano kwa nchi nyingi ambazo zimekuwa zikija na nyingine zikiendelea kuomba kujifunza namna Serikali inavyosimamia masoko haya na sekta nzima kwa ujumla.

Ndugu Wanahabari, kwa upande wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), tangu kuanzishwa kwake mnamo Mwaka 1972, hivi karibuni limeweza kufanya mapinduzi makubwa ya kiutendaji, kuimarisha uzalishaji na kujenga misingi mizuri ya kujiendesha kibiashara na kupunguza utegemezi wa moja kwa moja kwa Serikali. Kufuatia kuingia ubia na

wawekezaji kwa niaba ya serikali, Shirika hili limepunguza utegemezi kutoka asilimia 100 mwaka 1972/73 hadi asilimia 22 Mwaka 2021. Aidha, kipindi cha hivi karibuni Shirika limeongeza kasi ya kupunguza utegemezi, mathalani utegemezi wa Shirika umepungua kutoka asilimia 69.7 ya mwaka wa fedha 2018/19 hadi asilimia 22 kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Ndugu Wanahabari, haya ni mapinduzi makubwa kwa STAMICO wakati Taifa likifikia kipindi hiki cha miaka 60 ya uhuru. Ni jambo linalotia moyo sana kuona kuwa wakati ilifika mahali ambapo Bunge na Serikali ilitaka kulifuta shirika hili, hivi sasa STAMICO ni shirika linalofanya vizuri hadi kufikia hatua ya kuongeza wigo wa kutoa huduma ikiwa ni pamoja na kupata kandarasi za uchorongaji katika migodi mikubwa hapa nchini ikiwemo mgodi wa Geita ( Geita Gold Mine(GGM), Mgodi wa Buckreef na kwa Kampuni ya Uendelezaji wa Nishati ya Jotoardhi (TGDC) zenye jumla ya thamani ya bilioni thamani ya Shilingi bilioni 20. Aidha, kama mnavyofahamu hivi karibuni kimefunguliwa Kiwanda kikubwa cha kwanza nchini cha Kusafisha dhahabu cha Mwanza Precious Metals Refinery kiwanda ambacho ni cha Ubia kati ya Serikali kupitia Shirika la STAMICO na wabia kutoka Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Singapore. Kiwanda hiki cha kisasa Afrika Mashariki na Kati, kinasafisha dhahabu kwa kiwango cha Kimataifa cha 999 purity na uwezo wa kusafisha kilo 480 kwa siku, kiwanda hiki kinaweza kupanuliwa na kufikia kusafisha hadi kilo 960 kwa siku kulingana na upatikanaji wa dhahabu. Katika mradi huu, STAMICO ina hisa asimilia 25 na wabia wanamiliki asilimia 75 za hisa. Hisa za STAMICO zitakuwa zinaongezeka kwa asilimia 5 kila baada ya miaka miwili hadi zitakapofikia asilimia 51 na wabia asilimia 49. Ongezeko hilo la hisa halitakuwa na gharama yoyote kwa STAMICO.

Ndugu Wanahabari, utaona kwamba hivi sasa shirika hili linafanya vizuri ambapo kutokana na faida katika vyanzo vyake vya fedha. STAMICO imefanikiwa kutoa Serikalini jumla ya Shilingi bilioni 3.3 zikijumuisha Shilingi bilioni 1.2 za gawio kwa mwaka wa fedha 2020/21 na mchango Serikalini ya jumla ya Shilingi bilioni 2.1 kwa kipindi cha miaka miwili (2) mfululizo.

Aidha, Serikali kupitia Shirika hili mwaka 2014, lilianzisha kampuni tanzu iitwayo STAMIGOLD Company Limited ili kuendesha na kusimamia Mgodi wa Dhahabu wa Biharamulo. Mgodi wa STAMIGOLD ulichukuliwa na Serikali rasmi tarehe 15 Novemba, 2013 kutoka kwa kampuni ya Pangea Minerals Limited (PGM) baada ya kampuni hiyo kuurejesha mgodi kwa Serikali. Uhamishaji huu ulijumuisha mitambo ya uchenjuaji, maeneo ya uchimbaji, mining camp, na leseni ya uchimbaji Special Mining Licence. Kwenye mradi huu, STAMICO inamiliki hisa asilimia 99 na Ofisi ya Msajili wa Hazina inamiliki Hisa asilimia 1. Hivyo, katika Mgodi huu, Serikali ina umiliki wa asilimia 100 na unasimamiwa na watanzania. Tangu kuanzishwa kwake, mgodi umezalisha ajira kwa vijana wa Kitanzania zaidi ya 600 ikijumuisha Watumishi walioajiriwa na Mgodi moja kwa moja na watoa huduma za kandarasi mbalimbali.

Ndugu Wanahabari, kama mnavyofahamu shughuli za uchimbaji zinakwenda sambamba na utunzaji wa mazingira. Katika kuliona hilo, Shirika limeanza maandalizi ya awali ya mradi wa kuzalisha makaa ya mawe kwa matumizi ya majumbani (Coal Briquettes). Katika hatua ya awali Shirika litaanza na mtambo wenye uwezo wa kuzalisha tani 2 kwa saa (2tph) kufuatia kukamilika kwa majaribio ya awali ambayo yameonesha matokeo chanya. Mradi huu wa majaribio utakuwa katika eneo la TIRDO Jijini Dar es Salaam. Mradi huu wa majaribio unatarajia kuliingizia Shirika kiasi cha Shilingi Milioni 750 kwa mwaka 2021/22.

Ndugu Wanahabari, Pia, STAMICO inao mradi mwingine wa Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef na mbia mwenza Kampuni ya TANZAM 2000 ambao wanamiliki mradi wa uchimbaji madini ya dhahabu wa Buckreef mkoani Geita chini ya kampuni ya ubia ya Buckreef Gold Company (BGC). Katika Ubia huu Shirika linamiliki hisa asilimia 45 na mbia asilimia 55. Tayari Shirika limefanya uzalishaji wa majaribio ya uchenjuaji kwa mtambo wa tani 5 (tph) ambapo jumla ya Kilogramu 21.5 zimezalishwa na kuupatia mgodi kiasi cha Shilingi bilioni 3.69 katika kipindi cha Mwaka 2020/21.

Ndugu Wanahabari, vilevile, mwezi Julai 2014 STAMICO ilianza rasmi ununuzi wa madini ya bati wilayani Kyerwa kupitia Kampuni yake Tanzu ya Kyerwa Tin Company Ltd (KTCL). Hii ilifuatia utekelezaji wa Agizo la Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, wakati wa ziara yake mkoani Kagera mwishoni mwa mwaka 2013, kuwa STAMICO waanze ununuzi wa madini ya bati kutoka kwa wachimbaji wadogo wilayani Kyerwa. Lengo kuu la mradi huu ni kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini ya bati katika vijiji vya Kabingo, Murongo, Syndicate na Rugasha kupata soko la uhakika la madini ya bati. Aidha, ikumbukwe kuwa kama sehemu ya kuimarisha udhibiti wa biashara haramu na utoroshwaji wa madini ya Tin, Tantalum na Tungsten (3Ts), mwaka 2020 Tanzania ilipatiwa ithibati ya kutoa cheti cha uasilia kwa madini hayo baada ya Wizara kukamilisha taratibu za utoaji wa cheti hicho kwa mujibu wa makubaliano ya nchi wanachama wa ukanda wa Maziwa Makuu – (International Conference on the Grat Lakes Region-ICGLR)

Ndugu Wanahabari, kwa mmantiki hii hivi sasa tunajivunia Shirika hili kwani limepiga hatua kubwa za kimapinduzi, hivi sasa STAMICO ina jumla ya Leseni 50 za utafiti na uchimbaji wa madini. Kati ya leseni hizo, kumi na nne (14) zipo kwenye ubia (Buckreef 13 na TML 1), kumi na moja (11) zipo kwenye Kampuni Tanzu ya STAMIGOLD inayomilikiwa na Serikali. Aidha, Shirika lenyewe linamiliki kwa asilimia mia moja (100%) leseni zaidi ya ishirini za uchimbaji madini ikiwa ni pamoja na leseni mpya (Strate

gic License) za uchimbaji madini ambazo ni; Leseni ya Uchimbaji Dhahabu – Ikizu, Bunda Mara; Leseni ya Uchimbaji Dhahabu – Kigosi, Ushirombo Shinyanga; Leseni ya Uchimbaji Shaba - Chengube, Mwanga Kilimanjaro; na Leseni moja ya Makaa ya Mawe - Ilima, Songwe.

Ndugu Wanahabari,Tukiangazia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), hii ni taasisi kongwe na yenye uzoefu mkubwa katika masuala ya utafiti wa madini (mineral explorations) na uratibu wa majanga asili ya jiolojia katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Taasisi hii ilitokana na idara kongwe ya Serikali ya Mwingereza iliyojulikana kama Idara ya Jiolojia na iliyoanzishwa rasmi tokea Mwaka 1925. Kuanzishwa kwa GST kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko yaliyokuwa yanatekelezwa na Serikali ikiwa ni juhudi za kuvutia wawekezaji katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Madini.

Kwa kipindi cha miaka 60 ya uhuru (GST) mpaka sasa imefanikiwa kutambua jiolojia ya nchi nzima kwa asilimia 96. Ikiwa sehemu ya juhudi za kuimarisha upatikanaji, utunzaji na usambazaji wa taarifa, GST imefanikiwa kuboresha mfumo wa usambazaji wa taarifa/takwimu za jiosayansi. Uanzishwaji wa mifumo hii umerahisisha kwa kiasi kikubwa upatikanaji na usambazaji wa taarifa hizi kwa wadau.

Pamoja na mafanikio hayo, GST kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imefanikiwa kufanya tafiti mbalimbali katika Sekta ya Madini na jiosayansi, ambazo ni ukamilishaji uandaaji wa Ramani za jiokemia za nchi nzima (Country Wide Mult-Element Geochemical Maps) zinazoainisha wingi wa madini ya aina mbalimbali za metali (k.m. dhahabu, shaba, chuma, nikeli, bati n.k.) yanayopatikana katika sehemu mbalimbali za nchi. Kazi hii imefanywa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ambao ni Geological Survey ya Finland na Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA).

Ndugu Wanahabari, GST imefanikiwa kufanya tafiti kwenye madini mkakati ya Gesi ya Helium ambapo utafiti huo umeibua maeneo mapya kwenye ukanda wa kaskazini tofauti na ilivyozoeleka kuwa helium hupatika maeneo ya kusini. Kwa mujibu wa taarifa za kitafiti za gesi hiyo, Tanzania ina kiasi cha futi za ujazo bilioni 54 za gesi hiyo ambacho kinaizidi nchi ya Marekani yenye hazina ya futi za ujazo bilioni 24.2.

Kutokana na kuboreshwa kwa vifaa na miundombinu ya Maabara ya GST, sasa inaendeshwa kwa kufuata viwango vya kimataifa vya ISO 17025:2017 na ilipata ithibati (ACCREDITATION) katika viwango hivyo kutoka Shirika la Viwango la Kimataifa la SADCAS. Hivyo, matokeo ya uchunguzi unaofanywa na maabara ya GST yanakidhi viwango vya kimataifa. Aidha, katika juhudi za kuinua Sekta ya Kilimo nchini, GST imefanikiwa kuandaa Ramani inayoonesha viwango vya ubora wa PH (pH values) kwenye udongo, ramani inayohusisha maeneo ya nchi nzima imechorwa/imetengenezwa. Ramani hiyo inaonesha maeneo yenye PH ndogo na kubwa. Pamoja na hayo, GST imewasogezea huduma za maabara wachimbaji wadogo kwa kufungua ofisi ndogo katika maeneo zinakofanyika shughuli za uchimbaji mdogo wa madini kwa wingi, hivi karibuni tumeshuhudia ufunguzi wa ofisi ya GST mkoani Geita.

Ndugu Wanahabari, sambamba na mafanikio haya, GST inaamini kuwa upatikanaji wa taarifa sahihi za jiosayansi kupitia tafiti mbalimbali kutawezesha ufikiwaji wa azma ya Serikali kwa Sekta ya Madini kufikia asilimia 10 katika kuchangia Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025.

Ndugu Wanahabari, kama mnavyofahamu kwamba shughuli za madini pia zinaongozwa na Sheria za Kimataifa zinazosimamia masuala ya uwazi na uwajibikaji kwa kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Sheria hizi zinaitaka Serikali kuwajibika kwa wananchi wake kuhusu uwajibikaji wa kampuni zinazojishughulisha na masuala ya uziduaji.

Kifungu cha 16 cha Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika rasilimali madini, mafuta na gesi asilia ya mwaka 2015 (TEITA, 2015) kinaitaka Kamati ya TEITI kumuwezesha Waziri mwenye dhamana, kuweka wazi mikataba na leseni zilizoingiwa na kutolewa na Serikali katika Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

Katika kuweka wazi kwa Umma Ripoti za Ulinganishi wa Malipo ya Kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na Mapato ya Serikali, hadi sasa Tanzania imechapisha na kutoa ripoti kumi na moja kwa kipindi cha Julai 1, 2008 hadi Juni 30, 2019 zinazolinganisha kodi na malipo mengine yaliyofanywa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia kwa Serikali Kuu na katika Halmashauri ambazo zinapokea tozo (service levy) kutoka kwenye makampuni yanayojishughulisha na shughuli za uziduaji. Ripoti hizo zinaonyesha kuwa Serikali imeshapokea kiasi cha jumla ya dola za Marekani bilioni U$ 3.78 kutoka katika kampuni zilizofanyiwa ulinganishi wa fedha zilizolipwa na makampuni hayo na fedha zilizopokelewa na Serikali.

Ndugu Wanahabari, kama mnavyofahamu kuwa, msisitizo wa Serikali hivi sasa ni masuala ya Uongezaji Thamani Madini. Suala hili linakwenda sambamba na utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 1997. Pia, Serikali kupitia Sera ya Madini ya Mwaka 2009, iliazimia kuongeza manufaa yatokanayo na Sekta ya Madini na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini hapa nchini. Hivyo, kupitia Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) kilichoanzishwa Mwaka 2003, Serikali inatoa mafunzo ya uongezaji thamani madini katika taaluma mbalimbali za Sekta hii kwa ngazi mbalimbali. Aidha, kupitia mfuko mdogo wa maonesho ya Madini ya Vito Arusha (Arusha Gem Fair) Wizara kwa kushirikiana na wafanyabiashara wa madini ilianzisha mfuko wa kusomesha wanafunzi wa kike ambapo kwa mara ya kwanza Mwaka 2014 jumla ya wanafunzi 15 walidahiliwa kusoma lapidary. Serikali iliendelea na jitihada za kuzalisha wataalam wa ndani kwa kuleta mtaalam mwelezi kutoa mafunzo hayo kutoka nje ya nchi ikiwemo kuwapeleka wataalam katika nchi

mbalimbali kujifunza masuala hayo. Tangu kuanza kutolewa mafunzo hayo, jumla ya wanafunzi 221 wamehitimu mafunzo katika chuo hicho na 117 wanaendelea kupata mafunzo.

Ndugu Wanahabari, faida za mafunzo ya uongezaji thamani madini nchini ni pamoja na kupata wataalam wazawa wengi waliobobea katika masuala ya uongezaji thamani madini, kuchochea shughuli za uongezaji thamani madini nchini, kutoa fursa za ajira kwa watanzania, kupunguza utegemezi wa wataalam kutoka nje ya nchi na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa.

Ndugu Wanahabari, usimamizi wa Sekta ya Madini umechukua sura mpya miaka ya hivi karibuni baada ya Serikali kuanzisha utaratibu wa kukutana na wadau wa sekta kwenye Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini unaofanyika kila mwaka mwezi Februari. Mikutano hii inatangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika Sekta ya Madini, kuifungamanisha Sekta ya Madini na sekta nyingine za kiuchumi, inasaidia katika kubadilishana uzoefu wa kusimamia na kuendesha shugghuli za madini na nchi nyingine duniani, inafungua wigo wa wachimbaji wadogo wa madini kupata wabia wa kushirikiana katika shughuli za uwekezaji katika Sekta ya Madini na zaidi kujadili na kutatua kwa pamoja changamoto wanazokutana nazo wadau na wawekezaji katika Sekta ya Madini.

Ndugu Wanahabari, kupitia hadhara hii nipende kuwaalika wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye Sekta ya Madini kwani fursa za kibiashara zipo za kutosha na Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuwawezesha kufanya kazi zao kwa amani na usalama. kutoka ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye Sekta ya Madini kwani fursa za kibiashara zipo za kutosha na Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuwawezesha kufanya kazi zao kwa amani na usalama. Tanzania bado ina hazina kubwa ya rasilimali madini ambayo haijaguswa na inahitaji uwekezaji. Hadi sasa tumeyafikia madini yetu kwa asilimia 10 tu ikilinganishwa na utajiri uliopo ardhini hapa nchini kwetu. Kwa Taasisi za kifedha, nipende kuwashukuru kwa kutuelewa na kuanza kufanya kazi na Sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Bado natoa wito kwa taasisi za kifedha kuendelea kujifunza kuhusu sekta hii ili hatimaye tuweze kushirikiana katika kuwainua wachimbaji hususan wachimbaji wadogo hapa nchini ili hatimaye waweze kukua. Wachimbaji wadogo wanahitaji mitaji na vifaa ili wachimbe kwa tija, na sisi Serikali tunawahitaji wachimbaji kwa mustakabali wa ukuaji na maendeleo ya Sekta hii kwani juhudi na mchango wao katika kuchangia mapato ya Serikali unaendelea kukua na sasa unaonekana bayana. Vilevile, tunawahitaji wachimbaji wa kati na wachimbaji wakubwa katika kuchangia ukuaji wa viwanda, kwa uchumi imara na maendeleo endelevu ya Taifa letu kupitia sekta hii, hawa wote wanahitaji huduma na uhakika wa upatikanaji wa mitaji.

lengo letu kama Serikali kupitia Wizara hii ya Madini ni kuifanya Tanzania kuwa Kitovu "Hub" ya Madini Afrika na hatimaye duniani. Uwezo na sababu hizo tunazo kutokana na wingi wa rasilimal madini tulizonazo ikiwemo usimamizi madhubiti wa sekta ambao unaongozwa na Sheria zetu.



**MAFANIKIO YA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KATIKA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA**

Ndugu Wanahabari, Disemba 2021 nchi yetu inaadhimisha miaka 60 ya Uhuru tangu tarehe 09 Desemba, 1961 tulipoanza kujitawala hivyo, maadhimisho haya ni tofauti na miaka mingine kutokana na haja ya kutafakari kwa pamoja tulikotoka, tulipo na tunakoelekea. Maadhimisho haya yanaongozwa na Kaulimbiu isemayo "MIAKA 60 YA UHURU; TANZANIA IMARA, KAZI IENDELEE".

Tangu mwaka 1961, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekuwa ikitekeleza Sera, Miongozo na Sheria mbalimbali kulingana na maboresho ya muundo wa wizara kwa wakati husika. Kufikia mwaka 2016 Wizara mbili ziliunganishwa ambazo ni Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, hivyo kutengeneza Idara Kuu ya Afya inayoshughulikia masuala yote ya Afya na Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii inayoshughulikia Masuala yote ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee, Watoto na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Ndugu Wanahabari, huduma za tiba ya magonjwa pamoja na maendeleo ya jamii zimekuwepo kwa karne nyingi huku huduma za tiba ya asili zikiitangulia tiba ya kisasa. Aidha, baada ya karne ya 10 huduma ya tiba za kigeni iliingizwa na wafanyabiashara wa Kiarabu, Kireno, Kifaransa, n.k. Hata hivyo, Tiba asili na tiba mbadala pamoja na tiba ya kisasa zimeendelea kutolewa hadi sasa karne ya ishirini na moja. Aidha, maendeleo makubwa katika huduma za afya na maendeleo ya jamii yamejitokeza zaidi baada ya uhuru na katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru ukilinganisha na kipindi cha takribani miaka 71 ya ukoloni (Utawala wa Wajerumani, 1889 -1916 na Utawala wa Waingereza, 1916 – 1960).

Napenda kuanza kuangazia huduma za afya kabla ya Uhuru; kabla ya uhuru makabila yote 126 yalitumia tiba asili katika kutibu na kujikinga na magonjwa na kwa mara ya kwanza huduma za tiba za kigeni (Western Medicine) ziliingizwa nchini mwaka 1887 na kuanza kutolewa mwaka 1889-1916 na wamisionari kipindi cha utawala wa wajerumani. Vilevile, huduma za kinga hususan Chanjo ya Ugonjwa wa Ndui ilianza kutolewa kwa mara ya kwanza mwaka 1891. Hata hivyo, bado tiba asili iliendelea kuwepo hata wakati wa Utawala wa Mkoloni (Ujerumani na Uingereza) huku baadhi ya huduma za tiba asili zikipigwa marufuku na nyingine kuruhusiwa baada ya kukidhi masharti ya Mkoloni. Aidha, zile zilizopigwa marufuku ni zile zilizohusishwa na imani za kishirikina au uchawi. Kutokana na changamoto hizo, mwaka 1928 Sheria ya kwanza ilitungwa ya kuruhusu uhusishwaji wa tiba asili katika kutoa matibabu na kuwakinga wananchi.

Ndugu Wanahabari, huduma za afya za kisasa zilizokuwa zinatolewa wakati huo zilikuwa ni pamoja na Malaria, Chanjo ya Ndui, huduma za afya dhidi ya Tauni, Malale, Ukoma na Magonjwa ya akili. Hata hivyo, huduma hizo zilikuwa zikitolewa zaidi kwa Watumishi wa Serikali ya Kijerumani, Wafanyabiashara na Askari wa Kiafrika huku Vituo vya kutolea huduma hizo za tiba vikijengwa zaidi katika miji na makazi ya wajerumani na hospitali ya kwanza ikijengwa Mamboya, Mpwapwa.

Kwa kifupi, upatikanaji wa huduma za afya za kigeni au kisasa enzi hizo haukuwa na usawa kwa wote (equity) na huduma zilikuwa chache na mbali na wananchi walio wengi.

Ndugu Wanahabari, sura hii ya huduma za afya iliendelea hivyo hata baada ya vita Kuu ya Kwanza ya Dunia mwaka 1914 ambapo, nchi ya Tanganyika ilitawaliwa na Mwingereza kuanzia mwaka 1916-1960. Ni katika kipindi hicho ambapo, huduma za tiba zilizidi kuendelezwa kwa kiasi kikubwa huko huko maeneo ya mijini ikilinganishwa na maeneo ya vijijini huku zikitoa kipaumbele kwenye tiba zaidi kuliko kinga licha ya uwepo wa idara ya tiba na usafi kwa ajili ya afya ya jamii. Kwa upande Mwingine, watumishi wa afya waliongezeka kwa idadi na aina ya kada zikiwemo madaktari wa kigeni, matibabu (medical assistants), watoaji dawa (dispensers), wasaidizi maabara (African Laboratory assistants), wahudumu wa tiba (medical auxiliaries), wafunga vidonda (tribal dressers), wakaguzi wa usafi (urban sanitary inspectors), wauguzi, n.k

Aidha, juhudi zingine katika uboreshaji wa huduma za afya zililenga katika upatikanaji wa maji, huduma za utupaji taka, kuangamiza mazalia ya mbu huku vituo vingi vya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na hospitali vikijengwa.

Ndugu Wanahabari, Vita Kuu ya Pili ya Dunia iliyoanza mwaka 1939 ilirudisha nyuma maendeleo ya huduma za kijamii ikiwemo huduma za afya zilizokuwa zinasimamiwa na Wizara ya Afya na Kazi huku huduma hizo zikitolewa zaidi kwa wageni waliokuja nchini, hususan watumishi wa utawala wa kikoloni, wafanyabiashara na askari. Kwa hali hii ilikuwa vigumu kwa wananchi walio vijijini kupata huduma hizo. Aidha, katika kipindi hicho, kulikuwepo na uchache wa raslimali za kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya hasa watumishi, dawa, vifaa tiba na vituo vya huduma.

Ndugu Wanahabari, zifuatazo ni baadhi ya takwimu za hali ya upatikanaji wa raslimali kwa ajili ya huduma za afya kabla ya uhuru;

1. Idadi ya hospitali na zahanati kwa pamoja ilikuwa 1,343 zikiwa na jumla ya vitanda 18,832.

2. Aidha, hadi kufikia mwaka 1960 kulikuwa na hospitali kubwa 12 tu zikiwa na jumla ya vitanda 3,046. Kati ya hospitali hizo, Saba (7) zilikuwa zinamilikiwa na Serikali, Nne (4) Mashirika ya Kidini na Hospitali moja (1) binafsi. Hospitali hizo zilikuwa katika maeneo ya Dar es Salaam (Jimbo Mashariki), Tanga (Jimbo la Tanga), Moshi (Jimbo la Kaskazini), Peramiho (Jimbo la Kusini), Mwanza (Jimbo la Ziwa), Tabora (Jimbo la Magharibi), Morogoro (Jimbo Mashariki), Bumbuli (Jimbo la Tanga), Ifakara (Jimbo la Mashariki), Dodoma (Jimbo la Kati), Ndanda (Jimbo la Kusini) na Sumve (Jimbo la Ziwa).

3. Uwiano wa wagonjwa kwa vitanda ulikuwa ni kitanda 1 kwa kila watu 1,000 (1:1000). Ikumbukwe, hadi kufikia mwaka 1956 kulikuwa na uwiano wa vitanda 0.6 kwa kila watu 1,000 chini ya lengo la kitanda 1 kwa kila watu 1,000.
4. Uwiano wa vituo vya afya kwa idadi ya watu ulikuwa kituo cha afya 1 kwa watu 40,000 au 50,000.

5. Aina ya watumishi kwenye vituo hivyo ulikuwa:

a. Mganga Msaidizi mmoja (1),
b. Mkaguzi wa Afya mmoja (1),
c. Wakunga kijijini wawili (2),
d. Wauguzi wawili (2),
e. Mhudumu wa Afya mmoja (1), na
f. Watumishi wa kawaida wawili (2).

6. Watumishi waliofuzu shahada ya udaktari walikuwa 400 tu huku watanzania wazawa wakiwa chini ya 20.

7. Jumla ya madaktari waliosajiliwa na wenye leseni na kufanya kazi hadi mwaka 1961 walikuwa 403 tu (182 walikuwa katika vituo binafsi; 140 wakiwa serikalini; na 81 waliajiriwa na Mashirika ya Afya ya Kujitolea). Aidha, jitihada za kuongeza watumishi zilifanyika katika kipindi cha miaka 5 ya mwisho katika kipindi cha ukoloni wa Waingereza.

Ndugu Wanahabari, kwa mara ya kwanza mwaka 1960 zilianzishwa huduma za kinga kwa njia ya chanjo kwa watoto. Katika kipindi hiki Mashirika ya Kujitolea yalitoa mchango mkubwa katika utoaji wa huduma za mama na mtoto huku mama 1 kati 6 ndiye aliweza kupata huduma za uzazi kutoka kwa mtumishi wa afya aliyepata mafunzo.

Hadi kufikia Desemba 1961 hali ya utumiaji wa huduma za Mama na Mtoto ilikuwa kama ifuatavyo;-
Jumla ya Kliniki zilifikia 412 ambazo zilikuwa chini ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Kujitolea na ziliweza kutoa huduma za Kiliniki kwa jumla ya wajawazito 177,214.
1. Serikali Kuu ilikuwa ikimiliki Kiliniki 71 ambapo mahudhurio ya kwanza kwa mama wajawazito yalikuwa 48,667,

2. Serikali za Mitaa ilikuwa ikimiliki Kiliniki 204 ambapo mahudhurio ya kwanza ya Mama Wajawazito walikuwa 68,601; na

3. Mashirika ya kujitolea yalikuwa yakimiliki Kiliniki 137 ambapo akinamama wajawazito 59,946 walihudumiwa.

Ndugu Wanahabari, kipindi hicho (Disemba, 1961) pia kulikuwa na Kliniki za watoto zipatazo 454 ambapo;

1. Serikali Kuu ilimiliki 69 na watoto 29,715 walihudhuria hudhurio la kwanza;

2. Serikali za Mitaa ilimiliki Kiliniki 195 na watoto 52,635 walihudhuria hudhurio la kwanza; na

3. Mashirika ya kujitolea yalikuwa yakimiliki Kiliniki 137 ambapo akinamama wajawazito 59,946 walihudumiwa.

Ndugu Wanahabari, kipindi hicho (Disemba, 1961) pia kulikuwa na Kliniki za watoto zipatazo 454 ambapo;
1. Serikali Kuu ilimiliki 69 na watoto 29,715 walihudhuria hudhurio la kwanza;

2. Serikali za Mitaa ilimiliki Kiliniki 195 na watoto 52,635 walihudhuria hudhurio la kwanza; na

3. Mashirika ya Kujitolea yalimiliki Kiliniki 190 ambapo watoto 54,154 walihudhuria udhurio la kwanza.
Kwa ujumla wake Kliniki hizi za watoto ziliweza kutoa huduma za Kiliniki 136,504 tu.

Ndugu Wanahabari, endeshaji wa huduma za Afya Serikali Kuu ulikuwa katika ngazi tatu ambazo ni Wizara, Mkoa na Wilaya. Huduma za afya ziliendeshwa chini ya Wizara ya Afya na Kazi na Kiongozi Mkuu alikuwa Mganga Mkuu wa Serikali akiwa na wasaidizi wa aina tatu: Madaktari Waandamizi (Principal Medical Officers) 3; Muuguzi Mkuu (Principal Matron), na Mkaguzi Mkuu wa Afya (Chief Health Inspector). Huduma maalumu zilizosimamiwa zilikuwa: Mafunzo (Medical training); Huduma za maabara na dawa (pathology and pharmaceutical services); Huduma za afya ya akili (psychiatric services); na Vitengo maalumu: Malaria, Elimu ya Afya na Lishe.

Ndugu Wanahabari, sasa naomba nijielekeze kwenye hali ya Huduma za Afya baada ya Uhuru wa Desemba 9, 1961; tunapotimiza miaka 60 tangu kupatikana kwa Uhuru tunashuhudia mabadiliko na mafanikio makubwa ya maendeleo kwenye huduma za afya ukilinganisha na kabla ya uhuru.

Maendeleo au mafanikio haya yametokana na msingi mzuri na thabiti uliowekwa na Rais wa kwanza na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambapo alielekeza nguvu za Taifa katika kukabiliana na adui watatu wakubwa, yaani Ujinga, Umaskini na Maradhi huku viongozi wengine wa taifa hili awamu zote wakiendelea kupambana kutimiza ndoto hizo. Vilevile, mafanikio hayo yametokana kazi kubwa ya Serikali za Chama cha Mapinduzi na Ilani zake nzuri awamu zote sita za uongozi zilizowezesha kupata Marais mahiri na wenye uthubutu, kuwa na utashi wa kisiasa kwenye maendeleo nyakati zote, kuunda Serikali zenye uongozi bora na kupata Sera nzuri za Afya.
Pia, mafanikio haya yametokana na uboreshwaji wa ushirikiano na mashirika ya dini na binafsi, wadau wa maendeleo ikiwa ni pamoja wananchi wa taifa hili kwa ujumla wake.

**Kwa ujumla wake, mazingira haya yamewezesha utekelezaji wa masuala ambayo huko nyuma yalikuwa yanaoneka kama ndoto.**

Ndugu Wanahabari, mafanikio ya miaka 60 baada ya uhuru ni mengi na ni vigumu kuyaeleza kinagaubaga na kumaliza hivyo nitafupisha kwenye maeneo muhimu kama ifuatavyo; miaka 60 baada ya uhuru;-

1. Idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya ngazi zote imeongezeka hadi kufikia vituo 8,537 ikilinganishwa na vituo 1,343 Mwaka 1960. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 84.26. Aidha, kati ya vituo hivyo, Serikali inamiliki asilimia 64, Mashirika ya dini asilimia 9 na vituo binafsi asilimia 27.

2. Mtandao wa vituo vya huduma za afya umepanuka na kusogea karibu zaidi na wananchi ambapo; zahanati ni 7,242; vituo vya afya 926; na Hospitali za Wilaya ni 178, Hospitali zingine ni 151. Aidha, hospitali za kibingwa ngazi ya mikoa ni (28), ngazi ya Kanda Sita (6), hospitali za ubingwa maalumu ni Tano (5) na hospitali ya taifa ni moja (MNH).

3. Vituo vyote hivi vina jumla ya vitanda 90,488 ikiwa ni sawa na ongezeko la vitanda 71,656 sawa na asilimia 79.18. Kwa sasa uwiano wa vituo kwa idadi ya watu ni kituo kimoja kwa watu 6,751.5 (1: 6,751.5) tofauti na 1:40000-50000 kabla ya uhuru. Hivyo, Tanzania imefikia malengo ya umoja wa mataifa katika upatikanaji wa huduma za afya kwa kuzingatia idadi ya watu na jiografia.

4. Aidha, uwiano wa vitanda kwa idadi ya watu ni kitanda kimoja kwa watu 637 (1:637) ukilinganisha na 1:1000 kabla ya uhuru. Hadi mwaka 2020 uwiano wa wagonjwa kwa vitanda umekuwa kitanda kimoja kwa watu 19 (1:19).

5. Idadi ya watumishi na wigo wa kada za wataalamu kwenye vituo vya huduma umepanuka kiasi kwamba hivi sasa vituo vya afya vinafanya hadi huduma za upasuaji mkubwa ambao awali ulikuwa haufanyiki.

6. Idadi ya wataalamu wa baadhi ya kada mbalimbali za msingi kwenye afya waliosajiliwa imeongezeka hadi kufikia zaidi takribani 71,365 na usajili unaendelea kila siku. Hawa ni baadhi tu ya kada zinazojumuisha madaktari bingwa, wa kawaida, wauguzi, wataalamu wa maabara, mionzi, wafamasia na mionzi. Kabla ya uhuru wote hawa kwa ujumla walikuwa 435 tu. Hii ni hatua kubwa sana.

7. Hadi kufikia Juni, 2021 huduma za chanjo zimepanuka na kuimarika na kufanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazotekeleza kwa ufanisi eneo hili hususan chanjo za watoto chini ya mwaka mmoja (1) huku utekelezaji ukiwa umefikia asilimia 101. Aidha, kila kituo cha huduma za afya kina huduma ya chanjo kwa ajili ya Kinga ya ugonjwa wa Polio (OPV3), PENTA-3 kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya Dondakoo, Kifaduro, Pepopunda (tetanus), homa ya ini na homa ya uti wa mgongo na chanjo ya Surua/ rubella.

8. Idadi ya Kliniki za afya ya uzazi imeongezeka na sera ni kuwa katika kila kituo cha huduma za afya kuwe na huduma za afya ya uzazi na mtoto.

9. Mifumo ya uongozi na uendeshaji wa vituo vya huduma za afya imeboreshwa kiasi kwamba wananchi nao ni sehemu ya bodi za ushauri, uendeshaji na kamati za ushauri na uendeshaji kuanzia hospitali za kitaifa hadi zahanati. Hii ni pamoja na taasisi zote katika sekta ya afya. Hivyo, mipango, utekelezaji na tathmini vinafanywa siyo na wataalamu tu bali na wananchi wenyewe, fedha za mipango ya maendeleo na uendeshaji kwenye sekta ya afya sasa zinapelekwa moja kwa moja kwenye akaunti za vituo zinazosimamiwa na wananchi wenyewe (DHFF kwa ajili ya uendeshaji na kwa miradi ya ujenzi kupitia Force Account). Maendeleo haya ni makubwa yanahitaji kusimuliwa kwa sauti kubwa na kukumbukwa daima huku tukijivunia, kuyafurahia na kuyaenzi.

Ndugu Wanahabari, Hata sasa serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kazi ya kuboresha huduma za afya inaendelea kwa kasi kubwa Kama mlivyosikia hivi karibuni, juhudi za Mheshimiwa Rais katika kupambana na madhara ya UVIKO-19 zimewezesha Nchi kupata mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Kimarekani milioni 567.25 sawa na Shilingi trilioni 1.362 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) ambapo, tarehe 10/10/2021 wakati akizindua kampeni ya Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19 alitenga Shilingi Bilioni 466.781 (34%) kwa ajili ya Sekta ya Afya ziende;

1. Kuimarisha huduma za dharura, wagonjwa mahtuti na wanaohitaji uangalizi maalum; itakayogharimu Shilingi bilioni 254.4.

2. Kuimarisha huduma za maabara, mionzi na tiba mtandao; itakayogharimu Shilingi bilioni 111.5

3. Kuimarisha huduma za chanjo dhidi ya UVIKO - 19 na elimu ya afya kwa umma dhidi ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo; itakayogharimu Shilingi bilioni 43.2

4. Kuimarisha miundombinu katika vituo vya kutolea huduma za Afya; itakayogharimu Shilingi bilioni 41.8

5. Kufanya tafiti za kitaalam kuhusu Virusi vya Korona pamoja na kuwajenga uwezo watoa huduma za Afya; itakayogharimu Shilingi bilioni 15.9.

Hii ni kudhihirisha kuwa, mapambano dhidi ya adui maradhi bado yanaendelea hata kwenye serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi makini wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa JMT.
Ndugu Wanahabari, mapambano haya miaka kadhaa iliyopita baada ya uhuru yalipelekea kuzaliwa kwa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM-2007-2017) uliochangia;
1. Kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya nchi nzima;

2. Kupungua kwa vifo vya watoto;

3. Kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vyote;

4. Kuongezeka kwa udahili  wa wanafunzi;

5. Kuongezeka kwa ajira ya wataalam waliopelekwa katika ngazi zote za vituo vya kutolea huduma katik Halmashauri, Mikoa, Kanda na Taifa.

Vilevile, mapambano dhidi ya adui maradhi baada ya uhuru yaliifikisha nchi kwenye kuanzishwa kwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ambapo kama nilivyosema awali hivi sasa tunazo hospitali 12 za ubingwa daraja la juu zinazotoa huduma ikiwemo;

1. Upasuaji mkubwa wa moyo,

2. Huduma za usafishaji na upandikizaji wa figo,

3. Matibabu ya kisasa ya Saratani,

4. Matibabu ya mifupa na huduma nyinginezo nyingi ambazo zimepunguza rufaa ya wagonjwa kwenda nje ya nchi na hivyo kuokoa fedha nyingi za kigeni ambazo zingetumika kuhudumia rufaa hizo.

Ndugu Wanahabari, katika kuendeleza mapambano na adui maradhi, Serikali ya Awamu ya Sita katika mwaka huu wa 60 pia imetenga jumla ya Shilingi bil 149 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi kwenye Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (META), Hospitali ya Kanda Chato Awamu ya Kwanza pamoja na hospitali mpya za Rufaa za Mikoa ya Njombe, Simiyu, Geita, Songwe, Katavi na Sekou Toure, Mwanza. Vilevile, Manyara, na Mara – Hospitali ya Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere (Kwangwa), Kazi inaendelea.

Ndugu Wanahabari, ukiacha maendeleo ya miundombinu baada ya Uhuru, vilevile, maendeleo makubwa yamepatikana kwenye vifaa tiba vya kisasa na wataalamu bobezi wa tiba ambao, wamefanya kazi nzuri iliyopunguza rufaa za nje ambapo katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni 2021, ni wagonjwa 2 tu walipatiwa rufaa nje ya nchi, ukilinganisha na wagonjwa 554 waliopatiwa rufaa nje ya nchi mwaka 2015/16. Haya ni mapinduzi makubwa kwa kipindi cha miaka 60 tangu tupate uhuru.

Zifuatazo ni baadhi ya alama za mapinduzi haya kwenye baadhi ya hospitali za ubingwa bobezi nchini Tanzania kama ifuatavyo kwa ufupi;

**Hospitali ya Taifa Muhimbili huduma mpya zimeanzishwa zikiwemo;**

1. Kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo (Dialysis) ambazo pia zimeenea hospitali mbalimbali nchini hadi hospitali za rufaa za mikoa;

2. Kuanza upandikizaji Figo (Renal Transplant) ambapo hadi sasa wananchi 64 wamenufaika na huduma hiyo pia huduma hii inapatikana katika hospitali zingine kama BMH na zingine ziko mbioni kuanza;

3. Upandikiza vifaa vya kusaidia watoto kusikia (Cochlear Implant) kupitia Hospitali za umma katika ukanda wa Afrika Mashariki na zaidi ya watoto 32 na watu wazima wawili wamenufaika na huduma hizi; na

4. Tiba Radiolojia (Interventional Radiology) ambapo kwa miaka mingi wagonjwa waliokuwa na uvimbe kwenye kinywa na mataya walianza kufanyiwa upasuaji hapa nchini.

**Hospitali ya Saratani Ocean Road (ORCI);**
1. Sasa tunazo mashine za kisasa za teknolojia ya 3D za tiba mionzi za LINAC na CT simulator zilizogharimu Tsh 9.5 Bilioni zinazotibu saratani kwa sayansi ya kisasa na sahihi zaidi.
2. Serikali Imetoa jumla ya Tsh 14.5 Bilion za Mradi wa Jengo, na Mashine za Cyclotron na PET CT scan ili kuimarisha vipimo vya ugunduzi na uchunguzi wa saratani ambapo kwa sasa havifanyiki nchini wala Ukanda wa Africa mashariki na Kati.

Aidha, kuimarishwa kwa utoaji wa huduma hasa tiba mionzi, kumeendelea kuwavutia wagonjwa kutoka nje ya nchi kuja nchini kwa ajili ya tiba. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021 jumla ya wagonjwa wapya 55 kutoka nje ya nchi walipatiwa huduma za uchunguzi na tiba ya saratani. Maboresho yote haya yamepunguza rufaa za wagonjwa wa saratani nje ya nchi kwa asilimia 90% na Serikali imeokoa takribani Tshs 10 bilioni ambazo zingetumika kwa matibabu nje ya nchi.

**Hospitali ya tiba ya mifupa, ubongo na mishipa ya fahamo (MOI);** hivi karibuni serikali imenunua na kufunga mashine ya kupasua ubongo bila kufungua kichwa (Angio Suite iliyogharimu bilioni 7.9). Ikumbukwe, kufikia Januari 2021 mashine hii ilipofungwa hakukuwa na kama hii Afrika Mashariki bali ilikuwepo Afrika Kusini. Kufikia leo imeshawafanyiwa operesheni ya ubongo wagonjwa 68 bila kufungua kichwa.

**Hospitali ya tiba ya moyo (JKCI);** huduma nyingi mpya za kisasa za matibabu ya moyo zimeendelewa kutolewa na pia upo mtambo wa kisasa wa Cathlab na Carto 3 wa uchunguzi na kutibu magonjwa ya moyo wenye thamani ya Shilingi bilioni 4.6 ambapo, wagonjwa 6,513 wameshafanyiwa upasuaji wa moyo kupitia tundu dogo na 2,436 wametibiwa matatizo ya mishipa ya damu.

**Hospitali ya Rufaa Kanda ya Ziwa (Bugando);** huduma mbalimbali mpya za kibingwa zimeendelea kutolewa na zaidi;

1. Hospitali imenunua mashine ya tiba ya mionzi inayoitwa brachytherapy, mtambo wa kusafisha damu (renal dialysis), CT-Scan na mtambo wa kuzalisha maji tiba.
2. Umefanyika ununuzi wa MRI yenye Thamani bilioni 2.43 (Euro 900,000) katika Hospitali hii vilevile, imeanzisha huduma za upasuaji kwa Watoto wachanga waliozaliwa na ulemavu (Congenital Malformations).

**Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kaskazini (KCMC).**
1. Imewezeshwa kwa mashine za kisasa za uchunguzi wa magonjwa ikiwa ni pamoja na MRI, CT-Scan yenye ukubwa wa Slice 128.

2. Serikali inatekeleza mradi wa bilioni 4 wa ujenzi wa idara ya matibabu ya saratani kwa mionzi.

**Hospitali ya Kanda ya Kati ya (BMH) Dodoma;** Pamoja kuanza huduma mwaka 2017, imekua kwa kasi na kuanza kutoa huduma za ubingwa bobezi mathalani;
1. Imeshapandikiza figo wagonjwa 23 na kati ya hao 16 wamepandikizwa na madaktari wazawa.

2. Inatoa matibabu ya magoti kwa kutumia matundu madogo kwa watu wenye matatizo ya miguu,

3. Inazo huduma za kuondoa mawe kwenye figo kwa kutumia vifaa maalumu bila kulazimika kufanya upasuaji kwa mgonjwa;

4. Imeweza kutoa huduma ya kupandikiza Betri kwenye moyo kwa watu wazima wawili (2).

Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya).

Hii ilifunguliwa mwaka 1985 na Mtoto wa Malkia wa Uingereza (Prince Anne) na kufikia miaka 60 baada ya uhuru imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo;-

1. Kutoa huduma za kibingwa kama upasuaji wa kawaida na upasuaji kwa njia ya vitundu "Laparascopic Surgery" pamoja na usafishaji wa figo (haemodialysis).

2. Kumiliki maabara ya kisasa iliyopewa Ithibati "Accredation" yenye uwezo wa kufanya vipimo vya ngazi ya kimataifa pia ina uwezo wa kupima magonjwa ya Ebola na mengine yanayofanana na hayo.

3. Kuanzisha huduma ya Mkalimani wa Viziwi jambo ambalo limepelekea mafanikio kwa Taasisi na Jamii kwa ujumla. Imeweza kutoa huduma ya upasuaji mkubwa kwa viziwi sita (6) na kutoa huduma ya elimu ya uzazi wa mpango na kuepusha mimba zisizo tarajiwa kwa watu wenye matatizo ya kusikia.

4. Imeboresha miundombinu kwa kuanzisha kiwanda cha uzalishaji wa MAJI TIBA (Infusion).

Aidha, hospitali zote hizi pia zinatumia mifumo ya kisasa ya kidigitali katika kuhudumia wateja na kuweka kumbukumbu zao pia kudhibiti mapato na matumizi ya taasisi hivyo, kwa kiasi kikubwa zimepunguza utegemezi kwa serikali lakini pia zimeboresha huduma kwa mteja ukilinganisha na miaka kdhaa nyuma.

**Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe (Dodoma).**

Kabla ya Uhuru huduma za Afya ya Akili zilikuwa duni sana ikilinganishwa na hivi sasa. Aidha, idadi ya Wataalam wauguzi "Mental Nurses" katika eneo la Afya ya akili walikuwa 12. Wagonjwa kutoka sehemu mikoa yote ya Tanganyika walikuwa wakipelekwa Hospitali ya Mirembe na Isanga (Broadmoor).

Wagonjwa walisongamana sana katika hospitali hiyo na wengi walitibiwa mbali na ndugu zao bila mawasiliano na nyumbani kwao.

Baada ya Uhuru Serikali imefanikiwa kutekeleza masuala mbalimbali ikiwemo.

1. Kuanzisha kozi za "certificate na diploma in psychiatric nursing" katika hospitali ya Mirembe mwaka 1973 – 1980s. Katika miaka hiyo ya 1980 ikaanzishwa kozi ya AMO Psychiatry.

2. Kuanzishwa kwa masomo ya udaktari na udaktari bingwa wa magonjwa ya akili katika Chuo cha Sayansi ya Tiba Muhimbili ambapo hadi sasa tuna madaktari bingwa zaidi ya 40.

3. Kuanzishwa kwa Sheria ya Afya ya Akili ya mwaka 2008 "The Mental Health Act, 2008. Act No 21, 2008". Sheria hii ina madhumuni ya kuratibu na kusaidia Wagonjwa wa afya ya akili nchini na kuweka huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya akili, na kushirikisha jamii katika kutoa huduma kwa wagonjwa wa akili.

4. Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la Afya Ulimwenguni ilanzisha mpango wa Huduma ya Afya ya Akili Ngazi ya Msingi. Mradi huo ulifanywa kwa majaribio mikoa ya Kilimanjaro na Morogoro na ukawa wa mafanikio makubwa.

5. Kati ya 1980 hadi 1990, mikoa ilieendelea kuhimizwa kuanzisha wodi za wagonjwa wa akili pamoja na vijiji vya utengemao.

6. Vitengo vya wagonjwa wa akili vilianzishwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Tabora, Mwanza, Kigoma, Kagera na Kilimanjaro ili kuipunguzia mzigo Hospitali ya Mirembe.

7. Mikoa yote Tanzania bara sasa ina uwezo wa kuhudumia wagonjwa wa akili katika wilaya zao, hadi ngazi ya zahanati. Mafunzo ya kueneza stadi za kuwahudumia wagonjwa ngazi ya msingi zinapatikana katika vituo vya afya na zahanati.

8. Kuanzishwa tiba ya saikolojia ambayo inasaidia wagonjwa wanaoendelea na tiba za kibaolojia waendelee kuimarika na kurudi kataka kazi zao za kijamii.

**Hospitali ya Udhibiti wa Maambuki Kibong'oto (Kilimanjaro).**

Hospitali hii ilianzishwa mwaka 1926 kwa lengo la kukinga na kudhibiti kifua kikuu na magonjwa ambukizi. Aidha, mwaka 1952 ilibadilishwa rasmi kuwa hospitali ya TB na Lady Twining – Mke wa Gavana wa Tanganyika. Mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo;-

1. Kabla ya uhuru ilikuwa na wodi 3 zenye uwezo wa kulaza wagonjwa 200 kwa sasa hospitali ina wodi 7 zenye vitanda 300 vya kulaza wagonjwa, ambapo vitanda 120 ni kwa ajili ya wagonjwa wa TB sugu, vitanda 120 wagonjwa

wa TB ya kawaida na vitanda 60 kwa wagonjwa wengine.

2. Hospitali iligatua matibabu ya kifua kikuu sugu toka hospitali 1 ya kibongoto 2009 hadi kufikia vituo 179 nchini.

3. Serikali imenunua mashine maalumu ya kisasa (Migit) yenye uwezo wa kupima usugu wa dawa za kifua kikuu na kuotesha vimelea vya kifua kikuu cha kawaida na kifua kikuu sugu ndani ya muda mfupi (wiki 3 hadi 4) badala wiki nane mpaka 10 kwa kutumia njia ya kawaida ilivyokuwa kabla uhuru.

4. Uboreshwaji wa huduma za uchunguzi wa vinasaba (whole genomic sequencing) na kuweza kubainisha anuai ya virusi vinavyosababisa corona nchini ambako kabla ya uhuru huduma hii haikuwepo.

5. Pamoja na huduma hizi katika hospitali, inatoa huduma za kijamii kwa njia ya mkoba kwa kutumia gari maalumu la kisasa lenye kiliniki tembezi.

6. Serikali inaendelea na ujenzi wa maabara kubwa ya kisasa ya afya ya jamii yenye hadhi ya Biosafety level 3 ambayo inagharimu jumla ya shilingi 11,337,672,870.88.

Ndugu Wanahabari, katika kuzingatia upatikanaji wa huduma za kibingwa karibu zaidi na wananchi na kwa uwiano wa kijiografia nchini tofauti na kabla ya uhuru au miaka kadhaa iliyopita, Serikali inajenga zingine mpya ikiwemo Hospitali ya Kanda ya Chato na Hospitali ya Kanda ya Kusini Mtwara.

Aidha, inapanua miundombinu kwenye Hospitali kongwe za Mikoa, Kanda, Maalumu na Taifa kama ifuatavyo;

1. Mbeya; ujenzi wa jengo la ghorofa Sita (6) la afya ya uzazi na mtoto Mbeya (META).

2. KCMC; Ujenzi wa wodi ya wagonjwa wa saratani, upanuzi wa Idara ya kusafisha damu na figo (Hemodialysis) na kitengo cha Endoscopy.

3. Kibong'oto; Ujenzi wa Maabara ya Afya ya Jamii ngazi ya tatu (BSL3). Jengo la Maabara husika lina ghorofa tatu (Ground + 3 floors).

4. Mawenzi; jengo la afya ya uzazi na mtoto pia jengo la huduma za dharura.

Ndugu Wanahabari, katika kipindi hiki cha baada ya uhuru ukiacha ujenzi wa hospitali mpya za mikoa nilizotaja awali za Njombe, Songwe, Simiyu, Geita, Manyara, Songwe na Mara – Kwangwa na upanuzi wa hospitali kongwe za rufaa za mikoa, maendeleo mbalimbali yanafanyika ikiwemo;

1. Usimikaji wa mitambo ya kuzalisha hewa tiba kwa thamani ya shilingi bilioni 8.7 unaendelea katika Hospitali za Rufaa za Mikoa Saba (7) ambayo ni Geita, Manyara, Dodoma, Dar es Salaam-Amana, Mtwara, Ruvuma-Songea na Mbeya.

2. Ufungaji CT scan, Ultra Sound na vifaa vya mama na mtoto, upasuaji, utakasaji, incinerator umefanyika katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza Sekoutoure kwa thamani ya Shilingi. 2,228,448,375.00.

3. Ununuzi na usimikaji wa CT Scan yenye thamani ya shilingi bilioni 1,444,500,000 umefanyika katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa (Mwananyamala RRH).

4. Ununuzi na sambazaji wa vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 6 vya Mradi wa ORIO (Fluoroscopy, Digital X-ray, ultrasound, incinerator n.k) unaendelea kwenye hospitali tisa (9) hapa nchini; (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke, Kitete - Tabora, Shinyanga, Kigoma (Maweni), Bukoba - Kagera, Mara, Hospitali ya Wilaya Bukombe, Chato na Misungwi).

5. Ununuzi wa mashine za kidigitali za X-ray katika hospitali zote 28 za rufaa za mikoa kupitia mradi wa ORIO unaotekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Uholanzi.

6. Umefanyika ununuzi wa mashine za kisasa "GeneXpert" 239 za kupima Kifua kikuu zinazotoa majibu ndani ya masaa mawili ikilinganishwa na hadubini zinazotoa majibu baada ya masaa 24.

7. Baadhi ya miundombinu inayopanuliwa iweze kutoa huduma bora zadi kwenye hospitali hizi za mikoa ni pamoja na;

i. Ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala lenye ghorofa nne na pia Mawenzi Kilimanjaro.

ii. Ujenzi wa jengo la kutolea huduma za dharura (EMD katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma.

iii.Ujenzi wa jengo la Methadone lenye ghorofa tatu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tanga.

iv. Ujenzi wa jengo la huduma za upasuaji katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kigoma – Maweni.

v. Ujenzi wa jengo la huduma za dharura (EMD) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Iringa .

vi. Ujenzi wa jengo la huduma za dharura katika Hospitali ya Mkoa wa Tabora – Kitete.

vii. Ujenzi wa Jengo la Wodi ya wagonjwa walio chini ya uangalizi maalum, Wodi ya Upasuaji, jengo la huduma ya Upasuaji na utakasaji vifaa tiba pamoja na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya majengo ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya.

Ndugu Wanahabari, Serikali haikuzisahau hospitali za ngazi ya halmashauri, vituo vya afya na zahanati ambapo,

baada ya uhuru kupitia MMAM ilitoa msukumo mkubwa kwa ufupi kama ifuatavyo;

1. Ukilinganisha na kabla ya huru, hivi sasa kuna jumla ya Zahanati 7,242 Vituo vya Afya 926 na Hospitali za Halmashauri 178. Jumla ya Vituo vya Afya 487 kati ya vilivyopo vinafanya upasuaji wa dharura kwa maana hiyo, watumishi wa kada mbalimbali muhimu wanapatikana hadi ngazi ya vituo vya afya tofauti na kabla ya uhuru.

2. Huduma za uchunguzi wa maabara na mionzi nazo zimeimarika. Umefanyika ununuzi wa Xray za kidigitali (Digital X-ray 18) kwa gharama ya Shilingi za kitanzania 5,290,000,000.00 sawa na shilingi 264,500,000.00 kila moja na kusambazwa hospitali 14 za halmashauri; (Mangaka, Tunduru, Mbinga, Kasulu, Nyamagana, Butiama, Makambako, Makete, Mbarari, Tukuyu, Itumba, Nkasi, Usangi, na Same) na hospitali 4 za Wilaya (Kisarawe, Songwe/ Mwambani, Namtumbo, na Musoma/ Mwl.Nyerere memorial Hospital). Ununuzi huu umefadhiliwa wadau wa maendeleo Global Fund.

3. Huduma za uchunguzi kupitia Ultra Sound zimeanza kutolewa kwenye vituo vya afya 125 katika Halmashauri mbalimbali nchini.

4. Vipimo mbalimbali vya maabara vinafanyika ngazi zote za vituo vya afya ya msingi.

Ndugu Wanahabari, katika miaka sitini (60) ya Uhuru Serikali inaratibu uendeshaji wa huduma za afya kidigitali kupitia mkakati wa TEHAMA (Digital Health Strategy 2019-2024) ambapo mpaka sasa;

1. Imepeleka Mkongo wa Taifa wa mawasiliano (fiber optic cable) na kujenga miudombinu ya mtandao (Loca Area Network) kwenye hospitali zote za rufaa kuanzia ngazi ya Taifa, Kanda, Mkoa na hospitali maalumu (specialized hospital).

2. Imeboresha upatikanaji wa mtandao wa uhakika katika vituo vya ngazi ya msingi.

3. Imesambaza vifaa vya TEHAMA kama Kompyuta, “Server “, printer na vishikwambi katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kurahisiha matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika kutolea huduma na kukusanya taarifa.

4. Kwa mifumo hii, udhibiti wa raslimali fedha na bidhaa za afya na uwajibikaji pamoja na upatikanaji wa taarifa kwa wakati unaendelea kuimarika ulikinganisha na miaka kadhaa iliyopita.

Ndugu Wanahabari, katika kuimarisha huduma za afya baada ya uhuru serikali imefungua taasisi mbalimbali saidizi kama ifuatavyo;

**I. Taasisi ya Mfuko wa taifa wa Bima ya Afya;** Kabla ya uhuru huduma za matibabu zilikuwa bila malipo hadi kufikia miaka ya 1997 zilipoanza kutolewa kwa sera ya uchangiaji na msamaha kwa wasio na uwezo. Hata hivyo, mfumo huu ulibainika kupitwa na wakati hivyo serikali kuanzisha bima za afya ili kuwawezesha wananchi wananchi kumudu gharama za matibabu. Hivi sasa, Serikali inayo Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) na Bima ya Afya ya Jamii (CHF). Aidha, zipo na Bima mbalimbali za binafsi.

Kupitia mifuko hii ya bima za afya;

1. Hifadhi ya jamii imeimarika ambapo jumla ya watanzania 8,224,271 sawa na asilimia 14.7 ya watanzania wote wananufaika na huduma za mifuko ya bima ya afya. Kati ya wananchi waliojiunga na mfumo wa bima ya afya, asilimia 8 wamesajiliwa na NHIF, asilimia 5.4 wanahudumiwa na iCHF, asilimia 0.3 wananufaika na huduma kupita SHIB-NSSF na asilimia 1  wamejiunga na bima ya afya inayotolewa na makampuni ya bima binafsi za afya.

2. Hadi kufikia Juni 2021 jumla ya vituo 8,482 vya ngazi ya Zahanati hadi Taifa, vya Serikali, Mashirika ya Dini na Binafsi vinahuhumia wanachama wa NHIF ikilinganishwa na vituo 3,197 vya mwaka 2001/02. Mwanachama wa NHIF kwa kutumia kadi yake anatibiwa popote Tanzania Bara na Zanzibar katika vituo hivi vilivyosajiliwa. Hivyo, Kadi ya NHIF haina mipaka ya kimikoa.

Ndugu Wanahabari, Hivi sasa Mfuko umeweka utaratibu rahisi kwa kila kundi kuchangia, kujiunga na kuanza kunufaika kwa hiari ikilinganisha na kundi la watumishi wa umma tu ambalo liliwezeshwa kujiunga wakati Mfuko unaanzishwa.

Wanachama wa mfuko wa taifa wa bima ya afya wanapata manufaa mbalimbali ikiwemo;

1. Kupata huduma kuanzia za afya ya msingi hadi za kibingwa ikiwemo matibabu ya moyo, figo, saratani, upandikizaji wa viungo, vipimo vikubwa kama CT Scan na MRI. Awali huduma kwa wanachama zilikuwa chache mathalan idadi ya vipimo ilikuwa 9 na dawa 440 wakati mfuko unaazishwa mwaka 2001.

2. Sasa hivi kitita cha huduma kina jumla ya dawa 975 zikiwemo za magonjwa ya Sukari, Moyo na Saratani na vipimo 354 vikiwemo vikubwa na vidogo kulingana na maendeleo ya teknolojia ya tiba. Huduma za upasuaji mkubwa 210 na mdogo 167 na wa kibingwa 148. Aidha huduma za kulazwa, kujifungua, macho, meno, n.k zinatolewa kwa wanachama wa NHIF kulingana na miongozo ya tiba iliyopo.

3. Kulingana na mahitaji ya wanachama waajiri, Mfuko umeweka utaratibu unaowezesha waajiri kulipia watumishi wao huduma za ziada (Suplimentary package) ambazo hazipo kwenye kitita cha mafao cha NHIF. Mathalani, Huduma za Uokozi (Air and ground evacuation), dawa za majina ya kibiashara, huduma za miwani, n.k

Ndugu Wanahabari, kwa kutambua kuwa wananchi wengi (takriban asilimia 85.3) wako nje ya mfumo wa bima ya afya, Serikali inaendelea kukamilisha muswada wa sheria

ya Bima ya Afya kwa wote na imefikia hatua kubwa. Huu ni mwelekeo mzuri wa nchi katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru.

**II. Taasisi ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD);**
Ndugu Wanahabari, Ili kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, baada ya uhuru serikali ilianzisha taasisi ya MSD ambayo imeendelea kuboresha utekelezaji wake kwenye mambo makubwa kama ifutavyo;

1. Kuagiza dawa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji; hatua hii imewezesha kupata bidhaa hizo kwa gharama nafuu ambapo hadi sasa upatikanaji wa bidhaa za afya umeimarika kwa asilimia 55.

2. Kuingia mikataba na watengenezaji wa vifaa vya maabara na vitendanishi vyake, na mashine za kuchuja damu. Hatua hii imepunguza gharama za bidhaa hizo kwa asilimia 50 -100 na hatua hii inatarajiwa kuokoa shilingi bilioni 9.7 kwa mwaka.

3. Ujenzi wa kiwanda cha barakoa ambapo bei ya barakoa moja imeshuka kutoka kuuzwa shilingi 1,600 hadi kuuzwa shilingi 600 na kuokoa shilingi milioni 683,980,500 ambazo zingetumika kwa kuagiza kutoka nje ya nchi;

4. Kuanza uzalishaji wa bidhaa za afya ikiwa ni pamoja na Kiwanda cha Keko Pharmaceutical Limited (ambacho MSD imepewa jukumu la kukisimamia), Kiwanda cha Keko Pharmaceutical kina uwezo wa kuzalisha aina 10 za vidonge ambavyo kati ya hivyo, aina mbili ni vya maumivu na nane ni vya kuua vimelea vya magonjwa, yaani Antibiotics na moja ya kutibu fangasi.

5. Kujenga viwanda vinne vya uzalishaji dawa na vifaa tiba huko Idofi Makambako. Kiwanda cha mipira ya mikono, Vidonge, vidonge vya rangi mbili na dawa za majimaji (syrup) ambapo vitaipinguzia gharama Serikali kwa kuokoa kiasi cha shilingi Bilioni 33 kwa mwaka.

6. Serikali imeongeza bajeti ya fedha za kununulia dawa hadi kufikia shilingi Bilioni 277.49 mwaka huu.

**III.Taasisi ya Udhibiti wa Dawa na Vifaa tiba (TMDA);** taasisi hii imepata mafanikio makubwa yakiwemo;

1. Hadi kufikia Juni, 2021, Mamlaka ilikuwa imesajili jumla ya viwanda vya ndani 36, ambapo 11 vya dawa, viwanda 14 vya vifaa tiba na 11 vya gesi tiba vinavyofanya kazi ukilinganisha na kiwanda kimoja cha dawa kilichokuwa kimesajiliwa wakati wa Uhuru mwaka 1961.

2. Idadi ya bidhaa za dawa, zilizosajiliwa hadi kufikia mwaka 2020/21 ni 16,467 ikilinganishwa na 265 zilizosajiliwa mwaka 2003/04 ikiwa ni ongezeko 6,214%.

3. Idadi ya majengo yaliyosajiliwa ya biashara za bidhaa za dawa zinazodhibitiwa na Mamlaka hadi mwaka 2020/21 ni 11,156 ikilinganishwa na majengo 1,504 yaliyosajiliwa mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la 742%.

IV. Taasisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA); taasisi hii inahusika na kufanya uchunguzi wa kimaabara juu ya masuala mbalimbali ya kisayansi. Taasisi hii imeendelea kuimarika kutoka utumiaji wa mbinu duni za makaratasi ya uchunguzi hadi mbinu zinazotumia mitambo na vifaa vya kisasa. Mitambo hii imeifanya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa ya pili katika maabara zenye vifaa vya kisasa katika nchi za Afrika Mashariki, Kati, Kusini mwa Afrika ikitanguliwa na maabara chache za Afrika Kusini.

V. Taasisi ya Utafiti Afya (NIMR); taasisi hii inahusika na Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu ambapo imeweza kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali hapa nchini kuhusu Malaria, kifua kikuu (TB), UKIMWI, afya ya mama na mtoto, magonjwa ya kitropiki yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, magonjwa ya mlipuko, magonjwa yasiyoambukiza, muungano wa magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza (co-morbidities), viashiria vya afya vya kijamii pamoja na, magonjwa mtambuka ya binadamu na wanyama (One Health). Pia Taasisi imeendelea kutekeleza miradi ya utafiti inayolenga kuimarisha mifumo ya afya na tafiti hizo zililenga katika kutafiti na kusaidia kutatua changamoto ya upatikanaji wa dawa hata pale ambapo madawa katika bohari ya dawa yanapatikana.

**VI. Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC);** Taasisi hii inahusika na kuishauri serikali, wananchi pamoja na wadau wote wa lishe nchini namna ya kupambana na aina zote za utapiamlo.

Katika miaka 60 ya Uhuru, TFNC kwa kushirikiana na sekta nyingine imechangia kutekeleza afua ambazo zimepelekea kupunguza viwango vya utapiamlo kwa kiasi kikubwa kama ifuatavyo;-

1. Udumavu kwa Watoto chini ya miaka mitano kutoka zaidi ya asilimia 50 kabla ya uhuru kufikia asilimia 31.7 mwaka 2018;

2. Ukondefu kwa watoto chini ya miaka mitano umepungua kutoka asilimia 6 mwaka 1992 hadi kufikia asilimia 3.5 mwaka 2018;

3. Uzito pungufu kwa watoto chini ya miaka mitano kutoka asilimia 29 mwaka 1992 hadi kufikia asilimia 14 mwaka 2018:

4. Upungufu wa damu kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa (miaka 15-49) kutoka asilimia zaidi ya 50 hadi kufikia asilimia 28 mwaka 2018.

5. Pia Taasisi imewezesha kuhamasisha unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee kwa watoto wenye umri chini ya miezi sita kutoka asilimia 24 hadi kutikia asilimia 59 mwaka 2018.

Ndugu Wanahabari, zifuatazo ni takwimu chache za

utumiaji wa vituo vya kutolea huduma kwa rejea ya Huduma za Afya ya Uzazi (Mama) na Mtoto;-

1. Ongezeko la wajawazito waliohudhuria mahudhurio manne au zaidi ya kiliniki hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2021, asilimia 93.4 ya wajawazito walihudhuria kliniki.

2. Ongezeko la akinamama kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya limefikia hadi asilimia 83.1 mwaka 2020 ambayo ni zaidi ya lengo la Mpango Mkakati wa Nne wa Sekta ya Afya (HSSP IV) la asilimia 65.

3. Idadi ya akinamama waliojifungua na kurudi kiliniki siku mbili baada ya kujifungua imefikia asilimia 62. Mwitikio huu ni muhimu katika kuhakikisha usalama wa mama na mtoto, kwa kuwa asilimia 60 ya vifo vitokanavyo na uzazi hutokea kipindi cha baada ya kujifungua kutokana na matatizo ya kupoteza damu, kifafa cha mimba na maambukizi ya bakteria.

4. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya akina mama 332,620 walifanyiwa uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi kwenye vituo 794 vya uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi.

Baadhi ya vashiria vingine vya mafanikio ni pamoja na;

1. Chanjo kwa watoto vhini ya miaka mitano imeendelea kutolewa kwa wastani wa 95% kwa miaka mitano mfululizo kutoka mwaka 2015.

2. Ugonjwa wa Polio (Acute Flaccid Paralysis) (kupooza ghalfa kwa watoto) tumefanikiwa kuumaliza kwa chanjo na hivyo Tanzania kutangazwa kuwa huru dhidi ya ugonjwa huu toka mwaka 2015 na kupewa cheti cha kuwa huru miaka mitano baadae yaani mwaka 2020.

3. Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 112 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2004/05 hadi vifo 50 kila vizazi hai 1000 mwaka 2020. Tukumbuke mwaka 2013 Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi ambazo zilifanikiwa kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano kufikia malengo ya milenia ya nne (MDG 4).

4. Vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja (Infant Mortality) vimepungua kutoka 94 kwa vizazi hai 1000 mwaka 1992 hadi vifo 36 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2020 (DHS projection 2020).

5. Vifo vya watoto wachanga ndani ya siku 28 (neonatal mortality) vimepungua kutoka vifo 32 kwa kila vizazi hai 1000 (2004/05) hadi vifo 20 kwa kila vizazi 1000 (2020).

6. Vifo vya wajawazito vimepungua kutoka vifo 870 kwa kila vizazi 100,000 (1990) kufikia vifo 321 kwa kila vizazi hai 100,000 (2020).

7. Kuenea kwa malaria (prevalence) kumepungua kwa 50% kati ya miaka ya 90s hadi kufikia 7.5% mwaka 2017 (MIS - 2017). Vilevile, idadi ya wanaofariki kwa malaria imepungua kwa 61% kutoka vifo 6,311 mwaka 2015 hadi vifo 2,460 mwaka 2020.

8. Hali ya ugonjwa wa Ukoma imepungua kutoka wagonjwa 1889 (2015) mpaka wagonjwa 1217 kwa mwaka 2020.

9. Hali ya matibabu ya Kifua Kikuu nchini inazidi kuimarika ambapo tumeongeza uibuaji wa wagonjwa kutoka 62,180 (2015) mpaka 85,597 (2020). Aidha vifo vimepungua kutoka 55,000 (2015) mpaka 26,800 (2020). Hii inatokana na uwepo wa njia zilizoboreshwa za uchunguzi na elimu kwa jamii na Serikali kupeleka huduma za uchunguzi na tiba mpaka kwenye ngazi ya jamii.

Mafanikio haya pia yanajieleza kwa kuongezeka kwa umri wa kuishi wa mtanzania toka miaka 36 mwaka 1961 hadi miaka 66 mwaka 2020 ambayo inaashiria kuimarika kwa mifumo ya utoaji huduma za afya nchini. Hili ni ongezeko la mara mbili kwenye umri wa kuishi mtanzania.

Ndugu Wanahabari, katika kipindi hiki cha baada ya uhuru serikali imejiendeleza na kujiimarisha zaidi katika kukabiliana na magonjwa yanayozuilika (kinga) yakiwemo yanayoambukiza na yasiyoambukiza. Kwa upande wa mgonjwa yanayoambukiza mifumo ya kubaini, kuzuia na kudhibiti imeimarika hadi sehemu za mipakani ambapo sasa tuna vituo 40. Maabara kuu ya taifa imeimarika na ina vifaa vya kisasa na imefungua matawi yake manne katika Mikoa ya Dodoma, Mwanza, Mbeya na Arusha.

Kuhusu magonjwa yasiyoambukiza serikali imejielekeza kwenye mkakati mtambuka shirikishi wa sekta zote ili kuimarisha mapambano eneo hili. Hivi sasa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia magonjwa ya kuambukiza ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria na Ukoma ndiyo imepewa na jukumu la kusimamia magonjwa yasiyoambukiza. Huu ni mtazamo chanya na shirikishi kwenye vita hivi tofauti na awali kabla ya uhuru.

**Baadhi ya changamoto.**

1. Kuongezeka kwa wimbi la magonjwa mapya yanayoambukiza (Communicable Disease) na yasiyoambukiza (NCD).

2. Uchache wa raslimali kwa ajili ya uendeshaji huduma za afya hususan watumishi, dawa, vifaa Tiba na vipimo.

3. Baadhi ya Wananchi kushindwa kumudu gharama za tiba kutokana na kukosa Bima.

4. Utendaji wa mazoea wa baadhi ya waliopewa fursa ya kuwa watumishi wa umma sekta ya afya jambo linalohitaji maboresho makubwa kwenye mifumo ya motisha na uwajibikaji.

**Mwelekeo mpya.**

1. Kuwekeza kwenye ubora wa huduma baada ya

uwekezaji wa miundombinu (software engineering) sambamba na kuimarisha mifumo ya uwajibikaji wenye matokeo kwa kupima viashiria vya matokeo (performance merits by scorecards).

2. Kuimarisha Mifumo ya Tehama ili kuweza kuimarisha udhibiti wa raslimali na uwajibikaji pia kuharakisha huduma kwa mteja.

3. Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (UHI)

4. Kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji wa sekta binafsi katika Huduma za tiba na Viwanda vya dawa na vifaa tiba.

5. Kuendelea kupanua huduma za kibingwa na bingwa bobezi sambamba na raslimali watu na hivyo kufungua njia ya medical tourism.

6. Sambamba na kuendelea na maboresho ya afya ya msingi, kujikita kwenye afya kinga dhidi ya magonjwa yanayoepukika kwa kuimarisha ushirikishaji wa jamii katika kumiliki huduma za afya.

7. Kuongeza uwekezaji na Ugunduzi katika Tafiti za Tiba, Chanjo na Tiba Asili.

Ndugu Wanahabari
Kwa upande wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yafuatayo yamefanyika;-

Ndugu Wanahabari, Tangu miaka ya 1960 hadi 1980 Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii walikuwa chachu ya kutekeleza kampeni mbalimbali za kitaifa zinazohitaji ushiriki wa jamii ikiwemo Uhuru na Kazi; Siasa ni Kilimo; Kisomo Chenye Manufaa; Azimio la Arusha; Mtu ni Afya; Elimu kwa Wote; Chanjo ya Watoto wenye Umri Chini ya Miaka Mitano; Uhai, Ulinzi na Maendeleo ya Mtoto. Miaka ya 2019-2021 wataalam hawa wanaendelea kuamsha ari ya jamii kuboresha makazi yao kupitia Kampeni ya Ujenzi wa Nyumba Bora ambapo hadi sasa jumla ya nyumba 4,008 zimejengwa.

Ndugu Wanahabari, Katika kipindi cha Mwaka 2015 hadi 2020 Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wamewezesha kaya 617,100 kuboresha vyoo, kaya 305,724 kuboresha maeneo ya kunawa mikono, kujengwa madarasa ya shule za msingi 6,521 na sekondari 2,499, hospitali 67 za Halmashauri na miradi mingine vijijini na mijini.

Aidha, jamii ya sasa ina mwamko wa kujiletea maendeleo kwa kuanzisha miradi inayolenga kutatua changamoto zinazowakabili mfano ujenzi wa barabara, maboma ya madarasa, zahanati, vituo vya afya. Pia, jamii imeanza utaratibu wa kujitafutia mitaji kwa ajili ya uzalishaji na kujiwekea akiba kupitia vikundi vya VICOBA, Benki za kijamii na SACCOs. Vile vile kuna mwamko mkubwa wa jamii kutumia teknolojia ya Habari na Mawasiliano kupeana taarifa mbali mbali zikiwemo za masoko.

Ndugu Wanahabari, Serikali, kupitia wizara hii baada ya Uhuru, imeendelea kuzalisha wataalam wa Maendeleo ya Jamii ambao ni muhimu katika kuchochea mabadiliko na kufanya mageuzi ya kifikra miongoni mwa jamii ili kuwawezesha wananchi kushika hatamu ya maendeleo yao. Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru, Serikali imepanua wigo wa kutoa mafunzo ya wataalam wa maendeleo ya jamii ambapo miaka ya 1960 kulikuwa chuo kimoja tu cha Tengeru na leo hii kuna jumla ya vyuo 63 ambapo, kati ya hivyo vya Serikali ni 12 na vya binafsi ni 51. Kati ya vyuo 12 vya Serikali 9 vinasimamiwa na Wizara ambapo mafunzo hayo yanatolewa kuanzia ngazi ya Astashahada hadi Shahada ya uzamili.

Ndugu Wanahabari, Ili kuongeza thamani ya mafunzo yanayotolewa na vyuo vilivyo chini ya Wizara, imeanzishwa programu za uanagenzi zinazomuandaa mhitimu kujiajiri na kuajiriwa, programu za ubunifu zinazotoa fursa kwa wanafunzi na jamii inayozunguka vyuo kufanya kazi za ubunifu unaosaidia kutatua changamoto mbalimbali na ajira. Hadi sasa vimeanzishwa vituo Tisa (9) vya ubunifu wa kidigitali na programu za ushirikishwaji jamii kutatua changamoto zinazowakabili kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka zimeanzishwa.

Ndugu Wanahabari, baada ya Uhuru Serikali imejielekeza kwenye kuimarisha Ustawi wa Watoto ambapo, katika miaka ya mwanzo ya 1970 Wizara ilikuwa inaratibu na kusimamia upatikanaji wa haki na ulinzi wa mtoto kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977. Ili kuimarisha upatikanaji wa haki, maendeleo na ustawi wa mtoto, Serikali imeongeza wigo wa kutekeleza masuala ya watoto kwa kuridhia na kusaini mikataba ya kikanda na kimataifa.

Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (1989) na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (1990). Kupitia mikataba hii Wizara imeendelea kunufaika na usaidizi wa kitaalamu pamoja na rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa masuala yanayohusu upatikaji wa haki na ustawi wa watoto.

Ndugu Wanahabari, baada ya Uhuru, Serikali imepanua wigo wa majukwaa ya watoto katika kujadili masuala yanayowahusu ambapo, katika kipindi cha mwanzo cha Uhuru wa Tanzania Bara, jukwaa pekee la watoto la kujadili masuala yanayowahusu na kufikisha ujumbe ilikuwa ni kupitia shule ikijumuisha majukwaa kama chipukizi. Mfumo huu ulijumuisha watoto wale tu waliopo shule na kuwaacha watoto wasiokuwa shule na hivyo kutokutoa fursa sawa ya kushirikisha watoto wote.

Ndugu Wanahabari, Ilipofika mwaka 1991 Tanzania iliridhia na kusaini Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki ya Mtoto ambapo moja ya matakwa ya mkataba ni kuanzisha majukwaa ya watoto ili kujadili masuala yanayowahusu ikiwemo upatikanaji wa haki na ulinzi dhidi yao. Jukwaa hili huwajengea watoto uwezo katika nyanja za uongozi na uzalendo, uadilifu, ujasiliamali, stadi za maisha na masuala mtambuka yakiwemo utunzaji wa mazingira, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na kujilinda dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI.

Mnamo Disemba, 2002, Serikali iliratibu uundwaji wa mabaraza ya watoto katika ngazi zote kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa, Kata, Halmashauri, Mkoa hadi Taifa. Aidha, Wizara inaratibu uanzishwaji wa Madawati ya ulinzi wa watoto shuleni kwa lengo la kuwashirikisha watoto katika kutoa taarifa za ukatili dhidi yao ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya wakosaji. Kupitia madawati haya watoto wanajengewa ujasiri, uwezo wa kujieleza, kujiamini ili kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi yao.

Ndugu Wanahabari, Mara baada ya Uhuru, Serikali ilihakikisha uwepo wa Sera, Sheria, Miongozo na mifumo ya kushughulikia masuala ya watoto ili kuimarisha mifumo ya kusimamia haki, ulinzi na ustawi wa watoto na kuwakinga dhidi ya ukatili wa aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukatili wa kimwili, kingono na kisaikolojia. Sera ya kwanza ya Maendeleo ya Mtoto iliandaliwa mwaka 1996 na kurejewa 2008 ambayo imeainisha haki tano za msingi kwa watoto; haki ya kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushiriki na haki ya kutobaguliwa.

Aidha, Sheria mbalimbali za kumlinda mtoto zilitungwa ikiwa ni pamoja na Sheria ya mtoto Na 21 ya mwaka 2009 inayosimamia upatikaji wa haki za mtoto na kumlinda mtoto dhidi ya aina zote za ukatili. Hadi sasa, Wizara inaratibu huduma ya simu bila malipo kwa kutumia Na. 116 kwa ajili ya utoaji wa taarifa za matukio ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na ushauri wa namna ya kukabiliana na matukio hayo.

Ndugu Wanahabari, Katika kuimarisha huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya awali ya mtoto, Wizara imeratibu uandaaji wa Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/22-2025/26) yenye lengo la kumlea na kumkuza mtoto kwa utimilifu wake. Katika kutimiza azma hiyo, Wizara imenzisha vituo vya kijamii 30 vya mfano ambapo lengo ni kujenga vituo hivyo katika Vijiji/Mtaa yote nchini.

Vilevile, Serikali imesajili jumla ya vituo 2,133 vya kulelea watoto wadogo mchana kwa ajili ya kutoa huduma za malezi na uchangamshi wa awali. Aidha ili kukabiliana na changamoto za afya na Maendeleo kwa Vijana Balehe Wizara iliratibu uandaaji na inasimamia utekelezaji wa Ajenda ya Kitaifa ya kuwekeza katika Afya na Maendeleo kwa Vijana Balehe (2021/22 – 2024/25), lengo likiwa kukabiliana na changamoto zinazowakabili vijana balehe wenye umri wa 10-19 katika ya maeneo ya VVU/UKIMWI, mimba za utotoni, Ukatili, Lishe bora, Kuendelea kuwa shuleni na kujengewa ujuzi ili kupata fursa za kiuchumi.

Ndugu Wanahabari, Katika kuimarisha malezi ya watoto na familia katika mazingira ya sasa, Wizara kwa nyakati tofauti imekuwa ikiratibu upatikanaji wa huduma za malezi kwa watoto. Mnamo 2019, Wizara ilizindua Ajenda ya Kitaifa ya Malezi ya Watoto na Familia ijulikanayo kama "Familia bora, Taifa imara" lengo likiwa ni kuhimiza wazazi/walezi na jamii kwa ujumla katika kutekeleza jukumu lao la msingi la malezi na utoaji wa matunzo kwa watoto na familia ili hatimaye kuwakuza katika maadili mema na uzalendo kwa Taifa lao.

Vilevile, Katika kuimarisha mahusiano katika familia na jamii, Serikali imeendelea kuratibu utoaji wa huduma za unasihi na msaada wa kisaikolojia. Aidha, huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia na msaada wa kisaikolojia zimekuwa zikitolewa kwa njia ya mtandao ili kuweza kuwafikia wananchi wengi wanaokabiliwa na changamoto hizo.

Ndugu Wanahabari, Vilevile Serikali imeimarisha huduma za malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi kwa kuhakikisha uwepo wa programu za malezi mbadala kama vile huduma za malezi ya kambo, uasili wa watoto, malezi ya watu wa kuaminika kwa watoto walio nje ya malezi ya kifamilia na wale ambao wanakabiliwa na vitendo vya ukatili katika familia; pamoja na afua za utengemano na marekebisho ya tabia kwa watoto walio katika mkinzano na Sheria na wale wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Aidha, katika kukabiliana na changamoto ya makao ya watoto, Serikali inaratibu na kusimamia jumla ya makao ya watoto 239 ikilinganishwa na makao moja yaliyokuwepo mwaka 1960. Kwa upande mwingine, Serikali kwa kushirikiana na shirika la ABBOT FUND imejenga Makao ya Watoto katika Eneo la Kikombo Mkoani Dodoma ambayo yalizinduliwa na Mhe. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 16 Juni 2021. Makao haya yanachukua Watoto walio katika mazingira hatarishi ikiwemo wanaoishi na kufanya kazi mitaani kwa lengo la kuwapatia huduma za msingi, kurekebisha tabia zao kwa lengo la kuwaunganisha na familia zao.

Ndugu Wanahabari, Serikali pia imeweka utaratibu wa Maafisa Ustawi wa Jamii kusimamia upatikanaji wa haki kwa watoto katika mahakama 147 za watoto ambazo zilianzishwa hapa nchini kupitia Sheria ya Mtoto Na.21 ya mwaka 2009 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2019. Mahakama hizi zimesaidia kuharakisha upatikanaji wa haki kwa watoto waliokinzana na sheria pamoja na wale waliofanyiwa vitendo vya ukatili na wenye changamoto mbalimbali za malezi na uangalizi. Katika kipindi cha mwaka 2019/20, jumla ya watoto 737 walihudumiwa katika Mahakama za Watoto nchini. Kati yao, watoto 516 waliachiwa huru na watoto 221 walikutwa na hatia.

Ndugu Wanahabari, Serikali vilevile, imeendelea kuimarisha huduma za malezi, matunzo na ulinzi kwa Wazee katika makazi ambapo imeboresha miundombinu na upatikanaji wa huduma za msingi kama vile chakula, mavazi, malazi, matibabu n.k. kwa sasa Serikali inasimamia na kuratibu jumla ya makazi 15 yanayomilikiwa na Serikali yenye jumla ya wazee 277 (Me-166, Ke- 111) na makazi 20 yanayomilikiwa na taasisi binafsi yenye jumla ya wazee 537 (Ke-242,Me-295). Serikali imeimarisha ulinzi na usalama kwa wazee kwa kutekeleza afua mbalimbali ambazo zimesaidia kupunguza vitendo vya ukatili ikwemo mauaji kwa wazee.

Ndugu Wanahabari, Ushiriki wa Wazee katika masuala mbalimbali ya kijamii na kimaendeleo umeimarika baada ya Serikali kuweka utaratibu wa kuwa na Mabaraza ya Wazee katika ngazi zote, ambayo yameanzishwa kupitia Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003. Mabaraza 26 yameundwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na kufanya Mabaraza kufikia 20,748. Mabaraza haya yanatumika katika kusaidia jamii kuimarisha malezi ya vijana pamoja na utatuzi wa changamoto mbalimbali kwenye jamii.

Vilevile, wakati wa Uhuru mifumo ya utoaji huduma za afya kwa wazee imeboreshwa ambapo Serikali imekuwa ikifanya utambuzi wa wazee wasiojiweza na kuwapatia vitambulisho vya matibabu bila malipo. Aidha, Serikali imewezesha uundwaji wa timu za uratibu na usimamizi wa huduma katika hospitali na vituo vya afya nchini ili kutoa usaidizi na kuhakikisha wazee wanapata huduma. Timu hizo zinajumuisha wataalam watatu (3) ambao ni Daktari, Muuguzi na Afisa Ustawi wa Jamii. Aidha, Serikali imehamasisha na kuhakikisha kila kituo kinaweka utaratibu wa kuwa na bango linalosomeka 'Mpishe Mzee Kwanza' ili kukumbusha na kuhamasisha wajibu wa watoa huduma kujali wateja wa kundi hili pamoja na jamii kuona umuhimu wa kuwapisha wazee ili wapate huduma mapema.

Ndugu Wanahabari, Katika kushughulikia Maendeleo ya Wanawake na Jinsia, Serikali imefanya Jitihada za kuimarisha ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi ndani na nje ya nchi. Wakati Baraza la kwanza la Mawaziri linaundwa mara baada ya uhuru halikuwa na mwanamke hata mmoja. Mwanamke wa kwanza kuwa Waziri ilikuwa mwaka 1965 ambapo Bi Lucy Selina Lameck Somi aliteuliwa kuwa waziri mdogo wa Shirika na Maendeleo ya Jamii. Tangu kipindi hicho wanawake wameendelea kuaminiwa ambapo kwa sasa idadi ya Mawaziri wanawake imefika saba (7), Wabunge wanawake imeongezeka kutoka wabunge 127 mwaka 2015 hadi kufikia wabunge 145 mwaka 2020.

Ndugu Wanahabari, Kutokana na jitihada hizo, kwa mara ya kwanza nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina Rais wa Awamu ya Sita ambaye ni mwanamke Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na pia amewahi kushika nyazifa mbalimbali kabla ya kuwa Rais. Wengine ni Mheshimiwa Anna Makinda, Spika wa Kwanza mwanamke wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Tulia Akson ambaye ni Naibu Spika wa sasa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ndugu Wanahabari, Kimataifa nchi inajivunia Mheshimiwa Getrude Mongela aliyekuwa Katibu Mkuu wa Mkutano wa nne wa Umoja wa Mataifa wa kuhusu masuala ya wanawake Duniani uliofanyika mwaka 1995 Jijini Beijing China, Profesa Anna Tibaijuka alikuwa Katibu Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi Duniani (UNHABITANT) kuanzia mwaka 2006 hadi 2010; Dkt Asha Rose Migiro amewahi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kutoka kwaka 2007 hadi 2012 na Dkt Stergomena Lawrance Tax alikuwa mwanamke wa kwanza kuwa Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya SADC kwa kipindi cha miaka nane kutoka 2013 hadi 2021. Kwa sasa Dkt. Stergomena Tax ni mwanamke wa kwanza kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa.

Ndugu Wanahabari, Katika kuwezesha wanawake kiuchumi, Serikali katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru imewezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika uchumi ikiwemo kuwezesha nyenzo mbalimbali ikijumuisha kutoa mikopo isiyo na riba inayotokana na kutengwa kwa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Dirisha la mikopo kwa wanawake kupitia Benki ya Wanawake na sasa Benki ya Posta, VICOBA, SACCOS, Sekta binafsi, taasisi za fedha na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambayo huwezesha wanawake kiuchumi.

Serikali pia imeimarisha mifumo ya kupambana na kuzuia vitendo vya ukatili wa wanawake na Watoto kwa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto yaani MTAKUWWA (2017/18 2021/22). Jitihada hizi zimewezesha kamati 18,186 mpaka sasa kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa. Aidha, yameanzishwa Madawati ya Jinsia na Watoto 420 katika vituo vya Polisi, Madawati ya Jinsia 153 katika Jeshi la Magereza na Dawati katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa ajili ya kupambana na vitendo vya rushwa ya ngono kupitia Kampeni ya "Vunja Ukimya.

Ndugu Wanahabari, Serikali kupitia Wizara hii ina dhamana ya kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Sekta ya Mashirika yasiyo ya kiserikali haikutambulika katika kipindi cha uhuru kwani taasisi zilizojulikana kipindi hicho ni taasisi za Dini na vyama vya wafanyakazi. Mashirika haya yalianza kuibuka kwa kasi kuanzia miaka ya 1990 baada ya mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi.

Hivyo, katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa mashirika haya kwa kutunga Sheria Na. 24 ya mwaka 2002 ambayo ndiyo ilianza kuweka Taratibu za uratibu na usajili wa Mashirika hayo. Aidha, katika kuimarisha utoaji wa huduma za usajili na uratibu Serikali imefanikiwa kutengeneza Mfumo wa Kieletroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS) kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji kazi ili kuleta ufanisi na tija katika uratibu wa Mashirika hayo.

Ndugu Wanahabari, Mfumo huu umesaidia kupunguza gharama zilizokuwa zikitumiwa na wadau wa Mashirika kupata huduma mbalimbali kutoka Ofisi ya Msajili na kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu zikiwepo taarifa za fedha na taarifa za utekelezaji za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, pia kuongezeka kwa usajili kutoka Mashirika 404 mwaka 2005 hadi kufikia Mashirika 11,731 tarehe 29 Oktoba, 2021. Mashirika hayo yamechangia kuleta maendeleo kwa kutoa huduma za kijamii ikiwemo huduma za afya, elimu, kilimo, maji, mazingira, haki za binadamu, jinsia, na utawala bora.

Aidha, Serikali imeendelea kujenga na kuimarisha uhusiano kati yake na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuboresha mazingira ya Mashirika hayo kufanya kazi pamoja na kujenga uelewa kwa Mashirika hayo kuhusu masuala ya kodi, uhamiaji na uratibu wa pamoja wa mashirika katika ngazi zote zikiwemo Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa, Mashirika yenyewe na Sekta Binafsi.

Ndugu Wanahabari, Katika kuimarisha uhusiano huo, kwa mara ya kwanza katika historia, Serikali imefanikisha Mkutano wa sekta ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambao ulihutubiwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haya ni mafanikio makubwa kwa Sekta hii ambapo Serikali imeonesha dhamira ya kushirikiana nayo na kutambua mchango wao ambapo kwa mwaka 2020 jumla ya trillioni 1.1 zilitumika na mashirika hayo katika Miradi ya maendeleo na ajira za wazawa 6194 zilizalishwa na Mashirika hayo.
Vilevile, Serikali imefanikiwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.3/2019 pamoja na kutunga kanuni tatu zenye lengo la kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa sheria hiyo. Kuwepo kwa Sheria hii pamoja na kanuni zake imewezesha Mashirika mengi kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Taratibu, Mila na Desturi za Nchi na kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa mashirika hayo.

Mwisho niwatakie kila la Heri watanzania wote katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa nchi yetu. “MIAKA 60 YA UHURU; TANZANIA IMARA, KAZI IENDELEE”.


ayo

Ndugu Wanahabari Sekta ya Nishati ina historia ndefu kuanzia kipindi cha kabla ya kupata Uhuru wetu mwaka 1961 hadi kufikia kipindi hiki cha kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Taifa letu. Sekta hii imepitia maadiliko mbalimbali ya kimuundo, kisheria na kisera yakiwa na lengo la kuiboresha Sekta hii ili iweze kutoa huduma bora kwa watanzania. Wizara inayosimamia Sekta ya Nishati kwa mara ya kwanza iliundwa mwaka 1961 na iliitwa Wizara ya Biashara, Madini na Nguvu za Umeme, hata hivyo sekta ya nishati imekuwa ikitenganishwa au kuunganishwa na kuunda Wizara mbalimbali kutokana na mahitaji ya wakati husika.

Majina ya Wizara zilizohusisha sekta ya nishati kwa nyakati mbalimbali ni Wizara ya Biashara, Madini na Nguvu za Umeme (1961 – 1963); Wizara ya Viwanda, Madini na Nguvu Za Umeme (1963 -1965); Wizara ya Maji na Nguvu za Umeme (1970 – 1975);Wizara ya Maji, Nishati na Madini (1975 – 1980); Wizara ya Maji na Nishati (1980 - 1984); Wizara ya Maji, Nishati na Madini (1984 - 1985); Wizara ya Nishati na Madini (1985 - 1990); Wizara ya Maji, Nishati na Madini (1990 - 1995); Wizara ya Nishati na Madini (1995 – 2017); na Wizara ya Nishati (2017 mpaka Sasa).

Ndugu Wanahabari Mawaziri waliowahi kuongoza Wizara zinazohusu Sekta ya Nishati ni: Bw. A. H. Jamal, Bw. J. S. Kasambala, Bw. A. Z. Nsilo Swai, I. Elinawinga, Dkt. W. K. Chagula, Bw. Alnoor Kassum, Bw. John Samwel Malecela, Bw. Jackson Makweta, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Dkt. William Shija, Bw. Edgar Diones Maokola Majogo, Dkt. Abdallah Omari Kigoda, Bw. Daniel Yona, Bw. Ibrahim Msabaha, Bw. Nazir Mustapha Karamagi, Bw. Wiliam Mganga Ngeleja, Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Bw. George Simbachawene, Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Dkt. Medard Matogoro Kalemani na Waziri wa sasa ni Mhe. Bw. January Makamba.

Mawaziri Wadogo ambao wamewahi kutumika kumaanisha cheo cha sasa cha Naibu Waziri. Manaibu Waziri waliowahi kuongoza Wizara zinazohusu Sekta za Nishati na Madini ni: Bw. J. A. Mhaville, Bw. K. H. Ameir, Bw. Al-Noor Kassum, Bw. Mustapha C. Nyang'anyi, Bw. Manju Msambya, Bw. Edgar Diones Maokola Majogo, Meja Jakaya Mrisho Kikwete, Mhe. Ernest K. Nyanda, Mhe. Joseph F. Mbwiliza, Bw. Benard Membe, Bw. Lawrence Masha na Bw. Wiliam Mganga Ngeleja, Bw. Adam K. A. Malima, Bw. George Simbachawene, Bw. Steven Masele, Bw. Charles Kitwanga, Bw. Charles Mwijage, Dkt Medard Kalemani, Bi. Subira Mgalu na Naibu Waziri wa sasa ni Mhe. Wakili Stephen Byabato.

Makatibu Wakuu waliowahi kuongoza Wizara zinazohusu Sekta za Nishati na Madini ni: Bw. H. Halwenge, Bw. Jacob Dickson Namfua, Bw. Amon James Nsekela, Bw. Frederick Kilibata Lwegarulila, Bw. Harith Bakari Mwapachu, Bw. Athumani Iddi Janguo.

Bw. Samweli Rwakatare, Bw. Fulgence Michael Kazaura, Bw. Paul. J. Mkanga, Prof. Mark Mwandosya, Dkt. Ben Moshi, Bw. Rafael O. S. Mollel, Dkt. Jonas P.

Kipokola, Bw. Patrick Rutabanzibwa, Bw. Arthur G. K. Mwakapugi, Bw. David Kitundu Jairo, Bw. Eliakim Maswi, Prof. Justin Ntalikwa, Dkt. Hamisi Mwinyimvua, Mha. Zena Said na Katibu Mkuu wa sasa ni Mha. Leonard R. Masanja.

Ndugu Wanahabari Wizara ya Nishati ina Dira na Dhima kama ifuatavyo:

**Dira**
Kuwa taasisi yenye ufanisi na inayojali tija ili kuhakikisha kuwa rasilimali za nishati zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi kijamii na kiuchumi.

**Dhima**
Kuendeleza, kudhibiti na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za nishati kwa manufaa ya Watanzania.

**Malengo**
Wizara ya Nishati imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Wizara wenye malengo makuu sita (6) kama ifuatavyo:

i) Kuongeza uzalishaji wa umeme na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;

ii) Kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika matumizi mbalimbali ya nishati;

iii) Kuimarisha shughuli za utafiti na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia;

iv) Kuboresha rasilimali za Wizara ili kutoa huduma bora za nishati;

v) Kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Kuzuia Rushwa; na

vi) Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa waathirika.

Ndugu Wanahabari Majukumu ya Wizara ni Kusimamia Sekta ya Umeme na Nishati Jadidifu na Sekta ya Mafuta na Gesi.

## SEKTA YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Umeme na Nishati Jadidifu ni pamoja na:

1. Kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme nchini. Hadi kufikia Mwezi Septemba, 2021 upatikanaji wa umeme umefikia MW 1,609.91 ikilinganishwa na MW 17.5 kabla ya Uhuru. Mahitaji ya juu ya umeme nchini (peak demand) yamefikia MW 1,273.42 mwezi Oktoba, 2021. Uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyoungwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa umefikia MW 1,573.65 ambapo umeme wa nguvu ya maji (36.46%); gesi asilia 57.28(%); Mafuta (5.60%); na Tungamotaka (Biomass) (0.67%). Uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na

TANESCO ambayo huchangia (86.57%) na mitambo ya wazalishaji binafsi (IPPs/SPPs) ambayo huchangia (13.43%).

Uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyopo nje ya Gridi ya Taifa (off-grid) ni MW 36.26 ambapo TANESCO inamiliki mitambo yenye MW 31.26 na mzalishaji binafsi NextGen Solawazi (Kigoma) MW 5 kwa kutumia nguvu ya jua.

2. Kukamilika kwa mitambo wa kuzalisha umeme kwa nguvu ya maji ya: Hale MW 21 (mwaka 1964) na njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 11 kutoka Hale hadi Dar es salaam; Nyumba ya Mungu MW 8 (mwaka 1969) na njia ya umeme ya msongo wa kV 66 Kutoka nyumba ya Mungu hadi Arusha; Kidatu MW 240 (mwaka 1975- 1981); Mtera MW 80 (mwaka 1988); New Pangani Falls MW 68 (mwaka 1995); na kihansi wa MW 180 (mwaka 2000).

3. Kukamilika kwa ujenzi wa mitambo ya kufua umeme kwa kutumia gesi asili ya: Songas MW 189 (mwaka 2004); Ubungo I MW 102 (mwaka 2008); Ubungo II MW 105 (mwaka 2012); Tegeta MW 45 (mwaka 2009); Somanga Fungu MW 7.5 (mwaka 2010); Kinyerezi I MW 150 (mwaka 2016) na ujenzi wa njia za umeme wa kV 220 (Kinyerezi - Kimara) na kV 132 (Kinyerezi - Gongolamboto); Nyakato MW 63 (mwaka 2013), Kinyerezi II MW 248 (mwaka 2018) na Mtwara gas power plant MW 22 (mwaka 2019).

4. Kukamilika kwa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme za: kV 66 yenye urefu wa Kilomita 125 kutoka Mbala, Zambia hadi Sumbawanga (mwaka 2001); kV 220 kutoka Singida na Arusha (mwaka 1996) km 300; kV 132 kutoka Ubungo-Makumbusho (mwaka 2010) kilomita 7; kV 132 yenye urefu wa kilomita 80 kutoka Mtwara hadi Mahumbika (Lindi) pamoja na vituo vya kupoza umeme vya Mtwara na Mahumbika; kV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga kupitia Dodoma na Singida km 670 (mwaka 2016), kV 220 kutoka Makambako hadi Songea km 250 pamoja na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kupoza umeme vya Makambako, Madaba na Songea (mwaka 2018); na kV 220 Bulyanhuku Geita km 55 (mwaka 2020).

5. Kuendelea na Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu za: (REA I, REA II na REA III) na ambao umewezesha vijiji 10,361 kupatiwa umeme hadi kufikia mwezi Juni, 2021 sawa na asilimia 86 ya vijiji vyote 12,268; Kuendelea kuunganisha umeme wateja wapya nchini kwa kasi ambapo hadi Juni, 2021 jumla ya Watanzania wanaotumia nishati ya umeme wameongezeka kufikia takriban milioni 47 sawa na asilimia 78 ya Watanzania wapatao milioni 60.

6. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vipya vya kupoza umeme kwa ajili ya kuboresha upatikanaji na umeme vya Mbagala, Kipawa, Gongolamboto na Mburahati Mkoani Dar es Salaam; vituo vya kupoza umeme vya Njiro B, Mount Meru, Sakina, Unga Ltd, Kiltex na Themi Mkoani Arusha; vituo vya kupoza umeme vya Bomambuzi na Trade School Mkoani Kilimanjaro; ukarabati wa vituo vya kupoza umeme vya Mikocheni, Oysterbay, City Centre, Gongolamboto, Kariakoo, Mbagala, Chang'ombe, Kipawa na Ubungo Mkoani Dar es Salaam.

7. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vipya vya kupoza umeme vya Mbagala, Kipawa, Gongolamboto na Mburahati Mkoani Dar es Salaam; Njiro B, Mount Meru, Sakina, Unga Ltd, Kiltex na Themi Mkoani Arusha; Bomambuzi na Trade School Mkoani Kilimanjaro; Kukamilika kwa ukarabati wa vituo vya kupoza umeme vya Mikocheni, Oysterbay, City Centre, Gongolamboto, Kariakoo, Mbagala, Chang'ombe, Kipawa na Ubungo Mkoani Dar es Salaam; kukamilika kwa kituo cha kupoza umeme cha Dege, Kigamboni 132/33 kV pamoja na njia ya kV 132 toka Kibada hadi Dege.

8. Kukamilika kwa ujenzi wa njia za msongo wa kV 33, kV 11 na kV 0.4 kwa ajili ya kusambaza umeme katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe na Tanga kwa ufadhili wa Millenium Challenge Corporation (MCC).

.

9. Kukamilika kwa mradi wa kusambaza umeme wa Electricity V (2015) katika Wilaya za Bukombe, Kwimba, Magu, Mbogwe, Misungwi na Sengerema. Mradi huo ulihusu ujenzi wa njia ya kusambaza umeme wa Msongo wa kV 33, kufunga transfoma na kuwaunganishia umeme wateja 8,600.

10. Kujengwa na kukamilika "submarine cable" mbili zilizopita chini ya bahari zenye msongo vya Kilovoti 132 na kV 33 kwenda Visiwa vya Unguja na Pemba kV33 sawia.

11. Kukamilika mradi wa ORIO katika Miji ya Ngara, Biharamulo na Mpanda ambao umeimarisha upatikanji wa umeme katika miji hiyo.

12). Kukamilika kwa Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Nishati: Sera ya Taifa ya Nishati 1992, 2003 na 2015, Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008 na mabadiliko yake ya Mwaka 2020, Sheria ya Wakala wa Nishati Vijijini (2005), Sheria ya Mamlaka ya kuthibiti na Huduma za Nishati na Maji, (2001); Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme (Power System Master Plan) wa Mwaka 2008, 2012, 2016 na 2020, Mkakati na Mwelekeo wa Maboresho katika Sekta Ndogo ya Umeme (Electricity Supply Industry Reform Strategy and Action Plan (2014 – 2025), Programu ya Nishati Endelevu kwa Wote (Sustainable Energy for ALL (SE4ALL) Action Agenda 2015, Programu ya Umeme Vijijini (Rural Electrification Programu) 2016 na Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (Natural Gas Utilization Master Plan – NGUMP) 2016.

Kukamilisha kwa Kanuni (Rules) mbalimbali kwa ajili ya Udhibiti huduma za nishati. Kanuni hizo ni pamoja na: Kanuni za Uendelezaji na Usimamizi wa Miradi Midogo ya Umeme (The Electricity (Development of Small Power Projects) Rules, 2016, GN No. 217 of 2016); Kanuni za

Tozo na Ada za Leseni za Umeme (The Electricity (Licensing Fees) Rules, 2016, GN No. 287 of 2016); Kanuni za Usimamizi wa Mifumo ya Umeme (The Electricity (System Operation Services) Rules, 2016, GN No. 324 of 2016); Kanuni za Usimamizi wa Soko la Biashara ya Umeme (The Electricity (Market Operation Services) Rules, 2016, GN No. 325 of 2016); Kanuni za kusimamia Uuzaji umeme (The Electricity (Supply Services) Rules, 2017, GN No. 4 of 2017); na Usimamizi wa Biashara ya Rejareja ya Petroli Vijijini na kwenye Miji Midogo (The Petroleum (Retail Operations in Townships and Villages) Rules, 2017, GN No. 14 of 2017).

Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji umeme nchini. Kiwango cha upatikanaji wa umeme kwa ujumla (overall electricity access level) Tanzania Bara kimeongezeka na kufikia asilimia 78.4, ambapo mijini (urban electricity access level) imefikia asilimia 99.6 na vijijini (rural electricity access level) takriban asilimia 69.8.

15. Kuongezeka kwa idadi ya Taasisi zilizopatiwa umeme vijijini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya Taasisi na maeneo ya umma 15,200 yamepatiwa umeme chini ya Mpango wa REA ambapo taasisi za elimu (4,036), maeneo ya biashara (5,053), visima/mashine za maji (338), taasisi za afya (1,296) na nyumba za ibada (1,113).

16. Kuandaliwa na kuanza kutumika kwa mikataba mahsusi ya kuuziana umeme (Standardized Power Purchase Agreement - SPPA) kwa wawekezaji wadogo inayotoa mwongozo wa bei (Standandadized Power Purchase Tariff - SPPT), ambapo wawekezaji watano (5) - (TANWAT-MW 2.75, TPC-MW 20, Sao Hill-MW 16, Ngombeni-MW 0.5 na Mwenga-MW 3.36), wamepewa leseni za kuzalisha umeme wenye jumla ya MW 42.61.

17. Kukamilika kwa Mradi wa kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dar es Salaam. Mradi ulihusisha: ukarabati wa Kituo cha Ilala kV 132/33/11; ujenzi wa Jengo Jipya la “Control Center” la Ilala; ufungaji wa njia ya pili ya usafirishaji umeme wa Msongo wa kV 132 kutoka Ubungo hadi Ilala; kupanua Kituo cha kupoza umeme cha Msasani kV 33/11; ujenzi wa Vituo Vipya vinne (4) vya kupoza umeme wa kV 33/11 vya Jangwani Beach, Mwananyamala, Msasani na Muhimbili; ujenzi wa njia mpya za Msongo wa kV 33 kutoka Vituo vya kupoza umeme vya Makumbusho, City Centre na Tegeta kwenda Vituo Vipya vya Mwananyamala, Muhimbili, Jangwani na Msasani;.

18. Kukamilika kwa utekelezaji wa Programu ya Awamu ya Pili ya Mradi wa Sustainable Solar Market Package (SSMP – II) (2016). Mradi ilihusu ujenzi wa Mifumo ya Umeme Jua katika Wilaya nane (8) za Biharamulo, Bukombe, Chato, Kasulu, Kibondo, Namtumbo, Sikonge na Tunduru na kufungwa Jumla ya Mifumo Midogo ya Umeme 4,620 yenye uwezo wa kWp 115.

Kuunganishwa kwa Mikoa katika Gridi ya Taifa. Hadi kufikia Mwezi Septemmba, 2021 mikoa yote ya Tanzania Bara ilikuwa imeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa isipokuwa mikoa minne tu ya Kigoma, Katavi, Rukwa; baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Kagera. Hata hivyo, Mkoa na Kagera wanapata umeme kutoka nchi za Zambia na Uganda sawia.

Kusitisha matumizi ya mitambo ya kukodi ya binafsi ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta mazito katika kuzalisha umeme ikiwemo ya Aggreko na IPTL na kuokoa wastani wa jumla ya Shilingi bilioni 11.46 kwa mwezi.

21. Kusitisha uingizaji wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo, transfoma, nyaya na mita za LUKU ndani ya nchi na Kuendelea na kuhamasisha uzalishaji wa vifaa vya kuunganisha umeme hapa nchini na kuokoa wastani wa Shilingi bilioni 162.57 kwa mwaka.

22. Kugunduliwa kwa maeneo yanayoweza kuzalisha umeme kutokana na jotoardhi katika maeneo ya Songwe (Mbeya), Ziwa Manyara (Manyara), Maziwa Eyasi na Natron (Arusha), Luhoi (Rufiji-Pwani), ambapo takriban kati ya MW 150 – 650 zinaweza kuzalishwa, hivyo kuongeza vyanzo vya nishati nchini.

23. Kuwezesha matumizi ya umeme wa jua katika maeneo ya huduma za kijamii kama zahanati, shule za sekondari na taa za barabarani katika wilaya ya Sumbawanga vijijini kupitia mradi mkubwa wa umeme wa jua (Sustainable Solar Market Packages).

Ndugu Wanahabari, Mafaniko mengine kwa upande wa Sekta ya Umeme na Nishati Jadidifu ni:

(i) Kuendelea na Ujenzi wa Mradi wa kimkakati wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) MW 2,115 ambao hadi mwezi Septemba, 2021 ulikuwa umefika asilimia 55.1; Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Rusumo MW 80 ambao hadi Mwezi Septemba umefikia asilimia 82 na kuanza maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya kufua umeme ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222);

(ii) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kusafirisha umeme ikiwemo: kV 400 Julius Nyerere Hydro Power Project – Chalinze; kV 400 Singida – Arusha – Namanga; kV 220 Geita – Nyakanazi; kV 220 Rusumo – Nyakanazi; kV 220 kwa ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendo Kasi (SGR) Awamu ya Kwanza kutoka Dar es salaam hadi Morogoro na kV 220 kilomita 160, Morogoro – Dodoma – Singida (SGR II), kV 400 kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma hadi Sumbawanga kilomita 624; kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma kilomita 280; kV 132 yenye urefu wa kilomita 53.8 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe Mkoani Kigoma;

(iii) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Rusumo MW 80 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 82 na kuanza maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya kufua umeme ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222);

Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kusafirisha umeme ikiwemo: kV 400 Julius Nyerere Hydro Power Project –

Chalinze; kV 400 Singida – Arusha – Namanga; kV 220 Geita – Nyakanazi; kV 220 Rusumo – Nyakanazi;

(v) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kuunganisha gridi ya Taifa na nchi za jirani ambapo utekelezaji wa miradi ya Singida – Arusha – Namanga kV 400 wa kuunganisha nchi za Tanzania na Kenya, Iringa – Mbeya – Tunduma kV 400 wa kuunganisha nchi ya Tanzania na Zambia, na mradi wa Rusumo – Nyakanazi kV 220 utawezesha kuunganishwa kwa nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi; na

(vi) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme katika maeneo yaliyo pembezoni mwa miji yaani vijiji-miji (peri-urban). Jumla ya wateja 32,568 kati ya 37,713 wanaotarajiwa kuunganishwa wameshaunganishwa. Aidha, maeneo/vijiji/mitaa iliyopelekewa umeme ni 226 kati ya 227 inayotarajiwa kupelekewa umeme.

**SEKTA YA MAFUTA NA GESI**

Ndugu Wanahabari, Kabla ya uhuru biashara ya mafuta ilianza maeneo ya mwambao wakati Bw. Smith MacKenzie alipoanza kuingiza mafuta kwenye visiwa vya Zanzibar kama wakala wa Kampuni ya Shell. Kampuni hiyo ilipanua shughuli zake hadi maeneo ya Tanzania Bara na pia ilijihusisha na utafutaji wa mafuta hadi mwaka 1964.

Mwaka 1966, Serikali kwa kushirikiana na kampuni ya Agip iliunda kampuni ya Tanzania and Italian Petroleum Refinery (TIPER) ambayo ilihusika na kuagiza, kusafisha na kuuza mafuta kwa kampuni za usambazaji. Hata hivyo, kiasi cha mafuta kilichokuwa kinasafishwa na kampuni hiyo hakikukidhi mahitaji. Kutokana na sababu hiyo, mwaka 1969 Serikali ilianzisha Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1969 iliyotolewa kwenye Government Notice Na. 140 ya tarehe 30 Mei, 1969 na kuanza rasmi shughuli zake mwaka wa fedha 1973/74. TPDC pia ilikuwa na jukumu la kusimamia shughuli za utafiti wa awali na utafutaji mafuta kwa kushirikiana na kampuni nyingine chini ya mikataba ya Production Sharing Agreement (PSA).

Ndugu Wanahabari Serikali ilitoa leseni ya utafutaji wa mafuta ya petroli kwa Kampuni ya AGIP katika eneo la mwambao wa bahari ya Hindi kutoka Mtwara hadi Tanga. Shughuli za utafutaji wa mafuta zilianza rasmi mwaka 1973 na kampuni hiyo ikagundua gesi asilia katika eneo la Songo Songo mwaka 1974. Kwa kuwa lengo lilikuwa ni kupata mafuta, AGIP ilirudisha eneo hilo kwa Serikali mwaka 1975 na kuendelea na utafutaji wa mafuta. Wakati AGIP ikiendelea na juhudi za utafutaji mafuta, TPDC ilianza rasmi shughuli za uagizaji mafuta ghafi mwaka 1977. Mwaka 1980, Sheria ya Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta (Petroleum Exploration and Production Act, 1980) ilitungwa ili kuwezesha mikakati ya Serikali ya kuhamasisha ushiriki wa kampuni za kimataifa. Mwanzoni mwamiaka ya 1980, Serikali iliingia mikataba ya utafutaji (PSA) na kampuni za Shell, ELF, AMOCO na International Energy Development of America. Mwaka 1982, Kampuni ya AGIP iligundua tena gesi asilia katika eneo la Mnazi Bay na kurudisha eneo hilo kwa Serikali. Kwa upande wa mafuta, Serikali kupitia TPDC ilikuwa na utaratibu wa kuagiza mafuta ghafi na kuyasafisha nchini katika kiwanda cha TIPER. Kwa kuwa kiasi cha mafuta kilichosafishwa nchini hakikukidhi mahitaji, TPDC ilianza kuagiza mafuta yaliyosafishwa Mwaka 1983.

Mwaka 1984-1989, shughuli za utafutaji mafuta ziliongezeka baada ya TPDC kuanza kushiriki kikamilifu kwa kufanya kazi za kuchimba visima sita vya utafiti katika mwambao na kina kirefu cha bahari katika maeneo ya Songo Songo visima vitatu (3), Kimbiji visima viwili (2) na kisima kimoja (1) katika kina kirefu cha bahari.

Utafiti uliofanyika mwaka 1990 ulionesha kuwa eneo la Songo Songo lina hifadhi ya gesi asilia kiasi cha futi za ujazo bilioni 540. Aidha, gesi hiyo ilionekana kuwa na ubora wa hali ya juu kwa kuwa na kiasi kikubwa cha gesi ya methane, kutokuwa na sulphur na kuwa na kiasi kidogo cha maji. Serikali kupitia TPDC iliingia mkataba na kampuni ya mafuta ya India (ONGC) ya kuchimba visima vitatu katika eneo hilo ili kuhakiki kiasi cha gesi asilia kilichopo.

Kutokana na kuwepo kiasi kikubwa cha gesi asilia, Serikali ilibuni mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asili (Songo-Songo Gas to Electricity Project). Lengo la Serikali lilikuwa kutekeleza mradi huu kwa kutumia wawekezaji binafsi ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea katika ujenzi na uendeshaji. Mwaka 1994, kupitia utaratibu wa ushindani, Serikali iliichagua Kampuni ya Ocelot Energy Inc. na TransCanada Pipelines Ltd (OTC) consortium kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa Songo-Songo. Mkataba kati ya Serikali na Kampuni hiyo wa kuendeleza mradi ulisainiwa mwezi Oktoba, 1995. Kwa upande mwingine, Serikali ilifanya majadiliano na kampuni za World Wide Exploration (Australia), Dublin International Petroleum Ltd (Ireland), Kisoa (Dubai) na Hunt United (USA) kwa ajili ya utafutaji mafuta na gesi kwenye maeneo yaliyotarajiwa kupitishwa bomba la gesi. Kampuni hizo hazikuweza kugundua chochote.

Ndugu Wanahabari Mwaka 1996-2000 Serikali ilianzisha taratibu za kuwa na soko huria katika biashara ya mafuta ili kuleta ushindani ambao utarahisisha upatikanaji na unafuu wa bei za mafuta na bidhaa zake. Pamoja na kuanzishwa kwa soko huria bei za mafuta ziliendelea kupanda kiholela na kuleta adha kwa watumiaji. Kufuatia hali hiyo, mwaka 2006 Serikali iliunda Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Energy and Water Utilities Regulatory Authority-EWURA).

Kuanzishwa kwa Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, kuanzishwa kwa Taasisi ya Mdhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), kuwepo kwa Kanuni za utekelezaji kama vile za Bei ya Gesi Asilia, Ushirikishwaji wa Wazawa (Local Content Regulations), Ukusanyaji wa Tozo zitokanazo na mauzo ya gesi asilia (Annual levy – Fee and Charges), kumeimarisha utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa

shughuli za utafutaji mafuta na uzalishaji gesi asilia hapa nchini. Usimamizi wa sekta umezidi kuimarika baada ya kuwepo Sheria na Kanuni hizi ambazo zimeandaliwa na kupitishwa ndani ya miaka mitano, kuanzia mwaka 2015 hadi 2020.

Serikali iliweka mikakati ya kuhamasisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi na hadi kufikia mwaka 2015 idadi ya wazawa iliongezeka maradufu katika kazi za utafutaji mafuta na gesi na uzalishaji wa gesi asilia. Kwa mfano, idadi ya wazawa walioshiriki katika uchimbaji wa kisima cha Kitatange-1 katika bahari kuu mwaka 2016 walikuwa nane (8), wakati wazawa wapatao 58 kati ya wafanyakazi 160 waliokuwepo, walishiriki katika uchimbaji wa kisima cha Pilipili-1 kilichochimbwa katika bahari kuu mwaka 2018. Idadi ya wazawa walioajiriwa na kuchukuwa nafasi mbalimbali za uongozi katika Makampuni ya kigeni yanayotekeleza shughuli za utafutaji na uzalishaji gesi asilia hapa nchini imeongezeka. Kwa mfano, Katika kampuni la Statoil na Shell, idadi ya wazawa walioajiriwa katika nafasi za uongozi walikuwa chini ya asilimia 50%, wakati kwa mwaka 2020 imefika zaidi ya asilimia 90%.

Ndugu Wanahabari, Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015, Kampuni ya Mafuta ya Taifa (TPDC) imeanza kushiriki moja kwa moja katika utafutaji wa mafuta katika eneo la Eyasi Wembere lililopo katika Mikoa ya Tabora, Manyara na Simiyu kwa kutumia wataalamu wa ndani. Katika eneo la Eyasi Wembele, TPDC imefanikiwa kuchoronga visima viwili (2) vifupi (shallow borehole) vya utafiti wa awali, na inatarajia kuchoronga kisima kimoja (1) mwanzoni mwa Mwezi July 2020, hivyo kupelekea kuwa na jumla ya visima vitatu (3) katika eneo hilo. Pia, kwa sasa TPDC ipo katika maandalizi ya kuchoronga visima vya utafutaji wa mafuta na gesi katika Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini.

**Mafanikio katika Sekta ya Mafuta na Gesi**

Ndugu Wanahabari, tangu kupatikana kwa uhuru, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuiwezesha Sekta Mafuta na Gesi iweze kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi. Katika kipindi hicho mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwa ni pamoja na:

(a) Kugunduliwa kwa gesi asili katika maeneo ya Songo Songo (1974); Mnazi bay (mwaka 1982), Mkuranga (mwaka 2007), Kiliwani Kaskazini (mwaka 2008) na Kina Kirefu cha Bahari (mwaka 2010). Aidha, gesi iliyogunduliwa nchi kavu na kina kirefu cha bahari ni Futi za Ujazo Trilioni 57.54 mwaka 2021. Ugunduzi huo umewezesha kuanza kutumika kwa gesi asilia kama chanzo cha nishati, hususan kwa kuzalisha umeme, viwandani, majumbani na kwenye magari.

(b) Hadi mwezi Oktoba, 2021, viwanda 52 Jijini Dar es Salaam, Mkoani Pwani na Mtwara vinatumia gesi asilia. Aidha, vituo viwili vya kushindilia na kujazia gesi asilia kwenye magari jijini Dar es Salaam na Mtwara vinafanya kazi.

(c) Matumizi ya gesi asilia yamesaidia kupunguza utegemezi wa uzalishaji umeme kwa kutumia nguvu za maji ambapo hadi Novemba, 2021 takribani asilimia 60 ya umeme unazalishwa kwa kutumia gesi asilia.

(d) Katika kipindi cha mwaka 2004 hadi Juni, 2020 matumizi ya gesi asilia ya Mnazi Bay na Songo Songo yamesaidia Serikali kuokoa zaidi ya Shilingi Trilioni 38 ambazo zingetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya mitambo ya umeme na ya viwandani.

(e) Hadi mwezi Machi, 2021 mapato yanayotokana na mauzo ya gesi yamechangia zaidi ya Shilingi bilioni 208 katika Mfuko wa Mafuta na Gesi kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 baada ya kukamilika Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Mtwara/ Songosongo hadi Dar es Salaam.

(f) Hadi mwezi Desemba, 2020 Serikali imepata mapato ya zaidi ya shilingi bilioni 441 yanayotokana na kodi mbalimbali kuanzia mwaka 2015 baada ya kukamilika kwa mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Mtwara/ Songosongo hadi Dar es salaam.

(g) Shirika la Maendeleo ya Mafuta nchini (TPDC) limelipa zaidi ya shilingi bilioni 10 katika mwaka 2018/2019 na mwaka 2019/20 ikiwa ni gawio (Dividend) kwa Serikali.

(h) Hadi Juni, 2021 zaidi ya Magari 750 yamewekewa mfumo wa matumizi ya nishati ya gesi asilia.

(i) Kuanzishwa na kuendelea kuimarika kwa Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Bulk Procurement System – BPS) ambao umeongeza uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini na kupunguza gharama za uagizaji. Kuanzishwa kwa mfumo wa Bulk Procurement System (BPS) umeleta mafanikio mbalimbali ikiwemo:

i. Upatikanaji wa mafuta yanayotosheleza mahitaji ya nchi na yenye viwango vya ubora unaotakiwa wakati wote (security of supply);

ii. Kupata unafuu wa gharama za uletaji mafuta (premium) nchini kutokana na uagizaji wa pamoja (economies of scale) ambapo takribani shilingi bilioni 462 huokolewa kila mwaka ikilinganishwa na kabla ya mfumo husika kuanza kutumika;

iii. Kuwezesha Serikali kupanga ukusanyaji wa mapato kwa kuzingatia takwimu sahihi, kwani kumerahisisha katika kupanga/kufanya Makadirio ya Mapato ya kodi yatokanayo na mafuta yanaoyoingizwa nchini; na

iv. Kupungua kwa gharama za meli kusubiria nafasi ya kushusha mafuta (Demurrage Charges) kutokana na upangaji mzuri wa meli katika mfumo wa BPS, kwa sasa meli husubiria hadi siku 8 ikilinganishwa na siku 60 kabla ya mfumo wa BPS. Aidha, takribani bilioni 391 huokolewa kila mwaka ikilinganishwa demurrage zilizokuwa zikilipwa kabla ya mfumo wa BPS.

(j) Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu (PURA) ambapo kumewezesha kuongezeka kwa ushiriki wa Watanzania (Local Content) katika shughuli za

Mkondo wa Juu wa Petroli na kuimarika kwa Shughuli za Kaguzi za Gharama katika Mikataba ya PSAs (PSA Audit) ambapo kwa sasa kati ya PSA kumi (10) zilizofanyiwa ukaguzi, mbili (2) zimekamilika hadi mwaka 2020 na nane (8) zimekamilika hadi mwaka 2019. Kaguzi hizi hadi sasa zimewezesha kuokoa fedha takribani shilingi bilioni 35.91.

(k) Kuanzishwa kwa udhibiti wa huduma za nishati chini ya EWURA kumesaidia kuhakiki bei za bidhaa za mafuta. Aidha, upangaji wa bei elekezi (indicative price) na bei kikomo (cap price) katika biashara ya mafuta ya jumla na rejareja unafanyika kupitia mamlaka hiyo. Hatua hii imezingatia maslahi ya mtumiaji na muuzaji.

(l) Kuongezeka kwa ushiriki wa Watanzania katika miradi ya mafuta na gesi asilia ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba 2021 zaidi ya kampuni 1,000 zimeorodheshwa katika kanzidata inayomilikiwa na EWURA ikishirikiana na PURA iliyowezesha kampuni hizo kushiriki katika miradi mbalimbali.

(m) Kuanza kwa shughuli za utafutaji wa mafuta katika Kitalu cha Eyasi Wembere ambapo visima vifupi vitatu (3) vyenye kina cha urefu wa mita 300 vimechorongwa katika eneo la Kining'inila Wilayani Igunga (Tabora), Nyalanja wilayani Meatu (Shinyanga) na Luono wilayani Iramba (Singida);

(n) Kuanzishwa kwa Mradi Wa Kuchakata Na Kusindika Gesi Asilia (Liquefied Natural Gas - LNG). Mradi huu unalenga kuvuna, kuchakata na kusindika gesi asilia iliyogunduliwa kwenye kina kirefu cha Bahari ya Hindi katika Vitalu namba 1, 2 na 4 kuwa kimiminika ili iweze kuuzwa nje ya nchi na kutenga kiasi kingine kwa matumizi ya soko la ndani.

(o) Kuhuishwa kwa Bandari za Tanga na Mtwara katika kupokea Mafuta ambapo Bandari hizo zimeanza kupokea Mafuta kuanzia mwezi Julai, 2015 na Julai, 2018 mtawalia.

(p) Kujenga uwezo katika kusimamia Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa kudhamini mafunzo ya ufundi stadi kupitia vyuo vya ufundi stadi (VETA). Serikali imeendelea kutoa kozi mbalimbali zinazohusiana na mafuta na gesi katika vyuo vikuu hapa nchini kwa viwango vya Stashahada (Diploma), Shahada (Bachelor) na Uzamili (Masters).

(q) Kupungua kwa uchafuzi (uchakachuaji) wa mafuta kutoka wastani wa asilimia 19.2 mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa asilimia 4 mwezi Machi, 2020.

(r) Kuanzishwa kwa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi Kutoka Uganda Hadi Tanzania (East African Crude Oil Pipeline - EACOP). Mradi unaohusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi (crude oil) lenye urefu wa Kilomita 1,443 kutoka Kabaale nchini Uganda hadi Mkoani Tanga. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani bilioni 3.55 ambazo ni takriban Shilingi trilioni 8.1. Hadi sasa Serikali imewezesha Kusainiwa kwa Mkataba kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji (Host Government Agreement – HGA); Kusainiwa kwa Mkataba wa Ubia baina ya Wawekezaji (Shareholders' Agreement – SHA); Kukamilika kwa majadiliano na kuridhiwa kusainiwa kwa Mikataba ya uendeshaji wa Bandari ya Chongoleani na Mikataba ya ukodishaji wa ardhi ya mradi kwa maeneo ya kipaumbele na mkuza wa bomba; Kukamilika kwa malipo ya fidia kwa eneo la Chongoleani itakapojengwa Bandari; Kuendelea na ulipaji wa fidia kwa Wananchi wanaopisha ujenzi wa mradi; Utoaji wa elimu kwa wananchi katika maeneo yanayopitiwa na mradi ni kazi endelevu; na Kusainiwa kwa mkataba wa nchi zinazotekeleza mradi (Intergovernmental Agreement-IGA).

(s) Kuendeleza Ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Wizara zinazohudumu katika sekta ya Nishati kwa kutilia mkazo ushirikiano wa masuala ya umeme, na mafuta na gesi.

(t) Kuanzishwa kwa Miradi ya kimkakati ya usafirishaji wa Gesi Asili kwenda Kenya na Uganda. Miradi hii ipo katika hatua za awali za majadiliano na kukamilika kwake kutaleta manufaa katika kusambaza gesi asili maeneo mradi utakapopita kwa Tanzania; Serikali kupata fedha za kigeni kutokana na mauzo ya gesi katila nchi husika; na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na nchi za Kenya na Uganda.

(u) Kuwezesha ujenzi wa vituo vya mafuta vya gharama nafuu katika maeneo mbalimbali ya vijijini ili kuimarisha usalama na upatikanaji wa huduma bora za mafuta katika maeneo hayo.

(v) Kuongezeka kwa matumizi ya nishati ya kisasa ikiwemo gesi ya mitungi (Liquefied Petroleum Gas - LPG) kwa ajili ya kupikia katika maeneo ya mijini na vijijini.

**HITIMISHO**

Sekta ya Nishati ni miongoni mwa sekta muhimili katika kukuza na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Mwelekeo wa Sekta hii katika kipindi cha miaka ijayo ni kuhakikisha kuwa inaendelea kuchangia kwa kiwango kikubwa katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa, kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania. Hivyo, Wizara inadhamiria kuendelea kujiimarisha zaidi kiutendaji kwa lengo la kuzidi kuiimarisha Sekta hii ili iweze kutoa mchango stahiki kwa maendeleo ya Taifa letu.




# MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA NA MAFANIKIO KATIKA YA SEKTA YA MAJI

## 1. UTANGULIZI

### 1.1 Historia ya Wizara

Ndugu Wanahabari, huduma ya maji ilianza kutolewa katika miaka ya 1930 ambapo miradi mingi ilijengwa kwenye miji mikubwa na midogo, shuleni, vituo vya Wamisionari (misheni) na kwenye mashamba makubwa ya wakoloni hasa ya kahawa na katani. Ujenzi wa miradi ya maji kwenye vijiji ulianza mwishoni mwa miaka ya 1950. Mipango ya utoaji wa huduma ya maji iliandaliwa kukidhi mahitaji ya Serikali ya Ukoloni na hakukuwa na maelekezo ya kisera.
Ndugu Wanahabari, kuanzia mwaka 1970 hadi 1987, sekta ya maji iliendelea kusimamiwa na Wizara zilizokuwa na majukumu mengine. Mnamo tarehe 23 Machi 1987, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu Ally Hassan Mwinyi aliipa hadhi iliyokuwa Idara ya maji kuwa Wizara ikiitwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Wizara imeendelea kufanyiwa mabadiliko ya majina kwa nyakati tofauti na kuitwa: -

| NA | JINA LA WIZARA | MWAKA | WAZIRI |
|---|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Maji, Nishati na Madini | 1978 – 1982 | I. Elinewinga |
| 2 | Wizara ya Maji na Nishati | 1982 – 1984 | Ally Noor Kassum |
| 3 | Wizara ya Maji, Nishati na Madini | 1984 – 1985 | Ally Noor Kassum |
| 4 | Wizara ya Ardhi, Maji, Nyumba na Maendeleo ya Mijini | 1985 – 1987 | Dr. Pius Ng'w'andu |
| 5 | Wizara ya Maji | 1987 – 1990 | Dr. Pius Ngw'andu |
| 6 | | 1990 | Christian Kisanji |
| 7 | Wizara ya Maji, Nishati na Madini | 1990 - 1995 | Lt. Jakaya M. Kikwete |
| 8 | | 1995 | Jackson Makweta |
| 9 | Wizara ya Maji | 1996 - 1999 | Dr. Pius Ng'wandu |
| 10 | | 1999 - 2000 | Mussa Nkhangaa |
| 11 | Wizara ya Maji na Mifugo | 2000 – 2005 | Edward Ngoyai Lowasa |
| 12 | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | 2005 - 2006 | Stephen M. Wasira |
| 13 | Wizara ya Maji | 2007 - 2008 | Dr. Shukuru Kawambwa |
| 14 | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | 2008 - 2012 | Prof. Mark J. Mwandosya |
| 15 | Wizara ya Maji | 2012 - 2015 | Prof. Jumanne A. Magembe |
| 16 | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | 2015 | Prof. Makame M. Mbarawa |
| 17 | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | 2015- 2017 | Eng. Gerson H. Lwenge |
| 18 | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | 2017 - 2018 | Eng. Isack A. Kamwelwe |
| 19 | Wizara ya Maji | 2018 - 2020 | Prof. Makame M. Mbarawa |
| 20 | Wizara ya Maji | 2020 - | Jumaa H. Aweso |

### 1.2 Muundo na Majukumu ya Wizara ya Maji

Ndugu Wanahabari, Wizara ya maji inasimamia utekelezaji wa majukumu ya kulinda, kutunza, kuhifadhi vyanzo vya maji na kusimamia matumizi ya maji; kusimamia ubora wa maji; kusambaza majisafi, salama na ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya kijamii na kiuchumi; na kusimamia Taasisi za Sekta. Sera ya kwanza ya maji iliandaliwa mwaka 1991 na iliitwa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 1991. Kutokana na mabadiliko mbalimbali yaliyotokea kwa wakati huo, Sera hiyo ilifanyiwa mapitio na kuandaliwa kwa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 ambayo inatumika hadi sasa. Sekta ya maji imegawanyika katika maeneo makuu mawili ambayo ni usimamizi wa rasilimali za maji na usambazaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira mijini na vijijini.

## 2. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA SEKTA YA MAJI

Ndugu Wanahabari, nitumie pia fursa hii kuwashukuru waasisi wa Taifa hili kuanzia kwa Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Awamu ya Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Alhaji Ally Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Willium Benjamin Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu; Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne; Hayati Dr. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Awamu ya Sita.

Ndugu Wanahabari, katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru Sekta ya Maji imepata mafanikio kwa kutunza na kuhifadhi rasilimali za maji, kusimamia ubora wa maji, kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini.

### 2.1 Rasilimali za Maji

Aidha, kama bidhaa na huduma zinazohitajika migodini Ndugu Wanahabari, nchi yetu ina rasilimali za maji zipatazo mita za ujazo bilioni 126 ambapo bilioni 105 ni maji juu ya ardhi na bilioni 21 ni maji chini ya ardhi. Katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji, Serikali ilianzisha Bodi za Maji za Mabonde tisa zikiwa na kazi za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, utayarishaji wa mipango ya uwiano wa matumizi mbalimbali ya maji, kufanya utafiti na utunzaji wa mazingira ya vyanzo vya maji. Bodi za maji za mabonde zilizoanzishwa ni:-

i) Bonde la Mto Pangani lililoanzishwa mwaka 1991;
ii) Bonde la Mto Rufiji (1993);
iii) Bonde la Ziwa Victoria (2000);
iv) Bonde la Wami/Ruvu (2001);
v) Bonde la Ziwa Nyasa (2001);
vi) Bonde la Ziwa Rukwa (2001);
vii) Bonde la Kati (2004);
viii) Bonde la Ziwa Tanganyika (2004); na
ix) Bonde la Mto Ruvuma (2004).

Ndugu Wanahabari, mabonde saba kati ya tisa yaliyotangazwa nchini ni mabonde ya majishiriki. Mabonde hayo ni Bonde la Ziwa Victoria, Bonde la Mto Ruvuma, Bonde la Kati, Bonde la Mto Pangani, Bonde la Ziwa Nyasa, Bonde la Ziwa Tanganyika na Bonde la Ziwa Rukwa. Serikali kupitia Wizara ya Maji inashirikiana na nchi 17 pamoja na mashirika na taasisi za kimataifa zinazoshughulikia usimamizi wa rasilimali za majishiriki. Ushirikiano huo umeleta manufaa ikiwemo upangaji wa matumizi ya maji kwa pamoja, utunzaji wa vyanzo vya maji kuimarika na kuboreshwa kwa mahusiano katika sekta nyingine ikiwemo ya nishati na kilimo kupitia utekelezaji wa miradi ya pamoja inayotumia rasilimali za maji.

**2.2 Usimamizi wa Ubora wa Maji**

Ndugu Wanahabari, Serikali imeendelea kuimarisha maabara za maji ili ziendelee kutoa huduma kama inavyokusudiwa. Mafanikio katika eneo la usimamizi wa ubora wa maji ni pamoja na:

(i) Maabara ya Maji ya Mwanza iliteuliwa mwaka 2006 na Jumuiya ya Ulaya (EU) kupima ubora wa maji yanayotumika katika usindikaji wa minofu ya samaki kabla ya kusafirishwa kwenda katika soko la Ulaya na inaendelea na kazi hiyo;

(ii) Teknolojia ya kutumia mifupa ya ng'ombe yenye uwezo mkubwa wa kupunguza madini ya fluoride kufikia viwango ambavyo havina madhara kiafya imefanyiwa utafiti katika Maabara ya Ngurdoto Mkoani Arusha kwa muda mrefu na sasa inatumika kuwapatia Wananchi maji yenye kiwango cha fluoride kinachokubalika kitaifa; na

(iii) Maabara zetu za maji zimeendelea kutambulika kimataifa kwa kupatiwa ithibati (accreditation) kutokana na maboresho yaliyofanyika ambapo mpaka sasa maabara za Mwanza, Dar es salaam, Bukoba, Musoma, Kigoma, Singida na Shinyanga zimepatiwa ithibati.

2.3 Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira

2.3.1 Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

Ndugu Wanahabari, kwa kipindi kirefu, utoaji wa huduma ya maji vijijini ulikuwa ukisimamiwa na Wizara ya Maji pamoja na TAMISEMI. Hali hiyo ilileta changamoto katika usimamizi na utoaji wa huduma ya maji vijijini kutokana na wataalamu wa maji kuwajibika katika mamlaka mbili tofauti. Katika mwaka 2019, Serikali iliamua kuhamisha watumishi na majukumu ya Sekta kuwa chini ya Wizara yenye dhamana ya Maji. Mnamo mwezi Julai 2019, Serikali ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa lengo la kuimarisha usimamizi na utoaji wa huduma za maji katika maeneo ya vijijini.

Ndugu Wanahabari, mwezi Julai 2019, wakati RUWASA ikianza rasmi shughuli zake ilipokea miradi 632 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa iliyokuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji na miradi 177 ilkuwa imekamilika lakini haitoi huduma ya maji. Hadi kufikia Juni 2021, jumla ya miradi 566 kati ya miradi 632, sawa na asilimia 89.6 imekamilika. Vilevile, miradi 115 kati ya miradi 177, sawa na asilimia 65 ya miradi imeanza kutoa huduma kwa Wananchi. Miradi yote iliyosalia itakamilishwa ifikapo mwezi Juni 2022. Aidha, katika kipindi hicho, miradi mipya 912 ya maji vijijini ambapo kati ya miradi hiyo, miradi 458 imekamilika na kuanza kutoa huduma. Kukamilika kwa miradi hiyo na kuanza kutoa huduma kumeongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka asilimia 64.8 mwaka 2019 hadi asilimia 72.3 kufikia mwezi Juni 2021. Hadi sasa, jumla ya vijiji 8,708 kati ya 12,327 vinapata huduma ya maji.

Ndugu wanahabari, kwa kipindi kirefu miradi ya maji imekuwa ikitekelezwa na kukamilika lakini haiwi endelevu katika utoaji wa huduma iliyokusudiwa hususan katika maeneo ya vijijini. Katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara imefanya mageuzi makubwa ili kuhakikisha kuwa huduma ya maji inakuwa endelevu. Mageuzi yaliyofanywa ni ya kitaasisi, kifedha na kiufundi.

Ndugu wanahabari, kwa upande wa muundo wa kitaasisi Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 imetoa mwanya kwa Jumuiya za Utoaji Huduma za Maji Vijijini kuajiri wataalam wanaohusika na uendeshaji wa huduma ya maji ikiwa ni pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo. Hivi sasa, kuna vyombo vya utoaji wa huduma ya maji vijijini 2,115 ambavyo vimeajiri wahasibu 1,362 na mafundi 1,611.

Ndugu wanahabari, kwa upande wa ufundi hivi sasa RUWASA ipo kwenye mchakato wa kuanzisha vituo maalum vya utoaji wa msaada wa kiufundi katika ngazi ya mkoa (Regional Technical Support Centre), ambavyo vitakuwa na wajibu wa kusaidia Jumuiya za watoa huduma vijijini. Pia, vituo hivyo vitakuwa na vipuri vya mitambo ya maji ya teknolojia mbalimbali. Kuhusu fedha Wizara kupitia RUWASA ipo kwenye hatua za mwisho za kuanzisha utaratibu mpya wa makusanyo ya mauzo ya maji vijijini ambapo mauzo yote yatapitia kwenye mfumo wa makusanyo Serikalini (GePG). Hatua hii itaimarisha usimamizi wa makusanyo na matumizi ya fedha hizo kwa ajili ya uendelevu wa huduma za maji.

**2.3.2 Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini**

Ndugu Wanahabari, huduma ya maji mijini inatolewa na

Mamlaka za Maji ambazo zilianzishwa kwa Sheria ya Maji mijini ya mwaka 1997. Lengo lilikuwa kuboresha huduma ya maji katika maeneo ya mijini ili kuendana na kasi ya maendeleo ya miji. Hadi kufikia mwezi Oktoba 2021, jumla ya Mamlaka 96 za Miji Mikuu ya Mikoa, Miji midogo na Miradi ya Kitaifa zimeanzishwa na zinatoa huduma ya maji hapa nchini.

Ndugu Wanahabari, katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, wastani wa wakazi wa mijini wanaopata huduma ya majisafi na salama imeongezeka kutoka asilimia 25 ya wakazi wote wanaoishi mijini mwaka 1961 hadi kufikia wastani wa asilimia 86 mwaka 2021.

Ndugu Wanahabari, nipende kuwakumbusha baadhi ya miradi mikubwa iliyotekelezwa katika kipindi cha miaka 60:

i) Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka miji ya Kahama na Shinyanga;
ii) Uboreshaji wa huduma ya majisafi katika Jiji la Dar es Salaam kwa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu na Ruvu Chini na ulazaji wa bomba kuu;
iii) Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka miji ya Isaka na Kagongwa
iv) Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka miji ya Tabora – Igunga – Nzega;
v) Mradi wa maji kwa mji wa Lindi;
vi) Miradi ya maji na usafi wa mazingira katika miji ya Mwanza, Mbeya na Iringa;
vii) Mradi wa maji na usafi wa mazingira mjini Kigoma;
viii) Mradi wa kusambaza maji katika maeneo ya Kibamba na Kisarawe;
ix) Mradi wa Maji wa Misungwi;
x) Mradi wa Maji Nansio Ukerewe;
xi) Mradi wa Maji wa Longido;
xii) Mradi wa Maji wa Lamadi;
xiii) Mradi wa Maji wa Bokwa; na
xiv) Mradi wa Maji wa Sengerema.

Ndugu Wanahabari, aidha, miradi 26 ya maji mijini imekamilika na inatarajiwa kuzinduliwa na Viongozi wa Kitaifa.

**2.4 Chuo cha Maji**
Ndugu Wanahabari, kwa kutambua umuhimu wa kuwa na Wataalam wa maji nchini mwaka 1974 Serikali ilianzisha Chuo cha Maji ili kukabiliana na upungufu wa Wataalam ambao ulionekana mara baada ya Uhuru. Hadi sasa Chuo hicho kimetoa wataalam wengi ambao ni viongozi na watendaji wakuu katika ngazi mbalimbali ndani ya Wizara, katika Mashirika ya Umma na Vyuo Vikuu nchini na nje ya nchi. Chuo kinaendelea kuzalisha wataalam wengi wa fani mbalimbali zinazohusu maji ambao wanashiriki na kuchangia utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Maji na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Chuo kina uwezo wa kudahili wanafunzi 1,200 kwa mwaka katika ngazi ya astashahada, stashahada na shahada.

**2.5 Mfuko wa Taifa wa Maji**
Ndugu Wanahabari, Serikali ilianzisha Mfuko wa Taifa wa Maji kupitia Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na.12 ya mwaka 2009. Kwa sasa Mfuko unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019. Majukumu ya Mfuko ni kutafuta vyanzo vya fedha, kutoa fedha kwa watekelezaji kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na kufuatilia matumizi ya fedha hizo.

Ndugu Wanahabari, kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 vyanzo vya mapato ya Mfuko ni pamoja na fedha zitakazoidhinishwa na Bunge, misaada pamoja na fedha nyingine zitakazolipwa kwenye Mfuko kwa mujibu wa Sheria nyingine. Katikamwaka 2020/21 Mfuko wa T aifa wa Maji ulitengewaShilingi 175,912,837,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Kuanzishwa kwa Mfuko kumewezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kuwa mzuri ambapo kwa wastani shilingi bilioni 12 zinapatikana kila mwezi.

**2.6 Wataalam wa Sekta ya Maji**
Ndugu Wanahabari, Sekta ya maji imeendelea kuimarika kutokana na uwepo wa watumishi wa wenye weledi na wanaojituma. Hadi sasa kuna watumishi zaidi ya 8,700 ambao wanatekeleza miradi ya maji nchini.

**3. CHANGAMOTO**
Ndugu Wanahabari, changamoto kubwa katika sekta ya maji ni pamoja na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kulinda na kutunza miundombinu ili iendelee kutoa huduma endelevu kwa Wananchi mijini na vijijini. Aidha, athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi ambazo husababisha ukame, mafuriko na kupungua kwa upatikanaji wa rasilimali za maji sehemu mbalimbali nchini. Kwa mfano wakati tunapata uhuru idadi ya watu nchini ilikuwa milioni 10 na kila mtu aliweza kupata mita za ujazo 12,600 kwa mwaka, kiwango hiki kimepungua hadi kufikia mita za ujazo 2,250 kwa mtu kwa mwaka 2019.

**4. MWELEKEO WA SEKTA YA MAJI**
Ndugu Wanahabari, katika kufikia malengo ya Sekta, Wizara inatekeleza mipango yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2016 - 2030; Awamu ya Tatu ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025; na ahadi mbalimbali za Viongozi wa Kitaifa. Kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Serikali imeendelea kutekeleza mipango mbalimbali ambayo imekusudia kufanikisha malengo ya Sekta ya Maji yafuatayo: -

i) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa Wananchi waishio mijini inafikia zaidi asilimia 95 mwaka 2025;

ii) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa Wananchi waishio vijijini inafikia asilimia 85 mwaka 2025; na

iii) Kuwa na Rasilimali za maji endelevu kwa kulinda, kutunza, kuendeleza na kutafuta vyanzo vipya vya maji.

Ndugu Wanahabari, ili kufikia malengo ya sekta ya maji kwa wakati, Wizara imeweka mikakati ya utekelezaji iliyojikita katika maeneo mahsusi yafuatayo:-

a) Ujenzi wa Mabwawa ya Kimkakati
Ndugu Wanahabari, katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Wizara imepanga kujenga mabwawa makubwa (Farkwa, Kidunda, Songwe na Ndembera/Lugoda) na mabwawa ya ukubwa wa kati (Dongo) katika sehemu mbalimbali nchini.

b) Mpango wa Kutumia Vyanzo vya Uhakika vya Maji
Ndugu Wanahabari, Serikali imepanga kutekeleza miradi itakayotumia vyanzo vya maji vya uhakika vikiwemo maziwa makuu ya Tanganyika, Nyasa na Victoria na mito mikubwa kama mto Ruvuma, Rufiji, Kiwira, Songwe na Kagera. Miradi hiyo itahusisha ujenzi wa mtandao wa kusafirisha maji kutoka maeneo yenye maji mengi na kuyapeleka kwenye maeneo yenye uhaba (Intra Basin Water Transfer - IBWT). Baadhi ya miradi inatakayotumia vyanzo hivyo ni pamoja na:

- Mradi wa kutoa maji Mto Kiwira kupeleka Jiji la Mbeya

- Mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kupeleka miji ya Masasi, Mtwara, Nanyamba na Nanyumbu;

- Mradi wa kutoa maji Ziwa Nyasa ambao utahudumia wakazi wapatao 150,000 katika vijiji 30;

- Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka miji na vijiji iliyoko kandokando ya Ziwa hilo ikiwemo mkoa wa Simiyu, Geita na Mwanza unatarajiwa kuhudumia wananchi wapatao 2,854,2000 walipo katika vijiji 300.

- Mradi wa Kutumia Ziwa Tanganyika kupeleka katika Mikoa ya Katavi, Kigoma na Rukwa unatarajiwa kuwanufaisha wakazi wapatao 616,000 wa vijiji 73.

c) Kuimarisha Usimamizi na Utunzaji wa Rasilimali za Maji

Ndugu Wanahabari, Wizara itaendelea kuelimisha Wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na kuweka mkazo katika usimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Na. 11 ya mwaka 2009 na Kanuni zake ikiwemo kuwatoza faini wanaoharibu au kuchafua vyanzo vya maji.

d) Utekelezaji wa mradi wa maji wa Miji 28

Ndugu Wanahabari, Serikali imepata mkopo wenye masharti nafuu wa Dola milioni 500 kutoka Benki ya Exim ya India kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika miji 28 ya Tanzania Bara na mji wa Zanzibar. Miji hiyo ni Kasulu, Kayanga-Omurushaka, Mpanda, Kilwa Masoko, Muheza, Handeni, Korogwe, Pangani, Tarime, Rorya, Mafinga, Songea, Makonde, Urambo, Sikonge, Wanging'ombe, Makambako, Ifakara, Chemba, Chamwino, Geita, Mugumu, Rujewa, Chunya, Njombe, Manyoni, Kiomboi na Singida.

e) Programu na miradi inayotekelezwa

Ndugu Wanahabari, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inatekeleza miradi mbalimbali kupitia program za malipo kwa matokeo zinazolenga kuhakikisha uendelevu wa miradi ya maji vijijini. Hadi sasa jumla ya Shilingi bilioni 1,176 ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini. 688.81 zimetumika kuboresha huduma ya maji vijijini. Aidha, katika mwaka 2021/22, Serikali imepanga kutekeleza miradi.

Ndugu Wanahabari, Serikali inaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika mkoa wa Simiyu utakaogharimu Shilingi bilioni 444.6. Hadi sasa, Mtaalam Mshauri anaendelea kukamilisha usanifu wa mradi huo. Kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha wananchi wapatao 800,000 wa wilaya za Bariadi, Itilima na Busega. Aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya uboreshaji wa huduma ya maji katika miji ya Dodoma, Dar es Salaam, Mugango – Kiabakari, Mtwara, Mbeya, Mwanza, Bunda, Kyaka – Bunazi na Same – Mwanga – Korogwe.

f) Miradi inayotekelezwa kwa Kutumia Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO - 19
Ndugu Wanahabari, kupitia fedha za UVIKO 19 ambazo Wizara ya Maji imetengewa kiasi cha Shilingi bilioni 139.4 itatekeleza miradi 218 nchini kote. Aidha, jumla ya Seti 25 za mitambo ya kuchimba visima inanunuliwa, seti tano za mitambo ya ujenzi wa mabwawa na seti nne za vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi zitanunuliwa. Kwa hali hiyo ningependa niwahakikishie kuwa malengo ya kitaifa kwa Sekta ya Maji ifikapo 2025 yatafikiwa bila wasiwasi.

**5. HITIMISHO**
Ndugu wanahabari, nawashukuru kwa kuja na kupitia kwenu nimepata fursa ya kuongea na watanzania, kwa namna ya pekee niwashukuru viongozi wote wa kitaifa walioongoza kuanzia tunapata uhuru mpaka sasa kwani wametoa kipaumbele katika kuhakikisha sekta ya maji inakuwa hivi ilivyo, ninawashukuru wadau wote waliochangia kwa njia moja ama nyingine kufanikisha majukumu ya sekta ya maji. Ninapenda kuwashukuru wananchi wote




# MAFANIKIO YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KATIKA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

## UTANGULIZI

Ndugu wanahabari, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuwezesha kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Pia napenda kuchukua fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake kwa nchi hii ambayo ameijalia tunu za amani, utulivu, mshikamano, umoja na mtangamano katika kipindi chote cha miaka 60 ya Uhuru wa nchi yetu. Tunu hizo zimetuwezesha kuendelea na shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa na pia kutoa fursa kwa wananchi kuweza kufanyia shughuli zao za maendeleo.

Ndugu Wanahabari, Wizara ya Fedha na Mipango inatambua mchango wenu katika kuwaelimisha na kuwafikishia wananchi taarifa muhimu zinazohusu masuala ya kiuchumi na kijamii ili umma wa Watanzania uweze kuhabarishwa. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa mchango wenu huu mkubwa kwa Taifa.

Ndugu Wanahabari, kama tunavyofahamu sasa hivi tuko katika kipindi cha maandalizi ya kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru tulioupata kutoka kwa mkoloni mwaka 1961. Sote tunafahamu kuwa tangu wakati huo, jitihada mbalimbali zilifanyika zikiongozwa na viongozi wakuu wa nchi yetu nchini ya utawala wa chama cha TANU na baadae CCM kuanzia mwaka 1977. Ni kipindi ambacho uchumi wa nchi yetu umeendelea kuwa imara japo ulipitia katika vipindi mbalimbali vya mabonde na milima.

## MWENENDO WA UKUAJI WA UCHUMI

Ndugu Wanahabari, Tangu uhuru, uchumi wa Tanzania umepitia katika nyakati mbalimbali za mafanikio ya kiuchumi pamoja na changamoto kadhaa zikiwemo ukame katika miaka ya mwanzoni mwa 1970 na 2012, mdororo wa uchumi wa mwaka 2008, vita vya Kagera mwaka 1978 pamoja na ugonjwa wa UVIKO mwaka 2020. Hata hivyo, Serikali kupitia mikakati mbalimbali iliweza kujikwamua kutokana na magumu hayo iliyopitia na hii iliwezesha katika historia ya Tanzania kutokuwa na ukuaji hasi wa uchumi (recession) tangu uhuru. Takwimu zinaonesha kuwa ukuaji wa uchumi katika kipindi cha miaka sitini ya uhuru ulikuwa ukipanda na kushuka kutokana na sababu mbalimbali lakini haujawahi kufikia ukuaji hasi. Wastani wa ukuaji wa uchumi katika kipindi cha Serikali ya awamu ya kwanza (1967 – 1985) iliyoongozwa na mwasisi na Baba wa Taifa hili Hayati Mwalim Juluis Kambarage Nyerere ulikuwa asilimia 3.1; Serikali ya awamu ya pili (1986 – 1995) asilimia 3.0, Serikali ya awamu ya tatu (1996 – 2005) asilimia 5.7, Serikali ya awamu ya nne (2006 – 2015) asilimia 6.3, na Serikali ya awamu ya tano (2016 – 2020) asilimia 6.5.

Ndugu Wanahabari, mwaka 2020, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2019. Sababu kuu ya kupungua kwa kasi ya ukuaji ni athari za hatua zilizochukuliwa na mataifa mbalimbali duniani ambao ni washirika wakubwa wa biashara wa Tanzania katika kukabiliana na janga la UVIKO-19. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na mataifa hayo ni pamoja na kufunga mipaka, kusitisha safari za ndege za kimataifa na kusitisha baadhi ya shughuli za kiuchumi zinazohusisha mikusanyiko. Hatua hizo zilisababisha uchumi wa dunia kuporomoka mwaka 2020 ambapo nchi nyingi zilikuwa na ukuaji hasi na kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ni nchi 11 tu zilikuwa na ukuaji chanya kati ya nchi 45. Pamoja na kupungua kwa kasi ya ukuaji, Tanzania iliweza kuwa na ukuaji chanya kutokana na kutochukua hatua za kuzuia kufanyika kwa shughuli za kiuchumi isipokuwa kwa kipindi kifupi tu cha robo ya pili ya mwaka 2020 ambapo ilisitisha kwa muda baadhi ya shughuli zinazohusisha mikusanyiko ya watu kama shule, sanaa na burudani. Athari za janga la UVIKO-19 zilijitokeza zaidi katika shughuli za kiuchumi za malazi na huduma ya chakula pamoja na sanaa na burudani ambazo zilikuwa na ukuaji hasi mwaka 2020.

Ndugu Wanahabari, Serikali ya awamu ya sita imeingia madarakani katika kipindi ambacho dunia bado inapambana na athari za kiuchumi na kijamii za janga la UVIKO-19. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021, (Januari – Juni) uchumi umekua kwa asilimia 4.7 ikilinganishwa na asilimia 5.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kupungua kwa kasi ya ukuaji katika kipindi hicho kumetokana na athari za UVIKO-19 katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Shughuli nyingi za kiuchumi zimeendelea kuwa na viwango chanya vya ukuaji katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021 ingawa kasi yake ilipungua ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2020.

## TANZANIA KUINGIA KATIKA UCHUMI WA KATI

Ndugu Wanahabari, Tanzania ilikuwa nchi ya kipato cha chini kwa miaka 59 tangu kupata uhuru hadi mwaka 2020 Benki ya Dunia ilipoitangaza kwa mara ya kwanza kuwa nchi ya Uchumi wa Kati wa Chini. Hii ni baada ya mageuzi makubwa ya kiuchumi yaliyofanyika ambayo yalipelekea wastani wa pato kwa mtu (Per capita GNI) kuvuka kiwango kilichowekwa na Benki ya Dunia cha dola za Marekani 1,036 kufikia dola za Marekani 1,100 mwaka 2019. Mwaka 2020, uchumi wa nchi nyingi duniani uliyumba lakini pamoja na kasi ya ukuaji wa Tanzania kupungua bado tulifanikiwa kubaki ndani ya kundi la nchi za kipato cha kati cha chini kwa wastani wa Pato kwa mtu la dola za Marekani 1,080. Tanzania iliingia katika kundi la nchi ya uchumi wa kati mapema zaidi ikilinganishwa na malengo ya Dira ya Taifa ya kufikia hadhi hiyo mwaka 2025. Hii ilitokana na matokeo chanya katika vigezo vya kiuchumi ikiwemo kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi, utulivu wa thamani ya shilingi na mfumuko wa bei uliobaki katika wigo wa tarakimu moja kwa muda mrefu.

Ndugu Wanahabari, wastani wa Pato kwa mtu ulikuwa unaongezeka mwaka hadi mwaka kutoka wastani wa dola za Marekani 178.3 (1990 – 1995), wastani wa dola za Marekani 365 katika serikali ya awamu ya tatu, dola za Marekani 747 awamu ya nne, na wasatani dola za Marekani 1,010 awamu ya tano kwa kutumia kipimo cha Atlas cha Benki ya Dunia. Halikadhalika, kiwango cha umaskini kimeendelea kupungua ambapo kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi kimepungua hadi asilimia

25.7 mwaka 2020 kutoka asilimia 38.6 mwaka 1992. Kupungua kwa kiwango cha umaskini kumetokana na jitihada za Serikali katika kuboresha huduma za msingi za jamii ikiwemo upatikanaji wa maji, umeme, huduma za afya, utoaji wa elimumsingi bila ada na uwezeshaji wa kaya maskini kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF).

**MFUMUKO WA BEI**

Ndugu Wanahabari, mfumuko wa bei nao ulipitia katika nyakati mbalimbali za kupanda na kushuka. Kiwango cha juu kabisa cha mfumuko wa bei kilikuwa mwaka 1984 (asilimia 36.1), mwaka 1990 (asilimia 35.9) na mwaka 1994 (asilimia 35.3). Sababu kubwa ilikuwa ni kutokana na ukame na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia. Aidha, mara ya mwisho kuwa na mfumuko wa bei wa tarakimu mbili ilikuwa mwaka 2012 ambao ulifikia asilimia 16.1. Baada ya hapo, mfumuko wa bei umeendelea kupungua mfululizo hadi sasa.

dugu Wanahabari, katika kipindi cha miaka nane (8) mfululizo iliyopita (2013 – 2020), mfumuko wa bei umeendelea kuwa wa tarakimu moja na kubakia ndani ya malengo tuliyojiwekea sambamba na vigezo (convergency criteria) vilivyowekwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (asilimia 8) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (asilimia 3 – 7). Mwaka 2020, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2019. Kushuka kwa kiwango cha mfumuko wa bei kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo utekekezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kutengamaa kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, kuimarika kwa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu nyingine duniani, na kuimarika kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani.

Ndugu wanahabari, Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha bei ya bidhaa na huduma ikiwemo vifaa vya ujenzi kama vile saruji, nondo, bati, marumaru hazipandishwi kiholela. Jitihada hizo ni pamoja na kufanya majadiliano na wazalishaji ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa na kudhibiti usambaji ili kuendana na mahitaji na hivyo kupunguza uwezekano wa kuongezeka kwa mfumuko wa bei.

**SEKTA YA FEDHA**

Ndugu wanahabari, Sekta ya fedha ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Hadi miaka ya 1990 sekta ya fedha ilihusisha sekta ya benki pekee. Kutokana na mahitaji ya huduma za kifedha kuongezeka, sekta ya fedha imekuwa ikifanyiwa maboresho mbalimbali ikiwemo 'First and second generation financial sector reforms". Maboresho hayo yaliweka mazingira wezeshi katika sekta ya fedha kwa kutungu sera, sheria, kanununi na miongozo ya uendeshaji wa sekta hiyo. Kupitia maboresho hayo, Serikali ilianzisha sekta ndogo za masoko ya mitaji na dhamana, mifuko ya hifadhi ya jamii, bima na huduma ndogo za fedha. Hadi mwaka 2020, kulikuwa na benki na taasisi za fedha 55, kampuni za bima 32, kampuni za soko na mitaji 28 na mifuko ya hifadhi ya jamii 2. Kwa upande wa sekta ndogo ya fedha hadi Agusti 2021 kulikuwa na watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili (Non deposite taking) 549, watoa ndogo za fedha daraja la tatu (SACCOSS) 460 na watoa huduma ndogo daraja la nne (Vikundi vya kijamii vya huduma dogo za fedha) 11,149. Jitihada hizo zimewezesha kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma jumuishi za fedha kutoka asilimia 56 mwaka 2013 hadi asilimia 65 mwaka 2017 na inatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 75 mwaka 2022. Hii inaenda sambamba na mageuzi ya kiteknolojia yaliyowezesha kutumia mitandao ya simu za mkononi kuanzia miaka ya 2000 mwanzoni kufikisha huduma za fedha maeneo mengi nchini yakiwemo yale ambayo hayana matawi ya benki.

**KIWANGO CHA KUBADILISHA FEDHA**

Ndugu Wanahabari, katika kipindi cha mwaka 1966 hadi 1992 Serikali ilikuwa ikidhibiti viwango vya kubadilisha fedha (Fixed exchange rate). Utaratibu huu kwa kiwango kikubwa ulichangia mdororo wa uchumi katika miaka ya 1980 kwani thamani ya shilingi ilishuka kwa kiwango kikubwa na kusababisha akiba ya fedha za kigeni kupungua na kuongezeka kwa mfumuko wa bei. Katika kipindi hicho, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kukabiliana na mdodoro wa uchumi zikiwemo Structural adjustment Program (1982-1983) na Economic recovery program I &II (1986 & 1989). Kufuatia maboresho hayo, Tanzania ilianza kutumia viwango vya ubadilishaji fedha vinavyotegemea bei ya soko (Floating exchange rate policy) mwaka 1993. Utekelezaji madhubuti wa sera hiyo umeendelea kuimarisha thamani ya shilingi dhidi ya dola ya marekani na sarafu nyingine duniani. Tangu mwaka 1993 Serikali ilipoanza kutumia mfumo wa soko huria, thamani ya shilingi kwa sehemu kubwa ilikuwa inapungua japo kwa kiwango kidogo cha tarakimu moja. Hata hivyo, kiwango cha juu kabisa cha kuporomoka kwa thamani ya shilingi tangu wakati huo kilikuwa asilimia 20.1 mwaka 2015 na baada ya kuimarishwa kwa usimamizi katika sekta hiyo, thamani ya shilingi ilikuwa inapungua kwa kasi ndogo ya chini ya asilimia tatu (asilimia 3).

**MWENENDO WA MAPATO YA NDANI**

Ndugu Wanahabari, japo kulikuwa hakuna utaratibu wala mifumo madhubuti ya ukusanyaji wa mapato, katika Serikali ya awamu ya kwanza iliweza kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi milioni 5,557.3 kati ya mwaka 1966 – 1985. Kiasi hicho kilichokusanywa katika kipindi hicho kilikuwa cha wastani wa asilimia 18.3 ya Pato la Taifa. Jitihada mbalimbali ziliendelea kuchukuliwa na Serikali ili kuimarisha usimamizi wa mapato ikiwemo kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania mwaka 1997 na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Jitihada hizo zilizaa matunda ambapo mapato ya ndani yaliongezeka kufikia wastani wa shilingi milioni 130,853 katika kipindi cha awamu ya pili, wastani wa shilingi milioni 954,339 katika kipindi cha awamu ya tatu, wastani wa shilingi milioni 6,403,888 katika kipindi cha awamu ya nne, na wastani

wa shilingi milioni 18,957,084 katika kipindi cha awamu ya tano.

Ndugu Wanahabari, pamoja na mapato kuongezeka mwaka hadi mwaka yamekuwa hayafikii malengo tuliyoweka kwa mwaka husika. Hii ni changamoto inayotufanya kushindwa kufikia malengo yetu ya kuwafikishia wananchi huduma za msingi pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mathalani katika mwaka 2020/21 mapato ya ndani yalifikia asilimia 85.6 ya lengo. Mapato ya ndani yaliyokusanywa katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 yalifikia shilingi bilioni 5,492.1 sawa na asilimia 89.0 ya lengo la shilingi bilioni 6,170.9. Kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani kulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kukwepa kodi hususan kupitia njia za magendo, uhamishaji wa faida kwa kampuni zenye mtandao wa kimataifa na kutokutoa stakabadhi za kielektroniki wakati mauzo yanapofanyika hivyo kuathiri ukusanyaji wa mapato na uwepo wa majanga kama vile kama vile UVIKO – 19 ulioathiri shughuli za kiuchumi na kibiashara.

**MWENENDO WA MATUMIZI YA MAENDELEO**

Ndugu wanahabari, kabla ya mwaka 2015 bajeti ya Serikali ya maendeleo ilikuwa chini ya asilimia 25 ya bajeti yote. Hata hivyo, mwaka 2015/16 Serikali ilifanya maamuzi ya kuhakikisha bajeti ya maendeleo inaongezeka na kufikia kati ya asilimia 30-40 ya bajeti yote. Hatua hii pamoja na mambo mengine iliwezesha Serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati kwa ajili ya kuvutia uwekezaji na kukuza uchumi. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa (SGR) ambapo tangu uhuru Tanzania imekuwa ikitumia reli iliyojengwa na mkoloni kwa kiwango cha mita geji. Kutokana na mabadiliko ya teknolojia na kuongezeka kwa mahitaji, Serikali ilifanya uamuzi wa kutengeneza reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR) itakayounganisha Tanzania na nchi jirani ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) umefikia asilimia 93.0. Aidha, tangu nchi ipate uhuru Serikali ilikuwa na wazo la kutekeleza mradi wa kufua umeme katika bwawa la Mto Rufiji ili kuongeza uzalishaji wa umeme kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya majumbani na viwandani pamoja na kupunguza gharama za uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta. Wazo hilo halikutekelezwa hadi mwaka 2016 ndipo Serikali iliamua kuanza utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere utakaozalisha Mw. 2115 ambapo ujenzi umefikia asilimia 55.6. miradi mingine ni pamoja na: usambazaji wa umeme vijijini ambapo vijiji 10312 kati ya 12,317 sawa na asilimia 83.7 vimeunganishwa na huduma ya umeme; ujenzi wa barabara na madaraja ambapo hadi 2021 mtandao wa barabara uliojengwa kwa kiwango cha lami umefikia km 13,643.45; na uboreshaji wa huduma za jamii ikiwemo elimu, afya na upatikanaji wa maji.

**NAKISI YA BAJETI**

Ndugu wanahabari, katika historia ya nchi hii, tulishawahi kuwa na akiba ya bajeti (budget surplus) kwa miaka mitatu tu tangu uhuru nayo ni mwaka 1989 (shilingi milioni 6,782), mwaka 1990 (shilingi milioni 8,052) na mwaka 1991 (shilingi milioni 9601). Miaka mingine yote kwa takwimu zilizopo toka mwaka 1966 ilikuwa na nakisi ya bajeti (Budget deficit). Uwiano wa nakisi ya bajeti kwa Pato la Taifa ulikuwa mkubwa miaka ya mwishoni mwa 1970 na mwanzo mwa 1980 kwa wastani wa asilimia 7 ya pato la Taifa. Hata hivyo, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi, hali iliyowezesha kurejesha nakisi hiyo katika wigo uliokubalika kwa nchi za SADC na EAC wa chini ya asilimia 3.

**MISAADA NA MIKOPO**

Ndugu Wanahabari, Serikali katika vipindi tofauti imekua ikipokea misaada kutoka Wadau wa Maendeleo na Mashirika ya Fedha ya kimataifa kutokana na uwepo wa nakisi ya bajeti ili kugharamia utekelezaji wa bajeti kwa ufanisi. Aidha, utegemezi wa misaada na mikopo nafuu imeendelea kupungua kutoka wastani wa asilimia 20.7 ya bajeti yote katika miaka ya 2010/11 - 2014/15 hadi wastani wa asilimia 9.2 mwaka 2015/16 - 2019/20. Kupungua kwa utegemezi katika misaada na mikopo nafuu kulitokana na juhudi za Serikali katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani. Aidha, kiasi cha mikopo kiliongezeka na kutoka shilingi bilioni 2,357.3 mwaka 2011/12 hadi shilingi bilioni 5,214.9 mwaka 2020/21. Kuongezeka kwa kiwango cha mikopo kulitokana na uhitaji mkubwa wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayochangia ukuaji wa uchumi. Hadi Juni 2021, deni la Serikali lilifikia shilingi bilioni 64,497.8 ikilinganishwa na bilioni 56,449.8 Juni 2020. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha deni serikali linaendelea kuwa himilivu na mikopo inaelekezwa kwenye miradi yenye tija kwa Taifa.

**IDADI YA WATU**

Ndugu Wanahabari, idadi ya watu nchini imeendelea kuongezeka kila mwaka ambapo katika awamu ya kwanza (1966 -1985), wastani wa idadi ya watu ulikadiriwa kuwa milioni 16.1, awamu ya pili watu milioni 24.3, awamu ya tatu watu milioni 32.3 awamu ya nne watu milioni 42.4 na awamu ya tano watu milioni 51.8. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 na viashiria muhimu vya mabadiliko ya idadi ya watu kama vifo na vizazi, Tanzania ilikadiriwa kuwa na watu milioni 57.6 mwaka 2020 ikilinganishwa na watu milioni 55.9 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Ni matumaini yetu kuwa sensa ya watu na makazi itakayofanyika mwaka 2022 itatoa idadi halisi ya watu nchini. Hivyo, nitumie fursa hii kuendelea kutoa rai kwa watanzania wote kushiriki katika zoezi la kuhesabiwa ili kuiwezesha Serikali kupanga mipango ya maendeleo kwa ufanisi.

Ndugu Wanahabari, kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Mipango niwashukuru tena kwa ushirikiano wenu ambao mmekuwa mkiutoa pindi tunapowahitaji, na niwahakikishie kuwa Wizara itaendelea kufanya kazi nanyi bega kwa bega katika masuala yote ya kujenga uchumi wa Taifa letu ambayo wananchi wana haki ya kupata taarifa.

KAZI IENDELEE Asanteni kwa kunisikiliza




MAFANIKIO NA MAENDELEO YA SEKTA ZA UJENZI NA UCHUKUZI

KATIKA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

Ndugu Wanahabari, Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye kwa rehema zake nyingi ametujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo hii. Aidha, nipende kuchukua fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na kwa kuijalia nchi yetu tunu za amani, mshikamano, umoja katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru waTanzania Bara. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ni moja ya Wizara muhimu katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye jukumu la kusimamia masuala ya miundombinu na huduma za usafiri na usafirishaji ambazo ni kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara (1961 - 2021) tumepata mafanikio makubwa katika Sekta za Ujenzi na Uchukuzi. Aidha, kumekuwa na mabadiliko mbalimbali ya kisera yaliyoendana na utungwaji wa sheria kadhaa zilizowezesha sekta hizi mbili kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Ndugu Wanahabari, nikianza na Sekta ya Ujenzi, Nikianza na Sekta ya Ujenzi, Sekta hii ambayo inasimamia ujenzi, matengenezo na ukarabati wa barabara, madaraja, vivuko, viwanja vya ndege, nyumba na majengo ya Serikali imekwenda sambamba na ongezeko la Bajeti kutoka Shilingi bilioni 2.1 mwaka 1962/63 hadi kufikia zaidi ya Shilingi trilioni 1.5 mwaka 2021/22.

Sekta hii kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), inasimamia mtandao wa barabara zenye urefu wa takribani kilometa 36,361.88 ambapo kilometa 12,215.51 ni barabara kuu na kilometa 24,146.37 ni barabara za mikoa. Aidha, kati ya barabara hizo, barabara kuu za lami ni kilometa 9,058.2, na za mikoa ni kilometa 2,128.22.

Mtandao wa Barabara nchini umekuwa ukiboreshwa na kuongezeka kwa kuweka mkazo katika ujenzi na ukarabati wa Barabara Kuu, Barabara za Mikoa, Barabara za Wilaya na madaraja kwa lengo la kuleta uhakika na nafuu ya usafiri na usafirishaji nchini. Aidha, kipaumbele kimetolewa katika kutunza, kutengeneza na kukarabati Barabara kupitia mipango na miradi mbalimbali iliyoandaliwa na Wizara ambapo mpaka sasa wastani wa asilimia 88 ya barabara kuu na za mikoa zipo katika hali nzuri.

Ndugu Wanahabari, mafanikio yaliyojitokeza katika mtandao wa barabara tangu kupata uhuru mwaka 1961 ni kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami kutoka kilometa 1,360 (1961) hadi kufikia kilometa 11,186 (Septemba 2021) na hivyo kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Mfano ni kwa wakazi wa kanda ya ziwa ambao walikuwa wanatumia zaidi ya saa 30 kusafiri kwa kutumia usafiri wa mabasi kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na wakati mwingine kulazimika kupitia nchi jirani kama vile Kenya (Nairobi), ambapo kwa sasa wasafiri wanatumia chini ya saa 15 kwa safari hiyo.

Katika kipindi hiki, Serikali inaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 1,593 ambazo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Baadhi ya miradi inayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa barabara za Mzunguko wa Nje Dodoma (Dodoma Outer Ring Road) kilometa 112.3, Tabora – Koga – Mpanda kilometa 365.98 na Kabingo – Kibondo Town – Kasulu – Manyovu kilometa 286.5; Pangani – Tanga (km 50) pamoja na Barabara ya zege ya Lusitu – Mawengi (km 50)

Ndugu Wanahabari, mnamo mwaka 2001 Serikali iliamua kuanzisha miradi maalum ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami na madaraja kwa kutumia fedha zake yenyewe hali ambayo iliongeza kasi ya ujenzi wa barabara za lami na madaraja nchini. Mathalani baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na sehemu ya barabara ya kuunganisha Dar es Salaam na Mikoa ya kusini ya jumla ya kilometa 223 inayohusisha sehemu ya Somanga – Matandu (km 33), Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95) na Mbwemkuru – Mingoyo (km 95); sehemu ya barabara ya kuunganisha Dar es Salaam, Mikoa ya Kati na Kanda ya Ziwa ya jumla ya kilometa 455 inayohusisha sehemu ya Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 120), Geita – Usagara (km 90), Dodoma – Manyoni (km 127), na Manyoni – Singida (km 118) na katika Mkoa wa Tanga, barabara ya Korogwe – Handeni – Mkata (km 119) ilijengwa.

Aidha, barabara zingine zilizojengwa na kukamilika ni Nzega – Tabora – Urambo – Kaliua – Kazilambwa (km 294.8); Isaka – Ushirombo – Lusahunga (km 242) pamoja na Uyovu – Bwanga – Biharamulo (km 112); Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 171.80); Sumbawanga – Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 151.60) pamoja na Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112); Mbeya – Lwanjilo – Chunya – Makongolosi (km 111); Tabora – Nyahua – Chaya – Manyoni sehemu za Tabora – Nyahua (km 85) na Manyoni hadi Chaya (km 89.4). Vilevile, ujenzi umekamilika kwa Barabara ya Korogwe – Same – Mkumbara (km 172).

Kwa upande wa madaraja yaliyokamilika kujengwa kwa kutumia fedha za ndani ni pamoja na Daraja la Nyerere – Dar es Salaam (mita 680); Magufuli katika mto Kilombero - Morogoro (mita 384), Lukuledi II - Lindi (mita 30), Momba - Songwe (mita 84), Mara – Mara (mita 94), Sibiti - Singida (mita 82), Magara – Manyara (mita 84) na Daraja la Ruhuhu (linaunganisha Mikoa ya Ruvuma na Njombe (mita 98.7).

Ndugu Wanahabari, Ukuaji wa miji na kuongezeka kwa idadi ya watu kumesababisha kuwepo kwa msongamano wa magari katika barabara hususan katika miji na majiji makubwa. Serikali katika kutatua changamoto hiyo imeanza utekelezaji wa miradi ya kupunguza msongamano katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Arusha na Tanga pamoja na miji ya Iringa na Babati ambapo jumla ya kilometa 102.4 za barabara zilipangwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hizo zimekamilika na nyingine mpya zipo katika hatua mbalimbali za

utekelezaji.

Miradi ya Barabara na Madaraja yenye lengo la kupunguza msongamano kwenye majiji ambayo imekamilika ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Usagara - Kisesa (km 17), upanuzi wa barabara ya Mwaloni Furahisha – Pasiansi – Uwanja wa Ndege mkoani Mwanza (km 5.32), upanuzi wa Barabara ya Sakina – Tengeru (km 14.1) na ujenzi wa barabara ya mchepuo ya Arusha (Arusha Bypass), mkoani Arusha (km 42.4). Vilevile, ujenzi wa Daraja la Juu la Mfugale (Mfugale Flyover), kwenye Makutano ya TAZARA na Daraja la Juu la Kijazi (Kijazi Interchange), kwenye makutano ya Ubungo mkoani Dar es Salaam.

Miradi mingine iliyokamilika ni upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 19.2), kuwa njia nane, Upanuzi wa Barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3) na Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya I. Aidha, Kwa sasa ujenzi wa Awamu ya II ya BRT pamoja na Daraja la Gerezani unaendelea.

Pia, katika Jiji la Mbeya Serikali inaendelea na juhudi mbalimbali za kupunguza msongamano ambapo tayari Upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Igawa – Uyole – Songwe – Tunduma (km 217) na barabara ya mchepuo katika Jiji la Mbeya (Uyole – Songwe Bypass) yenye urefu wa kilometa 49 umekamilika. Kwa upande wa Jiji la Dodoma tayari ujenzi wa barabara za mzunguko wa Nje (Dodoma Outer Ring Roads) zenye urefu wa kilometa 112.3 unaendelea.

Ndugu Wanahabari, sera ya Serikali ni kuunganisha Makao Makuu ya mikoa yote nchini, ambapo hadi sasa mikoa yote imeungwa kwa barabara za lami isipokuwa mikoa michache ambayo hata hivyo Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya barabara ya kuunganisha mikoa hiyo. Miradi inayoendelea kutekelezwa kwa sasa ni pamoja na:

Ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Tabora – Usesula – Komanga – Kasinde – Mpanda (km 365.98) inayounganisha mikoa ya Katavi na Tabora.

Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe – Ndulamo – Makete (km 107.4), inayounganisha mikoa ya Njombe na Mbeya.

Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Makutano – Natta (sehemu ya Makutano – Sanzate (km 50) na sehemu ya Wasso (Loliondo) – Sale Jct (km 49) kwa ajili ya kuunganisha mikoa ya Mara na Arusha.

Serikali ina mpango wa kuanza ujenzi wa sehemu ya Mkiwa – Itigi – Noranga (km 56.9), kwa ajili ya kuunganisha mikoa ya Singida – Mbeya.

Ujenzi wa barabara sehemu ya Vikonge – Ruhafe (km 25) ipo katika hatua ya mwisho ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami, Barabara hiyo inaunganisha mikoa ya Katavi na Kigoma.

Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kibaoni – Sitalike (km 71.0), sehemu ya Kibaoni – Mlele inayounganisha mikoa ya Katavi na Rukwa.

Ndugu Wanahabari, pamoja na kuunganisha makao makuu ya Mikoa, Serikali pia imeunganisha nchi yetu na nchi jirani za Msumbiji, Kenya, Uganda, Rwanda na Zambia kupitia mtandao wa barabara.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Barabara za Mpemba – Isongole (km 50.3) (Tanzania/Malawi), Kabingo – Kasulu – Manyovu (km 260) (Tanzania/Burundi), na Bagamoyo – Tanga – Horohoro/Lungalunga (km 240) (Tanzania/Kenya

Vilevile, miradi ya barabara ambayo inaunganisha nchi yetu na nchi jirani ambayo usanifu umekamilika ni pamoja na Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105) (Tanzania/Uganda). Aidha, barabara ya Bugene – Kasulo/Benako (km 124) sehemu ya Bugene – Chato/Buligi (km 60) ipo katika hatua za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya kuunganisha Tanzania na Burundi.

Ndugu Wanahabari, katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru, Serikali pia imejenga madaraja makubwa na madogo nchini. Madaraja makubwa yaliyokamilika ni pamoja na Daraja la Kirumi (Mara), Daraja la Mto Kagera (Kagera), Daraja la Rusumo (Kagera), Daraja la Mkapa (Pwani), Daraja la Umoja (Mtwara), Daraja la Kikwete (Kigoma), Daraja la Sibiti (Singida), Daraja la Mara (Mara), Daraja la Mlalakuwa (Dar es Salaam), Daraja la Momba (Rukwa), Lukuledi II (Lindi), Ruhuhu (Ruvuma/Njombe), Magufuli (Morogoro), Magara (Manyara), Nyerere (Dar es Salaam), Kavuu (Katavi), Ruvu Chini (Pwani) na mengine mengi.

Madaraja makubwa yanayoendelea kujengwa ni pamoja na Daraja la Tanzanite (Dar es Salaam), Msingi (Singida), Daraja Jipya la Wami (Pwani), Kitengule (Kagera), Gerezani (Dar es Salaam) na Kigongo – Busisi (Mwanza). Aidha, madaraja mengine 7 yapo kwenye hatua ya usanifu ya ujenzi. Madaraja hayo ni Sukuma (Mwanza), Simiyu (Mwanza), Mkenda (Ruvuma), Mtera (Dodoma/Iringa), Godegode (Dodoma), Malagarasi Chini (Kigoma) na Ugalla (Tabora) yako kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji.

Ndugu Wanahabari, kumekuwa na mafanikio makubwa katika kuongeza idadi ya wataalamu katika taaluma ya kihandisi nchini ambapo usajili wao umekuwa ukiongezeka mwaka hadi ya mwaka.

Kwa mfano, mwaka 1961 wakati nchi yetu inapata uhuru wahandisi wazawa walikuwa wawili (2), tu ambapo kwa sasa wahandisi waliosajiliwa wamefikia 32,145.

Aidha, Bodi ya Usajili wa Wahandisi inaendelea kusimamia utekelezaji wa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa Wahandisi Wataalam na Wahandisi Washauri unaojulikana kama Continuing Professional Development (CPD) pamoja na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi Wahitimu (Structured Engineers Apprenticeship Programme - SEAP) 3,000 ambao wapo katika miradi yote mikubwa inayoendelea kute

kelezwa hapa nchini.

Ndugu Wanahabari,

Serikali inaendelea kuwajengea uwezo na kusajili makandarasi wazawa kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), ambapo hadi sasa makandarasi 12,382 wamesajiliwa kati ya hao makandarasi wazawa ni 11,916 na wa nje ni 466.

Serikali imekuwa ikitenga miradi mbalimbali ili kuwajengea uwezo makandarasi wazawa. Miradi hiyo ni pamoja na: -

Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kaliua – Urambo (km 28), iliyojengwa kwa ubia na Makandarasi M/s Salum Motor Transport Co. Ltd, M/s Annam Road Works Co Ltd na M/s Jossam Company Ltd;

Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Rudewa – Kilosa (km 24), unaotekelezwa na kampuni ya Umoja Kilosa JV ambayo ni ubia wa Makandarasi M/s Kings Builders Ltd, M/s Comfix & Engineering Ltd, Emirate Builders Co. Ltd, Halem Construction Company Ltd, Audacia Investment Ltd na Pioneer Builders Ltd;

Miradi mingine ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bulamba – Kisorya (km 51), na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nyakanazi – Kibondo (km 50), unaotekelezwa na Kampuni ya M/s Nyanza Road Works.

Upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 19.2), kutoka njia mbili hadi nane pamoja na ujenzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji unaotekelezwa na Kampuni ya M/s Estim Company Ltd na

Ujenzi wa Kiwanja Kipya cha Ndege cha Geita unaotekelezwa na Kampuni ya M/s Mayanga Contractors Company Ltd.

Ndugu Wanahabari, Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) imeendelea kuimarisha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi wa ndani (Contractors Assistance Fund - CAF), ili kuwawezesha kupata dhamana katika mabenki bila rehani ya kitu chochote.

Mpango huu unatoa dhamana kwa ajili ya zabuni (Bid Security) na malipo ya awali (Advance Payment Guarantees) kwa Makandarasi wadogo na wa kati (Madaraja ya 4 – 7 kawaida na 2-3 maalum). Aidha, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 Makandarasi 1,168 wamenufaika na huduma za mfuko huo.

Ndugu Wanahabari, kwa upande wa Vivuko, wakati Tanzania Bara inapata Uhuru wake mwaka 1961 hapakuwepo na vivuko vya kisasa isipokuwa vivuko 5 vya kuvutwa kwa Kamba. Kwa kuzingatia umuhimu wa vivuko kama kiungo muhimu kwenye usafirishaji, Serikali iliendelea kununua na kujenga vivuko vya kutumia Engine vinavyofikia 33 katika maeneo 22 hapa nchini na Boti 10 zinazotoa huduma katika maeneo mbalimbali wakati wa dharura.

Vivuko vinavyotoa huduma kwa sasa ni:-
• Dar es Salaam - MV Magogoni, Kigamboni na MV Kazi
• Mwanza - MV Mwanza, MV Sabasaba, MV Sengerema, MV Misungwi, MV Ukara, MV Ukara II, MV Temesa, MV Ilemela, MV Kome II na MV Tegemeo
• Geita - MV Chato na MV Chato II
• anga - MV Pangani, MV Pangani II na MV Bweni
• Kigoma - MV Ilagala na MV Malagarasi
• Kagera - MV Kyanyabasa na MV Ruvuvu
• Mtwara - MV Kilambo, MV Tangazo, MV Mafanikio na MV Kuchele
• Pwani - MV Mkongo na MV Kilindoni
• Mara - MV Musoma na MV Mara
• Lindi - MV Kitunda (Lindi) na MV Lindi.
• Ruvuma - MV Ruhuhu

Ndugu Wanahabari, kwa upande wa Nyumba na Majengo ya Serikali, Katika kipindi cha miaka 60, Serikali imejenga na kukarabati majengo ya Ofisi kwa ajili ya matumizi ya baadhi ya Wizara, Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya, Nyumba za Majaji, Viongozi na watumishi wa Serikali katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara.

Aidha, Serikali imefanya ukarabati mkubwa wa Ikulu ya Dar es Salaam na Dodoma pamoja na Jengo la Mahakama ya Biashara Kivukoni (Dar es Salaam).

Ndugu Wanahabari, Serikali pia inaendelea kuimarisha usafiri wa anga ambapo Viwanja vya Ndege vyenye lengo la kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji vimeendelea kujengwa na kukarabatiwa katika mikoa mbalimbali nchini. Hadi sasa Serikali ina jumla ya Viwanja vya Ndege 58 vilivyo chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na kimoja (01) kilicho chini ya KADCO.

Miradi iliyotekelezwa/inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na
• Jengo la tatu la kisasa la abiria (TB – III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere limejengwa;
• Uboreshaji wa Viwanja vya Ndege vya Mwanza (Phase I), Tabora (Phase II), Kigoma (Phase I), Bukoba (Phase I), Dodoma, Mpanda na Mafia ambavyo vimekalimika kwa kiwango cha lami;
• Ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Mtwara, Iringa, Songwe, Geita, Songea na Musoma upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji;
• Mkataba wa Ujenzi wa Mradi mpya wa Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Msalato Awamu ya Kwanza (package 1) unaohusisha ujenzi wa miundombinu ya Kiwanja (Airport Infrastructure); ambao utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3). umesainiwa tarehe 13 Septemba, 2021 kwa gharama ya Shilingi Bilioni 165,627,031,495.52. Kwa sasa Mkandarasi ameanza utekelezaji wa mkataba huo; na
• Maandalizi ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Moshi, Sumbawanga, Tabora (Awamu ya 3) Kigoma (Awamu ya pili), Shinyanga, Mwanza (Jengo jipya la abiria) na Arusha yanaendelea.

Serikali pia inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza

ujenzi wa viwanja vya ndege vya Lindi, Lake Manyara, Tanga na Simiyu.

Aidha, katika mpango wa miaka mitano ijayo kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022-2025/2026 Serikali imepanga kutekeleza ujenzi na ukarabati wa Viwanja vingine vya Ndege kadri ya upatikanaji wa fedha baada ya miradi inayoendelea kukamilika.

Ndugu Wanahabari, ili kuweza kuzilinda barabara zetu Serikali imefunga mizani 64 ya kupima uzito wa magari kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Udhibiti Uzito wa Magari ya Jumuiya Afrika Mashariki ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2018 katika maeneo mbalimbali ya kimkakati ya barabara kuu. Lengo la kufunga mizani hizo ni kuzuia uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja unaotokana na uzidishaji uzito wa magari na hivyo kufanya miundombinu hiyo kudumu kwa kipindi kilichokusudiwa wakati wa usanifu wake.

Vilevile Serikali imefunga mizani ya kisasa yenye uwezo wa kupima gari likiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion) katika mizani 13 hapa nchini ikiwa ni pamoja na Mizani za Nala – Dodoma, Njuki – Singida-Dakawa – Morogoro, Mikese (South) – Morogoro, Vigwaza – Pwani, Mpemba - Songwe na Wenda – Iringa kwa ajili ya kutatua changamoto ya foleni katika mizani. Katika mwaka huu wa fedha 2021/22, Wizara inatarajia kufunga mizani ya aina hiyo katika vituo vya Mikumi – Morogoro, Kimokouwa – Arusha na Rubana – Mara.

Aidha, Serikali inaendelea na uboreshaji wa mifumo ya usimamizi wa vituo vya mizani ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kupunguza mianya ya rushwa katika vituo vya mizani kwa kufunga mfumo wa kamera za kisasa za CCTV ambapo hadi sasa jumla ya mizani 13 zimefungwa mfumo huo. Mfano wa mizani hizo ni Mpemba (Songwe), Mikumi (Morogoro), Vigwaza (Pwani), Himo (Kilimanjaro), Njuki (Singida), Mutukula (Kagera), Usagara (Mwanza), Mikese (Morogoro), Nala (Dodoma), Mingoyo (Lindi) na Makuyuni (Arusha). Katika mwaka huu wa fedha 2021/2022, Wizara inatarajia kufunga mfumo wa aina hiyo kwenye mizani 42.

Ndugu Wanahabari mbali na mafanikio niliyoyaeleza, Sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo ni pamoja na:-

Uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya barabara (Road Reserve) unaofanywa na wananchi kwa ajili ya shughuli za kijamii katika maeneo ya hifadhi ya barabara na hivyo kusababisha usumbufu na uchelewaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara (Ujenzi), inaendelea na mpango wa kuelimisha umma kwa njia ya vyombo vya habari, vipeperushi, mikutano na semina ili waweze kufahamu vyema kuhusu Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007. Aidha, Wizara (Ujenzi), inashirikiana na wadau wengine kuhakikisha kuwa eneo la hifadhi ya barabara halichukuliwi kwa matumizi mengine.

Ndugu Wanahabari, changamoto nyingine ni uwezo mdogo wa mtaji kwa makandarasi wazawa hivyo kushindwa kushiriki katika fursa za miradi ya maendeleo kutokana na masharti ya upatikanaji wa dhamana za zabuni. Dhamana za ushiriki wa kazi, na mitaji ya kuwawezesha kufanya kazi kutoka mabenki kuwa ngumu na kutozingatia mahitaji halisi ya shughuli za kihandisi. Aidha, kushindwa kupata mitaji kunawafanya makandarasi kushindwa kukua na kupata fursa ambazo zitawawezesha kukua na kumudu miradi mikubwa.

Katika hili, Serikali inaendelea kuwashirikisha kikamilifu makandarasi wazawa katika miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara na madaraja kwa lengo la kuwajengea uwezo. Vilevile, Serikali kupitia Bodi ya Usajili ya Makandarasi (CRB), imeanzisha mfuko wa kusaidia makandarasi wazawa (wadogo na wa kati) ili kupewa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa makandarasi hao bila ya kuweka rehani kitu chochote.

Ndugu Wanahabari, changamoto nyingine ni Uzidishaji wa Uzito wa Magari unaofanya na Wasafirishaji na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara na madaraja.

Wizara (Ujenzi), inaendelea kusimamia utendaji kazi katika mizani za kudhibiti uzito wa magari barabarani. Jitihada nyingine ni ujenzi wa vituo vya pamoja vya ukaguzi (One Stop Inspection Stations – OSIS), ambavyo vinajengwa katika ukanda wa kati na Ukanda wa Dar es Salaam (TANZAM). Ujenzi wa vituo hivyo utasaidia kupunguza msongamano wa magari katika vituo vya mizani hasa magari yanayosaforosha mizigo nje ya nchi (Transit Vehicles).

Ndugu Wanahabari, Sekta ya Uchukuzi: Miundombinu ya uchukuzi pamoja na huduma zake ni kichocheo kikubwa katika kukuza uchumi wa nchi yeyote. Tanzania hatupo nyuma katika kutekeleza sera ya uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi hususan miundombinu ya reli, bandari na viwanja vya ndege. Aidha, tumeendelea kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara, reli, maji, anga pamoja na huduma za hali ya hewa.

Tukianza na usafiri wa reli; usafiri wa reli ni nguzo muhimu ya kuwezesha na kuchochea ukuaji wa uchumi na biashara. Hii inatokana na ukweli kwamba usafiri wa reli ni wa gharama nafuu ikilinganishwa na usafiri wa Anga na Barabara hususan katika usafirishaji wa mizigo mikubwa kwa umbali mrefu kuanzia kilometa 400 na zaidi. Kutokana na umuhimu huo, mwaka 1961, wakati Tanzania Bara inapata uhuru ilikuwa na mtandao wa reli wenye urefu wa km 2,068 unaojumuisha reli ya Dar es Salaam –Tabora (km 840); Tabora – Kigoma (km 411); Tabora – Mwanza (km 379); na Tanga – Moshi – Arusha (km 438). Mtandao huo ni wa reli nyembamba yenye upana wa mita moja (Meter Gauge Railway - MGR) na kihistoria ulijengwa katika kipindi ambacho Tanganyika ilikuwa chini ya utawala wa

Wajerumani na sehemu ya mtandao huo ilijengwa wakati Tanganyika ikiwa chini ya utawala wa Waingereza.

Baada ya Uhuru wa Tanzania Bara mwaka 1961, Serikali iliongeza mtandao wa reli ya kati kwa kujenga reli mpya ya jumla ya km 639 ili kufikia masoko mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Ongezeko hili la mtandao wa reli limewezesha reli ya Kati kuwa na mtandao wenye urefu wa jumla ya km 2,707. Reli zilizoongezeka ni pamoja na Ruvu Junction – Mruazi Junction (km 188); Kilosa – Kidatu branch line (km 108); Kaliua – Mpanda branch line (km 210); Manyoni – Singida branch line (km 115); na Kahe –Taveta (Mpakani na Kenya) branch line (km 18).

Ndugu Wanahabari, pamoja na uwepo wa mtandao wa reli ya Kati (Metre Gauge Railway - MGR), hivi sasa Serikali inaendelea na mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa yenye upana wa mita 1.435 (Standard Gauge Railway - SGR). Awamu ya kwanza ya mradi huo ni ya ujenzi wa Reli ya kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza (km. 1,219), ambayo imegawanyika katika vipande vitano (5). Kipande cha kwanza ni cha Dar es Salaam – Morogoro (km. 300); Kipande cha pili ni Morogoro – Makutopora (km. 422), kipande cha tatu ni Makutopora – Tabora (km. 376.5), kipande cha nne ni Tabora – Isaka (km. 162.5), na kipande cha tano ni Isaka – Mwanza (km. 341). Reli hii imesanifiwa kuwa na mwendokasi wa kilomita 160 kwa saa kwa treni ya abiria na kilomita 120 kwa saa kwa treni ya mizigo. Lengo la mradi huu ni kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo ya ndani na nje ya nchi kwa wingi na kwa muda mfupi ili kukuza uchumi wa nchi kwa kuziunganisha bandari zetu na nchi jirani ambazo hazipakani na bahari (land locked countries).

Ujenzi wa vipande vya Dar es Salaam – Morogoro (km 300), Morogoro – Makutopora (km 422) na Mwanza – Isaka (km 422), unaendelea. Hadi Septemba, 2021, Ujenzi wa reli kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro umekamilika kwa asilimia 93.73 na kazi ya majaribio ya uendeshaji wa treni inatarajia kuanza mwishoni mwa Disemba, 2021, Ujenzi wa reli kipande cha Morogoro hadi Makutupora (km 422), umekamilika kwa asilimia 72.43 na kwa mujibu wa mkataba kazi ya ujenzi kwa kipande hicho inatarajiwa kukamilika Februari, 2022, na ujenzi wa reli kipande cha Mwanza – Isaka umekamilika kwa asilimia 3.33 na kwa mujibu wa mkataba kazi ya ujenzi huo inatarajiwa kukamilika Aprili, 2024.

Ndugu Wanahabari, treni ya awamu ya kwanza inayoanzia Dar es Salaam hadi Morogoro itaanza kutoa huduma rasmi baada ya ujenzi wa reli na majaribio ya matumizi yake kukamilika. Ili kuwezesha kutoa huduma za usafiri huo, Mkataba wa ununuzi wa Vichwa viwili (2) vya Treni za umeme pamoja na Mabehewa 30 umesainiwa na vifaa hivyo vitawasili nchini Novemba, 2021 na majaribio ya kwanza ya Reli ya SGR yamepangwa kufanyika Disemba, 2021. Mkataba kwa ajili ya ununuzi wa vichwa vya treni za umeme 17, seti 10 za treni za umeme za abiria (EMU) umesainiwa tarehe 14 Julai, 2021 na vinatarajiwa kuwasili baada ya miezi 34, na Mkataba kwa ajili ya ununuzi wa mabehewa 59 ya abiria ulisainiwa tarehe 23 Septemba, 2020. Malipo ya awali yameshafanyika na hadi Juni, 2021 kazi ya matengenezo imefikia asilimia 45. Mkataba huu ni wa miaka miwili utakamilika tarehe 22 Septemba, 2022. Taratibu za ununuzi wa mabehewa 1,430 ya mizigo zinaendelea.

Ndugu Wanahabari, Serikali kupitia TRC ipo kwenye maandalizi ya kuanza Ujenzi wa reli ya SGR awamu ya pili kwa kipande cha Tabora - Kigoma (Km 411); Kaliua-Mpanda-Karema (Km 321), Keza - Ruvubu (km 36); Isaka - Rusumo (km 371), na Uvinza-Musongati (Km 240). Upembuzi yakinifu na Usanifu wa awali wa vipande hivi umekamilika na hatua inayoendelea ni kuandaa makabrasha ya zabuni.

Ndugu Wanahabari, Serikali inatambua umuhimu wa usafiri wa anga katika kuchangia ukuaji wa sekta nyingine hususan utalii wa aina zote; kilimo cha mboga mboga, matunda, nyama na samaki na kuinua uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi. Tanzania ina Kampuni ya Ndege inayojulikana kama Kampuni ya Ndege Tanzania (Air Tanzania Company Limited - ATCL). Uwepo wa Kampuni hii nchini ambayo pia ndiyo inatumika kuitangaza Tanzania (Flag Ship Company), umeendelea kuimarishwa ili kuifanya Tanzania kuwa kiungo (Hub) cha usafiri wa anga katika Afrika Mashariki na Kati.

Ndugu Wanahabari, Baada ya Tanzania kupata uhuru, kulikuwa na Shirika moja la ndege katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hadi Machi 10, 1977 lilipoanzishwa Shirika la Ndege Tanzania (ATC), baada ya kuvunjika kwa lililokuwa Shirika la Ndege la Afrika Mashariki. Shirika la Ndege Tanzania lilianza kutoa huduma za usafiri wa anga kwa kutumia ndege tatu, moja aina ya DC-9 na mbili aina ya Foker Friendships F27.

Baadaye Serikali ilinunua ndege nyingine aina ya Boeing B737-200 Combi (mbili), Foker Friendships (mbili), na Twin Otters (nne). Kutokana na kudorora kwa uendeshaji wa Shirika hilo ikiwa ni pamoja na kuiingizia Serikali hasara, mwaka 2002, Shirika hilo lilibinafsishwa na kuundwa Kampuni ya Ndege Tanzania (Air Tanzania Company Ltd (ATCL). Hadi kufikia mwaka 2002, ATC ilikuwa na ndege moja aina ya B737-200 na nyingine ya kukodi ya B737-300.

Ndugu Wanahabari, nia ya Serikali kubinafsisha Shirika la Ndege ilikuwa ni kulifanya shirika hilo kuwa imara na kutoa huduma bora za ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, baada ubinafsishaji na uundwaji mpya wa Kampuni ya Ndege Tanzania bado kampuni hiyo ilishindwa kukua na kujiendesha kwa hasara. Hali hii ilileta mzigo wa madeni kwa ATCL na Serikali iliamua kuvunja ubia kati ATCL na Shirika la Ndege la Afrika Kusini (South Africa Airways – SAA) mwaka 2006, kwa kununua hisa asilimia 49 zilizokuwa zinamilikiwa na SAA. Wakati ubia huu unavunjika, ATCL ilikuwa na ndege moja tu aina Dash Q 300.

Ndugu Wanahabari, kutokana na umuhimu wa Kampuni

ya Ndege, mwaka 2016, Serikali iliamua kufufua ATCL kwa kununua ndege mpya na kuboresha menejimenti na muundo wa Kampuni hiyo. Hadi kipindi hiki tunachoadhimisha miaka 60 tangu kupata uhuru, ATCL ina jumla ya ndege 12 za kisasa zinazotoa huduma ndani na nje ya nchi.

Ndege hizo ni aina ya Bombardier Dash 8 Q 400 tano (5), Air bus A220-300 nne (4), Boeing 787-8 Dreamliner mbili (2), na Dash 8 Q300 moja (1). Aidha, Agosti, 2021, Serikali imesaini na kulipa malipo ya awali ya ununuzi wa wa ndege mpya tano (5) aina ya Boeing 787-8 moja (1) Boeing 737-9 Max mbili (2), Ndege ya Mizigo (Freighter) Boeing 767-300 moja (1), na Bombardier Dash 8 Q400 moja (1). Kuwasili kwa ndege hizo kutaifanya ATCL kuwa na ndege 17 hadi kufika mwaka 2023, ambazo zitaimairisha mtandao wake wa safari za ndege kwa soko la ndani, kikanda na kimataifa.

Ndugu Wanahabari, licha ya kuwepo kwa janga la UVIKO – 19, ATCL imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga ndani ya nchi katika vituo kumi na tatu (13), ambavyo ni Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mpanda, Mwanza, Songea, Tabora na Zanzibar. Kwa vituo vya kikanda, ATCL imeendelea kutoa huduma katika vituo vitano (5) vya Entebbe, Uganda; Hahaya, Comoro, Harare, Zimbabwe, Lusaka, Zambia, na Mumbai, India.

Aidha, ATCL ilisimamisha kwa muda utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria katika kituo cha Bujumbura, Burundi na Guangzhou, China kutokana na athari za mlipuko wa UVIKO -19 na pia katika kituo cha Johannesburg, Afrika ya Kusini kutokana na masuala ya kisheria. Hata hivyo, Huduma za usafirishaji wa mizigo kwa kituo cha Guangzhou, China zinaendelea kutolewa hadi sasa.

Ndugu Wanahabari, baada ya Tanzania Bara kupata uhuru wake mwaka 1961, huduma za usalama wa usafiri wa anga zilikuwa chini ya Kurugenzi ya Usafiri wa Anga ya Afrika Mashariki yenye makao makuu nchini Kenya ambapo nchi za Tanzania, Kenya na Uganda zilikuwa na Ofisi ndogo. Majukumu ya Kurugenzi hii yalikuwa kutoa huduma za uongozaji ndege, huduma za mawasiliano, utoaji leseni, usajili wa ndege, utafutaji na uokoaji wa ndege zinazopotea na kupata ajali, utoaji leseni kwa mashirikia ya ndege, uchunguzi wa ajali za ndege na utoaji wa taarifa za anga. Baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, Tanzania ilianzisha Kurugenzi ya Usafiri wa Anga Tanzania ambayo ilipewa majukumu yote ambayo Kurugenzi ya Usafiri wa Anga Afrika Mashariki ilikuwa ikiyafanya na kuwekwa chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Ndugu Wanahabari, kutokana na mageuzi ya ki-mfumo na ki-uendeshaji, Kurugenzi hiyo ilibadilika na kuwa Wakala wa Serikali mwaka 1997 na hatimaye Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), mwaka 2003. Lengo la mabadiliko hayo likiwa ni kuipa madaraka ya kufanya maamuzi ya shughuli za udhibiti na ki-uchumi kwa haraka na ufanisi. Katika kuhakikisha kwamba usalama katika anga la Tanzania unakuwa mkubwa na wa kutosha, mwaka 1998 Serikali ilinunua Rada ya kuongozea ndege za kiraia ambayo ilifungwa katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA).

Ndugu Wanahabari, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania imeendelea kuimarisha usalama wa usafiri wa anga ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za uongozaji ndege zilizo salama kwa ndege zinazopita katika anga la Tanzania na ndege zinazotumia viwanja vya ndege nchini.

Aidha, ili kuendelea kuongeza imani kwa mashirika ya ndege ya kimataifa kutumia anga la Tanzania katika safari za ndege zao, mwaka 2019, Serikali kupitia TCAA ilinunua mitambo minne (4), ya rada zenye teknolojia ya kisasa za kuongozea ndege za kiraia. Rada hizo zimefungwa katika mikoa ya Dar es salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Mbeya. Hivi sasa ndege yoyote ya kiraia inayopita katika anga lote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaoneka kupitia Rada hizo. Kufungwa kwa rada hizi mpya kulisababisha rada iliyokuwepo awali kusitishwa kutoa huduma. Pamoja na uwepo wa Rada hizo, Serikali imeendelea na mipango yake ya kuimarisha mawasiliano ya huduma za uongozi ndege kwa kuendelea kubadilisha mifumo ya zamani na kuweka mifumo mipya ya mawasiliano yenye teknolojia ya kisasa ili anga la Tanzania liendelee kuwa salama na la kuvutia uwekezaji.

Ndugu Wanahabari, baada ya kupata uhuru mwaka 1961 hadi 1967, huduma za hali ya hewa nchini zilikuwa zinatolewa na Idara ya Hali ya Hewa ya Afrika Mashariki iliyokuwa na Ofisi zake Kabete, Kenya. Mwaka 1977, baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, huduma za hali ya hewa nchini zilihamishwa na kuwa chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kama Idara Kuu ya Hali ya Hewa (Directorate of Meteorology - DoM). Aidha, wakati tunapata uhuru, tulikuwa tunamiliki vituo viwili vya rada za hali ya hewa zilizokuwa Dar es Salaam na KIA, lakini kutokana na mabadiliko ya Teknolojia, Rada hizo zilipitwa na wakati na hivyo hazitumiki tena. Wakati huu ambao tunaadhimisha miaka 60 ya Uhuru, Tanzania tunazo Rada za kisasa za hali hewa zipatazo tatu (3) zilizofungwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Mtwara.

Hadi sasa wastani wa asilimia 85 ya malipo yamefanyika kwa ajili ya ununuzi wa rada nne (4), zitakazofungwa katika Mikoa ya Kigoma, Mbeya, Dodoma na Kilimanjaro. Kazi ya utengenezaji wa rada hizo inaendelea na itakamilika Machi, 2022. Ujenzi wa miundombinu ya majengo na njia ya umeme kwa vituo vya rada hizo unaendelea. Kufungwa kwa rada hizo kutaiwezesha Tanzania kuwa na Rada saba (7), za hali ya hewa na hivyo kukidhi matakwa ya Shirika la kimataifa la Hali ya Hewa (World Meteorological Organization - WMO).

Ndugu Wanahabari, katika kipindi cha miaka 60 iliyopita, huduma za usafiri katika maziwa Makuu ya Tanganyika, Victoria na Nyasa zimeendelea kutolewa na Kitengo cha Usafiri Majini kilichokuwa chini ya lilikuwa Shirika la Reli Tanzania (TRC) na baadaye kuanzia mwaka 1999 ziliendelea kutolewa na Kampuni ya Huduma za Meli (Marine

Service Company Limited - MSCL). Kampuni hii imeendelea kuwa kiungo muhimu kwa kufanya biashara na Nchi zinazotegemea huduma za meli kupitia maziwa hayo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kama Uganda, Kenya, Sudan Kusini, Rwanda, Burundi, DR-Congo, Zambia na Malawi.

Ndugu Wanahabari, mara tu baada ya Uhuru, Serikali iliendelea kutoa huduma ya usafiri wa majini katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kwa kutumia meli tatu (3) za M.V. Victoria na M.V. Clarias katika Ziwa Victoria; na M.V. Liemba katika Ziwa Tanganyika. Aidha, Serikali ilinunua meli mpya saba (7), zilizotumika kama ifuatavyo: M.V. Butiama, M.T. Ukerewe na M.V. Serengeti katika Ziwa Victoria; M.T. Sangara na M.V. Mwongozo katika Ziwa Tanganyika; na M.V. Songea na M.V. Iringa katika Ziwa Nyasa.

Meli hizo pamoja na meli nyingine zilizokuwepo kabla ya uhuru zimekuwa zikisafirisha abiria na mizigo katika maziwa hayo matatu na hivyo kusaidia kukuza biashara na kuboresha maisha ya jamii. Hadi mwaka 2015, Kampuni hii ilikuwa inamiliki meli 14 ambazo kati ya hizo Meli 9 zipo katika Ziwa Victoria, Meli 3 na Boti 1 katika Ziwa Tanganyika na Meli 2 katika Ziwa Nyasa. Meli nyingi kati ya hizi zimekuwepo tangu Uhuru wa nchi hii na hivyo zimechakaa na nyingine kusimamishwa kutoa huduma kutokana na usalama wake kwa maisha ya watu na mali zao. Hadi Januari, 2017, MSCL ilikuwa na meli tatu (3) za MV.Umoja, MV Liemba na MV Songea zilizokuwa zinatoa huduma.

Ndugu Wanahabari, kutokana na kudorora kwa Kampuni hii katika utoaji wa huduma pamoja na umuhimu wake kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya maziwa makuu na uchumi wa nchi kwa ujumla, Serikali iliamua kufufua huduma za usafiri kwa njia ya maji kwa abiria na mizigo katika maziwa hayo. Hivyo, mwaka 2018, Serikali ilianza kutenga fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi mikubwa minne katika Ziwa Victoria, kama awamu ya kwanza ya mpango wa kufufua huduma za usafiri katika maziwa makuu kupitia MSCL. Awamu hii ilihusisha ujenzi wa Meli mpya ya MV Mwanza "Hapa Kazi Tu", yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria, Mkataba wa ujenzi ulisainiwa Septemba, 2018 na unatarajiwa kukamilika Novemba, 2022. Ujenzi wa meli hii umekamilika kwa asilimia 81.

Mradi wa pili ni ujenzi wa Chelezo ambayo inatumika kama kitanda cha meli kabla haijashushwa katika maji wakati ikiundwa. Ujenzi wa chelezo hii katika Ziwa Victoria ulikamilika Machi, 2020 na upo kwenye kipindi cha uangalizi. Miradi mingine ilikuwa ni ukarabati wa Meli za MV Victoria na MV Butiama ambao umekamilika Aprili, 2020 na Meli hizo zinaendelea kutoa huduma katika Ziwa Victoria.

Ndugu Wanahabari, Awamu ya pili ya uboreshaji wa huduma za usafiri kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa inahusika miradi sita (6). Miradi hiyo ni:

i.Ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mabehewa ya mizigo katika Ziwa Victoria. Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 15 Juni, 2021 na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2023. Kwa sasa mkandarasi anaendelea na maandalizi (mobilization).

ii. Ukarabati mkubwa wa meli MV. Umoja inayobeba mabehewa katika Ziwa Victoria. Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 15 Juni, 2021 na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2023. Kwa sasa mkandarasi anaendelea na maandalizi (mobilization)

.

iii. Ukarabati wa meli ya kubeba shehena ya mafuta ya MT. Sangara katika Ziwa Tanganyika. Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 15 Juni, 2021 na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2022. Mkandarasi anaendelea na maandalizi (mobilization), tayari kwa ajili ya kuanza utekelezaji utakaofanyika katika Chelezo kilichopo bandari ya Kigoma.

iv. Ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Tanganyika. Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 15 Juni, 2021 na unatarajiwa kukamilika Machi, 2024. Kwa sasa, Mkandarasi anaendelea na maandalizi (mobilization), tayari kwa ajili ya kuanza utekelezaji utakaofanyika katika eneo la Chuo cha Uvuvi (FETA), Kibirizi, Mkoani Kigoma.

v. Ujenzi wa meli mpya ya kubeba shehena ya mizigo kiasi cha tani 2,800 katika Ziwa Tanganyika. Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 15 Juni, 2021 na unatarajiwa kukamilika Machi, 2024. Kwa sasa mkandarasi anaendelea na maandalizi (mobilization), tayari kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake utakaofanyika katika eneo la Chuo cha Uvuvi (FETA), Kibirizi Mkioani Kigoma.

vi. Ujenzi wa meli mpya ya kubeba shehena ya mizigo kiasi cha tani 2,700 katika Bahari Hindi. Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 15 Juni, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2024.

Serikali inaendelea na taratibu za kuanza Mradi wa Ukarabati mkubwa wa meli ya kubeba shehena ya mizigo (mafuta) ya MT. Nyangumi iliyopo Ziwa Victoria na Ukarabati wa meli ya uokozi na kuvuta matishari ya MT. Ukerewe.

Ndugu Wanahabari, bandari ni kiungo muhimu katika uchukuzi kati ya nchi kavu na majini na zaidi ya asilimia 85 ya biashara yote duniani inasafirishwa kupitia huduma za bandari. Tanzania ina ukanda wa bahari wenye urefu wa kilomita 960 na bandari kuu tatu ambazo ni Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Pia ina maziwa makuu matatu ambayo yana bandari kuu za Mwanza, Bukoba, Musoma na Kemondo katika Ziwa Victoria; Kigoma na Kasanga katika Ziwa Tanganyika; na Itungi na Mbambabay katika Ziwa Nyasa. Bandari zote hizo zinasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Aidha, bandari za Tanzania ni tegemeo katika kuhudumia shehena ya Tanzania na nchi za jirani za Burundi, Rwanda, Congo na Uganda ambazo zinatumia reli ya kati (TRC); na

Zambia, DR Congo na Malawi zinazotumia reli ya TAZARA. Usafiri wa barabara pia hutumika katika kusafirisha bidhaa za nchi hizi kutoka na kuingia bandarini.

Ndugu Wanahabari, wakati Tanzania Bara, inapata uhuru wake mwaka 1961, nchi tatu za Afrika Mashariki zilikuwa kwenye mkataba wa ushirikiano katika kumiliki vyombo vikuu vya usafirishaji njia ya reli, huduma ya barabara, huduma za meli na bandari, huduma za anga, na karakana kuu zilizokuwa katika miji ya Dar es Salaam na Nairobi. Kufuatia mvutano kati ya Tanzania na Kenya, uliosababisha kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, mali na madeni ya Jumuiya viligawanywa baina ya nchi hizo tatu na kila nchi ilikuwa huru na yenye mamlaka ya kuhifadhi mali zake. Hivyo, tarehe 11 Februari, 1977, Tanzania ilianzisha Mamlaka ya Bandari Tanzania (Tanzania Harbours Authority).

Ndugu Wanahabari, wakati wa mgawanyo wa bandari za Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, Tanzania ilikabidhiwa Bandari mbili (2) za Dar es Salaam na Tanga kwa ajili ya kuziendesha. Kutokana na mabadiliko mbalimbali ya kimuundo, kisheria na kiutendaji, hivi sasa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), inasimamia jumla ya Bandari rasmi 89 zinazotambuliwa na Sheria ya Bandari Sura ya 166 kama ifuatavyo:-

(a) Bandari 12 ziko katika mwambao wa Bahari ya Hindi ambazo ni Bandari ya Dar es Salaam ambayo ni lango kuu (1), bandari kuu mbili (2) za Tanga na Mtwara, bandari tano (5) ndogo za Kilwa, Lindi, Mafia, Pangani, Bagamoyo na Bandari ndogondogo nne (4);

(b) Bandari 24 zipo katika Ziwa Victoria ikiwa ni pamoja na Bandari kuu sita (6) za Mwanza Kusini, Mwanza Kaskazini, Bukoba, Kemondo Bay, Nansio na Musoma pamoja na Bandari nyingine ndogondogo 18
.
(c) Bandari 19 zipo katika Ziwa Tanganyika ikiwa ni pamoja na Bandari mbili (2) kuu za Kigoma na Kasanga pamoja na Bandari nyingine ndogondogo 17.
(d) Bandari 11 zipo katika katika Ziwa Nyasa ikiwa ni pamoja na Bandari kuu mbili (2) za Itungi na MbambaBay pamoja na Bandari nyingine ndogondogo tisa (9).

Aidha, zipo Bandari nyingine 23 zinazohudumiwa na TPA lakini hazijaainishwa kwenye Sheria Namba 17 ya Mwaka 2004 (The Ports Act No. 17). Kati ya bandari hizo, Bandari sita (6) zipo katika mwambao wa Bahari ya Hindi, Bandari saba (7) katika Ziwa Victoria, Bandari sita (6) katika ziwa Tanganyika na Bandari nne (4) za Ziwa Nyasa. Taratibu za kutambua Bandari hizi kisheria zinaendelea.

Hata hivyo, TPA imeendelea kutambua na kurasimisha bandari zisizo rasmi ambapo hadi Juni 2021, jumla ya Bandari 693 zisizohudumiwa na TPA zilikuwa zimetambuliwa. Kati ya hizo, Bandari 239 ziko katika mwambao wa bahari ya Hindi, Bandari 329 katika Ziwa Victoria, Bandari 108 katika Ziwa Tanganyika na Bandari 17 katika Ziwa Nyasa. Taratibu za kuidhinisha Bandari hizo kwa mujibu wa sheria zinaendelea kutekelezwa.

Ndugu Wanahabari, kumekuwa na ongezeko la Shehena kupitia bandari za Mamlaka tangu wakati wa Uhuru mwaka 1961 hadi mwaka 2021. Shehena imeongezeka toka tani Milioni moja laki moja na elfu themanini na tano (1,185,000) mwaka 1961 hadi kufikia tani Million kumi na saba laki saba na kumi na sita elfu mia nne na ishirini na tisa ( 17,716,429) zilizohudimiwa katika mwaka 2020/2021. Bandari ya Dar es salaam ndiyo kubwa kuliko bandari zote zilizo Tanzania. Katika mwaka 1961, lango la bandari hii lilikuwa na uwezo wa kuingiza meli zenye urefu wa mita 145 – 175 na kulikuwa na kina cha maji cha mita 7. Mwaka 1998 ilichimbwa kufikia kina cha mita 10.5 na upana wa mita 140 ili kuruhusu meli kuingia saa 24. Hivi sasa bandari hii ina kina cha mita 14.5 na lango linaruhusu meli zenye ukubwa usiozidi mita 234.

Ndugu Wanahabari, katika mwaka 1961, Bandari ya Tanga ilikuwa na kina kifupi kilichosababisha meli kufunga nje ya bandari (outer anchorage), na hivyo mizigo kupakiwa na kupakuliwa kwa kutumia pantoni. Hivi sasa kazi ya uboreshaji wa Bandari ya Tanga awamu ya pili unaendelea ili kuongeza kina cha gati za Bandari hiyo na hivyo kuondokana na gharama kubwa za kuhudumia meli nangani.

Bandari ya Mtwara ilianza mwaka 1954, ambapo gati mbili zilijengwa pamoja na reli ya Nachingwea. Reli ya Nachingwea iliondolewa mwaka 1963 na hivyo kuathiri shughuli za bandari. Kutokana na uchakavu wa bandari hii, Serikali inaendelea kuboresha bandari hii kwa kujenga gati nne za kisasa ambapo ujenzi wa gati moja (multipurpose terminal) lenye urefu wa mita 300 katika Bandari ya Mtwara ulioanza Machi, 2017 ulikamilika Oktoba, 2020.

Ndugu Wanahabari, wakati tunapata uhuru, katika Ziwa Victoria kulikuwa kuna Bandari za Mwanza, Bukoba, Nansio na Musoma; Ziwa Tanganyika ilikuwa Bandari ya Kigoma; na Ziwa Nyasa ilikuwa ni Bandari ya Kyela. Kutokana na mahitaji ya kuboresha miundombinu ya bandari iliyopo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bandari mpya ili kuhimili ongezeko la shehena, hivi sasa kuna ongezeko kubwa la bandari katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Hadi Juni, 2021, magati mapya yaliyojengwa katika Ziwa Victoria ni pamoja gati la Lushamba; gati la Ntama; gati la majahazi Mwigobero; gati la Nyamirembe; gati la Magarini; na ukarabati wa Bandari ya Mwanza, Kemondo na Bukoba. Katika Ziwa Tanganyika ni pamoja na gati la Kagunga; gati la Kalya (Sibwesa), na gati la Kabwe (Nkasi). Katika Ziwa Nyasa ni pamoja na bandari ya Kiwira.

**HITIMISHO:**
Taarifa hii inaonesha kwa ufupi historia ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi yenye hatua mbalimbali za ukuaji wa sekta kwa mantiki ya Miundombinu na huduma za Ujenzi na Uchukuzi kwa kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Takwimu zilizopo hapo juu zimeonesha tulikotoka tangu Uhuru wa Tanzania Bara Desemba, 1961 na tulipo sasa na tuendako katika maendeleo ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.
Hatuna budi kujivunia historia yetu ya maendeleo chanya

yaliyofanywa na Serikali za awamu ya kwanza chini ya Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere hadi awamu hii ya sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA NA KAZI IENDELEE……



MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA NA MAFANIKIO
KATIKA SEKTA ZA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**UTANGULIZI**

Ndugu Wanahabari, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ni miongoni mwa Wizara zenye sekta kongwe na za mwanzo kuundwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza tangu kupatikana kwa Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 chini ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, licha ya kuwa sekta hizo zimekuwa zikiwekwa katika Wizara mbalimbali.

Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliwahi kusema "Utamaduni ni kiini ama roho ya taifa lolote, taifa lisilo na utamaduni ni sawa na mkusanyiko wa watu usio na roho"

Wizara hii tangu ilipopata Uhuru mwaka 1961 imekuwa kinara wa kusimamia na kuhakikisha Taifa linaendelea kuenzi Utamaduni imara wa Mtanzania, kuwa na kazi bora za Sanaa na taifa lenye umahiri mkubwa katika michezo.

Mwaka 1962 Serikali ya kwanza iliunda Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana hatua inayodhihirisha kuwa ni sekta nyeti na muhimu katika kusimamia masuala ya utamaduni wa nchi.

Ninatumia nafasi hii kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuona umuhimu wa sekta hizo kwenye Serikali yake ya Awamu ya Sita na kuzipatia kipaumbele. Ni ukweli usiopingika kuwa tumeshuhudia mafanikio makubwa sana katika kipindi hiki kifupi.

Mathalani miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na eneo la soka la wanawake ambako kumekuwa na makombe mengi ya kimataifa kuliko wakati wowote; kufufua mashindano ya michezo ya shule za msingi (UMITASHUMTA) na sekondari (UMISSETA) ambayo yanazalisha vipaji vya wanamichezo; na kuanzisha tamasha kubwa la michezo kwa wanawake la Tanzanite lililotoa hamasa kubwa kwa wanawake kufanya vizuri kwenye michezo.

Ushindi wa kihistoria wa mashindano ya Miss and Mr Deaf Afrika ni jambo jingine kubwa; na Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo lililotumika vema kutangaza utalii wa nchi yetu.

**1.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA SEKTA YA UTAMADUNI NCHINI TANGU TULIPOPATA UHURU MWAKA 1961**

Ndugu Wanahabari, Tangu kupatikana kwa Uhuru wa Tanganyika kwa sasa Tanzania Bara, kumeshuhudia mafanikio mbalimbali katika Sekta ya Utamaduni nchini kama ifutavyo:-

a. Kuundwa kwa Wizara yenye dhamana ya Utamaduni ambapo tarehe 10 Desemba, 1962 Serikali iliunda Wizara hii kwa minajili ya kuondoa kasumba na fikra za kikoloni na kuwajengea wananchi hususan vijana moyo wa kujiamini na kupenda vitu vya asili yao na kubadilisha mitazamo yao;

b. Kukua kwa fani mbalimbali za Utamaduni zikiwemo Sanaa, Malikale, Makumbusho na Nyaraka. Kukua kwa fani hizi za Utamaduni kumesababisha fani hizi kuwa Sekta kamili zinazojitegemea kutokana na maendeleo yake nchini;

c. Kuanzishwa kwa Sera ya Taifa ya Utamaduni mwaka 1997. Sera hii imeendelea kutoa mwelekeo na dira ya utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Utamaduni nchini;

d. Kutungwa kwa Sheria, Kanuni za Taasisi na Asasi mbalimbali za kusimamia maendeleo ya Sekta ya Utamaduni ili kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni katika maeneo mahsusi. Hii ni pamoja na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) 1967, Bodi ya Filamu Tanzania (BFT) 1976, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) 1984 na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), 2007;

e. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Utamaduni nchini Mwaka 1998 ambao kutokana na kukua kwa Sekta ya Sanaa nchini, Mfuko huu umehuishwa na kuitwa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa. Lengo ni kuwajengea uwezo Wasanii na Wadau wa Utamaduni na Sanaa kuwa na ujuzi wa kuandaa kazi bora zinazohimili ushindani wa masoko, pamoja na kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wadau wa Sekta hizi;

f. Kukua kwa matumizi ya Lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi. Mwaka 2006 Kiswahili kilipitishwa rasmi kuwa lugha rasmi ya Umoja wa Afrika; mwaka 2019 Kiswahili pia imekuwa lugha rasmi katika Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Vilevile zaidi ya redio na idhaa 100 zinatumia Kiswahili kurusha matangazo yake katika Mataifa mbalimbali duniani;

g. Lugha yetu aushi na adhimu ya Taifa Kiswahili, chini ya Serikali imeendelea kuimarika na kutumika hatua inayoifanya kuwa lugha ya 10 kutumiwa na watu wengi duniani;

h. Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Mwaka 2005 Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliridhia Itifaki ya kuanzishwa kwa Kamisheni hii kwa lengo la kuratibu na kusimamia maendeleo na matumizi ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya jumuiya;

i. Kuanzishwa kwa vyama mbalimbali vya ukuzaji na uendelezaji wa lugha adhimu na aushi ya kiswahili nchini ikiwamo Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania – UKUTA; Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania - CHALUFAKITA; Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki – CHAKAMA; Chama cha Ukuzaji Kiswahili Duniani – CHAUKIDU; Chama cha Washairi Tanzania – CHAWASHATA; pamoja na Taasisi kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili – TATAKI;

j. Kuanzishwa kwa Vyuo Vikuu vinavyofundisha lugha ya kiswahili katika ngazi ya shahada za awali, umahiri na uzamivu. Wataalam wameendelea kutumika katika

kufundisha kiswahili ndani na nje ya nchi kama hatua ya ubidhaishaji wa lugha ya kiswahili kimataifa;

k. Kuridhiwa kwa Mikataba ya Kimataifa ya utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Utamaduni nchini mathalan Mikataba ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Mwaka 2011 Nchi iliridhia Mkataba wa UNESCO wa mwaka 2003 kuhusu Kulindwa kwa Urithi wa Utamaduni usioshikika, na Mkataba wa mwaka 2005 kuhusu Kukuza na Kulinda Uanuwai wa Kujieleza Kiutamaduni. Lengo la kuridhiwa kwa mikataba hii ni kushirikiana na Mataifa na Mashirika ya Kimataifa katika kulinda na kuhifadhi amali za urithi wa utamaduni nchini;

l. Kuridhiwa kwa mikataba ya ushirikiano katika sekta ya utamaduni (Cultural cooperation) na mataifa mbalimbali. Nchi yetu imeridhia mikataba ya ushirikiano na nchi mbalimbali duniani ikiwemo Jamhuri ya Watu wa China, Kenya, Burundi, na India. Utekelezaji wa mikataba hii umeipa nchi yetu fursa ya kubadilishana uzoefu na nchi zingine katika kuboresha sekta ya utamaduni nchini pamoja na kupatikana kwa nafasi za masomo kwa wataalam wetu katika nchi hizo;

m. Kutambuliwa na kupewa hadhi kwa taaluma ya utamaduni na fani zake kwa kufundishwa katika ngazi za vyuo vikuu na vyuo vya kati. Kuzingatiwa katika utoaji wa ajira kwa wataalam wanaotekeleza majukumu ya sekta ya utamaduni nchini;

n. Ongezeko la matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika sekta ya utamaduni kwa ajili ya kutangaza kazi za utamaduni na ubunifu pamoja na kuhifadhiwa kwa taarifa, nyaraka na kumbukumbu za kiutamaduni kwa njia ya kidigiti;

o. Kufanyika kwa tafiti mbalimbali za utamaduni, kutoa matokeo na kuyasambaza kwa umma. Kuhifadhi na kutoa machapisho, kutenga na kutambua maeneo ya kimila na kihistoria nchini;

p. Kuanzishwa kwa Programu maalum ya kuenzi historia ya ukombozi wa nchi yetu. Mwaka 2011 Umoja wa Afrika uliridhia Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kutekelezwa nchini. Programu hii ina lengo la kutambua, kuhifadhi na kuendeleza urithi wa Ukombozi uliotokana na mapambano ya kufauta uhuru. Aidha, inalenga kuenzi watu walishiriki katika vita vya ukombozi kwa kujenga minara ya kumbukumbu na kuandika upya historia ya ukombozi wa nchi yetu na kurithisha kwa vizazi vya sasa na vijavyo; na

q. Kuanzishwa kwa vituo mbalimbali vya kiutamaduni (Cultural centers) nchini. Vituo hivi vimeendelea kutumika kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za utamaduni ikiwemo matamasha ya utamaduni ili kuwawezesha wananchi waendelee kujivunia na kusherehekea utamaduni wao pamoja na kuuza kazi za mikono za kiutamaduni (cultural handcrafts) kwa minajili ya kujipatia mapato.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA SEKTA YA SANAA NCHINI TANGU TULIPOPATA UHURU MWAKA 1961**

Ndugu Wanahabari, tangu kupatikana kwa Uhuru wa Tanganyika kwa sasa Tanzania Bara, kumeshuhudia mafanikio mbalimbali katika Sekta ya Sanaa nchini kama ifutavyo:-

a. Katika kipindi hiki kumeundwa Idara ya Maendeleo ya Sanaa baada ya muundo mpya wa Wizara ya mwaka 2016. Kabla ya hapo Idara ilikuwa ni sehemu ndani ya Idara ya Maendeleo ya Utamaduni. Idara ya Sanaa ndiyo yenye dhamana ya kusimamia maendeleo ya sekta ya sanaa nchini ambayo ni pamoja na filamu, muziki, michezo ya kuigiza, ngoma, dansi, sarakasi na kazi za mikono kama vile uchoraji, uchongaji, uhunzi, usukaji, ufumaji, ushonaji na ususi;

b. Pia kuanzishwa kwa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ambapo mwaka 1984 Serikali ilitunga Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa namba 23 ambayo ilianzisha Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Pamoja na majukumu mengine husajili wasanii, kutoa vibali vya shughuli za sanaa, kuwatetea wasajiliwa wake, kuwatafutia masoko ya kazi zao na kusimamia uanzishwaji wa mashirikisho ya sanaa nchini. Kuwepo kwa Baraza kumeifanya sekta ya sanaa kushamiri hadi kufikia sekta hiyo kuongoza katika ukuaji wa pato la taifa kwa mwaka 2018/2019 kwa asilimia 13.7;

c. Kutokana na usimamizi wa Baraza, muziki wa bongo fleva na singeli umezaliwa, sanaa za uchongaji za kisasa (modern carvings) zimezalishwa (mfano Ujamaa, Mawingu, Kimbulumbulu), na pia sanaa za michoro kama tingatinga ambazo ni ngeli zinazoitanagaza Tanzania kimataifa;

d. Pia katika kipindi hiki, kumeanzishwa Taasisi ya Bodi ya Filamu Tanzania (TFB) ambapo mwaka 1976 Serikali ilianzisha na kuitambua kama Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Tanzania. TFB ilianzishwa kwa Sheria Namba 4 ambayo husimamia masuala yote ya filamu na michezo ya kuigiza, kusajili wasanii na wadau katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza, na kutoa vibali vya kuendesha shughuli husika. Bodi ya Filamu imewezesha kuzaliwa ngeli ya Bongo Movies ambayo sasa ni maarufu Afrika na duniani kote;

e. Chini ya Bodi ya Filamu, Waziri mwenye dhamana na Sanaa nchini alianzisha Kamati ya Kutetea Haki za Wasanii ambapo familia za wasanii kama marehemu Stephen Kanumba na marehemu King Majuto wamenufaika;

f. Vilevile kuanzishwa kwa Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) mwaka 1999 kwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ambapo pamoja na mambo mengine huwalinda na kuwatetea wabunifu dhidi ya matendo ya uharamia na kusaidia kukusanya mirabaha itokanayo na matumizi ya kazi zao;

g. Kupitia COSOTA Tanzania huunganishwa na mataifa mengine katika ulinzi wa masuala ya hakimiliki na hakishiriki kupitia mikataba ya pamoja (bilateral agreements) baina ya mataifa. Mabadiliko katika sayansi na

teknolojia yamefanya ulinzi katika matumizi ya kazi za sanaa kuwa ngumu. Serikali imeendelea kuongeza adhabu katika makosa, kuanzisha mifumo ya kidijiti na kupanua mawanda ya wanufaika hasa kupitia Retail Rights na usimamizi wa mikataba ya wasanii;

h. Fanikio jingine kubwa kuwa ni uanzishwa kwa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ambayo ni Kituo kilichotukuka Afrika Mashariki (East Africa Center of Excellence) katika mafunzo ya Sanaa na Utamaduni. Historia ya chuo cha sanaa Bagamoyo ilianzia mnamo mwaka 1962 ambapo kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanganyika iliundwa Wizara ya Vijana na Utamaduni;

i. Baada ya kuonekana kuna uhitaji mkubwa wa kuwa na mafunzo rasmi ya mambo ya sanaa mwaka 1972, Serikali ilianzisha Chuo cha Sanaa Bagamoyo (BCA). Mwishoni mwa mwaka 2005 uamuzi ulifanywa na iliyokuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwamba, Chuo cha Sanaa Bagamoyo kibadilishwe kuwa wakala wa Serikali chini ya mpango wa mabadiliko ya sekta ya umma. Kutokana na hivyo Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ilianzishwa Novemba 2007 kwa tangazo Na. 220 lililochapishwa kwenye gazeti la Serikali kwa mujibu wa sheria ya Wakala wa Serikali namba 30 ya mwaka 1997;

j. Taasisi hii imefanikiwa kuelimisha wasanii muhimu hapa nchini ambao sio tu wanaendesha shughuli zao kwa ufanisi, bali pia kitaaluma katika eneo lao la sanaa. Mifano hai ya wasanii waliotokana na chuo hiki ni pamoja na Mrisho Mpoto na mwanazuoni Profesa Frowin Paul Nyoni;

k. Pia katika kipindi hiki, Wizara inajivunia kuanzishwa kwa mifumo ya kielektroniki ya kusajili wasanii, kutoa vibali na leseni, pamoja na kufuatilia kazi za wasanii kwenye vyombo vya habari na mitandaoni ambapo Baraza la Sanaa la Taifa – BASATA, Bodi ya Filamu Tanzania – BFT na Taasisi ya Hakimiliki Tanzania – COSOTA wamekamilisha mifumo ya kielektroniki. Mifumo hii itatoa huduma zifuatazo kutokea popote duniani;

i. Kusajili Wasanii na kazi zao;

ii. Kuruhusu maombi na upatikanaji wa vibali vya kuendesha shughuli za Sanaa;

iii. Kuomba leseni za matumizi ya kazi za Sanaa;

iv. Kubainisha kazi za Wasanii zinavyotumika katika maeneo mbalimbali ya jamii; na

v. Kuruhusu usambazaji wa matangazo na kazi za Sanaa kwa matumizi ya jamii.

l. Mifumo hii inarahisisha maisha hasa kwa vijana ambao ni wadau wakuu wa sanaa, burudani na utamaduni, kuwapunguzia kadhia ya kufuata huduma Dar es Salaam na hivyo kupunguza gharama za kujiajiri katika Sekta;

m. Kurasimisha maeneo ya kuoneshea kazi za sanaa nchini; ambapo kwa sasa takribani maeneo 4000 yamerasimishwa;

Ndugu Wanahabari, Tangu kupatikana kwa Uhuru wa Tanganyika kwa sasa Tanzania Bara, kumeshuhudia mafanikio mbalimbali katika Sekta ya Sanaa nchini kama ifutavyo:-

a. Katika kipindi hiki kumeundwa Idara ya Maendeleo ya Sanaa baada ya muundo mpya wa Wizara ya mwaka 2016. Kabla ya hapo Idara ilikuwa ni sehemu ndani ya Idara ya Maendeleo ya Utamaduni. Idara ya Sanaa ndiyo yenye dhamana ya kusimamia maendeleo ya sekta ya sanaa nchini ambayo ni pamoja na filamu, muziki, michezo ya kuigiza, ngoma, dansi, sarakasi na kazi za mikono kama vile uchoraji, uchongaji, uhunzi, usukaji, ufumaji, ushonaji na ususi;

b.Pia kuanzishwa kwa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ambapo mwaka 1984 Serikali ilitunga Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa namba 23 ambayo ilianzisha Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Pamoja na majukumu mengine husajili wasanii, kutoa vibali vya shughuli za sanaa, kuwatetea wasajiliwa wake, kuwatafutia masoko ya kazi zao na kusimamia uanzishwaji wa mashirikisho ya sanaa nchini. Kuwepo kwa Baraza kumeifanya sekta ya sanaa kushamiri hadi kufikia sekta hiyo kuongoza katika ukuaji wa pato la taifa kwa mwaka 2018/2019 kwa asilimia 13.7;

c. Kutokana na usimamizi wa Baraza, muziki wa bongo fleva na singeli umezaliwa, sanaa za uchongaji za kisasa (modern carvings) zimezalishwa (mfano Ujamaa, Mawingu, Kimbulumbulu), na pia sanaa za michoro kama tingatinga ambazo ni ngeli zinazoitanagaza Tanzania kimataifa;

d. Pia katika kipindi hiki, kumeanzishwa Taasisi ya Bodi ya Filamu Tanzania (TFB) ambapo mwaka 1976 Serikali ilianzisha na kuitambua kama Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Tanzania. TFB ilianzishwa kwa Sheria Namba 4 ambayo husimamia masuala yote ya filamu na michezo ya kuigiza, kusajili wasanii na wadau katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza, na kutoa vibali vya kuendesha shughuli husika. Bodi ya Filamu imewezesha kuzaliwa ngeli ya Bongo Movies ambayo sasa ni maarufu Afrika na duniani kote;

e. Chini ya Bodi ya Filamu, Waziri mwenye dhamana na Sanaa nchini alianzisha Kamati ya Kutetea Haki za Wasanii ambapo familia za wasanii kama marehemu Stephen Kanumba na marehemu King Majuto wamenufaika;

f. Vilevile kuanzishwa kwa Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) mwaka 1999 kwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ambapo pamoja na mambo mengine huwalinda na kuwatetea wabunifu dhidi ya matendo ya uharamia na kusaidia kukusanya mirabaha itokanayo na matumizi ya kazi zao;

g. Kupitia COSOTA Tanzania huunganishwa na mataifa mengine katika ulinzi wa masuala ya hakimiliki na

hakishiriki kupitia mikataba ya pamoja (bilateral agreements) baina ya mataifa. Mabadiliko katika sayansi na teknolojia yamefanya ulinzi katika matumizi ya kazi za sanaa kuwa ngumu. Serikali imeendelea kuongeza adhabu katika makosa, kuanzisha mifumo ya kidijiti na kupanua mawanda ya wanufaika hasa kupitia Retail Rights na usimamizi wa mikataba ya wasanii;

h. Fanikio jingine kubwa kuwa ni uanzishwa kwa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ambayo ni Kituo kilichotukuka Afrika Mashariki (East Africa Center of Excellence) katika mafunzo ya Sanaa na Utamaduni. Historia ya chuo cha sanaa Bagamoyo ilianzia mnamo mwaka 1962 ambapo kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanganyika iliundwa Wizara ya Vijana na Utamaduni;

i. Baada ya kuonekana kuna uhitaji mkubwa wa kuwa na mafunzo rasmi ya mambo ya sanaa mwaka 1972, Serikali ilianzisha Chuo cha Sanaa Bagamoyo (BCA). Mwishoni mwa mwaka 2005 uamuzi ulifanywa na iliyokuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwamba, Chuo cha Sanaa Bagamoyo kibadilishwe kuwa wakala wa Serikali chini ya mpango wa mabadiliko ya sekta ya umma. Kutokana na hivyo Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ilianzishwa Novemba 2007 kwa tangazo Na. 220 lililochapishwa kwenye gazeti la Serikali kwa mujibu wa sheria ya Wakala wa Serikali namba 30 ya mwaka 1997;

j. Taasisi hii imefanikiwa kuelimisha wasanii muhimu hapa nchini ambao sio tu wanaendesha shughuli zao kwa ufanisi, bali pia kitaaluma katika eneo lao la sanaa. Mifano hai ya wasanii waliotokana na chuo hiki ni pamoja na Mrisho Mpoto na mwanazuoni Profesa Frowin Paul Nyoni;

k. Pia katika kipindi hiki, Wizara inajivunia kuanzishwa kwa mifumo ya kielektroniki ya kusajili wasanii, kutoa vibali na leseni, pamoja na kufuatilia kazi za wasanii kwenye vyombo vya habari na mitandaoni ambapo Baraza la Sanaa la Taifa – BASATA, Bodi ya Filamu Tanzania – BFT na Taasisi ya Hakimiliki Tanzania – COSOTA wamekamilisha mifumo ya kielektroniki. Mifumo hii itatoa huduma zifuatazo kutokea popote duniani;

i. Kusajili Wasanii na kazi zao;
ii. Kuruhusu maombi na upatikanaji wa vibali vya kuendesha shughuli za Sanaa;
iii. Kuomba leseni za matumizi ya kazi za Sanaa;
iv. Kubainisha kazi za Wasanii zinavyotumika katika maeneo mbalimbali ya jamii; na
v. Kuruhusu usambazaji wa matangazo na kazi za Sanaa kwa matumizi ya jamii.

l. Mifumo hii inarahisisha maisha hasa kwa vijana ambao ni wadau wakuu wa sanaa, burudani na utamaduni, kuwapunguzia kadhia ya kufuata huduma Dar es Salaam na hivyo kupunguza gharama za kujiajiri katika Sekta;

m. Kurasimisha maeneo ya kuoneshea kazi za sanaa nchini; ambapo kwa sasa takribani maeneo 4000 yamerasimishwa;

n. Kuimarisha usajili wa kazi za ubunifu zikiwemo za maandishi, filamu na muziki. Zaidi ya Wasanii 1,668 na kazi 2,132 zilisajiliwa kufikia Desemba 2020; na

o. Ongezeko la ajira kupitia Sekta ya Sanaa nchini, ambapo kufikia Novemba 2017, zaidi watu million 5.5 walikuwa wameajiliwa kwenye kupitia sekta ya Sanaa.

## 3.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA SEKTA YA MICHEZO NCHINI TANGU TULIPOPATA UHURU MWAKA 1961

Ndugu Wanahabari, tangu kupatikana kwa Uhuru wa Tanganyika kwa sasa Tanzania Bara, kumeshuhudia mafanikio mbalimbali katika Sekta ya Michezo nchini kama ifutavyo:-

a. Kwa upande wa Sekta ya michezo Tanzania imefanikiwa kupata jumla ya Medali 16 katika michezo mikubwa kabisa duniani ambayo ni ya Olympic (2); Jumuiya ya Madola (7); na Michezo ya Bara la Afrika (7); na kwamba timu zetu zimeshiriki katika michezo hii mikubwa bila kukosa tangu tupate uhuru wetu;

b. Tanzania imefanikiwa kuwa na wachezaji wakulipwa katika nchi mbalimbali tangu uhuru. Kwa sasa ina jumla ya wachezaji 54 wakulipwa katika nchi mbalimbali ambapo (28) ni wachezaji wa mpira wa miguu, (16) mpira wa kikapu, (4) mpira wa wavu, (2) Kabbadi, (2) Netiboli (1) kuogelea na (1) mchezo wa Roliball;

c. Tanzania imeshinda vikombe mbalimbali katika mashindano ya kimataifa tangu kupata uhuru wake ambapo kwa upande wa mpira wa miguu kwa wanawake, Tanzania imechukua vikombe vitano (5) katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ikiwa ni pamoja na COSAFA, Afrika Mashariki, na CECAFA. Aidha, kwa upande wa mpira wa miguu kwa wanaume timu zetu zimefuzu kushiriki kwenye mashindano mbalimbali ambapo Taifa stars imefuzu mara 2 kushikiri fainali za kombe la Afrika (AFCON) 1980 na 2019, na zile fainali za mashindano ya wachezaji wa ndani CHAN mara mbili.

d. Timu ya Gofu wanawake ilichukua ushindi wa Bara la Afrika mwaka 2018. Timu zetu za Kricketi chini ya umri wa miaka 19 na timu ya wanawake zimeshiriki na kushika nafasi za tatu katika Bara la Afrika mwaka 2021.
e. Wanawake hawakuwa wanashiriki katika baadhi ya michezo kabla ya uhuru, lakini sasa kumekuwa na ongezeko kubwa kushiriki katika michezo mathalan mpira wa miguu ambapo sasa ligi ya mchezo huo imeanzishwa na timu za Taifa za mchezo huo zimeundwa.
f. Watalaam wa michezo wameongezeka kwa kuongeza udahili katika vyuo vinavyo fundisha fani ya michezo ikiwa ni pamoja na Chuo cha Maendeleo Malya na Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Malya kilidahili wanafunzi 40 mwaka 2013 hadi kufikia mwaka 2020 kinadahili wanafunzi 137.

Aidha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilidahili wanafunzi 14 mwaka 1997 hadi kufikia mwaka 2020 kilidahili wanafunzi 105.

g. Kwa upande wa mchezo wa nguni pia kumekuwa na mafanikio makubwa ambapo mabondia wetu wameshinda katika mapambano mbalimbali na kujinyakulia ubingwa wa Bara la Afrika na mabara mengine duniani. Baadhi ya mabondia hao ni pamoja na Hassan Mwakinyo ambaye ni bingwa wa uzito wa walterweight; Bruno Melchony aliyenyakua mkanda wa International Super Featherweight; Tony Rashid mkanda wa Super Bantaman; Abdalah Shaban Pazi mkanda wa Asia Pacific Superweight; na Salin Jengo world Supe featherweight.

h. Katika mchezo wa riadha, Tanzania ilifanikiwa kupata jumla ya medali 10 (Dhahabu 3, Fedha 4 na Shaba 3).

i. Aidha, ili kuimarisha mchezo wa ngumi; Kamisheni ya Ngumi ilianzishwa mwaka 2019 ambapo sasa maslahi na mikataba ya wanamasumbwi yanalindwa kikamilifu.

j. Kwenye michezo ya walemavu, Tanzania ilishiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa, mathalan mwaka 2015 ilishiriki katika mashindano ya Special Olympics yaliofanyika Los Angeles, Marekani na kupata mafanikio makubwa. Mwaka 2019 Tanzania imeshiriki mashindano ya special Olympic yaliyofanyika Abu-Dhabi na Tanzania kupata jumla ya medali 16 katika mashindano ya riadha (12 Dhahabu, 1 Fedha na 2 Shaba). Mwaka 2020 Tanzania imeshiriki Special Olympic iliofanyika Misri na Tanzania kupata medali 11 (Dhahabu 6, Fedha 3, na Shaba 2). Timu ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu kwa mara ya kwanza walishiriki mashindano ya Bara la Afika kwa michezo hiyo na kushika nafasi ya 4.

k. Kwa upande wa miundombinu ya Michezo, Tanzania imepiga hatua kubwa ambapo viwanja vya michezo mbalimbali vimeboreshwa na kujengwa na Serikali pamoja na wadau wa Michezo ikiwa ni pamoja na: Uwanja wa Benjamini Mkapa uliogharimu Shilingi Bilioni 56.4, Kituo cha Michezo cha JK Park, Majaliwa Stadium – Ruangwa, Azam Complex, Black Rhino – Karatu, Ngarenaro Complex, Kilimanjaro Golf Club, na Lugalo Golf Club kwa uchache.

l. Viwanja vya Uhuru, Nyamagana na Kaitaba kuwekewa nyasi bandia, kuboreshwa kwa uwanja wa Ndani wa Taifa pamoja na kuwekwa taa kwa viwanja vya Jamhuri Dodoma na Majaliwa Stadium.Katika mwaka wa fedha wa wa 2021 – 2022, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi Bilioni 10.5 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Michezo katika mikoa ya Dar es Salaam, Geita na Dodoma. (Sports Recreational and Leisure Centers)

m. Kuanzishwa na kuongezeka kwa vituo vya kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya vijana katika michezo (Sports Centers and Academy) ambapo mpaka sasa kuna vituo 136 vilivyo sajiliwa hapa nchini, Mfano kwa uchache ni pamoja na; Alliance Academy, Azam Soccer Academy, Fountain Gate Academy, Aidha kupitia mradi wa maenndeleo wa FIFA, TFF inaendelea na ukamilishaji wa vituo vikubwa viwili katika mikoa ya Tanga na Dar es Salaam - Kigamboni.

Katika mwaka wa fedha 2021 – 2022 Serikali imetenga kiasi cha Shilingi Bilioni 1.3 kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikubwa cha kisasa (Centre of Sports Excellency) katika Chuo cha Michezo Malya kwa lengo la ukuzaji na uendelezaji wa vipaji vya michezo mbalimbali. Pia, Serikali imeteua shule 56 ambapo katika kila mkoa kutakuwa na shule maalumu zisizopungua mbili kwa ajili ya kulea na kuendeleza vipaji vya michezo kwa wanafunzi.

n.Katika hatua nyingine ya kuhakikisha kuwa tunakuwa na wataalamu wa fani mbalimbali za michezo, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha tahasusi kwa ajili ya masomo ya michezo kwa wanafunzi wetu wa kidato cha tano na cha sita.

o. Seikali ipo katika hatua nzuri ya kuanzisha mafuko wa maendeleo ya michezo ambao utasaidia kutatua changamoto za sekta hii nchini.

Ndugu Wanahabari, mafanikio haya ya Wizara ni mwanzo mpya unaotokana na maono yenye tija na uongozi thabiti wa Wizara chini ya Jemedari Mkuu, Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo yamejengwa kwenye dhima ya Taifa ya kukuza Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa lengo la kuleta maendeleo ya jamii kiuchumi kwa kuongozwa na kaulimbiu ya Serikali ya Awamu ya Sita “Kazi Iendelee”.




**MAFANIKIO YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MUUNGANO NA MAZINGIRA**

**KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA**

Ndugu Wanahabari, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa na afya njema ili sote kwa pamoja tuweze kuwapasha wananchi taarifa muhimu.

Tunatambua mchango wenu katika kuelimisha na kuwapasha habari wananchi kuhusu mchango wa Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu masuala ya Muungano na Mazingira ambayo imepewa jukumu la kuyasimamia.

Ndugu Wanahabari,
Kama tunavyofahamu sasa hivi tuko katika kipindi cha maandalizi ya kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara itakapofika tarehe 9 Desemba, 2021. Sote tunafahamu kuwa katika kipindi hicho cha miaka 60 ya Uhuru, Utumishi wa Umma umeendelea kuwa uliotukuka katika kuchangia ustawi wa Taifa.

Kama tunavyofahamu tarehe 9 Desemba, 2021 tutaadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara ambao umekuwa na mafanikio makubwa kwa mustakabali wa Wananchi na Taifa letu kwa ujumla.

Ndugu Wanahabari, Itambulike kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais ilianzishwa baada ya Muungano wa Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 26 Aprili, 1964 ulioasisiwa na Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume. Baada ya Muungano, Hayati Nyerere alikuwa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Hayati Rashid Mfaume Kawawa alikuwa Makamu wa Pili wa Rais.

Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ni pamoja na kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yasiyo ya Muungano, Kuandaa na kusimamia Sera zinazohusu Mazingira.

Aidha, majukumu mengine ni Kukuza uzalishaji unaozingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Hifadhi ya Mazingira na uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Kuratibu na kusimamia shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Ndugu Wanahabari, katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru mafanikio mengi yamepatikana kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ambayo ni chachu katika ustawi wa Taifa letu. Serikali inahakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa yenye umoja, amani na usalama na Muungano wetu unaendelea kulindwa, kudumishwa, kuendelezwa na kuimarishwa.

**Muungano**

Tukianza na mafanikio katika Muungano, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zimefanikiwa kusimamia utekelezaji wa mambo ya Muungano kwa ufanisi mkubwa na hivyo kuimarika kwa utaifa na umoja, amani na utulivu na hali ya maisha ya wananchi kutokana na ukuaji wa uchumi wa pande zote mbili za Muungano.

Ndugu Wanahabari, mambo 22 ya Muungano, kama yalivyoainishwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yanatekelezwa na Wizara na Taasisi zenye dhamana ya kusimamia mambo hayo. Mambo hayo yanahusu Katiba, Bunge na Utawala Bora; Uchumi; Fedha na Biashara; Ulinzi na Usalama; Diplomasia na Ushirikiano wa Kimataifa; Usafiri na Usafirishaji; Utabiri wa Hali ya Hewa; na Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Katika kipindi cha miaka 60, Serikali zote mbili zimefanikiwa kusimamia utekelezaji wa mambo hayo kwa ufanisi mkubwa na mafanikio yanaonekana katika nayanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**Mafanikio ya kiuchumi**

Ndugu Wanahabari, yamefanyika mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kiutawala kwa lengo la kufufua uchumi, kuimarisha utendaji kazi serikalini na kukuza demokrasia na utawala bora. Utekelezaji wa programu mbalimbali za mageuzi ya kiuchumi na mipango yetu ya kupunguza umaskini na kukuza uchumi imezaa matunda tunayojivunia leo.

Mwaka 1996, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilianzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura Namba 399. Mamlaka hiyo ina Ofisi pande zote mbili za Muungano (Tanzania Bara na Zanzibar) hivyo kurahisisha ukusanyaji wa mapato katika maeneo hayo.

Nchi imeimarisha miundombinu ya barabara, usafiri wa anga, usafiri wa majini na huduma za kijamii katika pande zote za Muungano na kuendelea kutumia maliasili vizuri kwa manufaa ya wananchi kuliko ilivyokuwa kabla ya Muungano. Mafanikio haya, bila shaka, ndiyo yaliwezesha Tanzania kutangazwa kuingia kundi la nchi za uchumi wa kati kutoka kundi la nchi maskini mwezi Julai, 2020.

**Mafanikio ya Ulinzi na Usalama**

Ndugu Wanahabari, Vikosi vya Ulinzi na Usalama vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wananchi wenyewe ni ngao muhimu ya kulinda na kutetea mipaka ya nchi, usalama wa nchi na usalama wa mali na raia.

Kwa kipindi chote cha Miaka 60 ya Uhuru, suala la kulinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Ardhini, Angani na Majini) limepewa kipaumbele. Mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuwa salama kutokana na ulinzi madhubuti wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na vikosi vingine na wananchi wa pande zote mbili za Muungano.

**Mafanikio ya Kijamii**

Ndugu Wanahabari, tunashuhudia uwepo wa Utaifa na Umoja ambapo Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umeunganisha watu wa nchi mbili na kuunda Taifa moja la

Tanzania. Historia ya uhusiano wa kidugu wa muda mrefu baina ya watu wa Tanganyika na Zanzibar, ulikuwa chachu muhimu ya kuibua hisia za utaifa na hivyo kupanda mbegu ya utaifa. Watanzania kwa ujumla wanajivunia utaifa wao popote wanapokuwa. Lugha adhimu ya Taifa, Kiswahili inayozungumzwa takribani na Watanzania wote imechangia kuwaunganisha Watanzania na kukuza utaifa.

**Elimu ya Juu**

Ndugu Wanahabari, tunashuhudia Ubora wa elimu ya juu ukiimarika kwa kiasi kikubwa kutokana na kuwepo kwa Taasisi za Elimu za Muungano kama vile Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Baraza la Mitihani la Taifa.Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inatoa mikopo kwa wanafunzi wenye sifa waliodahiliwa katika taasisi za elimu ya juu Tanzania Bara na Zanzibar. Kumekuwepo na ushirikiano mkubwa katika suala la elimu ya juu ambapo wanafunzi kutoka Zanzibar wanaodahiliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, wanapatiwa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Ndugu Wanahabari, katika kusogeza huduma karibu na wananchi wa Zanzibar Serikali imezielekeza Taasisi za Muungano kujenga au kufungua Ofisi Zanzibar. Taasisi zilizojenga au kufungua Ofisi Zanzibar ni Tawi la Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Ofisi ya Makamu wa Rais, Uhamiaji, Makao Makuu na Ofisi za Bunge, Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa, eneo la Uwanja wa Ndege, Zanzibar, Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu, Taasisi ya Sayansi za Bahari, Tume ya Mabadiliko ya Katiba, TANTRADE, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma nazo zimefungua Ofisi Zanzibar, Tume ya Atomiki (TAEC) na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) zina Ofisi za kudumu.

Aidha, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELSB), Baraza la Taifa la Mitihani la Taifa (NECTA), Idara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TAA), Kampuni ya Posta Tanzania, Kampuni ya Simu Tanzania, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Tume ya Pamoja ya Fedha, Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano na Mamlaka ya Bima Tanzania.

**Utatuzi wa changamoto za Muungano,**

Ndugu Wanahabari, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano iliyoundwa mwaka 2005 na kuanza vikao mwaka 2006, imekuwa ni nyenzo muhimu katika kuimarisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Vikao vinavyojumuisha wajumbe kutoka pande zote mbili za Muungano vimekuwa vikifanyika katika ngazi za Wataalamu, Makatibu Wakuu, Mawaziri na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMT chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha changamoto zinatafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa kushughulikia hoja za Muungano kupitia vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ mwaka 2006, hoja 25 zimejadiliwa na mpaka sasa hoja 18 zimepatiwa ufumbuzi.Hoja zilizopatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja za Muungano ni pamoja na Utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binadamu Zanzibar, Utekelezaji wa Sheria ya Usafirishaji Majini (Merchant Shipping Act) katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Uwezo wa Zanzibar Kujiunga na Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organisation - IMO).

Hoja nyingine ni Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili, Ushiriki wa SMZ katika masuala mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda, Gharama za Kushusha Mizigo (Landing Fees) Bandari ya Dar es Salaam kwa Mizigo inayotoka Zanzibar, Usimamizi wa Ukokotoaji na Ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Mikataba ya Mikopo ya Fedha za ujenzi wa miradi ya SMZ.

Pia, hoja za Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano, Mgawanyo wa mapato yatokanayo na: Misamaha ya Mikopo ya Fedha kutoka IMF, misaada ya kibajeti (General Budget Support – GBS), na Uwezo wa Zanzibar kukopa ndani na nje ya Nchi zimepatiwa ufumbuzi.

**Mazingira**

Ndugu Wanahabari, kwa upande wa Mazingira, tangu tupate Uhuru mwaka 1961, kumekuwa na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Serikali katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira ambapo Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliweka mkazo katika kuhakikisha wananchi wanahamasishwa kushiriki kwa vitendo katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Serikali imekuwa na kaulimbiu mbalimbali za kuhimiza hifadhi ya mazingira kama vile Mtu ni Afya na Kilimo cha Kisasa pamoja na kuanzisha miradi kama vile Hifadhi ya Ardhi Dodoma (HADO) mwaka 1973 na Hifadhi Ardhi Shinyanga (HASHI) mwaka 1986 kwa lengo la kuhifadhi ardhi; kuboresha kilimo na ufugaji; na kuzuia mmomonyoko wa udongo.

Pia, Serikali ilianzisha na kuimarisha muundo wa taasisi zake kwa kuweka nyenzo muhimu za usimamizi wa mazingira. Ilianzisha Idara ya Mazingira, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kutungwa kwa Sera ya Mazingira ya Mwaka 1997 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

Ndugu Wanahabari, Serikali imefanikiwa kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na vifungashio na mifuko ya plastiki kwa kupiga marufuku uingizaji nchini,

uzalishaji, usambazaji na matumizi ya vifungashio hivyo kuanzia Machi mosi, 2017 na kufanikisha kuondosha matumizi ya viroba nchini.

Ilipiga marufuku Uzalishaji, Usambazaji, Uingizaji nchini, Usafirishaji nje ya nchi na matumizi ya mifuko ya plastiki nchini kuanzia Juni mosi, 2019 na Ofisi imeendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa katazo hilo katika ngazi ya Kitaifa na Serikali za Mitaa hatua iliyosaidia kupunguza matumizi ya mifuko hiyo.

Kutokana na katazo hili, wajasiriamali na vikundi mbalimbali vya wajasiriliamali vimeanzishwa na vinatengeneza mifuko ya karatasi, nguo na vikapu ambapo hadi sasa, vikundi 2,772 vinavyotengeneza mifuko mbadala vimeanzishwa huku ikikadiriwa kuwa takriban ajira 50,000 zimetokana na usambazaji wa mifuko mbadala.

Ndugu Wanahabari, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti kwa lengo la kurejesha Uoto wa Asili na kupunguza hali ya kuenea kwa jangwa na ukame ambapo kila Halmashauri ya Wilaya imeelekezwa kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Hadi kufikia Mei 2020 takribani miti 608,494,464 ilipandwa katika mikoa yote 26 katika Halmashauri zote. Baada ya tathmini asilimia 62.8 ya miti iliyopandwa ndiyo iliyopona.

Pamoja na hayo kutokana na umuhimu wa kulinda hifadhi ya bahari, wananchi wameshirikishwa kupanda na kuhifadhi mikoko katika maeneo mbalimbali ya Pwani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani hatua inayosaidia kupunguza changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Ndugu Wanahabari, Ofisi imeendelea kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya nishati mbadala wa kuni na mkaa hususani katika taasisi za Serikali zinazotumia kiwango kikubwa cha nishati ya kuni na mkaa.

Wizara na Taasisi zikiwemo Magereza, Jeshi la Kujenga Taifa, Jeshi la Wananchi, Uhamiaji, Kurugenzi ya Huduma ya Wakimbizi pamoja na Vyuo na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii zimewasilisha mipango yao ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Uchambuzi unaonesha Taasisi nyingi zinatumia gesi ya kwenye mitungi (Liquefied Petroleum Gas - LPG) pamoja, vitofali vya mkaa (Briquettes) na umeme kwa ajili ya kupikia.

**Elimu kwa Umma kuhusu Hifadhi ya Mazingira**

Ndugu Wanahabari, katika kuhamasisha ushiriki wa jamii kwenye eneo la hifadhi na usimamizi wa mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo huadhimishwa kila ifikapo tarehe 5 Juni, Siku ya Kuadhimisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame Duniani ambayo huadhimishwa kila ifikapo tarehe 17 Juni na Siku ya Tabaka la Ozoni ambayo huadhimishwa kila ifikapo tarahe 16 Septemba.

Maadhimisho hayo huchagizwa na matukio mbalimbali yakiwemo maonesho ya shughuli za uhifadhi wa mazingira na upandaji miti.

Pia kupitia utoaji elimu, Mafunzo ya Tathmini ya Mazingira Kimkakati yamefanyika kwa Maafisa Mazingira wa Mikoa na Wilaya zote wapatao 220. Mafunzo hayo yamefanyika kwa kanda ambapo Kanda ya Mashariki yalifanyika mkoani Pwan, Kanda ya Kati (Morogoro), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na Kanda ya Magharibi (Kigoma).

Mafunzo haya yalihusu dhana na muktadha wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati; mchakato wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati; na ushirikishwaji wa wadau katika tathmini. Aidha, nakala 450 za Mwongozo zilisambazwa kwa wadau katika Kanda husika.

Aidha, Mafunzo kuhusu usimamizi na uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira yalitolewa kwa Wakaguzi wa Mazingira wapya 429. Wakaguzi hao wanatoka katika Wizara za Mambo ya Ndani ya Nchi (3), Maji (35), na Afya (17); Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (14), Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori (1), Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (40), NEMC (103) na Mamlaka za Serikali za Mtaa (216).

Ndugu Wanahabari, elimu kwa umma ilitolewa kuhusu utekelezaji wa katazo la matumizi ya mifuko ya Plastiki kupitia vipindi vya redio na runinga, makala kwenye magazeti, mabango 50 na video fupi 30. Vile vile, takribani watumiaji wa mitandao ya simu kupitia kampuni mbalimbali walifikiwa na ujumbe mfupi wa katazo husika.

Mafunzo kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni yalitolewa kwa Maafisa Forodha 31 kutoka katika vituo vya mipakani. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa mafundi mchundo 80 kuhusu teknolojia mpya na njia sahihi za kuhudumia vifaa vinavyotumia kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni.

Ndugu Wanahabari, Elimu kuhusu mabadiliko ya tabianchi na hifadhi ya bioanuai katika Taasisi za Elimu ilitolewa kupitia Shindano la Uandishi wa Insha kitaifa. Shindano hili lilihusisha wanafunzi wa Shule ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Juu. Lengo la mashindano haya lilikuwa kukuza na kupima uelewa, kuhamasisha ubunifu kwa wanafunzi na vijana kuhusu mabadiliko ya tabianchi na hifadhi ya bioanuai. Jumla ya wanafunzi 343 walishiriki, ambapo wa kike walikuwa 133 na wa kiume 202. Shule za msingi zilizoshiriki zilikuwa 58, shule za sekondari kidato cha I - IV zilikuwa 90, Shule za sekondari kidato cha V - VI zilikuwa 38 na vyuo 30 vilishiriki.

Mwongozo wa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira umepitiwa kuboreshwa na kusambazwa kwa wadau ili waweze kushiriki kikamilifu katika mashindano ya Tuzo. Maboresho yamesaidia kupanua wigo na kujumuisha masuala ya uzalishaji endelevu viwandani; matumizi ya nishati mbadala ya kupikia; uchimbaji endelevu wa madini; kilimo endelevu; usimamizi wa taka; ufugaji endelevu, na Afya na Usafi wa Mazingira.

**Mikakati ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

Ndugu Wanahabari, katika kuimarisha hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini Mikakati mbalimbali imeandaliwa na kutekelezwa. Mikakati hiyo nipamoja na:

i) Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Kemikali na Taka Hatarishi wa mwaka (2020 - 2025);

ii) Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa kukabiliana na Viumbe Vamizi wa mwaka (2019 – 2029);

iii) Mpango- Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji wadogo wa Dhahabu (2020 -2025);

iv) Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai (2015 - 2020);

v) Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa kudhibiti kuenea kwa Viumbe Vamizi (2019- 2029); na

vi) Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa kuongoa Mfumo ikolijia ya mto Ruaha (2017-2022)

Aidha, Mikakati iliyofanyiwa mapitio katika kipindi hiki ni pamoja na:

i) Mkakati wa Taifa wa kuhifadhi mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka 2019-2024;

ii) Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa wa mwaka 2019-2024; na

iii) Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2021-2026.

Changamoto za Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira

Ndugu Wanahabari,

a) Pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanyika, uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira bado ni mdogo katika baadhi ya maeneo na juhudi zaidi zinahitajika katika kutoa elimu ya mazingira kwa umma;

b) Baadhi ya mila na desturi bado zinarudisha nyuma juhudi za kuhifadhi mazingira. Kwa mfano, tatizo la uchomaji moto bado ni sugu katika maeneo mengi nchini na moja wapo ya sababu ni mila potofu, mfano; mtu akianzisha moto na ukawaka kwa muda mferu na kutekeleza eneo kubwa basi ana maisha marefu;

c) Tatizo la mabadiliko ya tabianchi na athari zake ni changamoto kubwa kwa jumuiya ya kimataifa na nchi yetu. Tayari nchi yetu imeshaanza kuathirika na athari zinakadiriwa kuwa zitaongezeka zaidi kwa kuwa kwa mujibu wa taarifa za kisayansi, uzalishaji wa gesijoto katika nchi zilizoendelea unaongezeka badala ya kupungua;

d) Juhudi za kimataifa za kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi zinakuja na changamoto pamoja na fursa. Kwa upande wa changamoto, matumizi ya sekta ya misitu yanaweza kuathiri usalama na haki ya kujitawala (sovereignty) pamoja na haki za binadamu iwapo tahadhari hazitachukuliwa katika utekelezaji wake. Aidha, kilimo cha mazao kwa ajili ya kuzalisha nishati hususan biofueli inaleta changamoto kwa usalama wa chakula na mazingira nchini;

e) Kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa utunzaji wa takwimu, taarifa na kumbukumbu za masuala ya mazingira na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa maamuzi ya kisera na kimkakati;

f) Kwa kiasi kikubwa Tanzania imeendelea kutekeleza shughuli za mazingira kwa kutegemea fedha za wafadhili jambo ambalo linasababisha kutekelezwa baadhi ya miradi ambayo siyo ya kipaumbele kwa taifa;

g) Baadhi ya wawekezaji wanakwepa kufanya tahmini ya athari kwa Mazingira kwa miradi wanayoitekeleza jambo linalosababisha kutokuwepo kwa uzalishaji endelevu;

h) Ufinyu wa bajeti ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati na programu zinazoandaliwa umepelekea kuendelea kwa uharibifu wa mazingira nchini;

i) Hali ya umasikini katika jamii inasababisha ongezeko la uharibifu wa mazingira nchini kutokana na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za misitu, maji, madini, bahari na maziwa;

j) Hali ya ukame katika baadhi ya mikoa inasababisha kutofikiwa kwa malengo ya idadi ya miti inayotakiwa kupandwa na hivyo kurudisha nyuma juhudi za utunzaji wa mazingira hususan katika mikoa ya Dodoma, Arusha, Manyara na Kilimanjaro; na

k) Suala la uchomaji wa moto misitu na uharibifu wa mazingira kwa njia ya ukataji miti ovyo kwa ajili ya nishati na kilimo katika baadhi ya maeneo nchini unaendelea kwa kasi licha ya kuwepo kwa juhudi zinazofanywa na serikali. Ukataji miti kwa ajili ya nishati unaosababishwa na kuwepo kwa gharama kubwa za kununua nishati mbadala kama vile umeme na gesi ambapo jamii inashindwa kumudu. Aidha, ongezeko kubwa la watu nchini linasababisha kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya kilimo na makazi.

Pamoja na changamoto hizi, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi imeendelea kutekeleza mipango, mikakati na programu mbalimbali kwa ajili ya kuhifadhi mazingira. Jamii inaendelea kuhamasishwa kuthamini mazingira na kuunga mkono juhudi mbalimbali za Serikali za kupambana na uharibifu wa mazingira ili tuweze kufikia maendeleo endelevu.

Ndugu Wanahabari, Ofisi imeendelea kutekeleza mipango na miradi mbalimbali ya hifadhi na usimamizi wa mazingira ambayo ni pamoja na Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Uhakika na Usalama wa Chakula katika

Maeneo Kame ya Tanzania, Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini, Mradi wa kujengea uwezo taasisi ili Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na ukataji miti na uharibifu wa misitu ifikapo mwaka 2022, Mradi wa kujenga uwezo wa Kitaifa kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Mradi wa Majaribio wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria.

Aidha, Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuweka mfumo wa Usimamizi wa Mazingira nchini tangu Azimio la Rio na kuanzishwa kwa Idara ya Mazingira. Serikali imeendelea kuungana na Jumuiya ya Kimataifa katika kukuza juhudi za kuhifadhi Mazingira kupitia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa. Serikali ya Tanzania imesaini na kuridhia jumla ya Mikataba 10 na Itifaki 8.

Ndugu Wanahabari, kwa kutambua na kuzingatia fursa na changamoto zilizopo, katika miaka ijayo, Serikali inatarajia kwamba Muungano utaimarika na mafanikio yaliyopatikana yataendelezwa kwa lengo la kuinua hali za maisha na ustawi wa wananchi wa pande mbili za Muungano.  Kuimarika na kudumu kwa Muungano kutakuwa ni nguzo muhimu ya kuendeleza udugu na matarajio ya Waasisi wa Muungano ya kuwa na Tanzania yenye uchumi imara, Amani, utulivu, haki na usawa kwa kila Mtanzania.

Aidha, katika hifadhi na usimamizi wa Mazingira tunatarajia kuendelea kuwashirikisha wadau mbalimbali katika shughuli za hifadhi mazingira ikiwemo: kuhamasisha upandaji miti na matumizi ya nishati mbadala kwa azma ya kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi; kulinda na kutunza vyanzo vya maji, udhibiti wa taka ngumu, kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, na kutekeleza Kampeni Kabambe ya hifadhi na usafi wa mazingira. Kimsingi tunatarijia mazingira endelevu yatakayochochea ukuaji wa kiuchumi, ustawi ya jamii na Tanzania ya kijani.

**Matarajio ya baadaye**

Ndugu Wanahabari, kwa kutambua na kuzingatia fursa na changamoto zilizopo, katika miaka ijayo, Serikali inatarajia kwamba Muungano utaimarika na mafanikio yaliyopatikana yataendelezwa kwa lengo la kuinua hali za maisha na ustawi wa wananchi wa pande mbili za Muungano.  Kuimarika na kudumu kwa Muungano kutakuwa ni nguzo muhimu ya kuendeleza udugu na matarajio ya Waasisi wa Muungano ya kuwa na Tanzania yenye uchumi imara, Amani, utulivu, haki na usawa kwa kila Mtanzania.

Aidha, katika hifadhi na usimamizi wa Mazingira tunatarajia kuendelea kuwashirikisha wadau mbalimbali katika shughuli za hifadhi mazingira ikiwemo: kuhamasisha upandaji miti na matumizi ya nishati mbadala kwa azma ya kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi, kulinda na kutunza vyanzo vya maji.

Matarajio mengine ni udhibiti wa taka ngumu, kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa

Mazingira na kutekeleza Kampeni Kabambe ya hifadhi na usafi wa mazingira iliyozinduliwa Juni 5, 2021. Kimsingi tunatarijia mazingira endelevu yatakayochochea ukuaji wa kiuchumi, ustawi ya jamii na Tanzania ya kijani.

**Hitimisho**

Ndugu Wanahabari, mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi cha miaka 60 ya Uhuru yametokana na jamii yenye umoja, mshikamano na isiyo na ubaguzi. Watu wa pande mbili za Muungano wanaishi na wanafanya kazi zao za kujiletea maendeleo katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kubughudhiwa. Aidha, Ofisi ya itaendelea kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi katika kutekeleza mipango, mikakati na programu mbalimbali za kuhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu.

Tunapoadhimisha Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, tuna kila sababu ya kuwakumbuka na kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume. Ni ukweli usiopingika kwamba, Muungano wetu ambao msingi wake ni historia ya karne nyingi ya ushirikiano wa watu wa pande hizo mbili na hatimaye kurasimishwa na Waasisi wetu mwaka 1964 umezidi kuimarika na kuenziwa. Mafanikio makubwa tuliyopata siyo ya kubezwa hata kidogo na yanapaswa kulindwa, kudumishwa na kuendelezwa kwa nguvu zote.

Ndugu Wanahabari, nawashukuru kwa ushirikiano wenu mnaotupa kila tunapowahitaji kwa ajili ya kuuhabarisha Umma kuhusu masuala ya Muungano na Mazingira yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais na niwaombe tena tuendelee kupeana ushirikiano.

Asanteni kwa kunisikiliza




# MAFANIKIO NA MAENDELEO YA SEKTA ZA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

Ndugu Wanahabari, awali ya yote napenda Kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana mahali hapa asubuhi hii ya leo. Niendelee Kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Neema zake kwa nchi yetu ambayo ameijaalia tunu za amani, utulivu, mshikamano, umoja na mtangamano katika kipindi chote cha miaka 60 ya Uhuru wa Taifa letu. Tunu hizi zimetuwezesha kupata ustawi kijamii, kiuchumi, kisiasa na pia kutoa fursa kwa Wananchi kuweza kujiletea maendeleo.

Ndugu Wanahabari, Wizara ya Habari; Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatambua mchango wenu katika kuwaelimisha na kuwafikishia wananchi taarifa zinazohusu masuala mbalimbali ikiwemo Sera, Mipango na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Hivyo basi napenda kuwapongeza kwa kazi hii ya kizalendo mnayofanya na ni imani yangu kuwa mtaendelea kufanya kazi zenu kwa moyo wa uzalendo na kuzingatia weledi katika kuiletea nchi yetu maendeleo hususani kupitia sekta hii adhimu ya Habari.

Nipo mbele yenu leo kwa ajili ya kuzungumza na Watanzania kuhusu mchango wa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Taifa letu. Aidha majukumu ya Wizara hii yamepitia mabadiliko mbalimbali ya kuundwa kwake, kabla na baada ya Uhuru. Hivyo basi ni muhimu kuyazingatia haya na kutambua tulipotoka, tulipo na tuendako.

Ndugu Wanahabari, vyombo vya habari vina jukumu kubwa la kutoa habari, kuburudisha, na kuelimisha jamii juu ya matukio na masuala mbalimbali yanayojiri ndani na nje ya Nchi na kuchangia katika kukuza na kuimarisha demokrasia na utawala bora.
Njia za mawasiliano zilizotumika kabla ya Uhuru ndani ya serikali na nje ya serikali, yaani baina ya mtu na mtu au taasisi na taasisi zilikuwa ni mawasiliano ya kuonana ana kwa ana na ikiwa ni mbali zilitumika simu za mezani, barua na kwa wananchi kulitumika zaidi, njia za asili kama vile ngoma, mbiu za mgambo na watu maarufu kama machifu, viongozi wa dini, wazee wa ukoo ndio waliotumika kutoa jumbe mbalimbali.

Aidha, watu walitembea umbali mrefu kufikisha au kufuata taarifa na habari kwa ajili ya maisha na maendeleo yao. Halikadhalika kulikuwa na juhudi mbalimbali za kuanzisha vyombo vya mawasiliano nyakati hizo. Kwa mfano, juhudi ziliwekwa pia katika kuanzisha Magazeti ambapo yalianzishwa magazeti kama vile gazette la Msimulizi (1888), na gazette la German East African Newspaper (1899). Magazeti haya yalianzishwa kuhabarisha umma na kurahisisha mawasiliano kwa kuzingatia malengo ya wale walioanzisha vyombo hivyo. Hata hivyo, vyombo hivi havikukidhi mahitaji ya kitaifa kwa kuwa vilikuwa vya maeneo fulani ya kijiografia, au kabila fulani, au kwa makusudi ya Mkoloni.

Ndugu Wanahabari; mara baada ya Uhuru, yalikuwepo magazeti machache yaliyotumika kuhabarisha umma. Magazeti ya awali kabisa yalikuwa ni Mwafrika, The Nationalist, Ngurumo, Uhuru, na The Standard.

Historia ya vyombo vya habari katika nchi yetu haiwezi kukamilika bila kuvitaja vyombo vyetu vya Shirika la Magazeti ya Serikali (TSN) na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC). Historia ya TSN ilianza mwaka 1930 wakati gazeti la Tanganyika Standard lilipoanzishwa kabla ya kutaifishwa na kuwa chini ya umiliki wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1970. Shirika hili linalochapisha magazeti ya Daily News, Sunday News, Habarileo na spotileo, lina jukumu moja kuu la kuwa chombo cha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi.

Ndugu Wanahabari; kwa upande wa Utangazaji, maendeleo ya redio katika nchi yetu yalianza pole pole tangu mwaka 1951 ambapo studio iliyokuwa inarusha matangazo ilijengwa eneo la Ilala katika jiji la Dar es Salaam na ilianza kwa kurusha matangazo kwa saa moja kwa siku kwa muda wa siku tatu kwa wiki.

Mwaka 1952 stesheni hiyo ilianza kurusha matangazo kila siku baada ya kuongezewa mitambo. Huduma zake ziliendelea kuimarika mwaka hadi mwaka na hadi kufikia mwaka 1961 wakati tunapata uhuru, TBC ilionekana kuwa chombo muhimu na chenye nguvu katika kutoa habari na elimu kwa umma kwenye masuala mbali mbali ya nchi yetu.

Ndugu Wanahabari; Mwaka 1965 Bunge lilipitisha Sheria ya kuvunja TBC na kuanzisha Radio Tanzania, Dar es Salaam (RTD). Maendeleo ya redio nchini yalikwenda sambamba na maendeleo ya magazeti. Serikali iliona ni busara kwa vyombo vya habari kuwa chini ya Serikali ili viweze kutoa huduma vyema kwa wananchi.

Mwaka 1972, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianzisha Televisheni ya kwanza ya rangi. Televisheni hiyo ilikuwa na vituo viwili vya Zanzibar na Pemba. Inaelezwa kuwa mwaka 1981 kulikuwa na seti za TV 40,000 Zanzibar ambazo zilikuwa zinahudumia asilimia isiyozidi 20 ya wananchi wengi wao ni wa mijini.

Ndugu Wanahabari; mwaka 1993 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuona umuhimu wa vyombo vya habari kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, iliamua kufungua milango na kuruhusu kuanzishwa kwa televisheni, redio na magazeti ya binafsi.

Kamisheni ya Utangazaji ilianzishwa Novemba 1993 chini ya Mwenyekiti wake Bwana Mark Bomani na kuanza majukumu ya kupokea maombi na kutoa leseni za redio na televisheni, kufuatilia na kusimamia urushaji wa matangazo ya redio na televisheni pamoja na kufuatilia na kutoa masafa kwa vyombo vya utangazaji vya binafsi.

Ndugu Wanahabari; Miongoni mwa vyombo vya mwanzo vya utangazaji binafsi vilivyopewa leseni ya kuanza kurusha matangazo ya TV nchini mwaka 1994 ni pamoja na Coastal TV Network (CTN), Independent Televisheni (ITV), Dar es Salaam Television (DTV) pamoja na Televisheni ya Chuo Kikuu cha Sokoine iliyopewa leseni mwaka 1995.

Ndugu Wanahabari; Miaka 60 baada ya Uhuru Taifa letu limeshuhudia ukuaji wa sekta hii ambapo kwa sasa kuna magazeti na machapisho yaliyosajiliwa 270, Radio zaidi ya 200, Vituo vya Televisheni 48, Blog 122, Radio mtandao zaidi ya 20. Vile vile, tumeshuhudia ukuaji na mabadiliko ya teknolojia nchini ambao umepelekea kuwa na Television Mtandao (online TV) zaidi ya 500 hadi sasa.

Ndugu Wanahabari; idadi hii ya vyombo vya habari inaonesha jinsi gani Taifa letu limepiga hatua kubwa katika kurahisisha na kuimarisha uhuru wa upatikanaji wa habari kwa wananchi wetu. Hivyo basi sote tutakubaliana kwamba kuna mafanikio mengi yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru yanayogusa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari hapa nchini, yanayohusisha utoaji wa taarifa mbalimbali za Serikali za kitaifa na kimataifa, taarifa za uchumi, siasa, michezo na burudani kwa wananchi kupitia redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii.

Ndugu Wanahabari, urahisi huu wa Mawasiliano na ufikishaji wa Habari kwa wananchi umefikiwa baada ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali pamoja na Sekta binafsi kwenye miundombinu ya mawasiliano.

Baada ya Uhuru wa Taifa letu, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Sekta mbalimbali zikiwemo Wizara, Taasisi za umma na binafsi inaendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi za mawasiliano ya simu, mifumo ya TEHAMA na utoaji wa taarifa kwa umma kwa kuboresha miundombinu ya mawasiliano ya simu, redio na runinga, ujenzi wa minara ya mawasiliano na ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Wengi wetu hujiuliza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ni kitu gani na una umuhimu gani?

Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ni mundombinu wa mawasiliano (Barabara ya kupitisha mawasiliano ya sauti na data) wenye uwezo mkubwa na kasi kubwa unaowezesha mawasiliano ya sauti na data. Mkongo huu unawezesha usafirishaji wa data na taarifa kwa kasi na ubora wa hali ya juu hivyo kuchangia katika maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Mwaka 2009, Serikali kupitia Wizara hii ilianza ujenzi wa muundombinu wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo hadi kufika mwaka 2016 kulikuwa na kilomita 7,910 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Mwaka 2020/21, Wizara imeongeza kilomita 409 za Mkongo huo ambazo zinafanya kuwa na urefu wa kilomita 8,319. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 170 kwa ajili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa kwa kushirikiana na miundombinu ya TANESCO ambapo jumla ya kilomita 4,442 zitaongezeka na kufikisha kilomita 12,761 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano sawa na asilimia 85 ya lengo la kufikisha kilomita 15,000 ifikapo mwaka 2025.

Ndugu Wanahabari, mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umejengwa katika mizunguko mitatu ya Kaskazini, Kusini na Magharibi kwa lengo la kuwa na mawasiliano ya uhakika na umeunganisha mikoa 25 ya Tanzania Bara na kuunganisha Zanzibar na umefanikisha kupeleka huduma za mawasiliano katika nchi saba (7) zinazopakana na Tanzania ambazo ni nchi ya Rwanda, Burundi, Kenya, Uganda, Malawi, Zambia na Msumbiji. Aidha, taratibu za awali za kuunganisha nchi ya Kongo zinafanyika. Vilevile, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umeunganishwa na Mikongo ya baharini ya SEACOM na EASSy. Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umefanikisha utoaji wa huduma za data na intaneti ndani ya nchi na katika nchi jirani ambapo huduma hizo zinatolewa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kwa niaba ya Serikali. Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umesaidia watoa huduma kufikisha huduma za mawasiliano kwa wananchi kwa haraka, uhakika na kwa gharama nafuu hivyo kuharakisha maendeleo ya Taifa kwa kuwa wananchi wanapata fursa ya kutumia TEHAMA kujiletea maendeleo.

Ndugu Wanahabari, (Je ni zipi faida za mkongo wa Taifa wa Mawasiliano)

Kuwepo kwa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye uwezo na ubora mkubwa unaoruhusu watoa huduma wote kuutumia bila upendeleo, kumeleta faida nyingi nchini ambazo ni:-

1. Kupunguza gharama za uwekezaji kwa watoa huduma (TTCL, TIGO, Zantel, Airtel, Vodacom, Simbanet, Viettel na Infinity Africa) kwa kujengwa Mkongo mmoja wa kitaifa kunapunguza gharama za kila mtoa huduma kujenga mkongo wake;

2. Kushuka kwa gharama za maunganisho ya jumla (interconnection fee) kwa simu za mkononi kutoka shilingi 115 kwa dakika mwaka 2009 hadi shilingi 10.4 mwaka 2020. Punguzo hili limewezesha kushuka kwa gharama za watumiaji wa mwisho na hivyo kufanya huduma za mawasiliano kutumiwa na wananchi wengi;

3. Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano unaoonekana kwenye ongezeko la matumizi ya simu za mkononi, intaneti, miamala ya kifedha na ongezeko la mifumo mbali mbali ya kutolea huduma kwa njia ya mtandao; Mathalani mnamo tarehe 9 Disemba 1961 wakati wa Uhuru Tanganyika ilikuwa na simu za mezani 16,238 zilizokuwa kwenye matumizi Tanganyika nzima, nyingi zilikuwa za taasisi na idara za Serikali. Hadi Juni 2021, kulikuwa na laini za simu za mkononi 53,111,246 na za mezani 71,405. Watumiaji wa intaneti wamefikia 29,152,713 ambao kabla ya uhuru hawakuwepo;

Wananchi wamepata ajira kwenye maeneo mbali mbali ikiwemo kwenye vituo vya kutolea huduma za intaneti, uwakala wa huduma za kifedha kupitia mitandao ya simu kama vile malipo yanayofanyika kwa njia za mtandao, na kufanya biashara mbali mbali kwa njia za mitandao, ubunifu wa mifumo na ajira rasmi kwenye kampuni za mawasiliano na Serikali;

5. Jamii kupata huduma mbali mbali zikiwemo za kifedha popote walipo (mobile banking; mobile money) nchini kama vile ulipaji wa kodi za mapato, leseni, pango la ardhi, majengo, adhabu na tozo mbali mbali, ankara za maji na umeme, na malipo mengine ya Serikali;

Ndugu Wanahabari, kama nilivyoeleza hapo awali, kabla ya Uhuru, nchi yetu ilikuwa na mapungufu makubwa sana katika sekta ya Mawasiliano. Maeneo mengi ya Nchi hayakuwa na mawasiliano. Hivyo, Mwaka 2009 Serikali iliamua kuanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ili kuwezesha jukumu la kufikisha huduma za mawasiliano maeneo ambayo hayana mawasiliano na hayana mvuto wa biashara ya mawasiliano hususan maeneo ya vijijini.

Hadi sasa nchi yetu ina jumla ya minara ya mawasiliano 12,902 ambapo minara 2,630 inatoa huduma ya 2G pekee na minara 9,579 inatoa huduma ya mawasiliano ya 2G, 3G au/na 4G. UCSAF imejenga minara 1,068 kati ya minara tajwa hapo juu kwa kutumia ruzuku ya Serikali kwa kushirikiana na watoa huduma ambapo hadi sasa takribani shilingi bilioni 161 zimetumika kujenga minara hiyo.

Hivyo, ujenzi wa minara ya mawasiliano umefanyika kwenye kata 2,579 za Tanzania Bara kati ya kata 3,956 ambazo ni sawa na asilimia 65 na kwa upande wa Zanzibar, minara hiyo imejengwa kwenye kata 101 kati ya kata 110 ambazo ni sawa na asilimia 92. Mnara mmoja una uwezo wa kutoa huduma za mawasiliano kutoka eneo mnara ulipo hadi eneo la umbali wa kilomita 11 kutegemea na jiografia ya eneo husika na aina ya masafa kwa kuwa huduma za mawasiliano kutoka katika mnara zinafika mbali zaidi kama eneo ni tambarare, halina misitu, miti mirefu, miinuko na milima.

Ndugu Wanahabari, Serikali katika azma yake ya kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya mawasiliano ya uhakika na kwa gharama nafuu, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote, hivi karibuni imetangaza zabuni ya shilingi bilioni 37.7 za ujenzi wa minara 224 ya mawasiliano katika maeneo ya kimkakati na mipakani; kuhuisha teknolojia zilizokuwa zikitumika kwenye baadhi ya minara ambazo zilikuwa zina uwezo wa 2G kwenda kwenye teknolojia ya 3G na 4G; kufikisha huduma ya mawasiliano kwenye halmashauri kumi nchini ambazo ni halmashauri ya Mbogwe, Tanganyika, Kakonko, Malinyi, Mtwara Vijijini, Msala Vijijini, Pangani, Bariadi, Nzega na Kilindi.

Lengo likiwa kila mwananchi aweze kupata huduma za intaneti bila kujali yupo mjini au vijijini kwa sababu huduma ya intaneti ni huduma ya msingi kama ilivyo huduma ya mawasiliano ya simu ambayo kila mwananchi ana haki ya kupata huduma ya intaneti. Aidha, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unatarajia kutangaza zabuni za huduma ya mawasiliano ya redio zenye jumla ya shilingi bilioni 1.5 kwa lengo la kuboresha mawasiliano ya redio ili kuongeza wigo wa wananchi kupata taarifa sahihi na kwa wakati.

Ndugu Wanahabari, Kufuatia mwelekeo wa ukuaji wateknolojia nchini, Mwaka 2003, Serikali iliunganisha iliyokuwa Tume ya Mawasiliano Tanzania (TCC) na Tume ya Utangazaji Tanzania (TCC) na kuanzisha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ambayo ndiyo Mamlaka inayosimamia na kudhibiti huduma za mawasiliano, utangazaji na posta nchini. Kwa kuzingatia maendeleo ya teknolojia duniani ambayo yamewezesha huduma mbalimbali za mawasiliano kuwa changamani, mwaka 2005 Serikali, kupitia TCRA, ilianzisha mfumo mpya wa leseni usioegemea teknolojia au huduma yoyote kutokana na mwingiliano wa teknolojia ambapo hivi sasa kwa kutumia kifaa kimoja kama simu ya mkononi unapata huduma ya redio, TV, simu (convergence license system) tofauti na hapo awali ambapo kila huduma ilikuwa inapewa leseni yake peke yake. Maendeleo haya yamewezesha wawekezaji kuongeza huduma mbalimbali bila kulazimika kuomba leseni kila wakati wanapotaka kuongeza huduma mpya. Jambo hili limewezesha uwekezaji na upatikanaji wa huduma mpya kwa watumiaji kama vile huduma za mawasiliano za 2G, 3G na 4G hapa nchini. Mfumo huo umechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza kasi ya maendeleo ya Sekta ya Habari na Mawasiliano Tanzania. Hivi sasa kuna aina za leseni za kuweka miundombinu ya mawasiliano 23, leseni za simu za mkononi na mezani 10 (kampuni saba zinatoa huduma), na leseni za huduma tumizi za mawasiliano 79, na redio 205.

Ndugu Wanahabari, Wizara yangu pia inasimamia huduma za Posta hapa Nchini. Hali ilikuwaje kabla ya Uhuru kwenye eneo hili na hali ikoje leo?

Hapo awali kabla ya Uhuru na mara baada ya Uhuru huduma za posta zilikuwa zinatolewa kwa kutumia watu waaminifu waliochaguliwa na jamii walioitwa mail runners mfano Mzee Rajab Yusufu aliyefanya kazi hiyo kwenye vituo viwili kati ya Nzega na Itobo halafu Itobo na Bukene vilivyopo mkoa wa Tabora kwa kuwa wakati huo hapakuwa na vijiji ila maeneo ya watu walipokuwa wanaishi. Mzee huyo alifanya mitihani wakati wa posta ya mkoloni, alifaulu na kuwa Afisa Msaidizi wa Posta, Tabora Mjini wakati wa mkoloni na baadae alijiendeleza na kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Posta Tanzania baada ya nchi kupata Uhuru na baadae kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Posta Afrika (Pan African Postal unioni PAPU).

Wakati wa Uhuru, Serikali ilianzisha huduma ya Ofisi Ndogo za Posta iliyojulikana kwa jina la Sub Post Office kwa ajili ya kuhudumia wananchi kutoa huduma za posta kwa siku maalum za mikusanyiko kama vile siku za magulio ambapo kunakuwa na mkusanyiko wa watu wengi. Serikali ilianza kuweka masanduku maalum ya posta ili kila mwananchi aweze kupata huduma za posta badala ya kusubiri huduma hizo kwa siku maalum na huduma hiyo imeendelea kuwepo mpaka leo.

Serikali kupitia Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa huduma za Shirika la Posta Tanzania kutoka kutoa huduma za barua na kupiga simu za mezani mpaka Shirika kuanza kutoa huduma zake kwa njia ya kidijitali kwa kuan

zisha huduma mbalimbali kama posta mlangoni, posta kiganjani ambapo laini ya simu ya mteja ndio sanduku lake la barua. Vilevile, huduma za duka la posta mtandao na kuendelea kupanua wigo wa usafirishaji wa mizigo, barua na vipeto. Shirika la Posta limeanzisha mashirikiano na taasisi mbalimbali za Serikali kwa kuanzisha huduma za uwakala ambapo mpaka sasa Shirika la Posta ni wakala wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Benki za CRDB na NBC, Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC). Shirika la Posta Tanzania limehuisha utaratibu wa utoaji wa huduma zake kwa wateja kwa kutumia TEHAMA kama vile huduma pamoja, posta kiganjani, smart posta ili kwenda sambamba na ukuaji na mabadiliko ya teknolojia duniani.

Kwa kazi njema ambayo Shirika la Posta Tanzania linafanya, 15/11/2021 shirika limekabidhiwa kifimbo cha Malkia (Queens Baton Relay) na kamati ya Olympic Tanzania kwa ajili ya kusafirishwa na Shirika kwenda sehemu mbalimbali Duniani!!! Nawakaribisha sana Watanzania ili tuendelee kutumia huduma za Shirika letu la Posta ambazo zimeboreshwa sana.

Ndugu Wanahabari, ili kuhakikisha Wananchi wananufaika na uwekezaji mkubwa ulitokana na mazingira mazuri ya uwekezaji kwenye eneo la Mawasiliano na Teknolojiaya Habari, Mwaka 2010, Serikali ilianza kutekeleza Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi. Mfumo huu unatambulisha mahali halisi ambapo mtu anaishi, mahali ilipo biashara yake au ofisi anayofanyia kazi kwa kufuata jina la barabara na mtaa, namba ya nyumba au jengo pamoja na Postikodi. Postikodi au simbo za posta kama inavyotambulika ni mfumo maalum wa tarakimu unaotambulisha eneo la kufikisha huduma za posta ambapo kwa nchi ya Tanzania inaanzia katika ngazi ya kata, wilaya, mkoa na kanda.

Serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatekeleza mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi nchini lengo likiwa ni kurahisisha mawasiliano, ufikishaji wa huduma za Serikali kwa wananchi na kufanyika kwa shughuli za kijamii, kiuchumi na kiutawala.

Kwa Mwaka wa fedha 2021/22, Serikali imepanga kutumia shilingi bilioni 45 kutekeleza mradi huu katika Halmashauri 194 nchini kati ya hizo halmashauri 184 ni za Tanzania Bara na Halmashauri 10 za Zanzibar lengo ni kila mwananchi awe na anwani ya makazi ifikapo mwaka 2023. Wizara ilifanya maamuzi ya kutumia shilingi bilioni 3 kukamilisha utekelezaji wa Mfumo huo katika jiji la Mwanza kama sehemu ya mfano kwa kuweka miundombinu ya Mfumo pamoja na kukusanya taarifa za makazi katika mwaka 2020/2021 ili maeneo yaliyobaki yapate mahali pa kujifunzia.

Mfumo wa Anwani za Makazi umetengeneza programu tumizi ya simu za mkononi inayoitwa NAPA Mobile App ambayo inaingizwa taarifa zote za makazi ya watu kwa mfano majengo ya ofisi za Serikali na binafsi, barabara, njia, majina ya vituo vinavyotoa huduma za kijamii kama hospitali, shule, zahanati n.k na inafanya kazi kama google map, ambapo mwananchi anaweza kuingia kwenye programu hiyo kupitia simu ya mkononi na kuandika mahali anapotaka kwenda kutoka mahali alipo kwa muda huo na programu hiyo itamuonesha njia ya kupita mpaka kufika sehemu husika.

**HITIMISHO**

Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru taswira ya maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Biashara kwa ujumla inaonesha matokeo na mwelekeo chanya. Hali hii inatokana na hatua madhubuti zilizochukuliwa na Serikali kwa lengo la kufungamanisha sekta hiyo na sekta nyingine ili kufikia azma ya Serikali ya Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda.

Mwenendo huo unaashiria kuwa Tanzania ni mahali sahihi na penye mazingira wezeshi na shindani yanayovutia wawekezaji wa ndani na nje. Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuchochea na kuhamasisha ukuaji wa sekta ya viwanda na biashara kwa kuweka msukumu katika kuimarisha tija kwenye sekta hiyo na sekta nyingine za uzalishaji na huduma zinazohusika moja kwa moja na ukuaji sekta ya viwanda na biashara hususan sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini.

Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mazingira ya biashara kama ajenda ya kudumu ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya utekelezaji wa Blueprint na kukuza ushindani wa sekta binafsi. Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa chagua la uwekezaji na mahali salama penye sera za biashara zinazotabirika kwa wawekezaji na wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara itaendeleza jitihada za kujenga ushirikianao mzuri na wenye tija baina ya Serikali na sekta binafsi ili kuhakikisha azma ya kuifanya sekta hiyo kuwa injini ya ukuaji endelevu na jumuishi wa uchumi linafanikiwa kwa vitendo kupitia sekta ya viwanda na biashara.

Wizara na Taasisi zake imejipanga na kujizatiti kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mipango ya Kitaifa na mipango na bajeti za kila mwaka. Katika kufikia malengo ya kiuchumi ya nchi suala la kuongeza tija katika sekta zote za uzalishaji zinazofungamana na sekta ya viwanda na biashara litapewa msukumo wa pekee ili kufikia malengo ya Tanzania tunayoitaka yenye maendeleo endelevu na jumuishi ya kiuchumi yaliyojengwa kwenye msingi imara wa viwanda.



MIAKA 60 YA KUKUZA NA KUENDELEZA VIWANDA NA BIASHARA

## UTANGULIZI

### 1.1 Historia fupi ya Wizara

Tangu mwaka 1961 Tanzania Bara ilipopata uhuru hadi sasa tunapoadhimisha miaka 60 ya uhuru, Wizara ya Viwsanda na Biashara imepitia mabadiliko mbalimbali ya Kisera, Kisheria na Kimuundo kulingana na mahitaji ya nyakati tofauti za uhai wa Sekta ya Viwanda na Biashara. Mabadiliko hayo yanajidhihirisha kwenye majina ya wizara zilizosimamia sekta ya viwanda na biashara katika vipindi tofauti ambapo mara baada ya uhuru kati ya mwaka 1962 na 1964 wizara ilijulikana kama Wizara ya Biashara na Viwanda. Kati ya mwaka 1964 na 1967 sekta hizo mbili zilitenganishwa ambapo sekta ya Biashara iliundwa kama Wizara ya Biashara na Ushirika na sekta ya viwanda iliundwa kama Wizara ya Viwanda, Madini na Umeme (1964-1965) na baadaye Wizara ya Viwanda, Madini na Nishati (1965 -1967).

Kati ya mwaka 1967 na 1976 sekta hizo ziliunganishwa tena na kuwa Wizara ya Biashara na Viwanda. Kutokana na umuhimu wa sekta hizo, kati ya mwaka 1976 na 1986 kila sekta ilijitegemea kama wizara kamili yaani Wizara ya Viwanda na Wizara ya Biashara. Sekta hizo ziliunganishwa tena na kuitwa Wizara ya Viwanda na Biashara kati ya mwaka 1986 na 2006. Kati ya mwaka 2006 na 2010 wizara ilijulikana kama Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko na baadaye kurudia tena jina lake la Wizara ya Viwanda na Biashara kati ya mwaka 2010 na 2015. Mwanzoni mwa Serikali ya Awamu ya Tano wizara iliongezewa jukumu la uwekezaji na kuitwa Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji kati ya mwaka 2015 na 2018 jukumu la uwekezaji liliporejeshwa Ofisi ya Waziri Mkuu; na jina kubaki kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara tangu mwaka 2018 hadi sasa.

1.2 Mawaziri Waliongoza Wizara Kuanzia 1961 - 2021
Bw. C. G. Kahama (Bukoba), Bw. J. S. Kasambala (Rungwe), Bw. A. K. Hanga (Unguja) Bw. J. S. Kasambala (Rungwe), Bw. A. M. Babu (Zanzibar), Bw. A. Z. Nsilo Swai (Arusha Urban), Bw. A. M. Maalim (Kuteuliwa Zanzibar), Bw. P. Bomani (Nyanza), Bw. A. H. Jamal (Morogoro), Bw. C. D. Msuya (Kuteuliwa), Bw. A. Rulegura (Sengerema), Luteni Kanali A. S. Mchumo (Temeke), Bw. Mustapha Nyang'anyi (Kondoa), Bw. Basil P. Mramba (Rombo), Mhe. J. C. Rwegasira (Mbunge wa Taifa), Mhe. Cleopa D. Msuya (Mwanga), Mhe. Dkt. William F. Shija (Sengerema), Mhe. Dkt. Abdallah O. Kigoda (Handeni), Mhe. Kingunge Ngombaremwiru (Kuteuliwa), Mhe. Iddi M. Simba (Ilala), Mhe. Dkt. Juma Alifa Ngasongwa (Ulanga), Mhe. Nazir M. Karamagi (Bukoba Vijijini), Mhe. Basil P. Mramba (Rombo), Mhe. Dkt. Mary M. Nagu (Hanang), Mhe. Dkt. Cyril A. Chami (Moshi Vijijini), Mhe. Dkt. Abdallah O. Kigoda (Handeni), Mhe. Charles J. P. Mwijage (Muleba Kaskazini), Mhe. Joseph George Kakunda (Sikonge), Mhe. Innocent Bashungwa (Karagwe), Mhe. Geoffrey Ildephonce Mwambe (Masasi Mjini), na Mhe. Prof. Mkumbo A. Kitila (Ubungo).

### 1.3 Manaibu Mawaziri kwa Vipindi Mbali Mbali (1961-2021)

Mhe. M. R. Kundya (Singida), Mhe. K. H. Ameir (Zanzibar), Mh.C. M. Mzindakaya (Lyangalile), Mhe. E. C. Mwanansao (Nkasi), Mh. Dk. Nicas Guido Mahinda (Morogoro), Mh. Shamim Parkar Khan (Viti Maalum), Mhe. Antony M. Diallo (Mwanza Vijijini), Mhe. Rita Louse Mlaki (Kawe), Mhe. David Mathayo David (Same Magharibi), Mhe. Hezekiah N. Chibulunje (Chilonwa), Mhe. Dkt. Cyril A. Chami (Moshi Vijijini), Mhe. Lazaro S. Nyalandu (Singida Mashariki), Gregory G. Teu (Mpwapwa), Mhe. Janet Z. Mbene, Mhe. Inj. Stellah M. Manyanya (Nyasa) na Mhe. Exaud S. Kigahe (Mufindi Kaskazini).

### 1.4 Makatibu Wakuu kwa Vipindi Mbali Mbali (1961-2021)

Bw. Fulgence Kazaura, Bw. Fadhil Mrina, Bw. Gilman Rutihinda, Bw. Ndewira Kitomari, Dkt. Fulgence J. Mujuni, Bw. Fadhil Mbanga, Bw. Silvanus Adel, Prof. Mark Mwandosya, Balozi Marten Lumbanga, Bw. Vincent Mrisho, Bw. Benard Mchomvu, Prof. Joshua Doriye, Balozi Charles Mutalemwa, Bw. Ahmada R. Ngemera, Bw. Wilfred L. Nyachia, Dkt. Stergomena L. Tax, Bibi Joyce K.G. Mapunjo, Bw. Uledi Mussa, Dkt. Adelhelm Meru na Prof. Adolf F. Mkenda, Prof. Elisante Ole Gabriel, Prof. Joseph Buchweshaija, Prof. Riziki S. Shemdoe na Bw. Doto M. James.

### 1.5 Manaibu Katibu Mkuu kwa Vipindi Mbali Mbali (2006-2021)

Bw. Godfrey Mkocha, Dkt. Florens M. Turuka, Dkt. Shabaan R. Mwinjaka, Bibi Maria Bilha, Bw. Inj. Joseph K. Malongo, Bw. Ludovick Nduhiye, Prof. Joseph Buchweshaija, Dkt. Edwin P. Mhede, na Dkt. Hashil T. Abdallah.

### 1.6 Majukumu ya Wizara

Wizara ya Viwanda na Biashara inatekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kutunga na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia

Sekta za Viwanda na Biashara.
ii) Kufuatilia na kufanya tathmini (M&E) ya maendeleo ya Sekta za Viwanda na
Biashara.

iii) Kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za Sekta za Viwanda na
Biashara.

iv) Kutafuta fursa mbalimbali za masoko ndani n a nje ya nchi kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania;

v) Kubuni na kutekeleza programu, miradi na mikakati ya kuendeleza Sekta za Viwanda na Biashara.

vi) Kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi ili kuongeza mchango wa sekta hiyo kwenye maendeleo ya Sekta za Viwanda na Biashara;

vii) Kukuza na kuhamasisha biashara ya ndani na nje;

viii) Kuimarisha utafiti kwa maendeleo ya Sekta za Viwanda na Biashara; na

ix) Kusimamia utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara

**1.7 Taasisi Zilizochini ya Wizara**

Taasisi zilizo chini ya Wizara ni 15 zikijumuisha Mashirika matano (5) ambayo ni Shirika la Maendeleo la Taifa (National Development Corporation - NDC); Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Small Industries Development Organization - SIDO); Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (Tanzania Industrial Research Development Organization - TIRDO); Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization – TEMDO); na Shirika la Viwango Tanzania (Tanzania Bureau of Standards - TBS).

Aidha, kuna Wakala mbili (2) ambazo ni Wakala wa Vipimo (Weights and Measures Agency - WMA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Business Registrations and Licensing Agency – BRELA). Pia kuna Mamlaka mbili (2) ambazo ni Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (Export Procesing Zones Authority – EPZA) na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tanzania Trade Development Authority – TANTRADE).

Vilevile kuna Mabaraza mawili (2) ambayo ni Baraza la Ushindani (Fair Competition Tribunal – FCT) na Baraza la Taifa la Utetezi wa Haki ya Mlaji (National Consumers Advocacy Council – NCAC). Taasisi nyingine ni Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (Centre for Agricultural Mechanisation and Rural Technology - CAMARTEC); Chuo cha Elimu ya Biashara (College of Business Education - CBE); Tume ya Ushindani (Fair Competition Commission - FCC); na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (Warehouse Receipts Regulatory Board – WRRB).

**MAENDELEO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA 1961 – 2021**

**2.1 Baada ya Uhuru (1961 – 1967)**
Katika miaka ya mwanzoni mwa 1960, Sera za Kiuchumi zilijikita zaidi katika uzalishaji na mabadiliko ya kimuundo. Lengo lilikuwa kubadili mfumo wa uchumi wa kikoloni uliojikita zaidi katika viwanda vya uchakataji (processing industries), kuzalisha bidhaa za kawaida (simple consumer goods) na kuagiza bidhaa muhimu kutoka nje. Baada ya Uhuru uzalishaji viwandani ulichukua mwelekeo wa kutumia zaidi nguvukazi badala ya mashine (labor intensive techniques) ikiwa ni pamoja na kuondokana na sera za viwanda za kikoloni zilizosisitiza uzalishaji kwa kutumia vibarua. Katika kipindi hicho viwanda vya uchakataji vilikuwa 220 vikiwa vimeajiri watu 200,000 kati ya idadi ya watu milioni tisa wakati huo. Aidha, Sekta ya viwanda ilichangia takriban asilimia 4 ya Pato la Taifa (GDP).

Asilimia kubwa ya viwanda vilivyokuwepo kwa kipindi hicho vilimilikiwa na sekta binafsi. Kati ya Viwanda 220 vilivyokuwepo, viwanda vikubwa vilivyo milikiwa na makampuni ya kimataifa vilikuwa 6 tu navyo ni British America Tobacco (sasa TCC - Sigara), East African Breweries (sasa TBL), Coca-cola, Tanganyika Packers, Metal box na Bata shoes (sasa Bora Shoes). Kimuundo wa uzalishaji, 30% vilikuwa ni vinu vya kuchambua pamba na kuzalisha nyuzi za katani; 25% vilizalisha bidhaa za chakula, vinywaji na tumbaku; 16% vilifanya matengenezo (repairs) ya machine na vyombo vya usafiri; 15% vilizalisha mbao na samani, na 14% vilizalisha viatu na sabuni.

Katika kipindi cha miaka ya 1961 – 1967, Serikali iliandaa na kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitatu (1961 – 1964) uliojielekeza katika kuhamasisha ukuaji wa viwanda ili kuleta matokeo makubwa na ya haraka. Mpango huo ulifuatiwa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (1964 – 1969) ukiwa pia na malengo ya kukuza viwanda. Hata hivyo, mipango hiyo ya Serikali haikuleta matokeo tarajiwa. Kutokana na hali matokeo yasiyoridhisha ya mipango hiyo Serikali ilitangaza Azimio la Arusha lililotekelezwa katika kipindi cha 1967 – 1992 ambapo sera za kiuchumi za Ujamaa na Kujitegemea ziliweka shughuli zote za uzalishaji chini ya Dola ambapo miundmbnu ya uchumi iliwekwa chini ya usimamizi wa Serikali au kupitia taasisi za umma.

**2.2 Azimio la Arusha (1967 – 1992)**
Azimio la Arusha lilitangazwa rasmi tarehe 25 Februari 1967 kwa nia ya kujenga msingi wa Sera ya uchumi wa kijamaa unaotekelezwa kwa Serikali kumili njia kuu za uchumi. Aidha, katika kipindi hicho, ushiriki wa wawekezaji binafsi na wafanyabiashara kutoka sekta binafsi ulipewa nafasi ndogo sana. Katika kipindi hicho, Serikali iliunda mfumo wa kitaasisi wa kusimamia uchumi wa nchi katika sekta za Viwanda na Bashara, ambapo ilitungwa Sheria ya Msajili wa Viwanda National Industries Licensing and Registration Act, 1967. Serikali iliunda Bodi za kusimamia biashara ya mazao ya biashara kama vie Pamba, Mkonge, Kahawa,Chai n.k. Pia Seriali ilianzisha bodi za kusimamia biashara za ndani na nje ambapo Bodi ya Biashara ya Ndani (Board of Internal Trade).

na (Board of Extarnal Trade) iliundwa kwa ajili ya kusimamia biashara za nje (exports). Serikali pia iliunda mashirika ya umma kwa ajili ya biashara mfano kwa mazao ya mikunde na Iliki iliunda shirika la The General Agricultural Products Exports Ltd (GAPEX). Katika Sekta ya Viwanda Serikali ilibadili majukumu ya iliyokuwa Shirika la Maendeleo (Tanzania Development Corporation) na kuwa Shirika la Taifa la Maendeleo (National development Corporation-NDC).

Maeneo mengine yaliyodhibitiwa na Serikali ni uingizaji wa bidhaa kutoka nje, ukuzaji wa viwanda na kuchukua uongozi katika mashirika ya umma yaliyoanzishwa. Umiliki wa kigeni wa njia kuu za uzalishaji ulidhibitiwa kwa kuweka sharti la kuingia ubia na Serikali. Aidha, wamiliki wa kigeni walishiriki kupitia mikataba ya uuzaji na usambazaji wa bidhaa za viwandani. Vilevile, Serikali iliongeza udhibiti wa moja kwa moja wa uzalishaji viwandani kwa

kuanzisha Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Viwanda na Shirika la State Trading Corporation (STC) kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Biashara.

STC ilianzishwa Februari 1967 ili kuwapunguzia wananchi mzigo wa bei kubwa kutokana na faida kubwa kwenda kwa wafanyabiashara binafsi. STC ilivunjwa mwaka 1973 baada ya kutokuwa na ufanisi uliotarajiwa. Badala yake iliundwa Bodi ya Biashara ya Ndani (Board of Internal – BIT) mwaka 1973 iliyoratibu shughuli za makampuni ya biashara ya mikoa (RTCs), Shirika la Ugawaji (NDL), Shirika la Biashara (Biashara Consumer Services – BCS) na makampuni sita ya uagizaji bidhaa nje: National Pharmaceuticals Company Ltd. (NAPCO), Agricultural and Industrial Supplies Company Ltd. (AISCO), Building, Hardwares, and Electric Supplies Company Ltd. (BHESCO), General Foods Comapany Ltd. (GEFCO), Domestic Appliances and Bicycles Company Ltd. (DABCO) na Household Supplies Company Ltd. (HOSCO).

**2.3 Uboreshaji wa Sera za Uchumi (1981 -2021) 2.3.1 Ulegezaji wa Masharti ya Biashara**

Katika kipindi cha mwaka 1981 hadi 1996 Serikali ilichukua hatua za kuboresha sera za biashara kwa kulegeza taratibu za uingizaji bidhaa na usimamizi wa fedha za kigeni. Wauzaji bidhaa nje ya nchi waliruhusiwa kubaki na kiasi fulani cha fedha za kigeni na kuzitumia kuagiza bidhaa toka nje. Marekebisho hayo ya Sheria yalichochewa na Programu ya Kurekebisha Uchumi ya mwaka 1986 ambayo iliondoa mfumo wa kupanga bei na vikwazo dhidi ya uagizaji bidhaa kwa kuanzisha mfumo wa leseni za uagizaji bila masharti (open general license). Programu hiyo ililenga kuanzisha hatua kwa hatua mfumo wa uchumi wa soko unaozingatia ushindani. Baadhi ya hatua za Kisera zilizotekelezwa kutokana na Programu hiyo ni pamoja na:

i) Mtangamano wa kiuchumi na utekelezaji wa Sera endelevu za Fedha na bajeti, kama vile mfumo wa ushindani wa kiwango cha ubadilishaji fedha za kigeni, riba za mabenki na urekebishaji wa mfumo wa vyombo vya fedha;

ii) Kulegeza masharti ya biashara ya mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na kurejesha mfumo huru wa vyama vya ushirika;

iii) Kurekebisha mfumo wa uendeshaji na kubinafsisha mashirika ya umma katika sekta za uzalishaji, huduma na biashara;

iv) Kurekebisha muundo na mfumo wa uendeshaji wa Sekta za kijamii, hususan, afya na elimu kwa madhumuni ya kuinua viwango vya utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wananchi wengi; na
v) Kurekebisha muundo na mfumo wa utumishi wa umma kwa nia ya kutoa huduma bora zaidi zinazohitajika na sekta binafsi; na kuweka mazingira yanayofaa kwa undeshaji biashara, ikiwa ni pamoja na kurekebisha mfumo wa sheria na taratibu zinazosimamia biashara.

Aidha, katika kipindi hicho Tanzania ilijielekeza katika kuimarisha uchumi unaoweza kuhimili ushindani katika soko la ndani, kikanda na kimataifa na hasa baada ya kujiunga na Shirika la Biashara la Dunia (WTO) na ushiriki wake katika Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda.

**2.3.2 Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma**

Mageuzi kwenye Mashirika ya Umma (Parastatal Sector Reforms) yalianza kutekelezwa mnamo mwaka 1992. Mwaka 1993, Serikali ilianza rasmi zoezi la urekebishaji wa mashirika ya umma ikiwa ni moja ya hatua za utekelezaji wa Mpango wa Kufufua na Kurekebisha Uchumi wa Mwaka 1986. Hatua hii ililenga kuiondoa Serikali katika ushiriki wa moja kwa moja wa shughuli za kiuchumi ikiwemo uzalishaji na biashara na badala yake kukabidhi jukumu hilo kwa sekta binafsi kwa utaratibu wa ubinafsishaji. Ubinafisishaji ulilenga kufufua viwanda ambavyo kwa wakati huo havikuwa na ufanisi, kuondoa umasikini kwa kuongeza ajira na pato la Taifa. Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (Presidential Parastatal Sector Reform Commision - PSRC) na Kitengo cha Kudai Madeni (Loans and Advances Realisation Trust – LART) vilihusika katika zoezi la ubinafishaji. Mashirika kadhaa yalirekebishwa aidha kwa kuyabadili na kuyafanya yajiendeshe kibiashara zaidi, kubinafsishwa au kufilisiwa.

**2.3.3 Sera na Mikakati ya Kuendeleza Viwanda**

Kutoka mwaka 1961 hadi 1974, Serikali iliendelea kutekeleza sera ya kuzalisha bidhaa zilizokuwa zikiagizwa kwa wingi toka nje (Import Substitution Industries). Serikali iliandaa na kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Viwanda vya Msingi (Basic Industries Strategy) wa mwaka 1975 - 1995 uliolenga kukuza uzalishaji wa bidhaa za walaji, bidhaa za kati na bidhaa za kimtaji (capital goods) zilizokuwa zinaagizwa nje. Serikali pia ilitunga Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 1996 (Sustainable Indutrial Developent Policy-SIDP) kwa lengo la kuchagiza maendeleo kwenye sekta ya Viwanda.

Malengo makuu ya SIDP yalikuwa kufanikisha maendeleo ya sekta ya viwanda kupitia mipango ya maendeleo ya Taifa, kuleta maendeleo endelevu ya watu kupitia Sekta ya Viwanda kwa kuweka ushiriki wa sekta binafsi kwenye ujenzi wa viwanda jukumu la Serikali likiwa ni kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta ya viwanda.Pamoja na sera hiyo Serikali pia iliandaa Mkakati wa utekelezaji wake - Mkakati Unganishi wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda (Integrated Industrial Development Strategy – IIDS, 2011-2025).

Ili kufikia malengo ya SIDP, Serikali ilitunga Sheria ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje ya mwaka 2003 – Export Processing Zones Act, 2003; na Sheria ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya mwaka 2006 na marekebisho yake ya 2012 – Special Economic Zones Act. Lengo la sheria hizo ni kutekeleza Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda kwa kuanzisha mitaa ya viwanda (industrial parks) na maeneo maalum ya viwanda (industrial zones) yaliyowekewa miundombinu ya msingi ya kiuchumi ili

kuvutia na kukuza uwekezaji; kuongeza uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje (export led industrialization), kuongeza mapato ya fedha za kigeni, fursa za ajira na usindikaji wa malighafi zinazozalishwa nchini.

**2.3.4 Ufuatiliaji wa Viwanda Vilivyobinafsishwa ambavyo Havifanyi Kazi**

Katika kutekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ikiwa ni pamoja na kufufua na kuendeleza viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi; kupitia Hotuba yake aliyoitoa tarehe 20 Novemba, 2015 wakati akizindua Bunge la Jamhuri ya Muungano, Mhe. Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alieleza azma ya Serikali ya kuvirejesha viwanda ilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi. Katika kutekeleza maagizo hayo Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa nyakati tofauti imekuwa ikifanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa viwanda na mashirika husika.

Katika kipindi cha Agosti, 2017 hadi Aprili, 2019, ufuatiliaji na tathmini ulifanyika kwa viwanda 156 na shirika moja (1) na kubaini kuwa viwanda 88 vinafanya kazi na viwanda 48 na shirika moja (1) havifanyi kazi na viwanda 20 kupoteza sifa ya kuwa viwanda kutokana na maeneo yake kugeuzwa matumizi. Kutokana na hali hiyo, Serikali iliamua kuvirejesha viwanda visivyofanya kazi kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo: Wawekezaji kutokuwa na uwezo wa kifedha (mtaji) na kitaalam kuviendesha kwa tija; na baadhi ya wawekezaji kukiuka masharti ya mkataba wa mauzo. Urejeshaji huo ulilenga kutafuta wawekezaji mahiri katika kuendeleza viwanda hivyo.

Hadi sasa Serikali imekamilisha kuvirejesha serikalini viwanda ishirini (20) na shirika moja (1) kutokana na ukiukwaji wa masharti ya mikataba ya mauzo na pia wawekezaji wake kutoonesha nia ya kutaka kuviendeleza. Wizara ya Viwanda na Biashara imepata ridhaa ya Mamlaka ya kubinafsisha upya viwanda vilivyokamilika urejeshwaji wake, aidha zoezi la kurejesha viwanda vingine 27 vilivybaki ambavyo wawekezaji wake wameshindwa kuviendeleza linaendelea.

## MAFANIKIO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA 1961- 2021

### 3.1 Maendeleo ya Sekta ya Viwanda

**3.1.1 Mchango wa Sekta ya Viwanda kwenye Pato la Taifa**

Mchango wa Sekta ya Viwanda kwenye Pato la Taifa umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo wakati wa Uhuru mwaka 1961, Sekta ya Viwanda ilikuwa ikichangia asilimia 3.5 ya Pato la Taifa (GDP). Hadi kufikia mwaka 2015 mchango wa sekta hiyo ulikuwa asilimia 7.9. Kutokana na jitihada za Serikali za kuhamasisha ujenzi wa viwanda mchango wa sekta ya viwanda kwenye Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 8.5 ya Pato la Taifa mwaka 2019. Mwaka 2020 mchango wa sekta ulishuka kidogo hadi asilimia 8.4.

**3.1.2 Mchango wa Sekta ya Viwanda kwenye Ajira**

Ajira katika Sekta ya Viwanda imeendelea kuongezeka ambapo mwaka 1961 Sekta ya Viwanda ilichangia asilimia 9 ya ajira zote nchini. Hadi kufikia mwaka 2015, ajira katika Sekta ya Viwanda zilikuwa zimeongezeka na kufikia ajira 254,786. Aidha, kutokana na msukumo mkubwa wa ujenzi wa uchumi wa viwanda, idadi ya ajira imeongezeka zaidi na kufikia ajira 482,601 mwaka 2021.

**3.1.3 Uendelezaji wa Maeneo ya EPZ/SEZ**

Jumla ya Makampuni 174 yamesajiliwa katika maeneo ya EPZ/SEZ na kuwekeza mtaji wa Jumla ya Dola za Marekani Bilioni 2.23. Kupitia uwekezaji huo jumla ya ajira 57,563 zimezalishwa. Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji kwenye maeneo ya EPZ/SEZ ili kuhakikisha mazao ya kilimo, misitu, mifugo, uvuvi na madini yanayozalishwa nchini yanaongezwa thamani na kutengeneza ajira kwa Watanzania badala ya kusafirishwa kama malighafi kwenda nje.

Kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na Mwekezaji ambaye ni Kampuni ya CMPort kutoka China na Mamlaka ya Uwekezaji ya Serikali ya Oman ili ujenzi wa Eneo Maalum la Kiuchumi Bagamoyo (Bagamoyo SEZ) uanze mapema iwezekanavyo. Vilevile, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuendeleza eneo maalum la kibiashara la Kurasini Trade and Logistics Centre lenye ukubwa wa ekari 60.

Aidha, Wizara ya Viwanda na Biashara imeandaa Mwongozo wa Uwekezaji katika Mitaa ya Viwanda nchini ili kurahisisha taratibu za uwekezaji katika Mitaa ya Viwanda na kuongeza kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.




*Eneo Huru la Uwekezaji kwa Mauzo Nje ya Nchi (EPZA) la Benjamin William mkapa lililopo Ubungo, Dar es salaam*

**3.1.4 Kujitosheleza kwa Mahitaji ya ndani kwa baadhi ya bidha za viwandani**

Kwa miaka 60 Nchi imeendelea kuwekeza katika viwanda na kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali. Hadi kufika mwaka 2020, nchi imefanikiwa kujitosheleza katika baadhi ya bidhaa muhimu zinazozalishwa nchini zikiwemo: saruji, marumaru, nondo, mabati na vifaa vya umeme. Matokeo hayo yamefikiwa kutokana na jitihada za serikali kuhamasi-

sha wawekezaji kujenga viwanda vipya pamoja na upanuzi wa viwanda vya zamani. Upanuzi wa viwanda vya saruji vya Tanga Cement Ltd na Mbeya Cement Ltd na kuanza kwa uzalishaji wa viwanda vipya kikiwemo Kiwanda cha Kilimanjaro Cement Ltd cha mjini Tanga kilichoanza kufanya kazi mwaka 2017 na ujenzi wa Kiwanda kipya na kikubwa cha Dangote mjini Mtwara umesababisha ongezeko la uwezo wa uzalishaji wa saruji hadi kufikia tani 9,080,000 kwa mwaka. Aidha, viwanda hivyo vinaweza kukidhi mahitaji ya saruji nchini ambayo yanakadiriwa kuwa tani 8,000,000 kwa mwaka na ziada kuuzwa nje hususan nchi za Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, DRC na Msumbiji.

Vilevile, jitihada za Serikali za kuhamasisha uwekezaji wa viwanda zimeleta mafanikio ya ujenzi wa viwanda vikubwa viwili vya marumaru vya Goodwill (T) Ceramic Co. Ltd na KEDA (T) Ceramic Co. Ltd. Kiwanda cha Goodwill (T) Ceramic Co. Ltd kina uwezo uliosimikwa wa mita za mraba milioni 18 ambapo uzalishaji halisi ni mita za mraba Milioni 14.4. Kiwanda cha KEDA kina uwezo wa uzalishaji wa mita za mraba 28.8 ambapo uzalishaji halisi ni mita za mraba milioni 18.



*Wafanyakazi wakiwa kazini katika kiwanda cha kutengeneza marumaru Keda (T) Ceramics Company limited, Chalinze, Mkoani Pwani.*

Pia, viwanda vya kuzalisha nondo na mabati hapa nchini vimeongezeka na kufikia kumi na nne (14) viwanda hivyo ni pamoja na ALAF Ltd, Kamal Steel Ltd (Tani 48,000 kwa mwaka), Lodhia Steel Industries Ltd, Bansal Steel Rolling, Iron and Steel Ltd, Lake Steel and Allied Products Ltd, African Dragon Enterprises, MMI Integrated Steel Mills Ltd (Tani 36,500 kwa mwaka), Kiluwa Steel Ltd, Hong Yu Steel Ltd, Metro Steel, na Sita Rolling Steel Ltd. Mwaka 2019, viwanda hivyo vilikuwa na uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,082,788 za aina mbalimbali za nondo, wakati mahitaji ya nondo nchini kwa mwaka ni tani 295,000 hivyo ziada huuzwa nje.

Viwanda vikuu viwili vinavyozalisha mabati ni ALAF na MMI Steel. Takwimu za sasa za uzalishaji kwa mujibu wa chama cha wazalishaji wa nondo zinaonesha kuwa uzalishaji wa bati kwa sasa ni tani 200,000 kwa mwaka(ambazo ni sawa na bati 14,949,703 za gauge 28.



*Bidhaa za nondo zinazozalishwa nchini Tanzania*

### 3.1.5 Uongezaji Thamani Mazao ya Kilimo

Viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo,uvuvi, misitu na madini vimeendelea kuongezeka. Viwanda 8 vya kusindika maziwa vimeongeza uwezo wa uzalishaji kutoka lita 167,620 kwa siku hadi lita 194,335 kwa siku. Vilevile, viwanda 17 vya kusindika nyama vimeongeza uwezo wa usindikaji wa nyama na kufanya idadi ya viwanda vya usindikaji wa mazao ya mifugo nchini kufikia viwanda 145. Viwanda hivyo vinajumuisha viwanda 33 vya nyama, viwanda 99 vya maziwa na viwanda 13 vya kusindika ngozi.

Pia, viwanda vitatu vya kusindika matunda na mbogamboga vimejengwa ambavyo ni Kiwanda cha Elven Agri, Sayona Fruits Limited na Dabaga. Aidha, viwanda vinne vya kusindika vyakula vya Dar Worth Company Limited kinachozalisha sembe, dona na unga wa lishe; Uniliver cha kusindika Chai; Murzah Wilmar Rice Millers cha kusindika Mpunga; na Mahashree Agroprocessing Tanzania Limited cha kufungasha mazao jamii ya kunde hususan mbaazi vimejengwa na kuongeza uwezo wa kuongeza thamani ya mazao nchini.

#### 3.1.5.1 Sekta ndogo ya Nguo na Mavazi

Sekta ya Viwanda vya Nguo kwa sasa ina viwanda 12 ikilinganishwa na kiwanda kimoja mwaka 1961. Sekta hii imeendelea kuimarika kutokana na matumizi ya teknolojia za kisasa na kuongezeka mitaji katika viwanda. Wakati wa uhuru viwanda vya nguo vilikuwa vikitumia teknolojia ya mkono (handloom) kutengeneza nguo wakati sasa sekta hii hutumia teknolojia ya kisasa ya computer. Kwa upande wa bidhaa zinazozalishwa, viwanda vya nguo na mavazi hivi sasa vinazalisha bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na mavazi ya T-shirts, polo shirt, suruali za jeans, nguo za michezo, vyandarua, mablanketi, vitambaa vya pamba (linen), nyuzi, shuka na mavazi, ikilinganishwa na bidhaa mbili tu za khanga na vitenge zilizokuwa zikizalishwa na viwanda vya nguo kwa kutumia malighafi ya pamba pekee kwa muda mrefu tangu mwaka 1961. Viwanda vya nguo na mavazi nchini vinatoa ajira ya moja kwa moja ya jumla ya wafanyakazi 15,300.



*Uzalishaji wa nguo zinazotokana na pamba katika Kiwanda cha nguo cha A to Z cha mkoani Arusha.*

**3.1.5.2 Sekta ndogo ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi**

Uzalishaji katika sekta ya ngozi wakati wa uhuru ulikuwa mdogo. Aidha, kuanzia mwaka 2005 utekelezaji wa Mkakati Unganishi wa Kufufua na Kuendeleza Viwanda vya Ngozi Nchini umekuwa na mafanikio ambapo usindikaji wa ngozi uliongezeka kutoka futi za mraba 6,038, 000 mwaka 2005 hadi futi za mraba 37, 305, 215 mwaka 2009 kwa kiwango cha wet-blue. Mauzo ya ngozi zilizosindikwa yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 1.6 mwaka 2005 hadi shilingi bilioni 16 mwaka 2009. Aidha, baadhi ya viwanda vimeanza kusindika ngozi hadi kiwango cha kati - crust leather na cha mwisho - finished leather kwa ajili ya kutengenezea bidhaa za ngozi hapa nchini. Vile vile, ajira katika sekta ya viwanda vya ngozi na bidhaa za ngozi imeongezeka kutoka 280 mwaka 2005 hadi 520 mwaka 2009.

Serikali imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi (Leather Sector Development Strategy) ambapo hadi sasa, Tanzania ina jumla ya viwanda 9 vya kusindika ngozi. Kati ya viwanda hivyo, viwanda 5 vinafanya kazi na vina uwezo uliosimikwa wa kusindika vipande vya ngozi ya ng'ombe 2,459, 000 kwa mwaka na vipande vya ngozi ya mbuzi 7, 638,000 kwa mwaka. Viwanda vitatu (3) vinasindika hadi kufikia hatua ya kati (wet blue) na viwili (2) vinasindika hadi hatua ya mwisho (finished leather).

Vilevile, kiwanda cha kuzalisha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro International Leather Ltd kilichopo Gereza la Karanga mjini Moshi kimeongeza uzalishaji kutoka jozi 150 hadi jozi 400 za viatu kwa siku. Aidha, kiwanda cha viatu cha BORA kilichobinafsishwa kimefufuliwa na kuanza uzalishaji wa bidhaa za ngozi; na viwanda vingine vidogo kama vile Woiso Shoes na Ital Shoe Ltd. kwa pamoja vimeongeza uwezo wa viwanda vya ndani wa uzalishaji wa viatu vya ngozi kufikia takriban jozi 1,200,000 kwa mwaka.



*Mfanyakazi akishona kiatu katika Kiwanda cha Kilimanjaro International Leather Industries kinachojihusisha na uzalishaji wa bidhaa za ngozi, Kilimanjaro.*

**3.1.5.3 Viwanda vya Kubangua Korosho**

Tanzania hivi sasa ina jumla ya viwanda 33 vya kubangua korosho ilkilinganishwa na viwanda 12 vilivyokuwepo miaka ya 1980s. Viwanda 15 kati ya hivyo ni vikubwa, viwanda 12 ni vya kati na viwanda 6 ni vidogo. Viwanda vyote vina uwezo uliosimikwa (Installed Capacity) wa kubangua tani 96,982 za korosho kwa mwaka. Viwanda vya korosho vinatoa ajira za moja kwa moja zaidi ya 18,015. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa ifikapo msimu wa 2024/2025, asilimia 60 ya korosho ghafi zinazozalishwa zinabanguliwa hapa nchini.

**3.1.5.4 Viwanda vya Mafuta ya Kula**

Mafuta ya kula ni moja ya bidhaa zinazoagizwa kwa wingi kutoka nje ya nchi ambapo huigharimu nchi fedha nyingi za kigeni. Kwa sasa kuna viwanda 21 vya kati na vikubwa vyenye uwezo wa uzalishaji uliosimikwa wa tani 764,000 na viwanda vidogo vipatavyo 750. Aidha, uzalishaji wa mafuta ya kula kwa sasa ni tani 200,000 wakati mahitaji yanakadiriwa kuwa tani 700,000 kwa mwaka. Hivyo, asilimia 70 ya mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni mafuta ya mawese (palm oil) yanayoagizwa kutoka nje ya nchi.
Hata hivyo, Serikali imechukua hatua za kukabiliana na upungufu wa mafuta ya kula nchini unaotokana na uzalishaji mdogo wa mbegu za mafuta ya kula zinazohitajika kama malighafi kwenye viwanda vya kuzalisha mafuta ya kula. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa zao la michikichi kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya mawese; na kuongeza uzalishaji wa mbegu za mafuta kama vile alizeti, ufuta, pamba na karanga.

**3.1.5.5 Viwanda vya Sukari**

Tanzania hivi sasa ina jumla ya viwanda vikubwa vitano vya sukari ikilinganishwa na viwili pekee vya Kilombero Sugar Co. Ltd na Mtibwa Sugar Estate vilivyokuwepo miaka ya 1960s ambapo uzalishaji wa sukari ulikuwa chini ya tani 50,000 ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 359,219.25 hivi sasa. Viwanda vikubwa vya sukari nchini ni Kilombero Sugar - I, Kilombero Sugar – II, Mtibwa Sugar Ltd vilivyopo mkoa wa Morogoro. Vingine ni Kagera Sugar Ltd kilichopo mkoa wa Kagera na TPC - Moshi kilichopo mkoa wa Kilimanjaro. Aidha, kuna kiwanda cheye ukubwa wa kati cha Manyara Sugar Co. Ltd kilichopo mkoa wa Manyara. Viwanda vya sukari nchini vina uwezo uliosimikwa (installed capacity) wa kuzalisha tani 462,863 kwa mwaka. Viwanda hivi kwa pamoja vinatoa ajira za moja kwa moja zinazofikia wafanyakazi 20,000.

Viwanda vya sukari hivi sasa vimeongeza tija katika uzalishaji ikilinganishwa na miaka ya 1960s, tija hizo ni pamoja na kuanza kutumia mabaki ya shughuli za uzalishaji kuzalisha nishati ya umeme unaotumika katika kuendeshea mitambo yake (Kilombero, TPC, na Kagera Sugar). Vilevile, baadhi ya viwanda kama Kilombero Sugar vimeanza uzalishaji wa ethanoli ili kukidhi mahitaji ya ndani na yale ya Afrika Mashariki.

### 3.1.5.6 Viwanda vya Kuunganisha Matrekta na Magari

i)Mradi wa kuunganisha matrekta aina ya URSUS
Ujenzi wa kiwanda kipya cha kuunganisha matrekta katika eneo la TAMCO Kibaha umekamilika. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya matrekta 822 yalikuwa yamepokelewa kutoka nchini Poland na kuunganishwa. Kati ya hayo, matrekta 724, majembe ya kulimia 511 na majembe ya kusawazisha 233 yalikuwa yameuzwa katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, kutokana na mradi huo, Taasisi za CAMARTEC, TEMDO na Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools (KMTC) zimeshirikiana katika usanifu na utengenezaji wa trela kwa ajili ya trekta hizo.

ii) Viwanda vya Kuunganisha Magari na Pikipiki
Katika eneo la Viwanda la TAMCO Kibaha kiwanda cha GFA kimeanza kuunganisha malori. Pia, jijini Dar es Salaam kiwanda cha Superdoll kinaunda matrela na kuna waunganishaji wa pikipiki watatu.

iii) Kiwanda cha kutengeneza betri za magari
Kiwanda cha kutengeneza betri za magari cha kampuni ya China Boda kimeanza uzalishaji kwenye Eneo la Viwanda la TAMCO Kibaha. Pia, kampuni ya TATA Africa Holding Limited inaendelea na ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha magari.

3.1.5.7. Viwanda vya Dawa za Binadamu na Vifaa Tiba
Kutoka kiwanda kimoja cha dawa cha Mansoor Daya Chemicals Ltd kilichoanzishwa mwaka 1962 kikiwa kinatengeneza aina nne za dawa (asprin tablets, chloroquine tablets; aspirin phenacetin caffeine compound and Vitamin B complex tablets), viwanda 15 vya Dawa na Vifaa Tiba vimejengwa. Ambapo viwanda 12 vinatengeneza dawa za binadamu, viwanda 2 dawa za mifugo na kiwanda 1 kinatengeneza vifaa tiba. Kampuni za Kairuki Pharmaceutical Industries Ltd na Vista Pharmaceuticals Limited ni mojawapo ya wawekezaji wanaoendelea na ujenzi wa viwanda vya dawa na vifaa tiba.



*Mfanyakazi akishona kiatu katika Kiwanda cha Kilimanjaro International Leather Industries kinachojihusisha na uzalishaji wa bidhaa za ngozi, Kilimanjaro.*

### 3.1.5.8 Viwanda vya Vioo

Tanzania ina kiwanda kimoja kikubwa cha kutengeneza bidhaa za vioo cha Kioo Ltd. ambacho kinazalisha chupa kwa ajili ya ufungashaji wa bidhaa hususan vinywaji na dawa. Kiwanda hicho kinazalisha tani 3,000 kwa siku.

### 3.1.5.9 Viwanda vya Mbolea

Serikali imewezesha kupatikana kwa mwekezaji kwenye kiwanda cha kuzalisha mbolea cha ITRACOM Fertilizer Tanzania Limited kinachowekeza mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 180 na kitaajiri wafanyakazi wa kudumu takriban 3,000 na kitakuwa na uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mbolea tani 500,000 kwa mwaka.

3.1.5.10 Viwanda vya Kutengeneza Chokaa
Kwa muda mrefu Tanzania haikuwa na kiwanda kikubwa cha chokaa ambapo kwa sasa kiwanda kikubwa cha Neelkanth Lime Ltd kilichopo katika eneo la Amboni mkoani Tanga kinazalisha tani 200,000 za chokaa kwa mwaka. Viwanda vingine vya chokaa ni ARM (T) Ltd ambacho kina uwezo wa kuzalisha tani 18,000 kwa mwaka na Simba Lime Factory Ltd chenye uwezo wa kuzalisha tani 40 kwa mwaka.



*Uzalishaji wa Chokaa katika Kiwanda cha Neelkanth Lime Ltd kilichopo katika eneo la Amboni mkoani Tanga*

### 3.1.6 Jitihada za Serikali katika Vita Dhidi ya COVID-19

Serikali ilihamsisha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za kujikinga na COVID-19 ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa ethanol inayotumika kama malighafi ya kutengeneza vitakasa mikono. Viwanda 40 vilisajiliwa kwa ajili ya kutengeneza vitakasa mikono. Aidha, viwanda 12 vilijihusisha na utengenezaji wa vifaa vingine vya kujikinga na ugonjwa huo kama vile barakoa na mavazi maalum ya kujikinga.

### 3.1.7 Utafiti na Maendeleo ya Viwanda i)Ubora wa Makaa ya Mawe

i)Ubora wa Makaa ya Mawe

Shirika la Utafiti wa Viwanda (TIRDO) limejenga maabara ya kisasa ya kupima ubora wa makaa ya mawe yanayozalishwa nchini. Upimaji huo umewezesha makaa ya mawe yanayozalishwa nchini kutumika kama nishati kwenye viwanda vya saruji na viwanda vingine; baada ya Maabara hiyo kuthibitisha ubora wa makaa hayo. Hii ilisaidia katika kufikia uamuzi wa kuzuia uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi.

ii) Upimaji mabaki ya sumu katika bidhaa za vyakula

Serikali pia imeiwezesha TIRDO kuboresha maabara ya chakula kwa kuongeza vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuhudumia viwanda vya kusindika vyakula nchini. Maabara hiyo ina uwezo wa kupima mabaki ya sumu, homoni na madini katika bidhaa kama asali, samaki, nyama, maziwa na maji. Hii imesaidia wasindikaji wa vyakula kupunguza gharama za kufanya biashara na kuwaongezea ushindani katika kuuza bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

iii) Uchunguzi wa Madini ya Chuma cha Liganga

Shirika la Utafiti wa Viwanda (TIRDO) lilifanya uhakiki wa viwango vya madini vilivyopo katika mgodi wa chuma ghafi Liganga kwa lengo la kujiridhisha kuhusu uwepo wa madini ya aina mbalimbali na viwango vyake ili kuhakikisha kwamba Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali zake. Uhakiki ulibaini viwango vya madini vilivyomo kwenye sampuli za chuma ghafi zilizopimwa ni asilimia 70.39 chuma ($Fe_2O_3$), asilimia 12.94 Titanium ($TiO_2$), asilimia 0.52 vanadium ($V_2O_5$) na asilimia 8.63 aluminium ($Al_2O_3$). Taarifa ya Upembuzi Yakinifu uliofanywa na mwekezaji ilionesha viwango vya asilimia 56 chuma ambavyo ni pungufu kwa zaidi ya asilimia 14 ikilinganishwa na matokeo ya vipimo vya TIRDO. Aidha, viwango vya vanadium vilikuwa asilimia 0.6 na titanium asilimia 10 ikiwa ni upungufu wa asilimia 2.94 wakati madini ya aluminium hayakuwa yameripotiwa na mwekezaji kwenye taarifa yake ya upembuzi yakinifu.

**3.1.8 Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati a) Mradi wa Magadi-Soda**

Utekelezaji wa mradi huu wa kimkakati utawezesha upatikanaji wa malighafi za viwanda vingine kama vile viwanda vya kutengeneza vioo na sabuni. Shirika la TIRDO limekamilisha upembuzi yakinifu (Techno-economic Study) na kubaini kuwa, mradi wa Magadi Soda Engaruka unatekelezeka kiufundi, ni endelevu kimazingira na una manufaa makubwa kiuchumi na kibiashara. Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta mwekezaji wa kutekeleza mradi kwa kutangaza zabuni.



*Mradi wa magadi soda katika bonde la engaruka mkoa wa Arusha.*

**3.1.9 Kiwanda cha Mashine na Vipuri (KMTC)**

Katika kipindi cha Serikali ya awamu ya sita, fedha kiasi cha shilingi milioni 760 zilitolewa kwa ajili ya kuboresha mtambo wa kuchemsha chuma (Galvanizing Plant). Ujenzi umeshaanza ukihusisha ukarabati wa mashine zitakazotumika kuandaa vyuma kwa ajili ya utengenezaji wa minara na ujenzi wa Galvanizing plant. Ujenzi wa galvanizing plant umefikia 95% ambapo matanki matano (5) yameshatengenezwa na kusimikwa. Kemikali kwa ajili ya kiwanda zinatarajiwa kuagizwa kabla ya 31 Oktoba 2021. Ujenzi wa mtambo huu unategemewa kukamilika mwezi Novemba 2021 na kuanza uzalishaji wa minara na vipuri vya TANESCO. NDC ilifanya mazungumzo na TANESCO na kuingia nayo mkataba wa awali (MOU) wa kuzalisha minara ya kuunganisha mradi wa umeme wa J.K. Nyerere hadi Chalinze. Mtambo huo unatarajiwa kuzalisha bidhaa zingine ikiwepo minara ya mawasiliano, vifaa vya ujenzi, usambaaji wa maji na kilimo.

Pia Serikali ya awamu ya sita imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.685 katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya ujenzi wa Tanuru la kuyeyusha Chuma (Foundry Plant) utakaofanyika kwa awamu mbili fedha hizi zikiwa ni za awamu ya kwanza.

Upatikanaji wa tanuru la kuyeyushia chuma (Foundry Plant) katika kiwanda hiki, utasaidia kuzalisha vyuma (castings) vikiwa kama malighafi ya kutengeneza vipuri kwa matumizi viwandani. Shirika limefanya utafiti (survey) kwa kutumia takwimu toka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kubaini mahitaji makubwa ya vipuri nchini ambapo katika kipindi cha miaka minne (2016 – 2019), Tanzania ilitumia jumla ya shilingi trilioni 10 kuagiza vipuri kwa ajili ya matumizi katika sekta mbalimbali zikiwemo; Viwanda, Nishati, Kilimo, Madini, Maji, Usafirishaji, Ujenzi, Misitu, n.k.

Kiwanda kimeendelea kuzalisha mashine za mbao, vipuri na zana mbalimbali kwa ajili ya viwanda vya kuchenjua madini, saruji, kemikali na kilimo. Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali ili kuhakikisha kiwanda hiki kinaboreshwa ili kiweze kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya viwanda nchini na kuinua maisha ya wananchi na kutoa ajira zaidi. Kiwanda cha KMTC kinategemewa kuwa ni kiwanda ambacho kitatumika katika mnyororo wa kuongeza thamani (downstream processing) ya chuma kitakachozalishwa Liganga.

**3.2 Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati (SMEs)**

Jasiriamali Ndogo na za Kati (SMEs) zimeendelea kuchukua nafasi muhimu katika uchumi wa nchi. Wizara ya Viwanda na Biashara imeendelea kuhudumia, kuratibu na kusimamia shughuli za Jasiriamali Ndogo na za Kati nchini. Lengo kuu la Serikali katika kuwahudumia Wajasiriamali Wadogo na wa Kati ni kuhakikisha ukuaji endelevu na uhitimu wa Wajasiriamali hao kutoka hatua moja kwenda nyingine ili kukuza upatikanaji wa fursa za ajira na kipato kwa wananchi na kuongeza mchango wao katika Pato la Taifa.

Idadi ya jasiriamali ndogo na za kati nchini imeongezeka kutoka milioni 1.7 mwaka 2012 hadi kufikia milioni 4.5 mwaka 2021. Vilevile, ajira zitokanazo na shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati zimeongezeka kutoka milioni 5.2 mwaka 2012 hadi milioni 8 mwaka 2021. Mchango wa jasiriamali ndogo na za kati katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 27 mwaka 2012 hadi asilimia 35 mwaka 2021.

**3.2.1 Kuwezesha Upatikanaji wa Mitaji kwa Wajasiriamali Wadogo**

Moja ya changamoto kubwa zinazowakabili Wajasiriamali wadogo na wa kati ni upatikanaji wa mitaji. Serikali imeanzisha mifuko ya uwezeshaji wajasiriamali kama vile Mfuko wa Kuendeleza Wafanyabiashara (National Entrepreneurship Development Fund - NEDF) chini ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) ambao umewawezesha wajasiriamali kupata mikopo nafuu kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi ya uzalishaji mali. Tangu mfuko wa NEDF ulipoanzishwa mwaka 1994 Serikali imechangia kiasi cha Sh. Bilioni 6.6 kwenye mtaji wa mfuko huo. Katika kipindi hicho maombi 234,887 ya mikopo yenye thamani ya Sh. 205,464,663,000.00 yalipokelewa. Kati ya maombi hayo, maombi 96,335 yenye thamani ya Sh. 82,636,982,000.00 sawa na asilimia 41.02 yaliidhinishwa na kupatiwa mikopo.

Aidha, ajira 199,768 zilipatikana kutokana na mikopo iliyoidhinishwa na kutolewa, ambapo mikopo 50,033 sawa na asilimia 51.9 yenye thamani ya Sh. 38,282,731.00 ilitolewa kwenye miradi ya wanawake; na mikopo 1,475 sawa na asilimia 1.5 yenye thamani ya Sh. 2,483,089 ilitolewa kwenye miradi ya ubia kati ya wanawake na wanaume. Pia, mikopo 34,081 yenye thamani ya Sh. 26,469,688 sawa na asilimia 35.4 iliyotolewa vijijini; na mikopo 62,254 yenye thamani ya Sh. 56,167,294.00 sawa na asilimia 64.6 ilitolewa mijini.

Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) linasimamia Mfuko wa Dhamana kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SME Credit Guarantee Scheme) uliozinduliwa mwaka 2015 kwa ushirikiano na Benki ya CRDB. Tangu kuanzishwa kwake hadi mwezi machi 2021, maombi 238 ya mikopo yenye thamani ya Sh. 8,491,000,000.00 iliwasilishwa CRDB; ambapo maombi 54 yaliidhinishwa na kupata mikopo yenye thamani ya Sh. 1,743,000,000.00.

Vilevile, SIDO kwa kushirikiana na Azania Bank, NEEC, NSSF na VETA imeanzisha mfuko kwa ajili ya kutoa mikopo ya uendelezaji viwanda vidogo na vya kati ujulikanao kama SANNV. Tangu Program ya SANNV Viwanda Scheme ilipozinduliwa mwaka 2020 kwa mtaji wa Sh. Bilioni 5 imetoa mikopo 28 yenye thamni ya Sh. Bilioni 1.6.

**3.2.2 Ujenzi na Ukarabati wa Majengo Viwanda Pamoja na Ofisi za SIDO**

Serikali imejenga majengo viwanda (industrial sheds) 473 kwenye maeneo mbalimbali nchini kote kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wazalishaji viwandani. Majengo hayo yametoa fursa za kuanzisha viwanda 523 vilivyotoa ajira 5,297.



*Majengo Viwanda (industrial sheds) yaliyopo Wilaya ya Chato Mkoa wa Geita*

**3.2.3 Mwongozo wa Kusimamia Ujenzi wa Viwanda**

Wizara imeandaa na kuchapisha Mwongozo wa Kusimamia Ujenzi na Maendeleo ya Viwanda kwa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Mwongozo huo ulizinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa tarehe 04 Julai, 2018 katika viwanja vya Maonesho ya Biashara ya Kimataifa vya Sabasaba. Lengo la Mwongozo huo ni kujenga uelewa wa pamoja kwa watendaji wa mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mwongozo pia utatoa maelekezo kwa watendaji, ili kurahisha usimamizi, utekelezaji na uendelezaji wa ujenzi wa viwanda. Hatua hiyo itasaidia na kuharakisha mafanikio ya ujenzi wa viwanda ambao ni endelevu na jumuishi. Pia, Mwongozo huo umeainisha wadau muhimu katika ujenzi wa viwanda ambao Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitapaswa kushirikiana nao ili kuharakisha maendeleo ya viwanda nchini. Wizara inaendelea kusambaza na kuhamasisha utekelezaji wa mwongozo huo nchini kote.

**3.2.4 Upatikanaji wa Teknolojia na Ubunifu**

Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) limeanzisha Vituo saba (7) vya Kuendeleza Teknolojia (Technology Development Centers -TDCs) katika mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Lindi na Shinyanga. Aidha, Serikali imetoa shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kununua mitambo kwa lengo la kuboresha Vituo vya Kuendeleza Teknolojia (TDCs) kwenye Mikoa ya Lindi, Shinyanga na Kigoma. Vituo hivyo vinazalisha teknolojia zinazorahisisha na kuendeleza shughuli za wajasiriamali za kuchakata mazao, kulima, kupanda na kuvuna. Teknolojia hizo zimewezesha miradi 7,651 na kuanzisha viwanda vipya 4,513 na kuongeza fursa za ajira 19,873 chini ya mkakati wa “Wilaya Moja, Zao Moja – ODOP”.

Teknolojia hizo zinahawilishwa kwa Wajasiriamali kupitia mafunzo katika maeneo ya ubanguaji wa korosho, usindikaji wa mihogo na ukamuaji wa mafuta ya mawese, usindikaji wa vyakula, upunguzaji wa matumizi ya kuni kama nishati, ufungashaji wa vyakula vilivyosindikwa, ufyatuaji matofali, utengenezaji wa chokaa na chaki, ukamuaji mafuta ya kula kutokana na michikichi, utengenezaji wa sabuni na usindikaji ngozi kwa kutumia njia za asili.

### 3.2.5 Masoko ya Bidhaa za Viwanda vodogo

Masoko ni msingi mkubwa wa kufanya shughuli za uzalishaji kuwa endelevu. Katika kipindi husika, Wizara kwa kushirikiana na SIDO iliandaa maonesho ya bidhaa za wajasiriamali wadogo ya kikanda na yale ya kitaifa. Maonesho ya kikanda yalifanyika katika kanda zifuatazo:Kanda ya Kaskazini (walifanyia Dodoma), Kanda ya Ziwa (Jijini Mwanza), Kanda ya Kati (mjini Tabora na Kasulu - Kigoma) na Kanda Nyanda za Juu Kusini (Jijini Mbeya na Iringa) na Kanda ya Kusini Mashariki (Morogoro na Lindi).

Aidha, katika kipindi husika, Wizara kwa kushirikiana na SIDO iliandaa maonesho makubwa ya kitaifa yaliyofanyika Simiyu (mwaka 2018) na Singida (mwaka 2019). Maonesho haya ya kitaifa kwa pamoja yalishirikisha wajasiriamali 1,063 (wanawake 961 na wanaume 372) ambao waliweza kuonesha bidhaa na huduma mbalimbali wanazotengeneza/toa na hivyo kuwezesha kufanyika kwa mauzo ya pesa taslimu Sh. 439 milioni na miadi mbalimbali yenye thamani ya Sh.1.023 bilioni. Kwa mwaka 2021, Maonesho ya SIDO Kitaifa yamefanyika Wilayani Kasulu Mkoani Kigoma na Kuwashirikisha wajasiriamali zaidi ya 710 kutoka nchini kote.

### 3.2.6 Ushauri wa Kiufundi kwa Wajasiriamali

SIDO imeendelea kutoa ushauri wa kiufundi kwa wajasiriamali katika maeneo ya udhibiti wa ubora wa bidhaa, ufungaji wa mashine, ukarabati wa mashine, michoro ya majengo ya viwanda, upangaji wa mashine viwandani na uchaguzi wa teknolojia sahihi. Aidha, Wajasiriamali wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya biashara mpya wameendelezwa kupitia programu ya kiatamizi (incubation program) kwa kupatiwa huduma mbalimbali kama vile maeneo ya kufanyia kazi, ushauri wa kiufundi na mitaji ili wakue na kufikia viwango vya kujitegemea. Miongoni mwa teknolojia zilizopata huduma hiyo zilihusu utengenezaji wa sabuni, uyeyushaji wa vyuma ili kupata vipuri vya aina mbalimbali, usindikaji vyakula, uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi na utengenezaji wa zana za kilimo.

## 3.3 Maendeleo ya Mtangamano wa Biashara

### 3.3.1 Fursa za masoko (Nchi na nchi, Kikanda na Kimataifa)

Wizara imefanikiwa kushiriki kikamilifu katika majadiliano mbalimbali ya biashara baina ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kuongeza fursa zaidi za biashara ya bidhaa na huduma kutoka Tanzania hii ikijumuisha kupata masoko yenye masharti nafuu kwa ajili ya wafanyabiashara wa Tanzania.

### 3.3.2 Masoko baina ya Nchi na Nchi

Kupitia majadiliano baina ya nchi na nchi (Bilateral Trade Negotiations) kumewesha kupatikana kwa fursa nafuu za biashara kati ya Tanzania na baadhi ya nchi ambazo ni masoko ya kimkakati ikiwemo nchi ya China ambapo Tanzania ina fursa ya kuuza bidhaa zake zaidi ya elfu nne (4,000) bila ushuru wala ukomo yaani Duty Free Quota Free Markeyt Access (DFQF). Pia kumewezesha kupatikana kwa fursa nafuu za biashara kimataifa hususan kwenye masoko ya nchi zilizoendelea ikiwemo kupitia Mpango Maalum kwa nchi za Afrika kuuza bidhaa zaidi ya elfu sita mia nne (6,400) nchini Marekani (AGOA).

### 3.3.3 Masoko ya Kikanda

Kupatikana kwa fursa nafuu za biashara kwa bidhaa na huduma zaidi ya elfu nane (8,000) kuuzwa kwenye masoko ya kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC); Kuridhia Mkataba wa kujiunga na Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA). Tanzania kujiunga na Mkataba huu inakuwa sehemu ya soko kubwa barani Afrika lenye takribani ya watu Bilioni 1.3 na pato ghafi la jumla ya kiasi cha Trioni 3.4. Ni kupitia mkataba huu Tanzania itanufaika kwa kuuza bidhaa na huduma na hivyo kupanua wigo wa kibiashara na ajira kwa wafanyabiashara Watanzania.

Aidha, kupitia majadiliano ya kibiashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)- Nchi za EAC tayari zimeondoleana ushuru wa forodha kwa asilimia 100 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)-Viwango vya ushuru kwa bidhaa zaidi ya asilimia 98% toka nchi wanachama wa SADC tayari pia vimeishapunguzwa hadi kufikia asilimia sifuri isipokuwa kwa baadhi ya bidhaa chache kutokana na sababu maalum ndani ya nchi husika (exclusive /sensitive list products).

### 3.3.4 Masoko ya Kimataifa

Kuwa mwanachama wa Shirika la Biashara la Dunia (WTO) kumeifanya Tanzania kupata masoko zaidi kwa bidhaa na huduma zake kwa kutetea maeneo yake ya kipaumbele kupitia makundi ya nchi zenye sura ya maslahi yanayofanana na Tanzania kama vile G33, G77, OACPs, na LDCs. Pia kumeiwezesha Tanzania kupata fursa ya kuuza kila kitu isipokuwa silaha katika nchi za Umoja wa Ulaya (Everything But Arms- EBA).

Aidha, Kuptia majadiliano ya Kimataifa, Tanzania imeweza kunufaika katika maeneo mbalimbali kama vile kujenga uwezo wa Chuo Cha Utalii (National Insitute of Tourism-NIT) ili kukuza sekta ya utalii na kuhakikisha inazidi kuchangia katika pato la Taifa ambapo kwa sasa ndio miongoni mwa Sekta za Huduma zinazoongozwa kwa pato la Taifa. Pia kumewezesha Tanzania kujenga maabara ya kisasa ya upimaji viwango katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika bidhaa ziingiazo nchini kwa ajili ya usalama wa afya za Watanzania.

Vilevile, Tanzania imeweza kuanzisha mfumo wa utoaji taarifa za biashara kwa njia ya mtandao ili kuwarahisishia wafanyabiashara kupata taarifa muhimu na kufanya maamuzi yenye tija (informed decision) katika biashara. Mfumo huo unahusisha taarifa za kuingiza bidhaa nchini na kuuza bidhaa nje ya nchi (Trade Information Portal). Mfumo huo unapatikana kupitia link hii https://trade.tanzania.go.tz/.

Ni kupitia pia majadiliano ya Kimataifa pamoja na uridhiwaji wa baadhi ya Mikataba katika Mashirika ya Kimataifa kama vile WTO ambapo Tanzania ni mwanachama, imeweza kuanzisha kamati za Kitaifa za Kuwezesha biashara (Trade Facilitation Committees) ambazo zinajukumu la kutatua vikwazo vya kibiashara baina ya Tanzania na nchi rafiki lakini pia kutetea wafanyabiashara watanzania katika kufikia masoko ya nje. Kamati hizo pia zinajukumu la kufuatilia na kushauri juu ya masuala ya kiufundi kama vile miundombinu yanayohitajika kwa ajili ya kuwezesha biashara.

Katika maendeleo ya mauzo nje ya nchi kwa ujumla kwa kipindi cha miaka 60, kunaongezeka kutoka dola za Marekani takriban milioni 800 mwaka 1961 hadi kufikia Dola za Marekani 6,371.7 milioni mwaka 2021. Hii ni sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 12.

**3.4 Maendeleo ya Biashara**
Sekta ya Biashara nchini imeendelea kuimarika zaidi tangu tulipopata uhuru mwaka 1961. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuimarisha sekta ya biashara ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa imehodhiwa na tabaka la wafanyabiashara wa kigeni. Hatua hizo ni pamoja na kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara (State Trading Corporation – STC) kwa ajili ya kuratibu sekta ya biashara nchini. Serikali pia ilianzisha Bodi ya Biashara za Ndani (Board of Internal Trade – BIT) na Kampuni sita za uingizaji bidhaa nchini chini ya BIT ambazo ni AISCO, BHESCO, NAPCO, DABCO, HOSCO na GEFCO; pamoja na Kampuni za Biashara za Mikoa (Regional Trading Companies – RTCs). Aidha, Serikali ilianzisha kampuni ya General Agricultural Products Exports Corporation (GAPEX) kwa ajili ya kusimamia uuzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi.

**3.4.1 Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara Nchini**
Serikali imeendelea na jitihada za kuweka mazingira wezeshi ya biashara kwa kutunga na kutekeleza Sera, Sheria, Programu na Mikakati mbalimbali kwa lengo kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma na kujenga uchumi unaostahimili ushindani.

katika masoko ya ndani na nje. Hatua zilizochukuliwa na Serikali kuboresha mazingira ya biashara, kuwezesha uwekezaji na kukuza ushindani wa Sekta Binafsi ni pamoja na hizi zifuatazo:

**3.4.1.1 Maboresho ya Mfumo wa Tozo, Kodi na Ada**
Serikali iliandaa na inaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara nchini (Blueprint for Regulatory Reforms to Improve Business Environment). Mpango huo umewezesha maboresho ya tozo 233 ambapo kati ya tozo hizo, tozo 163 zimefutwa na tozo 70 viwango vilivyokuwa vinatozwa vimepunguzwa. Kati ya tozo zilizofutwa, 114 ni za Sekta ya Kilimo na Mifugo, 5 za OSHA, 44 za TBS, GCLA, Utalii, Maji, Uvuvi na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa-TFDA.

Utekelezaji wa Blueprint pia umewezesha kuondoa mwingiliano wa majukumu miongoni mwa Taasisi za Serikali zinazotoa huduma mbalimbali kwa wafanyabiashara na wawekezaji. Mojawapo ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuhamisha jukumu la usimamizi wa masuala ya ubora wa chakula kutoka iliyokuwa TFDA kwenda TBS, ili kuwapunguzia wafanyabiashara usumbufu wa kukaguliwa na Taasisi mbili tofauti.

Aidha, hivi karibuni Serikali imechukua hatua ya kuhamisha jukumu la ukaguzi wa viwanda (industrial inspection) kutoka Wakala wa Vipimo (WMA) ambapo sasa jukumu hilo litatekelezwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Hatua hiyo itawapunguzia wenye viwanda kero ya muda mrefu na usumbufu wa kukaguliwa na Taasisi mbili tofauti za Serikali. Maboresho hayo yamesaidia kuondoa urasimu na kupunguza gharama za kufanya biashara kwa wenye viwanda, wafanyabiashara na wawekezaji.

**3.4.1.2 Uendelezaji wa Masoko ya Kimkakati na Biashara Mipakani**
Serikali imejenga Vituo 9 vya Utoaji wa Huduma kwa Pamoja Mipakani (One Stop Border Posts - OSBP) ili kurahisisha shughuli za Taasisi za usimamizi mipakani na kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao. Utekelezaji wa dhana ya OSBP imepunguza kwa kiasi kikubwa gharama na muda wa kupitisha shehena mipakani pamoja na kuimarisha biashara kwenye masoko ya mipakani. Mfumo huo unaotumia utaratibu wa Kituo Kimoja cha Utoaji Huduma za Serikali (One Stop Service Center) umewezesha ufanisi katika usimamizi wa taratibu za forodha na uhamiaji ikiwa ni pamoja na magari na bidhaa kukaguliwa mara moja wakati wa kuingia au kutoka katika mpaka husika badala ya utaratibu wa awali ambapo kila nchi ilikuwa inafanya ukaguzi upande wake wa mpaka.

Vituo hivyo ni pamoja na Holili/Taveta (Tanzania na Kenya), Sirari/Isebania (Tanzania na Kenya), Namanga-/Namanga (Tanzania na Kenya), Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi), Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda), Mtukula/Mtukula (Tanzania na Uganda), Horohoro/Lungalunga (Tanzania na Kenya), Tunduma/Nakonde (Tanzania na Zambia) na Kasumulu/Songwe (Tanzania/Malawi). Taasisi za Umma zilizopo mipakani ni pamoja na Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Polisi Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Vipimo, Shirika la Viwango Tanzania, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Madawa na Vifaa Tiba (TMDA), na Wizara ya Kilimo Kitengo cha Usalama wa Mimea na Vipando.

Vilevile, Taratibu za udhibiti bandarini na katika vituo vya mipakani zimerahisishwa kwa kuzifanya taasisi za udhibiti kama vile, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Wakala wa Vipimo, Wakaguzi wa mimea na mifugo kufanya kazi kwa utaratibu wa Kituo Kimoja cha Utoaji wa Huduma (One Stop Centre). Hii imerahisisha utoaji wa huduma za udhibiti na uondoshaji wa mizigo katika bandari na vituo vya mipakani.

**3.4.1.3 Kuanzishwa kwa Duka Mtandao (E-shop)**
Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Posta imeanzisha

duka mtandao (Posta e Shop) kwa lengo la kupanua fursa za masoko kwa wazalishaji wa bidhaa nchini. Duka hilo lilizinduliwa katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara (DITF) ya mwaka 2021 na hadi sasa lina wafanyabiashara zaidi ya 300 waliosajiliwa. Aidha, elimu zaidi inatolewa ili kuwawezesha wafanyabiashara wengi zaidi nchini kutumia fursa hiyo ya duka mtandao.

**3.4.1.4 Kuboresha na Kupanua Wigo wa Biashara Mtandao**

Wizara inazingatia matumizi ya TEHAMA katika kupokea, kutunza, na kusambaza taarifa mbalimbali zinazohusu masuala ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa taarifa muhimu kwa wadau na kwa wakati. Sekta. Wizara inatumia mtandao wa intaneti na teknolojia ya habari kusambaza taarifa ya bei za mazao ya kilimo, mifugo na vifaa vya ujenzi kama vile mabati, nondo na saruji kupitia simu za viganjani.

Serikali pia imeanzisha utaratibu wa kutoa taarifa za kibiashara kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa Tanzania National Business Portal unaosimamiwa na BRELA. Mfumo huo umewezesha utoaji wa leseni za biashara za Kundi A zinazotolewa na BRELA kutolewa kwa njia ya mtandao kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2019. Taratibu za kuunganisha mifumo ili kuwezesha leseni za biashara za Kundi "B" ambazo hutolewa na TAMISEMI kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutolewa kwa njia ya mtandao huo zinaendelea.

**3.4.1.5 Kuanzishwa kwa Soko la Mazao na Bidhaa Nchini**

Ili kuwa na soko la uhakika kwa mazao na bidhaa nchini, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imewezesha kuanzishwa kwa Soko la Mazao na Bidhaa Nchini (Commodity Exchange). Aidha, uanzishwaji wa soko hili unawezesha upatikanaji wa Masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.

**3.4.1.6 Uendelezaji wa Miundombinu ya Masoko**

Wizara imefanikisha ujenzi wa masoko saba (7) ya mipakani kupitia mradi wa District Agricultural Sector Investment Project (DASIP). Masoko hayo yamejengwa katika mipaka ya Sirari, Murongo, Mkenda, Kabanga, Kahama (Bandari Kavu), Manyovu, na Mtukula. Wizara pia imetekeleza Mpango Kabambe wa Kuendeleza Masoko kwa kuratibu ujenzi wa masoko ya kimataifa ya Segera na Makambako. Masoko hayo yamekabidhiwa kwa Halmashauri za Wilaya husika kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na uendeshaji wake.

**3.4.2 Udhibiti wa Ubora na Viwango vya Bidhaa ndani na nje ya Nchi**

Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara ilianzisha Taasisi ya Viwango nchini (Tanzania Institute os Standards – TIS) mwaka 1975 ambayo ilibadili jina na kujulikana kama Shirika la Viwango Tanzania (Tanzania Bureau of Standards – TBS) mwaka 1976. Maboresho ya Shirika hilo yameendelea ambapo mwaka 2009, Sheria ya uanzishwaji wa TBS iliboreshwa na kujumuisha masuala Udhibiti Ubora na Sayansi ya Ugezi. Shirika hilo ambalo pia linawakilisha nchi yetu katika majukwaa ya viwango na ubora ya Kikanda na Kimataifa limekuwa likiratibu uandaaji na uoanishaji wa viwango vya kitaifa katika sekta zote za kiuchumi.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa TBS katika kuandaa na kusimamia viwango vya bidhaa na udhibiti wa ubora wa bidhaa ni pamoja na:

i) Kuandaa viwango kwa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini na zile zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kwa lengo la kulinda afya za walaji na watumiaji wa bidhaa hizo ambapo jumla ya viwango 4,430 vimeandaliwa katika sekta za kilimo, chakula, nguo na kemikali.

ii) Kutoa leseni za ubora wa bidhaa kwa wazalishaji wa bidhaa katika viwanda ambapo leseni za ubora wa bidhaa zipatazo 1,587 zimetolewa kwa wazalishaji mbalimbali wa bidhaa hapa nchini. Leseni hizo zinawawezesha wazalishaji wetu wa Kitanzania kuyafikia masoko ya ndani na nje ya nchi, hivyo kukuza ushindani wa kibiashara, kuongeza wigo wa ajira, kupunguza umaskini na hatimaye kukuza uchumi.

iii) Shirika limetoa mafunzo ya ubora wa bidhaa katika makundi mbalimbali ya jamii ambapo watu 10,138 wamepatiwa mafunzo hayo. Aidha, Shirika limetoa vyeti 147,238 kwa waingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi;

iv) Shirika linatekeleza utaratibu wa kukagua magari yaliyotumika baada ya kufika nchini (Destination Inspection) tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo magari hayo yalikuwa yakikaguliwa huko yanakotoka kwa kutumia Mawakala (Pre-shipment Verification of Conformity – PVoC). Ukaguzi wa magari hayo hapa nchini ulianza tarehe 15 Aprili, 2021 na katika kipindi cha kuanzia tarehe 15 Aprili, 2021 hadi tarehe 30 Septemba, 2021 magari 18,537 yaliyotumika nje ya nchi yalikaguliwa na kuzalisha Shilingi 6,487,950,000 kama mapato ya Serikali ikilinganishwa na Shilingi 1,946,385,000 ambazo zingepatikana endapo ukaguzi huo ungeendelea kufanyika nje ya nchi kwa kutumia mawakala.

Tangu tarehe 17 Aprili, 2021 TBS inatekeleza jukumu la kuweka kinasaba kwenye mafuta ya petroli kwenye maghala (fuel depots) 19; jukumu lililokuwa linatekelezwa na EWURA. Lengo ni kuendelea kudhibiti ubora wa mafuta hayo na wakati huo huo kulinda mapato ya Serikali. Idadi ya maghala imeongezeka na kufikia 21 hadi kufikia tarehe 23 Septemba, 2021. Hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2021, lita 1,595,194,086 za mafuta ziliwekewa kinasaba na kuzalisha Shilingi Bilioni 22.33 kama mapato ya Serikali. Kati ya lita hizo, lita 652,207,181 ni petroli, lita 931,729,146 ni dizeli na lita 11,257,759 ni mafuta ya taa.

**3.4.3 Ukaguzi na Uhakiki Vipimo**

Wakala wa Vipimo inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo, Sura 340 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002 na Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245 kama ilivyorekebishwa mwaka 2009. Tangu kuan

zishiwa kwake, Wakala imekuwa na mafanikio katika kusimamia na kutekeleza Sheria ya Vipimo kwa kufanya uhakiki na kuidhinisha vipimo vya bidhaa ambapo jumla ya vipimo 807,719 vimehakikiwa na kuidhinishwa na Wakala kwa matumizi na Kufanya kaguzi za kushtukiza ili kubaini watuamiaji wa vipimo visivyohakikiwa na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria katika kipindi cha hivi karibuni Wakala wa Vipimo imefanikiwa kuongeza ushiriki kwenye zoezi la ununuzi wa Mazao ya Kimkakati kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na usawa baina ya Muuzaji (Mkulima) na Mnunuzi kwa ongezeko la mikoa 3 hivyo kufikia idadi ya mikoa 14 tofauti na 11 ya awali. Ongezeko hili limechangiwa na Serikali kutoa kibali cha kuajiri watumishi wa ajira za Mkataba 50 (Maafisa Vipimo) zaidi ambapo wamefikia 200 kutoka 150. Mikoa iliyoongezeka ni Singida, Geita na Katavi ambapo ya awali ilikuwa Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mwanza, Kagera, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mara na Pwani.

**3.4.4 Kukuza Ushindani na Kumlinda Mlaji wa Bidhaa na Huduma**

Ushindani na udhibiti wa uchumi wa soko ulianza miaka ya 1980 Serikali ilipofanya mabadiliko ya kisera ya kuachana na uchumi hodhi kwenda kwenye uchumi unaoendeshwa kwa nguvu za soko. Kutokana na mabadiliko hayo, yalifanyika marekebisho, uboreshaji na utungaji wa sheria mbalimbali za ushindani na udhibiti ili kwenda sambamba na mabadiliko ya uchumi yaliyotokea duniani. Katika kupitia sheria na kanuni mbalimbali, ilionekana pia ni muhimu kuifanyia marekebisho sheria ya udhibiti wa bei ya mwaka 1973 ili kuendana na mabadiliko ya mfumo wa kiuchumi wa soko huria. Chimbuko la mahitaji hayo ya mabadiliko ni kuonekana umuhimu wa sekta binafsi kuwa mhimili wa uchumi wa nchi.

Wizara iliratibu utungaji wa Sheria ya Ushindani (Fair Competition Act) ya mwaka 2003 ili kuhakikisha uwepo wa ushindani wa haki katika soko, kudhibiti vitendo hadaifu na bidhaa bandia katika soko. Sheria hiyo iliiwezesha Tume ya Ushindani (FCC) kuanza kutekeleza majukumu yake kama Taasisi mwezi Mei, 2007. Mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya FCC ni pamoja na:

Kuanzisha uchunguzi wa soko la uuzaji wa magari mapya nchini. Uchunguzi huu ulianza baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa Serikali ambayo ni mnunuzi mkubwa wa magari mapya nchini. Katika malalamiko hayo, FCC ilibaini uwezekano wa kuwepo kwa upangaji bei (price fixing) kati ya washindani pamoja na matumizi mabaya ya nguvu za soko kwa upande wa wauzaji. FCC ilibaini uwepo wa mikataba ya kipekee ya uagizaji na usambazaji wa magari mapya yenye ibara zinazofifisha na kuzuia ushindani (exclusive rights). Aidha, FCC ilitoa maamuzi ya awali (Provisional Findings) na kuwataka walalamikiwa kulipa faini kulingana na sheria pamoja na kuzuia kutumika kwa baadhi ya vifungu vinavyokiuka Sheria ya Ushindani. Katika shauri hili, FCC iliagiza kusitishwa kutumika kwa baadhi ya ibara za mikataba ya kipekee. Kusitishwa kwa ibara hizo kumeipa GPSA uwezo wa kutafuta wauzaji wengine ambao watauza kwa bei shindani.

Kukamata bidhaa bandia zenye thamani ya 3.824 bilioni zikiwemo betri za magari, betri za pikipiki na vifaa vya umeme.

**3.4.5 Uunganishaji wafanyabiashara na masoko ya ndani na nje ya nchi**

Wizara imeendelea kuratibu kwa mafanikio Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Dar es Salaam International Trade Fair) yanayofanyika mwezi Julai kila mwaka. Wizara pia imeratibu ushiriki wa Tanzania kwenye maonesho ya kibiashara ya ndani na nje ikiwa ni pamoja na Maonesho ya tatu ya Uwekezaji katika Sekta ya Madini mkoani Geita, Tamasha la Utalii na Maonesho ya Kwanza ya Biashara Mkoani Arusha na Maonesho ya Nane (8) ya Biashara na Utalii Mkoani Tanga. Tanzania pia inashiriki Maonesho ya Expo Dubai 2020 yanayofanyika Jijini Dubai tangu tarehe 01 Oktoba, 2021 ambayo yatahitimishwa mwezi Machi, 2022.

Madhumuni ya maonesho hayo ni kukuza biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani kwa kuzitangaza bidhaa za viwandani, sanaa za mikono, madini, fursa za utalii na kuvutia Wawekezaji. Vilevile, Wizara imeendelea kutafuta fursa za masoko kwa kuwaunganisha wazalishaji wa bidhaa, wasindikiaji na wafanyabiashara wa ndani na masoko ya nje ya nchi. Jitihada hizo zimewezesha kupatikana soko kwa mazao kama vile kahawa, korosho, mchele, mahindi na maharage.

Aidha, kampuni 54 zimeshiriki kwenye ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Kenya. Mojawapo ya mafanikio ya ziara hiyo ni kuwakutanisha wafanyabiashara wa Tanzania na wenzao wa Kenya pamoja na kupatikana wawekezaji kutoka nchi hiyo ambao ni Kampuni ya Hiltan Majedria - uzalishaji wa dawa, Rai Group - uzalishaji wa sukari na Bedi Investment Ltd –uzalishaji wa nguo. Pia, vikwazo zaidi ya 64 visivyo vya kikodi (NTBs) kati ya Tanzania na Kenya viliondolewa;

Jitihada nyingine za kutafuta masoko ya mazao na bidhaa nyingine ni pamoja na:

Kuratibu Kongamano la Wadau wa Alizeti, Maonesho pamoja na Mikutano ya Wafanyabiashara (B2B) kuanzia tarehe 10 – 15 Agosti, 2021 mkoani Singida ambapo jumla ya wadau 364 wa alizeti walishiriki. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na Kongamano hilo ni pamoja na kupatikana ekari 10,000 za ardhi zilizotolewa na Wilaya ya Handeni kwa ajili ya mashamba ya alizeti pamoja na shughuli za uongezaji thamani katika mnyororo wa thamani wa zao la alizeti. Wakala wa Mbegu (ASA) na kampuni ya N & N Trading Co. Ltd ziliingia mkataba kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza tani 2,000 za mbegu ya alizeti aina ya rekodi. Kutokana hatua hiyo, wasindikaji wadogo wawili (2) wameanza kusambaza mafuta ghafi kwa kampuni ya Pyxus Agriculture. Kampuni 32 zilipatiwa zana za kilimo kwa mikopo kupitia mpango wa “EFTAH

Loan Scheme ". Chini ya mpango huo unaoratibiwa na Wizara ya Kilimo, Kampuni 16 za wasindikaji wa alizeti waliingia mikataba ya kilimo cha mkataba na wakulima zaidi ya 32,000.

ii) Wizara imeshirikiana na Umoja wa Wasindika Mafuta ya Alizeti Nchini, (TASUPA) kupeleka ujumbe wa kampuni 7 zinazosindika mafuta ya alizeti nchini kwenda DRC kwa ajili ya kuangalia fursa za kibiashara kwa bidhaa zitokanazo na mbegu za alizeti, kama vile mafuta, mashudu, vipodozi, sabuni, na nta ya alizeti. Lengo ni kuongeza fursa za sekta binafsi kunufaika na soko la nchi za EAC na SADC.

Wizara imeshirikiana na Kituo cha Biashara ya Kimataifa (ITC), Umoja wa Wadau wa Viungo nchini (TASPA) chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) kuratibu zoezi la usanifu na usimamizi wa Nembo ya Taifa ya Viungo (Tanzania Spice Label) iliyozinduliwa tarehe 9 Julai 2021. Kampuni 10 zimekidhi vigezo vya kutumia Nembo hiyo ambapo wazalishaji wa Tanzania wataongeza fursa za kuuza bidhaa hizo katika soko la ndani na la kimataifa.

Katika kufanikisha uzalishaji wa bidhaa zenye ubora, Wizara imewezesha utambuzi wa bidhaa kwa kutumia nembo za mistari (bar code) ambapo sasa huduma hiyo inapatikana hapa hapa nchini na hivyo kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kupata masoko ya bidhaa zao kwa urahisi.

3.4.6 Uimarishaji Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Mabadiliko ya mfumo wa masoko tangu wakati wa uhuru uliathiri mfumo wa masoko kwa bidhaa za mazao ya kilimo hususan mazao ya biashara kama korosho, kahawa na pamba. Baada ya shughuli za kibiashara kuwekwa mikononi mwa sekta binafsi, wakulima waliyumbishwa sana na kusababisha kuuza mazao kwa bei ya chini isiyokidhi gharama za uzalishaji.

Kutokana na mazingira haya katika soko serikali ililazimika kutafuta utaratibu mbadala wa kuboresha uuzaji mazao kwa lengo kumlinda mkulima. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara ya Viwanda na Biashara ilianzisha Bodi ya Stakabadhi za Ghala chini ya Sheria ya Warehouse Receipt Act. No. 10 ya mwaka 2005 iliyoboreshwa mwaka 2016.

Sheria hiyo ilitungwa kwa lengo la kusimamia na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unaohakikisha usawa na uendelevu wa upatikanaji wa mikopo na Mfumo huo kwa sasa unatumika katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Dodoma, Kagera, Singida, Tabora na Manyara. Mazao yanayouzwa kupitia Mfumo huo ni pamoja mbaazi, dengu, soya, mpunga, ufuta, kakao, kahawa, alizeti, korosho, na mahindi. Aidha, Wizara ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika mikoa ya Kusini ya Ruvuma, Mtwara na Lindi.

Tathmini kabla na baada ya kuanzishwa kwa Taasisi hii inaonesha kuwa matumizi ya Mfumo yanaendelea kutatua changamoto ya bei na ubora wa mazao yanayouzwa ikilinganishwa na awali kabla ya utekelezaji wa Mfumo. Mafanikio mengine yaliyopatikana baada ya kuanzishwa kwa Bodi ya Stakabadhi za Ghala ni kama ifuatavyo na:-

i) Kuongezeka kwa Ukusanyaji na Mauzo ya Mazao.

Bodi imeratibu ukusanyaji wa tani 117,239.986 ikijumuisha ya choroko tani 14,407.477; kakao tani 2,628.750; kahawa tani 11,649.426 ufuta tani 81,118.815, mbaazi tani 6,432.602 na soya tani 1,002.916; mazao hayo yaliyokusanywa yalikuwa na wastani wa thamani ya Shilingi 221 Bilioni na kuingiza mapato ya Bodi ya Shilingi 175 Milioni. Mauzo ya zao la choroko yaliongezeka kutoka tani 1,130.453 msimu wa 2019/2020 hadi tani 14,407.477 msimu wa 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 1,274 kutokana na matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

ii) Kutekeleza Mfumo Maeneo Mapya.

Bodi imewezesha kuanza kutumika kwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwenye mkoa wa Songwe (Ufuta) na Morogoro (Kakao) licha ya upinzani mkubwa uliokuwa ukiletwa na wanufaika wa mifumo holela ya ununuzi wa mazao hayo katika maeneo hayo. Mkoani Songwe tani 348.850 za ufuta zenye thamani ya Shilingi Milion 772.8 ziliuzwa kupitia mfumo kwa bei ya wastani wa Shilingi 2,221.53 kwa kilo. Bei hiyo ilikuwa ya juu kuliko bei ya wastani wa Tsh 1,200.00 hadi 1,700.00 kwa kilo iliyopatikana kwa wakulima waliouza nje ya Mfumo. Mkoani Morogoro kwa mara ya kwanza wakulima waliuza kakao kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na kupata bei ya wastani wa Shilingi 4,892.50 kwa kilo. Bei hiyo ilikuwa ni ongezeko la bei la asilimia 244.6 kutoka bei ya wastani wa Shilingi 2,000.00 waliyokuwa wakipata kupitia mifumo holela.

iii) Utoaji wa Leseni kwa Waendesha Ghala
Bodi imetoa leseni 110 kwa Waendeshaji wa Ghala ikiwa ni ongezeko la ghala 56 kutoka ghala 54 zilizokuwepo. Mgawanyo wa leseni hizo kwa mazao ni korosho (33), Kahawa (7), Ufuta (40), Kakao (3), Soya (5), Mbaazi (11) na Dengu (1).

iv) Kuongeza mazao yanayotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Mazao 11 yanauzwa kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ambayo ni mbaazi, dengu, soya, mpunga, ufuta, kakao, kahawa, alizeti, korosho, choroko na mahindi; ikiwa ni ongezeko la mazao mawili (2) kulinganisha na mazao 9 ya awali. Aidha, miongozo miwili (2) mipya ambayo ni Mwongozo Namba 10 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika zao la korosho Toleo Namba 1 na Mwongozo wa biashara kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala wa mwaka 2021 kwa mazao ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu iliandaliwa na Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) .

3.4.7 Urahisishaji wa Huduma za Usajili wa Biashara na Leseni.

Ili kuwezesha shughuli za usajili wa Biashara kufanyika nchini, Wakala wa Usajili wa Leseni za Biashara (BRELA) ilianzishwa chini ya Sheria ya The Executive Agencies Act. Aidha, Sheria mbalimbali zinazotekelezwa na kusimamiwa na Wakala ni pamoja na Sheria ya Makampuni Sura ya 212, Sheria ya Majina ya Biashara Sura 213, Sheria ya Alama za Biashara na Huduma ya Mwaka 1986, Sheria ya Hataza ya Mwaka 1987 na Sheria ya Taifa ya Usajili wa Viwanda ya mwaka 1967. Vilevile, Wakala imeendelea kuzifanyia mapitio Sheria zake ili ziendane na hali ya mazingira ya biashara ya sasa.

Aidha, BRELA imewezesha utoaji wa huduma zake ikiwemo usajili wa Makampuni, Majina ya Biashara, Leseni za Viwanda, Hataza za Biashara na Alama za Biashara kwa njia ya mtandao wa Online Registration System – ORS tofauti na hapo awali ambapo Wafanyabiashara na Wawekezaji walikua wakilazimika kufika katika Ofisi za BRELA ili kupata huduma hizo. Mfumo huo unawezesha upatikanaji wa taarifa za makampuni, majina ya biashara, alama za biashara, leseni za viwanda na Hataza katika mtandao.

Serikali imefanikiwa kutekeleza mikakati ya kuweka mazingira wezeshi ya biashara nchini kwa lengo la kuvutia wawekezaji na kukuza biashara. Mafanikio kadhaa yamepatikana ikiwa ni pamoja na kuondoa ukaguzi unaofanywa na Mabwana Afya na Maafisa Mipango Miji kama sharti la kupata leseni ya biashara. Ukaguzi huo sasa unafanyika nje ya taratibu za kupata leseni za biashara ili kurahisisha taratibu na kuongeza kasi ya uanzishaji na uendeshaji wa biashara.

3.4.8 Ukusanyaji na Usambazaji wa Taarifa za Masoko
Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu mifumo ya taarifa za masoko ambayo imekuwepo kwa takriban miaka 20 sasa. Katika kipindi hicho Wizara imetoa vitendea kazi na mafunzo ya kujenga uwezo kwa wakusanya taarifa pamoja na kuboresha mifumo hiyo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Wizara inakusanya, kuchambua na kusambaza kwa wadau taarifa za mwenendo wa bei na masoko ya bidhaa. Taarifa hizo ni pamoja na bei za mazao makuu ya chakula (mahindi, mchele, mtama, uwele, ulezi, maharage, ngano na viazi mviringo) kutoka katika masoko makuu ya Mikoa. Wadau wa matumizi ya taarifa hizo ni pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu (Usalama wa Chakula), Ofisi ya Rais, Benki Kuu ya Tanzania Shirika la Chakula Duniani (WFP), NMB, Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA), Wizara ya Kilimo (Market Intelligence Unit), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, na Taasisi za Utafiti. Taarifa hizo hutangazwa kwa njia ya redio – Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), na kuchapishwa katika magazeti ya - The Gurdian na Mwananchi.
Aidha, taarifa za bei za mazao na mifugo zinazojumuisha nafaka, jamii ya kunde, mazao ya mizizi, mboga na (ng'ombe, mbuzi na kondoo), katika minada 58 katika matunda, viungo, mbegu za mafuta, bidhaa za viwandani, pembejeo na mwenendo wa biashara ya mifugo

Mikoa 26 ya Tanzania Bara zimeendelea kukusanywa, kuhifadhiwa, kuchambuliwa na kusambazwa kwa wadau nchini kupitia magazeti, radio na Tovuti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa za masoko na mwenendo wa bei.

3.4.9 Utoaji wa Elimu na Mafunzo ya Biashara
Wizara imetoa elimu na mafunzo kwa wadau wa Sekta ya Biashara ili kuwawezesha kuzalisha bidhaa zinazokidhi viwango vya kimataifa na kuwawezesha kuyafikia masoko ya ndani, kikanda na kimataifa. Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na:

i) Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imeshirikiana na OR – TAMISEMI kutoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Leseni za Biashara kwa Maafisa Biashara kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.
ii) Shirika la Viwango - TBS limeendelea na zoezi la utoaji wa wa elimu kwa umma kuhusu dhana nzima ya viwango na ubora wa bidhaa ambapo wadau wapatao 2,823 walipatiwa mafunzo ya ubora wa bidhaa nchini.

**HITIMISHO**
Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru taswira ya maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Biashara kwa ujumla inaonesha matokeo na mwelekeo chanya. Hali hii inatokana na hatua madhubuti zilizochukuliwa na Serikali kwa lengo la kufungamanisha sekta hiyo na sekta nyingine ili kufikia azma ya Serikali ya Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda. Mwenendo huo unaashiria kuwa Tanzania ni mahali sahihi na penye mazingira wezeshi na shindani yanayovutia wawekezaji wa ndani na nje. Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuchochea na kuhamasisha ukuaji wa sekta ya viwanda na biashara kwa kuweka msukumu katika kuimarisha tija kwenye sekta hiyo na sekta nyingine za uzalishaji na huduma zinazohusika moja kwa moja na ukuaji sekta ya viwanda na biashara hususan sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini.
Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mazingira ya biashara kama ajenda ya kudumu ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya utekelezaji wa Blueprint na kukuza ushindani wa sekta binafsi. Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa chagua la uwekezaji na mahali salama penye sera za biashara zinazotabirika kwa wawekezaji na wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara itaendeleza jitihada za kujenga ushirikianao mzuri na wenye tija baina ya Serikali na sekta binafsi ili kuhakikisha azma ya kuifanya sekta hiyo kuwa injini ya ukuaji endelevu na jumuishi wa uchumi linafanikiwa kwa vitendo kupitia sekta ya viwanda na biashara.
Wizara na Taasisi zake imejipanga na kujizatiti kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mipango ya Kitaifa na mipango na bajeti za kila mwaka. Katika kufikia malengo ya kiuchumi ya nchi suala la kuongeza tija katika sekta zote za uzalishaji zinazofungamana na sekta ya viwanda na biashara litapewa msukumo wa pekee ili kufikia malengo ya Tanzania tunayoitaka yenye maendeleo endelevu na jumuishi ya kiuchumi yaliyojengwa kwenye msingi imara wa viwanda.




# MAENDELEO YA SEKTA YA SHERIA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

Ndugu Wanahabari, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu kwa kuturuzuku uhai na kutujalia kukutana hapa siku ya leo, Alhamis tarehe 18 Novemba, 2021. Aidha, napenda kuishukuru tasnia ya Habari kwa mchango mkubwa ambao imeutoa na inaendelea kuutoa katika Sekta ya Sheria, hali iliyochangia katika kuimarisha amani, utulivu, mshikamano na umoja wa kitaifa tangu nchi yetu ipate uhuru. Haya yote yametuwezesha kama nchi, kupata ustawi wa kijamii, kiuchumi, kisiasa na kuwawezesha wananchi kujiletea maendeleo binafsi na Taifa kwa ujumla. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kuwaahidi ushirikiano wetu kama sekta kwenu ili nanyi pia muweze kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi na maslahi na matilaba mapana ya nchi yetu.

Ndugu Wanahabari, Desemba, 1961 yaani miaka sitini iliyopita Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa Bagamoyo alitoa tamko kuwa kwa muda wa miaka 10 tangu kupata uhuru, Tanganyika huru itafanya mambo mengi ya kuendeleza nchi yetu kuliko yote yaliyofanywa na wakoloni – wajerumani na waingereza katika miaka 75 waliokaa na kuitawala Tanganyika. Aliahidi kuwaalika tena watawala hao wa kikoloni nchi yetu itakapotimiza miaka 10 ya uhuru wake ili waje waone hatua iliyofikiwa katika kupambana na umaskini, maradhi na ujinga na kasi ya maendeleo kwa ujumla.

Mwaka 1971, miaka 10 baada ya uhuru Baba wa Taifa na Rais wa kwanza wa Tanganyika na baadaye Rais wa kwanza wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alifanya hivyo, aliwalika watawala wa Uingereza warudi tena kuiona Tanzania. Decemba, mwaka huo wa 1971, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitoa taarifa katika naafasi yake ya Rais wa TANU aliyoiita "Tanzania Miaka Kumi baada ya Uhuru" alisema:-

"… tumefanya mambo makubwa katika miaka kumi iliyopita. Tumeleta mabadiliko megi, na tumejenga sana; na sasa tumejenga msingi utakaoliwezesha Taifa letu kupiga hatua kwa haraka zaidi na kwa hakika zaidi katika siku za mbale. Kwa kweli mwezi Desemba, 1961 hatukuwa na msingi mzuri sana. Uhuru tuliosherekea mwezi ule ulikuwa wa siasa tu. Lakini ilikuwa sherehe muhimu na yenye msingi, maana kitendo kile kiliwapa wananchi wa Taifa hili haki ya kisheria kujiamulia mambo yao wao wenyewe. Bila ya haki hiyo tusingeweza kupata maendeleo yoyote, na kwa hiyo tulikuwa na haki ya kuisherekea siku ile ya Desemba, 1961. Lakini vile vile tulifanya jambo jema tulipotambua kwamba tulichopata kilikuwa haki ya kuanza kujifanyia kazi tu, basi."

Aidha, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika dibaji aliyoiandika katika kitabu kilichoandikwa mwaka 1961 na Mtanganyika Muasia, Sophia Mustafa (The Tanganyika Way: Personal Story of Tanganyika Growth to Independence" alisema:-

"We have great purposes for our independence country. We aim at building a non-racial democratic country, part of a United Africa, where every individual can start in human dignity, free from ignorance, disease and the misery of poverty. We do not have any specific against the dangers which beset our path, nor do we claim to know every detail of the way. But we believe that if we can maintain the courage ant the faith which has sustained us so far, we shall continue to overcome – or – by pass – The obstacles awaiting us on the next stage of our journey."

Hakika miaka sitini iliyopita, nchi iliyokuwa inaitwa Tanganyika ilipata Uhuru wake kutoka kwa Waingereza kupitia Baraza la Udhamini la Umoja wa Mataifa. Baraza hilo lilikuwa limeikabidhi nchi hii kwa Uingereza kuisimamia, Tanganyika ilikuwa ni Trust Territory yaani nchi ya udhamini pamoja na yale yote yaliyokuwa makoloni ya Ujerumani yaani Cameroon, Togo, Namibia na nchi iliyokuwa sehemu ya Koloni lake la Afrika Mashariki na baadaye kutenganishwa – Ruanda na Urundi.

Baraza la Umoja wa Mataifa ndilo lililotoa azimio la kuipa Tanganyika uhuru wake tarehe 28 Disemba, 1961. Hata hivyo, tarehe 28 Disemba, ilionekana ingekuwa vigumu kwa mume wa Malkia - Pince Philip kuweza kuja kwasababu ni baada ya Krismas na baada ya hapo walikuwa wanajiandaa kwa sherehe za mwaka mpya. Ndipo tena Baraza kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha Azimio jingine kubadili siku ya uhuru wa Tanganyika kutoka tarehe 28 Disemba, 1961 na kuwa tarehe 9 Disemba, 1961.

Uingereza kupitia ofisi yake ya makoloni, iliweka mifumo yake ya kisheria iliyochukua nafasi ya mifumo iliyowekwa na Wajerumani ambao waliitawala nchi hii kama koloni lao ikiwa ni pamoja na Rwanda na Burundi kama koloni moja tangu mwaka 1884 mpaka waliposhindwa katika vita kuu ya kwanza ya Dunia mwaka 1919. Uhuru huu ulitokana na juhudi mbalimbali zilizofanywa na waasisi wa Taifa letu akiwemo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mzee Rashidi Mfaume Kawawa, Mzee John Rupia, Mzee Abdul Sykes, Walid Sykes Bibi Titi Mohamed na wengine ambao walitumia kwa ufasaha mkubwa hoja ya Tamko la Haki za Binadamu la 1948 (The Universal Declaration of Human Rights) kuwa ni moja ya nguzo za kudai Uhuru wa Tanganyika na nchi nyingine ambazo zilikuwa bado ziko katika wimbi la kutawaliwa na mataifa mengine.

Katika miaka hii sitini, tuna mambo mengi ya kukukumbuka kuhusu tulikotoka, tulipo na wapi tunaelekea, kwa sasa tukiwa ni sehemu ya muungano adhimu na pekee ulio imara ambao unatokana na nchi mbili kuungana kwa hiari- yaani Jamhuri ya watu wa Tanganyika iliyopata uhuru wake mwaka 1961 na kuwa Jamhuri mwaka 1962 na Jamhuri ya watu wa Zanzibar iliyotokana na mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964 na nchi hizi mbili zikaungana tarehe 26 Aprili, 1964 na kupata Taifa moja nan chi moja - Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ni wakati wa kutafakari namna nchi yetu ilivyoweza kuondokana na taswira ya kuwa sekta ya sheria ya kufanikisha utawala wa Waingereza nchini Tanganyika, hadi kuwa sekta ya sheria inayo chochea ujenzi wa Taifa huru, linalozingatia uhuru, haki, udugu, amani na ustawi wa

wananchi.

Wakati tunaadhimisha miaka hii sitini ya Uhuru wa Tanzania Bara, wapo wenzetu wengi, ambao tulisherehekea kwa pamoja Uhuru wetu tarehe 09 Desemba, 1961, ambao wametangulia mbele ya haki. Tunawakumbuka viongozi wetu akiwemo Baba wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mzee wetu Rashidi Mfaume Kawawa, Mzee Benjamini William Mkapa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Tuwakumbuke pia watendaji na wananchi wote kwa ujumla, ambao wametangulia mbele za haki, ambao kwa pamoja na kwa namna moja ama nyingine, walichangia katika kupata Uhuru wetu, lakini pia maendeleo ambayo tumeyapata hadi sasa katika sekta yetu ya sheria na Taifa kwa ujumla.

Ndugu Wanahabari: kauli mbiu inayotuongoza katika kusherehekea miaka yetu sitini ya uhuru iliyowekwa na Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassa inasema, 'Tanzania Imara; Kazi Iendelee.'

Ndugu Wanahabari: orodha ya watumishi wa Umma mwaka 1961 inayopatikana katika idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, wakati wa Uhuru wa Tanganyika tarehe 9 Disemba, 1961, Mahakama Kuu ya Tanganyika haikuwa na Jaji yeyote Mtanganyika. Jaji Mkuu Sir Ralph Windham na majaji wengine wanne waliokuwepo, E.J.E. Law, E.B. Simmons, R.H. Murphy na L.P. Mosdell — wote walikuwa Waingereza. Masjala ya Mahakama Kuu Dar es Salaam mwaka huo wa 1961 ilikuwa chini ya Msajili wa Mahakama Kuu aliyeitwa R. McKay kutoka Scotland. Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, M.J.R. Cookley, na watumishi wote katika masjala hawakuwa Watanganyika.

Aidha, hadi Disemba 9 mwaka 1961 wakati wa uhuru, Tanganyika ilikuwa na Makimu Wakazi Waandamizi wanne wote wakiwa wazungu kutoka Uingereza. Majina ya Mahakimu hao waandamizi ni M.C.E.P. Biron (Hakimu Mwandamizi, Dar es Salaam); D.J. Williams, (Hakimu Mwandamizi, Arusha); L.D. Jefferies, (Hakimu Mwandamizi, Mwanza); na G.I. E. Reide, (Hakimu Mwandamizi, Tanga). Hata Mahakimu wakazi wengine 28, hawakuwa watanganyika. Kufikia mwaka 1965 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alimteua Jaji Mkuu wa kwanza Mweusi - Philip Telford Georges kutoka Trinidad na Tobago. Wakati wa uteuzi huu, orodha ya Watumishi ya Mwaka 1965 ilikuwa na majaji watanganyika wawili tu ambao ni Mark Peter Kimicha na Augustine Saidi ambao waliteuliwa tarehe 10 August, 1964.

Hali kadhalika, orodha ya Mawakili wa Kujitegemea ambayo inatunzwa na Chama cha wanasheria wa Tanganyika inaonesha kuwa kulikuwa na mawakili 250 ilipofika tarehe 9/12/1961 ambapo kati yao Watanganyika walikuwa wawili tu ambao ni Hamphey Noel Zgoba Mkondya mwenye namba ya usajili 246 (Roll Na. 246) na Juma Mawala mwenye namba ya usajili 249 (Roll Na. 249). Waliobaki walikuwa ni watu kutoka mataifa mengine.

Hivyo hivyo, tulipopata uhuru, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikuwa ni Mwingereza kwa jina la Roland Brown, Solicitor General pia alikuwa Mwingereza kwa jina la P.R Nines Fifoot na Mkurugenzi wa Mashtaka alikuwa Mzimbabwe kwa jina la Herbert Chitepo.

Ndugu Wanahabari: katika hali hii, Serikali ya Uhuru chini ya Baba wa Tafa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, haikuwa na njia bali kutafuta mbinu za haraka kuhakikisha kuwa sekta ya sheria inapata watumishi wazalendo wa kuchukua nafasi ya wataalamu wa Uingereza au kutoka mataifa mengine ili kuondoa taswira ya ukoloni. Waasisi wa Taifa letu walitambua kuwa Uhuru kamili wa Taifa lolote ni lazima uende sambamba na kuacha utegemezi wa wataalamu kutoka nje kuendesha wizara, taasisi na idara za Serikali. Hii ndiyo sababu, tarehe 17/5/1960 wakati wa Serikali ya Madaraka, Mwalimu Nyerere aliyekuwa Waziri Kiongozi (Chief Minister) akizungumza mbele ya Baraza la kutunga Sheria la Tanganyika alieleza wazi azma hiyo, huku akitambua kuwa pamoja na msisitizo wa Watanganyika kuchukua nafasi za wasio Watanganyika, yapo maeneo katika utumishi wa umma ambayo kuifikia azma hiyo ingechukua muda mrefu zaidi. Azma hiyo ilimsukuma Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuchukua uamuzi mzito wa kisiasa wa kuanza ufundishwaji wa Sheria nchini Tanganyika. Ndiyo maana tarehe 25 Octoba, 1961 Mwalimu Nyerere alizindua Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam ambacho kilianza na kitivo kimoja tu yaani kitivo cha sheria ambacho kilikuwa na walimu watatu na wanafunzi kumi na nne wakitumia majengo ya kukodi kwa wakati huo. Kati ya Wanafunzi hao kumi na nne, alikuwepo msichana mmoja Julie Catherine Manning ambaye mwaka 1974 alikuwa ndiyo Jaji wa kwanza mwanamke katika Mahakama Kuu ya Tanzania na mwaka 1975 akawa Waziri wa kwanza wa Sheria mwanamke.

Hali kadhalika juhudi ziliendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na kuwapeleka baadhi ya watumishi wa Watanganyika katika Chuo cha Mzumbe kusomea cheti na diploma ya sheria ili wakihitimu waweze kuajiriwa katika sehemu mbalimbali zilizohitaji kiasi fulani cha elimu ya sheria ikiwemo uhakimu. Pia, baadhi ya wananchi walikwenda nje ya nchi kusomea sheria na kurudi kulitumikia Taifa lao.

Vyuo Vikuu viliendelea kuanzishwa na kufikia vyuo kumi na tisa vyenye kufundisha shahada ya sheria hapa nchini. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu Huria, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro, Chuo Kikuu cha Iringa, Chuo Kikuu cha Theofilo Kisanji, Chuo Kikuu cha Bagamoyo, Chuo cha Archibishop James, Chuo cha Archibishop Mihayo, Chuo cha Jordan, Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala, Chuo cha Stela Maris, Chuo cha Tumaini, Dar es Salaam, na Chuo cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa.

Baadhi ya vyuo hivi kwa sasa vimesitisha utoaji wa shahada ya sheria kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo soko la wanasheria kupungua.

Ndugu Wanahabari: kutokana na juhudi hizo, leo Taifa letu likiadhimisha miaka sitini ya uhuru, tumepiga hatua kubwa sana kwa maana ya kuwa na sekta ya sheria inayoongozwa na Watanzania wenyewe, wenye weledi, ujuzi na maarifa ya kutosha kulihudumia Taifa lao katika maeneo mbalimbali, iwe katika masuala ya utawala, utoaji haki, utungaji wa sheria na masuala mengine ya watu binafsi au kitaifa.

Ndugu Wanahabari: kuhusu maendeleo ya Katiba, tumekuwa na historia ambayo imetupa Katiba tano tangu tupate uhuru tarehe 9/12/1961. Tulianza na Katiba ya Uhuru ya 1961 ambayo ilifanikisha kupata uhuru wetu, kuweka mifumo na mingi ya kujitawala na kuendesha nchi; tukaja na Katiba ya Jamhuri ya 1962 ambayo ilisaidia Taifa letu kuwa Jamhuri na kuweka msingi inayoendana na dhana hiyo; tukafika katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya 1964 ili kufanikisha muungano wetu na ndugu zetu wa Zanzibar, baadaye tukaelekea katika Katiba ya Muda ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1965 kwa zama hiyo hiyo ya kutekeleza kuimarisha muungano wetu, na ilipofika mwaka 1977 tulipata Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo ni Sura Na. 2 ya Sheria zetu.

Katiba hii ya 1977 hadi sasa imeshafanyiwa mabadiliko madogo mara kumi na nne. Mabadiliko ya kwanza yalikuwa mwaka 1979 yaliyowezesha kuunzishwa na kuingizwa kwenye Katiba Mahakama ya Rufani baada ya kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Mabadiliko ya pili yalifanyika Mwaka 1980 ambayo yalilenga kupunguza kero mbalimbali za muungano. Mwaka huo huo kulitokea mabadiliko ya tatu ambayo kwa ajili ya kufafanua mfumo mzima wa uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Serikali yake pamoja na Baraza la Wawakilishi. Mabadiliko ya nne yalitokea mwaka 1982 kwa ajili ya kuboresha mfumo wa uteuzi wa wakuu wa Mikoa. Mabadiliko ya tano yalikuwa mwaka 1984 ambapo ukomo wa Rais wa Tanzania uliwekwa kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano na kuingiza rasmi sura ya Haki za Binadamu kwenye Katiba pamoja na Tamko Haki la Binadamu kwenye Katiba. Mwaka 1990 kulitokea mabadiliko ya sita na saba, katika nyakati tofauti, na kuanzisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi na namna ya kupata mgombea mmoja katika kiti cha Urais wa Zanzibar. Mabadiliko ya nane yalifanyika mwaka 1992 kwa kuweka utaratibu wa mfumo wa vyama vingi ukiambatana pamoja na kuanzishwa kwa wabunge wa viti maalumu vya wanawake kufikia asilimia 15 kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano na viti vitano kwa Baraza la Wawakilishi. Mwaka huo huo pia kulitokea mabadiliko ya tisa ambayo yaliweka ndani ya Katiba jinsi ya kumwondoa Rais madarakani kwa kura ya Bunge na kuanzisha nafasi ya Waziri Mkuu Kikatiba. Mwaka 1993, kupitia mabadiliko ya kumi, uchaguzi wa Madiwani uliwekwa pamoja na uchaguzi wa wabunge na Rais. Mabadiliko ya kumi na moja yalitokea mwaka 1994 kwa kuanzisha nafasi ya mgombea mwenza na kuondokana na nafasi ya moja kwa moja ya Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais. Mabadiliko ya kumi na mbili yalifanyika mwaka 1995 ambayo yaliweka ukomo wa Rais wa vipindi viwili vya miaka mitano mitano na kuanzisha utaratibu wa kuwaapisha viongozi wa juu kuanzia Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wake, Waziri Mkuu na Rais wa Zanzibar.

Pia ni kupitia mabadiliko hayo utratibu wa kumapata Rais iwapo Rais aliyeko madarakana atafariki au kushindwa kutekeleza madaraka yake ulipowekwa na umeonesha uhimilivu wa hali ya juu wakati Taifa lilipoondokewa na shujaa wake Hayati John Pombe Joseph Magufuli tarehe 17 Machi 2021. Mungu aendelea kumpumzisha mahali pema peponi, amina. Mwaka 2000, kulitokea mabadiliko ya kumi na tatu, kwa kuweka utaratibu wa ushindi wa jumla kwa kura zozote zile zinazozidi wengine tofauti na mfumo wa zamani wa mshindi kupata angalau asilimia 51; na pia kumwezesha Rais kuteua watu 10 kuwa wabunge. Mabadiliko ya kumi na nne ni yale yaliyotokea mwaka 2005 kwa kuondoa clawback clauses zote kwenye sehemu ya haki za binadamu na kuongeza idadi ya viti maalumu kufikia asilimia 30 na kuboresha haki mbalimbali ikiwa ni pamoja na haki ya kutoa maoni, kushiriki na watu wengine na haki ya kuabudu.

Kwa mantiki hiyo, miaka sitini ni muhimu sio tu kwa kukumbuka historia ya Taifa letu, bali pia ni nafasi ya kutafakari kwa ujumla, nchi yetu, imetoka wapi, iko wapi, na inaelekea wapi. Nitatumia fursa hii kutoa mifano mbalimbali inayoonesha mambo makubwa ambayo yameshafanyika kupitia sekta ya sheria na pia kusisitiza kuwa, hakuna historia ya sekta ya sheria ambayo ni nje ya historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nchi yetu, kama nilivyosema, ni muungano ambao ni matokeo ya Uhuru wa Tanganyika wa tarehe 09 Desemba,1961 na Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12/1/1964 na nchi hizi kuungana ilipofika tarehe 26/4/1964. Sasa ni miaka hamsini na sita tangu muungano huu uasisiwe na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume. Mambo makubwa sita yaliyoazimiwa kufanywa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mara baada ya uhuru ambayo nitapenda niyaseme mwanzo kabisa ni kama ifuatavyo;:-

(1) Kuunganisha Mfumo wa Mahakama nchini yaani integration of court system kwasababu mpaka tunapata uhuru tulikuwa na mfumo wa Mahakama ambao mmoja ulikuwa ni kwaajili ya watu wasiokuwa Waafrika na mwingine kwa ajili ya Waafrika (Native Court).

(2) Kurasimisha Sheria za Kimila - Codification of customary law na kuzihuisha Sheria za Kiislam - Restatement of Islamic Laws;

(3) Kuweka kwenye mfumo wa sheria za ndoa – Unification of law of marriage;

(4) Elime ya Sheria itolewe nchini na iwe inaakisi hali halisi ya nchi;

(5) Decolonization of the legal sector; na

(6) Kuanzisha Tume ya Kudumu ya Uchunguzi – Permanent Commission of Inquiry kwa ajili ya kushughulikia kero za wananchi;

Sekta ya Sheria ina historia ndefu kuanzia kipindi cha kabla ya kupata Uhuru mwaka 1961 hadi kufikia kipindi hiki tunapoadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara mwaka 2021. Sekta hii imepitia mabadiliko mbalimbali ya kimuundo, kisheria, kisera na kimfumo yakiwa na lengo la kuiboresha ili iweze kutoa huduma bora za kisheria kwa watanzania.

Wizara inayosimamia Sekta ya Sheria kwa mara ya kwanza iliundwa mwaka 1961. Katika mwaka huo, Hayati Julius Kambarage Nyerere, Waziri Mkuu wa Tanganyika alimteua Chifu Abdallah Fundikira kuwa Waziri wa Sheria wa Kwanza mzawa, kabla nafasi hiyo kuchukuliwa na Sheikh Amri Abeid Kaluta mwaka 1963. Mhe. Hassan Nassor Moyo alishika wadhifa huo kuanzia mwaka 1964 hadi 1966 Wizara ya Sheria ilipovunjwa na shughuli zake kuhamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais.

Katika kipindi hicho, majukumu yote yaliyohusu mambo ya Sheria yaliendelea kuwa chini ya Makamu wa pili wa Rais hadi baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1975. Baada ya uchaguzi huo Wizara ya Sheria iliundwa tena kupitia Tangazo la Serikali Na. 10 la mwaka 1975 na Mhe. Julie Catherine Manning aliteuliwa kuwa Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali hadi mwaka 1982 alipoteuliwa Mhe. Joseph Warioba kushika nafasi hizo. Utaratibu huu uliendelea hata baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1985 wakati Mhe. Damian Lubuva alipoteuliwa kushika nyadhifa hizo mbili hadi mwaka 1990.

Mabadiliko makubwa ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa mwaka 1990 yalipelekea kufutwa kwa Wizara ya Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kubaki na kofia moja ya Uanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, shughuli za Wizara zilihamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwa upande wake, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa Idara inayojitegemea chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais. Mabadiliko haya yalifanywa kupitia Tangazo la Serikali Na. 140 la mwaka 1990. Mwaka 1992, Mhe. Alli Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliirudisha tena Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba na kumteua Mhe. Samuel Sitta kuwa Waziri wake.

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995, Mhe. Benjamin William Mkapa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda Wizara hii kupitia Tangazo la Serikali Na. 720 la mwaka 1995. Katika muundo huu mpya, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa chini ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba na Naibu Mwanasheria Mkuu alikuwa pia Katibu Mkuu.

Mwaka 2005, baada ya Uchaguzi mkuu, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda Wizara hii na kuiita Wizara ya Katiba na Sheria jina linalotumika hadi sasa. Hata hivyo, ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, mwaka 2008, Wizara ilitenganishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hatua hii ilipelekea kutenganishwa kwa nafasi ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ile ya Katibu Mkuu.

Mara baada ya uchaguzi mkuu wa Mwaka 2015, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Tangazo la Serikali Na. 143 la tarehe 22 Aprili 2016 aliiunda tena Wizara ya Katiba na Sheria. Wizara ilipewa majukumu mbalimbali kupitia Tangazo la Serikali Na. 144 la tarehe 22 Aprili, 2016 na Tangazo la Serikali Na. 144A la Juni 2016.

Kufuatia kifo cha Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tarehe 17 Machi, 2021; tarehe 19 Machi, 2021 Mhe. Samia Suluhu Hassan aliapishwa kuwa Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Rais kupitia Tangazo la Serikali Na. 384 na 385 ya tarehe 7 Mei, 2021 aliunda na kutoa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Ndugu Wanahabari, Wizara hii inajumuisha taasisi zifuatazo: - (i) Mahakama ya Tanzania iliyoanzishwa chini ya Ibara ya 107 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (Sura ya 2) na inaongozwa na Jaji Mkuu wa Tanzania; (ii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliyoanzishwa kupitia Ibara ya 59 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Gazeti la Serikali Na. 48 la 2018 na inaongozwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali; (iii) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliyoanzishwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 49 la 2018 na inaongozwa na Mkurugenzi wa Mashtaka anayeteuliwa chini ya ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977; (iv) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini ulionzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali (Sura ya 245) na inayoongozwa na Kabidhi Wasii Mkuu; (v) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliyoanzishwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 50 la 2018 na inayoongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali; (vi) Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliyoanzishwa kupitia Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Sura ya 171) na inayoongozwa na Mwenyekiti; (vii) Tume ya Utumishi wa Mahakama iliyoanzishwa kupitia Sheria ya Utawala wa Mahakama (Sura ya 237) na inayoongozwa na Jaji Mkuu wa Mahakama; (viii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliyoanzishwa na Ibara ya 129 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inayoongozwa na Mwenyekiti; (ix) Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania iliyoanzishwa kupitia Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (Sura ya 425) na inayoongozwa na Mkuu wa Taasisi; (x) Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto kilichoanzishwa kupitia Sheria ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto (Sura ya 405) na kinaongozwa na Mkuu wa Chuo; na (xi) Baraza la Elimu ya Sheria lililoanzishwa na Sheria ya Mawakili (Sura ya 341) ambalo linasimamiwa na Jaji Mkuu wa Tanzania.

Ndugu Wanahabari, Dira ya Wizara ni "Katiba na Sheria Wezeshi kwa Maendeleo ya Taifa" na Dhima ni "Kuwa na Mfumo Madhubuti wa Kikatiba na Kisheria Wenye Kufanikisha Mipango ya Maendeleo ya Taifa".

Majukumu ya Wizara ni kama ifuatavyo:- i) Kushughulikia Sera za masuala ya kikatiba na kisheria na kuhakikisha utekelezaji wake; ii) Masuala ya kikatiba; iii) Haki na mfumo wa utoaji haki; iv) Uandishi wa Sheria; v) Uendeshaji wa mashtaka ya jinai; vi) Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi yanayohusu Serikali; vii) Uhakiki Mikataba mbalimbali inayohusu Serikali; viii) Masuala ya Sheria za kimataifa; ix) Masuala ya Haki za Binadamu; x) Huduma ya Msaada wa Kisheria; xi) Urekebu wa Sheria; xii) Masuala ya usafirishaji wa wahalifu kuletwa nchini au kwenda nje ya nchi; xiii) Masuala ya ushirikiano wa kisheria na mataifa mengine katika masuala mbalimbali ya jinai; xiv) Usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka, ufilisi, udhamini na kuasili watoto; xv) Uangalizi na ufuatiliaji wa utajiri asilia na maliasilia za nchi; xvi) Utendaji na uendelezaji wa rasilimaliwatu katika Wizara; na xvii) Shughuli za Taasisi, mipango na miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara.

Ndugu Wanahabari, maboresho makubwa yaliyofanyika katika sekta ya Sheria kuanzia mwaka 1961 hadi 2021 ni kama ifuatavyo:

(a) Kati ya Mwaka 1961 – 1971 Serikali ilijikita katika kutengeneza mifumo ya kiutawala, kitaasisi na kisheria. Kwa upande wa Sekta ya Sheria kipindi hiki kilikuwa ni kufanya mabadiliko makubwa ya kisheria ili kuwa na mifumo ya kisheria ya nchi huru; kuteua majaji wa Mahakama Kuu wakiwemo wazawa ili kushika hatamu kwenye mfumo wa utoaji haki; kuanzisha Chuo Kikuu cha kutoa shahada ya Sheria na ambacho kilikuwa Chuo pekee cha Sheria Afrika Mashariki; kuteua wazawa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali; ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho mbalimbali ya Katiba ya Mwaka 1962, 1963, 1964 na 1965 na kuungana kwa nchi ya Tanganyika na nchi ya Zanzibar na kuunda taifa moja la Tanzania.

(b) Kati ya Mwaka 1971 – 1981 Serikali ilikuwa inafanya tathmini ya mifumo mbalimbali ya kitaasisi ikiwemo Sekta ya Sheria. Katika kipindi hiki, Katiba ya Jamhuri ya Muungano ilitungwa upya mwaka 1977. Hali kadhalika, iliundwa Tume ya Msekwa ya 1975 - 1977 kwa lengo la kufanya tathmini ya masuala mbalimbali ya kisheria na uboreshaji wa utendaji wa mfumo wa haki na muundo wa taasisi za utoaji haki nchini; na kupelekea kufanyika kwa mabadiliko ya Kwanza ya Katiba ya 1979 na kuanzishwa kwa Mahakama ya Rufani ya Tanzania kufuatia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki;

(c) Mwaka 1981 - 1991 Serikali iliendelea na utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Msekwa pamoja na kuimarisha mifumo ya kisekta. Katika kipindi hiki Mwaka 1981 ilianzishwa Tume ya Kurekebisha Sheria ili kufanya utafiti wa sheria za nchi na kutoa mapendekezo ya kuhuisha au kutungwa kwa sheria mahsusi kwenye eneo lililofanyiwa utafiti. Aidha, Mwaka 1984, Katiba ilifanyiwa mabadiliko makubwa kwa kuzitambua na kuzijumuisha ndani ya Katiba masuala ya Haki za msingi na wajibu katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mamlaka yake ilitambuliwa rasmi kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, mifumo ya kisheria ya utoaji wa ushahidi Mahakamani na taratibu mbalimbali za uendeshaji wa mashauri ya jinai iliwekwa. Aidha katika maendeleo ya Katiba, Mwaka 1990 Tume Huru ya Uchaguzi ilianzishwa ili kushughulika na masuala ya uchaguzi ambyao hapo awali yalikuwa yakisimamiwa na Chama Tawala.

(d) Mwaka 1991 – 2001 Mifumo ya kidemokrasia ilimarishwa na kuwekwa kwenye Katiba kwa kuruhusu uwepo wa vyama vingi vya siasa na kuondokana na mfumo wa chama kimoja kushika hatam mwaka 1992. Hili liliawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika mfumo wa kidemokrasia wa kuchagua na kuchaguliwa kupitia uchaguzi mkuu wa vyama vingi mwaka 1995. Vile vile, katika kipindi hiki, muundo wa Bunge la Muungano ulibadilka kwa kuanzisha viti maalum vya wanawake kufika 15% na viti 5 kutoka Baraza la Wawakilishi - Zanzibar. Aidha, iliundwa Tume ya Bomani ya 1993 – 1996 ili kufanya tathmini ya Tume ya Msekwa ya 1977 na kutoa mapendekezo ya maboresho ya mifumo ya kisheria na Katiba. Hali kadhalika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilianzishwa kikatiba na kuchukua majukumu ya iliyokuwa Tume ya Uchunguzi ya mwaka 1965. Tume hii ilianzishwa kama chombo huru cha cha kupokea na kushughulikia malalamiko mbalimbali kuhusu uvunjaji na ukiukwaji wa haki za Binadamu dhidi ya mtu au taasisi yoyote.

(e) Mwaka 2001 - 2011 Sekta ya Sheria ilishuhudia kutambuliwa kwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Katiba kama msaidizi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya marekebisho ya 14 ya Katiba. Aidha, Marekebisho hayo, yalimtambua Mkurugenzi wa Mashtaka na kumfanya kuwa huru na asiyeingiliwa na mtu au chombo chochote katika utekelezaji wa majukumu yake ya kushtaki, kufuta na kuendesha mashauri ya jinai nchini. Kutokana na mabadiliko haya, mwaka 2008 ilitungwa Sheria iliyoanzisha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji wa mashtaka (Civilianization of prosecution). Katika kipindi hiki jukumu la kuendesha mashtaka liliondolewa kwa Jeshi la Polisi na kuwa chini ya Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka ili kuondoa migongano ya kimaslahi kwa taasisi moja kukamata, kupeleleza na kuendesha mashtaka kwa lengo la kupunguza ubambikwaji wa kesi. Katika kipindi hiki zlifunguliwa Ofisi za mashtaka katika mikoa yote na Wilaya 6 na hivyo kusogeza huduma za mashtaka karibu na wananchi ili kupunguza mlundikano wa mashauri na msongamano wa mahabusu magerezani.

Katika kipindi hiki, mwaka 2006 ulianzishwa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini ili kuongeza kasi ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu. Aidha, kufuatia mapendekezo ya Tume ya Msekwa (1977) na Tume ya Bomani (1996), mwaka 2007 ilianzishwa Taasisi ya Mafunzo ya

Uanansheria kwa Vitendo ili kujenga uwezo kwa wanasheria wahitimu wa shahada ya Sheria kwa kunolewa zaidi kabla ya kuingia ama kwenye ajira au kujiajiri.

(f) Mwaka 2011 – 2021 Katika kipindi hiki, Muundo wa Mahakama ulifanyiwa marekebisho makubwa kwa kuanzisha Mfuko wa Mahakama na kutenganisha shughuli za kimahakama na shughuli za utendaji katika Mhimili wa Mahakama kwa kuanzisha nafasi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama. Sanjari na hayo, kufuatia mahitaji ya Katiba Mpya, mwaka 2012 iliundwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba na kuanza kwa mchakato wa Mabadiliko ya Katiba yaliyopelekea kuwa na Katiba Inayopendekezwa.

Aidha, katika kipindi hiki mfumo ya kikatiba ya kuwalinda mashahidi na watoa taarifa za uhalifu na ule wa upatikanaji wa taarifa uliwekwa. Katika kupambana na masuala ya rushwa na uhujumu uchumi, mwaka 2016 ilianzishwa Divisheni maalum ya Mahakama Kuu ya kushughulikia makosa ya rushwa na uhujumu uchumi nchini. Mwaka 2017 yalifanyika maboresho makubwa ya maendeleo ya Katiba kwa kuziainisha haki za msingi za Katiba na za kiuchumi kwa kutambua mamlaka ya nchi juu ya utajiri asili na maliasilia zake ili kuwanufaisha wananchi. Sambamba na hilo uliwekwa mfumo wa kuwasajili, kuwasimamia, kuwaratibu na kuwatambua watoa huduma ya msaada wa kisheria ili kuhakikisha haki inapatikana na kuwafikia wananchi karibu na maeneo yao. Katika kipindi hiki pia, Mahakama ya Tanzania iliandaa Mpango wa Miaka 5 uliowezesha ujenzi wa miundombinu ya Mahakama nchi nzima na kuimarisha mfumo wa utendaji kazi ndani ya mhimili wa mahakama.

Pamoja na hayo, yalifanyika maboresho makubwa ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuianzisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ndani ya Muundo wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuitenganisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutoka kwenye Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, mwaka 2019 yalifanyika maboresho makubwa ya Mfumo wa Haki Jinai na kuanzishwa kwa Mahakama zinazotembea ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Katika kipindi hili pia, lugha ya Kiswahili ilifanywa kuwa lugha ya Uandishi wa Sheria na Utoaji Haki ili kuwezesha wananchi kuwa na uwelewa na masuala yanayowahusu kwa maendeleo yao. Aidha, kwa lengo la kuimarisha mifumo ya utoaji haki kwa kuanzisha Kituo cha Masuala ya Mirathi na Familia.

Ndugu Wanahabari, maendeleo ya watumishi katika Sekta ya Sheria katika kipindi cha miaka 60 ni kama ifuatavyo:- Hadi sasa kuna jumla ya Majaji wa Mahakama Rufani 25 ambapo wanaume 15 na wanawake 10 ikilinganishwa na Majaji 5 wa Mahakama ya Rufani ilipoanzishwa mwaka 1979; kuna jumla ya Majaji 84 wa Mahakama Kuu wakiwemo wanaume 56 na wanawake 28 ikilinganishwa Majaji 7 wa kiume wote ambao walikuwa wa kigeni; kuna Wasajili 41 katika Mahakama Kuu wakiwemo wanaume 27 na wanawake 14 ikilinganishwa na Msajili mmoja (1) wa kiume mwaka 1961; kuna jumla ya Mahakimu 1,122 wakiwemo wanaume 567 na wanawake 555 ikilinganishwa na Mahakimu 28 wote wanaume mwaka 1961; kuna jumla ya Mawakili 10,449 ambapo 2,057 ni Mawakili wa Serikali na 8,392 ni Mawakili wa Kujitegemea ikilinganishwa na Mawakili 9 waliokuwepo mwaka 1961.

Ndugu Wanahabari, maendeleo ya Miundombinu kwenye Sekta ya Sheria katika kipindi cha miaka 60 ni kama ifuatavyo, hadi kufikia Novemba, 2021 kuna Mahakama ya Rufani ambayo inatekeleza majukumu yake kupitia vituo 12 ambavyo ni Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga, Mtwara, Arusha, Dodoma, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Bukoba, Iringa na Mbeya ambapo jumla ya vikao 33 vinafanyika kwa mwaka ikilinganishwa na mwaka 1961 ambapo Mahakama ya Rufani haikuwepo na ilianzishwa mwaka 1979; kuna Masijala ya Mahakama Kuu 24 kati ya hizo Kanda ni 17, Divisheni 4, Masijala kuu 1, Kituo Jumuishi cha Masuala ya familia 1 na Kituo cha Usuluhishi 1 ikilinganishwa na Masijala 2 za Mahakama Kuu zilizokuwepo mwaka 1961; kuna Mahakama za Hakimu Mkazi katika Mikoa 29 ya Kimahakama; Kuna Mahakama za Wilaya 139 zinazotoa huduma za mahakama nchini ikilinganishwa na Mahakama za Wilaya 63 zilizokuwepo mwaka 1961; Kuna Mahakama za Mwanzo 960 zinazotoa huduma za Mahakama; Kuna Ofisi za Mwendesha Mashtaka katika mikoa 26 na Wilaya 16 ikilinganishwa na Ofisi za Kanda 7 zilizokuwepo mwaka 1961; kuna Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mikoa 10 ya Tanzania Bara ikilinganishwa na Ofisi za kanda 7 zilizokuwepo mwaka 1961; kuna Ofisi 294 na vituo 8,817 vya kuandikisha vizazi, Ofisi 155 na vituo 898 vya kuandikisha vifo, Ofisi 139 vya kuandikisha ndoa, Ofisi 2 za usajili wa Wadhamini, usajili wa Watoto wa kuasili na ufilisi ikilinganishwa na ofisi 48 za kuandikisha vizazi, kuandikisha vifo, kuandikisha ndoa na ofisi moja ya Usajili wa Wadhamini, Watoto wa Kuasili na Ufilisi mwaka 1961; kuna Ofisi 6 za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ikilinganishwa na Ofisi moja ya Tume ya Uchunguzi mwaka 1965; na kuna Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ambapo mwaka 1961 mafunzo hayo yalikuwa yanafanyika katika Ofisi mbalimbali ikiwemo Tanganyika Legal Corporation na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Ndugu Wanahabari, kwa upande wa utunzi wa Sheria kuna jumla ya Sheria Kuu 1,574 zimetungwa kuanzia Mwaka 1962 hadi mwaka 2021. Kati ya Sheria hizo, Sheria 446 zinatumika na Sheria 1,128 zilifutwa. Kati ya Sheria zinazotumika mgawanyo wake ni kama ifuatavyo: Sheria za Utawala 180, za Kiuchumi 130, Sheria zinazohusu Jamii 117 na Sheria zinazohusu sayansi na teknolojia 39 ikilinganishwa na Sheria Kuu 69 zilizotungwa mwaka 1961 ikijumuisha kwa mchanganuo wa Sheria Utawala zilikuwa 31, Sheria za Kiuchumi zilikuwa 24, Sheria zinazohusu Jamii zilikuwa 11 na Sheria zinazohusu Sayansi na Teknolojia zilikuwa 3.

Kwa upande wa urekebu na Tafsiri ya Sheria, Sheria Kuu 415 zilifanyiwa urekebu Toleo la Mwaka 2002 (Revised Edition) na Sheria 430 zimefanyiwa Urekebu Mwaka

2021 na zoezi la urekebu wa sheria zilizosalia liko katika hatua ya mwisho kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali ikilinganishwa mwaka 1961. Kuna jumla ya Sheria 154 zimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kwa hatua ya rasimu ya kwanza na zoezi la kutafsiri linaendelea ikilinganishwa mwaka 1961 ambapo hakukua na Sheria yoyote iliyokuwa katika lugha ya Kiswahili.

Kuhusu upekuzi na uhakiki wa mikataba jumla ya mikataba 10,067 inayoanzia thamani ya Shilingi Bilioni moja imefanyiwa upekuzi na uhakiki. Mikataba hii inahusisha masuala ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali, makubaliano ya kifedha, makubaliano ya Kimataifa na Hati za Makubaliano 478 ikilinganishwa mwaka 1961.

Ndugu Wanahabari, moja ya majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria ni kuendesha mashauri ya jinai, madai na usuluhishi ambapo hadi kufikia Juni, 2021 jumla ya Mashauri ya Jinai 53,146 yaliendeshwa katika Mahakama za Wilaya, Mkoa, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Kati ya hayo, jumla ya mashauri ya Jinai 23,308 yalihiti mishwa katika kipindi husika; wastani wa mashauri ya madai 4,612 yanafanyiwa kazi kwa mwaka kufikia Novemba, 2021 kati ya hayo Mashauri 4,353 ni Madai ya Ndani, Mashauri 15 Madai ya Nje na mashauri 244 ni Madai ya Kikatiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi. Vilevile Mashauri ya Usuluhishi 138 ambapo 111 usuluhishi wa Kitaifa na 27 Usuluhishi wa Kimataifa yalifanyiwa kazi.

Ndugu Wanahabari, haki za binadamu zimekuwa sehemu ya maendeleo ya nchi hata kabla ya dhana ya haki za binadamu kuzingatiwa kama ilivyo sasa duniani. Tanzania imekuwa na sera ya maendeleo inayozingatia haki za binadamu tangu mwaka 1967 ilipotungwa kwa Azimio la Arusha. Hii ilikuwa mwongozo wa maendeleo wa nchi baada ya uhuru na ilizingatia uhuru na kujitegemea (self-reliance) na upatikanaji wa haki za kisiasa, kiraia, kiuchumi, kijamii na za kiutamaduni. Azimio la Arusha lilizingatia dhana ya usawa na kutobaguliwa kwa kueleza kwamba: Watu wote ni sawa na kila mtu ana haki ya utu wake na kuheshimiwa; na Kila mtu ana haki ya uhuru wa kujieleza, uhuru wa kwenda mahali anakotaka, uhuru wa kuamini dini anayotaka na kulipwa ujira kutokana na kazi zake.

Pia, Azimio la Arusha lilizingatia Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu la Mwaka 1948 kwa kuelekeza kwamba Serikali inatakiwa kulinda heshima na utu ya kila mtu kwa kuzingatia Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu.

Ndugu Wanahabari, katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977 katika sehemu ya pili ya malengo muhimu na msingi ya mwelekeo wa shughuli za Serikali, Ibara 8(1) inaeleza kwamba "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii." Pia Ibara 9(f) ya Katiba inaeleza kwamba "Mamlaka ya Nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika kuelekeza sera na shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha heshima ya binadamu inahifadhiwa na kudumishwa kwa kufuata Kanuni za Tamko la Dunia kuhusu Haki za Binadamu (Universal Declaration of Human Rights of 1948)." Katiba yetu ni kati ya Katiba chache duniani iliyozingatia Tamko la Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu kwenye matamko yake.

Katika kukuza, kulinda na kuendeleza Haki za Binadamu, mwaka 1984 Katiba yetu ilifanyiwa marekebisho na kuingiza sehemu ya Haki na Wajibu Muhimu. Hapa ndipo haki za binadamu, wajibu na mipaka ya haki za binadamu zimeainishwa. Ibara 12 hadi 24 ni haki, Ibara 25 hadi 28 ni wajibu kwa jamii na Ibara 29 na 30 ni masharti ya wajibu na mipaka kwa haki, uhuru na hifadhi kwa haki na wajibu. Aidha, Serikali imekuwa ikitunga sera, sheria, kanuni, mipango na mikakati kwa kuzingatia misingi ya usawa na kutobaguliwa kama ilivyoainishwa kwenye Ibara ya 12 na 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
Utekelezaji wa maboresho haya ya Katiba ilihusisha kutungwa kwa Sheria ya kutekeleza Haki na Wajibu, Sura ya 3 (The Basic Rights and Duties Enforcement Act) mwaka 1995. Sheria hii inamwezesha mtu kudai haki zake zilizoainishwa chini ya Ibara 12 hadi 28 ya Katiba kwenye Mahakama.

Ndugu Wanahabari, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikitimiza wajibu wake wa kimataifa na kikanda wa kukuza na kulinda haki za binadamu na haki za watu kwa kuwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Katika kutekeleza majukumu na matakwa ya uanachama wa Jumuiya za Kimataifa, Serikali imeweza kutekeleza yafuatayo:-

Serikali imeridhia mikataba mikuu ya Haki za Binadamu chini ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika wa Haki za Binadamu na haki za watu.

Mikataba iliyoridhiwa chini ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu ni pamoja:-
Mosi, Mkataba wa Haki za Kiraia na Kisiasa (1966), tuliridhia 11 Juni 1976;

Pili, Mkataba wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (1966), tuliridhia 11 Juni 1976;

Tatu, Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (1979), tuliridhia 20 Agosti 1985;

Nne, Mkataba wa Kuondoa Ubaguzi wa Rangi (1965), tuliridhia 27 Oktoba 1972;

Tano, Mkataba wa Haki za Mtoto (1989), tuliridhia 10 Juni 1991;

Sita, Mkataba wa Nyongeza wa Mkataba wa Haki za Mtoto onaohusu Haki za Watoto kwenye Vita (2000), tuliridhia 11 Novemba 2004.;

Saba, Mkataba wa Nyongeza wa Mkataba wa Haki za Mtoto unaohusu Usafirishaji Haramu wa Watoto na Kuhusisha Watoto kwenye masuala ya Ngono (2002), tuliridhia 24 Aprili, 2003;

Nane, Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu (2006), tuliridhia 10 Novemba, 2009.

Mikataba chini ya Mfumo wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu ni pamoja na:-

Mosi, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka1981 tuliridhia tarehe 21 Oktoba, 1986.

Pili, Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa mwaka 1987 tuliridhia tarehe 29 Novemba, 1999.

Tatu, Mkataba wa nyongeza kwa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na watu unaohusu Haki za wanawake wa Afrika wa mwaka 2005 tuliridhia tarehe 3 Machi, 2007.

Nne, Mkataba wa nyongeza kwa Mkataba wa Nchi za SADC kuhusu haki za msingi za kijamii unaohusu maendeleo ya Jinsia ulianza kutumika Agosti, 2008

Vilevile, Serikali imekuwa ikishirikiana na Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu chini ya mfumo wa kutoa taarifa za haki za binadamu wa Mapitio katika kipindi Maalum (UPR) iliyoanzishwa na Umoja wa Mataifa mwaka 2006. Kwenye mfumo huu kila nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa anatoa taarifa ya jitihada za Serikali yake za kulinda na kukuza haki za binadamu baada ya kila miaka minne. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikiwasilisha Taarifa yake chini ya mfumo huu bila kukosa, kwenye mzunguko wa kwanza, wa pili, wa tatu na sasa tumeingia kwenye mzunguko wa nne.

Ndugu Wanahabari, vilevile, Serikali imekuwa ikishiriki kwenye vikao vya Baraza la Haki za Binadamu, Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Kamati ya Wataalam wa Afrika wa Hifadhi na Haki ya Mtoto, Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Hali ya Wanawake (UN-Commission on the Status of Women), Kamati za Baraza la Umoja lwa Mataifa, vikao vya Afrika Mashariki na vikao vya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Ushirikiano huo unajumuisha kupokea wataalam wao kutembelea Tanzania na kutoa maoni na kuishauri Serikali kuhusu haki za watoto na watu wenye ualbino.

Kwa upande wa Haki ya kutambuliwa, hadi kufikia Novemba 2021 jumla ya Wananchi 9,104,776 wamesajiliwa na kupewa vyeti vya kuzaliwa ikilinganishwa na Wananchi 5,303 waliokuwa wamesajiliwa na kupewa vyeti vya kuzaliwa mwaka 1961.

Kwa upande wa haki ya kupata taarifa; Serikali imesajili na kutoa leseni kwa vyombo vya Habari 1,160 vinavyojumuisha vituo vya runinga 48, vituo vya runinga mtandao 500, magazeti na machapisho 270, vituo vya redio 200, vituo vya redio mtandao 20 na blogs 122 vilivyoongeza wigo wa upatikanaji wa Habari kwa Wananchi ikilinganishwa na idadi ya vyombo vya habari 6 ambavyo ni magazeti 5 na kituo redio 1 mwaka 1961.

Kuhusu haki ya kupata taarifa, Serikali ilitunga Sheria ya Kupata Taarifa Sura Na. 9 ya mwaka 2016 ambayo imeweka misingi imara ya kuwezesha wananchi kutafuta, kupata na kusambaza taarifa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Ndugu Wanahabari, katika eneo la ufikiwaji wa Haki, hadi kufikia Novemba, 2021 Serikali imeweka utaratibu wa uratibu na usimamizi wa watoa huduma za msaada wa kisheria nchini kwa lengo la kuhakikisha ubora wa huduma zinazotolewa. Jumla ya watoa huduma ya msaada wa kisheria ambao wamesajiliwa kwa majukumu ya kutoa msaada wa kisheria nchini ni Mashirika 187 na Wasaidizi wa Kisheria 675 ikilinganishwa mwaka 1961 ambapo kulikuwa hakuna mfumo rasmi wa kusajili watoa huduma ya msaada wa kisheria nchini.

Vilevile zimeanzishwa kamati 17 za uratibu za msaada wa kisheria katika mikoa 17 ambayo ni Simiyu, Tanga, Kagera, Katavi, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Njombe, Kigoma, Ruvuma, Mbeya, Morogoro, Tabora, Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara na Lindi. Aidha, Huduma za msaada wa Kisheria zinazotolewa ni kuwaelekeza wananchi mahali sahihi kupata haki zao, kuandaa nyaraka za kimahakama, elimu kuhusu masuala ya kisheria, utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala, kupata ushauri wa kisheria na kuwasimamia katika mashauri yao mahakamani. Huduma za msaada wa kisheria zinatolewa kwenye makosa ya jinai, mashauri ya madai na utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala katika maeneo mijini na vijijini Tanzania Bara ikilinganishwa na huduma za msaada wa kisheria zilizokuwa zinatolewa katika makosa ya jinai tu mwaka 1961 ambazo zilijikita zaidi mijini.

Ndugu Wanahabari, kuhusu uimarishaji wa huduma ya utoaji haki kwa haraka na kwa wakati, Sekta ya Sheria inaendelea na matumizi ya mifumo ya TEHAMA nchini. Mahakama ya Tanzania ina jumla ya mifumo 6 ya Kielektoniki inayowezesha ufikakaji wa huduma za mahakama ikiwemo mfumo mama wa Takwimu Jumuishi za Mahakama (Judiciary Statistics Dashboard System), Mfumo unaoonesha maeneo ambapo Mahakama zilipo nchini (Judicial Mapping), Mfumo wa Maktaba Mtandao (e-library), Mfumo wa usikilizaji mashauri kwa njia ya mtandao (virtual Court-video conference), Mfumo wa Usimamizi wa Mawakili Tanzania (Advocate Management System) na Tovuti ya Mahakama ikilinganishwa mwaka 1961 ambapo kulikuwa hakuna mfumo wowote wa Kielektroniki katika utoaji huduma za Mahakama.

Wizara ya Katiba na Sheria ina jumla ya Mifumo sita ikiwemo Mfumo wa kushughulikia usajili wa Malalamiko yanayowasilishwa Wizarani, Mfumo wa Kushughulikia urejeshwaji wa Wahalifu ndani na nje ya Nchi, Mfumo wa Kushughulikia Vibali vya Kuongeza muda wa kuwasilisha Kesi Mahakamani, Mfumo wa Kushughulikia Amri ya Kuwaachia Wahalifu Wenye Matatizo ya Afya ya Akili,

Mfumo wa Kushughulikia Masuala ya Huduma ya Msaada wa Kisheria, Mfumo wa Kushughulikia Dirisha moja la Ubadilishanaji wa Taarifa katika Sekta ya Sheria, Mfumo wa Kusajili Watoa Huduma za Majadiliano, Maridhiano, Upatanishi na Usuluhishi na Mfumo wa Uangalizi na Usimamizi wa Masuala ya Utajiriasili na maliasilia za Nchi ikilinganishwa na mwaka 1961 ambapo Wizara ilikuwa haina mfumo wowote wa kielektroniki kwa ajili ya huduma za kisheria.

Vilevile, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) wana mifumo 8 ya Kielektroniki ikiwemo Mfumo wa Usajili wa Vizazi na Vifo, Mfumo wa Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka 5, Mfumo wa Usajili Vifo uliogatuliwa, Mfumo wa Usajili wa Ndoa, Mfumo wa Usajili wa Talaka, Mfumo wa Usajili wa Vizazi na Vifo kwa njia ya mtandao na Mfumo wa Usimamizi wa Wadhamini. Kwa upande wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ina mfumo wa kushughulikia malalamiko (Case Management System) unaowezesha mwananchi kutoa malamiko na kushughulikiwa kupitia mtandao.

Halikadhalika, Chuo cha Uongozi wa Mahakama kina mifumo ya kielektroniki ya kurahisisha majukumu ya kutoa mafunzo endelevu kwa Watumishi wa Mahakama Tanzania na wadau wengine wa Sekta ya Sheria ikiwemo nyenzo za kufundishia kwa njia ya video (Video teaching tools), Mikutano kwa njia Mtandao (video conference) mathalani kituo cha taarifa na mafunzo (kisutu training and information resources), na jukwaa la virtual court la Mahakama Tanzania.

Ndugu Wanahabari, mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Sheria kwa kipindi cha miaka 60 uhuru wa nchi yetu ni pamoja na:-

(i) Kuanza kwa Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Mifumo ya Utoaji Haki na Uandishi wa Nyaraka za Kisheria;

(ii) Kuboreshwa na kuimarika kwa upatikanaji wa Huduma za Kimahakama kutokana na Miradi inayoendelea kutekelezwa ya ujenzi wa Mahakama katika ngazi zote hapa nchini;

(iii) Kuimarika kwa mfumo wa kushughulikia Mashauri ya Madai na Usuluhishi ambao umepanua wigo wa ufikishaji na upatikanaji haki kwa wananchi;

(iv) Kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA katika Utoaji Haki ambapo kumepunguza gharama za uendeshaji wa Mashauri, kuimaisha upatikanaji wa haki kwa wakati na kuimarika kwa utoaji wa huduma ya msaada wa Kisheria;

(v) Kuimarisha usimamizi na uangalizi wa utajiri asilia na maliasilia za nchi ili ziweze kutumika, kumilikiwa na kuendelezwa kwa maslahi mapana ya wananchi;

(vi) Kuokelewa kwa fedha na mali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu ambazo zimerejeshwa Serikalini kutokana na kuboreshwa kwa mfumo kwa Haki Jinai Nchini;

(vii) Kujenga na kuanzisha Masijala za Mahakama Kuu kwenye mikoa 17 ya Tanzania Bara ikiwemo Divisheni tano za Mahakama kuu za Biashara, Ardhi, Kazi, Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, na Mirathi na masuala ya familia;

(viii) Ujenzi wa vituo jumuishi sita (6) vya utoaji haki katika mikoa ya Dar es Salaam (Temeke na Kinondoni), Mwanza, Morogoro, Arusha; na Dodoma unaoharakisha na kurahisisha ufikiaji wa haki kwa wananchi na wadau;

(ix) Kuanzishwa kwa matumizi ya huduma za Mahakama zinazotembea katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza kwa lengo la kusogeza huduma za upatikanaji haki karibu na wananchi;

(x) Kuimarisha mashirikiano ya kikanda na kimataifa katika mapambano dhidi ya uhalifu ikiwemo kuzuia wahalifu kunufaika na uhalifu, kurejesha wahalifu, kubadilishana nyaraka za Ushahidi na masuala mengine anuai katika sekta ya sheria. Katika kipindi hicho Wizara imekuwa Mwenyeji wa Mikutano ya Taasisi ya kimataifa ya Mashauriano ya ya Kisheria ya Nchi za Asia na Afrika (AALCO) na, SADC, na pia imeshiriki katika mikutano mbalimbali ya nje ya nchi iliyoandaliwa na jumuiya za kikanda na kimataifa kuhusu masuala ya kisheria;

(xi) Kuimarika kwa mfumo wa kuwasilisha Taarifa za Haki za Binadamu kwenye vyombo vya Kimataifa na Kikanda kuhusu jitihada za Serikali za kukuza na kulinda Haki za Binadamu kunakowezesha kutimiza jukumu letu kimataifa na kusafishwa taswira ya nchi dhidi ya tuhuma za ukiukwaji wa haki za binadamu;

(xii) Wigo wa wananchi kuelewa na kudai haki zao umeongezeka na Serikali iliimarisha maeneo mbalimbali katika kukuza na kulinda haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii kwa kutekeleza Mpango Kazi wa Haki za Binadamu wa mwaka 2013 -2017;

(xiii) Kuruhusu Mahakama za Mwanzo kuwatumia Mahakimu wenye Shahada ili kuongeza tija na ufanisi katika utoaji haki na kuruhusu mawakili kuwawakilisha Wadaawa katika mashauri ya Mahakama za Mwanzo ili kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa haki kwa wakati; na

(xiv) Kuongezeka kwa usajili wa vizazi vya watoto wa umri wa chini ya miaka 5 kutoka 13% mwaka 2012 hadi kufikia 65% kwa mwaka 2021.

Ndugu Wanahabari, Muono mbele wa Sekta ya Sheria ni pamoja na:-

(i) Kuanzisha Ofisi Jumuishi za Taasisi za Sekta ya Sheria ili kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma za pamoja za haki kwa Wananchi na Wadau Wengine;

(ii) Kuendelea na mpango wa kujenga Mahakama Jumuishi

Kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa Huduma za utoaji haki katika mikoa yote ya Tanzania, kujenga Mahakama za Wilaya katika Wilaya ambazo hazina majengo ya Mahakama, kujenga Mahakama za Mwanzo katika tarafa ambazo hazina majengo hayo na kuongeza huduma za Mahakama zinazotembea sita ambazo zitafanya kazi katika maeneo mbalimbali hapa nchini;

(iii) Kuendelea na Mpango wa Kutafsiri Sheria kutoka Lugha ya Kingereza kwenda Lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuimarisha matumizi ya Kiswahili katika utoaji wa haki ili kurahisisha Wananchi kuzielewa sheria na kufikia huduma ya upatikanaji haki;

(iv) Kuendelea kutunga na kurekebu Sheria ili kuweka mazingira mazuri yatakayokidhi mahitaji na maendeleo ya wananchi; na

(v) Kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika mfumo wa utoaji wa Haki Nchini kwa lengo kutanua wigo wa ufikiwaji haki kwa wananchi.

Ndugu wanahabari: kwa kumalizia nitaje tu Mafanikio makubwa saba ambayo nchi yetu imeyapata katika kipindi hiki cha miaka sitini (60) ya uhuru wetu.

Mosi, tumshukuru Mungu kutujalia kuadhimisha miaka 60 ya uhuru wetu tukiwa Taifa (We a nation) na sio mkusanyiko wa makabila yasiyo na umoja (a conglomeration of tribes) kama ilivyo katika baadhi ya nchi za Afrika.

Pili, tunaadhimisha miaka 60 ya uhuru wetu wakati nchi yetu ikiwa imeingia katika uchumi wa kati miaka mitano kabla ya muda uliokuwa umepangwa yaani mwaka 2025. Mafanikio haya yamepatikana katika kipindi kigumu ambacho uchumi wa dunia umeyumba kutokana na janga la UVIKO 19.

Tatu, tunaadhimisha miaka 60 ya uhuru wetu tukiwa ni taifa linalojiamini na linaloendelea kuenzi na kudumisha tunu za taifa ambazo ni amani, umoja, mshikamano, utu, haki, heshima ya mwanadamu, uhuru na demokrasia.

Nne, tunaadhimisha miaka 60 ya uhuru wetu tukiwa Taifa lenye uthubutu na moyo wa kujitegemea. Katika miaka 60 ya uhuru wetu, Watanzania wanajiamini kuwa wana uwezo wa kujenga nchi yao na kuboresha maisha na ustawi wao bila kumtegemea mtu yeyote lakini kwa kushikiana na mataifa na watu wengine wenye nia njema na maslahi ya nchi hii. Hili limedhihirishwa na ujenzi wa miradi mikubwa ya kielelezo kwa kutumia fedha na nguvu zetu wenyewe kwa lengo la kuongeza uwezo wetu wa kutoa huduma endelevu kwa watu wetu. Tumeidhihirishia dunia kuwa tuna uwezo wa kutoa elimu bila malipo kwa watoto wetu katika shule za msingi na Sekondari. Tumeweza na tunaendelea kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za Wilaya, hospitali za kanda, kusambaza umeme vijijini, maji vijijini na mijini na mengineyo mengi kwa kasi kubwa. Hii haina maana kwamba hatuthamini michango inayotolewa na wahisani mbalimbali, la hasha bali ni kutambua kwamba, ni wajibu wetu kujitegemea katika kujiletea maendeleo na wengine watuunge mkono katika jitihada hizo.

Tano, tunashrehekea miaka 60 ya uhuru, tukiwa tumetangaza rasmi na dunia nzima imetuelewa kwamba, utajiri na mali asilia zilizopo nchini mwetu ni mali yetu na tumerejea upya mikataba yote iliyokuwa na masharti hasi ili tufaidike na utajiri na maliasilia zetu. Katika nchi za Afrika tunathubutu kusema sisi ni wa kwanza kufanikisha hilo.

Sita, tunaadhimisha miaka 60 ya uhuru wetu,Kiswahili ambayo ndiyo lugha tuliyoitumia kugombania uhuru wetu, sasa ikiwa ni lugha ya ukombozi na utambulisho wa hadhi na heshima ya Mwafrika na Diaspora ya Kiafrika walioondoka miaka mia tano iliyopita kama watumwa na sasa lugha hii ni lugha ya kimataifa. Nipende kuwataarifu kwamba, Shirika la Elimu Sayansi na Utamaduni – UNESCO limetangaza tarehe 7 Julai ya kila mwaka itakuwa ni World Kiswahili Language Day. Hii ni fahari kwa taifa letu kwa kuwa lugha hii ni yetu, ilitusaidia katika harakati za uhuru na pia kutusaidia katika kulijenga taifa moja na nchi yetu sasa inaendelea kuimarika.

Saba tunaadhimisha miaka 60 ya uhuru, tukiwa tumeidhihirishia Dunia ukomavu wetu wa kisiasa na umadhubuti wa ukatiba (Constitutionalism) katika nchi yetu kwa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kukabidhiwa madaraka ya kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 baada ya kufariki akiwa madarakani Hayati Dr. John Pombe Joseph Magufuli. Amani na utulivu huo wa hali ya juu, pamoja na umoja na mshikamano uliokuwepo katika kipindi hiki cha mpito ni wa aina yake katika bara la Afrika. Nasi hatuna budi kumshukuru Mungu kwa kutujalia hayo yote.



MIAKA 60 YA UHURU ILIVYOIMARISHA DIPLOMASIA YA TAANZANIA KIMATAIFA

Ndugu wanahabari na wananchi mnaofuatilia matangazo haya mubashara,

ninawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ...... Kazi iendelee!!!

Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa na afya njema. Pia nitumie fursa hii kuwashukuru kwa namna ya pekee kwa kufika kwenu kwa wingi. Ni matarajio yangu kuwa kupitia vyombo vya habari mnavyoviwakilisha, watanzania na dunia kwa ujumla itaweza kufahamu kuhusu mafanikio ya Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, wakati huu Taifa likielekea kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Pili, nawapongeza kwa kuendelea kutekeleza majukumu yenu kwa weledi na uzalendo ambao umeiwezesha nchi yetu kuendelea kuwa Taifa lenye amani, umoja na mshikamano, na sasa tunaelekea kuadhimisha miaka 60 ya uhuru tukiwa imara na wamoja kama Taifa.

Ndugu Wanahabari, kama mnavyofahamu, kila ifikapo tarehe 9 Desemba nchi yetu huadhimisha uhuru wa Tanzania Bara, na kipekee kwa mwaka huu Serikali imetoa kipaumbele katika kuuhabarisha umma wa Watanzania na dunia kwa ujumla kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miongo sita iliyopita. Na kwa muktadha huo nitaeleza kwenu, kwa uchache, mafanikio ambayo Tanzania imeyapata kupitia mahusiano ya kimataifa kwa kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje katika kipindi cha miaka 60 iliyopita. Maelezo yangu yataainisha utekelezaji wa majukumu, malengo na mikakati ya Wizara ninayoiongoza katika kipindi husika.

Ndugu wanahabari, kabla sijaendelea, napenda kuwafahamisha kuwa, dhamana ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kusimamia uhusiano kati ya Tanzania na mataifa mengine duniani, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa kwa lengo la kulinda na kutetea maslahi ya Tanzania kimataifa. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara unaongozwa na Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 pamoja na miongozo mingine ya Serikali.

**HISTORIA YA WIZARA**

Ndugu wanahabari, kama ilivyo kwa Wizara nyingine, historia ya Wizara hii inaanzia pale Tanzania Bara (wakati huo Tanganyika) ilipopata uhuru kutoka kwa Uingereza tarehe 09 Desemba 1961. Wizara ilianza ikiwa ni Idara ya Mambo ya Nje na Ulinzi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambaye kwa wakati huo alikuwa ni Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mwaka 1963, Idara ya Mambo ya Nje na Ulinzi ilibadilishwa na kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ulinzi. Mwaka 1965, majukumu ya ulinzi yaliondolewa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na tangu hapo jina la Wizara hii limekuwa likibadilika kutokana na dhamana na majukumu ya wakati husika.

Mwaka 2016, majukumu ya zilizokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki yaliunganishwa na kuundwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Ndugu wanahabari, mara tu baada ya kupata uhuru, kipaumbele cha Serikali kilikuwa ni kuongeza ushirikiano na uhusiano na mataifa mengine duniani na taasisi za kimataifa ambapo ilitulazimu kufungua ofisi za uwakilishi na kupeleka watumishi nje ya nchi ili kuongeza ufanisi wetu katika kushiriki masuala ya kimataifa. Mnamo mwaka 1962 Serikali iliteua mabalozi wa kuiwakilisha Tanzania katika nchi ya Uingereza na Umoja wa Mataifa - New York, Marekani. Aidha, Serikali ilifungua milango kwa nchi nyingine na mashirika ya kimataifa kufungua ofisi za uwakilishi hapa nchini, ambapo Serikali za Uingereza na Ujerumani zilikuwa ni nchi za kwanza kufungua Balozi zao hapa nchini.

Ndugu Wanahabari, kwa sasa tunapoelekea kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, Nchi yetu ina Balozi 44 na Konseli Kuu 6 katika nchi mbalimbali duniani ambapo katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita (6) Ubalozi mmoja (1) umefunguliwa Vienna, Austria. Pia, Tanzania ni mwenyeji wa Balozi 62 na Mashirika ya Kimataifa 30.

Ndugu Wanahabari, ili kuwezesha watumishi katika balozi zetu nje kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi, Serikali imekuwa ikinunua, kujenga au kupanga majengo ya ofisi na makazi ya watumishi balozini, ambapo hadi hivi sasa Serikali inamiliki viwanja 12 na majengo 106 nje ya nchi. Serikali imeendelea kukarabati majengo hayo na kuendeleza kwa awamu viwanja hivyo, ambapo kwa sasa inatekeleza miradi minne (4) ya ujenzi wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi kwenye Balozi za Tanzania Nairobi - Kenya, Kinshasa – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Moroni - Comoro na Muscat - Oman.

Ndugu Wanahabari, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhamiria kuendelea kuimarisha ushirikiano na uhusiano baina ya nchi yetu na mataifa mengine, jumuiya za kikanda na kimataifa, ambapo katika kipindi kifupi cha kuwepo madarakani tayari imepeleka watumishi wengi zaidi kuhudumu katika balozi zetu.

Ndugu wanahabari, tangu uhuru hadi sasa, Serikali kupitia Wizara hii imetekeleza kwa mafanikio ya kujivunia sera ya mambo ya nje ambayo mwanzo ilijikita katika kutetea haki za wanyonge na kupiga vita ukoloni na ukoloni mamboleo; kupinga siasa za ubaguzi na ukandamizaji wa aina zote; kuendeleza Umoja wa Afrika; na kuunga mkono sera ya kutofungamana na upande wowote. Mafanikio yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa sera hiyo ni pamoja na kulinda, kutetea na kudumisha uhuru wetu; na mchango wa Tanzania katika ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika, kutokomeza siasa za ubaguzi wa rangi Afrika Kusini na kujenga umoja na mtangamano wa kikanda na Bara la Afrika.

Ndugu wanahabari, ilipofika miaka ya 1990, msisitizo wa Sera ya Mambo ya Nje ulihuishwa na kujumuisha masuala ya kiuchumi na kijamii baada ya nchi nyingi barani Afrika hususani zilizopo kusini mwa Afrika kupata uhuru na kukomeshwa kwa siasa za kibaguzi nchini Afrika Kusini. Sababu nyingine za kuhuisha sera yetu ya mambo ya nje ni pamoja na kumalizika kwa vita baridi duniani na kuibuka kwa utandawazi na mageuzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kwa kuzingatia mabadiliko hayo, mwaka 2001 Serikali ilitunga sera mahsusi kwa ajili ya kusimamia mambo ya nje ambayo iliendelea kubeba misingi ya kulinda uhuru wa kujiamulia mambo yetu wenyewe; kuheshimu mipaka ya nchi na uhuru wa kisiasa; kulinda uhuru, haki za binadamu, usawa na demokrasia; kukuza ujirani mwema; kuendeleza Umoja wa Afrika; kukuza ushirikiano wa kiuchumi na wabia wa maendeleo; kuunga mkono utekelezaji wa sera ya kutofungamana na upande wowote; kuimarisha ushirikiano wa nchi zinazoendelea; na kuunga mkono Umoja wa Mataifa na jitihada zake za kuimarisha maendeleo ya uchumi wa kimataifa, amani na usalama.

Ndugu wanahabari, Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 iliweka bayana azma ya Serikali kukuza uchumi na maendeleo ya Taifa kupitia mahusiano ya kimataifa, ambapo msisitizo mkubwa ulielekezwa katika kutekeleza diplomasia ya uchumi. Jitihada za Serikali zilielekezwa katika kuongeza wigo wa biashara ya kimataifa kupitia utafutaji wa masoko ya bidhaa mbalimbali za Tanzania nje ya nchi, kuvutia uwekezaji wa mitaji na teknolojia kutoka nje katika sekta za kijamii na kiuchumi, kutangaza vivutio vya utalii, kuongeza fursa za ajira na masomo kwa watanzania nje ya nchi na kushawishi upatikanaji wa misaada na mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo nchini.

## MAFANIKIO YA TANZANIA KATIKA HARAKATI ZA UKOMBOZI BARANI AFRIKA

Ndugu wanahabari, tangu kupata uhuru hadi miaka ya 1990, Tanzania ilikuwa mstari wa mbele kupigania ukombozi wa nchi za Afrika hususan zile za Kusini mwa Afrika kutoka katika utawala wa kikoloni sanjari na kupinga ubaguzi dhidi ya mwafrika. Katika kipindi hicho, Tanzania ilichangia rasilimali fedha, askari pamoja na ardhi yake kusaidia wapigania uhuru kutoka nchi nyingine za Afrika ikiwemo Angola, Namibia, Zimbabwe, Afrika Kusini na Msumbiji. Imani ya waasisi wa nchi yetu wakati huo ilikuwa ni kwamba uhuru wa Tanzania hautakuwa kamili endapo nchi zinazotuzunguka zitakuwa hazijapata uhuru wa kujitawala zenyewe.

Ndugu wanahabari, ili kufanikisha azma hiyo, Tanzania ilishirikiana pia na nchi nyingine za Afrika zilizokuwa zimepata uhuru kipindi hicho na ambazo viongozi wake walikuwa na dhamira sawa ya kuchangia katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika. Mnamo mwaka 1970 Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliungana na Hayati Kenneth Kaunda, Rais wa Jamhuri ya Zambia na Hayati Seretse Khama, Rais wa Botswana na kuanzisha umoja wa Nchi zilizo Mstari wa Mbele (Frontline States) katika kupigania ukombozi wa nchi zilizo kusini mwa Afrika kutoka katika utawala wa kikoloni na kupinga ubaguzi uliokuwa ukifanywa na Makaburu katika nchi ya Afrika Kusini pamoja na utawala wa wachache katika nchi ya Rhodesia.

Ndugu Wanahabari, pamoja na harakati za ukombozi wa kisiasa na vita dhidi ya ubaguzi, majadiliano kati ya Nchi Zilizo Mstari wa Mbele kuhusu ushirikiano wa kiuchumi yalianza kupewa msukumo katika miaka 1970, na hatimaye nchi hizo (Frontline States) na nchi zilizopata uhuru baadaye ziliungana na kuanzisha mtangamano wa kiuchumi ambao awali ulijulikana kama Jukwaa la Uratibu wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCC) mwaka 1980 kabla ya kuwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) mwaka 1992. Kupitia SADC Tanzania imeendeleza harakati zake za kulinda amani na usalama katika ukanda wa kusini mwa Afrika ambapo tumechangia kutafuta ufumbuzi wa migogoro katika nchi za Lesotho, Madagascar, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Msumbiji.

Ndugu Wanahabari, mchango wa Tanzania katika harakati za ukombozi na kupigania uhuru katika nchi za kusini mwa Afrika umehifadhiwa katika juzuu maalum kupitia Mradi wa Hashim Mbitta ulioanzishwa na SADC kuenzi harakati hizo. Hii ni heshima ya kipekee kwa Tanzania, kwani kumbukumbu hizo zitadumu na kuifanya historia ya mchango wa nchi yetu katika ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika kuishi vizazi na vizazi.

Ndugu Wanahabari, mbali na nchi za Kusini mwa Afrika, Tanzania ilifanikiwa kuiondoa madarakani Serikali ya Hayati Iddi Amin, iliyokuwa ikitawala kimabavu nchini Uganda kupitia vita inayojulikana na wengi kama Vita ya Kagera mwaka 1977-1978. Uamuzi wa Serikali ya Tanzania kipindi hicho ulikuwa ni muhimu kwa lengo la kulinda usalama wa mipaka ya nchi yetu. Aidha, hatua hiyo ilirejesha utawala wa sheria nchini Uganda na utulivu wa kisiasa ambao umedumu hadi hivi sasa.

Ndugu Wanahabari, jitihada hizo pamoja na utulivu wa kisiasa na uwepo wa amani nchini uliodumu kwa kipindi chote tangu Uhuru, imeifanya Tanzania kujijengea heshima na kutambulika na jumuiya ya kimataifa kama kisiwa cha amani na mshirika katika masuala ya ukombozi, ulinzi na usalama katika Bara letu la Afrika na duniani kwa ujumla, jambo ambalo Tanzania inajivunia hata sasa tunapoadhimisha miaka 60 ya Uhuru wetu.

## MAFANIKIO YA TANZANIA KATIKA ULINZI WA AMANI NA USALAMA BARANI AFRIKA NA DUNIANI

Ndugu wanahabari, Tanzania inajivunia mchango wake katika juhudi za kuhakikisha uwepo wa amani, ulinzi na usalama Barani Afrika na duniani kwa ujumla, katika kipindi cha miaka 60 iliyopita. Masuala hayo (amani, ulinzi na usalama) pia ni miongoni mwa tunu na urithi wa Taifa letu.

Ndugu Wanahabari, katika kipindi hicho, Tanzania

imeshiriki katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya mazungumzo kwenye nchi mbalimbali duniani. Ushiriki wa Tanzania katika harakati hizo umekuwa wa moja kwa moja au kupitia jumuiya za kikanda. Kwa mfano, mwaka 1999 Tanzania ilishiriki katika kuzipatanisha pande mbili zilizokuwa zikihasimiana nchini Burundi. Mpatanishi Mkuu katika mgogoro huo alikuwa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kabla ya kifo chake na baadaye juhudi hizo ziliendelezwa na Hayati Benjamini Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu. Usuluhishi wa mgogoro huo ulitamatishwa kwa pande zinazohasimiana kusaini Makubaliano ya Amani na Maridhiano ya Arusha mwaka 2000 na Makubaliano ya Kusitisha Mapigano mwaka 2005, ambayo yamedumisha amani nchini Burundi hadi hivi sasa.

Halikadhalika, mwaka 2015 Jumuiya ya Afrika Mashariki ilimteua Hayati Benjamin Mkapa kuongoza Majadiliano ya Amani ya Burundi baina ya pande zilizokuwa zikihasimiana nchini humo kufuatia mgogoro wa kikatiba uliombatana na machafuko yaliyotokana na tofauti za kisiasa.

Ndugu Wanahabari, Vilevile, mwaka 2008 na 2013, Tanzania ilishiriki katika upatanishi wa pande zilizokuwa zikihasimiana nchini Kenya kutokana na tofauti za kisiasa zilizoambatana na vurugu za uchaguzi mkuu. Mwaka 2008, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne alialikwa kuzipatanisha pande zilizokuwa zikihasimiana nchini Kenya. Mwaka 2013, Hayati Benjamin Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu alishiriki kwenye upatanishi wa pande zilizokuwa zikihasimiana nchini Kenya akiwa kama mjumbe wa jopo la watu mashuhuri chini ya uangalizi wa Umoja wa Afrika. Jopo hilo lilikuwa likiongozwa na Hayati Koffi Annan, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Ndugu Wanahabari, pamoja na kushiriki katika usuluhishi wa migogoro na upatanishi, katika kipindi cha miaka 60 Tanzania pia imetoa hifadhi kwa raia wanaozikimbia nchi zao kutokana na changamoto za kiusalama hususani nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu. Baadhi ya wakimbizi hao, hususani walioishi nchini kwa muda mrefu au kuzaliwa na wazazi wao wakiwa ukimbizini hapa nchini, wamepatiwa uraia na wanaendelea na shughuli za kijamii na kiuchumi kama walivyo raia wengine wa Tanzania.

Ndugu Wanahabari, mifano hiyo michache inaonesha jinsi gani nchi yetu ilivyo kuwa katika mstari wa mbele kulinda, kutetea na kudumisha amani katika nchi nyingine majirani na duniani. Aidha ushiriki wa Tanzania katika usuluhishi na upatanishi wa migogoro ni kielelezo cha kuaminiwa kwa nchi yetu katika kudumisha amani kimataifa.

Ndugu wanahabari, Tanzania pia imechangia walinda amani kwenye misheni tano za kulinda amani za Umoja wa Mataifa, ambapo hadi kufikia mwezi Septemba 2021, ilikuwa na jumla ya walinda amani 1,483 katika Misheni za MINUSCA (Afrika ya Kati), MONUSCO (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), UNIFIL (Lebanon), UNISFA (Abyei, Sudan) na UNIMISS (Sudan Kusini). Idadi hiyo ya walinda amani inaifanya Tanzania kuwa nchi ya 13 kati ya nchi 122 zinazochangia kwa wingi walinda amani katika misheni za kulinda amani duniani.

Ndugu Wanahabari, tunapoelekea kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, mipaka ya nchi yetu imeendelea kubaki salama ikichagizwa na utulivu na amani iliyopo nchini. Aidha, hali ya ujirani mwema pamoja na uhusiano wa kidugu uliopo baina yetu na nchi zinazotuzunguka, imesaidia nchi yetu kuendelea kuwa na amani katika ukanda wetu ambao una baadhi ya nchi zinazokabiliwa na migogoro ya wenyewe kwa wenyewe pamoja na changamoto za kiusalama.

Ndugu Wanahabari, kama kielelezo cha sifa adhimu ya utulivu na amani iliyopo nchini, Taarifa ya Global Peace Index ya mwaka 2020 imeitaja Tanzania kuwa ni nchi ya kwanza (1) kwa amani na utulivu kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na ya saba (7) katika nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Ndugu Wanahabari, ninatoa rai kwenu na kwa Watanzania wote kuendeleza amani, umoja na mshikamano uliodumu kwa kipindi cha miaka 60 iliyopita. Aidha Serikali ya awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano huo sambamba na kuendelea kutetea, kulinda na kudumisha usalama na amani duniani kwa kushirikiana na jumuiya ya kimataifa.

## MAFANIKIO YA TANZANIA KATIKA USHAWISHI NA UONGOZI NDANI YA JUMUIYA NA TAASISI ZA KIMATAIFA

Ndugu Wanahabari, ushiriki wa nchi yetu ndani ya jumuiya na taasisi za kimataifa katika miongo sita (6) iliyopita umekuwa wa mafanikio ambapo Tanzania imekuwa mstari wa mbele kupaza sauti na kuishawishi jumuiya ya kimataifa katika masuala mbalimbali yenye maslahi kwa Taifa letu na dunia kwa ujumla. Mathalan, mwaka 1972 Tanzania iliungana na baadhi ya nchi zinazoendelea kuzishawishi nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuirejeshea nafasi ya kudumu Jamhuri ya Watu wa China katika Baraza la Usalama la Umoja huo iliyokuwa imetwaliwa na Jamhuri ya China (Taiwan). Vilevile, Tanzania kupitia Ushirikiano wa Nchi za Kusini (South South Cooperation) imekuwa ikikemea mifumo kandamizi ya kiuchumi na kisiasa na kutetea haki na usawa kwa nchi zote. Aidha, kupitia ushirikiano huo, Tanzania imeendelea kuzitaka nchi zilizoendelea kuheshimu ahadi zao za kutoa asilimia moja ya utajiri wao kuzisaidia nchi zinazoendelea kujikwamua na umaskini.

Katika kuendeleza msimamo huo wa kutetea haki na usawa kwa nchi zote ulimwenguni, katika miaka ya hivi karibuni Tanzania imekuwa mstari wa mbele kuitaka jumuiya ya kimataifa, hususani nchi za magharibi, kuiondolea Zimbabwe vikwazo vya kisiasa na kiuchumi. Sambamba na hilo, Tanzania imeweka bayana msimamo

wake wa kupinga ukandamizaji unaofanywa kwa nchi mbalimbali duniani ikiwemo Cuba na mataifa ya Saharawi ya Magharibi na Palestina.

Ndugu wanahabari, katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na athari za kiafya na kiuchumi kutokana na mlipuko wa UVIKO-19, Tanzania kupitia majukwaa mbalimbali ya kikanda na kimataifa imeeleza waziwazi msimamo wake wa kuzitaka nchi zilizoendelea kuyawezesha mataifa yanayoendelea kujijengea uwezo wa kuzalisha chanjo, dawa na vifaa tiba ili kukabiliana na magonjwa mbalimbali ya mlipuko ikiwemo UVIKO-19. Ndugu wanahabari, kutokana na msimamo huo thabiti pamoja na ushawishi wa nchi yetu katika jumuiya ya kimataifa, Tanzania kwa nyakati tofauti imeaminiwa na kupewa dhamana za uongozi katika ngazi mbalimbali ndani ya jumuiya za kikanda na kimataifa. Mfano, Tanzania imewahi kuwa mwanachama asiye wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa vipindi viwili, mwaka 1975 hadi 1976 na mwaka 2005 hadi 2006.

Aidha, Tanzania imechaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Kikao cha 76 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA 76) kinachoendelea hivi sasa New York, Marekani.

Tanzania pia imekuwa mwenyekiti wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) ambao kwa sasa unajulikana kwa jina la Umoja wa Afrika (AU) mara mbili, mwaka 1984 hadi 1985 na mwaka 2008. Tanzania imekuwa mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa vipindi viwili, mwaka 2004 na 2019. Kipekee, pia Tanzania imekuwa mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa miaka miwili (2) mfululizo mwaka 2015 na 2016.

Kadhalika, Watanzania mbalimbali wamechaguliwa kushika nyadhifa za juu na za maamuzi katika jumuiya za kikanda na kimataifa. Mfano, Mhe. Balozi Salim Ahmed Salim, Waziri Mkuu Mstaafu, alikuwa Katibu Mkuu wa OAU kwa vipindi viwili mfululizo kuanzia mwaka 1989 hadi 2001; Mhe. Balozi Mstaafu Getrude Mongela alikuwa Spika wa kwanza wa Bunge la Umoja wa Afrika kuanzia mwaka 2004 hadi 2009; Mhe Balozi Dkt. Asha – Rose Migiro, ambaye kwa sasa ni Balozi wa Tanzania nchini Uingereza alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia 2007 hadi 2012; Balozi Liberata Mulamula (Mb), ambaye kwa sasa ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki alikuwa Katibu Mtendaji wa kwanza wa Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR) kuanzia 2006 hadi 2011; na Mhe. Dkt. Stergomena Tax (Mb), ambaye kwa sasa ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alikuwa Katibu Mtendaji wa kwanza mwanamke wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa vipindi viwili mfululizo kuanzia mwaka 2013 hadi 2021.

Ndugu Wanahabari, watanzania wengine waliowahi kushika nyadhifa za uongozi katika jumuiya za kimataifa ni pamoja na Mhe.Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyewahi kuwa Mjumbe wa Jopo la Ngazi ya Juu la Wataalam wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Masuala ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi; Prof. Anna Tibaijuka, aliyewahi kuwa Katibu Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi; Dkt. Winnie Mapunju Shumbusho, aliyewahi kuwa Mkurugenzi Msaidizi wa Shirika la Afya Duniani ; na Hayati Balozi Augustine Mahiga, aliyewahi kuwa Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu mgogoro wa Somalia.

Ndugu Wanahabari, wapo pia watanzania ambao hivi sasa wanaongoza jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa. Kwa kuwataja wachache ni pamoja na Balozi Ali Mchumo, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la International Bamboo and Rattan Organisation kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2019 hadi 2022; Mhe Jaji Imani Aboud ambaye ni Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa kipindi cha miaka sita kuanzia 2021; na Mhe Balozi Maimuna Tarishi, Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania ndani ya Umoja wa Mataifa – Geneva na Vienna ambaye ni Rais wa Bodi ya Biashara na Maendeleo ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia 2021 hadi 2022.

Ndugu Wanahabari, wingi wa wanawake katika orodha ya watanzania walioshika nyadhifa za uongozi na maamuzi katika jumuiya za kimataifa ni kielelezo cha Serikali yetu kuthamini mchango wa mwanamke katika masuala ya uongozi na uhusiano wa kimataifa.

Ndugu Wanahabari, Serikali ya Awamu ya Sita imelipa kipaumbele suala la kuongeza ajira kwa Watanzania nje ya nchi na katika taasisi za kimataifa, ambapo katika kipindi cha muda mfupi tangu kuingia madarakani, fursa za ajira nje ya nchi zipatazo 70 zilitangazwa kwa umma kwa watanzania wenye sifa kuzichangamkia. Fursa hizo zinajumuisha nafasi nne (4) za ajira katika Shirika la Afya Duniani; Umoja wa Afrika (22); Umoja wa Mataifa (1); Benki ya Maendeleo ya Afrika (26); Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (1); Shirika la Jumuiya ya Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (5); na Shirika la Kuzuia Matumizi ya Silaha za Kemikali (6). Ninatoa wito kwa watanzania kuendelea kufuatilia fursa za ajira za kimataifa zinazotangazwa na Serikali mara kwa mara na kuomba nafasi hizo ili kuongeza wigo wa watanzania kwenye ajira kimataifa.

## UENYEJI WA TAASISI NA MASHIRIKA YA KIKANDA NA KIMATAIFA PAMOJA NA MIKUTANO YA KIMATAIFA

Ndugu wanahabari, ishara mojawapo ya kuaminika na kukubalika kwa nchi yoyote kimataifa ni nchi husika kupewa uenyeji wa taasisi na mashirika ya kikanda na kimataifa pamoja na kuandaa mikutano ya kimataifa. Tanzania katika miaka 60 inajivunia kuwa mwenyeji wa taasisi na mashirika ya kimataifa. Miongoni mwa taasisi na mashirika ya kimataifa yenye makao makuu au ofisi za uwakilishi hapa nchini ni pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika

Mashariki, Bodi ya Ushauri ya Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa na Mashirika yake, Taasisi ya Afrika ya Sheria za Kimataifa, Chuo cha Upasuaji cha Afrika Mashariki, Kati na Kusini, Umoja wa Posta Afrika na Chuo cha Afrika Mashariki cha Takwimu.

Ndugu wanahabari, pamoja na mashirika na taasisi hizi kuitangaza nchi yetu kimataifa, uwepo wake una faida za kiuchumi pia. Miongoni mwa faida za kiuchumi tunazopata kwa kuwa mwenyeji ni pamoja na ajira kwa watanzania, upatikanaji wa fedha za kigeni na uhawilishaji wa ujuzi na utaalam.

Ndugu wanahabari, katika kuonesha dhamira yake ya kuendelea kuvutia mashirika na taasisi za kimataifa kuwa na makao makuu au ofisi za uwakilishi nchini, Serikali imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 431 la Lakilaki, jijini Arusha kwa ajili ya ujenzi wa taasisi za kimataifa. Hadi sasa Mahakama ya Kimataifa ya Masalia ya Kesi za Mauaji ya Kimbari ya Rwanda imeanzisha ofisi zake katika eneo hilo.

Ndugu wanahabari, Tanzania pia inajivunia kuwa mwenyeji wa mikutano ya kimataifa katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru. Baadhi ya mikutano ya kimataifa ambayo tumekuwa nchi mwenyeji ni pamoja na Mikutano ya Wakuu wa Nchi na Serikali ya SADC iliyofanyika mwaka 2004 na 2019; Mkutano wa Sullivan uliofanyika mwaka 2008; Mkutano wa Smart Partnership uliofanyika mwaka 2013; Mikutano mbalimbali ya Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Mkutano wa Nordic-Africa uliofanyika mwaka 2019.

Ndugu wanahabari, tunapoelekea kuadhimisha miaka 60 ya uhuru na kuanza safari ya miaka mingine 60 ijayo, Tanzania itaendelea kuwa mwenyeji wa mikutano ya kimataifa ikiwemo, Mkutano wa 65 wa Kamisheni ya Afrika na Jukwaa la Pili la Uwekezaji kwenye Utalii uliopangwa kufanyika mwaka 2022. Mikutano hiyo pamoja na kuitangaza nchi kimataifa, ni kichocheo cha ukuaji wa sekta mbalimbali za uchumi kama vile utalii, biashara, uchukuzi, malazi na hoteli.

Ndugu wanahabari, kiashiria kingine cha uimara wa uhusiano kati ya Tanzania na jumuiya ya kimataifa ni uwepo wa miadi na ziara za viongozi wakuu wa kitaifa na mashirika ya kimataifa. Katika kipindi cha miaka 60 iliyopita, viongozi wakuu wa kitaifa kwa nyakati tofauti wamekuwa wakifanya ziara nje ya nchi na viongozi wakuu kutoka mataifa mengine pamoja na mashirika ya kimataifa wamekuwa wakiitembelea Tanzania. Kupitia ziara hizo Tanzania imenufaika na uwekaji saini makubaliano na mikataba ya ushirikiano katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mfano, kufuatia ziara ya Mhe. Barack Obama, Rais Mstaafu wa Marekani hapa nchini mwaka 2013, nchi yetu ilijumuishwa katika Mpango wa Kukabiliana na Changamoto za Milenia (Millenium Challenge Compact-MCC), ambapo kupitia Awamu ya Kwanza ya Mpango huo tulipata fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni 698.1 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Baadhi ya maeneo yaliyonufaika na miradi ya MCC-I ni Dodoma, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Kigoma, Mwanza, Manyara, Njombe, Geita na Zanzibar.

Ndugu wanahabari, orodha ya ziara za viongozi wakuu wa kitaifa na mashirika ya kimataifa wa ndani na nje katika kipindi cha miaka 60 ni ndefu na manufaa yake kwa nchi yetu ni makubwa. Kwa kutambua hilo, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imezipa msukumo ziara za kimataifa ambapo, tangu kuingia madarakani nchi yetu imepokea viongozi mbalimbali wa kitaifa na mashirika ya kimataifa.

Aidha, Mhe. Rais amefanya ziara katika nchi mbalimbali zenye manufaa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mfano, kufuatia ziara ya Mhe. Rais Samia nchini Kenya mwezi Mei 2021, Tanzania na Kenya zilikubaliana kuondoleana vikwazo vya muda mrefu visivyo vya kiforodha 46 kati ya 64. Hatua hiyo imechochea ukuaji wa biashara na uwekezaji baina ya nchi hizi mbili, ikiwemo Tanzania kuwa na urari chanya wa biashara baina yake na 13 Kenya. Taratibu za kuondoa vikwazo 18 vilivyosalia ambavyo ni vya kiutawala zinaendelea.

Ndugu wanahabari, ninatoa rai kwenu kuendelea kuuhabarisha na kuuelimisha umma wa watanzania na dunia kwa ujumla kuhusu manufaa ya ziara zinazofanywa na viongozi wetu wa kitaifa nje ya nchi pamoja na zara za viongozi kutoka mataifa mengine nchini.

**MAFANIKIO YA TANZANIA KATIKA KUKUZA MATUMIZI YA LUGHA YA KISWAHILI DUNIANI**

Ndugu wanahabari, historia inaonesha kuwa, lugha ya Kiswahili imetumika katika harakati za ukombozi na kupigania uhuru katika nchi za ukanda wa Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika ikiwemo Tanzania. Kiswahili pia kinazungumzwa kwa wingi katika nchi zenye uhusiano wa karibu wa kihistoria na nchi za mashariki mwa Afrika kama vile nchi ya Oman, kutokana na lugha hiyo kutumika kurahisisha ufanyaji wa biashara kabla na wakati wa ukoloni. Hata hivyo, nchi yetu imekuwa kinara katika matumizi ya lugha hiyo kiasi cha kutambulika kimataifa kama nchi waasisi wa lugha hiyo. Kwa kutambua manufaa ya lugha ya Kiswahili, Tanzania imeendelea kukuza na kueneza matumizi ya lugha hiyo Barani Afrika na duniani kwa ujumla. Kufuatia jitihada hizo, lugha ya Kiswahili sasa inakadiriwa kuwa ya tatu kwa kuwa na watumiaji wengi barani Afrika baada ya Kiingereza na Kiarabu, na ya kumi (10) duniani.

Ndugu wanahabari, katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru, Tanzania inajivunia lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi inayotumika katika mikutano ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Aidha, Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inakuwa lugha rasmi katika Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Mataifa, ambapo hadi sasa Kiswahili kinatumika kutafsiri mijadala katika mikutano ya wakuu wa nchi na serikali wa Umoja wa Afrika. Pia, Idhaa ya Kiswahili imeanzishwa katika Radio na Televisheni ya Umoja wa Mataifa. Vilevile, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) limeit

angaza tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa siku maalum ya kuadhimisha lugha ya Kiswahili duniani.

Halikadhalika, Serikali kupitia baadhi ya Balozi za Tanzania nje, imeanzisha madarasa ya kufundisha lugha ya Kiswahili katika ngazi za awali, kati na juu. Mfano Ubalozi wa Tanzania Seoul, Jamhuri ya Korea umefanikiwa kufundisha jumla ya wanafunzi 150 ambao ni raia wa nchi hiyo. Serikali pia imesaini makubaliano ya ushirikiano katika matumizi ya Kiswahili na Serikali za Afrika Kusini, Namibia, Ethiopia na Misri.

Ndugu wanahabari, kukua kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nchi nyingine, jumuiya za kikanda na kimataifa ni fursa ya ajira kwa watanzania katika kada mbalimbali zikiwemo ualimu na ukalimani. Vilevile, matumizi ya lugha hiyo kimataifa yanatoa fursa ya kukuza na kuimarisha uhusiano wa kijamii na kiuchumi baina yetu na nchi nyingine.

Ndugu wanahabari, tunaposherekea maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru, ninatoa rai kwenu kutumia taaluma yenu kukuza na kueneza matumizi ya lugha adhimu ya Kiswahili, ambayo pia ni urithi wetu, katika mataifa mengine duniani.

**MAFANIKIO YA TANZANIA KIUCHUMI KUPITIA UHUSIANO WA KIMATAIFA**

Ndugu wanahabari, Tanzania imepata mafanikio ya kiuchumi kupitia uhusiano baina yake na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa. Uhusiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na nchi nyingine unatokana na uwepo wa mikataba na makubaliano ya ushirikiano katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Mathalan, kupitia makubaliano ya ushirikiano katika biashara baina ya Tanzania na nchi za Oman, Qatar, Kuwait na Saudi Arabia, nchi yetu inauza mbogamboga, nyama na bidhaa za nyama katika masoko ya nchi hizo. Kadhalika, kupitia makubaliano ya hivi karibuni ya biashara kati ya Tanzania na China, kampuni 72 za kitanzania zimepata ithibati kutoka katika mamlaka za China kuuza maharage ya soya katika soko la nchi hiyo ambapo zaidi ya tani 120 za bidhaa hiyo tayari zimeuzwa nchini humo.

Ndugu wanahabari, kupitia ushirikiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na washirika wa maendeleo wanaojumuisha nchi na taasisi, Serikali imepokea misaada na mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mfano, Serikali ya India ilitoa mkopo wa masharti nafuu wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kusambaza maji katika miji mbalimbali hapa nchini. Vilevile, Serikali ya Kuwait kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (Kuwait Fund) ilitoa mkopo wa masharti nafuu wenye thamani ya Shilingi bilioni 117 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Chaya-Nyahua yenye urefu wa kilometa 85.4 mkoani Tabora, ambayo ujenzi wake umekamilika mwezi Machi 2021. Mfuko huo pia umefadhili mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Luiche lenye ukubwa wa ekari 3,000 mkoani Kigoma. Kadhalika, Tanzania na Umoja wa Ulaya (EU) zilisaini mikataba 6 ya msaada yenye thamani ya Shilingi bilioni 307.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za nishati, kilimo na uhifadhi wa mazingira.

Ndugu wanahabari, ni wazi kuwa, mifano niliyotaja ni michache ikilinganishwa na historia ndefu iliyopo ya ushirikiano kati ya Tanzania na washirika wa maendeleo, ambao umeisaidia Serikali kutekeleza miradi na program za maendeleo kwa lengo la kupunguza umaskini na kuongeza ustawi wa wananchi. Serikali inazishukuru nchi na taasisi washirika wa maendeleo kwa michango yao ya kifedha na utaalam. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita inaahidi kuendeleza na kukuza ushirikiano huo.

Ndugu wanahabari, vilevile, Tanzania ni mwanachama katika jumuiya za mtangamano wa kikanda, ambapo kupitia uanachama wake imenufaika na makubaliano ya kuondoleana vikwazo vya kiforodha na visivyo vya kiforodha katika biashara ya bidhaa na huduma. Mathalan, kupitia utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Afrika Mashariki (EAC) na Eneo Huru la Biashara la SADC, bidhaa za Tanzania zinauzwa katika nchi wanachama wa EAC na SADC bila kutozwa ushuru wa forodha. Serikali imeendelea kuwawezesha wafanyabiashara kunufaika na fursa za biashara katika mtangamano wa kikanda kwa kutoa vyeti vya uasili wa bidhaa ambavyo vinawasaidia kupata unafuu wa kodi kwa kutolipa ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazozalishwa nchini na zinazokidhi vigezo vya uasili wa bidhaa vya jumuiya hizo.

Kutokana na fursa hiyo, mauzo ya Tanzania katika jumuiya za EAC na SADC yamekuwa yakiongezeka na kuinufaisha nchi yetu kwa fedha za kigeni pamoja na ajira. Pia, kupitia utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, Tanzania imenufaika na mitaji, ujuzi na uhawilishaji wa teknolojia baina yake na nchi nyingine wanachama wa EAC. Kupitia utekelezaji wa itifaki hiyo, Watanzania wanaweza kupata ajira au kuanzisha biashara katika mojawapo ya nchi za EAC bila kubaguliwa na vivyo hivyo raia kutoka nchi nyingine za jumuiya wanaweza kupata ajira na kuwekeza nchini.

Ndugu wanahabari, Tanzania pia inanufaika na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kikanda katika sekta mbalimbali kama vile miundombinu ya usafirishaji, nishati, maji, afya na elimu. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa nchini kupitia ushirikiano wa kikanda ni Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Ziwa Victoria unaotekelezwa kupitia EAC katika Wilaya za Geita na Sengerema; Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kufua Umeme cha Rusumo (MW 80), unaotekelezwa kwa ubia baina ya Tanzania, Rwanda na Burundi; Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Bagamoyo-Tanga-Horohoro/Lungalunga-Malindi (Km 425) kati ya Tanzania na Kenya. Utekelezaji wa miradi hiyo, pamoja na kuimarisha mtangamano wa kiuchumi, pia inasaidia kuboresha ustawi wa wananchi na kufungua fursa za kiuchumi na kijamii.

Ndugu wanahabari, katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru

wa Tanzania Bara, nchi yetu imekuwa mstari wa mbele katika kupigania haki na usawa wa kiuchumi duniani kupitia majukwaa ya kimataifa kwa kupaza sauti na kushawishi mageuzi katika taasisi na mashirika ya kimataifa kama vile Shirika la Biashara Duniani. Dhamira ya Tanzania ni kutaka kuwepo kwa mazingira sawa ya kiuchumi duniani yatakayoziwezesha nchi zinazoendelea kustawi kiuchumi kupunguza pengo lililopo kati yao na nchi zilizoendelea. Vilevile, Tanzania imeshiriki kikamilifu katika kutekeleza program za maendeleo chini ya Umoja wa Mataifa ambazo zimekuwa na manufaa ya kiuchumi na kijamii.

## MCHANGO WA WATANZANIA WANAOISHI NJE YA NCHI (DIASPORA)

Ndugu Wanahabari, kwa kutambua mchango wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora), mnamo mwaka 2010 Serikali ilianzisha Kitengo cha Diaspora chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ajili ya kuratibu masuala yote yanayohusu Diaspora. Vilevile, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi yatakayochochea ushiriki wa Diaspora katika shughuli za maendeleo kwa kuchangia rasilimali fedha (mitaji), elimu, ujuzi na teknolojia. Vilevile, Diaspora ni kiungo muhimu cha kuitangaza nchi yetu kimataifa na kuhamasisha uwekezaji kutoka nje.

Ndugu Wanahabari, mchango wa Diaspora katika Taifa letu umeendelea kukua ambapo kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu ya Tanzania, fedha zinazoingizwa nchini na Diaspora (remittances) zimeongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 465.7 mwaka 2016 hadi Dola za Marekani milioni 497.9 mwaka 2019. Vilevile, Diaspora wamekuwa wakichangia katika sekta za afya, elimu na huduma nyingine za kijamii. Mathalani, kati ya mwaka 2015 na 2019 Watanzania wanaoishi Marekani na Uingereza wamefanikisha ziara takribani tano za kitabibu zilizofanyika Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, Diaspora wamekuwa mstari wa mbele katika kuitangaza lugha adhimu ya Kiswahili ulimwenguni kupitia ufundishaji wa lugha hiyo katika nchi mbalimbali. Mathalani, takwimu zinaonesha kuwa kuna vituo takribani 30 vya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na Utamaduni wa Mtanzania vinavyomilikiwa na kuendeshwa na Diaspora katika nchi za Afrika Kusini, Misri, Malawi, Uingereza, Zimbabwe, Ubelgiji, Comoro, Jamhuri ya Korea, Ufaransa na China.

## MAFANIKIO YA TANZANIA KATIKA MASUALA MENGINE MTAMBUKA YA KIMATAIFA

Ndugu wanahabari, Tanzania inajivunia miaka 60 ya kushiriki kikamilifu katika kutekeleza masuala mengine mtambuka ya kimataifa yakiwemo jinsia; uhifadhi wa mazingira na mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi; haki za binadamu na utawala bora; na mapambano dhidi ya rushwa, makosa yanayovuka mipaka (mfano biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu na dawa za kulevya). Katika miongo sita ya uhuru, nchi yetu imesaini na kuridhia mikataba ya kimataifa inayohusu utekelezaji wa masuala hayo mtambuka, hivyo kujijengea heshima na kutambulika na jumuiya ya kimataifa kwa mchango wake.

Ndugu wanahabari, Serikali imetenga eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 400,000 kama eneo tengefu sawa na asilimia 37 ya eneo lote la nchi kavu. Vilevile, Tanzania ni mshirika wa Itifaki ya Kyoto kuhusu Mapambano Dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi ya mwaka 1997, ambapo kwa kudhihirisha uthabiti wake na dhamira yake katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki kikamilifu katika Mkutano wa 26 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP26) uliofanyika mwezi Oktoba 2021 jijini Glasgow, Scotland. Kupitia mkutano huo, nchi yetu iliungana na nchi nyingine duniani kuzitaka nchi vinara wa uchafuzi wa mazingira kutekeleza kwa vitendo makubaliano ya kupunguza kiwango cha hewa ukaa wanachozalisha. Vilevile, Tanzania kwa kinywa kipana ilizitaka nchi zilizoendelea kutimiza ahadi zao za kuzisaidia nchi zinazoendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Ndugu wanahabari, Tanzania imepiga hatua katika utekelezaji wa masuala ya jinsia ambapo Serikali za awamu zote zimekuwa zikitoa kipaumbele kwa watu wa jinsia zote kushika nyadhifa za uongozi na maamuzi bila kujali kigezo cha jinsia. Hilo linajidhihirisha hivi sasa ambapo nafasi ya juu ya uongozi katika Serikali inashikiliwa na mwanamke, hatua ambayo imeifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache barani Afrika na nchi pekee katika Ukanda wa Mashariki mwa Afrika kuwa na kiongozi mkuu wa Serikali mwanamke. Aidha, kama nilivyoeleza awali wanawake wameshika nyadhifa za juu za uongozi na maamuzi katika mashirika ya kimataifa ambapo utumishi wao ni wa kutukuka, wenye tija na sifa kwa nchi yetu kimataifa.

Ndugu Wanahabari, Tanzania ni mwanachama wa Mpango wa Hiari wa Kujitathmini Kiutawala Bora wa Umoja wa Afrika (APRM). Vilevile, kupitia majukwaa ya kikanda na kimataifa Tanzania imeshiriki kikamilifu kushawishi na kusisitiza masuala ya utawalaprogram na miradi inayohusu masuala hayo mtambuka.

bora. Serikali ya Tanzania pia imeendelea kuaminika kimataifa kwa kuheshimu haki za binadamu, utawala wa sheria na demokrasia kutokana na kutekeleza sera, sheria, mipango, mikakati, program na miradi inayolenga kuongeza ustawi wa wananchi na kupunguza umaskini pamoja na kutoa uhuru wa kushiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Ndugu wanahabari, kadhalika, nchi yetu imekuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya rushwa na aina nyingine za uhalifu zikiwemo uharamia, utakasishaji wa fedha, ugaidi, usafirishaji haramu wa binadamu na dawa za kulevya, kupitia utekelezaji wa makubaliano baina yake na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na kimataifa. Kama kielelezo cha ushiriki thabiti wa Tanzania katika mapambano dhidi ya uhalifu wa kimataifa, nchi yetu ni mwenyeji wa Kituo cha Kupambana na Ugaidi cha SADC. Jitihada

hizo zimeipatia nchi yetu sifa nzuri na kutambulika kimataifa kama mshirika thabiti katika kupiga vita aina zote za uhalifu.

Ndugu wanahabari, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itaendelea kuheshimu makubaliano ya kimataifa kwa kutekeleza sera, mipango, mikakati, program na miradi inayohusu masuala hayo mtambuka.

**HITIMISHO**

Ndugu wanahabari, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, itaendelea kutekeleza sera, mipango na mikakati yenye lengo la kudumisha na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara katika uhusiano wa kimataifa. Baadhi ya malengo ya Serikali katika kipindi kijacho ni kukuza sauti ya Tanzania katika jumuiya za kikanda na kimataifa; kushiriki kikamilifu katika mikutano ya kikanda na kimataifa na kulipa michango yake ya uanachama; na kuendelea kuchangia juhudi za kulinda amani na usalama duniani na kutetea haki na usawa kwa kupinga mifumo kandamizi ya kiuchumi na kisiasa duniani.

Vilevile, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi nchini kuongeza ushiriki wake katika masuala ya kimataifa; kuweka mazingira wezeshi kwa Diaspora kuendelea kutoa mchango wao katika maendeleo ya Taifa; na kuendelea kuziwezesha Balozi zetu nje kutekeleza kikamilifu majukumu yake hususani diplomasia ya uchumi.
Ndugu Wanahabari, baada ya kusema hayo, ninawashukuru sana kwa mwitikio wenu, na ni matarajio yangu kuwa mtatumia vyombo vyenu vya habari kueneza taarifa ya mafanikio ya Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru kwa Wananchi na dunia kwa ujumla.
Ndugu Wanahabari, nimalizie kwa kuwasilimu tena kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania......Kazi iendelee!!!




## MIAKA 60 YA UHURU NA USTAWI KATIKA SEKTA ZA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Ndugu wanahabari, Tanzania ina eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 948,132.89. Eneo la nchi kavu lina ukubwa wa kilometa za mraba 886,100 ambapo Tanzania Bara ina kilometa za mraba 883,600 na Zanzibar ina kilometa za mraba 2,500. Aidha, kilometa za mraba 61,500 ni eneo la maji na maili za bahari 200. Tanzania ina jumla ya eneo la ardhi lenye ukubwa wa hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo na kati ya hizo ni hekta milioni 16 sawa na asilimia 36.3 zinazotumika kwa uzalishaji.

Sekta ya ardhi ina historia ndefu kuanzia kipindi cha kabla ya Uhuru wa Tanzania Bara mwaka 1961 hadi kufikia kipindi cha kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Taifa letu ifikapo tarehe 9 Desemba 2021. Aidha, sekta ya ardhi imepitia mabadiliko mbalimbali ya kisera, kisheria na kimuundo yakilenga kuiboresha sekta hii muhimu katika kuwawezesha wananchi kupata ardhi kwa gharama nafuu kwa ajili ya kuanzisha shughuli za kiuchumi, kijamii, na hivyo, kupunguza umaskini na kukuza pato la Taifa. Hivyo, katika awamu tofauti za uongozi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeendelea kuboresha sekta ya ardhi kwa kutunga na kusimamia Sera na Sheria mbalimbali, kuandaa kanuni na miongozo, kuandaa mikakati mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa milki salama za ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Pia, sekta ya ardhi imeendelea kuwa kiungo wezeshi kwa sekta nyingine za uzalishaji ikiwemo viwanda, kilimo, mifugo, miundombinu na maendeleo ya makazi.

Baada ya uhuru, Serikali ilirithi Sera na sheria za kikoloni zilizokua zinasimamia Sekta ya ardhi na makazi. Sera na sheria hizo zilikua za kibaguzi nao zilishindwa kukidhi matarajio ya nchi baada ya uhuru. Hali hiyo ilipelekea kufanyika kwa mabadiliko ikiwemo kutunga na kufanya mapitio ya Sera na Sheria hizo ili kukidhi mahitaji ya wakati huo ikiwemo kuwezesha wananchi kumiliki ardhi, kuwezesha wananchi kiuchumi na kupunguza migogogoro ya ardhi. Miongoni mwa Sheria zilizotungwa/kurejewa ni kama ifuatavyo:

i) Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995;

ii) Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000;

iii) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;

iv) Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya114;

v) Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138;

vi) Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216;

vii)Sheria ya Upimaji Ardhi, Sura ya 324;

viii) Sheria ya Usajili Wapima Ardhi, Sura ya 270;
ix) Sheria ya Utwaaji Ardhi, Sura ya 118;

x) Sheria ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116;

Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipangomiji, Sura ya 426; xii) Sheria ya Mipangomiji, Sura ya 355;

xiii) Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 334;

xiv) Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura ya 117;

xv) Sheria ya Umiliki wa Sehemu ya Jengo, Sura ya 416;

xvi) Sheria ya Usajili wa Rehani za Mali Zinazohamishika, Sura ya 210; na xvii)Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa, Sura ya 295.

Sera na Sheria hizi zimekua zikifanyiwa mapitio ili kuendana na mabadiliko yanayotokea ndani na nje ya nchi katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisayansi na teknolojia; kimazingira n.k. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha rasimu ya Sera ya Nyumba kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Ndugu wanahabari, katika miaka 60 ya uhuru, Tumepanga; Tumepima; Tumemilikisha; tumewawezesha wananchi kuwa na makazi bora; Tumeboresha mifumo; Tumetengeneza fursa za uwekezaji; Tumeweka mfumo mzuri wa utatuzi wa migogoro na tumesogeza huduma za ardhi karibu kabisa na wananchi.

Na sasa nitawaeleza moja badala ya jingine kwa kina: -
Ndugu wanahabari, baada ya uhuru na hususan baada ya kuanza kutumika kwa sheria nilizozitaja:
Tumeipanga ardhi yetu katika matumizi mbalimbali. Miji imesanifiwa na kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa ajili ya ustawi wa jamii katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kimazingira. Ili kukabiliana na ongezeko la watu nchini usanifu wa miji umewezesha kupatikana kwa huduma muhimu kwa wananchi na kukuza uchumi wa nchi.

Ndugu wanahabari, ongezeko la watu nchini limeendele kuongezeka tangu nchi ilipopata uhuru mwaka 1961. Kwa mujibu wa sensa ya kwanza kufanyika baada ya uhuru mwaka 1967, Tanzania ilikuwa na watu 12,313,469 ambapo asilimia 5.7 walikuwa wakiishi mjini na asilimia 94.3 vijijini. Katika kipindi cha miaka 60 ongezeko la watu nchini limefikia takribani watu 59,441,988 kwa makadirio ya mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 79.7. Kwa sasa inakadiriwa idadi ya watu wanaoishi mjini ni sawa asilimia 35 ya idadi ya watu. Ukuaji huu wa idadi ya watu umechagiza mahitaji makubwa ya matumizi ya ardhi iliyopangwa kwa shughuli za makazi, kilimo, ufugaji, miundombinu, uwekezaji na biashara.

Jumla ya michoro ya mipangomiji 21,844 yenye idadi ya viwanja 6,784,426 imesanifiwa kwa matumizi mbalimbali yakiwemo Makazi, Makazi Biashara, Taasisi, Viwanda, Maeneo ya Huduma za jamii, maeneo ya wazi n.k.

Jumla ya maeneo 496 yametangazwa kuwa ya kupangwa nchini. Kutangazwa kwa maeneo hayo kumewezesha kupangwa, kuendelezwa na kusimamiwa kimji kwa kuzingatia Sheria ya Mipangomiji Sura ya 355.

gatia Sheria ya Mipangomiji Sura ya 355.

Katika maeneo yalioendelezwa kiholela na ambayo yalikuwa ni mtaji mfu kwa wananchi tumerasimisha makazi 1,992,245 na kuwezesha wananchi hawa kuwa rasmi, usalama wa milki zao, na hadhi ya kukopesheka. Kuipanga ardhi kumewezesha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa azma ya Serikali ya kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu.

Katika kutimiza azma ya Serikali ya kuwa na ardhi ya uwekezaji, ardhi yenye ukubwa wa ekari 885,144 zilitengwa na kumilikishwa kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa shughuli mbalimbali ikiwamo viwanda, kilimo, hoteli na biashara. Pia ardhi yenye ukubwa wa ekari 224,439.4 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji kupitia Mipango Kabambe ya miji, mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya na Vijiji. ardhi iliyomilikishwa kwa wawekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZA) na ardhi ya akiba (Land Bank).

Ndugu wanahabari, mafanikio makubwa zaidi yaliyopatikana katika masuala ya upimaji ni upatikanaji wa vifaa vya kisasa na usimikaji wa miundombinu ya kisasa ya upimaji yenye kurahisisha upimaji. Miundombinu hii ipo sambamba na teknolojia za kisasa duniani. Tumebadili mfumo wa upimaji kutoka Mfumo wa zamani wa Arc 1960 ambao ulikuwa umejengwa juu ya mtandao hafifu wa alama za msingi za upimaji , kwenda mfumo mpya wa kisasa wa TAREF 11(Tanzania Reference Frame of 2011) ambao ni mfumo wa kimataifa unaowezesha upimaji kati ya nchi na nchi na wenye alama zenye usahihi wa hali juu.

Vile vile, tumesimika mtandao wa alama za msingi za mfumo huu nchi nzima katika kila mkoa na kila wilaya kwa umbali wa kilomita 40. Hii imewezesha kila mahali kupimwa bila ya kuwa na shida za alama za kuanzia. Aidha, mfumo huu umepunguza gharama za upimaji na kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi nchini.

Sambamba na usimikaji wa mfumo wa upimaji tumenunua vifaa vya upimaji vya kisasa na kuvisambaza katika mikoa yote na baadhi ya halmashauri. Hivyo kwa sasa kuna kasi kubwa ya upimaji wa ardhi na utoaji wa hati miliki. Tumeagiza vifaa vya kisasa vya kuandalia ramani za msingi kwa ajili ya kuwezesha utayarishaji na uchapaji ramani na tumeshanunua ndege isiyokuwa na rubani maalum kwa ajili ya upigaji picha za anga zinazowezesha uandaaji wa ramani za msingi na kuzifanyia marejeo. Kutokana na mfumo na vifaa vya kisasa, viwanja 2,783,278 na mashamba 28,784 yamepimwa nchini kote.

Na kwa sasa kasi imeongezeka zaidi, tumepeleka bilioni 50 katika halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya kupanga,kupima na kumilikisha ardhi.

Ndugu wanahabari, baada ya uhuru na hususan baada ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Ardhi (Sura 113) na Sheria ya Ardhi ya Vijiji (Sura 114) fursa ya raia wa Tanzania waishio mijini na vijiji kuwa na milki salama za ardhi imeongezeka ikilinganishwa na kabla ya uhuru.

Vilevile, wananchi waishio katika maeneo yasiyopangwa mijini milki zao zimetambuliwa kwa kupewa Leseni za Makazi.Wakati tunapata uhuru tulikuwa na miliki za ardhi 26,499. Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru tuna jumla ya miliki za ardhi 2,067,044 ambapo milki za ardhi katika ardhi ya jumla ni 1,615,365, vyeti vya ardhi ya kijiji 11,744 na Hati za Hakimiliki ya Kimila 867,148 zimetolewa. Aidha, Leseni za Makazi 112,787 zimetolewa kwa wananchi waishio katika maeneo yasiyopangwa mijini. Baadhi ya wananchi wanazitumia hati hizo kama dhamana kupata mikopo katika taasisi za fedha kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Sheria ya ardhi ya sasa inatambua kwamba ardhi ina thamani na imeweka ulinzi zaidi kwa wananchi wanaomiliki ardhi. Ardhi haitachukuliwa na Serikali bila ya fidia. Na katika kuhakikisha mwananchi analipwa fidia stahiki: -

1. Tumetunga Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ya mwaka 2016;
2. Tumeanzisha Bodi ya Uthamini kwa lengo la kusimamia utendaji wa Wathamini na Usajili wa Wathamini;
3. Tumewezesha ulipaji wa malipo ya fidia kwa miradi mbalimbali ya umma;
4. Tumeandaa miongozo ya uthamini, ikiwemo muongozo wa uthamini wa fidia; na 5. Uandaaji wa viwango vya bei ya soko la ardhi na mazao kwa ajili ya uanzishwaji wa kanzidata ya takwimu za uthamini (Valuation Database).

Ndugu wanahabari, mara tu baada ya kupata Uhuru mwaka 1961 Serikali ilianza kuboresha mazingira ya uendelezaji milki nchini pamoja na kuanzisha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) mwaka 1962 kwa sheria ya Bunge Na. 45 kwa lengo la kuwapatia wananchi makazi bora. Sawia na hatua hiyo, Serikali ilianzisha wakala wa Ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Serikali (TBA) na taasisi zingine za serikali zinajishughulisha na ujenzi wa ofisi na majengo mengine kwa shughuli mbalimbali za ofisi. Pia watu binafsi wanashiriki katika ujenzi wa nyumba za kuishi na biashara.

Shirika lina majengo 2,728 yenye sehemu ya nyumba (units) zipatazo 18,622 katika maeneo mbalimbali nchini na ina viwanja vipatavyo 2,561. Rasilimali hizi zinalifanya Shirika kuwa na utajiri wa mtaji (Capital base) wa shilingi trilioni 5. Nyumba za makazi ni asilimia 59 na za biashara ni asilimia 41. Katika jumla ya nyumba hizo, asilimia 59.3 ziko katika Jiji la Dar es Salaam. Nyumba hizi 18,708 zinaliingizia Shirika kodi ya wastani wa shilingi bilioni 8 kwa mwezi.

Kwa sasa Shirika linaendelea kujenga nyumba za kuuza, kupangisha na biashara karibu kila mkoa na wilaya. Kwa upande wa Mkoa wa Dodoma Shirika linakamilisha ujenzi wa nyumba 1,000 Jijini Dodoma.

Mwaka 1992, Serikali ilianzisha Mfuko wa Mikopo ya

Nyumba kwa Watumishi wa Serikali (Revolving Housing Loan Fund) ili kuwawezesha watumishi wa Serikali kupata mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kujenga nyumba za kuishi. Hadi sasa Serikali imetoa mikopo ya nyumba yenye thamani ya shilingi 9,159,902,229.85 kwa watumishi wa Serikali wapatao 1,689. Aidha, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuboresha makazi ya wananchi ilianzisha kampuni ya kutoa mikopo ya gharama nafuu kwa benki ili kuwezesha wananchi kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Hadi sasa jumla ya taasisi za kifedha 32 zinatoa mikopo kwa wananchi. Serikali imekwishatoa kiasi cha shilingi bilioni 474.5 kuwezesha wananchi katika ujenzi wa nyumba.

Ili kuboresha ustawi wa Jamii katika maeneo ya vijijini ambapo takribani asilimia 75 ya idadi ya watanzania wanaishi, Wizara imeandaa na kusambaza ramani za ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kuandaa mwongozo wa upangaji na ujenzi wa nyumba bora vijijini. Utekelezaji wa mwongozo huu utawezesha uboreshaji wa ubora wa nyumba katika maeneo ya vijijini.

Mwakani Serikali inatarajia kufanya sensa ya majengo yote nchini ili kupata taarifa ya majengo na kuiwezesha Serikali kupanga mipango endelevu ya kuboresha sekta ya nyumba nchini na kuboresha sera na sheria. Hivyo basi, natoa rai kwa wananchi wote kuandaa taarifa muhimu za umiliki wa maeneo yao na kutoa ushirikiano kwa makarani wote wa sensa watakapofika katika maeneo yenu kukusanya taarifa ya sekta ya nyumba.

Ndugu wanahabari, Mmsingi mkuu wa ulinzi wa haki za miliki za ardhi ni kumbukumbu. Katika kipindi cha miongo minne tangu Uhuru, Wizara ilikua inatumia mfumo wa majalada pekee katika kutunza kumbukumbu za ardhi (analogia). Mfumo huo ulihifadhi kumbukumbu za upimaji, ramani, mipango miji, uthamini, hatimiliki katika nakala ngumu. Hali hii ilisababisha uhitaji wa eneo kubwa la kuhifadhi majalada, muda mwingi wa kutafuta majalada, ongezeko la kero zinazotokana na milki pandikizi na mahitaji makubwa ya rasilimali watu na fedha.

Kwa kutambua changamoto hiyo, mwaka 2016:-
(i) Wizara ilijenga kituo cha kuhifadhi na kuchakata taarifa za ardhi. Kituo hicho kinalenga kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kutumia TEHEMA. Kituo kinahifadhi na kuchakata taarifa za ardhi za nchi nzima.

(ii) Wizara ilisanifu na kujenga Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (Integrated Land Management Information System - ILMIS) katika Jiji la Dar es Salaam (Manispaa zote) ambapo kumbukumbu zote za ardhi zimehifadhiwa kidijitali na hati za kielektroniki zinaendelea kutolewa kwa wamiliki. Aidha, usimikaji mfumo wa ILMIS katika Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Dodoma unaendelea kukamilishwa pamoja na uingizaji wa taarifa muhimu za wamiliki ardhi.

Mfumo wa ILMIS unaunganisha kwa njia ya kieletroniki utendaji kazi wa Uthamini, Mipangomiji, Upimaji na Ramani; Utawala wa Ardhi na Usajili wa Hati kwa kuratibu mtiririko wa miamala inayofanyika kuanzia ngazi ya Halmashauri, ofisi za Ardhi za Mikoa na Ofisi ya Makao Makuu. Mfumo huu pia unarahisisha utendaji kazi, kuharakisha mchakato wa utoaji wa milki, kuimarisha usalama wa milki, kuondoa ugumu wa kupata taarifa sahihi kwa wakati, kuongeza mapato ya Serikali, kuongeza uwazi na kuleta dhana ya kwa watumishi wa Sekta ya Ardhi kwa kuwa ufuatiliaji wa miamala umerahisishwa.

Aidha, mfumo huu umewezeshwa kutoa huduma za kiganjani katika ukusanyaji taarifa za ardhi na huduma kwa wateja. Inatarajiwa kuwa maboresho haya yatakuwa yamekamilika ifikapo Juni 2022 katika Jiji la Dodoma.

Mfumo huu unawezesha muamala wa milki kukamilika baada ya saa moja ikiwa kuna taarifa sahihi na hatua za muamala zinatekelezwa kwa mfululizo. Aidha, Mfumo huu unasaidia kutoa huduma kwa uwazi, kuondoa umilikishaji wa kiwanja kimoja kwa zaidi ya mtu mmoja na kutoa huduma kwa haraka na kwa usahihi.

Mfumo huu utakuwa unasimikwa kwa awamu na kuenezwa katika Ofisi zote za ardhi za mikoa na halmashauri nchini.

Ndugu wanahabari, baada ya uhuru, utatuzi wa migogoro ya ardhi ulikuwa unafanyika kupitia mabaraza ya kimila na mfumo wa mahakama za kawaida. Hata hivyo, utatuzi wa migogoro ya ardhi kupitia mfumo wa mahakama ulibainika kuwa na changamoto za mrundikano wa mashauri na matumizi ya mbinu nyingi za kisheria katika utatuzi wa migogoro. Kutokana na changamoto hizo, Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 ilielekeza uanzishwe mfumo mahsusi wa utatuzi wa migogoro ya ardhi. Hivyo, Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 (Sura ya 216) ilitungwa na kubainisha mfumo maalum wa utatuzi wa migogoro ya ardhi unaojumuisha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Mabaraza ya Kata, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa. Tangu kutungwa kwa sheria hiyo mwaka 2002, jumla ya mashauri 214,588 yalifunguliwa na mashauri 187,618 yameamuliwa. Aidha, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yameanzishwa katika Wilaya zote 139 ambapo kati ya hayo, Mabaraza 60 yanatoa huduma. Dhamira ya Wizara ni kuhakikisha kuwa Mabaraza katika Wilaya zote nchini yanatoa huduma.

Aidha, Wizara imeendelea kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero kubwa nchini kadri inavyojitokeza kwa njia ya kiutawala Migogoro hiyo ipo katika sura mbili ambazo ni migogoro ya mipaka ya kiutawala na migogoro inayotokana na mwingiliano wa matumizi ya ardhi. Aidha, kupitia tathmini iliyofanyika imebainika kwamba vyanzo vya migogoro ni pamoja na ongezeko la watu, na mwingiliano wa matumizi ya ardhi kutokana na mahitaji mbalimbali ya watumiaji. Wizara imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kushughulikia utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu utatuzi wa migogoro kwa

kushirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa, kuanzisha madawati ya malalamiko katika ofisi za ardhi za halmashauri nchini pamoja na programu ya 'Funguka kwa Waziri'. Jumla ya migogoro 149,081 imetatuliwa kiutawala.

Kutokana na kukithiri kwa migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya makundi mbalimbali nchini Serikali iliunda Kamati ya Mawaziri ya Kisekta ya Wizara Nane.

(8) mwaka 2018 inayojumuisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI); Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira); Maliasili na Utalii; Mifugo na Uvuvi; Kilimo; Maji; na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa migogoro hiyo. Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo na kuridhiwa na Baraza la Mawaziri mwezi Septemba, 2019 ni kuhalalishwa rasmi kwa vijiji 920 kati ya vijiji 975 vilivyokuwemo ndani ya hifadhi, mapori ya akiba na ranchi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na kijamii. Kwa sasa hatua za utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri zinaendelea ambapo Mawaziri wa Kisekta wanaendelea kufanya ziara kwenye mikoa husika kutoa taarifa ya maamuzi ya serikali pamoja na kufanya tathmini uwandani kwenye maeneo ambayo yanahitaji hatua zaidi za utatuzi.

Ndugu wanahabari, mwaka 2007 Wizara ilianzisha Ofisi za Ardhi za Kanda nane (8). Pamoja na kuanzishwa kwa ofisi hizo, Wizara iliona kuna umuhimu wa kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi hivyo mwaka 2020 Serikali ilianzisha Ofisi za Ardhi za Mikoa 26 zinazoongozwa na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi. Ofisi hizo zinatoa huduma zote za upangaji, upimaji na ramani, umilikishaji, uthamini na usajili wa hati na nyaraka na huduma nyingine za ardhi kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji (Halmashauri). Huduma za Usajili wa Hati na Nyaraka inajumuisha (i) Usajili wa Miamala ya Hatimiliki; mathalan, reheni, pango, usajili wa wasimamizi wa mirathi na warithi n.k na (ii) Usajili wa nyaraka; mathalan, Hati za kutoa mamlaka, Hati za kubadilisha majina n.k.

Kuanzishwa kwa ofisi hizo kumewezesha wananchi kupata huduma za ardhi karibu na maeneo yao, kwa wakati na pia kupunguza gharama za kupata huduma hizo. Ili kuimarisha usimamizi wa sekta ya ardhi kwa ufanisi zaidi, mwaka 2018 Serikali iliwahamisha watumishi wa sekta ya ardhi waliokuwepo katika halmashauri mbalimbali kuwa chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kiutendaji maafisa hao wanafanya kazi kwa karibu za mamlaka za upangaji ambazo ni Halmashauri.

Pamoja na kusogeza huduma kwa wananchi tumechukua hatua mbalimbali kuhakikisha wananchi wanapata huduma Bora.

i) Tumeanzisha Kamati ya Maadili na Kudhibiti uadilifu kwa kuzingatia matakwa ya Mkakati wa Taifa wa Mapamabano dhidi ya Rushwa awamu ya 3 (National Anti-Corruption Strategy Phase III) za Mwaka 2018 na kuendelea kuwachukulia hatua kali za kinidhamu watumishi wanaojihusisha ma masuala ya rushwa;

Tumeimarisha usimamizi wa watumishi kuanzia ngazi ya Makao Makuu, Mikoa ishirini na sita (26) na Halmashauri zote 184;

Tumepanga upya watumishi wa sekta ya ardhi kwa madhumuni ya kuwa na uwiano kwa kada zote muhimu ili kukudhi utoaji wa huduma kwa wananchi;

Tumeanzisha Bodi za Kitaaluma ili kudhibiti utendaji na maadili katika taaluma za kada za sekta ya Ardhi (Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini na Halmashauri ya Wapima Ardhi);

v) Tumeweka Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Client Service Charter) kwa madhumuni ya kujenga dhana ya uwajibikaji dhidi ya wateja kwenye huduma zote za Sekta ya Ardhi zinazotolewa; na

vi) Tumeboresha muundo wa Wizara katika kusimamia majukumu yake ambapo baadhi ya Idara na Vitengo zimeimarishwa na kupandishwa hadhi ili kuongeza ufanisi.

Ndugu wanahabari, umilikishaji wa ardhi kwa wananchi umewapa fursa wananchi kuchangia pato la Taifa. Wizara inakusanya maduhuli ya sekta ya ardhi kutoka katika vyanzo mbalimbali kama vile: - Kodi ya Pango la Ardhi; Ada za Upimaji wa Ardhi na Machapisho Mbalimbali; Ada ya Uthamini; Ada za Usajili wa Hati na Nyaraka Mbalimbali. Mwaka 1996/97 wakati Wizara ya Ardhi tulipopewa mamlaka ya kukusanya maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi tulikusanya shilingi bilioni 1.4.

Kwa miaka 10 ya hivi karibuni (Juni, 2011 hadi Jalai, 2021) tumekusanya jumla ya shilingi bilioni 735.8. Hivyo, maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi yameongezeka kutoka shilingi bilioni 1.4 kwa mwaka wa fedha 1996/97 hadi kufikia shilingi bilioni 121 katika mwaka wa fedha 2020/21. Na kwa mwaka huu (2021/2022) tuna malengo ya kukusanya bilioni 221. Matarajio ni kuhakikisha sekta hii inachangia zaidi katika pato la Taifa ikiwemo mapato ya kodi.

Sekta ya ardhi ni miongoni mwa sekta muhimili katika kuwezesha sekta nyingine katika uzalishaji mali, kukuza pato la Taifa na kuleta maendeleo ya wananchi kiuchumi na kijamii. Mwelekeo wa sekta hii katika kipindi cha miaka ijayo ni kuwahakikishia wananchi na taasisi zote nchini usalama wa milki zao kwa kuwapatia hatimiliki za ardhi na huduma zingine muhimu za ardhi na hivyo, kudhibiti migogoro baina ya watumiaji ardhi. Azma hii itafikiwa kwa kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2020-25 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2021/22- 2025/26.




MAFANIKIO YA OFISI YA WAZIRI MKUU

KATIKA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

## 1.0. HISTORIA YA OFISI YA WAZIRI MKUU

a) Chimbuko la Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa ni Ofisi ya Waziri Kiongozi (Chief of Ministers) iliyoanzishwa na Serikali ya Kikoloni baada ya Uchaguzi Mkuu wa Pili wa Tanganyika uliofanyika mwaka 1960. Katika uchaguzi huo, Chama cha TANU kilishinda viti vingi vya uchaguzi kwenye Baraza la kutunga Sheria na Waziri Kiongozi wa kwanza katika Serikali hiyo alikuwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyeapishwa tarehe 03 Septemba, 1960 kuwa Waziri Kiongozi, Uchaguzi huu ulikiwa ni maandalizi ya kukabidhi madaraka kwa Watanganyika kutoka utawala wa Waingereza.

b) Ofisi ya Waziri Kiongozi ilikoma rasmi kupitia Tangazo la Serikali Namba 415 la tarehe 1 Desemba 1961 na kuanzishwa Ofisi mpya ya Waziri Mkuu. Siku ya Uhuru tarehe 09 Desemba 1961 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliapishwa kuwa Waziri Mkuu wa Kwanza wa Tanganyika akichukua nafasi ya kuongoza Serikali kutoka utawala wa Gavana wa kiingereza, Sir Richard Turnbull. Hata hivyo, Kiongozi wa nchi aliendelea kuwa Malkia wa Uingereza hadi mwaka tarehe 9 Desemba, 1962 Tanganyika ilipokuwa Jamhuri

## 2.0 UONGOZI WA OFISI YA WAZIRI MKUU

Katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru, tangu kuanzishwa rasmi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu viongozi wafuatao wameongoza Ofisi hiyo;

a. Mawaziri Wakuu 11;
b. Mawaziri wa Nchi 23;
c.Mawaziri Wadogo wanne (4) na Naibu Mawaziri watano (5);
d. Makatibu Wakuu 18; na
e. Naibu Makatibu Wakuu 17.

Kwa muhtasari historia ya Mawaziri Wakuu kuanzia mwaka 1961 hadi 2021 ni kama ifuatavyo: -

i. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Mwaka 1961 hadi 1962;
ii. Rashid Mfaume Kawawa Mwaka 1962 (Februari – Desemba) na pia mwaka 1972 hadi mwaka 1977
iii. Tarehe 9 Desemba 1962 Nafasi ya Waziri Mkuu ilivunjwa na kurudishwa mwaka 1977
iv. Edward Moringe Sokoine mwaka 1977 hadi 1980 pia mwaka 1983 hadi 1984;
v. Cleopa David Msuya mwaka 1980 hadi 1983 pia mwaka 1994 hadi 1995;
vi. Salim Ahmed Salim mwaka 1984 hadi 1985;
vii. Joseph Sinde Warioba mwaka 1985 hadi 1990;
viii. John Samwel Malecela mwaka 1990 hadi 1994;
ix. Frederick Tluway Sumaye mwaka 1995 hadi 2005;
x. Edward Ngoyai Lowassa mwaka 2005 hadi 2008;
xi.Mizengo Peter Pinda mwaka 2008 hadi 2015; na
xii. Kassim Majaliwa Majaliwa mwaka 2015 hadi sasa.

Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru Taifa letu litawakumbuka Viongozi hawa kwa mambo yafuatayo;

a) Kupigania Uhuru;
b) kusimamia mpango wa kugawa madaraka kwa waafrika (Maarufu kama operation vijiji ya mwala 1975);
c) Walisimamia utekelezaji wa misingi ya Azimio la Arusha mwaka 1977;
d) kuanzisha maduka ya vijiji ;
e) Kusimamia vita baina ya Tanzania na Uganda (Vita ya Kagera) ilioanza mwaka 1978 na kuisha mwaka 1979;
f) kuanzisha vita ya uhujumu uchumi na wakwepaji kodi (Mwaka 1983, 1984);
g) Kuhamasisha Kampeni ya nguvu Kazi;
h) Kusimamia uanzishwaji na utekelezaji wa Elimu kwa wote;
i) Kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango;
j) Kuanzisha na kutunisha mfuko wa nguvu kazi;
k) kuanzisha usafiri wa daladala katika Jiji la Dar es salaam miaka ya 80;
l) Kuelekeza siku ya jumamosi kuwa siku ya mapumziko ili Wafanyakazi watumie siku hiyo kushiriki katika mashamba ya umoja na shughuli za uzalishaji mali;
m) Kuanzisha viwanda vya msingi mfano Kiwanda cha Karatasi Mgololo, Mang'ula, Machine Tools Moshi, UFI na vingine vingi;

n) Kusimamia Sera za Fedha zilizotutoa kutoka kwenye uchumi hodhi kwenda kwenye uchumi huru
o) Kushiriki katika utatuzi wa migogoro Barani Afrika;
p) Kushiriki katika harakati za Ukombozi na Uhuru wa Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika;
q) Kusimamia na kuwezesha Wananchi wa kipato cha chini kupata mahitaji ya msingi;
r) Kutilia mkazo masuala ya kilimo pamoja na kuanzisha Sera ya kuhifadhi chakula kwa kujenga Maghala hadi vijijini;
s) Kusimamia urejeshwaji wa mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa (1992);
t) Walisimamia kuundwa kwa Tume ya Jiji la Dar es salaam iliyoleta mabadiliko makubwa ya kimuundo na kiutendaji katika Jiji la Dar es salaam
u) Kusimamia uanzishwa wa Mpango wa Maendeleo ya Shule za Msingi pamoja na Shule za Sekondari
v) Kusimamia uanzishwaji wa zahanati katika kila Kijiji na vituo vya Afya kwenye kila Kata
w) Kusimamia uanzishwaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo;
x) Kusimamia uanzishwaji wa Mpango wa Elimu ya Sekondari;
y) Kusimamia uanzishwaji na utekelezaji wa Mpango wa Kilimo Kwanza (Pinda)

z) Kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya uanzishwaji wa viwanda, uendelezaji wa mazao ya kimkakati, masoko pamoja na ujenzi wa miundombinu. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri Wakuu wote walioongoza nchi yetu katika kipindi chote cha miaka 60.

Aidha, kipekee Ofisi ya Waziri Mkuu tunamshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa uongozi wake mahiri na utendaji kazi mzuri. Tunamshukuru kwa mchango wake mkubwa katika kuhimiza uzalishaji wa Mazao ya Kimkakati mfano Chai, Kahawa, Korosho, Pamba, Tumbaku Mkonge, Chikichi, Alizeti Zabibu, na Parachichi. Mchango huo umesaidia kufufua mazao hayo

ya kibiashara na kuwanufaisha Watanzania walio wengi waliojiajiri kwenye kilimo; tunamshukuru kwa kuhimiza uchapa kazi kwa Viongozi na Watendaji wa Umma kutokana na kuzuru maeneno yote ya nchi hii ya Tanzania Bara na Zanzibar. Vilevile, amekuwa akisimamia kwa vitendo matumizi ya fedha za Serikali katika ngazi zote na hasa kwenye Halmashauri ili thamani ya fedha za Wananchi ionekane sambamba na kuwataka viongozi waguswe na matatizo ya wananchi akihimiza wananchi kufuatwa kwenye maeneo yao, kusikilizwa na kuhudumiwa. Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa amewezesha utekelezaji wa shughuli za Serikali Bungeni kwa mafanikio makubwa na amekuwa mstari wa mbele katika kuimarisha Muungano wa Tanzania Bara na Zanzibar kwa kufanya ziara na mikutano mbalimbali upande wa Zanzibar ambayo imezidisha na kuimarisha zaidi Muungano.

## 3.0 MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU

Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Hati Idhini ya Mgawanyo wa Majukumu ya Mawaziri iliyotolewa tarehe 7 Mei, 2021 kupitia Tangazo la Serikali Na. 385. Kwa mujibu wa Hati hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu ina majukumu yafuatayo;

a) Uratibu wa Shughuli za Serikali;
b) Kuongoza Shughuli za Serikali Bungeni;
c) Kuwa kiungo kati ya Vyama vya Siasa na Serikali;
d) Kuratibu Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa;
e) Kusimamia na Kuratibu Shughuli za Dharura na Maafa;
f) Uwezeshaji na Utekelezaji wa Mipango ya Uendelezaji wa Mji wa Dodoma na Makao Makuu ya Tanzania na Kuratibu Uhamiaji wa Serikali Dodoma;
g) Kuchapisha Nyaraka za Serikali;
h) Kuratibu Shughuli za Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI;
i) Kuratibu Shughuli za Kudhibiti Uingizaji, Biashara na Matumizi ya Dawa za Kulevya;
j) Kusimamia Utekelezaji wa Sera na Sheria za Kazi;
k) Kuratibu Utekelezaji wa Sheria na Mikakati ya Kukuza Ajira na Kutoa Huduma za Ajira ili Kuongeza nafasi za ajira kwa Watanzania ndani na nje ya nchi;
l) Kusuluhisha na kuamua migogoro inayotokana na kazi;
m) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera na Mikakati ya maendeleo ya Vijana;
n) kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sheria za Hifadhi ya Jamii;
o) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu;

p) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya fidia kwa wafanyakazi;
q) Kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri;
r) Kusimamia masuala ya Usalama na Afya mahala Pa kazi; na
s) Kusimamia Taasisi za Umma zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

## 4.0 SERA, SHERIA NA MIONGOZO INAYOSIMAMIWA NA OFISI YA WAZIRI MKUU

Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza jukumu la msingi la kuratibu utekelezaji wa Sera zote za Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 52 (1-3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Pamoja na jukumu hilo la uratibu, Ofisi inasimamia moja kwa moja utekelezaji wa Sera, Sheria na miongozo ifuatavyo:-

a) Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2001;
b) Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004;
c) Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008;
d) Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003;
e) Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004;
f) Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007;
g) Sera ya Taifa ya Usalama n a Afya Mahali pa Kazi mwaka 2010.

## 4.2 SHERIA

a)Sheria ya Menejimenti ya Maafa, Na. 7 ya 2015 - (The Disaster Management Act, No. 7/2015);
b) Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419 - (The National Leaders Funerals Act, Cap.419); Marekebisho yalifanyika 2019;
c) Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 - (The Drug Control and Enforcement Act, (CAP.95); Marekebisho yamefanyika 2021;
d) Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 - (The National Elections Act, Cap 343);
e) Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 mwaka 1992 kama ilivyorekebishwa 2019, - (The Political Parties Act, Cap 258 );
f) Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278 - (The Elections Expenses Act, Cap 278);
g) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Virusi vya Ukimwi, Sura ya 431 - (The HIV and AIDS (Prevention and Control) Act, Cap 431); Marekebisho yalifanyika 2019;
h) Sheria ya Tume ya Ukimwi, Sura ya 379 - (The Tanzania Commission for AIDS Act, Cap 379); Marekebisho yalifanyika 2015;
i) Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Na. 1 ya Mwaka 2015 – (The Non-Citizen (Employment Regulations), Act, No.1 of 2015); kama ilivyorekebishwa Mwaka 2021;
j) Sheria ya Taifa ya Kukuza Huduma za Ajira, Na. 9 ya mwaka 1999 - (National Employment Promotion Services Act, No.9 of 1999);
k) Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Na. 9 ya mwaka 2010 - (The persons With Disability Act No. 9 of 2010);
l) Sheria ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135 – (The Social Security Act, Cap 135); kama ilivyorejewa Mwaka 2019;
m) Sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Na. 2 ya mwaka 2018 - (The Public Service Social Security Fund Act, No.2 of 2018);
n) Sheria ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50 - (The National Social Security Fund Act, Cap 50);
o) Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 – (The Workers Compensation Act, Cap 263); kama ilivyorekebishwa 2021;

p) Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, Sura ya 297 - (The Occupational Health and Safety Act, Cap 297 ya mwaka 2003.
q) Sheria ya Taasisi za kazi, sura 300 kama ilivyorejewa mwaka 2019.
r) Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini, sura 366 kama ilivyorejewa mwaka 2019.
s) Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania Na. 12 ya mwaka 2015.

**4.3 MIONGOZO**

a) Mwongozo wa Taifa wa Menejimenti ya Maafa wa Mwaka 2014;
b) Mwongozo wa Taifa wa Utambuzi wa Mapema na Afua Stahiki kwa Watoto Wenye Ulemavu wa Mwaka, 2021;
c) Mwongozo wa uwekezaji wa fedha za wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;
d) Mwongozo wa kuandikisha wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;
e) Mwongozo wa usimamizi wa hadhari;
f) Mwongozo wa kusimamia uthamini wa mifuko ya hifadhi ya jamii;
g) Mwongozo wa utunzaji wa taarifa za wanachama;
h) Mwongozo wa gharama za uendeshaji;
i) Mwongozo wa uendeshaji mikutano ya mwaka;
j) Mwongozo wa mwenendo wa shughuli za Bodi ya Wadhamini;
k) Mwongozo wa ujumuishaji wa vipindi vya uchangiaji (totalization of benefits);
l) Mwongozo wa Kuwafikia Watumiaji wa Dawa za Kulevya katika Maeneo yao na Kuwapatia Elimu, Ushauri Nasaha pamoja na Upimaji wa VVU ili Kufahamu Kiwango cha Maambukizi Miongoni Mwao;
m) Mwongozo wa Uanzishaji wa Vituo vya Tiba kwa Watumiaji wa Dawa za Kulevya Nchini;
n) Mwongozo wa Madaktari wa Utoaji Huduma za Dawa kwa watumiaji wa Dawa za Kulevya;
o) Mwongozo wa Stadi za Maisha kwa Vijana walio nje ya Shule;
p) Mwongozo wa Huduma za Ajira;
q) Mwongozo wa Kitaifa wa Utarajali (Internship);
r) Mwongozo wa Kitaifa wa Uanagenzi (Aprenticiaship);
s) Mwongozo wa kufanya tathmini ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;
t) Mwongozo wa Uwekezaji wa Fedha katika Mifuko ya Hifadhi Jamii;
u) Mwongozo wa Utunzaji wa Taarifa za Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;
v) Mwongozo wa Ukaguzi katika maeneo ya Kazi;
w) Mwongozo wa Maadhimisho na Shughuli za Kitaifa;
x) Mwongozo wa Ziara za Viongozi Mikoani;
y) Mwongozo kwa Waajiri wa kukuza usawa na kuondoa ubaguzi sehemu za kazi;
z) Mwongozo kwa waajiri kuhusu masuala ya UKIMWI na VVU sehemu za kazi;

aa) Muongozo wa Shughuli za Mwenge wa Uhuru na
bb) Muongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana;
cc) Mwongozo wa Ukaguzi wa mwaka (Labour Inspection Manual);
dd) Mwongozo kwa Waajiri wa kukuza usawa na kuondoa ubaguzi sehemu za kazi;
ee) Mwongozo kwa Waajiri wa masuala ya UKIMWI / VVU sehemu za kazi;

**4.4 MIKAKATI**

a. Mkakati wa Kitaifa wa kupambana na utumikishwaji wa mtoto;
b. Mkakati wa Kukuza Ujuzi;
c. Mkakati wa Mawasiliano Wakati wa Dharura; na
d. Mkakati wa kitaifa wa kukuza fursa za ajira.

**5.0 MAFANIKIO YA OFISI YA WAZIRI MKUU KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 60 YA UHURU**

Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kipindi cha miaka 60 ya Uhuru imepata mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo: -

5.1 Kuimarisha Mifumo ya TEHAMA

Katika kuimarisha na kuboresha utekelezaji wa majukumu yake, Ofisi ya Waziri Mkuu imefanikiwa kufanya mabadiliko makubwa ya kiutendaji kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, lengo likiwa ni kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza tija katika utendaji wa Idara, Vitengo na Taasisi za Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla. Mifumo hiyo ni ifuatayo;

a) Mfumo wa Kielektroniki wa Uandikishaji Wapiga Kura (Biometric Voters Registation System – BVR) pamoja Mifumo mingine.

Kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa uandikishaji wapiga kura, (Biometric Voters Registration System-BVR); Mfumo wa utambuzi wa alama za vidole (Automatic Fingers Identification System - AFIS); mfumo wa usimamizi wa matokeo (Result Management System- RMS), Mfumo wa uandikishaji wagombea (Candidate Management System - CMS). Mifumo.

mingine ni Mfumo wa uhakiki wa taarifa za mpiga kura (Voter interaction System - VIS) na mfumo wa watazamaji wa uchaguzi (Observers Management System – OMS);
b) Mfumo wa Kielektroniki wa kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kwa raia wa kigeni.

Kusimamia, kuboresha na kusanifu Mfumo wa eVibali. Mfumo huu umepunguza muda wa kushughulikia maombi ya kibali kutoka siku za kazi 14 zilizopo kisheria hadi siku 7 kutokana na kupungua kwa hatua za uombaji wa kibali kutoka hatua 33 hadi hatua 3 pekee. Aidha, Mfumo huu umeunganishwa na Mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na inategemewa Taasisi nyingi zaidi za Serikali zitaendelea kuunganishwa na Mfumo huu. Mafunzo kuhusu utumiaji wa Mfumo yametolewa kwa watendaji wa ndani na nje ya Serikali. Aidha, mfumo umeimarisha uwazi na uwajibikaji, kupunguza urasimu na vihatarishi vya rushwa katika kushughulikia vibali.

c) Mfumo wa Kielektroniki wa Uratibu na Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali (Dashboard), Mfumo huu umeandaliwa maalum ili kuwajibisha watendaji ndani ya Serikali, pia kuimarisha uwajibikaji wa pamoja wa Serikali katika kutekeleza shughuli mbalimbali zilizoainishwa katika maeneo yafuatayo:

i. Uratibu na ufuatailiaji wa utekelezaji wa Shughuli za Serikali;
ii. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Sera, maagizo ya Viongozi wa Kitaifa, Ahadi za Mgombea Urais; na
iii. Umewezesha upatikanaji wa uhakika wa takwimu sahihi kwa wakati.

d) Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kaguzi Mahala Pa Kazi Nchini
Mfumo huu umeanzishwa kupitia Sheria ya Usalama na Afya Mahala Pa Kazi ambapo Mfumo huu unawapa uwezo waajiri kusajili maeneo ya kazi, kupata cheti cha usajili, kuomba mafunzo, kutoa taarifa za ajali, kuwasilisha nyaraka za kujifanyia tathmini ya hali ya usalama na afya ya maeneo yao ya kazi wakiwa katika maeneo yao ya kazi. Kupitia Mfumo huu waajiri wanaweza kujifanyia tathmini ya namna walivyokidhi viwango vya usalama na afya (Self Assesment) na hivyo kurahisisha upatikanaji wa leseni ya kukidhi viwango vya usalama na afya;

e) Mfumo wa Kielektroniki wa PSSSF Kiganjani
Mfumo huu una maeneo mawili, eneo la Wanachama na eneo la waajiri. Mfumo huu unatoa fursa kwa mwanachama ya kupata taarifa ya mwajiri kuhusu mawasilisho ya michango ya wanachama, usajili na madeni ya michango yake ambayo haijalipwa. Pia unarahisisha upatikanaji wa taarifa za michango ya wanachama, unarahisisha ufuatiliaji wa malipo ya Pensheni ya kila mwezi kwa mwanachama.

f) Mfumo wa Kielektroniki wa WCF wa WCFePG.
Mfumo huu unatumika kusajili ulipaji wa michango. Katika kulipa michango moduli ya WCFePG umewezesha mwajiri kuingiza wafanyakazi na payroll yake katika mfumo wa WCFePG, kuandaa orodha ya malipo na kutengeneza control number. Aidha huchaua njia ya kulipa michango kwa Benki au simu na akishalipa hupata risiti.

g) Mfumo wa Kielektroniki wa Huduma za Ajira
Mfumo utawezesha vijana wanaotafuta kazi ndani na nje ya Nchi kuhudumiwa kwa ufanisi, mfumo utawezesha waajiri na wawekezaji kupata vijana wa kitanzania walioandaliwa vizuri kufanya kazi kwa weledi katika soko la Ajira. Aidha mfumo huu utawaunganisha wadau muhimu wa Sekta ya ajira kama vile Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) na Mawakala Binafsi wa Huduma za Ajira.

5.2 Kuratibu Serikali kuhamia Dodoma
Ofisi ya Waziri Mkuu imefanikiwa kutekelza azma ya baba wa taifa Hayati Julius kambarage Nyerere ya kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Dodoma aliyoku wa nayo toka mwaka 1973. Mpaka sasa Serikali imefanikiwa kufanya yafuatayo katika kuhamisha Serikali kuja Dodoma;
a. Kuanzisha kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) mwaka 1978 ambapo majukumu yake yalihamishiwa kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma mwaka 2016.
b. Kutungwa kwa Sheria ya tamko la Kuitambua Dodoma kama makao makuu ya Nchi ya Mwaka 2018 (The Capital City Decraration Act, 2018)
c. Kuanzia mwaka 2016 hadi sasa, Ofisi ya Waziri Mkuu imeratibu kuhamisha Ofisi za Serikali na Watumishi 18,300 kutoka Dar es salam kuja Dodoma. Zoezi linaendelea;
d. Kuratibu ujenzi wa Ofisi za Wizara na Taasisi katika Mji wa Serikali Mtumba kwa awamu ya kwanza na kuanza awamu ya pili ya ujenzi;
e. Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya maji taka na maji safi, barabara, njia za chini za umeme, mawasiliano, ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi, mkongo wa mawasiliano.

f. Kukamilika kwa Mpango Kabambe wa Mji wa Serikali.

5.3 Mafanikio katika usimamizi katika Sekta ya Kazi na Ajira

Katika eneo hili, Ofisi ya Waziri Mkuu imefanikiwa katika maeneo yafuatayo;

a) Kufanikiwa kufanya utafiti wa Watu wenye uwezo wa kufanya Kazi mara sita ambapo mara ya kwanza ulifanyika mwaka 1965 kisha kufanyika tena Mwaka 1991, 2001, 2006, 2014 na 2021. Tafiti hizi ziliiwezesha Serikali kupata viashiria muhimu vya soko la ajira, ambavyo ni nyenzo humu ya kimkakati katika kuunda Sera, Sheria na Programu zitakazosaidia kukuza ajira na ufuatiliaji wa mienendo ya ajira, soko la ajira na hali ya ukosefu wa ajira nchini kwa maendeleo ya Taifa.

Nchi yetu imefanikiwa kutekeleza makubaliano iliyoyaingia katika Kikao cha nchi za Umoja wa Afrika zilizoyaingia mwaka 2013 zilizowataka wanachama wote kufanya utafiti wa nguvukazi kila baada ya mika mitano (5) Kutokana na Tafiti hizo Serikali ilifanikiwa kutengeneza Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira kwa kuzingatia mahitaji ya waajiri. Mkakati huo una Programu tano zifuatazo;

i.Mafunzo ya ukuzaji ujuzi kwa njia ya Uanagenzi.
Mafunzo haya yalianza kutolewa mwaka 2018 ambapo mpaka sasa jumla ya vijana 43,381 wamepatiwa mafunzo haya. Aidha mafunzo haya ni endelevu na hata sasa vijana 14,440 wanaendelea na mafunzo.
ii. Urasimishaji Ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo (Recognition of Prior learning skills).
Hadi sasa mfumo huu umefanyika kwa vijana 20,334 na 4,316 wanaendelea kurasimisha ujuzi wao. (SGR, Bwala Mwalimu Nyerere, Bomba la Kusafirisha Gesi).

iii. Mafunzo ya Utarajali (Internship)
Mafunzo haya yalianza mwaka 2019/20 na yamewezesha vijana 6,300 kupatiwa mafunzo haya. Aidha kwa sasa vijana wengine 2,591 wanaendelea na mafunzo haya.

iv. Mafunzo ya kujenga uwezo kwa waliopo makazini kwa sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Skills Upgrading) Mafunzo haya yalianza mwaka 2020/21 ambapo mpaka sasa kwa sekta binafsi wafanyakazi 1,550 na sekta ya umma 2,400 wamejengewa uwezo.

v. Kuwajengea Ujuzi katika Kilimo cha Kisasa

• Kuwajengea uwezo katika Kilimo cha Kisasa kupitia teknolojia ya Kitalu nyumba

Programu hii ilianza kutekelezwa mwaka 2019 na hadi sasa imeifikia mikoa 17 na Halmashauri 117. Vijana 12,580 wamenufaika na Programu hii ambapo kati ya vijana hao, vijana 2,340 walipatiwa mafunzo ya kujenga vitalu nyumba;

• Kuwajengea uwezo vijana wa kitanzania katika masuala ya Kilimo. Mafunzo hayo yanafanyika nchini Israel ambapo tayari vijana 134 wamehitimu mafunzo yao vijana 300 wanatajaria kuanza mafunzo hivi karibuni. Aidha, Serikali inakamilisha Mfumo wa Kielektroniki wa kuwatambua vijana ili kujua wanachokifanya baada ya kumaliza mafunzo haya;

• Kuwawezesha vijana waliohitimu kutoka katika Vyuo vya Kilimo kutekeleza kilimo mfano JATU (DSE Listed Company iliyowawezesha mtaji wao kukua hadi bilioni 8), SUGECO na RIWADE;

b) Kufanikiwa katika kutengeneza Mfumo wa kudumu wa ufuatailiaji wa fursa na uzalishaji wa ajira katika sekta na wizara zote kupitia bajeti za kila mwaka (Fomu namba 15a na 15b).

c) Tangu kupata Uhuru Serikali imeridhia Mikataba 32 ya Shirika la Kazi Duniani (ILO). Kupitia Mikataba hii Serikali imeboresha Sheria za Kazi kwa kuzingatia viwango vya kazi vya Kimataifa. Kati ya Mikataba hiyo, Mikataba 8 ni Mikataba ya Msingi (Core Convertions), Mikataba 24 ni Mikataba ya Haki na Miongozo mbalimbali kuhusu masuala ya Kazi na Ajira.

d) Mwaka 2001 Serikali imefanya maboresho ya Sheria mbalimbali za Kazi ambazo zimewezesha kuunda Taasisi za kazi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kushughulikia masuala ya kazi na ajira ambapo Sheria hizo zimetenganisha majuku ya Kisera na Kiutendaji wa Taasisi hizo. Taasisi zilizoundwa ni pamoja na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Idara ya Kazi, Bodi za Mishahara za sekta ya Umma na sekta Binafsi na Baraza la Ushauri wa Masuala ya Mazi, Uchumi na Kijamii (LESCO) na Kamati ya Huduma Muhimu,
e) Mwaka 1998, Serikali ilifanikiwa kuweka Mfumo wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri ambapo huko nyuma vyama hivyo vilikuwa sehemu ya jumuiya ndani ya Chama Tawala. Mfano kabla ya mwaka 1998 Vyama vya Wafanyakazi vilikuwa ni sehemu ya Chama Tawala vikiwemo JUWATA na OTTU. Hadi sasa kuna Vyama Huru 32 vilivyosajiliwa katika Sekta mbalimbali.
f) Kuimarisha na kuboresha mfumo wa ushirikishwaji wafanyakazi ambapo hapo awali kupia Agizo la Rais Na. 1 la Mwaka 1970 wafanyakazi katika Mashirika ya Umma na makampuni walipewa fursa ya kushirikishwa katika masuala mbalimbali ya kuboresha maslahi yao. Mwaka 2004 katika Sekta mbalimbali za umma na binafsi kumewekewa utaratibu wa ushirikishwaji ambao umepunguza malalamiko na migomo sehemu za kazi.

g) Kuwepo kwa majadiliano ya pamoja kupitia utatu kwa ajili ya kuishauri Serikali na waziri mwenye dhamana ya Kazi kuhusu masuala ya kazi na ajira kupitia Baraza la Ushauri wa masuala ya Kazi, Uchumi na Kijamii (LESCO) na upangaji wa kima cha chini cha mishahara katika Sekta mbalimbali.

5.4 Sekta ya Maendeleo ya Vijana
Katika kipindi cha Miaka 60 Ofisi ya Waziri Mkuu imepata mafanikio katika maeneo yafuatayo:

a) Kuanzishwa kwa Wizara inayoshughulikia Masuala ya Vijana Nchini

Kutokana na umuhimu wa kundi la vijana katika maendeleo ya nchi Serikali za Awamu zote ziliunda Wizara inayoshughulikia masuala ya vijana kwa mfano Wizara ya Utamaduni na Vijana iliyoundwa mwaka 1962 na kwa sasa masuala ya vijana yanasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu iliyopo sasa.

b) Mipango mbalimbali ya maendeleo ya vijana nchini iliyoandaliwa;

i) Kuanzishwa kwa Programu ya Vikundi vya Vijana vya Kuzalisha Mali (VVKM)

Programu ya Vikundi vya Vijana vya Kuzalisha Mali (VVKM) ilianzishwa mwaka 1979 na inaendelea kutekelezwa mpaka sasa. Programu hii ni moja ya mikakati iliyoandaliwa kupitia Wizara inayoshughulikia masuala ya vijana ili kuwafikia na kuwatambua vijana kote nchini hasa wale waliokuwa nje ya shule kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefo wa ajira. Jitihada zilifanyika kuhamasisha vijana hawa kujiunga katika vikundi vya kuzalisha mali ambavyo vilijumuisha vijana wa kike, wakiume na Wenye Ulemavu ili kusaidiwa kubuni na kuanzisha miradi ya uzalishaji mali. Serikali ilikuwa na jukumu la kuviwezeshwa vikundi hivi kuendesha miradi yao kwa ufanisi kwa kuvipatia mafunzo kuboresha shughuli zao pamoja na kuimarisha mitaji yao kwa kuvipata ruzuku kwa fedha tasilimu au vifaa vya kazi na pia kunufaika na programu mbalimbali za Serikali za uwezeshaji.

ii) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kutokana na Maboresho kwenye sekta isiyo rasmi
Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF) ulianzishwa rasmi na Serikali Mwaka 1993/94 chini ya Sheria ya Fedha (The Exchequer and Audit Ordinance,

Cap 439) Na. 21 ya Mwaka 1961 kifungu cha 17 (1). Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu ni kuwawezesha vijana wote nchini kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye

masharti nafuu ili kuanzisha au kuendelza miradi yao uzalishaji mali.
Tangu kuanzishwa kwa Mfuko huu mikopo yenye thaamani ya Shilingi Bilioni 17.9 imetolewa kwa vikundi vya vijana 535 yenye wanachama 3,745.

iii) Mikopo inayotokana na 4% ya mapato ya ndani ya Halmashauri utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa vikundi vya Vijana ulianzishwa mwaka 1993/94. Hatua hii ni moja ya jitihada ya Serikali katika kuwasaidia vijana kupata mitaji kwa njia ya mikopo ya masharti nafuu kutokana na ukweli kwamba umaskini wa vijana uliwafanya washindwe kumudu masharti ya kupatiwa mikopo na taasisi za kibenki. Hata hivyo, kutokana na mahitaji ya vijana kuwa makubwa kulinganisha na uwezo wa Mfuko wa Maendeleo ya vijana kuwahudumia wahitaji Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa SURA 290 ambayo inazitaka Halmashauri kutenga 4% ya fedha zao za mapato ya ndani kwaajili ya mikopo ya vijana isiyo na riba. Tangu kuanzishwa kwa Sheria hii Halmashauri zote nchini zimekuwa zikitenga fedha kwa ajili ya mikopo ya vijana ambapo hadi Mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya shilingi 54,734,550,230 zimetolewa kwa vikundi vya vijana 15,349 vyenye idadi ya wanachama 115,781 na kuweza kuanzisha ajira mpya 163,051.

iv) Mkakati wa Utengaji wa Maeneo ya shughuli za kiuchumi kwa vijana
Moja ya changamoto ambayo imekuwa ikiwakabili vijana katika shughuzi zao za kiuchumi na uzalishaji mali ni kukosekana kwa maeneo rasmi ambayo yatawaezesha kufanya shughuli zao za Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, biashara na shughuli nyinginezo bila bugudha yoyote. Changamoto hii ya kihistoria ambayo pia inatokana na mila na desturi za makabila mengi nchini ambayo yanatoa fursa ya umiliki wa ardhi kwa wazee. Kutokana na changamoto hii Serikali ilianzisha Mkakati na kuzielekeza Halmashauri zote nchini kutenga maeneo rafiki na yenye miundombinu rafiki kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kwa vijana Mafanikio yanayotokana na mkakati huu ni kuwa hadi sasa Halmashauri 111 tayari zimetenga maeneo yenye ukubwa wa ekari 217,882.32 na vijana zaidi ya 3,232 wamepatiwa maeneo hayo.

v) Mpango wa Maalum wa Utoaji wa zabuni katika ununuzi wa umma kwa makundi maalum
Vijana ambao ni kubwa ya Nguvu Kazi ya Taifa wanakabiliwa na changamoto ikiwemo ukosefu wa ajira. Ili kutatua changamoto hii ya ajira moja ya mikakati ya Serikali imekuwa ni kuimarisha sekta isiyo rasmi na kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika sekta hii ili waweze kujiajiri. Aidha, kupitia Ununuzi wa Umma Serikali ilifanyia marekebisho Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na kuelekeza makundi maalum ya Vijana, Wanawake na Wenye Ulemavu kutengewa 30% ya bajeti ya Ununuzi katika taasisi zote za Serikali. Mpango huu umeweza kuchochea vijana waliohitimu elimu ya juu kuanzisha makampuni na kuunganishwa katika zabuni za Umma.

Kupitia mpango huu vijana wameweza kuhamasishwa kuanzisha Makampuni yao ambapo hadi sasa Zaidi ya makampuni 217 ya vijana yameanzishwa na kati ya makampuni haya makampuni zaidi ya 89 yameunganishwa na fursa ya utoaji zabuni za umma.

vi) Kuanzishwa kwa Kada ya Afisa Maendeleo ya Vijana katika ngazi za Mikoa na Halmashauri usimamizi wa shughuli za maendeleo ya vijana katika ngazi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilikuwa ni changamoto ya muda mrefu sana kutokana na kukosekana kwa wataalam mahsusi wa kusimamia shughuli hizo katika ngazi hizo kwani kwa muda mrefu shughuli za Maendeleo ya vijana zilikuwa zikisimamiwa ma maafisa wasiostahili wakiwemo Maafisa Utamaduni na Michezo.
Ili kutatua changamoto hii mwaka 2008 Serikali ilifanya marekebisho ya muundo ya kuanzisha kada ya Maafisa Maendeleo ya Vijana. Mafanikio yaliyofikiwa hadi sasa Sekretarieti za Mikoa 18 kati ya 26 tayari wameajiri Maafisa Vijana na Halmashauri 58 kati ya 184 pia zimeajiri Maafisa Vijana.

vii) Kuanzishwa kwa Wiki ya Taifa ya Vijana
Serikali ilianzisha Wiki ya Taifa ya Vijana mwaka 2000. Wiki ya Taifa ya Vijana ilianzishwa kwa lengo la kuwawezesha vijana na hasa walio katika Makampuni ya Vijana na vikundi vya uzalishaji mali, kuonesha ujuzi, vipaji na uwezo walionao wa kubuni na kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia malighafi zilizopo hapa nchini, pamoja na kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa wanazozalisha. Wiki ya Taifa ya Vijana pia inalenga kuwakutanisha vijana na kuwawezesha kubadilishana mawazo na uzoefu kutokana na maarifa na mbinu mbalimbali walizokuwa nazo katika masuala mbalimbali ya kijamii na kiuchumi. Vilevile lengo ni kuwapa vijana fursa ya kushiriki kwenye mijadala na makongamano mbalimbali yanayoendeshwa kwenye maadhimisho hayo kama vile masuala ya UKIMWI, Dawa za Kulevya, na Rushwa. Aidha vijana hupatiwa fursa ya kupima afya zao katika wiki hii.

**5.5Sekta ya Hifadhi ya Jamii**

Tangu tupate Uhuru, Sekta ya Hifadhi ya jamii imepitia mabadiliko chanya yaliyolenga kuboresha huduma za Hifadhi za Jamii kwa Wananchi wa Tanzania kama ifuatavyo;

a. Mwaka 1962, Serikali ilipanua wigo wa Watumishi wanaohudumiwa na  Mfumo wa Pensheni kwa kuwajumuisha Waalimu wazalendo kwani kabla ya hapo Mfumo ulikuwa unahudumia watumishi wa Serikali Kuu pekee.
b. Mwaka 1964 ulianzishwa Mfuko wa Akiba kwa watumishi kwa Sekta Binafsi (NPF) baadaye mwaka 1998 ulianzishwa Mfuko wa NSSF ambao unahudumia watumishi wa Sekta Binafsi. Hata hivyo, mifuko ya GEPF (1942), LAPF (1944) iliyokuwa imeanzishwa kabla ya Uhuru ambayo ilihusisha Wafanyakazi wa Serikali kuu waliokuwa wa Mikataba (Non Pensionable) na Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa.
c. Mwaka 2010, 2014 na 2018 Serikali ilifanya mabadiriko makubwa ya kuboresha  Sekta ya Hifadhi ya jamii kwa kufanya yafuatao;

(i) Mwaka 2010 Serikali ilianzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (Kazi inayofanywa sasa na Ofisi ya Waziri Mkuu);

(ii) Mwaka 2014 Serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ya SSRA ili kuwianisha mafao kwa watumishi wanaostaafu katika sekta ya Umma na Binafsi;
(iii) Mwaka 2008, Serikali ilitunga Sheria mpya na kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanya Kazi (WCF) ambao ulianzishwa rasmi mwaka 2015 ili kuondokana na Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ya Mwaka 1957 na mapitio yake ya mwaka 2002 ambayo haikuwa inatenda haki katika kuoanisha viwango vya malipo ya fidia kwa ulemavu na madhara yatokanayo na kazi;

(iv) Mwaka 2018 Serikali iliunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii minne ya GEPF, LAPF, PSPF na PPF kuwa mfuko mmoja wa PSSSF wa watumishi wa Umma kwa lengo la;
- kupunguza gharama za uendeshaji;
- kuongeza ufanisi katika kutoa huduma;
- kuifanya kuwa endelevu;
- kuondoa ushindani usiokuwa na tija;
- kutengeneza mifumo imara ya kusimamia uwekezaji.

(v) Kwa sasa Ofisi ya Waziri Mkuu inakamilisha utekelezaji maelekezo ya Serikali ya kuimarisha Mfumo wa Mafao ya watumishi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

**5.6 Mafanikio ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika Kuratibu Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa.**
Mfumo wa Demokrasia ya vyama vingi vya Siasa ulikuwapo kabla ya uhuru na mara baada ya uhuru. Kati ya mwaka 1965 mpaka 1992 tulikuwa na mfumo wa chama kimoja. Mwaka 1992 Nchi yetu ilirejesha mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya Siasa ili kupamua wigo wa demokrasia. Mwaka 1992, Sheria ya Vyama vya Siasa na. 5 ilitungwa na kuanzishwa kwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini. Vyama vya Siasa vilianza kusajiliwa tena mwaka 1992 ambapo katika Uchaguzi Mkuu wa vyama vingi vya Siasa mwaka 1995 vyama vya Siasa 13 vyenye usajili kamili viliweka wagombea. Toka mwaka 1992 mpaka sasa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imekwisha toa vyeti vya usajili wa muda kwa vyama vya Siasa 81 na imetoa vyeti vya usajili kamili kwa vyama vya Siasa 25 na kufuta usajili wa vyama vya Siasa vyenye usajili kamili 6 ambavyo vilikiuka masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa. Hivyo, hivi sasa nchi yetu ina vyama vya Siasa vyenye usajili kamili 19 na Chama Kimoja cha Siasa chenye usajili wa muda.

Aidha, Sheria ya vyama vya Siasa imekuwa ikiboreshwa mara kwa mara ili kuendana na mahitaji ya wakati husika na kuiwezesha kukabili changamoto zilizopo na zitakazojitokeza.

Tangu kutungwa mwaka 1992, Sheria ya vyama vya Siasa imerekebishwa mara nane (8), mara ya mwisho ikiwa ni mwaka 2019. Katika marekebisho ya Mwaka 2009, Sheria ya Vyama vya Siasa ilianzisha Baraza la Vyama vya Siasa ambalo ni chombo kinachokutanisha Viongozi wa Kitaifa wa Vyama vya Siasa vyenye usajili kamili kubadilishana mawazo kuhusu maendeleo ya demokrasia ya Vyama vingi nchini sambamba na kudumisha amani, utulivu, uzalendo na umoja wa Taifa.

**5.7 Kuanzishwa kwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi**
Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilianzishwa tarehe 14 Januari, 1993 chini ya Ibara ya 74(i) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Aidha, Ibara ya 74 (7) na (11) inaeleza kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni Huru na katika utekelezaji wa majukumu yake haipokeiamri au maelekezo kutoka kwa mtu au Taasisi yoyote. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni kuendesha, kusimamia na kuratibu Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani chini ya Mfumo wa Siasa wa Vyama Vingi. Majukumu mengine ya Tume ni pamoja na Kusimamia na kuratibu Uandikishaji wa Wapiga Kura katika Uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara; Kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Majimbo ya Uchaguzi wa Wabunge na Kutoa Elimu ya Mpiga Kura Nchini kote.

Mpaka sasa Tume ya Uchaguzi imefanikiwa kusimamia Chaguzi Kuu 6 za mwaka 1995, 2000, 2005, 2010,2015, 2020.

**5.8 Udhibiti wa UKIMWI**
Katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru, Tanzania imeweza kuchukua hatua madhubuti za kukabiliana na changamoto ya ugonjwa wa UKIMWI na Virusi vya UKIMWI nchini kwa kufanya yafuatayo;
a) Kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI nchini (TACAIDS) tarehe 1 Desemba, 2000;
b) Kuanzishwa kwa Sera ya Taifa ya UKIMWI ya mwaka 2001;
c) Kuongeza watumiaji wa Dawa za Kufubaza Virusi vya UKIMWI (ARV);
d) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI (AIDS Trust Fund) Kupitia Marekebisho ya Sheria; na
e) Kuanzishwa kwa ujenzi wa vituo vya Upimaji wa Virusi vya UKIMWI na utolewaji wa Dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI (ARVs) – CTC

Matokeo chanya ya Juhudi hizi ni pamoja na;
i. Kupungua kwa unyanyapaa kwa WAVIU
ii. Kiwango cha upimaji wa VVU kimeongezeka kutoka 61% ya makisio ya watu wanaoishi na VVU (WAVIU) mwaka 2016 hadi kufikia 83% mwaka 2019.
iii. Matumizi ya dawa za kufubaza VVU (ARVs) kwa WAVIU wanaojua hali zao za maambukizi yameongezeka kutoka 95% mwaka 2016 hadi 98% asilimia mwaka 2019.
iv. Kiwango cha kufubaza VVU kwa wale wanaotumia ARV kimeongezeka kutoka 87% mwaka 2016 hadi 92% mwaka 2019.
v. Vifo vitokanavyo na UKIMWI vimepungua kwa 50% kutoka vifo 64,000 mwaka 2010 hadi vifo 32,000 mwaka 2020.
vi. Takwimu za kiwango cha maambukizi katika jamii (HIV prevalence) zinaonyesha kiwango kilishuka kutoka 7%

mwaka 2003/04 hadi 4.7% mwaka 2016/17.
vii. Maambuzi mapya ya VVU kwa watu wazima (miaka 15 na zaidi) nzhini Tanzania yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka 2020
viii. Maambuzi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (Mother to Child transmission) yameshuka kutoka 18% mwaka 2010 hadi 7% mwaka 2020.
ix. WAVIU wanaofahamu hali zao za mambukizi ni 85%, WAVIU wanaofahamu hali zao za mambukizi na wapo kwenye matibabu ni 98% na WAVIU waliopo kwenye matibabu na wamefubaza VVU ni 95%.

**5.9 Kuimarika kwa Mapambano Dhidi ya Biashara na Matumizi ya Dawa za Kulevya**
Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeendelea kuweka na kutekeleza mikakati ya kupambana na uzalishaji, usambazaji, uuzaji na utumiaji wa dawa hizo. Mafanikio yaliyopatika katika kipindi cha miaka 60 ni yafuatavyo;
a) Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015 na kuanza kazi rasmi mwezi Februari, 2017;
b) Kupungua kwa uingizaji wa dawa za kulevya Nchini kwa zaidi ya 90%;
c) Kuandaa Miongozo ya Kuhakikisha Huduma Bora za Tiba na utengemao;
d) Kuvunja na kudhoofisha mitandao mikubwa ya dawa za kulevya Nchini, kuwakamata wafanyabiashara wa dawa za kulevya, kuwafikisha Mahakamani na kuhukumiwa kwa mujibu wa Sheria;
e) Upanuzi wa Huduma za Tiba kwa Waathirika wa Dawa za Kulevya. Huduma hii, ilianza rasmi Nchini mwaka 2011 ambapo hadi 2016 kulikuwa na vituo vitatu tu nchini ambavyo vilihudumia waathirika 3,500. Tangu kuanzishwa kwa Mamlaka mwaka 2017, kumekuwa na ongezeko la vituo nane zaidi na hivyo kufanya jumla yake kuwa vituo kumi na moja (11) vinavyohudumia zaidi ya waathirika 10,565 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Songwe, Arusha, Tanga, Dodoma na Pwani;
f) Uanzishaji wa Nyumba 31 za Upataji Nafuu (Sober Houses). Nyumba hizi zinaendeshwa na Asasi za Kiraia ambapo waraibu wa dawa za kulevya wameendelea kupata huduma kwa kupitishwa kwenye hatua 12 za upataji nafuu bila kutumia dawa ya aina yoyote; na
g) Kufanikiwa kwa vijana walioondokana na matumizi ya dawa za kulevya katika Programu ya mafunzo ya kukuza ujuzi.

**5.10 Menejimenti ya Maafa**
Katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa nchi yetu Ofisi ya Waziri Mkuu imepata mafanikio yafuatayo;

a) Kutungwa kwa Sheria ya Menejimenti ya Maafa Na. 7 ya mwaka 2015. Sheria hii iliwezesha kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Misaada ya Maafa ambao umekuwa ukichangiwa na wadau pindi maafa yanapotokea;
b) kuanzishwa kwa Kamati za Maafa katika ngazi ya Taifa, Mikoa, Wilaya, Kata na Kijiji ambazo zinajukumu la kushughulikia maafa kabla na yanayotokea katika maeneo yao;
c) Kuanzishwa kwa Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura (EOCC) ambacho kinatumika kufanya ufuatiliaji wa hali ya maafa na operesheni za dharura hapa nchini. Uwepo wa Kituo umeongeza uwezo wa upatikanaji wa taarifa za matukio ya maafa kwa wakati, kutoa taarifa za tahadhari na maelekezo na hivyo kuiwezesha Serikali na wadau mbalimbali kuchukua hatua stahiki kwa wakati;
d) Kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa maafa nchini kwa kuandaliwa miongozo, mikakati na taratibu za utendaji zinazowezesha utekelezaji wa majukumu kwa kuzingatia Sheria na taratibu.

e) Kuandaa mipango na miongozo ya kisekta ya kujiandaa na kukabiliana na maafa katika sekta mbalimbali zilizo katika hatari ya kukabiliwa na majanga yanayosimamiwa na Sekta husika mfano; Mipango na Miongozo ya Afua za Kinga na Tiba ya Kukabiliana na Ugonjwa wa virusi vya Korona - 19 (UVIKO – 19); Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Sumu Kuvu; Mpango Mkakati wa Taifa wa Afya Moja; Mkakati wa upatikanaji wa uhakika wa Malisho na Maji kwa Mifugo; Mwongozo wa Taifa wa Huduma ya Lishe wakati wa Mlipuko wa UVIKO – 19; na Mwongozo wa Utendaji wa Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura;

f) Kuratibu udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza (Non - Communicable Diseases – NDC);
g) Kuanzishwa kwa maghala ya kuhifadhi vifaa vya huduma za kibinadamu katika kanda sita nchini katika Kanda ya Kusini (Lindi), Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam), Kanda ya Kaskazini (Kilimanjaro), Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Ziwa (Shinyanga) na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya);
h) Kuimarisha upatikanaji wa taarifa za tahadhari ya awali nchini ambapo Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imefanikiwa kuweka vituo 36 vya hali ya hewa pamoja na vituo vya Rada katika maeneo mbalimbali nchini. Hatua hii imeboresha utabiri wa hali ya hewa kufikia uhakika kwa asilimia 87. Hivyo kuweza kutoa tahadhari yenye uhakika kwa wananchi na wadau wote wanaotumia huduma za hali ya hewa nchini;

i) Ofisi ya Waziri Mkuu imefanikiwa kuratibu na kurejesha hali kufuatia maafa mbalimbali yaliyotokea yakiwemo;
i. Ukame uliotokea katika Mikoa 13 ya Shinyanga, Pwani, Kilimanjaro, Mwanza, Mbeya, Lindi, Mara, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Iringa na Arusha mwaka 1974-1975, 1975-1976, na 1976-1977;
ii. Ajali ya Meli ya MV. Bukoba iliyotokea Ziwa Victoria tarehe 21 Mei, 1996. Watu zaidi ya 1000 walipoteza maisha, mali nyingi ziliharibiwa vibaya;

iii. Mafuriko makubwa yaliyotokea baada ya mvua kubwa kunyeshwa katika wilaya za Kilwa, Tarime, Ruangwa, Lindi Vijijini, Morogoro Vijijini, Arumeru, Monduli, Nkasi, Serengeti na Kilombero ambapo wananchi 68 walipoteza maisha na wengine kukosa makazi mwaka 1996 na 1997;
iv. Ajali ya Gari Moshi iliyotokea katika Kijiji cha Msangali Mpwapwa Dodoma Tarehe 24 Juni, 2002. Ajali hiyo

ilisababisha vifo vya watu 294 ikijumuisha waliofariki hospitalini baadaye na wengine 539 kujeruhiwa. Aidha, Taifa lilipata hasara ya takriban Shilingi bilioni 5.1 kutokana na uharibifu wa mabehewa na reli;
v. Ajali ya Gari Moshi iliyotokea katika Stesheni ya Mzaganza na Kidete katika Wilaya ya Kilosa, (Morogoro) mwaka 2004. Katika Ajali hiyo watu sita walikufa papo hapo na wengine 10 kujeruhiwa;
vi. Milipuko ya Mabomu katika Kambi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania Mbagala (Dar es Salaam) Tarehe 29 Aprili, 2009;
vii. Milipuko ya Mabomu katika Kambi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania Gongo la Mboto (Dar es Salaam) tarehe 15 Februari, 2011;
viii. Tetemeko la Ardhi Mkoani Kagera Mwaka 2016;
ix. Mafuriko yaliyotokea katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kilimanjaro na Tanga, tetemeko la ardhi Mkoani Kagera mwaka 2016 na 2017;
x. Ajali ya kivuko cha MV Nyerere katika Kisiwa cha Ukerewe, Mwanza mwaka 2018; na
xi. Ajali ya kulipuka moto kwa gari la mafuta katika Manispaa ya Morogoro mwaka 2019.

5.11 Kuimarika kwa Ushughulikiaji wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu

Katika kipindi cha miaka 60 kumetokea mabadiriko makubwa katika kutambua na kushughulikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu. Katika kipindi husika mafanikio yafuatayo yamepatikana;
a) Kutungwa kwa Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye ulemavu ya mwaka 2010; Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010 pamoja na kanuni zake za Mwaka 2012; Kusaini na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu wa mwaka 2007 na kuridhiwa kwa Mkataba wa Marrakesh wa Mwaka 2019 pamoja na kukamilishwa kwa Mwongozo wa Kitaifa wa Utambuzi wa Mapema na Afua Stahiki kwa Watoto wenye Ulemavu wa Mwaka 2021 ili kuimarisha ustawi wa Watu wenye Ulemavu hapa nchini;

b) Kuratibu utoaji wa Mafunzo ya Stadi za Kazi na Huduma za Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu katika Vyuo vya Yombo –Dar es Salaam, Sabasaba - Singida Masiwani - Tanga, Luanzari- Tabora, Mirongo – Mwanza na Mtapika – Masasi; Vyuo vya Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu Wenye Ulemavu vimekuwa vikitoa mafunzo katika fani mbalimbali zikiwemo; Useremala, Uungaji vyuma; Ushonaji nguo na Usekete-ji; Ushonaji wa viatu, mikoba, mabegi na kazi nyingine za mikono; Kilimo na ufugaji, Umeme wa Majumbani, Mapambo na Ujenzi; Mpango huu wa mafunzo unalenga kuwawezesha Watu Wenye Ulemavukupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri na kuajirika;

c) Watu Wenye Ulemavu wanajumuishwa kwenye vyombo vya maamuzi na nafasi za juu za Uongozi Serikalini na kuwapa kipaumbele kwenye suala la ajira. Mathalan, Kufanyika kwa teuzi mbalimbali za Watu Wenye Ulemavu katika nafasi za juu za uongozi Serikalini zikiwemo nafasi za Naibu Waziri 1, Makatibu Wakuu 2, Naibu Makatibu Wakuu 3, Wabunge 9, Mabalozi 2, Madiwani 16 pamoja na Wakurugenzi wa Idara na Vitengo mbalimbali vya Serikali;

d) Kutekeleza Mkakati wa ujenzi wa vyuo vipya viwili (2) na ukarabati wa vyuo sita (6) vilivyopo vya Watu Wenye Ulemavu ;

e) Kuratibu na kusimamia uundwaji wa Kamati za kuhudumia Watu wenye Ulemavu ambazo zimeundwa katika Mikoa 26, Halmashauri 184, Vijiji 5034, na Mitaa 2284 pamoja na na kusimamia Vyama vya Watu wenye Ulemavu. Vyama hivyo vinaunda Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA);

f) Uanzishwaji na uendeshaji wa Baraza la Taifa la Ushauri kwa Watu Wenye Ulemavu ambapo Mwenyekiti ni Mtu Mwenye Ulemavu na 70% ya Wajumbe ni Watu Wenye Ulemavu.

5.12 Mbio za Mwenge wa Uhuru

Mwenge wa Uhuru uliwashwa kwa mara ya kwanza tarehe 9 Desemba, 1961 na kuwekwa juu ya Mlima Kilimanjaro kama sehemu ya kusheherekea Uhuru.

Mwaka 1964 Mbio za Mwenge zilianzishwa kwa kuashiria dhamira ya Mwalimu Nyerere ya kufikisha ujumbe wake pande zote za Tanzania. Katika miaka minne ya kwanza (1964 – 1968) Mwenye wa Uhuru ulikimbizwa na Serikali. Hatimaye mwaka 1969 hadi 1976 ulikimbizwa na Vijana wa Vyama vya Siasa vya TANU na ASP. Kuanzia mwaka 1977 hadi 1992 Mwenge wa Uhuru ulikimbizwa na CCM kupitia Umoja wa Vijana. Kuanzia mwaka 1993 hadi sasa mbio za Mwenge wa Uhuru zinasimamiwa na Serikali.

5.13 Kuratibu Shughuli za Bunge

Katika kipindi cha Miaka 60 ya Uhuru, Ofisi ya Waziri Mkuu imeweza kuratibu mambo yafuatayo;
a. Kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya Sheria mbalimbali;
b. Kuwasilisha Bungeni Mapendekeo ya Bajeti na Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano na Mwaka Mmoja mmoja;
c. Kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa Shughuli za Serikali;
d. Kutoa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge; na
e. Kuratibu uridhiwaji na Bunge Maazimio, Itifaki na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa.

6.0. MAENEO YA KIPAUMBELE YA MIAKA 60 IJAYO;

a) Kuimarisha upigaji chapa wa nyaraka za Serikali;
b) Kuimarisha usalama na afya mahala pa kazi;
c) Kuunganisha mamlaka za Usimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu;
d) Kuimarisha uwezo wa nchi katika kukabiliana na maafa; na
e) Kujenga kituo cha ufuatiliaji na udhibiti wa maafa.
f) Kuimarisha na kusimamia Mfumo wa Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali 'Dashboard' ili uwezeshe kuratibu shughuli zote za Serikali zinazotekelezwa kitaifa ikiwemo Ilani ya Uchaguzi, Maagizo ya Viongozi wa Kitaifa, na Sera za Kitaifa.

g) Kukamilisha mfumo wa Kitaifa wa Taarifa za soko la ajira. Mfumo huu utakuwa na Moduli 5 ambazo ni;
i. Usimamizi wa masuala ya kazi
ii. Fursa za Ajira
iii. Huduma za Ajira
iv. Mafunzo na ujuzi
v. Intelligentsia ya soko la ajira – data zimetokana na tafiti mbalimbali
h) Kuweka kanzidata ya wadau wnaohusika na masuala ya ukuzaji Ajira Nchini.
i) Kufanya utafiti wa Taifa wa Wataalam / Rasimali watu nchini (Manpower survey)
j) Ukuzaji ujuzi katika sekta ya Uchumi wa Blue (Blue economy) na Uchumi wa Kijani
k) Kuendelea kutekeleza program ya Taifa ya kukuza ujuzi nchini.

i. Mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya uanagenzi
ii. Kurasimisha ujuzi uliopatikana katika mfumo usio rasmi
iii. Mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu
iv. Mafunzo ya kukuza ujuzi kwa walio makazini

l) Kukamilisha sera ya Taifa ya Ajira
m) Kukamilisha Sera ya taifa ya Vijana
n) Kukamilisha Sera ya Taifa ya hifadhi ya Jamii
o) Kutekeleza Mkakati wa Taifa wa kukuza fursa za ajira
p) Kukamilisha Kamusi ya Kitaifa ya kazi (Tanzania standard of classification of occupations)

q) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa Sheria za kazi na Mikataba ya Shirika la kazi Duniani (ILO) ili kuboresha mahusiano mema baina ya Waajiri na Wafanyakazi na hatimaye kukuza kazi za staha nchini.
r) Kuimarisha ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika kuimarisha Viwango vya kazi.
s) Kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kwa kuimarisha ushughulikiaji vibali vya kazi kwa raia wa Kigeni.
t) Kuendelea kutoa ushauri na Elimu kwa Waajiri na wafanyakazi kwa lengo la kutekeleza sheria za kazi nchini.
u) Kuendelea kuratibu na kusimamia majadiliano ya pamoja ya utatu yenye lengo la kuboresha maslahi ya wafanyakazi, kuimarisha mahusiano na kukuza ufanisi na tija sehemu za kazi;
v) Kuongeza wigo wa Hifadhi ya Jamii kwenye Sekta isiyo rasmi;
w) Kukamilisha Mwongozo wa usimamizi wa hifadhi ya jamii kwa sekta isiyo Rasmi;
x) Ujenzi wa Kiwanda cha Mpiga Chapa Dodoma;
y) Ujenzi wa Vyuo vipya vya Watu Wenye Ulemavu;
z) Maeneo Mengine ya Kipaumbele
(i) Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi 'Agriculture and Fisharies Development Programu (AFDP)' unaolenga kuimarisha uzashaji wa Mbegu za Kilimo na Uvuvi kwenye Bahari kuu. Meli nane (8) za uvuvi bahari kuu zitanunuliwa ikiwa nne (4) kwa ajili ya Tanzania Bara na nne (4) kwa ajili ya Zanzibar;
(ii) Kupitia Mradi wa kukabiliana na Vitendo vya Kiharifu katika Maziwa na Bahari kuu Nchini kutajengwa Miundombinu ya Kukaushia Samaki, Ununuzi wa Boti ya Doria, na Kuandaa mwongozo wa Kitaifa wa kuratibu mapambano dhidi vitendo vya Kiharifu katika Maziwa na Bahari kuu.
aa) Mchango wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Katika Uchumi wa Viwanda
(i) Kukamilisha uanzishwaji wa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Karanga likichopo Moshi 'Karanga Leather Industries Co. Ltd (Kilimanjaro International Leather Industries Co. Ltd"

(KLICL)'. Kiwanda hiki kitaajiri watu 3000 wa ajira za moja kwa moja na 7000 zisizo za moja kwa moja.
(ii) Kuboresha kiwanda cha Nyama cha Nguru hill Ranch Kilichopo Mvumero - Morogoro. Kiwanda hiki kitaajiri watu 150 wa ajira za moja kwa moja.
(iii) Kuboresha Uzalishaji wa kiwanda cha Kuchakata Tangawiza cha 'Mamba Ginger Factory Limited' kilichopo Same-Kilimanjano. Kiwanda hiki kitaajiri watu 35 wa ajira za moja kwa moja.
(iv) Kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha sukari Mbigiri, Morogoro.
(v) Kukaratabati majengo pamoja na Mitambo ya Kiwanda cha kusindika Chai cha Mponde kilichopo Mkoani Tanga.

**7.0. HITIMISHO**
Ofisi ya waziri Mkuu inamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu katika kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, weledi na kwa mafanikio makubwa zaidi katika kipindi cha miaka Sitini ijayo.

''JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA ….
KAZI IENDELEE''




# UKUAJI NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA ZA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KATIKA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

**Ndugu Wanahabari; nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**
Leo tupo hapa tukiendelea na maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku hii salama tukiwa na afya njema. Aidha, Napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha katika mkutano huu ambao unalenga kuelezea mafanikio ya Sekta ya Elimu wakati tunaadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Ninawashukuru kwa namna ambavyo ninyi waandishi mmekuwa mkiibua mijadala mbalimbali inayolenga kuboresha elimu yetu. Sisi kama Wizara tunaendelea kupokea michango yenu pamoja na ya wananchi wengine kwa ujumla ambao wanatoa maoni yao kuhusu masuala ya Elimu, sayansi na Teknolojia.
Ndugu Wanahabari;

Mara tu baada ya Tanganyika kujipatia Uhuru wake, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitangaza vita dhidi ya maadui watatu ambao ni Ujinga, Umasikini na Maradhi.

Katika kupambana na adui hawa, hasa ujinga, Watanzania tumeendelea kushuhudia mafanikio na mageuzi makubwa katika sekta ya elimu ambayo ina mchango mkubwa katika kumkomboa Mtanzania dhidi ya adui ujinga. Ni dhahiri kuwa mapambano dhidi ya adui Ujinga ndiyo msingi wa mapambano dhidi ya Maradhi na Umaskini. Bila shaka yeyote ukiondoa Ujinga utakuwa pia umepunguza Maradhi pamoja na Umaskini.

Katika miaka 60 ya Uhuru, tumeshuhudia ongezeko kubwa la fursa za upatikanaji wa elimu katika ngazi zote za elimu. Hii imetokana na uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya elimu na uimarishwaji wa mifumo ya uthibiti na ithibati ya elimu. Tunaendelea kushuhudia maendeleo katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Aidha, ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma za elimu nchini katika ngazi zote unaendelea kuimarika.

Ndugu Wanahabari; tunaposherehekea miaka 60 baada ya Uhuru wa nchi yetu, ni vizuri tujikumbushe tulikotoka, tulipo sasa na matarajio yetu ya baadaye.

Kumbukumbu za mapambano dhidi ya ujinga zinaturudisha hadi wakati wa Utawala wa Kijerumani na Kiingereza, ambapo kwa kiasi kikubwa elimu ilitolewa na Wamisionari. Elimu hiyo ilitolewa kufuatana na imani yao na historia ya nchi walikotoka ambapo walisisitiza zaidi uenezi wa dini. Kulikuwa na shule chache za serikali za kikoloni. Shule ya kwanza nchini, Tanga School, ilijengwa na Wajerumani mwaka 1892. Aidha Waingereza walianzisha Tabora School mwaka 1922. Shule nyingine zilizokuwapo zilikuwa ni za madhehebu ya dini na waliosoma walikuwa ni wanafunzi wa dhehebu husika.

Kwa ujumla mifumo ya elimu kabla ya Uhuru ilikuwa na misingi ya ubaguzi wa rangi. Nafasi bora zaidi za elimu zilitolewa kwa watoto wa Kizungu na Kiasia kuliko watoto wa Kiafrika. Lengo kubwa la elimu lilikuwa ni kupata watumishi Waafrika ambao wangetumika katika kutetea matakwa Na maslahi ya wakoloni, pamoja na kufanya kazi za ofisini kama wahudumu na makarani.

**Elimu baada ya Azimio la Arusha**
Katika historia ya Elimu Tanzania Bara, Azimio la Arusha ni tukio muhimu lililotoa mweleko mahsusi wa elimu na harakati za ujenzi wa Taifa kwa ujumla. Azimio hili lilitangazwa mwaka 1967 mjini Arusha na lengo lake lilikuwa ni kurekebisha kasoro zilizojitokeza baada ya Uhuru ili kujenga taifa linalofuata 'Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea'. Siasa hiyo ilizaa Falsafa ya 'Elimu ya Kujitegemea', yenye lengo la kumkomboa Mtanzania kutokana na utegemezi. Elimu ilitakiwa kuzingatia ujenzi wa maarifa, ujuzi, stadi na mwelekeo ya kupenda na kuthamini kazi kwa lengo la kumwezesha mhitimu kutumia rasilimali zilizo katika mazingira yake kwa maendelo yake binafsi, jamii na Taifa lake kwa ujumla. Sheria ya Elimu ya mwaka 1969 (Education ACT, 1969) ilitolewa ili kuwezesha utekelezaji wa mabadiliko ya elimu kulingana na tamko la Elimu ya Kujitegemea.

**Matumizi ya Lugha ya Kiswahili**
Kufuatia Azimio la Arusha, mwaka 1968 ulitolewa mwongozo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia kwenye shule za msingi na katika kuendeshea mikutano ya walimu na wanafunzi katika shule za sekondari.

Sote ni mashahidi kwamba, matumizi ya Lugha ya Kiswahili yamewezesha kuleta umoja wa Kitaifa. Aidha, Kiswahili kimeendelea kutumika kikanda na hata katika ngazi ya kimataifa. Kwa sasa Kiswahili kinatambulika kama lugha rasmi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa (SADC).

**Mabadiliko ya Mitaala**
Ubora wa mitaala ni jambo la msingi katika kuhakikisha kuwa nchi inatoa elimu stahiki. Tangu tulipopata Uhuru mwaka 1961, mitaala yetu imebadilishwa mara tano kama ifuatavyo:

Mabadiliko ya Kwanza ya mitaala yalifanyika Mwaka 1967 yakilenga kuondokana na mitaala ya kibaguzi iliyokuwa ikitolewa na wakoloni. Mitaala iliyoandaliwa ililenga kujenga uzalendo kwa kuzingatia Falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea. Mwelekeo wa mabadilliko ya mitaala hii ulikuwa ni kupambana na maadui watatu - Ujinga, Umaskini na Maradhi.

Mabadiliko ya pili yalifanyika Mwaka 1979 yakiwa na msisitizo kwenye elimu ya nadharia na vitendo ambapo masomo ya michepuo yalianzishwa rasmi. Hatua hiyo iliwezesha kuwa na shule za Ufundi, Kilimo, Biashara na Sayansi-Kimu. Lengo ilikuwa kuongeza stadi zitakazowawezesha wahitimu wa ngazi za Sekondari kujikwamua kiuchumi na kujengewa uwezo wa kujitegemea.

Mabadiliko ya tatu yalifanyika Mwaka 1997. Mabadiliko haya yalizingatia matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995 na mapendekezo ya Tume ya Makweta ya

Mwaka 1982. Pamoja na mambo mengine, msisitizo uliwekwa katika kuboresha utoaji wa elimu kwa vitendo ili kujenga uwezo zaidi wa vijana katika kujikwamua kiuchu mi huku wakijengewa ari na moyo wa uzalendo kwa nchi yao.

Mabadiliko ya nne yalifanyika Mwaka 2005 ambayo yalilenga kuingiza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa umahiri, yaani Competence-Based Curriculum. Mtaala huu pia uliweka msisitizo wa somo la TEHAMA pamoja na uchopekaji wa masuala mtambuka kama vile Elimu ya UKIMWI, Afya ya Uzazi, Stadi za Maisha, pamoja na utunzaji wa Mazingira.

Mabadiliko ya Tano yalifanyika mwaka 2014 kwa lengo la kuimarisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika Ngazi ya Elimu ya Awali, Darasa la 1 na la Pili.

**Mapitio yanayoendelea Sasa ya Mitaala**
Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamnhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuboresha elimu kwa kuhakikisha mitaala inayotumika inakidhi mahitaji sasa. Hivyo, Mheshimiwa Rais ameilekeza Wizara ya Elimu kufanya mapitio ya mitaala katika ngazi zote. Lengo ni kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inajenga ujuzi na stadi zinazoendana na mahitaji ya sasa. Kazi hiyo ya maboresho ya mitaala inaendelea kufanyika. Wadau wa Elimu wanashirikishwa ili kupata maoni yatakayowezesha kupata mitaala yenye msisitizo katika kujenga ujuzi. Marekebisho hayo yatakapokamilika, yatakuwa ni marekebisho ya sita ya Mitaala tangu nchi yetu ilipopata Uhuru.

**Sera ya Elimu ya Watu Wazima ya Mwaka 1970**
Moja kati ya mafanikio makubwa katika sekta ya elimu ilikuwa ni kampeni ya kufuta ujinga kwa watu wazima. Kampeni hii ilitokana na Sera ya Elimu ya Watu Wazima ya mwaka 1970 ambayo ilitaka kila mtu mzima aweze kusoma, kuandika na kuhesabu. Mkakati uliwekwa wa kutimiza lengo hilo ifikapo Desemba 1975. Utekelezaji wa mpango huo wa kitaifa wa kufuta ujinga ulishika kasi na ulipata mafanikio makubwa sana kutokana na msukumo wa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Kwanza wa Tanzania.

Mwalimu Nyerere alisisitiza juu ya umuhimu wa kufuta ujinga kwa ajili ya maendeleo na pia kumkomboa Mtanzania kifikra.

Ndugu Wanahabari; katika kupiga vita adui ujinga, hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kupunguza idadi ya Watanzania wasiojua kusoma na kuandika. Hatua hizo ni pamoja na uanzishaji wa Programu za Kisomo Chenye Manufaa, Kisomo cha Kujiendeleza na Elimu ya Wafanyakazi. Jitihada hizo zilizaa matunda na kuwezesha idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika kupungua kutoka asilimia 48 mwaka 1970 hadi asilimia 22 mwaka 2012 (kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012).

Elimu ya Watu Wazima ilitumika kuratibu Kampeni za Kitaifa za kuelimisha umma kuhusu masuala mtambuka ya maendeleo. Kampeni hizo ni pamoja na:

Kupanga ni Kuchagua (1969): Ililenga kushirikisha wananchi katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
2. Siasa ni Kilimo (1973): Ililenga kudumisha Kilimo cha Kisasa ili kuleta maendeleo;
3. Mtu ni Afya (1974): Ililenga kuelimisha Jamii kuhusu namna ya kujikinga na magonjwa ya milipuko kama vile kipindupindu;

4. Chakula ni Uhai (1975): Ililenga kuelimisha jamii kuhusu uzalishaji wa mazao ya chakula na umuhimu wa lishe bora;
5. Misitu ni Mali (1980): Ililenga kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza misitu ili kuzuia kuenea kwa jangwa nchini;
6. Elimu kwa Wapiga Kura (1995): ililenga kuelimisha jamii kuhusu demokrasia na namna ya kushiriki kugombea na kupiga kura katika uchaguzi wa mfumo wa vyama vingi vya siasa; na
7. Tubadili Tabia Tushinde UKIMWI (2001): Ililenga kujenga uelewa kwa makundi yote ya jamii ya Watanzania juu ya janga la UKIMWI na athari zake.

Tume ya Rais ya Elimu ya Mwaka 1982
Pamoja na mafanikio ambayo yalikuwa yamefikiwa katika sekta ya elimu, bado kulikuwa na haja ya kufanya tathmini ya kina na kupata maoni ya kuiwezesha elimu yetu kuwa bora zaidi. Hivyo mwaka 1982 iliundwa Tume Maalum ya Rais ya kufanya tathmini hiyo. Tume hiyo iliongozwa na Hayati Jackson Makweta na ilijulikana zaidi kama "Tume ya Makweta". Majukumu makubwa ya Tume ilikuwa ni kufanya tathmini ya mfumo wa elimu uliokuwepo na kupendekeza mfumo unaozingatia hali halisi katika nchi kwa wakati huo.

**Malengo mahsusi yalikuwa ni:**
(i) kupata mambo yanayothaminiwa kitaifa, kijamii, kitamaduni na kimaadili ili yaweze kuzingatiwa katika utoaji wa elimu;
(ii) kubainisha malengo ya Elimu katika ngazi mbalimbali ili kila mmoja awe ameandaliwa vya kutosha kujitegemea kimaisha na kuliendeleza Taifa; na
(iii) kubainisha maandalizi yaliyotakiwa ili madhumuni na malengo ya elimu yaweze kufikiwa.

Moja ya mapendekezo ya Tume hiyo ilikuwa ni kuingizwa kwa Elimu ya Awali katika mfumo rasmi Hatimaye, Elimu ya Awali iliingizwa kwenye mfumo rasmi mwaka 1993. Pia Tume hiyo iliweka msisitizo katika kuongeza shule za sekondari.

Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuimarisha mfumo wa utoaji elimu ikiwa ni pamoja na kuanzisha Vyombo vya kuthibiti Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi yaani Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) 1994 na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo (NACTE) 1999. Kufuatia kuanzishwa kwa Vyombo hivyo, kumekuwa na uthibiti wa ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa.

Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Wote (Universal Primary Education – UPE)
Mwaka 1977 Serikali ilianzisha "Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Wote" yaani Universal Primary Education – (UPE). Mpango huu ulikuwa na lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu kwa watoto wote. Kupitia mpango huu shule nyingi za msingi zilifunguliwa na kuandikisha watoto wengi zaidi. Aidha, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji, wahitimu wa Darasa la Saba walipata Mafunzo ya Ualimu ili wafundishe Darasa la Tatu na Nne kwa kusaidiwa na walimu wakuu, ambapo baadae waliendelea na mafunzo na kuwa walimu kamili.

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM)
Baada ya mafanikio makubwa ya Mpango wa UPE, serikali ilikuja na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Huu ulikuwa ni mpango wa kwanza katika Sekta ya Elimu na utekelezaji wa Mkakati wa Serikali wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA). Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ulianza mwaka 2002 ukiwa na malengo yafuatayo:

(i) Kuongeza uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya Msingi;
(ii) Kuinua ubora wa Elimu itolewayo;
Kujenga uwezo wa watendaji wa MMEM katika ngazi zote za usimamizi wa elimu;
(iv) Kuimarisha taratibu za Kitaasisi; na
(v) Kuimarisha elimu ya masuala mtambuka.

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES)
Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) ulikuwa ni mpango wa pili katika Sekta ya Elimu wa utekelezaji Mkakati wa Serikali wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA) baada ya ule wa Elimu ya Msingi (MMEM).

MMES ulianza kutekelezwa kuanzia mwaka 2004 kwa Lengo Mahsusi la kuongeza idadi ya vijana wa Tanzania wanaosoma na kuhitimu Elimu ya Sekondari iliyo bora wakiwa na matokeo mazuri.

Ili kufikia lengo hili, MMES ulijikita katika maeneo makuu yafuatayo:

Kuongeza upatikanaji wa Elimu ya Sekondari (access);
(ii) Kutoa elimu kwa uwiano sawa (equity);
(iii) Kuongeza ubora wa Elimu ya Sekondari (quality);
(iv) Kuboresha usimamizi na uendeshaji wa shule (strengtherning Institutional arrangement); na
(v) Kuzingatia masuala mtambuka katika mitaala ya Elimu (cross-cutting issues).

Utekelezaji wa MMES ulikuwa na mafanikio makubwa katika kuongeza fursa za Elimu ya Sekondari. Tulishuhudia mpango wa ujenzi wa Sekondari za kata ukitekelezwa kwa kasi na kufanya idadi ya Shule za Sekondari kuongezeka kutoka 828 mwaka 2004 hadi 3,039 mwaka 2009. Hatua hiyo ililenga kuongeza shule mahali wanafunzi kuwapunguzia umbali mrefu waliokuwa wanatembea kufuata shule. Serikali imeen delea kuongeza Shule za Sekondari ambapo baadhi ya Kata zina shule zaidi ya moja.

**Mafanikio Katika Sekta ya Elimu**
Ndugu Wanahabari; sasa naomba nijielekeze katika mafanikio ya Sekta ya Elimu tangu nchi yetu ilipopata Uhuru. Mafanikio haya yametokana na kazi iliyotukuka iliyofanywa na serikali kwa awamu zote sita. Wadau mbalimbali wa maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali na jamii nzima ya Kitanzania imetoa mchango mkubwa katika mafanikio hayo. Hivyo, kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau wote wa elimu hapa nchini ambao kwa pamoja tunajivunia mafanikio yalipatikana kwa kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa nchi yetu.

**Elimu ya msingi na Sekondari**
Ndugu Wanahabari; katika Elimu ya msingi na sekondari, baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na:

Kuongezeka kwa idadi ya shule za msingi zilizosajiliwa kutoka shule 3,270 mwaka 1961 hadi shule 18,546 mwaka 2021. Kati ya shule 18,546, shule 16,656 ni za Serikali na 1,890 za Binafsi;

Shule za sekondari zimeongezeka kutoka 41 mwaka 1961 ambapo shule 2 zilikuwa za Binafsi, hadi kufikia 5,460 mwaka 2021 ambapo shule 3,983 ni za Serikali na shule 1,287 ni za binafsi. Takwimu hizi zinaonesha wazi namna ambavyo baada ya kupata Uhuru, Serikali imetoa nafasi kubwa kwa sekta binafsi kushiriki katika elimu. Hali hii imewezesha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari kuongezeka kutoka wanafunzi wa Kidato cha Kwanza 4,432 mwaka 1961 hadi wanafunzi 803,085 mwaka 2021. Ongezeko hilo limechangiwa na mikakati mbalimbali ya Serikali ikiwemo utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo ulioanza kutekelezwa 2016 chini ya Serikali ya Awamu ya Tano na unaendelea kutekelezwa. Pia ujenzi wa shule za sekondari za Kata uliofanyika kuanzia mwaka 2005 na unaendelea kufanyika hadi sasa umewezesha elimu ya sekondari kutolewa karibu na wanaposhi wanafunzi.

Serikali ya Awamu Sita Chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan inaendeleza kwa vitendo upatikanaji wa fursa za elimu ya sekondari kwa wanafunzi wote wanaofaulu mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi. Katika kipindi cha miezi nane tu tangu aliposhika hatamu ya uongozi wa nchi yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amewezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya sekondari 12,000 na KAZI hiyo INAENDELEA. Aidha, Serikali ya awamu ya sita itaendelea kuchukua hatua mahsusi za kuongeza idadi ya shule za Kidato cha tano na Sita ili kuongeza fursa zaidi kwa wanafunzi A-level.

**Elimu Maalum**
Ndugu Wanahabari; elimu ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania bila kujali mazingira yake. Sera za Elimu zimekuwa zikisisitiza juu ya umuhimu wa elimu jumuishi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo baadhi ya mafanikio yalipatikana ni pamoja na:

Kuongezeka kwa idadi ya Shule za Msingi zinazochukua wanafunzi wenye mahitaji maalum kutoka shule nne za Wamisionari (Tabora, Buigiri, Irente na Uhuru Mchanganyiko) mwaka 1961 hadi kufikia shule 776 mwaka 2021. Shule za sekondari zimeongezeka kutoka shule moja (Mpwapwa sekondari) mwaka 1960 hadi kufikia shule 74 mwaka 2021.

(ii) Kuongezeka kwa Vyuo Vikuu vinavyopokea wanafunzi wenye mahitaji maalum kutoka Chuo Kikuu kimoja cha Dar es Salaam mwaka 1961 hadi Vyuo Vikuu 11 mwaka 2021.

Ongezeko hilo limetoa fursa kwa wanafunzi kuchagua vyuo na fani wanazotaka kusomea.

(iii) Kuanzishwa kwa Mafunzo ya Elimu Maalum mwaka 1976 ambapo Wizara ya Elimu ilianza kuandaa walimu kwa wanafunzi Wasioona na Viziwi katika Chuo cha Ualimu Tabora. Aidha, Mwaka 1983 Chuo cha Ualimu Tabora kilianza kuandaa walimu kwa ajili ya wanafunzi wenye Ulemavu wa Akili. Vilevile Mwaka 1996 Chuo cha Ualimu wa Elimu Maalumu Patandi kilianza kutoa kozi mbalimbali za Elimu Maalumu.

(iv) Ufundishaji wa lugha ya alama umeimarishwa ili kuwawezesha watoto viziwi kujifunza. Aidha, lugha ya alama inawawezesha pia kupata habari ambapo baadhi ya vyombo vya habari huvitumia.

Ndugu Wanahabari

**Elimu ya Juu**
Elimu ya Juu imekuwa ikitolewa kwa lengo la kuwezesha wanufaika kupata maarifa na umahiri katika fani stahiki.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilianza kama Chuo Kikuu Kishiriki cha London mnamo tarehe 25 Oktoba, 1961 siku chache kabla ya Uhuru wa Tanganyika. Chuo hiki kilipoanzishwa kilikuwa na Kitivo kimoja tu cha Sheria, wahadhiri 6 na wanafunzi 14 ambapo mwanamke alikuwa mmoja tu aliyeitwa Julie Manning. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilipata hadhi ya kuwa Chuo Kikuu kamili mwaka 1970 kupitia Sheria Na. 12 ya mwaka 1970.

Miaka 60 tangu kuanzishwa kwake, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeendelea kukua Kitaaluma, Kitafiti na Kimiundombinu ambapo idadi ya wanafunzi imefikia 43,307 katika mwaka wa masomo 2020/21 ambapo wanawake ni 19,785 sawa na asilimia 45.7. Chuo hiki kimekuwa na mchango mkubwa katika kuzalisha rasilimaliwatu yenye umahiri katika nchi yetu.

Aidha, tumeshuhudia uanzishwaji wa Vyuo Vikuu vingine vya kimkakati ikiwa ni pamoja na: Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Chuo Kikuu Huria ambacho kinatoa fursa kwa elimu ya juu kwa njia ya masafa. Hadi kufikia mwaka 2021 kuna jumla ya Taasisi za Elimu ya Juu 78 zikiwemo za Umma 48 na binafsi 30.

**Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo**
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilianzishwa rasmi tarehe 01 Julai, 1984 kwa Sheria ya Bunge Na.6 ya mwaka 1984. Chuo kilipewa jina hilo kwa heshima ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati huo Mhe. Edward Moringe Sokoine aliyefariki dunia mwaka 1984.

Chuo hiki kilianzishwa ili kuandaa wataalam wa kilimo katika nyanja mbalimbali. Chuo kilianza na program 3 za masomo mwaka 1984; ambapo zimeongezeka na kufikia 116 mwaka 2021. Aidha, Chuo kimeendelea kujiimarisha kwa kutoa mafunzo kwa vitendo na kufanya tafiti zenye lengo la kuongeza tija katika kilimo na kuongeza thamani ya mazao.

Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET)
Mradi huu uliidhinishwa na Bodi ya Benki ya Dunia mnamo tarehe 27/05/2021. Makubaliano kati ya Benki na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu utekelezaji wa mradi huu yaliyosainiwa tarehe 19/8/2021 chini ya uongozi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Mradi huu utatekelezwa ndani ya miaka mitano una thamani ya Dola za Kimarekani milioni 425 sawa na Shilingi za Tanzania Bilioni 972. Mradi unatarajia kufanya mambo yafuatayo;

(i) Utajenga mabweni 34, vyumba vya mihadhara na madarasa 130, kumbi za mikutano ya kisayansi 23, maabara/karakana 108, na vituo atamizi 10; na kuboresha mitaala zaidi ya 290;

(ii) kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma programu za sayansi, teknolojia, uhandishi na hisabati (STEM) kutoka wanafunzi 40,000 kwa mwaka 2020 hadi kufikia 106,000 mwaka 2026;

(iii) Utasomesha Wahadhiri 623 (wanawake 268, wanaume 355) katika shahada ya Uzamivu (PhD) na Wahadhiri 477 (wanawake 197, wanaume 280) katika shahada ya Umahiri (MSc);

kujenga Chuo Kikuu kipya cha Mwalimu Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia, Butiama; na
(v) kujenga Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Muhimbili cha Afya na Sayansi Shirikishi katika eneo la Mloganzila.
Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kufanikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mradi huu muhimu ambao kwa hakika utaleta mageuzi makubwa katika Elimu ya Juu nchini.

**Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**
Maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu yamekuwa yakitiliwa mkazo na kupewa kipaumbele tangu miaka ya 1960. Sera ya kwanza ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Utafiti ilianzishwa mwaka 1985. Sera hii ilikuwa na malengo ya kutoa mwongozo wa jinsi ya kusimamia masuala ya

sayansi, teknolojia na utafiti nchini, ikiwa ni pamoja na kuchagua, kutathmini na kuhawilisha teknolojia; na kupunguza utegemezi katika teknolojia kutoka nje ya nchi. Mwaka 1996, sera hiyo ilifanyiwa mapitio na kuwa Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 (National Science and Technology Policy, 1996). Mafanikio yaliyofikiwa kwenye Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ni pamoja na:

Kuanzishwa kwa vyuo vya sayansi na teknolojia nchini ambavyo ni: Chuo cha Ufundi cha Dar es Salaam (1962) ambacho sasa kinajulikana kama Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),

Chuo cha Ufundi cha Mbeya (mwaka 1986) ambacho kwa sasa kinajulikana kama Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya; na Chuo cha Ufundi Arusha. Vyuo hivi vilianzishwa mahsusi kwa ajili ya kuzalisha mafundi sanifu katika fani mbalimbali za uhandisi;

Kuanzishwa kwa Chuo cha Ufundi Dodoma ambacho ujenzi wake unaendelea kwa gharama ya shilingi bilioni 17.3 ikiwa ni hatua muhimu kwa Serikali ya awamu ya sita chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kuhakikisha kuwa elimu inaweka msisitizo katika kujenda ujuzi. Ujenzi ulianza Mwezi Agosti 2021 na unatarajiwa kukamilika Februari 2023;

Kuanzishwa kwa Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela, iliyoanza kutoa mafunzo rasmi mwaka 2011. Taasisi hii ilianzishwa ili Kuchochea Sayansi na Teknolojia katika viwango vya kimataifa Barani Afrika. Chuo hiki kinatoa program zinazolenga kujenga uwezo wa nchi ili kuendana na mahitaji ya mapinduzi ya nne ya viwanda;

Kuanzishwa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (Tanzania Atomic Energy Commission - TAEC) kwa Sheria ya Jamhuri ya Muungano Tanzania Na. 7 ya mwaka 2003 ili kusimamia, kudhibiti na kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia nchini;

Kuanzishwa kwa kumbi za atamizi na ubunifu ambapo kumbi ya kwanza iitwayo Buni Hub ilianzishwa Mwaka 2011, ikijikita kwenye ubunifu katika masuala ya TEHAMA. Hadi kufikia mwaka 2021 kuwa jumla kumbi na atamizi za ubunifu 41 ambazo zimewezesha kuanzishwa kwa makampuni machanga 94. Makampuni hayo yamezalisha ajira za moja kwa moja kwa wananchi takribani 600 na ajira zisizo za moja kwa moja kwa wananchi takribani 15,000;

Kupitia mradi wa Mageuzi ya Kiuchumi wa Elimu ya Juu Serikali ya awamu ya sita itaongeza kumbi za atamizi na ubunifu 10 ili kukidhi lengo la Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha wabunifu wanaendelezwa ili bunifu zao zifikie kiwango cha kuingia kwenye kiwango cha biashara; na

Kuanzishwa kwa vituo vya umahiri katika fani za: Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Teknolojia ya ngozi, Teknolojia katika usafiri wa anga, pamoja na Maji na Nishati Jadidifu. Vituo hivi vya umahiri vinajengwa kupitia mradi wa ESTRIP wenye thamani ya shilingi bilioni 174 ambao unatekelezwa katika Chuo Cha Ufundi Arusha, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji.

**Mweleko wa Sekta ya Elimu**

Ndugu Wanahabari; mwelekeo wa Sekta ya Elimu baada ya Miaka 60 ya Uhuru wa nchi yetu ni kuendelea kutoa elimu bora itakayoipatia jamii maarifa na ujuzi unaokidhi mahitaji Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Serikali itachukua hatua zifuatazo ili kuimarisha elimu na kuondoa vikwazo katika upatikanaji wa Elimu:

Serikali itahakikisha kwamba inaboresha mitaala ya elimu katika ngazi zote na kuweka msisitizo zaidi

katika masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Sayansi, Ujasiliamali, Stadi za kazi na masuala mtambuka. Aidha, fani za kimkakati kama vile uhandisi, kilimo, udaktari zitendelea kupewa kipaumbele;

Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya shule ili kuendelea kutoa fursa zaidi kwa watoto wa kike na wa kiume. Kazi hii inafanyika kwa kasi zaidi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ambapo sambamba na ujenzi wa madarasa 15,000 unaoendelea nchini Serikali inatarajia kujenga shule 1,000 za sekondari za kutwa na shule za sekondari 26 za wasichana katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Utekelezaji umeanza kwa shule 274 za kutwa na shule 10 za Wasichana ambapo serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 1,405 mnamo tarehe Novemba, 2021.

3. Elimu ya Ufundi na mafunzo ya ufundi stati itaendelea kuimarishwa. Kwa sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa Vyuo vya ufundi stadi katika Wiaya 29 na Mikoa. Lengo ni kutoa fursa zaidi kwa vijana kupata ujuzi na umahiri utakaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa. Kwa msingi huo,

mafunzo kwa vitendo yatapewa uzito stahiki sambamba na kuimarisha ushirikiano na viwanda ili kuhakikisha wanafunzi wanapata mafunzo yanayozingatia mahitaji halisi ya soko la ajira;

4. Serikali itaendelea kuimarisha elimu maalum kwa kuhakikisha miundombinu inayojengwa ni rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Aidha, Serikali itaendelea kununua vifaa visaidizi ili kuwawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kujifunza kwa ufanisi zaidi;
5. Serikali itaendelea kuondoa vikwazo katika upatikanaji wa fursa za elimu. Wanafunzi waliokatiza masomo yao kwa sababu mbalimbali watapewa fursa ya kurejea shuleni. Fursa hizo zitajumuisha wasichana ambao wanapata ujauzito wakiwa katika shule za msingi au sekondari. Wanafunzi hao wataruhusiwa kuendelea na masomo yao katika mfumo rasmi baada ya kujifungua; na

6. Wanafunzi wanaobainika kufanya udanganyifu katika Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, ambao matokeo yao hufutwa, pamoja na wanafunzi wanaoshindwa kufaulu

mtihani au wanaopata matatizo yoyote wakati wa mitihani watapewa fursa ya kurudia Mtihani mwaka unaofuata. Baraza la Mitihani la Tanzania litatoa utaratibu wa kurudia mitihani. Aidha, wanafunzi ambao na watakaofaulu mitihani ya marudio watapata fursa ya kuchaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari katika shule za serikali. Hatua hiyo imezingatia kuwa, watahiniwa wa Kidato cha Nne na Kidato cha Sita wanaofutiwa matokeo yao, wanashindwa kufaulu na wanaopata matatizo hupewa fursa ya kurudia mtihani. Hivyo, Serikali imeona umuhimu wa kuwapa nafasi ya pili wanafunzi wanaomaliza Elimu ya Msingi kama inavyofanyika kwa wanafunzi wa Sekondari. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa hatua kali za kinidhamu zinachukuliwa dhidi ya watumishi wote watakaobainika kuhusika na udanganyifu katika mitihani yote ya Taifa.

Serikali itaendelea kutoa elimu bila malipo ili kuhakikisha kuwa watoto wote wakitanzania wanapata elimu bila vikwazo. Aidha, Serikali itaendelea kutoa mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti iliyoongezeka kutoka bilion 464 hadi 570.

Ndugu wanahabari; Naomba nihitimishe kwa kusema kwamba Serikali ya Awamu Sita itaendelea kuboresha elimu, sayansi na teknolojia kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake ya dhati ya kuinua sekta ya elimu. Tumeshuhudia mambo makubwa ambayo yamefanyika katika sekta ya elimu ndani ya kipindi cha miezi nane tu ya uongozi wake. Hivyo, ninawaomba na kuwasihi saana watanzania wenzangu tuendelee kumuunga mkono Rais wetu ili dhamira yake njema ya kuleta maendeleo katika nchi yetu na ustawi wa watanzania iweze kufikiwa.

Mwisho nichukue nafasi hii kuwapongeza Watanzania wote kwa kusherehekea Miaka 60 ya Uhuru wa nchi yetu na KAZI IENDELEE.

Mungu Ibariki Tanzania Mungu Wabariki Watanzania Wote Asanteni kwa Kunisikiliza.



# MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

UTANGULIZI

Ndugu Wanahabari, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijalia Nchi yetu neema ya kuwa na rasilimali nyingi za asili ikiwemo rasilimali kubwa ya mazao ya mifugo, uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji.

Ndugu Wanahabari, kabla sijaendelea, kwa namna ya pekee, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi yetu kwa busara, hekima na umakini mkubwa, ambao umeiwezesha Nchi yetu kuendelea kupiga hatua kubwa za kimaendeleo katika nyanja za kijamii na kiuchumi. Ni dhahiri kuwa tunapoelekea kufikia kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru, ifikapo tarehe 9 Desemba, 2021 tumesikia kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia na sisi wenyewe tumeshuhudia mafanikio mengi na makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi thabiti wa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ndugu Wanahabari, mafanikio hayo yanajumuisha yale yaliyopatikana kupitia kwa Viongozi wa Serikali wa awamu zilizotangulia kuanzia mwaka 1961 Nchi yetu ilipopata Uhuru. Nichukue fursa hii kumwombea Kiongozi wetu kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa yeye na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa, afya njema, hekima na busara ili waendelee kuiongoza Nchi yetu kwa weledi mkubwa na kuiwezesha kupata maendeleo endelevu na maisha bora kwa kila Mtanzania.

Ndugu Wanahabari, naomba nitumie fursa hii kuwatambua, kuwaenzi na kuwashukuru Waasisi wa Taifa letu, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uongozi wao thabiti uliofanikisha Taifa letu kupata Uhuru mwaka 1961 na kufanikisha Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Ndugu Wanahabari, ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia sisi Watanzania na Nchi yetu kuweza kulinda na kudumisha tunu za Taifa letu zilizoasisiwa na Waasisi wetu ambazo ni amani, umoja na mshikamano, Uhuru wa Nchi yetu; Muungano na Mapinduzi ya Zanzibar. Tunu hizi ni muhimu kwa ajili ya kuwawezesha Wananchi wetu wote wakiwemo wafugaji, wavuvi na Wakuzaji wa viumbe maji kuendelea kutekeleza shughuli zao za kimaendeleo kwa amani na utulivu, bila hofu.

Ndugu Wanahabari, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatambua mchango mkubwa wa vyombo vya habari na Wanahabari kwa kufanya kazi nzuri ya kuwafikishia Wananchi taarifa muhimu za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa; sambamba na kuwaelimisha kuhusu masuala mbalimbali ya Nchi yetu ikiwemo kufahamu mafanikio yaliyoatikana kwa kiindi cha miaka 60 ya Uhuru. Kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Wanahabari kwa mchango wenu mkubwa na muhimu kwa Taifa letu. Aidha, kwa namna ya pekee niwashukuru kwa kuitangaza sekta ya mifugo na uvuvi ambayo ni tegemeo la Watanzania wengi. Takwimu zinaonyesha kwamba Sekta hizi za mifugo na uvuvi ambazo kwa tafsiri za kimataifa za kitakwimu zipo ndani ya sekta pana ya kilimo zinatoa ajira kwa kaya takriban asilimia 65 ya Watanzania.

**A: SEKTA YA MIFUGO**

**1.0 Idadi ya Mifugo Nchini**

Ndugu Wanahabari, idadi ya mifugo imeongezeka kutoka ng'ombe milioni 8.0, mbuzi milioni 4.4, kondoo milioni 2.99 na nguruwe 22,000 mwaka 1961 hadi ng'ombe milioni 33.9, mbuzi milioni 24.5, kondoo milioni 8.5 na nguruwe milioni 3.2 mwaka 2020 (Taarifa ya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, 2020). Pia, katika mwaka 2021 wapo kuku milioni 87.7 wakiwemo kuku wa asili milioni 40.4 na kuku wa kisasa milioni 47.3. Aidha, ongezeko kubwa la mifugo kutoka milioni 15.4 mwaka 1961 hadi kufikia milioni 67.3 limesababisha changamoto ya migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ambapo Mhe. Rais wa awamu ya Tano aliagiza kuundwa kwa Kamati ya mawaziri 8 ambayo ilizunguka nchi nzima na kuwasilisha taarifa ambayo ilipelekea Mhe. Rais kutoa maelekezo yafuatayo:

(i)Kurasimisha vijiji 975 ambavyo vilikuwa na migogoro ya matumizi ya ardhi na hifadhi, mashamba, ranchi, mapori ya akiba na vyanzo vya maji visiondolewe katika maeneo vilipo.
(ii)Kufuta baadhi ya maeneo ya hifadhi za misitu na maeneo tengefu na kuagiza yagawiwe kwa wananchi kwa kwa ajili ya mifugo, kilimo na makazi. Jumla ya mapori Tengefu 12 yenye jumla ya ekari 707, 659.94 yamefutwa na misitu saba (7) yenye ukubwa wa ekari 46,247.56 yamefutwa.
(iii)Hifadhi 14 na mashamba 16 yasiyoendelezwa yamegwe na kugawiwa kwa wananchi kwa shughuli za mifugo,kilimo na makazi.
(iv)Kuweka mwongozo wa matumizi kwa maeneo ya mita 500 katika maeneo ya kinga (buffer zone) katika hifadhi nchini na mita 60 katika hifadhi ya vyanzo vya maji ili ziendelee kutumiwa na wananchi namna ambayo haitaathiri mazingira.

1.1Uboreshaji wa mifugo nchini na miundombinu ya minada

Ndugu Wanahabari, asilimia 97 ya ng'ombe wanaofugwa hapa nchini ni wale wa asili ambao uzalishaji wake ni kiwango cha chini. Katika kutatua chamgamoto hiyo Serikali imeongeza matumizi ya mbegu bora kwa njia ya uhimilishaji yameongezeka kutoka uhimilishaji wa ngombe 12,500 mwaka 1961 hadi ng'ombe 77,400 kwa mwaka 2020/2021. Kituo cha Taifa cha uhimilishaji (National Artificial Insemination Center – NAIC) Usa River kimejengewa uwezo na kufikia uwezo wa kuzalisha dozi 1,000,000 za mbegu bora za mifugo kwa mwaka. Katika juhudi za kufikisha teknolojia ya uhimilishaji kwa wafugaji, vituo saba (7) vya kanda vimeanzishwa. Vituo hivyo vimeanzishwa katika Kanda za Mashariki (Kibaha), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Njombe na Mpanda), Ziwa (Mwanza), Kati (Dodoma) na Kusini (Lindi). Aidha, wizara imeendelea kujenga uwezo wa wataalam wa uhimilishaji ambapo katika mwaka 2021 kuna jumla ya wataalamu 2,700 waliopatiwa mafunzo ya uhimilishaji.

Ndugu Wanahabari, Katika upande wa minada mwaka 1961 kulikuwa na minada ya awali 300 ikilinganishwa na minada ya wali 506 mwaka 2021, minada ya upili 8 na minada ya mpakani 4 ikilinganishwa na minada ya upili 18 na minada ya mpakani 13 mwaka 2021. Aidha, ongezeko hili limechangiwa na juhudi kubwa ya serikali katika kuwekeza kwenye ukarati na ujenzi wa minada mipya ili kuwezesha mazingira bora ya biashara kwa wafugaji wa ndani na nje ya nchi.

1.2 Uzalishaji wa Maziwa

Ndugu Wanahabari, uzalishaji wa maziwa wakati nchi inapata uhuru (1961) ulikuwa lita 334,000 kwa mwaka ikilinganishwa na lita bilioni 3.1 kwa mwaka katika mwaka 2020/2021. Aidha idadi ya ng'ombe wa maziwa wameongeka kutoka takribani 198,000 mwaka 1961 hadi milioni 1.2 mwaka 2021. Ongezeko kubwa la ng'ombe hao limetokana na kuingizwa kwa ng'ombe kutoka nje ya nchi, kuwepo kwa miradi hususan ya kopa ng'ombe lipa ng'ombe, mashamba ya watu binafsi ya kuzalisha mitamba na utekelezaji wa mazozi ya uhimilishaji. Pia, Wizara inazalisha mitamba ya ng'ombe wa maziwa kutoka kwenye mashamba ya Mabuki, Ngerengere, Sao Hill, Nangaramo na Kitulo ambayo huzalisha wastani wa mitamba 3,500 kwa mwaka.

1.3 Usindikaji wa Maziwa

Ndugu Wanahabari, Usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka wastani wa lita 41,026,000 kwa mwaka 1961 hadi wastani wa lita milioni 75.9 kwa mwaka 2021. Aidha, idadi ya viwanda vya kusindika maziwa imeongezeka kutoka viwanda 7 vya umma mwaka 1974 vilivyokuwa vinasindika maziwa kutokana na maziwa ya unga yaliyotoka nje ya nchi hadi viwanda vya sekta binafsi 105 mwaka 2021 vinavyosindika maziwa yanayozalishwa hapa nchini. Viwanda hivi kwa sasa (2021) vina uwezo wa kusindika wastani wa lita 871,700 za maziwa kwa siku. Mafanikio haya yametokana na viwanda kuwa na vyanzo vya kupata maziwa kutoka kwa wafugaji wadogo, vikundi na vyama vya ushirika vya wafugaji. Kwa mfano; Kiwanda cha Tanga Fresh, ASAS, Kilimanjaro Fresh, Galaxy Food and Bevarage na Milcom wanapata maziwa kutoka mtandao wa vyama 33 vya ushirika vya kukusanya maziwa

1.4 Tasnia ya Nyama

Ndugu Wanahabari, uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani 97,000 mwaka 1961 hadi tani 738,166 mwaka 2021. Kati ya hizo, nyama ya ng'ombe ni tani 508,355.17, mbuzi na kondoo tani 102,137.22, nguruwe tani 41,467.82 na kuku tani 86,205.78. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya nyama .. Aidha, Uzalishaji wa Nguruwe unatokana na nguruwe chotara kati ya nguruwe wa asili na aina za Large White, Landrace na Hampshire. Uzalishaji wa nyama ya nguruwe ni wastani wa kilo 50 kwa nguruwe mmoja

1.5 Viwanda vya kusindika nyama

Ndugu Wanahabari, viwanda vya kusindika nyama vimeongezeka kutoka kiwanda kimoja mwaka 1961 (Tanganyika Parkers) kilichokuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 800 kwa siku hadi kufikia viwanda 11 vyenye uwezo wa kusindika tani 374 kwa siku . Machinjio za kisasa 24 zenye uwezo wa kuchinja ngombe 6,360, mbuzi na kondoo 16,050 na kuku 36,500 kwa shift moja kwa siku mwaka 2021 zenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 324,800 na mbuzi/kondoo 800,000 kwa mwaka. Viwanda hivi vimeongeza upatikanaji wa nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Aidha, soko la nyama nje ya nchi mwaka 1961 lilikuwa tani 2,150 ikilinganishwa na tani 5,560 kwa mwaka 2020/2021

**1.6 Tasnia ya Ngozi**

Ndugu Wanahabari, tangu mwaka 1961 biashara ya ngozi ilifanywa na sekta binafsi ikiwemo kampuni ya Tom Booth kutoka nchini Uingereza. Zao la ngozi ndilo limekuwa likiuzwa zaidi nje ya nchi ikilinganishwa na mazao mengine yatokanayo na mifugo na kuipatia nchi fedha za kigeni. Ukusanyaji wa ngozi umeongezeka kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe milioni 1.1, za mbuzi milioni 1.275 na za kondoo milioni 0.4 mwaka 1965 na kufikia ngozi za ng'ombe milioni 4.17, za mbuzi milioni 5.96 na za kondoo milioni 1.64 mwaka 2021. Aidha, mwaka 1961 jumla ya vipande 1,518 vya ngozi viliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na vipande milioni 1.5 vilivyouzwa nje ya nchi katika mwaka 2020/2021. Mwaka 1961, tulikua tuna kiwanda kimoja cha ngozi (Himo Tanneries) ambacho kilikuwa kinamilikiwa na sekta binafsi. Hadi kufikia mwaka 2021 tuna viwanda 9 vya kuchakata ngozi, aidha viwanda vinavyofanya kazi ni vinne ambavyo ni Ace leather, Himo Tanneries and Planters, Phiss Tannery na Moshi Leather.

**1.7 Hali ya Magonjwa ya Mifugo nchini**

**1.7.1 Magonjwa ya kipaumbele**

Ndugu Wanahabari, udhibiti wa magonjwa ya mifugo nchini ulianza katika miaka ya 1880 wakati wa ukoloni chini ya utawala wa Wajerumani. Katika kipindi hicho, maabara ya kwanza ilijengwa Ngarenanyuki mkoani Arusha ambayo baadae ilihamishiwa Mpwapwa. Huduma za mifugo katika miaka ya 1880 zilianza kutokana na matukio mbalimbali ya Ugonjwa ya Sotoka na Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (Contagious Bovine Pleuro-pneumonia, CBPP). Katika mwaka 1905, kupitia Kituo cha Utafiti – Mpwapwa Serikali ya Kikoloni ilijenga josho la kwanza Afrika ya Mashariki katika eneo la Nunge - Mpwawa ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe.

Ndugu Wanahabari, kumekuwepo na Mafanikio ya udhibiti wa magonjwa ambayo yametokana na kuwa na mfumo endelevu wa uratibu wa udhibiti wa magonjwa ya mifugo kulingana na miongozo ya kitaifa na kimataifa. Katika kuhakikisha udhibiti wa magonjwa unafanyika kwa ukamilifu Serikali ili tambua magonjwa 13 ya kipaumbele ambapo uwekezaji mkubwa umefanyika katika kuyadhibiti kwa kujenga kiwanda cha chanjo cha Serikali kinachozalisha chanjo aina 7 mwaka 2021 ikilinganishwa na chanjo 0 mwaka 1961.

Ndugu Wanahabari, Chanjo aina 7 za magonjwa ya kipaumbele zinazalishwa kupitia Taasisi ya kuzalisha Chanjo Tanzania (TVI) iliyopo Kibaha. Aidha, aina ya chanjo za magonjwa ya mifugo zinazozalishwa ndani ya nchi ni ya Mdondo kwa kuku; Kimeta kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo; Chambavu kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo; Chanjo mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu; Ugonjwa wa Kutupa Mimba kwa ng'ombe; Homa ya Mapafu ya ng'ombe; na Homa ya Mapafu ya mbuzi. Pia, chanjo mbili (2)

mpya za Kichaa cha Mbwa na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo ziko katika hatua za awali za utengenezaji.

Ndugu Wanahabari, mwaka 2021, chanjo mpya (Tatu Moja) imegunduliwa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Chanjo hiyo inatumika kuzuia magonjwa matatu ya kuku (Mdondo, Ndui ya Kuku na Mafua ya Kuku) ambayo imeanza kutumika kuanzia tarehe 01 Machi na inazalishwa na Kiwanda cha NOVABI kilichopo Morogoro.

Ndugu Wanahabari, pia, Kiwanda cha kuzalisha Chanjo cha Hester Bioscience kilichopo Mkoani Pwani ujenzi wake umekamalika na uzalishaji wa Chanjo za Wanyama zaidi ya (27) unategemea kuanza hivi karibuni.

Ndugu Wanahabari, Kufuatia juhudi nilizozitaja hapo juu kumekuwepo na ongezeko la dozi za chanjo zinazozalishwa nchini kwa mwaka ambapo mwaka 1961 hakukuwa na chanjo zilizokuwa zikizalishwa nchini hadi kufikia dozi milioni 63.6 (sawa na 6.8% ya mahitaji) mwaka 2020/2021 ambayo ni jumla ya dozi 936,269,700. ili kuwezesha upatikanaji wa uhakika chanjo, Serikali iliweka utaratibu wa kuagiza chanjo ambazo hazizalishwi hapa nchini ambapo uagizaji umeongeka kutoka dozi 1328 mwaka 1961 hadi kufikia dozi 13,750,000 mwaka 2020/2021. Juhudi hizi zimeongeza kiwango cha uchanjaji kutoka 15% mwaka 1961 hadi kufikia 56% mwaka 2021 kwa magonjwa ya kipaumbele.

**1.7.2 Kutokomeza Ugonjwa wa Sotoka (Rinderpest)**

Ndugu Wanahabari, idadi kubwa ya vifo vya mifugo vilivyotokana na Sotoka viliripotiwa kwa mara ya kwanza mwaka 1928 Loliondo - Arusha. Ugonjwa huu ulidhibitiwa kwa kuweka karantini, kudhibiti uhamaji holela wa mifugo pamoja na kutoa chanjo ya kinga ya ‘hyperimmun sera’ iliyotengenezwa Mpwapwa. Katikati kipindi cha miaka ya 1960 kampeni ya chanjo ya ng’ombe dhidi ya Sotoka ilitokomeza ugonjwa huo katika Afrika ya Mashariki. Ugonjwa huo ulilipuka tena mwaka 1982 ambapo Serikali iliendesha kampeni dhidi ya Sotoka kila mwaka na hatimaye kuutokomeza nchini mwaka 2005. Tanzania imepata cheti cha Shirika la Wanyama Ulimwenguni (OIE) cha kuwa huru na maambukizi ya Ugonjwa wa Sotoka mwaka 2007.

**1.7.3 Udhibiti wa Magonjwa yaenezwayo na Kupe**

Ndugu Wanahabari, kazi ya udhibiti wa kupe na magonjwa yaenezwayo na kupe ilianza na ujenzi wa josho Mpwapwa mwaka 1905, ikifuatiwa na kutungwa kwa Sheria ya Uogeshaji Mifugo (Animal Diseases Ordinance) ya mwaka 1940. Wakati wa uhuru, Tanzania ilikuwa na jumla ya majosho 707 na kwa sasa kuna jumla ya majosho 2,763 sawa na ongezeko la asilimia 344. Changamoto kubwa ya miundombinu ya majosho kwa kipindi kirefu imekuwa ikitelekezwa na kuharibiwa ikiwa ni pamoja na kuingiliwa na miji na shughuli za kibinadamu. Ili kukabiliana na changamoto hii Serikali imeanzisha mkakati wa kuyatambua na kuyapima maeneo yote yenye miundombinu kwa lengo la kuyamilikisha kwa jamii za watumiaji.

Katika jitihada za kudhibiti kuenea kwa magonjwa yaenezwayo na kupe, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

(i) Serikali kununua dawa za kuogesha mifugo ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe ambapo wafugaji hupatiwa dawa hizo kwa ruzuku ya asilimia 100;

(ii) Wastani wa uogeshaji wa mifugo kwa mwaka ni michovyo 360,000,000 sawa na asilimia 23 ya mifugo iliyopo ikilinganishwa na michovyo 5,891 mwaka 1960 sawa na asilimia 0.001 ya mifugo iliyokuwepo.

(iii) Magonjwa yaenezwayo na kupe yamepungua kutoka matukio 1,256 mwaka 1961 hadi matukio 5,985 mwaka 2021.

1.7.4 Udhibiti wa Magonjwa yanayoenezwa na Mbung’o

Ndugu Wanahabari, mbung’o anaeneza Ugonjwa wa Nagana kwa mifugo na Malale kwa binadamu. Tukio la kwanza la ugonjwa wa malale (sleeping sickness) liliripotiwa katika Wilaya ya Maswa, mkoani Shinyanga mwaka 1929. Mwaka 1967, uchunguzi wa mtawanyiko wa mbung’o ulibaini kuwa asilimia 60 ya eneo la nchi linakaliwa na mbung’o.
Katika miaka ya 1960 hadi 1980 mbinu za udhibiti wa mbung’o ziliendelea kuwa za ufyekaji wa vichaka na mapori pamoja na kunyunyizia viuatilifu. Aidha, teknolojia hiyo ilikuwa inaharibu mazingira.

Baada ya miaka ya 1980 teknolojia mpya ambazo haziharibu mazingira zilianza kutumika ili kudhibiti mbung’o. Teknolojia hizo ni pamoja na mitego ya mbung’o, vyambo (vitambaa vya rangi ya buluu na nyeusi) pamoja na kupaka/kuogesha ng’ombe kwa kutumia viuatilifu. Aidha, teknolojia ya mbung’o hasi (Sterile Insect Technique - SIT) ambao wanafugwa katika maabara ya Kituo cha Utafiti wa Mbung’o na Ndorobo kilichopo Tanga ilitumika katika kisiwa cha Unguja kutokomeza mbung’o aina ya Glossina austeni mwaka 1997.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na jitihada za kudhibiti mbung’o na magonjwa waenezayo ni pamoja na:-

(i) Uanzishwaji wa makazi, kilimo na ufugaji katika maeneo yaliyokuwa hayatumiki kutokana na kukaliwa na mbung’o;

(ii) Kupungua kwa ugonjwa wa malale kwa binadamu kutoka wagonjwa 1,700 (1991 - 1995) hadi wagonjwa 6 (2019 - 2021);

(iii) Mwaka 1997, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kutokomeza mbung’o (aina ya Glossina austeni) na ugonjwa wa Nagana katika Kisiwa cha Unguja kwa kutumia teknolojia ya Sterile Insect Technic (SIT); na

(iv) Kupungua kwa eneo lililokuwa linakaliwa na mbung’o nchini kutoka asilimia 60 mwaka 1967 hadi asilimia 33 mwaka 2021.

1.8 Viwanda vya Dawa za Wanyama

Ndugu Wanahabari, uzalishaji wa dawa za wanyama nchini ulianza baada ya Uhuru ambapo kwa sasa vipo viwanda vinne (4) vinavyozalisha dawa za wanyama ambavyo ni Farmers Centre (Buguruni –DSM); Farmbase (DSM) ; Farm Access Ltd (Arusha) na Tanveterina (Kibaha-Pwani).

1.9 Utambuzi wa Mifugo kwa Kutumia Hereni za Kieletroniki

Ndugu Wanahabari, utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ulianza mwaka 2014 mpaka 2017 ambapo ng'ombe zaidi ya milioni 17 walitambuliwa kupitia njia ya asili (walipigwa chapa) ambapo kanzidata ya TANLITS ilitumika kuweka kumbukumbu za utambuzi ili kuwezesha ufuatiliaji wa mifugo. Utambuzi wa mifugo kwa njia ya asili ulikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na utunzaji duni wa kumbukumbu za mifugo na wakati mwingine kuharibika kwa ubora wa ngozi kutokana na vidonda.

Kati ya mwaka 2019 na 2020, Serikali ilianza utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kawaida hususani kwa ng'ombe wa maziwa. Mwaka 2021, Serikali ilianza kutumia mfumo wa matumizi ya hereni za kielektroniki (elektroniki eartags) ambapo taarifa za mifugo zinawekwa kwenye mfumo wa kielektroniki ambao unawezesha kupatikana kwa taarifa za mifugo kupitia vifaa mbalimbali vya mawasiliano ikiwemo simu janja.

1.10 Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Mifugo na Wataalam

Ndugu Wanahabari, usimamizi wa utoaji wa huduma za mifugo na wataalam ulianza kuratibiwa toka mwaka 1958 chini ya Sheria ya Veterinary Surgeons Ordinance (CAP 376)

Mafanikio yaliyopatikana tangu uhuru katika kusimamia utoaji wa huduma za mifugo na taaluma ya veterinari ni pamoja na:-

(i) Idadi ya Madaktari wa Mifugo waliosajiliwa imeongezeka kutoka madaktari 39 mwaka 1961 ambao wote walikuwa ni wageni hadi Madaktari 1,061 mwaka 2021 ambapo asilimia zaidi ya 99 ni Watanzania;

(ii) Kuandikishwa na kuorodheshwa wataalam wasaidizi wa afya ya wanyama ambapo hadi sasa jumla ya wataalam wasaidizi 4,332 wenye astashahada (2317) na stashahada (2015) wameandikishwa na kuorodheshwa sawia;Pia wakaguzi wa nyama (858), wahimilishaji (74) na wataalam wa maabara (65) wamepewa leseni za kutoa huduma ikilinganishwa na mwaka 1961 ambapo kulikuwa na wataalam (25) tu waliokuwa wamesajiliwa na kuorodheshwa; na

(iii) Aidha, vituo vya kutolea huduma ya afya ya wanyama (Veterinary facilities) vimeboreshwa. Hadi mwaka 2021 jumla ya vituo 2047 vya kutolea huduma ya wanyama vimesajiliwa. Vituo hivyo vinajumuisha Hospitali ya wanyama (1), Kliniki za wanyama (24), na Vituo vya afya ya wanyama na karantini (2022) ikilinganishwa na vituo (12) mwaka 1961.

**1.11 Malisho na Maji ya Mifugo**

Ndugu Wanahabari, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi na Halmashauri za Wilaya, imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazohusu utengaji na upimaji wa maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo malisho ya mifugo.Mwaka 1961 utaratibu wa kupanga matumizi ya ardhi ikiwemo maeneo ya malisho kwa mifugo haukuwepo. Juhududi zilizofanywa na serikali ni kutunga Sheria ya ardhi ya vijiji sura 114, sheria ya upangaji matumii ardhi sura 116, sheria ya maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula vya wanyama sura 180, kuundwa kwa tume ya Taifa ya matumizi ardhi kwa lengo la kupanga matumizi ya ardhi. Kufuatia juhudi hizo jumla hekta 3,060,562.27 zimepatikana mwaka 2020/2021. Vilevile mwaka 1961 kulikuwa na mabwawa/malambo ya maji 60 na hakukuwa na visima virefu vya maji ya mifugo ikilinganishwa na mabwawa/malambo 1,302 na visima virefu 103 kwa mwaka 2021.

1.12 Matarajio ya Baadaye kwa Sekta ya Mifugo

Ndugu Wanahabari, Wizara inaendelea kutekeleza Mpango Kabembe wa Sekta ya Mifugo (Tanzania Livestock Master Plan – TLMP) unaotekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2017/18 hadi 2031/32. Pia, Wizara imeandaa Mpango Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi 2025/26. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2021/22 hadi 2025/26), Serikali ina matarajio yafuatayo kwa sekta ya mifugo:-

(i) Kubadilisha mfumo wa ufugaji kutoka ufugaji wa asili kuwa na ufugaji wa kibiashara wenye tija kubwa zaidi ili kuiwezesha sekta ya mifugo kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Lengo ni kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya mifugo kutoka asilimia 5.0 hadi asilimia 6.5 kwa mwaka.

(ii) Kuongeza ulaji wa mazao ya mifugo hususan ulaji wa nyama kutoka kilogramu 15 hadi 25 kwa mtu kwa mwaka; unywaji wa maziwa kutoka lita 54.7 hadi 100 kwa mtu kwa mwaka. Ongezeko hilo la ulaji wa mazao ya mifugo litatokana na kuongeza uzalishaji wa nyama na maziwa pamoja na kuhamasisha ulaji wa mazao hayo kwa ajili ya kuboresha lishe za kaya.

(iii) Kupunguza vifo vya mifugo kutokana na magonjwa kutoka asilimia 27 hadi asilimia 12 kwa mwaka. Lengo hili litafikiwa kwa kuongeza idadi ya majosho kutoka 2,763 hadi 11,738; na kuongeza uogeshaji kutoka asilimia 25 hadi 50.

(iv) Kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita bilioni 3.1 hadi lita bilioni 4.3 kwa mwaka. Ongezeko hili litatokana na kuongeza idadi ya ng'ombe bora wa maziwa kwa kuhimilisha ng'ombe 1,000,000 kila mwaka na kuongeza uzalishaji wa mitamba kutoka katika mashamba ya Serikali na watu binafsi. Pia, Serikali kwa yanayozalishwa nchini.

kushirikiana na sekta binafsi itaongeza usindikaji wa maziwa kutoka asilimia 5 hadi 14 ya maziwa yote

(v) Kuongea uzalishaji wa nyama kutoka kwa ng'ombe wa asili (uzito wa ng'ombe kwa Kg – Carcas weight) kutoka kilogramu 75 hadi kilogramu 130. Ongezeko hili litatokana na kuboresha mbari za mifugo ya asili na kuhamasisha wafugaji kuingia katika mifumo ya unenepeshaji mifugo.

(vi) Kuongeza uzalishaji wa nyama kutoka tani 750,000 hadi tani 951,700 kwa mwaka kwa kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vya nyama na machinjio za kisasa. Pia, Serikali kwa kushirikiana na wadau hususan kutoka sekta binafsi itaongeza usindikaji wa nyama kutoka Tani 300 hadi 500.

(vii) Ili kuwawezesha wafugaji kufikiwa na huduma za ugani Serikali itaanzisha mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuwafikia wafugaji wengi zaidi na huduma za ugani. Pia, Serikali itaongeza idadi ya mashamba darasa na mashamba ya mfano ya malisho katika vijiji, halmashauri za wilaya na miji kutoka mashamba darasa 108 hadi 1,088.

(viii) Kuongeza eneo la malisho kwa kutenga, kupima, kumilikisha na kuendeleza maeneo hayo kutoka hekta milioni 3.06 hadi hekta milioni 6.0. Ongozeko hilo la maeneo ya malisho litapunguza migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi pamoja na kuwaepusha wafugaji kuhamahama wakitafuta malisho.

(ix) Kutekeleza Mwongozo wa Upatikanaji, Uendelezaji na Usimamizi wa Maeneo ya Malisho. Utekelezaji wa Mwongozo huo, utasaidia upatikanaji wa maeneo ya malisho na maji ikiwa ni pamoja na kuweka mifumo endelevu ya usimamizi wa maeneo ya malisho na miundombinu ya maji. Serikali imepanga kuongeza idadi ya malambo kutoka 1,384 hadi 1,487 na visima virefu kutoka 1,842 hadi 2,067 kwa ajili ya mifugo.

## SEKTA YA UVUVI

### 2.0 Rasilimali za Uvuvi

Ndugu Wanahabari, Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi za uvuvi, ambapo eneo la ardhi lililofunikwa na maji lina ukubwa wa takribani kilomita za mraba 62,000 sawa na asilimia 6.5 ya eneo lote la ardhi katika mgawanyiko ufuatao: Ziwa Victoria kilomita za mraba 35,088; zenye wingi wa samaki tani 3,465,913; Ziwa Tanganyika kilomita za mraba 13,489 zenye wingi wa samaki tani 295,000; Ziwa Nyasa kilomita za mraba 5,760 zenye wingi wa samaki tani 168,000; Ziwa Rukwa kilomita za mraba 3,000; Ziwa Eyasi kilomita za mraba 1,000, na maeneo madogo ya maji (maziwa madogo, mito, na mabwawa) kilomita za mraba 1,000. Kwa upande wa maji bahari, nchi ina eneo la kilomita za mraba 1,000. Kwa upande wa maji baridi, nchi ina eneo la kilomita 64,000 na ukanda wa pwani wenye urefu wa kilomita 1,424 kutoka mpaka wa kaskazini na Kenya hadi mpaka wa kusini na Msumbiji. Ukanda wa Uchumi wa Bahari una ukubwa wa maili za majini zipatazo 200 sawa na kilomita za mraba 223,000 linaloipa nchi eneo la bahari na rasilimali za uvuvi. Maeneo haya ya maji yana rasilimali nyingi za uvuvi pamoja na fursa za uendelezaji wa ufugaji viumbe kwenye maji katika maji ya bahari na maji baridi.

2.1 Umuhimu wa Sekta Ya Uvuvi

Ndugu Wanahabari, kwa ujumla, sekta ya uvuvi ni miongoni mwa sekta tatu za Kilimo ambazo zinaajiri wananchi wengi. Sekta ya Uvuvi imeweza kutoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi 195,435 na wakuzaji viumbe maji wapatao 30,064. Aidha, zaidi ya wananchi milioni 4.5 wanakadiriwa kupata kipato chao cha kila siku kutokana na shughuli za Uvuvi, zikiwemo kuunda na kutengeneza boti, kushona nyavu, biashara ya samaki na mazao yake pamoja na Baba na Mama lishe. Pia, samaki huchangia takriban asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama. Sekta hii inachangia katika Pato la Taifa kwa asilimia 1.7.

### 2.2 Mafanikio Yaliyopatikana Katika Sekta ya Uvuvi Kuanzia 1961 Hadi 2021

### 2.2.1 Sera, Sheria, Kanuni, Mipango na Mikakati

Ndugu Wanahabari, Sekta ya Uvuvi ni mwongoni mwa sekta za uzalishaji mali ambayo ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya usimamizi na uratibu wa uendeshaji wa shughuli za uvuvi nchini. Pia, ina jukumu la kuendeleza Wataalam (rasilimali watu) katika sekta hizi;

Ndugu Wanahabari, Nchi yetu ilipopata uhuru mwaka 1961, Sekta ya Uvuvi haikuwa imeainishwa kama sekta kamili, kwa hiyo shughuli za uvuvi zilikuwa zikifanyika chini ya sekta ya kilimo iliyokuwa chini ya Wizara ya Kilimo, Misitu na Wanyamapori. Kutokana na hali hiyo, hapakuwepo na sera mahsusi ya maendeleo ya sekta ya uvuvi Nchini, bali shughuli za uvuvi zilisimamiwa kupitia Sheria ya Uvuvi iliyojulikana kama "Fisheries Ordinance and Trout Protection Ordinance - CAP 368". Kupitia Sheria hiyo, mfumo wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi ulikuwa ni kutoka juu kwenda chini (Centralized management).

Ndugu Wanahabari, Sera ya kwanza ya Sekta ya Uvuvi iliandaliwa Mwaka 1997. Aidha, kutokana na mabadiliko yaliyojitokeza ya kiuchumi, kijamii na maendeleo ya teknolojia kuhusiana na matumizi ya rasilimali za uvuvi, hasa kuanzia miaka ya 2000 na 2010, Serikali ilifanya mapitio ya Sera ya awali ya Uvuvi ya mwaka 1997 na kutunga Sera Mpya ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015. Sera hiyo mpya inalenga kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, matumizi endelevu na udhibiti wa masoko, kuendeleza ukuzaji wa viumbe maji na uhifadhi wa ikolojia na mazingira ya kwenye maji pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Pia, Sera ililenga kukuza uvuvi wa kibiashara kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari (EEZ).

Ndugu Wanahabari, kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 1961 hadi 2021 Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) imefanikisha kutungwa kwa jumla ya Sheria tano (5) zinazohusika na usimamizi wa matumizi ya rasilimali za uvuvi pamoja na kuandaliwa kwa Kanuni zinazohusu Sekta ya Uvuvi kumi na tatu (13) na Miongozo sita (6). Baadhi ya Sheria na Kanuni hizo zimefutwa, au kufanyiwa marekebisho ili kuendana na wakati na mabadiliko ya kisera, kiuchumi na

kijamii. Aidha, zoezi la kutafsiri Kanuni za uvuvi kutoka lugha ya kiingereza kwenda lugha ya kiswahili linaendelea ili kuwezesha wadau wa Kanuni hizo kuzielewa vizuri.

**2.2.2 Kuimarisha Usimamizi wa Sekta ya Uvuvi Nchini**

**2.2.2.1 Uvunaji wa Rasilimali za Uvuvi kutokana na maji asili (Uvuvi mdogo)**

Katika kipindi cha mwaka 1961 – 1988 shughuli za uvuvi katika maeneo yote ya uvuvi nchini zilikuwa zikifanywa na wavuvi wadogo. Kiasi cha samaki kilichozalishwa na wavuvi wadogo kutoka kwenye maji asili kimeonekana kuongezeka kutoka tani 385,771.80 zenye thamani ya shilingi Bilioni 7.73 mwaka 1986 hadi tani 473,592.24 zenye thamani ya shilingi Trilioni 2.36 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 18.54. Kwa ujumla uzalishaji wa samaki umeonekana kuongezeka na kupungua mwaka hadi mwaka. Hali hii inaashiria kuboreka kwa shughuli za uvuvi na maisha ya wavuvi wadogo nchini.

**2.2.2.2 Uvunaji wa Rasilimali za Uvuvi kibiashara**

Baada ya nchi yetu kupata uhuru, wavuvi wadogo waliendelea kutumia zana duni za uvuvi ambapo takribani asilimia 80 ya vyombo vyote vya uvuvi vilikuwa vikitumia kasia kama nyenzo. Mwaka 1987, kati vyombo 6,667 vilivyokuwa vikifanya shughuli zake katika Ziwa Victoria, ni vyombo 172 vilivyokuwa vikitumia injini za kisasa ukilinganisha na mwaka 2008 kati ya vyombo vya uvuvi 58,231, vyombo 8,191 vilikuwa vikitumia mashine za kisasa, idadi hii imeendelea kuongozeka hadi kufikia 13,593 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 65%.

Kumekuwepo na ongezeko la idadi ya wavuvi, vyombo vya uvuvi na kiasi cha samaki kilichovunwa kuanzia mwaka 1995, ambapo idadi ya wavuvi ilikuwa 75,621, vyombo vya uvuvi 22,976 na kiasi cha tani 255,900.74 za samaki zenye thamani ya TShs. 70,467,575.96 zilivunwa ukilinganisha na idadi ya wavuvi 195,435 waliotumia vyombo 58,231 na kuvuna tani 473,592.24 za samaki zenye thamani ya TShs. 2,367,961,211.36 mwaka 2020. Uvuvi wa kibiashara ni ule ambao hufanyika kwa kuvua Kambamiti kwenye Maji ya Kitaifa pamoja na uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (Exclusive Economic Zone – EEZ). Uvuvi katika EEZ hulenga samaki aina ya Jodari na Jamii ya Jodari (Tuna and Tuna like species) ambao kwa kiasi kikubwa huuzwa masoko ya nje ya nchi.

**a) Uvuvi wa Kambamiti**

Uvuvi wa Kambamiti wa kibiashara wa kutumia meli kubwa za kukokora (trawlers) ulianza mwaka 1988 kwa idadi ya meli 13. Idadi hiyo iliendelea kuongezeka hadi kufikia meli 25 mwaka 2004 na 2005. Pia, kiasi cha Kambamiti waliovuliwa kiliongezeka kutoka tani 650.93 mwaka 1988 hadi kufikia tani 1,026.63 mwaka 1994, tani 1,193.69, mwaka 2001 na tani 1,320.06 mwaka 2003. Kiasi hicho kilianza kupungua na kufikia tani 202.46 mwaka 2007. Mwelekeo huu wa uvunaji uliashiria tishio la kutoweka kwa rasilimali hii, hivyo Serikali ikafanya maamuzi ya kufunga uvuvi huo kuanzia mwaka 2007 hadi 2016. Uvuvi huu ulifunguliwa tena mwaka 2017 baada ya taarifa za kitafiti kuonyesha kuwa kuna ongezeko la rasilimali hii majini.

**b) Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari**

Ndugu Wanahabari, Tanzania iliridhia kuanzisha Ukanda wa Uchumi wa Bahari (Exclusive Economic Zone – EEZ) mwaka 1989. Uvuvi wa kibiashara katika EEZ ulianza mwaka 1998 ambapo leseni tisa (9) za kuvua kwenye eneo hilo zilitolewa upande wa Tanzania Bara. Idadi ya meli zilizopewa leseni ziliendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutoka meli 9 mwaka 1988 hadi meli 44 mwaka 2003 na meli 85 mwaka 2004. Idadi ya meli hizo ilipungua hadi meli 79 mwaka 2005 na kuongezeka tena hadi meli 87 mwaka 2006, meli 66 mwaka 2007 na meli 36 mwaka 2008.

Ndugu Wanahabari, Mwaka 2010 utaratibu wa kutoa leseni za uvuvi kwenye EEZ ulibadilika kutoka kwenye utaratibu wa kila upande wa Jamhuri ya Tanzania (SMT na SMZ) kutoa leseni hizo na kuanza kutolewa na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari Kuu (Deep Sea Fishing Authority – DSFA). Kuundwa kwa Mamlaka (DSFA) kumeimarisha usimamizi endelevu na udhibiti wa rasilimali za uvuvi katika Eneo la EEZ ya Tanzania na kuimarisha mchango wa Sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa kutokana na rasilimali zinazopatikana kwenye Bahari Kuu. Tangu kuanzishwa kwa Mamlaka hadi mwaka 2021/2022, jumla ya meli za uvuvi 502 zimepatiwa leseni zenye thamani ya Shilingi 24,314,736,449/= ambapo jumla ya tani za ujazo 67,437.90 za samaki zilivuliwa katika EEZ ya Tanzania kwa wastani wa tani 6,130.7 kwa mwaka.

**2.2.3 Kuimarisha Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi**

Ndugu Wanahabari, Tanzania ilianza juhudi za kulinda na kudhibiti rasilimali za uvuvi tangu ilipotunga sheria ya kwanza ya uvuvi iliyoitwa 'Fisheries Ordinance and Trout Protection Ordinance CAP 368'. Tangu nchi yetu ipate uhuru, juhudi mbalimbali zimefanyika ili kuwezesha usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi zikiwemo: - kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali, kuanzisha Kanda nne (4) na vituo 35 vya doria na Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Kupambana na Uhalifu wa Mazingira (National Mult- Agency Task Team-NMATT) na kuimarisha usimamizi shirikishi kwa kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) 754 nchi nzima. Uimarishaji wa usimamizi umewezesha kupungua kwa uvuvi haramu katika Maziwa Makuu takribani asilimia 80 na uvuvi wa milipuko katika Bahari ya Hindi kwa zaidi ya 95%.

**2.2.4 Usimamizi wa Ubora, Usalama na Viwango vya Mazao ya Uvuvi**

Ndugu Wanahabari, Upatikanaji wa soko kwa ajili ya samaki na mazao ya uvuvi hutegemea sana kiwango cha ubora na usalama wa mazao hayo. Serikali imeendeleza jitihada za kuthibiti ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi ili kulinda soko la ndani na nje ya nchi. Jitihada hizi ni pamoja na kuanzisha Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi Mwaka 1997.

Ndugu Wanahabari, Vilevile, katika kuimarisha ubora wa mazao ya uvuvi katika mnyororo wa thamani, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwemo ujenzi na ukarabati wa mialo ya kupokelea samaki na masoko. Hadi sasa kuna jumla ya mialo ya kisasa 33 na masoko 17 ikilinganishwa na mwaka 1961 ambapo hapakuwa na mialo iliyoboreshwa na masoko ya kisasa.

Ndugu Wanahabari, Kufuatia juhudi hizo kiasi cha mazao ya uvuvi yanayouzwa nje ya nchi yameendelea kuongezeka kutoka tani 17,269.90 na samaki wa mapambo 4,116 zenye thamani ya shilingi Bilioni 11.93 mwaka 1995 hadi tani 40,477.97 na samaki wa mapambo 128,316 zenye thamani ya shilingi Bilioni 386.37 mwaka 2020. Aidha, mauzo hayo yaliingizia Taifa shilingi milioni 629.57 mwaka 1995 ikilinganishwa na shilingi Bilioni 21.67 mwaka 2020 kama mrahaba.

**2.2.5 Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kwenye Sekta ya Uvuvi**

Ndugu Wanahabari, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi kwa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya kuboresha Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu. Aidha, Wizara imeanzisha Dawati la Sekta Binafsi kwa ajili ya kutoa elimu, kuwaunganisha wadau wa uvuvi na taasisi za kifedha ili kuwawezesha kupata mikopo yenye masharti nafuu. Mazingira hayo yamehamasisha wawekezaji kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi; ikiwemo uvuvi wa kibiashara, viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na kutengeneza zana za uvuvi.

Kwa jitihada hizo, idadi ya viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi imeongezeka kutoka viwanda 4 vilivyokuwa na uwezo wa kuzalisha tani 3 mwaka 1992 hadi 15 vyenye kuzalisha tani 40 – 60 kwa siku kwa mwaka 2021.

Pia, kuna viwanda vitano (5) vya kutengeneza nyavu vya Nyota Venture na Nyamagara Fish Net (Dar Es Salaam), Fanaka Fish Net, CFN na Ziwani Fish Net (Mwanza) na viwanda vinne (4) vya kuunda boti vya Songoro Marine/Pasiansi Boatyard (Mwanza); Yatch Club (Dar es Salaam); Sam and Anzai Co. Ltd (Dar es Salaam - Kunduchi); na Seahorse Co. Ltd (Dar es Salaam).

**2.2.6 Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi - Kilwa Masoko**

Ndugu Wanahabari, Wizara inaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kupitia Mtaalam Mwelekezi ambaye ni Kampuni ya M/S Sering Ingegneria ya Nchini Italia kwa gharama ya shilingi 1,421,041,703. Serikali tayari imechagua eneo la Kilwa Masoko kwa ajili ya kujenga bandari ya uvuvi. Katika mwaka huu wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi Bilioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bandari hiyo mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu. Aidha, jitahada za kutafuta wawekezaji wa kujenga miundombinu mingine ya uvuvi katika eneo hilo zinaendelea vizuri.

Ndugu Wanahabari, ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika ukanda wa Pwani utawezesha meli zinazovua kutia nanga kwa lengo la kuhaulisha na kuuza samaki, kutoa takwimu sahihi za mazao ya uvuvi, kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuchakata samaki na huduma na huduma nyingine, kuzalisha takriban ajira 30,000 na kuongeza pato kwa jamii.

**2.2.7 Uendelezaji wa Ukuzaji wa Viumbe Maji**

Ndugu Wanahabari, ukuzaji viumbe maji unajumuisha ufugaji wa samaki, kambamiti, chaza, kaa, majongoo bahari na kilimo cha mwani na ulianza mwaka 1927 ambapo samaki aina ya "rainbow trout" walipandikizwa katika mito iliyopo nyanda za juu za Kusini (Mbeya) na Kaskazini Kilimanjaro) kwa ajili ya uvuvi wa burudani (Sport fishing). Mnamo miaka ya 1950, Serikali ya kikoloni ilianzisha majaribio ya ufugaji wa samaki aina ya Sato katika mikoa ya Mwanza (Malya) na Tanga (Korogwe) kwa dhumuni la kuzalisha vifaranga wa kupandikizwa katika malambo. Baada ya uhuru kufikia mwaka 1963 kulikuwa na mabwawa ya kufugia samaki takriban 10,000. Mwanzoni mwa 1980, Serikali kwa kushirikiana na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya FAO na UNDP ilianza ujenzi wa kituo cha ufugaji samaki cha Kingolwira katika mkoa wa Morogoro kwa lengo la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kuzalisha vifaranga vya samaki. Mwaka 1992 idadi ya vifaranga 5,000 vilizalishwa katika Kituo cha Kingolwira.

Ndugu Wanahabari, Mwaka 2008 Serikali ilianzisha Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji katika iliyokuwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kuhamasisha, kuendeleza na kusimamia tasnia ya ukuzaji viumbe maji. Moja ya mafanikio muhimu ni kuongezeka kwa idadi vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji (Aquaculture Development Centres) kutoka kimoja (1) cha Kingolwira hadi kufikia vitano (5) vilivyopo sasa (2021) ambavyo ni Kingolwira – Morogoro, Mwamapuli – Tabora, Ruhila – Ruvuma, Nyengedi/Mtama – Lindi na Machui – Tanga. Wizara inaendelea kufanya ukarabati na upanuzi wa vituo hivyo katika mwaka 2021/2022 mashamba darasa 10 yataanzishwa. Idadi ya vifaranga kwenye vituo vya Serikali imeongezeka kutoka 5,000 mwaka 1992 hadi 3,191,160 mwaka 2021/2022 wakati idadi ya vitotoleshi kwa sekta binafsi na umma vimefikia 28 vyenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya vifaranga 25,000,000. Pia kuna jumla ya viwanda 11 vya chakula cha samaki ambavyo vina uwezo wa kuzalisha tani 1,000.

Ndugu Wanahabari, Idadi ya vizimba katika maziwa makuu na malambo imeongezeka kutoka 50 mwaka 2014/2015 hadi 473 mwaka 2020/2021. Kuwepo kwa mifumo ya ukuzaji viumbe maji inayorejeleza maji (Recirculation Aquaculture System na In-Pond Raceways) imepelekea kuongezeka kwa uzalishaji kwani idadi ya mabwawa imeongezeka kutoka 8,611 mwaka 1992/1993 hadi kufikia 30,034 mwaka 2020/2021. Idadi ya wakuzaji viumbe maji imefikia 30,064 na uzalishaji wa mazao ya viumbe maji umeongezeka kutoka tani 1,350 mwaka 1992/1993 hadi kufikia tani 22,793.2 mwaka 2020/2021 zinazojumuisha tani 20,258 za samaki, tani 2,438 za mwani, tani 97 za kambamiti, kilo 115 za majongoo bahari na vipande 360 vya lulu. Uwekezaji wa sekta binafsi katika ufugaji samaki kibiashara umeongezeka kufuatia uwekezaji wa shilingi bilioni 11 uliofanywa na Kampuni za TanGreen (Bilioni 6.4) – Magu na Tanlapia (Bilioni 4.6) – Bagamoyo ambazo zinatarajia kuzalisha zaidi ya tani 15,000 za samaki aina ya Sato.

### 2.2.8 Kuanzishwa kwa Taasisi Zilizopo chini ya Sekta ya Uvuvi

#### 2.2.8.1 Taasisi ya Kusimamia Mafunzo Ya Uvuvi

Ndugu Wanahabari, baada ya nchi yetu kupata uhuru, mwaka 1966, Serikali ilianzisha Chuo cha Uvuvi Mbegani na Chuo cha Uvuvi Nyegezi kwa lengo la kupata Wataalam wa Uvuvi. Vyuo hivyo vilikuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi wachache kwa mwaka na idadi yao ilikuwa wanafunzi 71 mwaka 1966. Kati ya Mwaka 2006 na 2010, Serikali iliamua kuimarisha Vyuo hivyo na ilipofika tarehe 28 Oktoba 2011 Serikali iliunda Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (yaani Fisheries Education and Training Agency - FETA) kupitia Tangazo la Serikali Na. 356. Baada ya kuundwa kwa Wakala, huduma zimeimarika ambapo kwa sasa FETA ina Kampasi tano (5) za Mbegani-Makao Makuu, (Bagamoyo), Nyegezi (Mwanza), Kibirizi (Kigoma), Mikindani (Mtwara) na Gabimori (Mara). Kampasi hizo za FETA zina uwezo wa kudahili wanafunzi wa fani mbalimbali wapatao 1,409 mwaka 2021. Mafunzo yanayotolewa ni katika ngazi ya Astashahada na Stashahada na mafunzo ya muda mfupi. Idadi ya Wahitimu wa mafunzo ya uvuvi tangu kuanzishwa kwa Vyuo vya uvuvi hadi sasa imefikia 7,472.

#### 2.2.8.2 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)

Ndugu Wanahabari, Shughuli za Utafiti katika uvuvi mara baada ya Uhuru mwaka 1961 zilikuwa zikifanywa na iliyokuwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Afrika Mashariki (East African Fisheries Research Organization-EAFRO) iliyoundwa mwaka 1967. EAFRO ilikuwa ni miongoni mwa Taasisi zilizokuwa chini ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ikiwa na jukumu la kuendeleza na kuratibu utafiti wa uvuvi.

Ndugu Wanahabari, baada ya kuvunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) iliundwa chini ya Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na. 11 ya Mwaka 1980. TAFIRI imeendelea kuimarishwa na hadi sasa ina Vituo vinne (4) vya kusimamia utafiti wa uvuvi nchini vya Dar es Salaam; Mwanza, Kyela (Mbeya), na Kigoma na kituo kidogo cha Sota (Mara). TAFIRI Kupitia Vituo hvyo, imefanya tafiti mbalimbali ikiwemo kujua wingi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo ya uvuvi hususan Ziwa Victoria. Aidha TAFIRI wamefanya tafiti za vyakula na mbegu bora za samaki na upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvuliwa. Matokeo ya TAFITI hizo yamewezesha kutunga Será, Mipango na Mikakati ya kusimamia Sekta ya Uvuvi Nchini. Baadhi ya matokeo chanya ya tafiti hizo ni kuanzishwa kwa maeneo ya hifadhi, maeneo yanayofaa kwa uvuvi na kutunga Sheria na Kanuni imara za kusimamia uvuvi endelevu.

#### 2.2.8.3 Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu

Ndugu Wanahabari, shughuli za uhifadhi wa mazingira ya baharini nchini Tanzania zilianza miaka ya mwanzo ya uhuru ambapo Sheria ya Uvuvi Na. 6 ya mwaka 1970 ilisimamia shughuli za Uvuvi na uhifadhi wa maeneo ya uvuvi, mwaka 1975 ndipo Maeneo Tengefu nane (8) ambayo ni Mbudya, Bongoyo, Pangavini, Maziwe, Funguyasini, Kinasi, Kitutia na Chole yalianzishwa na kusimamiwa na Idara ya uvuvi. Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kilianzishwa Mwaka 1995 chini ya Sheria ya Hifadhi za baharí na Maeneo Tengefu Na. 29 ya Mwaka 1994 kwa lengo la kuanzisha na kuimarisha maeneo ya uhifadhi katika Sekta ya Uvuvi na utalii ikolojia. Kitengo hicho kimeendelea kuimarishwa ambapo hadi sasa kuna maeneo yaliyohifadhiwa 18 yanayojumuisha Hifadhi za Bahari tatu (3) (Mafia, Mnazi Bay na Tanga Silikanti) na Maeneo Tengefu 15. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha na kusimamia masuala ya uhifadhi, na ulinzi wa maeneo yenye rasilimali za uvuvi katika maji bahari na maji baridi.

Ndugu Wanahabari, pamoja na usimamizi wa hifadhi za bahari na maeneo tengefu, kitengo pia kinafanya shughuli za utalii katika maeneo hayo kutokana na vivutio mbalimbali vilivyopo kama vile matumbawe, nyasi bahari, samaki na wanyama wa baharini kama kasa, nyangumi n.k. Kutokana na vivutio hivyo, MPRU kwa kushirikiana na mwekezaji kampuni ya Thanda Tanzania Limited wamejenga hoteli ya kitalii ya nyota tano iitwayo Thanda Island katika eneo tengefu la kisiwa cha Shungimbili wilayani Mafia. Pamoja na kulipa maduhuli ya Serikali, uwekezaji huu umeleta faida kubwa kwa nchi ikiwemo kuitangaza Tanzania kwa kushinda tuzo ya Africa's Leading Luxury Island kwa mwaka 2021 na kuchaguliwa katika kushindanishwa na nchi nyingine duniani katika tuzo ya World's Leading Exclusive Private Island 2021 katika Tuzo za Safari Duniani za mwaka 2021 (World Travel Awards 2021).

#### 2.2.8.4 Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)

Ndugu Wanahabari, Shirika la Uvuvi Tanzania (Tanzania Fisheries Corporation – TAFICO) lilianzishwa kupitia Amri ya Rais (Presidential Order) ya mwaka 1974 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Na. 17 ya mwaka 1969 na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 58 la tarehe 1 Machi, 1974. Lengo kuu la kuanzishwa kwa TAFICO lilikuwa ni kuendeleza shughuli za uvuvi wa kibiashara nchini. Kufuatia kuanzishwa kwake TAFICO ilianza kuendesha shughuli za uvuvi katika maeneo ya Ukanda wa Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika.

Ndugu Wanahabari, licha ya Shirika kuwa na mali hizo, mwaka 1996 TAFICO iliwekwa kwenye orodha ya mashirika ya umma yaliyotakiwa kubinafsishwa. Hata hivyo, halikuweza kubinafsishwa hadi liliporejeshwa tena Serikalini mwaka 2005. Kwa sasa Serikali inakamilisha taratibu za kulifufua upya Shirika la Uvuvi Tanzania ili liweze kufanya majukumu yake na kuendeleza uvuvi kibiashara kwa kushirikisha sekta Binafsi. Kupitia Shirika hili, Serikali itanunua meli tano (5) za uvuvi wa Bahari Kuu ambapo meli moja (1) itapatikana kupitia Msaada wa Serikali ya Japani na meli nne (4) kupitia Mradi wa IFAD.

Ndugu Wanahabari, kufuliwa kwa TAFICO na ununuzi wa meli utawezesha Taifa kushiriki kikamilifu katika uvunaji wa rasilimali za uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Baharí pamoja na kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za Nchi katika ukanda huo. Aidha, hatua hiyo itawezesha Nchi kuongeza mapato ya ndani ya Serikali na fedha za kigeni.

### 2.2.9 Huduma za Ugani wa Uvuvi

Ndugu Wanahabari, huduma za ugani katika sekta ya uvuvi zilianza kuimarika katika miaka ya 1990s. Katika kipindi hicho, hadi sasa huduma za ugani zilizotolewa ni pamoja na elimu kwa umma ambapo jumla ya vipindi vya redio vipatavyo 1,456 na vipindi vya luninga vipatavyo 50 viliandaliwa na kurushwa hewani. Aidha, vipeperushi 34,000, mabango 14,118, kalenda 18,500 na vijitabu 2,118 vilichapishwa na kusambazwa.

Ndugu Wanahabari, katika kipindi hicho, mafunzo rejea yalitolewa kwa wadau wa uvuvi wapatao 47,279. Aidha, nakala 47,000 za machapisho yaliyohusu ufugaji bora wa samaki, athari za uvuvi haramu, uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi, Vyama vya Ushirika vya wavuvi na wakuzaji viumbe maji na Agenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji ya Mwaka 2020–2025 yalichapishwa na kusambazwa kwa wadau wa uvuvi kwa lengo la kutoa elimu.

Ndugu Wanahabari, Serikali imehamasisha wavuvi na Wakuzaji viumbe maji kujiunga katika vyama vya Ushirika ili kuwajengea uwezo na kuwawezesha kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwenye taasisi za fedha. Hadi kufikia Mwaka 2021 kulikuwa na jumla ya vyama vya ushirika vya wavuvi 147 vinavyotambuliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini. Serikali imeendelea kuhamasisha Taasisi za fedha kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa Vyama vya ushirikia wa wavuvi. Hivi karibuni kuanzia Mwaka 2019/2020 Vyama vitatu (3) vya Bukasiga Fisheries - Ukerewe, Zilagula Fisheries – Buchosa na Kikumba Itale Fishers-Chato vimepata mikopo yenye jumla ya shilingi milioni 520 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB). Aidha, vyama 40 vipo katika hatua mbalimbali za kupata mikopo kutoka Benki ya TADB. Vilevile, Serikali imeviwezesha vikundi 32 kupata injini za boti za kupachika.

**2.2.10 Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa**

Ndugu Wanahabari, Sekta ya Uvuvi imefanikiwa kujiunga na mikataba/makubaliano na Uanachama kwenye Jumuiya mbalimbali za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi hususan katika maji tunayochangia na nchi nyingine.

2.2.11 Changamoto za Sekta ya Uvuvi

Ndugu wanahabari, moja ya changamoto inayoikabili Sekta ya Uvuvi ni kuendelea kuwepo kwa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi. Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya Kukabiliana na changamoto hiyo ikiwemo kufanya yafuatayo:

(i) Kutoa elimu kwa wadau kuhusu athari za uvuvi haramu kwa uendelevu wa rasilimali za uvuvi

(ii) Kuhamasisha usimamizi na ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi

(iii) Kuimarisha Vituo vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi hususan mipakani ili kudhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi.

2.2.12 Matarajio ya Baadaye kwa Sekta ya Uvuvi

Ndugu wanahabari, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) imefanya tathmini ya mahitaji ya samaki nchini ambapo makadirio ni tani 750,000 kwa mwaka ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 496,390, sawa na upungufu wa tani 253,615. Aidha, kiwango cha ulaji wa samaki kwa sasa ni kilo 8.5 kwa mtu kwa mwaka ikilinganishwa na kiwango kinachopendekezwa na Shirika na Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) cha kilo 20.3 kwa mtu kwa mwaka. Juhudi zinazoendelea za kuongeza uzalishaji wa Samaki nchini zitaongeza ulaji wa Samaki kwa watanzania kufikia kilo 10.5 ifikapo mwaka 2026 Aidha, ili kukidhi mahitaji ya samaki nchini na kuongeza kiwango cha ulaji wa samaki, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina matarajio ya baadaye yafuatayo: -

(a) Uvuvi katika Maji ya Asili

Ndugu wanahabari, Katika eneo la Uvuvi kwenye maji asili tunatarajia kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi kutoka tani 473,592 mwaka 2020 hadi tani 600,000 ifikapo Juni 2026 kwa kufanya yafuatayo:

i). Kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga na kukarabati mialo, masoko na kuboresha teknolojia za uhifadhi ili kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kutoka asilimia 30 hadi asilimia 10 baada ya kuvunwa;

ii). Kuhamasisha teknolojia sahihi za uvuvi na matumizi ya zana bora kwa wavuvi wadogo kutoka vyombo 13,593 vinavyotumia injini hadi vyombo 25,000;

iii). Kujenga Bandari ya Uvuvi na kununua meli nne (4) za TAFICO ili kuimarisha uwekezaji katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (EEZ);

iv). Kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi kwa kuimarisha ulinzi na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kutoka asilimia 80 hadi asilimia 95;

v). Kuongeza maeneo ya uhifadhi wa mazalia na makulia ya samaki kutoka asilimia moja (1) hadi asilimia 10 kwenye maji ya bahari na maziwa;

(b) Ukuzaji Viumbe Maji

Ndugu wanahabari, Katika eneo la Ukuzaji Viumbe Maji tunatarajia kuongeza uzalishaji wa mazao ya ukuzaji viumbe maji kutoka tani 22,000 mwaka 2020 hadi tani 50,000 ifikapo Juni 2026 kwa kufanya yafuatayo:

i). Kuimarisha huduma za ugani kwa kuongeza idadi ya vituo vya ukuzaji viumbe maji kutoka tisa (9) vilivyopo sasa hadi vituo 12. Vile vile, kuanzisha shamba darasa katika Halmashauri 184. Kila shamba darasa litakuwa na mabwawa manne (4) yenye ukubwa wa jumla ya mita za mraba 2,400 zitakazotunza samaki 9,600 na kuvuna jumla ya kilo 2,400 za samaki kila baada ya miezi sita (6);

ii). Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika vitotoleshi ili kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki kutoka milioni 24.2 kwa sasa hadi kufikia milioni 90;

iii). Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya uzalishaji wa vyakula vya samaki kutoka tani 710 kwa sasa hadi tani 2,500;

iv). Kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wadau wapatao 10,000 kila mwaka kuhusu matumizi ya mbinu bora na teknolojia sahihi za ukuzaji viumbe maji ili kuongeza tija;

**2.2.13 Hitimisho**

Ndugu wanahabari, Wizara ya Mifugo na Uvuvi itahakikisha kuwa sekta ya mifugo inaendeshwa kibiashara ili kuleta tija kwa Wafugaji na Taifa kwa ujumla. Aidha, itahakikisha kuwa rasilimali za uvuvi zinasimamiwa ipasavyo ili kuwa na uvuvi na ukuzaji viumbe maji endelevu, maendeleo ya viwanda, ukuaji wa kipato cha mtu mmoja mmoja na Pato la Taifa kwa ujumla. Aidha, Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta Binafsi ili kukuza na kuendeleza Sekta za mifugo na uvuvi kwa kasi zaidi, chini ya uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



**MAFANIKIO YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA**

**HISTORIA YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**1. UTANGULIZI**
Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliundwa tarehe 15 Disemba mwaka 1961 baada ya Tanganyika kupata Uhuru. Kuanzishwa kwa Wizara hii kulilenga kuunda chombo ambacho kingesimamia masuala ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao katika mazingira ya Nchi huru. Chombo hiki kimeiwezesha Nchi yetu kuondokana na sera za kikoloni ambazo zilianzishwa kwa ajili ya kulinda maslahi ya wakoloni. Majukumu ya Wizara kwa wakati huo yalitekelezwa kwa kupitia Jeshi la Polisi na Idara ya Magereza. Hata hivyo, hivi sasa majukumu ya Wizara yanatekelezwa na Jeshi la Polisi; Jeshi la Magereza; Idara ya Uhamiaji; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Idara ya Huduma kwa Wakimbizi; Idara za Huduma za Uangalizi; Msajili wa Jumuiya na Sekretarieti ya Kupambana na Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu.

**1.1 JESHI LA POLISI**

**JESHI LA POLISI KABLA YA UHURU**
1.1.1 Jeshi la Polisi wakati wa Utawala wa Kijerumani 1886-1919
Utawala wa Kijerumani haukuanzisha Jeshi rasmi la Polisi badala yake Wajerumani walikuwa wakiwatumia watawala wa Vijiji (Maakida na Majumbe) katika kutekeleza majukumu ya kipolisi. Kwa upande mwingine Askari wa Jeshi na vikundi vingine vya ulinzi (para–military groups) vilitumika kudhibiti upinzani wa ndani pamoja na kulinda mipaka. Mnamo mwaka 1916 Wajerumani walianzisha Jeshi la Polisi la kiraia (Civilian Police Force) baada ya kuelekea kushindwa na majeshi ya Kiingereza katika Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, ili kulinda vitega uchumi, makazi ya Wajerumani na mipaka ya koloni la Tanganyika. Kikosi hiki cha Polisi kilichokuwa na askari 31 chini ya Meja S. T. Davies kutoka Afrika ya Kusini kilitekeleza majukumu ya kipolisi hadi mwaka 1919 Wajerumani waliposhindwa na Waingereza.

1.1.2 Jeshi la Polisi wakati wa utawala wa Waingereza 1919-1961
Waingereza walianzisha taasisi mbalimbali ikiwemo Jeshi la Polisi lilojulikana kama “Tanganyika Police Force and Prisons Service” chini ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Magereza ya mwaka 1919 (The Police Force and Prisons Ordinance Cap.40). Tarehe 25 Agosti 1919 Serikali ya Kiingereza ilianzisha rasmi Jeshi la Polisi kupitia tangazo la gazeti la Serikali Na. 1. Vol. I Na. 21-2583 ambapo Maafisa 31 (NCO) kutoka Afrika Kusini kuwasili Tanganyika wakiwa na silaha aina ya Rifle kufanya kazi za Polisi.

Makao Makuu ya Jeshi la Polisi yalikuwa Lushoto (Wilemstal) Tanga. Major S. T. Davies aliteuliwa kuwa Kamishna wa kwanza wa Jeshi hilo na baadaye nafasi yake ilichukuliwa na P. F. Brownie Esq aliyehamishwa kutoka Kenya. Tofauti na utawala wa Kijerumani, Jeshi hili lilipewa majukumu ya kipolisi, Magereza, Usalama wa Taifa, kimahakama na ya kiutawala pale ambapo hapakuwa na Maofisa Tawala au Wakuu wa Wilaya.

Mwaka 1920 Kikundi cha Wakaguzi kutoka Ulaya kilifika na kuanzisha kituo cha Mafunzo Morogoro. Aidha, mwaka 1925 kilifunguliwa Kituo cha Kwanza cha Polisi Lupa Tingatinga Mbeya kwenye machimbo ya dhahabu Chunya. Mwaka 1930 Makao Makuu ya Jeshi yalihamishwa kutoka Tanga - Lushoto kwenda Dar es Salaam na Chuo cha Polisi Morogoro kilihamishiwa Moshi. Mwaka 1958 kwa mara ya kwanza wanawake waliajiriwa ndani ya Jeshi la Polisi. Lengo kubwa la Jeshi hili kipindi cha ukoloni lilikuwa ni kulinda maslahi ya mkoloni kwa kumkandamiza mtanganyika.

Ingawa Jeshi la Polisi lilijitenga na shughuli za kijeshi bado lilikuwa na jukumu la kulinda maslahi ya wakoloni wa Kiingereza. Hali hii ilijionesha kwenye muundo wa Jeshi la Polisi ambapo nafasi za juu zilishikwa na wazungu, nafasi za kati zilishikwa na Waasia na vyeo vya chini vilibaki kwa wazawa. Katika mwaka 1922 kulikuwa na Wazungu 68 wenye vyeo kuanzia Wakaguzi hadi Makamishna, Wakaguzi 25 wenye asili ya Asia na Waafrika 748 wa vyeo vya chini. Pamoja na kuongezeka kwa idadi ya Waafrika ndani ya Jeshi la Polisi, hali ya kubaguliwa iliendelea. Kwa mfano, mwaka 1930 Jeshi la Polisi lilikuwa na Wazungu 78 kwenye nafasi za juu, Waasia 67 kwenye vyeo vya kati na Waafrika 1719 kwenye nafasi za chini. Mbali na kushika nafasi za chini katika Jeshi la Polisi, Waafrika pia walibaguliwa kwa taratibu za kiutawala, makazi na stahili.

Wakati wa Utawala wa Kiingereza shughuli za kipolisi zilifanywa kwenye maeneo ya miji na vijiji vilivyokuwa na idadi kubwa ya walowezi wa kizungu. Katika maeneo haya vituo vya polisi vya muda (Detached Police Stations) vilianzishwa kwa ajili ya kulinda mashamba ya walowezi. Katika kipindi cha Vita Kuu ya Pili ya Dunia (1939-1945) utawala wa Kiingereza ulipanua wigo wa ajira ndani ya Jeshi la Polisi na kuongeza idadi ya Maofisa wa Kiafrika katika nafasi za kati na za juu. Mpaka kufikia mwaka 1960, kulikuwa na Waafrika 28 kwenye ngazi za juu za Jeshi la Polisi.

Kwa upande wa Zanzibar, Jeshi la Polisi lilianzishwa mwaka 1873 kwa ajili ya kusimamia Sheria za kupinga biashara ya utumwa. Jeshi hili lilijumuisha askari wa Kiingereza na wa Sultani wa Zanzibar. Mwaka 1877 Serikali ya Kiingereza ilimteua Kamanda wa Kikosi cha Maji, Lloyd Mathews, kuongoza askari 1300 wakiwemo Waafrika 300. Mwaka 1907 wakati Zanzibar ikiwa chini ya uangalizi wa Waingereza (Protectorate), Sultani alilivunja Jeshi la Polisi baada ya askari wake kugoma kutokana na mishahara midogo na mazingira duni ya kazi na kuunda Jeshi la Polisi lililojumuisha askari wa akiba kutoka Tanganyika.

1.1.3 Jeshi la Polisi kuanzia mwaka 1961
Baada ya Tanganyika kupata uhuru tarehe 9 Desemba 1961 jukumu la Jeshi la Polisi lilibadilika kutoka kusimamia maslahi ya kikoloni na kuwa Jeshi la Kusimamia utekelezaji wa Sheria ndani ya Tanganyika huru. Kimsingi muundo na majukumu ya Jeshi la Polisi yalibaki kama yalivyo. Mabadiliko makubwa yaliyojitokeza wakati huo ni kuongezeka kwa Maofisa wa Kiafrika wenye vyeo vya juu ili kuchukua nafsi zilizokuwa zikishikiliwa na Wazungu. Hii ilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya kuwapatia nafasi Waafrika katika Serikali (Africanization Policy). Mwaka 1962 Elangwa Shaidi aliteuliwa kuwa Mwafrika wa kwanza kushika nafasi ya juu kabisa katika Jeshi la Polisi, ya Kamishna wa Polisi akichukua nafasi ya Kamishna wa Polisi aliyekuwa Mzungu Kamishna wa Polisi (CP) M.S Wilson. Mwaka huo 1962 Maafisa 10 wa kiafrika waliteuliwa kuchukua nafasi za Wakuu wa

Polisi wa Mikoa (Regional Police Commanders) kwa lengo la kuhakikisha mikoa hiyo inakuwa katika hali ya usalama.

Tarehe 26/04/1964 Tanganyika na Zanzibar zilipo ungana na hivyo kuunda Tanzania, Elangwa Shaidi alipandishwa cheo na kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi (IJP) nchini Tanzania ambaye alikaa katika nafasi hiyo kwa miaka saba kuanzia Mwaka 1964 hadi 1970. Alisaidiwa na Makamishna watatu wa Polisi ambao ni: - Edington Kisasi Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamza Azizi Kamishna wa Polisi Bara na Akena Kamishna wa Polisi CID.

1.1.4 Jeshi la Polisi mwaka 1964
Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, majukumu na muundo wa Jeshi la Polisi yalibadilika hasa baada ya masuala ya ulinzi na usalama kuwa ya Muungano. Sheria za Jeshi la Polisi la Zanzibar zilifutwa na iliyokuwa Sheria ya Polisi ya Tanganyika ilianza kutumika Tanzania Bara na Zanzibar. Jeshi la Polisi lilianzisha nafasi ya Inspekta Jenerali wa Polisi na Elangwa N. Shaidi aliteuliwa kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi wa kwanza. Katika kipindi hiki utendaji wa Jeshi la Polisi ulikwenda sambamba na mabadiliko ya Sera za kisiasa. Kwa mfano, ilikuwa ni lazima kwa mtu anayetaka kuajiriwa ndani ya Jeshi la Polisi kuwa na kadi ya Chama cha TANU au ASP. Jeshi la Polisi liliendelea kuwa sehemu ya Chama Tawala hadi Julai Mosi, 1992 baada ya kuanzishwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa.

Jeshi la Polisi limeundwa kisheria na kupewa jukumu la kusimamia usalama wa raia na mali zao pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sheria za Nchi. Majukumu ya Polisi yametajwa katika Kifungu cha 5 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Cap.322 (R.E. 2002). Majukumu haya ni kuzuia na kupambana na uhalifu, kuwakamata wahalifu, kupeleleza makosa ya jinai, kuhakikisha Sheria za Nchi zinafuatwa na kudumisha amani ya Nchi.

1.1.5 Mabadiliko na Mafanikio ya Jeshi la Polisi katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru
Jeshi la Polisi limepita mabadiliko mbalimbali kwani baada ya Serikali ya Awamu ya Nne kuingia Madarakani, Jeshi la Polisi liliondolewa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuundiwa Wizara mpya ya Usalama wa Raia, ambayo ilipewa jukumu pekee la kutekeleza shughuli za Usalama wa Raia na Mali zao. Hata hivyo, tarehe 12 Februari 2008, Serikali ilifanya tena mabadiliko ambapo Wizara ya Usalama wa Raia iliunganishwa tena na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuitwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Jeshi la Polisi limefanikwa kufanya mapitio na mabadiliko ya muundo wa utawala wa Jeshi la Polisi mara mbili. Mabadiliko ya kwanza yalikuwa mwaka 2013 ambapo muundo wa Jeshi la Polisi ulibadilishwa na kuwa na Kamisheni 8 na pia uwepo wa Kamishna wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam badala ya Kamisheni 4 zilizokuwepo mwaka 2010/11. Kamisheni hizi ziliongozwa na maafisa wa cheo cha Kamishna wa Polisi. Aidha, muundo huo ulitambua uwepo wa cheo cha Naibu Inspekta Jenerali.

Mabadiliko ya mara ya pili yalifanyika Julai, 2018 ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliridhia Muundo wa Jeshi la Polisi kwa kuondoa nafasi ya Naibu Inspekta Jenerali na Kamishna wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam na kuendelea kukubali uwepo wa Kamisheni 8 ambazo ni Kamisheni ya Utawala na Menejimenti ya Rasilimali watu, Kamisheni ya Operesheni na Mafunzo, Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Kamisheni ya Intelijensia ya Jinai, Kamisheni ya Ushirikishwaji wa Jamii, Kamisheni ya Fedha na Lojistiki, Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi na Kamisheni ya Polisi Zanzibar.

Kutoka mwaka 1964 hadi sasa Jeshi la Polisi limeshaongozwa na Wakuu wa Polisi 9 na wa sasa ni wa 10. Aidha Jeshi la Polisi limepanuka kutoka Makamishna watatu hadi wanane kutokana na kuongezeka kwa watu, shughuli za kiuchumi, kijamii na ukuaji wa sayansi na teknolojia.

Jeshi la Polisi hadi sasa lina Makamanda wa Polisi wa Mikoa 35 na Makamanda 17 wa Vikosi ukilinganisha na Makamanda 10 waliokuwepo baada ya kupata uhuru.

Kwa kipindi hicho kuanzia Nchi yetu ilipopata Uhuru hadi sasa, Jeshi la Polisi limefanikiwa kufanya maboresho mbalimbali ili kuongeza usasa, weledi na ushirikishwaji wa jamii. Jambo ambalo limeendelea kusaidia kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu nchini kwa ufanisi mkubwa.

Jeshi la Polisi limefanikiwa kuajiri askari wa vyeo mbalimbali wakiwa na elimu ya kuanzia kidato cha Nne, cha Sita, Astashahada, Stashahada, Shahada, Shahada ya Uzamivu na Uzamili ambao wamebobea katika fani mbalimbali ukilinganisha na walioajiriwa baada ya kupata uhuru.

Aidha, kumewepo na maboresho ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya maafisa na askari wa vyeo mbalimbali kutoka za bati kuwa za kisasa.

Jeshi la Polisi limefanikiwa kujenga vituo vya Polisi daraja 'A' – 112, 'B' – 93, 'C' – 166, Ofisi za Makamanda wa Polisi 20, za Wakuu wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia 24 na Zahanati 35 za Jeshi la Polisi ambazo askari wa Jeshi la Polisi, familia zao na raia wa kawaida hupata huduma za matibabu.

Jeshi la Polisi limefanikiwa kuanzisha madawati ya Jinsia na Watoto 420 Nchi nzima, ambayo yamekuwa nyenzo kubwa ya kubaini, kuzuia na kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto.

Kutokana na maboresho yanayoendelea katika Jeshi la Polisi hadi sasa Mikoa yote ya kipolisi 33 imeunganishwa katika Mkongo wa Taifa ambao umekuza matumizi ya tehama ndani ya Jeshi.

Jeshi la Polisi katika kuimarisha usawa wa kijinsia limendelea kupandisha vyeo maafisa na askari wa kike kufikia hadi ngazi ya Kamishna wa Polisi, mfano, Kamishna wa Polisi Mstaafu Elice Mapunda na wengine kufikia cheo cha Naibu Kamishna. Pia wapo wanaongoza Vitengo mbalimbali vya Makao Makuu ya Polisi na wengine kuwa Makamanda wa Polisi wa Mikoa na

Vikosi.

Katika kuondokana na mfumo uliorithiwa kutoka kwa wakoloni Jeshi la Polisi katika Maboresho yake limeanzisha programu ya Polisi Jamii ambayo ndani yake kuna miradi takribani 25 inayotekelezwa Tanzania nzima ikiwepo Uwa jamii, Ulinzi Shirikishi, Polisi Kata  na Usalama Wetu Kwanza, ambayo imewafanya wananchi kuwa na imani na Jeshi la Polisi na kuwa karibu nalo pamoja na wao wenyewe kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu na kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi katika mitaa.

Jeshi la Polisi Tanzania limekuwa na ushirikiano na majeshi ya Polisi ya Nchi jirani na Nchi zingine na kujiunga katika Mashirikisho ya Wakuu wa Polisi ya Kikanda na Kimataifa kama vile EAPCCO, SARPCCO, CAPCCO na INTERPOL. Hii imewezesha Jeshi la Polisi Tanzania kupata fursa za mafunzo kwa askari wake, kubadilishana taarifa mbalimbali za uhalifu na wahalifu na kufanya operesheni za pamoja za makosa yanayovuka mipaka kwa ufanisi mzuri.

Baada ya Maboresho mbalimbali kwenye maabara yetu ya Polisi na kuifanya kuwa maabara ya kisasa ya Uchunguzi wa Kisayansi wa Jinai ambayo kwa sasa inaongozwa na Kamishna wa Polisi katika uchunguzi wa Silaha na Milipuko, kwa kipindi cha mwaka 1961 hadi 2004 jumla ya kesi 2,352 zilichunguzwa wakati ikiitwa Idara ya Utambulisho ikilinganishwa na kesi 2,085 zilizochunguzwa kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2021.

Uchunguzi wa Alama za Vidole, kwa kipindi cha mwaka 1961 hadi 2004 jumla ya alama za Vidole za watu 597,506 zilichunguzwa ikilinganishwa na alama za Vidole 1,818,150 zilichunguzwa kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2021.

Jumla ya Hati za Tabia Njema 1,089,448 zilitolewa kwa kipindi cha mwaka 1961 hadi 2004 ikilinganishwa na hati za tabia njema 380,040 zilizotolewa kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2021.

Wahalifu waliotambuliwa kuwa na makosa ya nyuma, kwa kipindi cha mwaka 1961 hadi 2004 ni 73,982 ikilinganishwa na 3,682 kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2021.

Uchunguzi wa hati zinazobishaniwa, kwa kipindi cha mwaka 1961 hadi 2004 jumla ya kesi 12,255 zilichunguzwa ikilinganishwa na kesi 5,067 zilizochunguzwa kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2021.

Mwaka 2005 Jeshi la Polisi lilifanikiwa kuanzisha maabara ya uchunguzi wa makosa ya kimtandao ambapo hadi sasa imefanikiwa kuchunguza jumla ya kesi 6,616 zilizohitaji uchunguzi wa aina hiyo.
Jeshi la Polisi limefanikiwa kuongeza wigo wa kutoa huduma kutoka ngazi ya Makao Makuu ya Polisi hadi ngazi ya Mikoa na Wilaya (Regional Forensic Bureau office na District Forensic Bureau office) na kuanzishwa Kanda tano (5) za uchunguzi wa hati zinazobishaniwa na Kanda mbili (2) za uchunguzi wa makosa ya kimtandao Dodoma na Zanzibar.

Jeshi la Polisi baada ya kuwajengea uwezo wa kimafunzo limewezesha Maafisa na Askari 736 kwenda kwenye operesheni za ulinzi wa Amani katika Nchi mbalimbali, ambapo wanaume ni 566 na wanawake 170. Kwa sasa waliopo kwenye operesheni kama hizo wanaume ni 22 na wanawake ni 21.

1.2 JESHI LA MAGEREZA
1.2.1 Jeshi la Magereza wakati wa ukoloni
Jeshi la Magereza lilianzishwa rasmi tarehe 25/8/1931 baada ya mgawanyiko wa Majeshi ya Polisi na Magereza.  Kabla ya mwaka 1931 Jeshi la Polisi lilifanya pia kazi za Magereza kufuatana na madhumuni ya wakoloni. Wakati Jeshi la Magereza lilipoanzishwa liliitwa Idara ya Jela ambapo shughuli zake kubwa zilihusu kuwadhibiti wafungwa pamoja na kuwafanyisha kazi ngumu.

1.2.2 Jeshi la Magereza Baada ya Uhuru
Mara baada ya Uhuru mwaka 1961, Serikali ilibadili sura na mwelekeo wa Magereza nchini kwa kuanzisha rasmi Sera ya Urekebishaji wa Wahalifu (Rehabilitation of Prisoners) ambayo iliwekwa wazi na Sheria Mpya ya Magereza ya Mwaka 1967 (Prisons Act, 1967).  Sheria hii iliweka viwango vya Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu na Utunzaji wa Wafungwa. Falsafa ya urekebishaji ilianza kutekelezwa mwaka 1963 kwa uteuzi wa Kamishna wa Magereza, Mtanzania wa kwanza marehemu Obadia Rugimbana. Sheria Kuu ya Magereza Na. 34 ya mwaka 1967 na Kanuni zake za mwaka 1968 na 1969 zilianza kutumika katika uendeshaji wa Magereza chini ya uongozi wa Kamishna wa Magereza Bw. Ramadhani Nyamka ambaye aliongoza mwaka 1967 hadi 1977.

Kati ya mwaka 1964 na 1974 Mikoa iliongezwa kutoka majimbo 8 yaliyokuwepo kabla ya Uhuru hadi Mikoa 20. Wakuu wa Magereza makubwa nane katika majimbo waliongezewa madaraka ya kuongoza Magereza katika zaidi ya Mkoa mmoja. Wakuu hao walijulikana kama Mrakibu Msaidizi wa Mkoa, Mrakibu au Mrakibu Mwandamizi kufuatana na cheo cha Afisa husika. Mgawanyo wa Mikoa hiyo ulikuwa:-

| | | |
|---|---|---|
| Mashariki | - | Pwani na Morogoro |
| Magharibi | - | Tabora na Kigoma |
| Ziwa | - | Mwanza, Kagera, Mara na Shinyanga |
| Kati | - | Dodoma na Singida |
| Kaskazini | - | Kilimanjaro na Arusha |
| Kusini | - | Mtwara, Ruvuma na Lindi |
| Nyanda za Juu | - | Iringa na Mbeya |
| Tanga | - | Tanga |

Mwaka 1974 Jeshi lilianza kuongozwa na Kamishna Mkuu wa Magereza badala ya Kamishna wa Magereza. Kamishna Mkuu wa Kwanza alikuwa Ramadhani Nyamka. Wakuu wa Magereza wa Mikoa waliteuliwa kusimamia uendeshaji wa Magereza katika kila Mkoa. Maafisa hao walipewa Cheo cha Kamishna Msaidizi wa Magereza. Ofisi ya Makao Makuu ya Magereza ilipanuliwa ili kujumuisha Sehemu Kuu Nne ambazo ni Utawala, Ujenzi, Kilimo na Mifugo na Viwanda. Baadaye Sehemu Kuu mbili zaidi ziliongezwa. Sehemu

hizo ni Sheria na Urekebishaji na Ustawi wa wafungwa.

Kabla ya mwaka 1983, idadi ya Maafisa na Askari wa Magereza ilikuwa watumishi 5,000 ambao hawakukidhi mahitaji. Hivi sasa Jeshi lina Watumishi 13,000. Mwaka 1990 Wizara ya Mambo ya Ndani ilianzisha Tume ya Polisi na Magereza chini ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Tume ya Huduma za Magereza Na. 8 ya mwaka 1990 (The Police Force and Prisons Service Commission Act, No.8 of 1990) kwa ajili ya kushughulikia malalamiko ya askari. Jeshi pia lilitunga Kanuni za Utumishi wa Magereza mwaka 1997 (Prisons Service Regulations, 1997) ili kuimarisha maslahi ya kazi ambayo awali yalisimamiwa na Sheria ya Utumishi wa Umma, 1962 (Civil Service Act, 1962) na Kanuni za Huduma za Magereza (Prisons Service - Civil Service – Regulations) za mwaka 1969.1.2.3 Muundo na Majukumu ya Jeshi la Magereza Mwaka 1992 Muundo wa Jeshi la Magereza ulibadilika kwa kuunda Divisheni tatu za kiutawala hivyo Jeshi likawa na Makamishna Watatu kutoka Kamishna mmoja aliyekuwepo tangu mwaka 1974. Wakuu wa Sehemu katika Muundo huu walikuwa Makamishna Wasaidizi wa Magereza hadi mwaka 1999 kilipoanzishwa rasmi cheo cha Naibu Kamishna wa Magereza ambaye hadi sasa ndiye anapaswa kuwa Mkuu wa Kitengo au Sehemu. Muundo huo ulidumu hadi mwaka 2020 ilipogawanywa Divisheni Utawala na Fedha na kuunda Divisheni mbili, moja ya Utawala na Rasilimaliwatu na nyingine ya Fedha na Mipango, na kufanya Jeshi kuwa na Makamishna wanne na Manaibu Kamishna 17 ambao wanakuwa Wakuu wa Sehemu na Vitengo 17 vya Makao Makuu.

1.2.3.1 Uongozi katika Ngazi ya Mikoa
Katika Mikoa kuna Wakuu wa Magereza wa Mikoa na chini yao Wakuu wa Magereza Makubwa ya Ngome (Central Prisons), Magereza ya Wazi ya Kilimo (Open Farm Prisons), Magereza ya Wilaya (District Prisons) na Kambi za Magereza (Prison Camps). Magereza ya Ngome yapo 12 na huweka wafungwa wa aina zote. Magereza Makubwa ya Wazi yapo 46 na yanahifadhi wafungwa wanaotumikia kifungo kisichozidi miaka 10. Magereza ya Wilaya yapo 69. Magereza haya yanahifadhi mahabusu na wafungwa wa miaka isiyozidi 10. Makambi ya Magereza huanzishwa kwa kazi maalum na huweka wafungwa wa miezi isiyozidi 12. Kwa sasa Tanzania ina makambi 40.

Hivi sasa kuna gereza moja tu la Wanawake. Gereza hilo ni gereza la Kingolwira (Morogoro). Wafungwa wa kike pia wanahifadhiwa kwenye sehemu za wanawake kwenye Magereza ya Ngome na Magereza ya Wilaya nchini kote. Aidha, kuna Gereza Maalum la Vijana Wami, Morogoro kwa ajili ya wafungwa wa umri chini ya miaka 21 na Gereza la Wahalifu wenye matatizo ya akili Isanga (Dodoma) (Therapeutic Institution for Criminal Lunatics).

Jeshi la Magereza lina vyuo vinne. Vyuo hivi ni Chuo cha Maafisa wa Magereza Ukonga, Chuo cha Mafunzo ya Awali Kiwira, Chuo cha Ufundi Stadi Ruanda, na Chuo cha Ufundi Magari na Udereva Kingolwira.

Kabla ya Uhuru Ofisi za Magereza za Mikoa hazikuwepo katika muundo wa Jeshi la Magereza, Ofisi hizi zilianzishwa mwaka 1974 na hadi sasa kila Mkoa una Ofisi ya Magereza ya Mkoa japokuwa Mikoa mingine haina majengo stahiki ya Ofisi hizi.

1.2.3.2 Magereza yaliyopo
Wakati tunapata Uhuru mwaka 1961 kulikuwa na magereza 85 yaliyojengwa katika miji mikuu na Makao Makuu ya wilaya. Baada ya Uhuru yalijengwa magereza mengine 44 mengi ya hayo ni magereza ya kilimo na Gereza Segerea. Aidha, zilianzishwa Kambi maalum 40 kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali. Kambi hizi ambazo ni aina ya vigereza vidogo zilianzishwa katika maeneo yenye shughuli za uzalishaji mali ambayo yako mbali na gereza. Mfano wa Kambi hizo ni Kambi Mvuti na Kimbiji za Dar es Salaam, Kambi Mkoka ya kongwa na Dodoma.

1.2.3.3 Rasilimali watu
Wakati tunapata Uhuru Jeshi la Magereza lilikuwa na jumla ya maafisa na askari 2479, kati ya hao maafisa walikuwa 55 askari walikuwa 2424, wengi wa askari hawa walikuwa na elimu ya msingi au hawakuwa na elimu kabisa. Kwa sasa Jeshi la Magereza lina jumla ya watumishi 12,470, kati ya hao 1,815 ni maafisa, 10,567 ni askari na watumishi raia ni 88. Tofauti na wakati wa Uhuru kwa sasa Jeshi lina wasomi katika fani mbalimbali kuanzia astashahada hadi shahada ya uzamivu ambao wanaweza kufanya kazi zote za kitaalamu za Jeshi bila kuhitaji msaada wa taasisi nyingine.

Aidha, mafunzo ya kijeshi yameboreshwa zaidi kwa kufundishwa mambo ya msingi ya kufanyia kazi badala ya kuteswa na kufanyishwa vitu vigumu kwa lengo la kuwatesa bila kuwa na lengo la kumjenga askari katika maeneo Fulani ya kiutendaji.

1.2.3.4 Uzalishaji mali
Katika eneo la uzalishaji mali Jeshi la Magereza limepiga hatua kwa kuanzisha Miradi mbalimbali ya kilimo na Viwanda. Viwanda vilivyopo ni Viwanda vine (04) vya kutengeneza Samani, Kiwanda cha maziwa, Kiwanda cha ushonaji, Kiwanda cha sabuni, Viwanda vya Chumvi vitatu (03), Kiwanda cha kutengeneza bidhaa za ngozi vikiwemo viatu vya kijeshi na viwanda vingine vidogo vidogo.Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na PSSSF limeingia ubia uliounda kampuni hodhi ya Mkulazi kwa ajili ya kujenga Kiwanda cha Sukari katika Gereza Mbigiri.

1.2.3.5 Kilimo
Jeshi la Magereza limeimarisha shughuli za kilimo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Gereza Idete, ujenzi wa mradi huu uko katika hatua za mwisho za kukamilisha ambapo kukamilika kwake kutaimarisha uzalishaji wa mpunga katika shamba hilo. Ujenzi wa mradi huu umefikia asilimia 67 na maji yameshafika shambani, kazi iliyobaki ni kusambaza maji shambani.

Jeshi pia limeendelea kununua matrekta na mitambo mbalimbali ya kilimo zikiwemo mashine za kuvunia mazao (combine harvesters). Kwa sasa Jeshi linamiliki matrekta 99, kati ya hayo matrekta 41 mazima na yanafanya kazi na matrekta 58 ni mabovu. Matrekta haya yanasaidia katika

uzalishaji mashambani badala ya kutegemea nguvukazi ya wafungwa.

1.2.3.6 Kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa
Katika jitihada za kujitosheleza kwa chakula, Jeshi la Magereza limeanzisha miradi mbalimbali ya kusaidia kuongeza mapato katika magereza, miradi iliyoanzishwa ni pamoja na ufyatuaji wa matofali ya kuuza, ujenzi wa majengo ya biashara ya kupangisha (fremu). Zaidi ya mashine 30 za kufyatua matofali zimenunuliwa na kusambazwa vituoni kwa ajili ya miradi ya matofali.

Kwa upande wa majengo ya biashara maeneo yaliyoendelezwa kwa kiasi kikubwa ni Kituo cha biashara cha Isanga, Dodoma (Isanga Business Center) na maduka ya Ukonga Magereza. Katika vituo vingine kazi kama hiyo imefanyika ila kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na hayo ya Isanga na Ukonga.

1.2.3.7 Ushiriki wa masuala ya Kimataifa
Jeshi la Magereza ni mwanachama wa Jumuia mbalimbali za Kimataifa kama vile SADC, ACSA na mengineyo. Ushirikiano huu wa Kimataifa unaliongezea Jeshili hili ujuzi katika shughuli za ulinzi na usalama.

Jeshi la Magereza limekuwa linashiriki katika ulinzi wa Amani katika Nchi mbalimbali ambazo zina migogoro ya kisiasa. Nchi ambazo Maafisa wa Magereza wanashiriki ulinzi wa Amani ni Kongo Kinshasa, Sudan Kusini, Darfur na Liberia.Kwa upande mwingine Jeshi la Magereza linashirikiana na Jeshi la Magereza Shelisheli ambapo jumla ya maafisa na askari 17 walikwenda Shelisheli kufanya kazi za kimagereza katika magereza ya Shelisheli.

1.3 JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI
1.3.1 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kabla ya Uhuru
Huduma ya Zimamoto na Uokoaji Tanzania Bara ilianza baada ya vita vya pili vya Dunia mwaka 1939 hadi 1945. Kwa upande wa Zanzibar shughuli hizi zilianza mwaka 1930. Hapo awali Kikosi hicho kiliitwa Brigedi ya Polisi ya Zimamoto "Police Fire Brigade". Wakati wa utawala wa Kiingereza Kikosi hiki kilianzishwa kutokana na uelewa wao wa madhara ya moto yaliyokuwa yamewakumba huko kwao. Kituo cha kwanza cha Zimamoto kilikuwa katika eneo zilipo Ofisi za Polisi Usalama Barabarani, Dar es Salaam. Kikosi hiki kilipoanzishwa kilifanya kazi katika mazingira magumu. Kikosi hakikuwa na vifaa vya kukabiliana na majanga ya moto na vya mafunzo. Kwa kuwa kuchanganywa kwa kazi za Polisi na Zimamoto kuliathiri shughuli za Zimamoto, Serikali ya Kikoloni iliamua kutenganisha shughuli hizo mwaka 1950. Huduma za kuzimamoto iligawanywa katika makundi yafuatayo: -

(i) Zimamoto ya Manispaa chini ya usimamizi wa Manispaa.

(ii) Zimamoto ya Kiwanja cha Ndege chini ya usimamizi wa Idara ya Kazi.

1.3.2 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji baada ya Uhuru
Baada ya Muungano Serikali iliamua Zimamoto zote nchini ziwe chini ya mwajiri mmoja yaani Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Waraka wa Baraza la Mawaziri Namba 37. Mwaka 1985 Bunge lilipitisha Sheria Na. 3 ya mwaka 1985 ya kuanzisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili huduma ya Zimamoto na Uokoaji zitolewe katika misingi ya nidhamu za Kijeshi. Ili kuboresha shughuli za Zimamoto na Uokoaji Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2007 lilipitisha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji (The Fire and Rescue Force Act, No. 14 ya 2007). Kupitishwa kwa Sheria hii kulisababisha kutungwa kwa Kanuni za Utumishi (Service Regulation) na Kanuni za Ukaguzi za Usalama wa Moto (Fire Safety Inspection Regulations), za mwaka 2008.

1.3.3 Muundo na Majukumu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji
Muundo wa Utumishi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ulirekebishwa na kutolewa kwa mara ya mwisho kwa Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 16 wa Mwaka 1991 Kumb. Na. MU/B/41/038 wa tarehe 11 Desemba, 1991. Muundo huo sasa unahuishwa kwa kuzingatia Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Na.14 ya Mwaka 2007, Kifungu cha 4 na Kanuni ya 3 ya Kanuni zaUtumishi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji za Mwaka 2008.

1.3.3.1 Changamoto za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji
Pamoja na mafanikio yaliyopo Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linakabiliwa na changamoto zifuatazo: -
(i) Upungufu wa rasilimali watu katika vituo mbalimbali vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linahitaji kuwa na rasilimali watu ya kutosha hususan kipindi hiki ambacho Serikali inatekeleza miradi mikubwa na ya kimkakati ikiwemo ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege, ujenzi wa viwanda, miradi ya umeme na gesi, ujenzi wa bomba la mafuta, treni ya umeme na uchimbaji wa madini.
(ii) Uchache wa vituo vya Zimamoto na Uokoaji nchini. Jeshi lina vituo 75 ikilinganishw ana mahitaji halisi ya Vituo 177 nchi nzima.
(iii) Uhaba wa magari ya Kuzima moto na ya maokozi pamoja na magari kwa ajili ya shughuli za utawala na magari ya kubebea wagonjwa (ambulances). Kwa sasa Jeshi lina magari ya kuzima moto 66 ikilinganishwa na mahitaji ya magari 237 na magari ya maokozi yapo saba (7) tu ikiwa mahitaji halisi ni magari 35. Aidha, magari ya utawala yapo 13 ambayo ni chakavu tofauti na mahitaji halisi ya magari 230, magari ya kubebea wagonjwa yapo mawili (2), ikilinganishwa na mahitaji halisi ya magari 159 na pikipiki zilizopo ni 42 wakati mahitaji halisi ni pikipiki 150.Magari ya ngazi (Turntable ladder) yanahitajika 9 yaliyopo ni moja(1).
(iv) Ukosefu wa Fire Hydrants katika maeneo mengi ya mijini na uchakavu wa vyanzo vilivyopo. Katika fire hydrants 2,304 zilizopo nchini, hdrants 1356 ni nzima na hydrants 848 zilizosalia ni mbovu. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kufanya mawasiliano na Mamlaka za Maji katika mikoa mbalimbali nchini ili kufanikisha matengenezo ya fire hdrants hizo. Kimsingi, Jeshi linapaswa kuwa na fire hydrants 285,000 nchini kote ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
(v) Ukosefu wa miundombinu muhimu ya kufundishia katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Handeni,

Tanga.

(vi) Ujenzi holela wa nyumba (Miundombinu) katika maeneo mengi ya mijini na kusababisha kutofikika kwa urahisi wakati wa dharura za kuzima moto na uokoaji

1.3.3.2 Mipango Ya Baadaye ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji
(i) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kuomba vibali vya ajira kila mwaka kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kukabiliana na upungufu wa Maafisa na Askari uliopo.
(ii) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea kuimarisha vitendea kazi ikiwemo magari ya kuzima moto na maokozi pamoja na ununuzi wa vifaa vya kuzimamoto na kufanya maokozi kadri bajeti ya miradi ya maendeleo itakavyokuwa ikitolewa kila mwaka.
(iii) Elimu ya namna ya kujikinga na majanga ya moto itaendelea kutolewa kwa umma kupitia vyombo mbalimbali vya habari kuhusu namna bora ya kuchukua tahadhari dhidi ya majanga ya moto pamoja na majanga mengine.

(iv) Ujenzi wa Vituo vya zimamoto na uokoaji 177 katika maeneo yote yenye uhitaji.
(v) Jeshi litaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa na Askari ili kuwajengea uwezo zaidi katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.
(vi) Jeshi litaendelea kujenga miundo mbinu muhimu ya Chuo kwa ajili ya kufundishia kutoka katika bajeti ya maendeleo.
(vii) Kuendelea kufanya mawasiliano na Mamlaka za maji ili Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liweze kushirikishwa katika hatua za utekelezaji wa miradi ya maji ili Fire hydrants ziweze kufungwa sehemu zote zinapohitajika.
(viii) Kuendelea kuimarisha mahusiano na Nchi wahisani ili tuendelee kupatiwa misaada ya vifaa vya kuzima moto na maokozi.

1.4 IDARA YA UHAMIAJI
1.4.1 Idara ya Uhamiaji Kabla ya Uhuru
Masuala ya udhibiti wa wahamiaji yalianzishwa mnamo mwaka 1924 chini ya Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1924 “Immigration Ordinance Cap 37 of 1924” ili kusimamia Uhamiaji ndani ya Tanganyika. Sheria hiyo ilianza kutumika tarehe 1 Februari, 1925. Kuanzia mwaka 1924 hadi mwaka 1948, shughuli za udhibiti wa wahamiaji na utoaji wa pasipoti zilifanywa na Kitengo maalum ndani ya Idara ya Polisi.

Idara ya Uhamiaji ilianzishwa rasmi Julai 13, 1949 na iliendelea kuwa chini ya Kamishna wa Polisi hadi alipoteuliwa rasmi Afisa Uhamiaji Mkuu (Principal Immigration Officer) mnamo mwezi Oktoba, 1949 ambapo pia Idara ilibadilishwa jina na kuitwa Idara ya Uhamiaji na Pasipoti (Immigration and Passport Department).

Lengo la kuanzishwa kwa Idara ilikuwa ni kuimarisha udhibiti wa wageni hususani wazungu kutoka Mataifa hasimu dhidi ya Uingereza ambao walihitaji kuingia ndani ya Koloni la Tanganyika kutoka mataifa yao au sehemu nyingine za makoloni mengine ndani ya Afrika yasiyo chini ya Himaya ya Muingereza.
Baadhi ya Waafrika waliruhusiwa kutoka sehemu moja hadi nyingine bila udhibiti kutokana na mahitaji ya “manamba” kwenye mashamba ya wakoloni, isipokuwa makabila kama Wakikuyu, Wakamba na Wajaluo kutokana na kushiriki katika vuguvugu la Ukombozi na nia ya kumwondosha Mwingereza.

1.4.2 Majukumu ya Idara ya Uhamiaji Kabla na Baada ya Uhuru;
Jukumu la msingi kabla ya Uhuru wa Tanganyika lilikuwa ni kudhibiti uingiaji na ukaazi wa wageni Pamoja na kuwatambua raia wa Uingereza katika Himaya husika. Majukumu hayo yalitekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiaji ya Mwaka 1924 na Sheria ya Uraia ya Mwaka 1948 (The British Nationality Act of 1948).

Baada ya Tanganyika kupata uhuru mnamo tarehe 9 Disemba 1961, Idara iliendelea kutambulika kama Idara ya Uhamiaji na Pasipoti hata baada ya Sheria kubadilika. Majukumu yaliongezeka ikijumuisha utoaji wa Viza kwa wageni, kufanya misako, doria pamoja na shughuli nyingine za upelelezi. Katika kutekeleza majukumu hayo, Idara iliongozwa na Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1961 (Immigration Ordinance of 1961) iliyofutwa na Sheria Na. 41 ya mwaka 1963 (Immigration Act Na. 41 of 1963), iliyofutwa na Sheria ya Uhamiaji Na. 8 ya mwaka 1972 (The Immigration Act Na. 8 of 1972) ambayo pia ilifutwa na Sheria ya Uhamiaji Na.7 ya Mwaka 1995.

Kwa upande wa masuala ya Uraia, Idara iliongozwa na Sheria ya Uraia Na. 3 ya Mwaka 1961 (The Tanganyika Citizenship Act.of 1961, CAP 512) na Sheria ya Uraia ya Mwaka 1961 (The Tanganyika Ordinance 1961), ambazo zote zilifutwa na Sheria Na. 6 ya mwaka 1995 (The Tanzania Citizenship Act Na. 6 of 1995).

Kufuatia mabadiliko hayo, Idara ya Uhamiaji iliendelea kutekeleza majukumu yake katika sura ya Muungano (Kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar). Na shughuli zilizohusu masuala ya Uhamiaji na Uraia zilibainishwa kuwa ni miongoni mwa masuala kumi na moja yaliyoafikiwa kuwa ni ya Muungano.

Aidha, Sheria zilizosimamia masuala ya Uhamiaji na Uraia ziliendelea kubaki kama ilivyokuwa kabla ya Muungano hadi yalipofanyika mabadiliko na maamuzi ya kuwa na Sheria moja inayosimamia masuala la Uhamiaji na nyingine kuhusu Uraia zilipotungwa mwaka 1995 pamoja na Kanuni zake za mwaka 1997. Sambamba na udhibiti wa wageni kuvuka mipaka, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia ilitunga Sheria Na. 20 ya mwaka 2002 ya Pasipoti na Hati nyingine za Safari na Kanuni zake za mwaka 2004, ili kuwezesha na kusimamia utokaji na uingiaji wa raia wa Tanzania nchini.

Sheria zote za Uhamiaji Na. 7 ya mwaka 1995, Sheria ya Uraia Na. 6 ya mwaka 1995 na ile ya Pasipoti na Hati za Safari Na. 20 ya mwaka 2002 pamoja na Kanuni zake zilitungwa ili kuhakikisha kuwa suala ya ulinzi na usalama wa mipaka ya Nchi yetu linaimarishwa kwa kutoa Huduma zifuatazo:
(i) Kuwezesha na kudhibiti uingiaji, utokaji wa watu na ukaazi

wa wageni nchini,
(ii) Kutoa huduma za Pasipoti na Hati nyingine za Safari kwa raia wa Tanzania wenye sifa,
(iii) Kutoa hati na vibali vya ukaazi kwa raia wa kigeni wanaohitaji kuishi hapa nchini kwa madhumuni mbalimbali,
(iv) Kuratibu mchakato wa maombi ya uraia wa Tanzania kwa wageni waliokidhi vigezo na sifa kwa mujibu wa sheria ya uraia ya Tanzania.

1.4.2.1 Muundo wa Idara ya Uhamiaji
Baada ya Muungano, Idara ya Uhamiaji ilifanywa kuwa miongoni mwa Idara za Muungano, chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mwaka 1995 Serikali ilifanya mabadiliko ya Muundo wa Uongozi wa Idara ya Uhamiaji na kuwa na Mkurugenzi wa Uhamiaji aliyesaidiwa na Wakurugenzi Wasaidizi Watatu; Mkurugenzi Msaidizi aliyesimamia masuala ya Uhamiaji Zanzibar, Mkurugenzi Msaidizi aliyeshughulikia masula ya Huduma na Mkurugenzi Msaidizi aliyeshughulikia masuala ya Sheria.

Aidha, Mwaka 2007 Serikali ilifanya tena mabadiliko ya Kimuundo wa Kiutawala wa Idara ya Uhamiaji na kutolewa kwenye utumishi wa umma na kuwa na Muundo wa kiaskari wenye mtiririko wa vyeo kama ifuatavyo; Kamishna Mkuu, Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Kamishna wa Uhamiaji Utawala na Fedha, Kamishna wa Uhamiaji wa Pasipoti na Uraia, Kamishna wa Uhamiaji Vibali vya ukaazi na Pasi, Kamishna wa Uhamiaji Huduma za Sheria, Kamishna wa Uhamiaji wa Usimamizi na udhibiti wa Mipaka.
Mwaka 2016 Serikali ilifanya tena mabadiliko katika Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 rejeo la mwaka 2016 na kuwa na Muundo wa Kijeshi kama ifuatavyo: Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Kamishna wa Uhamiaji Fedha na Utawala, Kamishna Uhamiaji Zanzibar, Kamishna wa Uhamiaji Uraia na Pasipoti, Kamishna wa Uhamiaji Vibali na Pasi, Kamishna wa Uhamiaji wa Usimamizi na Udhibiti wa Mipaka, Kamishna wa Uhamiaji Huduma za Sheria, Kamishna wa Uhamiaji Mafunzo.

1.5 MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)
Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ni mojawapo ya taasisi za Jamhuri ya Muungano waTanzania, iliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, iliyoanzishwa chini ya Hati ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya mwaka 2008 (Establishment Instrument, 2008) GN 122/2008. Jukumu kuu la Mamlaka ni kusimamia suala la Usajili na Utambuzi wa watu pamoja na utoaji wa Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi, wageni wakaazi pamoja na wakimbizi halali wenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Mamlaka inafanya kazi zake kwa kutekeleza Sheria ya Usajili na Utambuzi wa watu ya Mwaka 1986 na marejeo ya mwaka 2012 [CAP 36 R.E 2012] na Kanuni za Usajili na Utambuzi za Mwaka 2014.

1.6 IDARA YA HUDUMA KWA WAKIMBIZI
Idara ya Wakimbizi ilianzishwa rasmi mwaka 1997. Idara hii ilitungiwa Sheria ya Wakimbizi Na. 9 ya mwaka 1998 kwa madhumuni ya kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu wakimbizi. Kabla ya kuundwa kwa Idara hii shughuli zake zilikuwa zikifanywa na Kitengo chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Mambo ya Ndani ya Nchi.
Wakimbizi walianza kuingia nchini kuanzia miaka ya 1940 kwa vikundi vidogo vidogo na kuishi na wenyeji. Hata hivyo, wimbi kubwa la kwanza la wakimbizi kuingia Tanganyika lilikuja mwaka 1959 kutoka Rwanda. Kundi hili lilikuwa la kabila la Watutsi ambao walikuwa wakikimbia machafuko yaliyotokea Rwanda.

Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili 1964, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Hadhi ya Wakimbizi (The 1951 Geneva Convention on the Status of Refugees). Uamuzi huu ulipelekea kufunguliwa kwa Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) hapa nchini tarehe 12 Mei 1964. Kuanzia mwaka 1961 hadi 1965 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haikuwa na Sheria yoyote ya kuhudumia Wakimbizi bali kulikuwa na miongozo na matamko mbalimbali ambayo yalikuwa yanatolewa na viongozi wa juu wa Serikali ambayo yalisisitiza umoja wa Afrika.

Tanzania ilikuwa ni kitovu na makao makuu ya harakati za ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika. Nchi ya Tanzania ilijiona ina wajibu wa kuwapokea wakimbizi kwa sababu iliamini kuwa uhuru wa Tanzania haukuwa na maana mpaka Afrika yote iwe huru. Ndio maana Tanzania iliwahifadhi wapigania uhuru kutoka Nchi mbalimbali zikiwemo Msumbiji, Afrika Kusini, Zimbabwe, Angola, na Namibia. Kutokana na hali hiyo, Tanzania imehifadhi wakimbizi wengi kutoka Nchi hizo na sehemu zingine kwa nyakati tofauti. Baada ya kupatikana uhuru wa Nchi hizo wakimbizi hao walirejea katika Nchi zao za asili. Tanzania iliendelea kupokea wakimbizi kwa nyakati tofauti. Kutokana na migogoro ya kisiasa.
1.6.1 Hifadhi ya wakimbizi kwenye Makazi 1960 – 1980
Katika kipindi hiki, makundi ya wakimbizi yaliendelea kuingia nchini. Mfano kundi la pili la wakimbizi baada ya lile la mwaka 1959, lilikuja Tanzania mwaka 1964. Wakimbizi wapatao elfu tatu (3000) waliingia Tanzania kutoka Rwanda. Wakimbizi hawa walitoka jimbo la Kivu nchini Zaire ambako walikimbilia awali na baadaye kuletwa Tanzania kwa makubaliano na UNHCR. Hivyo kufikia mwishoni mwa mwaka 1965 kulikuwa na wakimbizi wapatao 15,000 kutoka Rwanda. Wakimbizi wa Rwanda waliokuwa wanaishi katika Mikoa ya Kagera na Rukwa, walipewa uraia mwaka 1980 na kupelekea makazi yao kufungwa.

Mwaka 1964 lilitokea wimbi lingine la wakimbizi kutoka Msumbiji baada ya Chama cha FRELIMO kuanzisha harakati dhidi ya ukoloni wa Kireno ambapo wakimbizi wapatao 10,000 walikimbilia Tanzania toka nchini humo. Wakimbizi hao walirejea kwao mwaka 1975 baada ya Msumbiji kupata uhuru. Wakimbizi wa Msumbiji walianza tena kukimbilia nchini mwaka 1986 baada ya kuzuka vita nchini humo kati ya majeshi ya Serikali na ya RENAMO. Wakimbizi hao walirejea nchini Msumbiji katika miaka ya 1990.

Mwaka 1972 wakimbizi wengine waliingia Tanzania kutokea Burundi kufuatia vurugu za uasi nchini humo. Kundi hili lilikuwa na wakimbizi wapatao 130,000, wengi wao wakiwa wa jamii ya Kihutu. Hali hii ilisaba

bisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzisha Makazi ili wakimbizi waweze kuwa na sehemu ya kuishi na kuendesha shughuli zao hasa za kilimo. Sera ya wakati huo iliruhusu wakimbizi kupewa ardhi kwa ajili ya makazi na shughuli za kilimo. Aidha, Jumuiya ya Kimataifa kupitia UNHCR ilijenga miundo mbinu mbalimbali kwenye maeneo hayo kama vile Shule, Zahanati na Barabara ili wakimbizi waweze kuishi maisha mazuri. Kutokana na kuwepo wakimbizi hawa wa Burundi, mnamo mwaka 1972 Makazi ya Wakimbizi ya Ulyankulu, katika Wilaya ya Urambo, mkoani Tabora, yalianzishwa kwa ajili ya wakimbizi hawa. Mwezi Agosti, mwaka 1973 yalianzishwa Makazi ya Katumba, katika wilaya ya Mpanda, mkoani Rukwa, na makazi ya Mishamo, ambayo pia yalikuwa wilayani Mpanda, yalianzishwa mwanzoni mwa mwaka 1978.

Jumuiya za Kimataifa kupitia UNHCR na mashirika ya kimataifa yanayohusu misaada ya kibinaadamu, walitoa huduma kwa wakimbizi hawa hadi tarehe 28 Juni 1980 yalipokabidhiwa rasmi kwa Serikali baada ya kuonekana kuwa wakimbizi walikuwa wakijitosheleza kwa chakula na huduma nyingine za kijamii. Awali, Makazi ya Katumba yalikabidhiwa kwa Serikali mwezi Juni 1978 yakiwa na wakimbizi 60,000. Makazi ya Mishamo yalipoanzishwa yalikuwa na wakimbizi wapatao 37,000.

Makazi mengine yaliyowahi kuhifadhi wakimbizi nchini ni Pangale na Kigwa mkoani Tabora, Mwese mkoani Katavi, Karagwe (ilyogawanyika sehemu 3 za Nkwenda, Kimuli na Sina) na Muyenzi mkoani Kagera, Rutamba na Matekwe mkoani Lindi; Lundo, Mahukuru, Mputa na Likuyu Sekamaganga mkoani Ruvuma. Makazi ya Chogo mkoani Tanga yalihifadhi wakimbizi kutoka Somalia (Somali – Bantu). Wakimbizi waliohifadhiwa katika Mikoa ya Lindi na Ruvuma walitoka nchini Msumbiji na wale waliohifadhiwa katika Mikoa ya magharibi walitokea Burundi, Rwanda na DR Kongo (zamani Zaire).

1.6.2 Hifadhi katika makambi ya Wakimbizi miaka ya 1990

Mwaka 1993 kulitokea jaribio la kupindua Serikali nchini Burundi ambalo lilisababisha wakimbizi wapatao 300,000 kukimbilia Tanzania baada ya kuuawa kwa Rais wa Kwanza wa Burundi aliyechaguliwa kidemokrasia, Melchior Ndadaye ambaye aliuawa tarehe 21 Oktoba 1993. Vilevile katika Nchi ya Rwanda, miaka 1990 kulizuka mapigano ya waasi wa Rwandese Patriotic Front (RPF) na Serikali ya Rais Habyarimana ambaye alifariki kwa ajali ya ndege pamoja na Rais wa Burundi Aprili 1994 na kusababisha wakimbizi wa Rwanda wapatao zaidi ya milioni moja kuingia nchini kuomba hifadhi ya ukimbizi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 1995 kulikuwa na wakimbizi wapatao 700,000 kutoka Rwanda.

Kwa kuwa idadi ya Wakimbizi iliongezeka sana Serikali ya Tanzania iliamua kubadili sera ya kupokea na kuhifadhi wakimbizi. Badala ya kuwaweka kwenye Makazi na kuwagawia hekta mbili na nusu za ardhi kwa kila familia, walipangiwa kuishi kwenye maeneo maalum ya makambi yaliyotengwa kisheria (designated areas) na kupatiwa huduma zote za kibinadamu ikiwemo chakula, dawa, malazi na huduma hizi zilitolewa na Jumuiya ya Kimataifa kupitia UNHCR. Tofauti ya Makazi na Makambi ni kuwa katika makazi wakimbizi hupewa ardhi kwa ajili ya kujikimu na kujihudumia wenyewe bila msaada wa Serikali au mashirika ya kimataifa, na huendesha shughuli zao za kujipatia chakula na huduma zingine za jamii, wakati makambi ni maeneo maalum kwa ajili ya wakimbizi ambao hupewa eneo la mita 1600 za mraba kwa ajili ya kujenga makazi yao na kwa ajili ya bustani ndogo ndogo (kitchen gardening) na hupatiwa huduma nyingine zote na UNHCR kwa kushirikiana na mashirika yanayotoa misaada ya kibinadamu. Kambi ya Benaco iliyokuwepo wilayani Ngara na kuhifadhi wakimbizi 250,000 ndiyo iliyokuwa kambi kubwa zaidi duniani kwa kuhifadhi idadi kubwa ya wakimbizi kwa wakati huo. Wakimbizi wa Rwanda walirejea kwao kwa hiari mwishoni mwa mwaka 1997.

Mnamo mwaka 2015 Tanzania ilipokea wimbi jingine kubwa la wakimbizi kutoka Burundi ambao waliingia nchini kuanzia mwezi Aprili 2015, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2016 idadi ya walioingia nchini ilifikia 245,000. Kuingia kwa wakimbizi hao kuliifanya Serikali kuamua kufungua upya kambi zilizokuwa zimefungwa za Nduta na Mtendeli mkoani Kigoma. Wakimbizi hao walianza kuhifadhiwa katika kambi ya Nyarugusu ambayo ilikuwa kambi pekee iliyobaki kwa wakati huo. Idadi ilipozidi ya Wakimbizi hao, wengine wakahamishiwa kambi za Nduta na Mtendeli.

Serikali ya Tanzania pia imefanya juhudi kubwa katika kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi wanaohifadhiwa nchini. Tangu kuanzishwa kwa makambi miaka ya mwanzoni ya 1990, zaidi ya wakimbizi 1,200,000 wamerejeshwa katika Nchi zao za asili kwa hiari. Kwa upande mwingine zaidi ya wakimbizi 200,000 wamepewa uraia wa Tanzania ikiwa ni pamoja na wakimbizi warundi 162,156 wa mwaka 1972 ambao walipewa uraia mwaka 2009/2010; wengine ni Wanyarwanda wapatao 36,000 hawa walipewa uraia miaka ya 1980 na Wasomali 1,430 waliopewa uraia miaka ya 2005 – 2010, wengine ni wakimbizi kadhaa wanaoishi vijijini waliopewa uraia kwa masharti nafuu miaka ya 1990. Aidha, katika kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi zaidi ya 39,000 wamepelekwa Nchi ya tatu katika mpango maalum wakuhamishia wakimbizi Nchi ya tatu ulioanza mwaka 2007.

Pia, katika kundi la wakimbizi Warundi walioingia nchini kuanzia mwaka 2015, wakimbizi zaidi ya 139,000 wamerejea katika Nchi yao ya asili kwa hiari.

Kwa sasa tunao wakimbizi 255,275 kutoka nchi za, Burundi wapo 175,498, DRC 79,337 mataifa mengine 440

1.7 IDARA YA HUDUMA ZA UANGALIZI

Idara ya Huduma za Uangalizi (Probation Services Division), inasimamia utekelezaji wa adhabu mbadala ya kifungo gerezani kupitia Sheria ya Huduma kwa Jamii, Sura ya 291 (The Community Service Act, Cap 291), Sheria ya Probesheni, Sura 247 (The Probation of Offenders Act, Cap, 247), Sheria ya Magereza Na. 34/1967 (Kifungu cha 52), ambapo, wahalifu waliohukumiwa vifungo visivyozidi miaka mitatu (3), kwa mujibu wa Sheria

hizo hutumikia/hupendekezwa kutumikia adhabu zao nje ya magereza.Idara ilianza kufanya kazi ikiwa kama Sekretarieti katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma. Baadaye ilipanda hadhi na kuwa Idara na kufanikiwa kupanua wigo wake kwa kuifikia Mikoa yote ya Tanzania Bara.

1.8 SEKRATARIETI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA BIASHARA HARAMU YA USAFIRISHAJI WA BINADAMU

Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binamu ilianzishwa mwaka 2011, baada ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2000 kusaini Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia Uhalifu wa Kimataifa wa Kupangwa (United Nations Convention against Transnational Organized Crime, 2000) na Itifaki ya Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu, hususan wanawake na watoto (Parlemo Protocol, 2000) Mwaka 2008, Serikali ilitunga Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu Na. 6/2008 inayoharamisha vitendo vyote vinavyohusiana na biashara ya binadamu. Sheria hii ni ya Muungano na ilifanyiwa marekebisho mwaka 2016 na mwaka 2021 ili kuboresha utekelezaji wake.

1.9 KITENGO CHA MSAJILI WA JUMUIYA

Usajili wa Jumuiya nchini ulianza rasmi mwaka 1954 chini ya Sheria ya Jumuiya Sura ya 337 (The Societies Ordinance, Act No. 11 of 1954, Cap 337). Katika kipindi hicho, usajili ulikuwa ukifanyika na Msajili wa Vyama (Registrar of Societies). Aidha, mwaka 1955 wadhifa wa Msajili ulibadilika na kuwa Msajili Mkuu (Registrar General) ambaye alikuwa chini ya Idara ya Ardhi na Utafiti. Baada ya uhuru wa Tanganyika, usajili jumuiya ulikuwa chini ya Msajili wa Vyama aliyekuwa ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Tangu mwaka 1954 hadi mwaka 1971, Jumuiya zote nchini zilikuwa zinasajiliwa chini ya Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337 ikiwa ni pamoja na Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Siasa, vyama vya Michezo na asasi zote za kiraia.

Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya Sheria mbalimbali ambayo yamekuwa yakifanyika katika kipindi chote hadi kufikia mwaka 2019, baadhi ya vyama na taasisi zililazimika kuhamisha usajili wake kwenda kwenye mamlaka tofauti za usajili. Hivi sasa, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya ambayo iko Winzara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inasajili Jumuiya za Kidini na Jumuiya zisizo za Kidini

2 MAFANIKIO MAKUBWA YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 60 YA UHURU

2.1 Hali ya Ulinzi na Usalama

Baada ya Uhuru, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepitia katika hatua kadhaa za mafanikio, ikiwemo kusimamia jukumu kubwa la kuhakikisha Nchi yetu na watu wake wanakuwa katika hali ya amani, utulivu na usalama hivyo kuwafanya watanzania na wageni kuendelea kuishi katika hali ya Amani, Utulivu na Usalama, huku wakiendelea na shughuli za kiuchumi na kimaendeleo.Sambamba na kufanikiwa kudhibiti matukio ya mauaji ya vikongwe, walemavu wa ngozi na uchunaji wa ngozi ya binadamu katika mikoa ya nyanda za juu kusini na mikoa ya kanda ya ziwa.

2.2 Mabadiliko ya Kimuundo

Mafanikio mengine ni mabadiliko ya Kimuundo kwa baadhi ya Idara zake kuwa Jeshi kamili, ambapo Kikosi cha Zimamoto kilibadilishwa na kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji kuwa Jeshi la Uhamiaji.

2.3 Ujenzi na Uboreshaji wa Ofisi na Makazi ya Maafisa na Askari

2.3.1 Makazi ya Maafisa na Askari

Umefanyika uboreshaji wa Ofisi na Makazi ya Askari wa vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama vilivyoko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambapo kwa sasa Wizara imebadilisha mfumo wa ujenzi wa nyumba za askari kutoka nyumba za mabati na kuwa za kisasa. Baada ya Uhuru, Jeshi la Polisi limejenga nyumba 10,048 za makazi ya Maafisa na Askari wake katika Mikoa mbalimbali nchini. Kati ya mwaka 2016 hadi sasa Jeshi la Magereza limejenga nyumba 310 za kisasa zenye uwezo wa kuhudumia familia 564 kwa ajili ya makazi ya Maafisa na Askari. Kwa upande wa Idara ya Uhamiaji ina jumla ya nyumba 491 za Maafisa na Askari wake katika Mikoa mbalimbali Nchini zilizonunuliwa na kujengwa baada ya Uhuru. Jeshi la Zimamoto limefanikiwa kujenga nyumba 95 kwa ajili ya makazi ya Maafisa na Askari katika Mikoa mbalimbali Nchini ukilinganisha na nyumba za makazi ya Askari ya kutosha familia 14 zilizokuwepo wakati wa Uhuru.

2.3.2 Ofisi, Vituo vya Polisi na Zimamoto na Uokoaji

Wizara kupitia Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyo chini yake, imeendelea kuboresha Ofisi zake, ambapo karibu Vyombo vyote vina Ofisi katika Mikoa na Wilaya nchini, ukilinganisha na hali ilivyokuwa baada ya Uhuru. Aidha, Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Makao Makuu ya Jeshi la Magereza zimejengwa Dodoma, Ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji unaendelea, jijini Dodoma. Serikali imelipatia Jeshi la Polisi jengo la Ofisi za Makao Makuu jijini Dodoma. Jeshi hilo, limejenga Vituo 371 vya Polisi nchini na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limejenga Vituo vya Zimamoto 78 nchini ukilinganisha na vituo vinne vya Kikosi cha Zimamoto vilivyokuwepo kabla ya Uhuru. Aidha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa NIDA imefanikiwa kufungua Ofisi 151 katika Wilaya 150 za Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, Idara ya Uhamiaji ina jumla ya majengo 57 ya Ofisi katika Mikoa mbalimbali nchini ukilinganisha na majengo machache ya Ofisi yaliyokuwepo wakati Nchi yetu inapata Uhuru, kwani Idara ofisi zake nyingi zilikuwa katika majengo ya Serikali au watu binafsi.

2.4 Uanzishwaji na Uboreshaji wa Vyuo vya Taaluma na Mafunzo ya Kijeshi

Umefanyika upanuzi wa Shule ya Polisi Moshi (TPS) mkoani Kilimanjaro iliyoanzishwa wakati wa ukoloni, ambapo mabweni ya kuishi wanafunzi 662 na madarasa ya wanafunzi 320 yamejengwa, ujenzi wa bweni la ghorofa nne la kuishi wanafunzi 180 umekamilika na pia ujenzi wa mabweni ya maghorofa matatu yanaendelea kujengwa. Ghorofa moja lenye madarasa ya kuweza kutumiwa na wanafunzi 140 pamoja na ofisi na ukumbi wa mikutano vimejengwa katika Chuo cha Taaluma ya Polisi

Dar es Salaam (DPA-Chuo kilichokuwepo wakati wa ukoloni). Vyuo vilivyoanzishwa baada ya Uhuru ni Chuo cha Polisi Zanzibar, Chuo cha Polisi Kidatu na Chuo cha Polisi Wanamaji Mwanza. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limefanikiwa kuanzisha Chuo cha Zimamoto na Uokoaji katika eneo la Chogo, Wilaya ya Handeni, Jijini Tanga ambacho kinatumika kwa ajili kutoa mafunzo mbali mbali kwa Maafisa na Askari wakati wa kupandishwa vyeo na mafunzo ya awali. Chuo kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 700.

Idara ya Uhamiaji imefanikiwa kuanzisha Vyuo vya Mafunzo kwa Maafisa wa Ngazi ya Juu – TRITA ambacho pia hutoa mafunzo kwa Maafisa na Askari kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwingineko. Aidha, hutoa pia mafunzo kwa wadau wengine wa masuala ya kiuhamiaji Kitaifa na Kimataifa. Vilevile, Jeshi la Uhamiaji limeanzisha Kambi ya Boma Kichakamiba Mkoani Tanga kwa ajili ya kuendesha Mafunzo ya Awali na Ngazi ya Uongozi Mdogo kwa Askari kabla ya kupanda au kupata Vyeo vipya. Hatua hii ni mafanikio makubwa kwani kabla ya Uhuru Idara haikuwahi kuwa na Vyuo vyake yenyewe bali ilikuwa inategmea vyou vya Polisi, Magereza na Jeshi (JKT).

2.5 Mfumo wa Uhamiaji Mtandao

Huduma za Kiuhamiaji baada ya Uhuru zilikuwa zikitolewa kwa njia ya kuandikwa kwa Mkono "manual" hali iliyosababisha ucheleweshaji wa huduma kwa wateja na kuongezeka kwa matukio ya kughushi nyaraka mbalimbali za Uhamiaji. Mpango wa uboreshaji mifumo ya utoaji Huduma za Uhamiaji kidijitali zilianza kutekelezwa wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu ya Mhe. Benjamin William Mkapa, ambapo Pasipoti zilianza kutolewa katika mfumo wa Kompyuta (zenye uwezo wa kusomeka kwa mashine). Mwaka 2018 mwezi Januari Idara ulizindua mfumo wa Uhamiaji Mtandao unaounganisha Mifumo yote ya Utoaji huduma za kiuhamiaji kama vile Pasipoti, Visa, Vibali vya Ukaazi pamoja na Udhibiti na Usimamizi wa Mipaka kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huu ambao umeleta mageuzi makubwa kiutendaji katika Idara ya Uhamiaji umewezesha kubadilishana taarifa na mifumo mingine iliyo nje ya Idara yenye kutunza kumbukumbu mbalimbali za watu, kwa mfano NIDA, RITA, Police.

Tangu kuzinduliwa kwa Mfumo wa utoaji Huduma kwa njia ya kielektroniki mwaka 2018, Jumla ya hati za kusafiria 442,173 zimetolewa kwa watanzania waliopo nchini na kupitia Ofisi za Balozi zetu nje ya Nchi. Aidha, Mfumo wa Uhamiaji Mtandao, umesaidia kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi, Kudhibiti Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali na Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Kiuhamiaji kwa raia wa Tanzania na wageni wanaoingia na kuishi nchini, kwa madhumuni mbalimbali.

Idara imefanikiwa kusimika mfumo wa Uhamiaji Mtandao katika Ofisi ya Uhamiaji Kurasini - Dar es Salaam, Afisi Kuu Zanzibar, Ofisi za Uhamiaji Mikoa yote nchini, Balozi za Tanzania 44 zilizopo Nje ya Nchi, Vituo vya Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vya JNIA (DSM), AAKIA (Zanzibar) na KIA (Kilimanjaro) pamoja na Vituo vya kutolea huduma kwa pamoja Mipakani (OSBP) vya Tunduma, Namanga, Horohoro, Holili, Sirari, Mtukula, Rusumo, Kabanga na Kasumulu.

Pia mfumo huu umesimikwa katika Vituo vya Uwekezaji nchini (TIC) na Mamlaka Maalum ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje (EPZA) na Kituo cha Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa lengo la kurahisisha/kuwezesha upatikanaji wa Vibali vya Ukaazi kwa Wafanya biashara wa kigeni na wawekezaji.

Aidha, Idara imeboresha utoaji wa Vibali vya Ukaazi vya karatasi na kuanza kutoa Vibali vipya katika "format ya Smart Card". Vibali hivi ni bora, vya kisasa na vyenye usalama wa hali ya juu. Ni vibali ambavyo haviwezi kughushiwa au kuharibika kirahisi kwa kuingia maji au kuchanika kwa kuwa vinachapwa kwa kutumia Kadi ngumu.

Umefanyika uboreshaji wa miundombinu ya utoaji Huduma za Uhamiaji, na kwa sasa huduma zote utoaji wa Pasipoti, Visa, Hati za Ukaazi na Pasi, pamoja na matumizi ya Mfumo wa Udhibiti na Usimamizi wa Mipaka (e-border systems). hutolewa kwa njia ya kieletroniki. Aidha, Idara ilipata tuzo ya kuwa na Pasipoti yenye bora kwa Ukanda wa Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika kwa kukidhi viwango vya ubora wa kiusalama (Passport Security Features) iliyotolewa tarehe 26 Machi, 2019 katika visiwa vya Malta.

Vilevile, huduma ya Pasipoti imefanikiwa kupata TUZO MBILI hapa nchini zinazotolewa na kampuni ya "Tanzania Digital Awards" ambapo Idara iliibuka kuwa mshindi wa kuwa Taasisi Bora ya Serikali inayotoa huduma zake kupitia mifumo ya kieletroniki (Best Government Agency on Digital) na Tuzo nyingine ni kuwa Taasisi yenye ubunifu katika mifumo ya kielektroniki (Digital Innovation of the Year) kwa mwaka 2020.

2.6 Ujenzi wa Viwanda

Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza, (SHIMA) kupitia Ubia baina yake na PSSSF Nchini limekamilisha ujenzi wa Viwanda vinne vya utengenezaji wa bidhaa za ngozi, vinavyojengwa katika eneo la Gereza Karanga Mjini Moshi. Aidha, kimejengwa Kiwanda cha Ushonaji cha Jeshi la Polisi Tanzania katika eneo la Kurasini Jijini Dar es Salaam, kitakapo kamilika kitakuwa na uwezo wa kushona sare 500 kwa siku ukilinganisha na kilichorithiwa toka wakoloni kinachozalisha sare 200 kwa siku. Kiwanda hicho hivi sasa kinatengeneza "crown', kushona vyeo mbalimbali vya askari "rank and file' na kuokoa fedha zilizokuwa zikitumika kuagiza nje. Aidha Idara ya Uhamiaji 2021 imeanzisha Kiwanda kidogo cha Ushonaji wa nguo na Sare mbalimbali za askari na Maafisa wa Uhamiaji, lengo likiwa ni kutosheleza mahitaji ya ushonaji wa sare za askari na Maafisa kiwandani hapo badala ya kupeleka kwenye viwanda ambayo gharama zake ni kubwa.

Idara ya Uhamiaji imeendelea kuboresha Kiwanda chake cha Uchapaji Kijichi (KPU-Kijichi Printing Unit) kilicho nunuliwa mwaka 2001 kutoka Benki ya Taifa ya Kibiashara (NBC) kwa ajili ya kuchapa nyaraka mbalimbali za Idara ya Uhamiaji ambazo zimekuwa zikitumika tangu baada ya Uhuru hadi sasa. Kuwepo kwa kiwanda hicho

kumepunguza gharama za uchapaji wa nyaraka nje ya Idara na pia imesaidia kulinda usalama wa nyaraka zake. Aidha kwa sasa Idara ina lengo la kuwezesha kiwanda hicho kujiendesha kibiashara ili kutimiza maelekezo ya Serikali kuwa kila taasi ya Kijeshi iwe na miradi inaingiza faida.

2.7 Huduma za Zimamoto na Uokoaji
Kwa Upande wa utoaji wa Huduma za Zimamoto na Maokozi/Uokozi, kati ya mwaka 2015 hadi 2021, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limefanikiwa kuzima moto na kufanya maokozi katika matukio 13,168 ambayo kama yasingedhibitiwa yangeleta madhara zaidi kwa wananchi. Jeshio la Zimamoto na Uokoaji limefanikiwa kuwa na fire hdrants 2,042, ukilinganisha na fire hydrants 503 zilizokuwepo kabla ya miaka 60 ya uhuru.
Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeshirikishwa katika utoaji ushauri wa kitaalam katika Miradi Mikubwa inayoendelea inayotekelezwa na Serikali ikiwemo; Mwalimu Nyerere hydro-electric Power, Standard Gauge, Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) mpaka Tanga (Tanzania) na ujenzi wa Jengo jipya Namba 3 la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Pia Jeshi limeshafanikiwa kupeleka gari la zimamoto pamoja na Askari kwa ajili ya kutoa huduma za zimamoto na uokoaji katika mradi wa (Mwalimu Nyerere hydro-electric Power).

2.8 Ukusanyaji ya Maduhuli ya Serikali
Mwaka 2013, Idara ya Uhamiaji ilianzisha utaratibu wa kukusanya maduhuli kupitia Benki za CRDB na NMB ambapo baada ya kuzinduliwa kwa Uhamiaji Mtandao makusanyo ya maduhuli ya Serikali yanakusanywa kwa kupitia "Control number". ukilinganisha na baada ya Uhuru wakati makusanyo yalikuwa yanafanyika kwa Mhasibu kupokea ada ya huduma mkononi na baadaye kuwasilisha Benki. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali (FSIRMS)-'Fire Safety Revenue Management System' ambao husaidia kupunguza upotevu wa maduhuli ya Serikali.

2.9 Uanzishwaji wa Madawati ya Kijinsia
Mwaka 2009 Dawati la Jinsia na Watoto lilizinduliwa rasmi katika Kituo cha Polisi Oysterbay Dar es Salaam, kwa niaba ya Vituo vyote vya Polisi Tanzania. Kwa sasa Madawati ya Jinsia na Watoto 420 yameanzishwa Nchi nzima lengo likiwa ni kuzuia na kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto.

2.10 Uanzishwaji wa Mashirika ya Uzalishaji Mali.
Yameanzishwa Mashirika mawili ya Uzalishaji Mali likiwemo Shirika la Uzalishaji Mali la Mag ereza linaloendesha miradi 23, kati ya hiyo 15 ya kilimo na 8 ya viwanda. Shirika lingine ni la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi lililoanzishwa mwaka 2013 ambalo hadi sasa limejenga Kituo cha kisasa cha Oysterbay, nyumba 23 za maafisa mikocheni, nyumba 330 za kambi ya Polisi Kunduchi. Aidha Shirika hili limeweka mifumo mbalimbali itakayo wezesha Jeshi la Polisi kujiongezea uwezo wa kiuchumi.

2.11 Usajili na Utambuzi wa Wananchi
Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inaendelea na jukumu la usajili na utambuzi wa watu na kugawa vitambulisho kwa wananchi wote wenye sifa. Hadi kufikia tarehe 15 Novemba, 2021 jumla ya wananchi 22,728,453 walikuwa wamesajiliwa kati ya watu 25,000,000 waliokusudiwa ambao ni sawa na asilimia 90.9. Jumla ya namba za utambulisho (NIN) 19,148,423 zilikuwa zimezalishwa ambazo ni sawa na asilimia 84.3 ya watu waliosajiliwa. Aidha, Mamlaka imefanikwa kuzalisha jumla ya vitambulisho 10,254,560 kati ya Namba za Utambulisho 19,148,423 kiasi amabcho ni sawa na asilimia 53.6.

Hata hivyo mpaka sasa jumla ya Vitambulisho 1,103,822 kati ya Vitambulisho vilivyozalishwa na kusambazwa sehemu mbalimbali wilayani, bado havijachukuliwa na wananchi. Miongoni mwa hivyo, 206,959 vipo katika ofisi za Usajili za wilaya na 896,863 vipo katika ofisi za serikali za kata na vijiji/Mitaa katika mikoa 31 ya Tanzania Bara na Visiwani.

2.12 Kuandaa na Kutunza Daftari la Taifa la Usajili na utambuzi wa watu na kushirikisha taarifa hizo na wadau wengine
Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imefanikiwa kujenga na kutunza Daftari la kieletroniki la Usajili na Utambuzi wa watu. Daftari hili kwa sasa lina jumla ya Namba za Utambulisho 19,102,234 zilizounganishwa na alama za vidole. Namba hizi zinatumiwa na taasisi nyingine katika kuhakiki taarifa za mwananchi kabla ya kumpatia huduma.

Baada ya kujenga Kanzidata ya watu wote nchini kwa kutumia NIN, Mamlaka imefanikiwa kuhamasisha matumizi ya namba za utambulisho wa Taifa katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Hivyo, kwa sasa, taasisi zinatumia Kanzidata ya Mamlaka kwa matumizi mbalimbali. Matumizi ya Kanzidata iliyojengwa na Mamlaka yametokana na Mamlaka kubuni mfumo maalumu unaoitwa 'Common Interface Gateway'.

Mfumo umebuniwa na kujengwa kwa kutumia watalaamu wa ndani wa Mamlaka. Mfumo huu una uwezo wa kupokea miamala (Verification Transactions) zaidi ya Milioni 2 kwa siku, umewezesha taasisi za Serikali na binafsi kupata huduma za Utambulisho wa Taifa kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Mpaka sasa jumla ya taasisi 51 zimeunganishwa kimtandao na Kanzidata ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa na zinatumia mfumo wa Utambuzi katika kutoa huduma kwa wananchi.

Baadhi ya mafanikio ya matumizi ya Mfumo wa Utambuzi kijamii na kiuchumi ni pamoja na Kuunganisha Mfumo wa Usajili na Utambuzi na Kampuni za Simu nchini na Kufanikisha usajili laini za simu takribani Milioni 53 kati ya Milioni 54.6 sawa na 97.1% ya laini zote, Kuunganisha na mfumo wa BRELA katika Usajili wa Kampuni, Kuunganisha na Mfumo wa Usajili wa walipa kodi (Tax Identification Number-TIN) na kufanikisha utoaji wa Online TIN hivyo, kufanikisha ukusanyaji wa mapato pamoja na Kuunganisha na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) katika utoaji wa bima za afya kwa wananchi na

hivyo kudhibiti matumizi ya bima kwa wasio walengwa.

Matumizi mengine ambayo pia yanatokana na kujengwa kwa Kanzidata yenye taarifa za watu katika Mamlaka ni pamoja na Kuunganisha na taasisi za kifedha kurahisisha ufunguaji wa akaunti za benki; Kuunganisha na mfumo wa utoaji wa Hati za Kusafiria kuhakikisha hati hizo zinatolewa kwa watanzania na kufanikisha utoaji wa Hati za viwanja; Kuunganisha na mfumo wa Usajili wa Kaya Maskini kupitia mfuko TASAF ili kuhakikisha wanaostahili ndio wananufaika na mfuko huo.

Matumizi ya mfumo wa kushirikishwa taarifa, umewezesha Mamlaka kukusanya maduhuli ya shilingi 23 bilioni tangu julai, 2020 iliporuhusiwa kukusanya maduhuli hadi Oktoba 2021. Hivyo, kuongeza wigo wa makusanyo ya fedha za Serikali ni moja ya mafanikio yanayotokana na Mamlaka kuwa na Kanzidata yenye taarifa za watu.

2.13 Kutekeleza Afua Mbalimbali za Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu.
Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kuzuia biashara ya binadamu, ikiwa ni pamoja na kufanya upelelezi na operesheni ya pamoja (Joint Operation) ili kusambaratisha mitandao inayojihusisha na biashara hii, kuwatia mbaroni wahalifu na kuwaokoa wahanga. Kufikia Novemba, 2021 jumla ya kesi 75 zinazohusiana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu zimefunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini na jumla ya wahalifu 63 wamehukumiwa kutumikia vifungo vyao gerezani. Sambamba na hilo, Serikali imeokoa na kusaidia jumla ya wahanga 973 waliokuwa wakitumikishwa kuomba mitaani, kufanyishwa kazi ngumu, kutumikishwa majumbani na kutumikishwa kingono. Kati yao, wahanga 936 waliokolewa hapa nchini ambapo wahanga 857 ni Watanzania, 20 kutoka Burundi, 25 kutoka Nepali, 30 kutoka India, 2 kutoka Pakistani, 1 kutoka Msumbiji na 1 kutoka Afrika Kusini. Wahanga 37 wa kitanzania waliokolewa kutoka nje ya Nchi hususan katika Nchi za Thailand (7), India (4), Oman (3), Yemeni (1), Kenya (14), Malaysia (2), Uganda (1) na Iraq (5). Katika jitihada za kuimarisha huduma kwa wahanga, mwaka 2021 Serikali ilianzisha Mfuko wa Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu (The Anti-Trafficking Fund) ili kusaidia kutoa huduma mbalimbali kwa wahanga wanaookolewa.

2.14 Uratibu na Ushirikiano wa Kitaifa na Kimataifa
Wizara kupitia Secretarieti hii, imeendelea kuimarisha ushirikiano miongoni mwa Wizara, Idara, na Taasisi za Serikali, Serikali za Mitaa, Asasi za Kijamii na wadau wengine katika kupambana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Hii ikiwa ni pamoja na kuweka mfumo wa kupeana taarifa, mfumo wa kutoa rufaa kwa wahanga, kuhuisha Daftari la Kitaifa la wadau linaloorodhesha majina na anwani za Taasisi na Mashirika yote nchini yanayotoa huduma kwa wahanga na kuimarisha upatikanaji wa takwimu. Vile vile, Wizara imeendelea kuimarisha uratibu na ushirikiano na wadau katika ngazi ya Kikanda ambapo mwaka 2018 Serikali ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa SADC wa Kuzindua Taarifa ya Kikanda kuhusu Takwimu za Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu kwa Nchi wanachama wa SADC uliofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 21 – 24 Agosti 2018 na Mkutano wa Viongozi Waandamizi wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) wa kupitisha Sera ya Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu uliofanyika kuanzia tarehe 6 – 8 Oktoba 2021, Unguja Zanzibar. Sambamba na hilo, Serikali imeendelea kushiriki kikamilifu katika mikutano ya kimataifa na mikutano baina ya Nchi mbili juu ya kuzuia na kupambana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

2.15 Kupunguza msongamano wa wafungwa Magerezani:
Katika kipindi hicho Idara imefanikiwa kuwasajili Wafungwa 24,087 (kati yao wanaume ni 19,475 na wanawake ni 4,612) na kuwawezesha kutumikia adhabu nje ya magereza hivyo kupunguza msongamano magerezani.

2.16 Kuipunguzia Serikali gharama za kuendesha magereza:
Idara imefanikiwa kutoa wafungwa 24,087, imeokoa shilingi 224,009,100,000/= (2,500x24,087x30x124) ambazo zingetumika kuwalisha chakula wafungwa kwa kutumia Tsh. 2,500 kwa mfungwa mmoja kwa siku na shilingi 228,338,560,000/= (4,000x23,018x20x124) ambazo zingetumika kuwalipa vibarua ambao wangeajiriwa kufanya majukumu hayo yaliyofanywa wafungwa wa kifungo cha nje.

2.17 Usajili wa Jumuiya
Tangu usajili wa Jumuiya ulipoanza mwaka 1954 hadi kufikia mwezi Novemba 2021, Kitengo cha Msajili wa Jumuiya kimefanikiwa kusajili Jumuiya 10,108, ambapo Jumuiya za Kidini ni 1,226 na Jumuiya zisizo za Kidini ni 8,882. Kitengo kimefanikiwa Kulinda na kudumisha tunu za Amani, umoja na Mshikamano katika Nchi yetu, kwa kuhakikisha kuwa malengo ya jumuiya zote zinazoomba usajili zinazingatia tunu hizo na kuhakikisha shughuli zao haziendi kinyume na kuathiri mila, desturi na utamaduni wa Kitanzania.

2.18 Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko
Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeanza kutumia Mfumo wa Ki – elektroniki wa kushughulikia malalamiko uitwao e-mrejesho ambao umeongeza ufanisi na utaongeza kasi ya kupokea, kushughulikia na kutoa mrejesho kwa walalamikaji.




# MAENDELEO YA SEKTA YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 60 YAUHURU WA TANZANIA BARA

## 1 MAFANIKIO YA KILIMO

### 1.1 KILIMO KIMEENDELEA KUKUA NA KUCHANGIA KATIKA UCHUMI

Tangu mwaka 1961, ukuaji wa sekta ya kilimo umekuwa ukipanda na kushuka kutokana na sababu mbalimbali, kubwa ikiwa ni mabadiliko ya hali ya hewa. Kuanzia miaka ya 1970 hadi mwishoni mwa miaka ya 1990, kilimo kilikuwa kikikua kwa wastani wa asilimia 3.1 kwa mwaka. Kutokana na sera na mikakati ya kuendeleza `sekta ya kilimo iliyoandaliwa na Serikali, kuanzia mwaka 1995 kilimo kilianza kuongeza kasi ya ukuaji. Kwa mfano katika kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 1995 hadi 2005 kilimo kilikua kutoka wastani wa asilimia 2.1 hadi wastani wa asilimia 6. Katika kipindi cha kuanzia 2005 hadi 2010 sekta ya kilimo imekua kwa wastani wa asilimia 4.02. Aidha, kati ya mwaka 2015 hadi 2020, sekta ya kilimo imekua kwa wastani wa asilimia 5.1 huku sekta ndogo ya mazao ikikuwa kwa wastani wa asilimia 5.7.

Mwaka 1961 wakati tunapata uhuru, mchango wa kilimo katika mapato ya fedha za kigeni ulikuwa ni zaidi ya asilimia 75. Kadhalika, idadi ya Watanzania waliokuwa wanaendesha maisha yao kwa kutegemea kilimo ilikuwa ni zaidi ya asilimia 90 kati ya Watanzania milioni 9.8. Mchango wa sekta ya Kilimo katika Pato Ghafi la Taifa (Gross Domestic Product – GDP) ulikuwa zaidi ya asilimia 70, wakati kilimo kilikuwa kinachangia karibu asilimia 81 ya mapato ya mauzo ya nje. Mapato kutokana na mauzo ya mazao ya kilimo yalikuwa Dola za Marekani Milioni 115 mwaka 1961.

Kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita yaani kutoka mwaka wa 2010 hadi 2020, mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa umefikia wastani wa asilimia 29.1. Katika kipindi hicho, sekta ndogo ya mazao imechangia kwa wastani wa asilimia 14.9. Takwimu hizo zinaonesha kuwa kilimo bado kinachangia kiasi kikubwa katika uchumi ingawa kiwango cha uchangiaji kimekuwa kikishuka kutokana na kukua kwa mchango wa sekta nyingine hususan madini, viwanda, ujenzi na huduma.

## 2. UTAFITI, HUDUMA ZA UGANI NA MAFUNZO YA KILIMO

### 2.1 UTAFITI

Katika kipindi cha miaka 60 iliyopita, vituo vya utafiti wa kilimo vimezalisha teknolojia mbalimbali za kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji, tija na kipato kwa mkulima na Taifa kwa ujumla. Katika kuimarisha shughuli za utafiti na ugunduzi wa kilimo, Serikali ilianzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kupitia Sheria ya Bunge Na. 10 ya Mwaka 2016 (TARI's Act No. 10 of 2016). Aidha, utafiti wa kilimo nchini umeendelea kuimarisha mahusiano na wadau katika ngazi ya taifa, kikanda na kimataifa. Taasisi hizo ni pamoja na CGIAR Research Centres – (IRRI, IITA, CIAT, ICRISAT, ASARECA, CCARDESA na FARA), Vyuo Vikuuu, Wadau wa Maendeleo (Gates Foundation, AGRA, IFAD na FAO), Taasisi binafsi za hapa nchini na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs).

#### 2.1.1 Uanzishwaji wa Vituo vya Utafiti

Wakati Tanganyika inapata Uhuru, kulikuwa na vituo vitano ambavyo vilikuwa vimeanzishwa katika nyakati tofauti. Vituo hivyo ni TARI Tumbi kilichoanzishwa mwaka 1930; TARI Mlingano mwaka 1934; TARI Ukiriguru mwaka 1938; TARI Ilonga mwaka 1947 na TARI Maruku mwaka 1948. Hivyo, uanzishwaji wa vituo vya utafiti wa kilimo umeongezeka kutoka vituo 5 kabla ya Uhuru hadi kufikia vituo 17, ambavyo ni TARI Uyole mwaka 1968, TARI Kibaha 1970, TARI Tengeru mwaka 1975, TARI Makutupora mwaka 1979, TARI Selian mwaka 1980, TARI Dakawa mwaka 1984, TARI Kifyulilo mwaka 1985, TARI Hombolo mwaka 1972, TARI Mikocheni mwaka 1996, TARI Naliendele mwaka 1970, TARI Ifakara mwaka 1970, na TARI Kihinga mwaka 2018. Kuongezeka kwa idadi ya vituo vya utafiti kumesaidia kuongezeka kwa tafiti na upatikanaji wa teknolojia mbalimbali za kilimo kwa kuzingatia ikolojia.

#### 2.1.2 Mbegu Bora Zilizogunduliwa na Wazawa

Kabla ya kupata uhuru Tanzania haikuwa na wagunduzi wazawa wa mbegu ukilinganisha na miaka ya 2020 ambapo watafiti wa mbegu bora za mazao ni wazawa. Watafiti hao wazawa wamegundua aina 461 za mbegu bora za mazao ya nafaka, mikunde, mafuta, mizizi, mboga, migomba, miti, miwa na nyuzi. Mbegu hizo zina sifa za kutoa mavuno mengi, kustahimili mabadiliko ya tabia nchi, kukomaa haraka na ukinzani dhidi ya wadudu na magonjwa. Matumizi ya mbegu bora yamechangia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao, kwa mfano, zao la mahindi uzalishaji umeongezeka kutoka wastani wa tani 0.5 kwa hekta kabala ya Uhuru hadi tani 1.5 kwa hekta baada ya Uhuru. Aidha, uzalishaji wa zao la mpunga umeongezeka kutoka wastani wa tani 1.0 hadi tani 2.3 kwa hekta. Matumizi ya mbegu bora za muhogo yameongeza uzalishaji toka wastani wa tani 3.0 hadi tani 7.9 kwa hekta.

#### 2.1.3 Idadi ya Watafiti na Viwango vya Elimu

Kabla ya Uhuru hakukuwa na watafiti wenye elimu ya uzamivu (PhD). Aidha, idadi ya watafiti imeongezeka hadi kufikia wastani wa zaidi ya 100 katika miaka 60 ya Uhuru ambapo taasisi ina watafiti 55 wenye PhD, 213 wenye shahada ya uzamili (Masters), na 171 wenye shahada ya kwanza (degree). Kwa mfano, mwaka 2005/2006 watafiti walikuwa 311 na wameongezeka hadi 439 mwaka 2021/2022, sawa na ongezeko la 41%. Ongezeko hilo limechangia upatikanaji wa mbegu na miche bora na usambazaji wa teknolojia ambapo kwa wastani teknolojia 70 zinasambazwa kwa mwaka tofauti na miaka ya 1960 ambapo teknolojia zilikuwa hazisambazwi wala kuhamasishwa matumizi yake kwa wadau. Katika kusambaza teknolojia hizo, TARI imeanzisha tovuti pamoja na mitandao ya kijamii ambayo hutumika kusambaza teknolojia mbalimbali za kilimo zikiwemo habari na matukio yanayojiri katika vituo vyote 17 vya TARI ambapo imeweza kuwafikia wakulima 1,204,475 kwa mwaka 2020.

## 2.2 HUDUMA ZA UGANI

Huduma za Ugani nchini zilianza wakati wa Ukoloni ambapo msisitizo mkubwa ulikuwa kuongeza uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ambayo ni pamba, mkonge, chai, kahawa, pareto na korosho. Baada ya Uhuru kati ya mwaka wa 1962 na 1967, Serikali

ilitumia mbinu kuu mbili za kuongeza tija katika kilimo. Mojawapo ya mbinu hizo ilizingatia kutoa huduma za ugani kwa wakulima katika vijiji vyao vya asili na mbinu nyingine ilikuwa kuwahamishia wakulima katika makazi maalum ya kilimo. Matumizi ya mbinu hizo mbili yalilenga kuongeza kasi ya uzalishaji wa mazao hayo. Mabadiliko makubwa ya huduma za ugani yalitokea mwaka 1972 ambapo Sera ya Madaraka Mikoani ilianza. Usimamizi na utekelezaji wa Huduma za Ugani ulihamishwa kutoka Serikali Kuu na kupelekwa kwa Wakurugenzi wa Maendeleo wa Mikoa na Wilaya kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, katika miaka ya 1973 na 1978 Bodi na Mamlaka za Mazao, pamoja na Vyama vya Ushirika vilianza kutoa huduma za ugani.

Mabadiliko mengine yalitokea mwaka 1983 ambapo usimamizi na utekelezaji wa huduma za ugani ulirejeshwa Wizara ya Kilimo. Mwaka 1988 ulianzishwa Mradi wa Taifa wa Kuboresha Huduma za Ugani katika Kilimo na Mifugo (National Agriculture and Livestock Extension Rehabilitation Project - NALERP). Lengo kuu la mradi huo lilikuwa kuwawezesha wakulima na wafugaji kwa pamoja kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo na mifugo. Katika kufikia lengo hilo watalaam wa ugani wa ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Kijiji walipewa vitendea kazi. Programu ya Taifa ya Huduma za Ugani (NAEP II) ilianzishwa mwaka 1995 msukumo mkubwa ukiwa kumwezesha mkulima kubaini matatizo yake, kuyachambua, kuweka katika kipaumbele, kuangalia rasilimali aliyonayo na kuandaa mkakati na programu ya kutatua matatizo.

Mwaka 1997, Serikali ilirudisha majukumu hayo Serikali za Mitaa na Halmashauri za Wilaya. Kuanzia mwaka 1998, huduma za ugani zinaendeshwa kupitia vikundi vya wakulima, miradi ya kilimo, Wakala wa Huduma za Pembejeo, Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo, Vituo vya Wakulima (FTCs) na Vituo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs), Vyama vya Wakulima, Mashirika yasiyo ya Serikali (Non Government Organizations - NGOs), mashirika ya kijamii (Community Based Organizations – CBOs), mashirika ya dini, makampuni ya zana za kilimo, sekta binafsi , vyombo vya habari, maonesho ya kilimo na siku za wakulima.

### 2.2.1 Mafunzo ya Kuwaandaa Maafisa Ugani Tarajali

Miaka ya 1970 kulikuwa na Mwongozo wa "kijiji kimoja bwana shamba mmoja" wakati huo kulikuwa na mtaala mmoja ambao ulikuwa ukitoa cheti katika ngazi ya Astashahada ya AGROVET. Kutokana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi, Serikali iliendelea kufanya maboresho katika mitaala ya vyuo vya kilimo. Hadi mwaka 2021 Serikali imeweza kuandaa mitaala mipya saba (7) ya kilimo ambayo ni Agricultural Mechanization, Agriculture Production, Crop Production, Food Technology and Human Nutrition, Horticulture, Irrigation Engineering na Agricultural Land Use Planning and Management. Mitaala hii imeandaliwa katika mfumo wa umahiri (Competence Based Education and Training-CBET) na imethibitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi- NACTE.

Tangu mwaka 2009 hadi mwaka 2021 vijana 16,129 wamehitimu mafunzo ya stashahada na astashahada katika vyuo vya kilimo (MATIs) kama inavyoonesha katika jedwali Na.1. Mafunzo hayo yalitolewa katika vyuo 14 vya Serikali . Wengi wa wahitimu hawa wameajiriwa kama maafisa ugani katika Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Sekta Binafsi. Katika kuimarisha huduma za ugani nchini, Serikali imeongeza rasilimali fedha kwenye huduma za ugani kutoka Shilingi Milioni 603 mwaka 2020/2021 hadi Bilioni 11.5 katika bajeti ya mwaka 2021/2022.

### 2.2.2 Matumizi ya Teknolojia katika Huduma za Ugani

Katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima, Wizara imeanzisha mfumo wa M-Kilimo katika utoaji wa huduma hizo. Mfumo huo unawaunganisha wakulima na maafisa ugani, wakulima na masoko kwa njia ya simu ya kiganjani. Hadi sasa Wizara imefanikiwa kuwasajili maafisa ugani 6,986, wakulima 5,101,833 na Wafanyabiashara wa mazao 6,951 kwa mikoa yote ya Tanzania Bara. Kazi ya usajili na utoaji elimu inaendelea.

## 2.3 MAFUNZO

2.3.1 Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo

Katika kipindi cha mwaka 1961- 2021Tanzania ina jumla ya vyuo 29. Kati ya hivyo 14 vinamilikiwa na Serikali na 15 vinamilikiwa na Sekta binafsi. Katika kuimarisha vyuo vya mafunzo nchini, Wizara imekuwa ikikarabati miundombinu (ofisi, madarasa, maktaba, maabara, karakana, mabwalo ya chakula, mabweni, nyumba za watumishi, mifumo ya maji na umeme, vitengo vya mifugo na barabara za mashambani). Hadi kufika mwaka 2021, jumla ya vyuo 11 vimekarabatiwa na kusaidia kuongeza udahili wa wanafunzi hadi kufikia 3,360 kwa wakati mmoja. Aidha, ongezeko hilo limesaidia katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima wa maeneo mbalimbali nchini.

## 3. ZANA ZA KILIMO

Katika miaka ya 1960 sekta ya kilimo imekuwa ikitumia zana za kilimo zilizohusisha nguvu kazi ambayo ilisababisha kulima eneo dogo na kuzalisha mazao ya chakula na siyo ya kibiashara. Wizara imefanya jitihada katika kuongeza upatikanaji na matumizi ya zana bora za kilimo kwa kulenga kupunguza matumizi ya jembe la mkono na harubu zinazotokana na zana duni za kilimo. Zana bora za kilimo zimesaidia kuongeza uzalishaji na tija pamoja na kuwafanya wakulima kufanya kilimo cha kibiashara na kuongeza idadi ya wakulima wakati. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi imeweza kuongeza makampuni yanayoingiza zana nchini kama vile mashine ndogo za kuvuna mpunga (combine harvesters), mashine za kupandikiza mpunga (rice transplanters), mashine za kukata mpunga (reapers/cutterbars) na nyinginezo kutoka 8 mwaka 2000 hadi kufikia 56 mwaka 2021.

**3.1 Upatikanaji na Matumizi ya Trekta**
Idadi ya matrekta makubwa na madogo ya mkono yanayotumika katika kilimo yameongezeka kutoka 2,580 mwaka 1960 hadi kufikia 20,146 mwaka 2020 sawa na asilimia 23 ya matumizi ya matrekta katika kilimo. Aidha, Serikali katika kuhamasisha matumizi ya trekta imefuta kodi ya ushuru wa forodha na Ongezeko la thamani kwa matrekta na zana zake. Hii imesaidia kupunguza bei ya matrekta na zana zake ili kuwezesha wakulima wengi kununua na kuyatumia.

**3.2 Matumizi ya Wanyamakazi**
Kumekuwa na ongezeko la matumizi ya wanyamakazi katika kilimo na usafirishaji katika maeneo mbalimbali nchini. Matumizi ya maksai yameongezeka na kufikia asilimia 27 baada ya uhuru. Ongezeko la wanyamakazi hawa limesaidia wakulima kuweza kulima maeneo ambayo mashine za moto kama trekta haziwezi kulima, kusaidia kusafirisha mazao kutoka mashambani na kupita katika njia ambazo vyombo vingine vya moto haviwezi kupita na hivyo kusaidia wakulima kufanya shughuli za kilimo kwa ufanisi mkubwa.

**3.3 Msamaha wa kodi katika zana za kilimo**
Baada ya uhuru, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148 ambayo ilijumuisha kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa mashine na vifaa vya kukusanya ( pick up balers ), kuvuna nafaka (combine harvester)na zana za kuvuna marisho (hay making machinery) na zana za kukatia majani (mowers) na. Serikali pia ilisamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye mashine za kukausha na kukoboa mpunga (rice dryers and mills), mashine za kupandia mbegu (planters), na matrekta ya kukokota kwa mkono (power tillers). Aidha, kwa kuzingatia Sheria Na. 24 ya Mwaka 1997 ya Ongezeko la Thamani, pembejeo zote na zana za kilimo zimesamehewa kodi ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa Forodha (Zero rated). Zana zinazohusika ni pamoja na matrekta, majembe yanayokokotwa na wanyamakazi (plough), harrow, mashine za kupandia mbegu, mabomba ya kunyunyiza viuatilifu, majembe ya mkono, reki, rato, sululu, mashoka na mapanga.

## 4. KILIMO HIFADHI NA MAZINGIRA
Tangu uhuru, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kilimo imeendelea kutekeleza sera, mikakati, sheria na kanuni za usimamizi wa mazingira. Wizara pia imekuwa ikijihusisha na uratibu na utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa inayohusu mazingira kama mabadiliko ya tabianchi; kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame; udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la hewa ya Ozoni na hifadhi ya bayoanuai. Wizara imezingatia matumizi ya mbegu zinazostahimili ukame, wadudu waharibifu na magonjwa. Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wizara imefanikiwa kuhamasisha shughuli za hifadhi ya mazingira katika kazi za maendeleo ya kilimo ili kuongeza uzalishaji na kuwa na kilimo endelevu chenye tija.
Katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Wizara imetekeleza Mpango-Kazi wa Mazingira katika Sekta ya Kilimo (Agricultural Sector Environmental Action Plan, 2012 - 2017) katika kanda saba (7) za kilimo na kusambaza Mwongozo wa Tathmini ya Athari ya Mazingira katika shughuli za kilimo kwa Halmashauri zote za wilaya nchini.

Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, DFID, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) ilifanikiwa kuandaa Mpango wa Kilimo cha Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Agriculture Climate Resilience Plan, 2014 - 2019) kwa lengo la kupunguza athari za mazingira. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inatekeleza Programu ya Taifa ya Kilimo kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi (National Climate Smart Agriculture Programme, 2015– 2025) na imeandaa Mwongozo wa Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi (Climate Smart Agriculture Guideline( CSA guideline) mwaka 2017 ambao unatumika katika Halmashauri za Wilaya 129.

Katika kipindi cha 2015 – 2021, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira inatekeleza Mradi wa Kutunza Mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa unaolenga kupunguza shughuli za kibinadamu zinazoathiri mazingira. Kupitia mradi huo, Wizara imeibua shughuli mbadala zikiwemo ufugaji wa nyuki, ujenzi wa kitalu nyumba kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya mboga, uvuvi wa kisasa, kuhamasisha uzalishaji wa kakao na michikichi kwa kutoa miche ya kisasa na uzalishaji wa zao la korosho kwenye vijiji 15 vya Wilaya za Makete, Kyela, Nyasa, Mbinga na Ludewa.

Mafanikio mengine ni pamoja na kusaidia wakulima kutengeneza Mipango ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Jamii (Environmental and Social Management Plans) kwa kusudi la kupunguza uharibifu wa mazingira katika Vijiji vinavyozunguka mashamba ya uwekezaji manne (4) ya Mpanga-Ngalimila, Lukulilo, Mkulazi na Kitengule pamoja na ujenzi wa maghala 68 yaliyopo katika wilaya za Mbozi, Momba, Songea, Njombe, Iringa, Mpanda na Sumbawanga. Vilevile, kupitia mradi wa Kilimo Himilivu kwa kutumia Mfumo Ikolojia Vijijini (EBARR) iliwezesha Halmashauri ya Kishapu kuanzisha kitalu cha mkonge cha ekari 20 ambacho kinawanufaisha wakulima zaidi ya 300 katika wilaya ya Kishapu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa, imeandaa Mwongozo wa maafisa ugani na wakufunzi kuhusu tafsiri na matumizi ya huduma na taarifa za hali ya hewa kwa lengo la kuelimisha wakulima namna ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi.

## 5. UPATIKANAJI WA PEMBEJEO ZA KILIMO
Tangu nchi ipate Uhuru zimekuwepo jitihada mbalimbali za kuongeza upatikanaji wa mbegu bora, mbolea na viuatilifu ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60 ni kama ifuatavyo:-

**5.1 Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu Bora**
Mwaka 1973, kampuni ya kwanza ya mbegu bora iliyoitwa Tanzania Seed Company (TANSEED) ilianzishwa kwa lengo la kuzalisha na kusambaza mbegu bora nchini. Hadi mwaka 1980 kampuni hiyo iliweza kuzalisha tani 6,781 ilipofika mwaka 1999 uzalishaji huo ulipungua hadi kufikia tani 589.4 wakati mahitaji yalikuwa tani 120,000. Ili kukabiliana na mapungufu hayo Serikali iliruhusu makampuni binafsi kuingiza mbegu bora kutoka nje. Serikali pia ilianzisha Wakala wa Mbegu za Kilimo (Agricultural Seed Agency) mwaka 2006 kwa lengo la kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora nchini. Aidha, ASA kwa kushirikiana na makampuni binafsi imeongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 2,584.8 hadi kufikia tani 3,037.47. Pia, imeweza kuzalisha pingili 1,700,000 za muhogo na miche 64,725 ya michikichi. Katika kuhakikisha ubora wa mbegu zinazozalishwa, ASA imejenga maabara kwa ajili ya kuhakiki ubora.Lengo la Serikali ni kuongeza upatikanaji pamoja na matumizi ya mbegu bora ili kupunguza uagizaji wa mbegu hizo kutoka nje ya nchi.

Vilevile, uzalishaji wa miche umeongezeka kutoka miche 5,000,000 mwaka 2015 hadi kufikia miche 22,707,871 mwaka 2019. Pamoja na mambo mengine, mafanikio hayo yametokana na kuongezeka kwa eneo la uzalishaji wa mbegu na miche kutoka hekta 10,887 mwaka 2015/2016 hadi hekta 94,368 mwaka 2019/2020. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) imezalisha jumla ya tani 9,128 za mbegu bora ya nafaka na mikunde ambazo zimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika mikoa mbalimbali.

Katika kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora nchini, Wizara imeimarisha maabara ya Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Nchini (TOSCI) na hivyo kupata ithibati ya Shirika la Kimataifa la Uthibiti wa Ubora wa Mbegu (International Seeds Testing Association – ISTA) pamoja na kujiunga na Skimu za Mbegu za Shirika la Kimataifa (OECD Seed Schemes) ambayo itaiwezesha nchi kufanya biashara ya mbegu kimataifa.

**5.2 Upatikanaji wa Mbolea**
Kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa sera ya mfumo wa soko huru mwaka 1985, Serikali ilihusika moja kwa moja na uagizaji, usambazaji na uuzaji wa mbolea za viwandani kupitia Kampuni ya Mbolea ya Tanzania (Tanzania Fertilizer Company-TFC) na Vyama vya Ushirika. Baada ya mfumo wa soko huru kuanza idadi ya waagizaji na wasambazaji wa mbolea iliongezeka. Aidha, udhibiti wa ubora wa mbolea ulisimamiwa na Sheria ya Mbolea na Chakula cha Mifugo ya mwaka 1962. Hali hiyo ilisababisha Serikali kutunga Sheria Mpya ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009 ili kukidhi mabadiliko ya kijamii na kiuchumi kulingana na soko huru.

Wizara ilianzisha mfumo wa Ununuzi wa Pamoja wa Mbolea (Bulk Procurement System- BPS) kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa mbolea nchini. Pamoja na jitihada zingine zilizofanywa na Serikali, mfumo huo umeongeza upatikanaji wa mbolea kutoka tani 302,482 mwaka 2015/2016 hadi 678,017 mwaka 2020/2021. Aidha, idadi ya viwanda vinavyotengeneza mbolea na visaidizi vya mbolea (fertilizer suppliments) vimeongezeka kutoka viwanda vinne (4) mwaka 2015 hadi viwanda 13 mwaka 2019. Kati ya viwanda 13, viwanda viwili (2) ni vya visaidizi na 11 ni vya mbolea.

Aidha, Wizara imeanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Mbolea (Fertilizer Information System- FIS) ambao umeboresha utoaji wa huduma za usajili wa wafanyabiashara wa mbolea, utoaji wa leseni na vibali. Mfumo huo umefanikiwa kutoa leseni zaidi ya 1,100 za wauzaji, waingizaji, watengezaji na wasambazaji wa mbolea hadi kufikia mwezi Septemba, 2021. Kutokana na mazingira wezeshi y/a ufanyaji biashara nchi, Wawekezaji wa Kampuni ya ITRACOM (Itracom Fertilizers Limited) kutoka nchi ya Burundi wameanza ujenzi wa Kiwanda cha kuzalisha mbolea ya asili yenye mchangayiko wa madini ya Phosphate na samadi katika eneo la viwanda la Nala mkoani Dodoma. Kiwanda hicho kitakakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 500,000 kwa mwaka.

**5.3 Upatikanaji wa Viuatilifu**
Upatikanaji wa viuatilifu (sumu ambayo hutumika kuua, kuangamiza, kufukuza, au kuzuia visumbufu) vya milipuko kama vile panya, nzige, kweleakwelea na viwavijeshi vamizi katika mimea umeongezeka kutoka tani 4,111.50 mwaka 2015 hadi tani 16,869.10 mwaka 2019. Vilevile, Serikali imeanzisha Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu kupitia Sheria ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Na. 4 ya mwaka 2020 ambayo imetokana na kuunganisha Sheria Na. 18 ya mwaka 1979 iliyoanzisha Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Ukanda wa Kitropiki (TPRI) na Sheria Na.13 ya Hifadhi ya Mimea ya mwaka 1997. Hatua hiyo imesaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali na kupunguza taratibu za usajili wa viuatilifu na ukaguzi wa mazao hivyo kupunguza gharama za kufanya biashara. Aidha, Wizara kwa kushiriana na Taasisi nyingine za Serikali imewezesha kupatikana kwa mwekezaji wa ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha viuatilifu mkoani Arusha chenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 7.2 kwa mwaka na kutoa ajira takribani 300 . Mwekezaji anakamilisha taratibu za kuanza ujenzi.

**6 UENDELEZAJI WA MAZAO**
Serikali imeendelea kusimamia uendelezaji wa mazao nchini kwa lengo la kujitosheleza kwa chakula na kuongeza kipato. Malengo hayo yanafikiwa kwa kuongeza matumizi ya teknolojia bora katika mnyororo wa thamani wa mazao hayo.Katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru, Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-.

**6.1 Uzalishaji wa Mazao Makuu Asilia ya Biashara**
Uzalishaji wa mazao asilia ya biashara yakiwemo pamba, kahawa, chai, pareto, tumbaku, korosho, mkonge na miwa umeongezeka kutoka tani 796,502 mwaka 2015/2016 hadi tani 1,058,798 mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la asilimia 32.9.

**6.1.1 Mauzo ya Mazao makuu ya Biashara**
Katika kipindi cha mwaka 2015/2016, kiasi cha tani

1,613,000 za mazao ya kahawa, pamba, katani, chai, tumbaku na korosho kiliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa Dola za Marekani Milioni 3,419.77.

## 7. MAZAO YA BUSTANI

Katika kipindi cha 1960's msisitizo wa uzalishaji wa mazao ulikuwa katika mazao ya asili ya biashara kwa ajili ya malighafi katika nchi za Ulaya. Aidha, kupitia Azimio la Iringa lililohusu Siasa ni Kilimo, Serikali iliendelea kuweka msisitizo katika mazao ya asili ya biashara na mazao ya chakula. Mazao ya bustani yameanza kupata msukumo zaidi katika kipindi cha miaka ya 1990. Tangu kipindi hicho, Wizara imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuimarisha maendeleo ya mazao ya bustani nchini kwa kuweka mazingira wezeshi ya sekta binafsi kushiriki katika sekta ya kilimo.

Mazao ya Bustani ni kundi la mazao yanayojumisha matunda, mbogamboga, viungo, maua na vikolezo ambayo hutoa viinilishe (vitamini na madini), mapambo na tiba. Tasnia ya mazao ya bustani inaendelea kukua kutokana na kuongezeka kwa mahitaji katika masoko ya ndani na nje pamoja na nguvu kazi hususan vijana na wanawake waliohamasika kushiriki kwenye kilimo cha mazao haya. Mauzo ya mazao ya bustani kwa mwaka 2017/2018 yalifikia Dola za Marekani Milioni 779 sawa na ongezeko la asilimia 89 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 412 kwa mwaka 2015/16. Pia, tasnia ya mazao ya bustani ilichangia asilimia 38 ya fedha za kigeni zinazotokana na sekta ya kilimo.

Zao la parachichi ni miongoni mwa mazao ya bustani yanayochipukia na limeonyesha mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka minne ambapo, uzalishaji umeongezeka kutoka tani 20,000 mwaka 2015 hadi kufikia tani 190,000 mwaka 2018. Kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa zao hili, mauzo ya parachichi nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 3,279 mwaka 2015 hadi tani 9,000 mwaka 2018. Mauzo hayo yenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 8.5 yamefanyika katika soko la ulaya katika nchi za Ufaransa, Uholanzi na Uingereza.

## 8. MAZAO YA MBEGU ZA MAFUTA

Katika kipindi cha miaka ya 1960 mahitaji ya mafuta ya kula hayakuwa makubwa kama ilivyo katika kipindi cha miaka ya 2000 ambapo mahitaji yameongezeka kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mafuta hayo. Ongezeko hilo lilitokana na ongezeko la idadi ya watu na mahitaji ya mafuta ghafi kwa ajili ya viwanda. Kutokana na ongezeko la mahitaji ya mafuta ya kula, Wizara imeendelea kufanya jitihada mbalimbali za kuimarisha uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta kwa lengo la kuhakikisha nchi inajitosheleza kwa mafuta ya kula. Mazao ya mafuta ni pamoja na alizeti, chikichi, karanga, ufuta, na soya. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita uzalishaji umefikia wastani wa tani 1,149,476 kwa mwaka.

## 9. MAZAO YA CHAKULA

Hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula hapa nchini imeendelea kuwa ya kuridhisha ambapo kwa kipindi cha zaidi ya miaka saba (7) mfululizo kuanzia mwaka 2013/2014 hadi 2020/2021 nchi imekuwa inajitosheleza kwa kati kiwango cha utoshelevu (Self Sufficiency Ratio-SSR) kati ya asilimia 118 hadi 126. Uzalishaji wa Mazao ya Chakula Msimu wa 2020/2021 na Upatikanaji wa Chakula kwa Mwaka 2021/2022 imeonesha kuwa, hali ya uzalishaji wa chakula inatarajiwa kufikia kiasi cha tani 18,425,250 kwa mlinganisho wa nafaka (Grain Equivalent). Kwa msimu wa uzalishaji wa 2020/2021, uzalishaji wa mazao ya nafaka unatarajiwa kufikia tani 10,639,990. Katika kipindi cha miaka 25 baada ya Uhuru hali ya uzalishaji ilikuwa mbaya hasa miaka ya 90 ambapo nchi ilikuwa haijitoshelezi kwa chakula. Kutokana na mikakati mbalimbali iliyofanywa na Wizara ya Kilimo hali imeendelea kuimarika hadi kutoka upungufu wa chakula hadi kufikia uzalishaji wa utoshelevu na ziada.

### 9.1 Utoshelevu wa Chakula

Wizara ya Kilimo ina jukumu la kuhakikisha usalama wa chakula na lishe nchini. Katika kutimiza jukumu hilo, kwa kipindi cha miaka 60 ya Uhuru Wizara imefanikiwa kuhakikisha hali ya usalama wa chakula na lishe nchini umetengamaa kwa kuongeza uzalishaji, kuboresha hali ya lishe kwa kuzalisha mazao yenye virutubishi mbalimbali kama zinki, vitamin A na kupunguza upotevu wa mazao.

Pamoja na kujihakikishia usalama wa chakula na lishe kuna changamoto mbalimbali ambazo Wizara inaendelea kuzifanyia kazi ili kuondokana kabisa na upungufu wa chakula na lishe mbaya hapa nchini. Aidha, upungufu hujitokeza hapa na pale katika baadhi ya Halmashauri za mikoa ambapo NFRA na sekta binafsi husambaza mahindi kutoka mikoa yenye ziada kwenda kwenye mikoa yenye upungufu na hivyo kuwezesha wananchi kupata mahitaji ya chakula kwa bei ya kuridhisha.

### 9.2. Ujenzi wa Miundombinu ya Hifadhi ya Nafaka

Pamoja na ongezeko la uzalishaji wa mazao nchini Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa kuhifadhi chakula kupitia ujenzi wa ghala mpya, ukarabati na kuhamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu. Uwezo wa kuhifadhi chakula ni tani 501,000. Wizara inaendelea na ujenzi wa vihenge vya kisasa nane (8) vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 190,000 MT na ghala mpya tano (5) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000. Hadi sasa ujenzi huo umefikia asilimia 82.7 kwenye mikoa ya Manyara, Dodoma, Songwe, Njombe, Shinyanga, Ruvuma, Rukwa na Katavi. Ghala nne (4) zenye uwezo wa tani 63,500 pia zimekarabatiwa kwenye mikoa ya Arusha, Songwe, Rukwa na Dodoma.

Wizara kupitia Mradi wa Kudhibiti sumukuvu nchini inajenga ghala 14 zenye uwezo wa tani 21,500 ambapo ghala kumi na mbili (12) zinajengwa Tanzania Bara na mbili (2) Tanzania Visiwani. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia mpya za uhifadhi wa mazao hususan teknolojia zisizoruhusu hewa ili kupunguza upotevu wa chakula nchini.

## 10. HALIYALISHENCHINI

Wizara ya kilimo kwa kushrikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara za Kisekta na Wadau wa Maendeleo, imeendelea na juhudi za kuhakikisha hali ya utapiamlo nchini inapungua kupitia mikakati na

programu za kitaifa zinazoratibiwa na Mpango Jumuishi wa Masuala ya Lishe wa kitaifa wa kupunguza utapiamlo nchini (NMNAP 2016/2021). Kutokana na mkakati wa uzalishaji wa vyakula vilivyoongezewa virutubishi, hali ya utapiamlo nchini imepungua kutoka asilimia 34.7 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 31.8 mwaka 2018. Wizara inaendelea kutoa elimu ya ulaji wa vyakula mchanganyiko ili hali ya lishe nchini iwe bora zaidi.

**11. MASOKOYAMAZAOYAKILIMO**

Katika kipindi cha 1950 hadi 1966 Bodi za mazao ya kilimo zilihusika katika kushughulikia masoko ya mazao asilia ya biashara kwa kuuza ndani na nje ya nchi. Hadi mwaka 1966, uchumi wa Tanzania ulikuwa huria ambapo Serikali ilitekeleza Sera na miongozo ya Benki ya Dunia inayohusu maendeleo ya kilimo kama sehemu ya Mpango wake wa kwanza wa Miaka Mitano. Wakati wa uchumi hodhi, 1967 hadi 1985 hatua mbalimbali za maboresho zilitokea ikiwemo kuanzishwa kwa Azimio la Arusha. Bodi za kutafuta masoko ya mazao ya kilimo zilianzishwa na zilikuwa na jukumu la kutafuta masoko na kupanga bei. Baadhi ya bodi hizo za masoko ni Bodi ya Masoko ya Pamba, Bodi ya Masoko ya Kahawa na Bodi ya Masoko ya Korosho. Katika kipindi hicho, mashirika mbalimbali ya Umma yalianzishwa NMC (1968), GAPEX (1972) na Kampuni za biashara za mikoa (RTC) ambazo zilihusika na masoko ya ndani.

Katikati ya miaka 1980 na 1990 kulikuwa na Programu za Magezi ya Kimfumo (SAPs) ambapo Tanzania ilihama kutoka kwenye mifumo wa masoko inayosimamiwa na Mamlaka za mazao na ushirika kwenda kwenye mfumo wa masoko huria ambapo wafanyabiashara na vyama vya ushirika walishindana. Sekta binafsi waliruhusiwa kununua mazao kwenye vyama vya ushirika na wakulima na utaratibu wa upangaji wa bei ulisitishwa na kuwepo bei rejea ya masoko ya nje na baadae bei ya soko.

Miaka ya 1990 hadi 2000, Bodi za mazao ziliacha kujihusisha na masoko ya mazao ya mazao ya kilimo na kubaki na jukumu la udhibiti na muhamasishaji wa tasnia husika. Kuanzia 2000 hadi 2021, Serikali zililazinisha majukumu kazi na upatikanaji wa fedha za kugharamia Bodi za Kilimo na kuamua kuwa wakulima wasitozwe kodi kwa ajili ya mifuko ya kuendeleza mazao, Bodi zigharamiwe kwa asilimia mia moja na Serikali. Kufuatia kufutwa kwa kodi na tozo za kuendeleza mazao, mwaka 2009 Sheria za tasnia ya Mazao zilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Marekebisho Madogo Na.20 ya Mwaka 2009. Aidha, utekelezaji wa Sheria hiyo bado unaendelea hadi sasa.

Katika kuhakikisha mazao ya kilimo yanapata soko ndani na nje ya nchi, Wizara imeanzisha Sehemu ya masoko inayosimamia utafutaji wa masoko, kufanya tafiti za masoko na bei za mazao pamoja na kufuatilia mifumo ya uuzaji wa mazao. Kupitia sehemu hiyo kwa kushirikiana na Wizara za kisekta pamoja na sekta binafsi, Serikali imeingia makubaliano na nchi mbalimbali ili kuuza bidhaa za mazao ya kilimo katika nchi hizo. Baadhi ya nchi hizo ni pamoja na China (muhogo na Soya), Misri (mahindi ya njano), Afrika ya Kusini (Parachichi) na Kenya (Mahindi)

Aidha, Tanzania imenufaika na masoko ya nje yenye masharti nafuu ambayo hayana ukomo wa bidhaa wala ushuru wa forodha (Duty Free Quota Free - DFQF) ili kuuza mazao ya kilimo.

Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Sekta binafsi imeimarisha matumizi ya mifumo ya masoko ikiwemo soko la bidhaa (TMX), stakabadhi za ghala, minada na kilimo cha mkataba.

Mazao yanayouzwa kwa mfumo wa minada ni korosho, kahawa na ufuta; mfumo wa stakabadhi za ghala kwa mazao ya korosho na mbaazi; mfumo wa soko la moja kwa moja kwa mazao ya kahawa na kakao; mfumo wa soko la bidhaa (TMX) kwa mazao ya kahawa na ufuta; mfumo wa ununuzi wa moja kwa moja kwa mazao ya mahindi na mpunga; na mfumo wa kilimo cha mkataba kwa mazao ya tumbaku, alizeti, pamba na kahawa. Matokeo ya mifumo hiyo ni pamoja na kuwezesha na kusimamia vyama 16 vya ushirika vya wabanguaji wadogo wa korosho kutumia mfumo wa Stakabadhi za Ghala na kuuza zaidi ya tani 200,000 kwa mwaka kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 katika nchi za India, China na Vietnam.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni matumizi ya mifumo hiyo kusaidia kuimarika kwa bei ya mazao ya kilimo, kwa mfano bei ya zao la ufuta imeongezeka kutoka Shilingi 1,500 kwa kilo mwaka 2015/2016 hadi kufikia Shilingi 3,500 kwa kilo mwaka 2019/2020; bei ya kakao kutoka Shilingi 3,200 mwaka 2015/2016 kwa kilo hadi Shilingi 5,000 kwa kilo mwaka 2019/2020; bei ya zao la korosho imeimarika kutoka wastani wa Shilingi 1,820 mwaka 2015/16 kwa kilo hadi kufikia wastani wa Shilingi 3,000 kwa kilo mwaka 2019/20; na bei ya singa za mkonge imeongezeka kutoka Shilingi 2,083 kwa kilo mwaka 2015/16 hadi Shilingi 2,745 kwa kilo mwaka 2018/19 kwa mauzo ya ndani ya nchi. Aidha, bei ya kahawa aina ya Arabika katika soko la ndani imeimarika zaidi kwa kuuzwa kwa Dola za Marekani 112 ikilinganishwa na bei ya Dola za Marekani 107.04 katika soko la Dunia kwa gunia la kilo 50 na bei ya kahawa aina ya Robusta iliimarika kwa kuuzwa kwa Dola za Marekani 87.13 katika soko la ndani ikilinganishwa na Dola za Marekani 73.90 katika soko la Dunia kwa gunia la kilo 50.

Kuimarisha mfumo wa soko kwa kuwaunganisha wakulima na wanunuzi wa ngano, ambapo bei ya ngano imeongezeka kutoka Shilingi 650 mwaka 2019/2020 hadi Shilingi 1,000 kwa kilo mwaka 2020/2021; Vilevile, bei ya soya imeongezeka kutoka Shilingi 1,500 msimu wa 2019/2020 hadi Shilingi 2,200 msimu wa 2021/2022; Wizara imetoa vibali kwa wafanyabiashara wa zao la soya kusafirisha Soya nje ya nchi na kusaidia kuongeza

kiwango cha mauzo nje na Pato la Taifa; Aidha, Wizara imeafanikiwa kuvutia

wafanyabiashara wa mazao ya bustani ikiwemo ndizi kwa ajili ya soko la Kenya, parachichi kwa ajili ya soko la india na mazao ya viungo katika soko la nchi za Jumuiya ya Ulaya.

**12. MAENDELEO YA KILIMO CHA UMWAGILIAJI**

Kabla ya Uhuru, Serikali ya kikoloni ilianzisha shamba la umwagiliaji kwa kilimo cha mpunga huko Kilangali, mkoani Morogoro likiwa na ukubwa wa hekta 1,000. Hadi mwaka 1970 hekta 2,600 zilikuwa zimeendelezwa ambazo ni asilimia 26 ya malengo ya miaka 10 ya kuendeleza hekta 10,000. Skimu za umwagiliaji zilizojengwa ni zile zilizokuwa na maeneo ya ukubwa wa hekta 200 hadi 2,000; kwa lengo la kufikia hekta 150,000 ifikapo mwaka 1985. Katika kusimamia utekelezaji wa kazi hiyo, mwaka 1981 Wizara iliunda kanda sita za umwagiliaji na Kanda ya saba iliundwa mwaka 2003/04 ili kufikisha huduma kwa wananchi wengi zaidi katika wilaya. Kanda hizo ni Mbeya (Mbeya, Iringa na Rukwa); Kilimanjaro (Kilimanjaro, Arusha na Tanga); Mwanza (Mwanza, Mara, Kagera na Shinyanga); Tabora (Tabora, Kigoma); Mtwara (Mtwara, Lindi na Ruvuma); Morogoro (Morogoro, Pwani na Dar es Salaam); na Kanda ya Kati inayojumuisha mikoa ya Dodoma, Manyara na Singida. Mwaka 2001/2002, eneo la skimu za umwagiliaji ambalo miundombinu iliendelezwa lilikuwa hekta 191,900. Eneo hilo liliongezeka hadi hekta 331,490 mwaka 2010/2011.

Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 461,326 mwaka 2015/2016 hadi hekta 695,045 mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 50.7. Ongezeko hilo limechangiwa na kukamilika kwa miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa uboreshaji miundomibinu ya Skimu ya umwagiliaji ya Dakawa yenye ukubwa hekta 2,000; skimu 8 kati ya Skimu 16 zenye ukubwa wa hekta 2,547 za Mradi wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo (SSIDP); ukarabati wa miradi 4 ya skimu za umwagiliaji zenye jumla ya ukubwa wa hekta 2,000; na kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa mawili ya Itagata iliyopo Itigi (Singida) na Dongobesh (Mbulu).

Kilimo cha umwagiliaji kimesaidia kuongezeka kwa tija ya uzalishaji katika skimu mbalimbali za umwagiliaji zilizoendelezwa ambapo zao la mpunga tija imeongezeka kutoka wastani wa tani 1.8 – 2.0 kwa hekta mwaka 2015/2016 hadi wastani wa tani 4.0 – 5.0 kwa hekta mwaka 2018/2019; zao la mahindi kutoka wastani wa tani 1.5 kwa hekta mwaka 2015/2016 hadi tani 3.7 - 5.0 kwa hekta mwaka 2018/2019; zao la vitunguu kutoka wastani wa tani 13 kwa hekta mwaka 2015/2016 hadi 26 kwa hekta mwaka 2018/2019; na zao la nyanya kutoka wastani wa tani 5 kwa hekta mwaka 2015/2016 hadi tani 18 kwa hekta mwaka 2018/2019.

**13. MAENDELEOYAUSHIRIKA**

Kabla na baada ya uhuru hasa katika mazao ya kahawa na pamba na baadaye katika mazao mengine kama tumbaku, korosho na chai ulikuwa tayari ni imara na wenye nguvu. Nguvu hiyo ilikuwa siyo tu katika uuzaji wa mazao ya wakulima pekee bali katika kuwapatia pembejeo na mikopo. Aidha, baadhi ya vyama vikuu ya ushirika vilianzisha miradi mikubwa ya elimu kwa kumiliki shule za sekondari na vingine vilitoa ufadhili wa elimu ya juu kwa watoto wa wanachama. Katika kujiimarisha kimtaji, vyama vya ushirika vilimiliki ardhi, majengo, mitambo na viliunda benki (National Cooperative Bank). Hata hivyo baada ya uhuru, ushirika ulikumbwa na changamoto za kimuundo na kiuendeshaji zilizosababisha Serikali kuunda kamati mbalimbali ili kutatua changamoto hizo. Kamati hizo ni Kamati ya Mhaville mwaka 1966; Kamati ya Massomo mwaka 1975; Kamati ya Ngwilulupi mwaka 1981; Tume ya Nyirabu ya mwaka 1990 na Kamati ya Kahama ya mwaka 2000.

Changamoto zilizobainishwa na Kamati ya Kahama ya mwaka 2000 ni pamoja na Ushirika usiokidhi mahitaji ya wanachama, ukosefu wa mitaji, uongozi mbovu na ubadhilifu, miundo duni ya ushirika, udhaifu wa taasisi za Serikali zinazohusika na ushirika, elimu duni ya ushirika, ushirika kutoenea katika sekta mbalimbali za kiuchumi na ushirika kutokupewa kipaumbele na Serikali. Kutokana na changamoto hizo za ushirika, Serikali iliandaa Mkakati wa Kuleta Mageuzi katika Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika ambao uluhusisha masuala yafuatayo;-

Kuundwa kwa Wizara ya Ushirika na Masoko; Kusimamia Marekebisho ya Sera ya Ushirika ya Mwaka 1997 na kuandaa Sera Mpya ya Ushirika ya Mwaka 2002; Kusimamia kutungwa kwa Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2003; Kusimamia Uimarishwaji wa Taasisi zinazosimamia maendeleo ya Ushirika ikiwa ni COASCO na kukiinua Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu. Aidha, Serikali ilibuni na kusimamia utekelezaji ya Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenazesheni ya Ushirika (CRMP) ya Mwaka 2005.

Utekelezaji wa CRMP ulikuwa na malengo ya kuleta mageuzi katika maendeleo ya ushirika nchini. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006 hadi mwaka 2009/2010 ufufuaji wa vyama vya ushirika vilivyokuwa vimeshindwa kuwahudumia wanachama kwa kuviwezesha kufanya biashara kwa kujitegemea ulianza. Mwaka 2007/2008, ufufuaji uliviwezesha vyama vya ushirika kununua mazao ya korosho kutoka kwa wakulima kwa bei nzuri. Aidha, ubora wa mazao ya wakulima yaliyouzwa kupitia vyama hivyo uliongezeka na hivyo kuvutia wanunuzi na kuongeza ushindani. Kati ya mwaka 2005 na 2010, kupitia Programu hiyo uratibu uliendelea kuimarishwa ikiwa ni pamoja na kusimamia chaguzi za viongozi wa vyama vya ushirika vya msingi, vyama vikuu, kilele na shirikisho.

Katika kipindi cha 2011 na 2021, Wizara imeendelea kuhamasisha ushiriki wa wananchi kwenye Vyama vya Ushirika kwa kutoa

elimu ya ushirika kwa umma na Vyama vya Ushirika. Mafanikio ya jitihada hizo ni pamoja na: kuongezeka kwa wanachama wa vyama vya ushirika kutoka milioni 2.4 mwaka 2015 hadi milioni 5.9 Mwaka 2020 sawa na asilimia 146 ya ongezeko la wanachama; Kuongezeka kwa idadi ya wanachama na wananchi wanaonufaika na huduma za kifedha kupitia Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOs). Idadi ya wananchi waliojiunga na kunufaika na huduma za SACCOs imeongezeka kutoka 676,202 mwaka 2015 hadi 2,447,332 mwaka 2020.

Mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa mikopo iliyotolewa na SACCOs kwa wanachama wake kutoka Shilingi bilioni 854.3 mwaka 2015 hadi Shilingi trilioni 1.5 mwaka 2020 na mitaji ya SACCOs kupitia akiba, amana na hisa Shilingi bilioni 428.8 mwaka 2015 na kufikia Shilingi bilioni 819.0 mwaka 2020; Kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zinazozalishwa na wanaushirika kutokana na kuhamasisha na kuhimiza Vyama vya Ushirika kuanzisha na kufufua viwanda. Jumla ya viwanda 75 vya kuchakata mafuta ya alizeti na chikichi, kutengeneza samani za majumbani, kuchakata pamba na mazao ya nafaka vimeanzishwa na kufufuliwa katika maeneo mbalimbali ya nchi. Idadi hiyo inafanya viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika vinavyofanya kazi kufikia viwanda 117 kwa mwaka 2020; na Kurejeshwa kwa mali za Vyama vya Ushirika zilizokuwa zimeuzwa kiholela na nyingine kuporwa zikiwemo nyumba za makazi, maghala, viwanda na viwanja. Mali zilizorejeshwa zilitoka katika Chama Kikuu cha Ushirika NCU (1984) Ltd (Mwanza), Chama Kikuu cha Ushirika SHIRECU Ltd (Shinyanga), Chama kikuu cha Ushirika KNC (1984) Ltd (Kilimanjaro) na Chama Kikuu cha Ushirika KCU (1990) Ltd (Kagera).

Vilevile, Vyama vya Ushirika wa mazao ya kakao na kahawa vimeunganishwa katika mfumo wa soko la moja kwa moja (direct export) na nchi za Uswizi, Afrika kusini, Japani na Uholanzi na kuuza mazao kwa bei shindani. Katika mwaka 2018/19 mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na gunia la kahawa la kilo 60 kuuzwa wastani wa Dola za Marekani 160.63 ikilinganishwa na bei ya mnada ya Dola za Marekani 84.97, na kilo moja ya kakao kuuzwa kwa bei ya juu ya Shilingi 5,011 ikilinganishwa na bei ya Shilingi 3,200 ya msimu wa 2017/18. Pia, Vyama vya Ushirika vya mazao ya pamba vimeunganishwa na taasisi za fedha ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) na taasisi nyingine ili kuviwezesha kupata zana za kilimo ikiwemo matrekta. Hadi kufikia 2019 Vyama vya Ushirika (AMCOS) 32 vilikopeshwa matrekta yenye jumla ya thamani ya Shilingi bilioni 1.5.

## 14. MAZINGIRAYAUWEKEZAJIKATIKASEKTAYAKILIMO

Tangu mwaka 1961, Wizara imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya kilimo kwa kuandaa na kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Mikakati na programu mbalimbali katika sekta ya kilimo. Aidha kwa sasa, Wizara ya kilimo inatekeleza mikakati mbalimbali na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) ambayo imezingatia Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013 inayokidhi mahitaji ya kuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji katika sekta ya kilimo. Kwa mfano: Katika kipindi cha mwaka 2015/16 hadi 2019/20, Serikali imefuta ushuru, tozo na ada 105 na kupunguza nne (4) kati ya 146 zilizokuwa zinatozwa katika mazao ya kilimo, pembejeo za kilimo na ushirika ambazo zimesaidia kumuondolea mkulima kero, kupunguza gharama za uzalishaji na kuchochea uzalishaji na uwekezaji katika kilimo. Hatua hiyo imevutia Sekta binafsi kuwekeza takribani Shilingi Trilioni 3.7 kwenye mnyororo wa thamani wa kuendeleza mazao ya chai, kahawa, mkonge, ngano, shayiri na mpunga. Uwekezaji huo umezalisha ajira 41,798.

**Baadhi ya uwekezaji huo ni kama ifuatavyo:**

(i) Kuanzishwa kwa viwanda tisa (9) vyenye uwezo wa kubangua tani 25,000 za korosho kwa mwaka vimeanzishwa katika mikoa ya Mtwara (6), Dar es Salaam (1) na Pwani (2). Idadi hiyo imefanya viwanda vya kubangua korosho kuongezeka kutoka viwanda 21 hadi 30 na mikoa inayolima korosho imeongezeka kutoka mikoa 5 hadi 20;

(ii) Kuanzishwa kwa viwanda vitatu (3) vya chai kikiwemo kiwanda cha chai cha Kabambe Tea Factory (Unilever) cha mkoani Njombe chenye uwezo wa kusindika majani mabichi ya chai tani 50 kwa siku. Kiwanda hicho kimewekeza mtaji wa Shilingi Bilioni 17.8 na kinaajiri watu 250 hadi 300 kwa siku. Vingine viwili ni pamoja na Tropical Treasres Limited kilichopo Kilimanjaro chenye uwezo wa kusindika kilo 1,000 za majani mabichi kwa siku na Chai Collection Tanzania Limited kinachochanganya na kufunga chai kwenye vikasha kwa ajili ya Hotel kubwa na kuajiri watu 15 hadi 20 kwa siku;

(iii) Viwanda 11 vya mkonge, vyenye uwezo wa kuchakata mkonge tani 7,193 kwa mwaka na viwanda vidogo 70 vyenye uwezo wa kuchakata mkonge tani 7,343.2 kwa mwaka vimeanzishwa na kuzalisha jumla ya ajira 37,907; Uwekezaji wa takribani Shilingi bilioni 160.8 katika uzalishaji na uendelezaji wa viwanda vya kahawa; na Kuanzishwa kwa kiwanda cha Murzah Wilmar Rice Millers cha kukoboa mpunga eneo la Kihonda Morogoro chenye uwezo wa kukoboa tani 600 kwa siku;

(iv) Kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye bia zinazotengenezwa kwa kutumia shayiri iliyozalishwa hapa nchini kutoka Shilingi 760 hadi Shilingi 620 kwa lita na kuanzisha kiwanda cha kimea ili kuchochea uwekezaji wa kilimo cha shayiri hapa nchini; na

(v) Kuridhiwa kwa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary-SPS Measures) kutaharakisha maendeleo katika Sekta ya Kilimo.

## 15. USHIRIKIWAVIJANAKATIKAKILIMO

Wizara imendelea na jitihada za kuhakikisha vijana wanashiriki katika kilimo kwa kuwawekea mazingira rafiki. Katika kufanikisha hilo, Wizara iliandaa Mkakati wa Taifa wa Kuwashirikisha Vijana kwenye Kilimo ambao unazingatia masuala mbalimbali ya kumshawishi kijana kujihusisha na mnyororo wa thamani wa kilimo ikiwemo upatikanaji wa ardhi, rasilimali fedha, uongezaji wa thamani, upatikanaji wa pembejeo, zana bora za kilimo, kuweka Miundombinu bora ya Matumizi ya kilimo cha Umwagilia

ji, kuboresha na kuwa na Masoko ya uhakika, kuzingatia mabadiliko ya Tabianchi, kuhamasisha vijana na kuwajengea ujuzi na mbinu za ujasiriamali. Tangu Mkakati huo uanzishwe takribani miaka mitano (5) iliyopita, Wizara ya Kilimo imeshuhudia wadau mbalimbali wakiwezesha vijana kushiriki katika kilimo kwa kuzingatia malengo ya mkakati huo. Vilevile, vijana wengi wameendelea kuvutiwa kuingia katika shughuli za kilimo kwa lengo la kujipatia ajira na pale wanapofanikiwa basi kuajiri vijana wenzao.
Wizara kwa kushirikiana na Sekta binafsi imetekeleza miradi mbalimbali ya vijana katika kilimo ikiwemo:

**15.1. Mradi wa Farmer to Farmer (IESC F2F) Tanzania kuanzia Oktoba 2018- Februari 2020**
Mpaka sasa mradi umefanikiwa kuleta nchini wataalamu 12 na kufanikiwa kuwafikia jumla ya vijana 3000 wanaofanya kazi za kilimo katika mikoa mbalimbali ya Tanzania ikiwemo Pwani, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Iringa, Njombe, Mbeya, Mwanza, Kagera, na Karagwe na Zanzibar na kutumia jumla ya Shilingi milioni mia moja hamsini na moja laki mbili na therathini elfu(151,230,000). Vilevile mradi umeweza kuwafikia zaidi ya wadau (Host Organizations) 20 ambao kati ya hao 6 ni taasisi za kifedha (Benki na SACCOS), wakulima, SMEs, wafanyabiashara (exporters) wa mazao ya kilimo, wasindikaji na NGOs zinazoshughulika na vijana katika kilimo.

**15.2 Mradi wa Programu Jumuishi wa Vijana katika Afrika Mashariki (EAYIP)**
Mradi wa Programu Jumuishi wa Vijana katika Ukanda wa Afrika Mashariki (The East Africa Youth Inclusion Program -EAYIP) ni mradi wa miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2021. Programu hii inatekelezwa na Shirika la Heifer International katika mikoa ya Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa ambayo imewafikia vijana elfu 10,300 kati yao wanawake ni 4,120 na 6,180 wanaume wenye umri kati ya miaka 15- 24 kwa kuzingatia masuala ya jinsia na mnyororo wa thamani nchini Tanzania.

**15.3 Mradi wa Kilimo na Masoko wa Vijana chini ya FAO**
Mradi unatekelezwa katika mikoa ya Singida, Dodoma, Morogoro na Pwani. Mradi huo umekuwa ukilenga kilimo cha umwagiliaji ili Vijana waweze kuwa na uhakika wa shughuli za kilimo na kuwapatia vifaa vya umwagiliaji kama mashine (Irrigation Pumpus). Mradi umefanikiwa kuwafikia vijana 2,080 na kupatiwa ujuzi na maarifa katika sekta ya kilimo.

**15.4 Miradi inayotekelezwa na Ushirika wa SUGECO**
Mradi huu unakuza na kuongeza ujuzi wa kilimo kwa vijana tangu mwaka 2015 kwa kufundisha Vijana waliohitimu vyuo vikuu katika kambi za Morogoro na Mkongo wilayani Rufiji katika mkoa wa Pwani. Mradi umefanikiwa kuwafikia vijana 1,000 kwa kuwapatia mafunzo ya kilimo. Kati ya hao, vijana 225 wamepata mafunzo nchini Israel na vijana 87 Marekani.

**15.5 Mkopo wa Halmashauri wa Asilimia 10 kwa Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu**
Serikali ilielekeza halmashauri zote nchini kutenga asilimia 10 ya bajeti kwa ajili ya Vijana, wanawake na Wenye Ulemavu katika maeneo yao na utaratibu huo umekuwa ukifanyika katika halmashauri zilizo nyingi, ambapo asilimia 4 ni kwa Vijana, asilimia 4 kwa Wanawake na asilimia 2 ni kwa wenye Ulemavu.

**15.6 Mradi wa Vitalu Nyumba kwa Vijana**
Mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa lengo la kukuza ujuzi kwa vijana ili waweze kujiajiri na kuajiri vijana wenzao. Katika kutekeleza azima hiyo, Serikali imeamua kutoa mafunzo ya stadi za kazi kwa vijana katika kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba (Greenhouse technology). Kwa msingi huo katka mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imejenga vitalu nyumba 84 katika halmashauri 81 za mikoa 12 kwa ajili ya kutolea mafunzo ya kilimo ambapo vijana 8,700 wamepewa mafunzo hayo.

**15.7 Mpango wa Serikali kwa Halmashauri kutenga Ardhi kwa ajili ya vijana**
Katika kuhakikisha upatikanaji wa ardhi ya kilimo kwa vijana, Serikali kupitia Halmashauri inatakiwa kutenga ardhi ya kilimo kwa ajili ya Vijana ambapo hadi kufika mwaka 2020 zaidi ya Hekta 217,882.36 zimetengwa katika Halmashauri 48 kati ya Halmashauri 184 nchini. Halmashauri zinaendelea kuhimizwa kuendelea kutenga ardhi kwa ajili ya ushiriki wa vijana kwenye kilimo.

## 16. CHANGAMOTO NA UTATUZI KATIKA SEKTA YA KILIMO
Pamoja na jitihada kubwa za Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo, kilimo bado kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo hazinabudi kupangiwa mikakati mipya ya kufanikisha azma ya kuwa na nchi ya uchumi wa viwanda.

## 17. MWELEKEOWAMAENDELEOYAKILIMOBAADAYAMIAKA60YA UHURU
Katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania bara, Wizara ya Kilimo imejipanga kuendelea kutekeleza majukumu yake kupitia mipango na mikakati iliyopo na inayotarajiwa kubuniwa ili sekta ya kilimo iweze kutoa mchango unaotarajiwa katika harakati za kufikia malengo ya Maendeleo ya Endelevu 2030, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (FYDP-III 2021-2025). Katika kutekeleza malengo hayo, Wizara inaendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP-II 2017-2028). Mwelekeo wa kilimo katika miaka 60 ijayo ni kuhakikisha kuwa kilimo kinakuwa cha kisasa, tija, na cha kibiashara ili kuongeza kipato cha wakulima wadogo na wakati kwa ajili ya kuboresha maisha yao, kuongeza uhakika wa usalama na lishe na pia kuchangia kwenye Pato la Taifa. Hivyo, katika miaka 60 ijayo (2021-2081) Wizara itaendelea kutekeleza maeneo yafuatayo ya

kimkakati:-
7.1 Kuongeza Uzalishaji na Tija ya mazao
Mazao ya kipaumbele yatakayopewa msukumo ni pamoja na mazao ya chakula, biashara, bustani na mafuta. Kilimo cha umwagiliaji kitapewa kipaumbele ili Taifa liendelee kujitosheleza kwa Chakula na ziada ya kuuza katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Wakulima katika skimu za umwagiliaji watawezeshwa kupata mbolea, mbegu bora, huduma za ugani, zana bora za kilimo, matumizi ya teknolojia na elimu kuhusu matumizi bora ya ardhi na maji. Kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) na Sekta binafsi, Aidha, TOSCI itaendelea kujengewa uwezo ili kusimamia udhibiti wa mbegu bora. Mambo mengine yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa mkakati huu ni pamoja:-

**17.2 Kuimarishwa Upatikanaji wa Masoko ya Bidhaa za Kilimo**
Upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo utaimarishwa kwa kuboresha huduma za kukagua viwango vya viuatilifu kwenye mazao na bidhaa za kilimo kwa kujenga uwezo wa TPHPA ili iweze kutoa vyeti vya usafi wa mazao na bidhaa za kilimo vinavyotambulika kitaifa (Accredited Laboratories). Ujenzi wa miundombinu ya masoko ya mipakani (Strategic Boarder Markets) utafanyika kwa ajili ya maghala ya kuhifadhia mazao ya wakulima. Maghala hayo yatatumika kwa ajili ya stakabadhi ghalani na baadaye kuanzisha Mfumo wa Soko la Bidhaa (Commodity Exchange). Mambo mengine yatakayotekelezwa ni kutoa elimu ya ujasiriamali kuhusu namna ya kuendesha biashara ya kilimo cha mazao:-

i. Kuimarisha Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (Ward Agricultural Resources Centre) ili vitumike katika kutoa mafunzo kwa wakulima;
ii. Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuunganisha nguvu za kukabiliana na mashindano katika biashara ya kuuza mazao ya kilimo nje ya nchi;
iii. Kuimarisha usimamizi wa ubora wa mazao kupitia bodi za mazao na vituo vya mipakani vya ukaguzi wa mazao na mimea na kujenga maabara ya kupima kiwango cha sumu kilichomo kwenye pareto ya wakulima kupitia Bodi ya Pareto; na
iv. Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) utaongezewa uwezo wa kununua na kuhifadhi mazao na pia kuiwezesha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kununua mazao hayo.

**17.3 Kuongeza Thamani ya Mazao ya Kilimo**
Wizara itaendelea kuhamasisha uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo kwa ajili ya kupata bei nzuri na soko la uhakika. Katika kutekeleza hilo, Wizara itawawezesha wajasiriamali wa mazao ya kilimo kama vile wasindikaji wa mazao, kuboresha na kusambaza teknolojia za kuhifadhi mazao ya kilimo. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha taasisi za fedha na sekta binafsi kutoa mikopo kwa ajili ya vifaa vya kisasa vya usindikaji wa mazao ya kilimo.

**17.4 Kuendelea Kuboresha Uwezo wa Wizara kutoa Huduma**
Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara katika ngazi zote kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali. Aidha, Wizara itakarabati na kujenga vituo vya utafiti na vyuo vya mafunzo ya kilimo na kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa watumishi.

**17.5 Kuimarisha Sera, Mikakati na Usimamizi katika Sekta ya Kilimo**
Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati, Programu na Miongozo kwa kuzingatia mahitaji ya sekta ya kilimo na kupitia upya sheria za kilimo ili ziendane na matamko ya Sera ya Taifa ya Kilimo. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya kilimo kwa kufanya marekebisho kwa kuondoa ama kupunguza ada, tozo na kodi. Wizara pia, itaimarisha uratibu ikiwa ni pamoja na kuoanisha nguvu na rasilimali zilizopo, kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ili ijumuishe mipango na programu hizo, na kuboresha mfumo wa ukusanyaji takwimu na kuanzisha benki ya takwimu (data bank) itakayokuwa na taarifa za miradi na programu.

**17.6 Kuzingatia Masuala Mtambuka katika Kilimo**
Wizara itaendelea kuzingatia masuala mtambuka kama vile UKIMWI na VVU, mazingira, jinsia, lishe, na ushiriki wa vijana katika sekta ya kilimo katika utekelezaji wa shughuli za kilimo.

**17.7 Kuimarisha Ushirika katika sekta ya kilimo**
Wizara kupitia Tume ya Ushirika itaendelea kuimarisha uongozi na usimamizi katika vyama vya ushirika na kuwezesha kuwepo kwa weledi na utaalam katika vyama vya ushirika kuhusiana na masoko na mnyororo wa kuongeza thamani. Aidha, masuala mengine yatakayozingatiwa ni pamoja na kuweka mazingira yatakayowezesha kukua kwa ushirikiano baina ya Vyama vya Ushirika hususan katika nyanja za uzalishaji, masoko, mitaji, teknolojia na habari, na kuviwezesha vyama vya ushirika kuimarisha biashara za mazao. Jitihada zingine ni kuimarisha SACCOS na mabenki ya ushirika ili yaweze kufikisha huduma zake kwa watu wenye kipato duni, vijana na walemavu sambamba na kuhamasisha vijana wanaoshiriki katika kilimo kuunda vyama vya ushirika.

**17.8 Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji, Uchambuzi, Uhifadhi na Usambazaji wa Takwimu na Taarifa za Kilimo**
Kwa kutambua umuhimu wa kuwa na takwimu sahihi katika kuendeleza kilimo, Wizara itaendelea na utekelezaji wa jukumu la kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza takwimu za kilimo. Wizara pia, itaendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia ya TEHAMA kama vile mfumo wa ARDS kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa za kilimo.




## MAFANIKIO YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KATIKA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

**UTANGULIZI**

Ndugu wanahabari pamoja na wananchi wote mnaofuatilia matangazo haya mubashara, ninawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuendelea kutupa uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo kupokea Taarifa ya Mafanikio katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Naomba niwashukuru kwa kuitikia wito na kufika hapa. Ni matumaini yangu kuwa kupitia Vyombo vya Habari mnavyoviwakilisha, hadhira ya Watanzania na dunia kwa ujumla itaweza kufahamu mafanikio katika Sekta ya Ulinzi wakati Taifa likiadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Ulinzi wa Taifa letu unaongozwa na Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara. Aidha, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Ulinzi wa Taifa (National Defence Act - NDA), Sera ya Mambo ya Nje, na miongozo ya Serikali kuhusu ulinzi. Kwa ujumla, hayo ndiyo mambo yanaweza kutumiwa kupima mafanikio ya Wizara, tangu nchi yetu ipate uhuru.

**HISTORIA YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Ndugu wanahabari, historia ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) inaanza mara tu baada ya kupata Uhuru wa Tanzania Bara mwaka 1961. Wakati huo, ilijulikana kwa jina la Wizara ya Mambo ya Nje na Ulinzi (Ministry of External Affairs and Defence), Waziri akiwa Hayati Oscar Salatiel Kambona. Mwaka 1964 ilibadilishwa jina na kuitwa Wizara ya Ulinzi, Jeshi la Kujenga Taifa na Vijana na kuhamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais, akiwa Hayati Rashid Mfaume Kawawa. Mabadiliko mengine yalifanyika mwaka 1972, ambapo Wizara iliondolewa Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais na kuwa Wizara inayojitegemea ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mwaka 1989 Wizara ilihamishiwa Ofisi ya Rais huku ikiendelea kuitwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na Mawaziri wake waliitwa Mawaziri wa Nchi. Mwaka 1995 Wizara ilihamishwa kutoka Ofisi ya Rais, na kuwa Wizara kamili ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa jina linaloendelea kutumika.

Hadi sasa Wizara hii imeongozwa na Mawaziri kumi na nane (18) ambao ni Mhe. Oscar Kambona (1962 - 1967), Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa (1967-1972 na 1977 - 1980), Mhe. Edward Moringe Sokoine (1972 - 1977), Jenerali Abdallah Twalipo (1980 - 1982), Brigedia Jenerali Muhidini Kimario (1982 - 1985), Mhe. Dkt. Salim Ahmed Salim (1985 - 1989), Jackson Makweta (1989 - 1990), Mhe. Amran Mayagila (1990 - 1991), Kanali Abdulrahman Kinana (1991 - 1995), Mhe. Edgar Maokola Majogo (1995 - 2000), Mhe. Profesa Philemon Sarungi (2000 - 2005), Mhe. Profesa Juma Kapuya (2006 - 2007), Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (2007 - 2012 na 2014 - 2020), Mhe. Shamsi Vuai Nahodha (2012 - 2014), Mhe. Elias John Kwandikwa (2021) na Dkt. Stergomena Lawrence Tax (2021 - hadi sasa).

**DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA**

Dira ya Wizara ni "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye amani na usalama" na Dhima yake ni "kulinda mamlaka, mipaka ya nchi, na maslahi ya Taifa kwa kutekeleza Sera ya Ulinzi wa Taifa katika kudumisha amani na usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".

Majukumu ya Wizara ni pamoja na: Kuliongezea uwezo wa kimedani Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia vifaa na zana bora pamoja na mafunzo na mazoezi, kuwapa Vijana wa kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na uwezo wa kujitegemea; kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia; kuendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Akiba katika mikoa yote; kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi na kiulinzi; na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa Umma wa Wizara.

**MUUNDO WA WIZARA**

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inajumuisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), na Mashirika (Tanzania Automotive Technology Centre – TATC (NYUMBU), Shirika la MZINGA, na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT).

**MAFANIKIO**

Tangu kupata Uhuru miaka 60 iliyopita, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi, na hivyo kuliwezesha Taifa kupata mafanikio mbalimbali ifuatavyo:

**Uanzishwaji wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania**

Sambamba na uanzishwaji wa Wizara, JWTZ pia limepitia hatua mbalimbali za mabadiliko. Mara baada ya uhuru wa Tanganyika tarehe 9 Desemba, 1961, Serikali mpya ya Kizalendo ilifuta Jeshi la Kikoloni lililojulikana kama King's African Rifles (KAR) na kuanzisha Jeshi jipya lililojulikana kwa jina la Tanganyika Rifles (TR) ambalo pia linajulikana kama Tanganyika Military Force (TMF). Kama ishara ya kuanzishwa rasmi kwa Jeshi Jipya, yalifanywa makubaliano ya kukabidhiana bendera ambapo jeshi la kikoloni la KAR, lilikabidhi bendera hiyo kwa Jeshi jipya la Tanganyika huru (Tanganyika Rifles).

Pamoja na makabidhiano hayo, Jeshi jipya la Tanganyika huru (TR) halikufanyiwa mabadiliko makubwa ya uongozi, Maafisa na Askari wa Kiingereza waliendelea kutetea dola ya kikoloni, na siyo kutetea Taifa jipya la Tanganyika, na taratibu za Jeshi jipya la TR ziliendelea kuwa zile za KAR. Aidha, Jeshi liliendelea pia kutumia bendera ya KAR hadi tarehe 20 Juni, 1963 zilipobadilishwa rasmi. Mabadiliko hayo ya bendera, bado hayakuleta mabadiliko makubwa kwani TR liliendelea kuendeshwa kulingana na taratibu za kikoloni, na uongozi wa Jeshi ulibaki mikononi mwa Waingereza bila kuwashirikisha Maafisa wazalendo kikamilifu. Hivyo, pamoja na kuwa Amiri Jeshi Mkuu alikuwa mzalendo, Maafisa wa Jeshi waliendelea kuwa wa wakoloni. Hali hiyo ilizua utata mwingi na hata kupelekea Jeshi la TR katika kambi ya Colito (sasa Lugalo) kufanya maasi tarehe 20 Januari, 1964. Maasi hayo ndiyo yalipelekea kuanzishwa kwa JWTZ.

Siku tano tangu kutokea kwa maasi, hapo tarehe 25 Januari, 1964 aliyekuwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu Mwl J.K. Nyerere alitangaza kulivunja rasmi Jeshi Jipya la Tanganyika Rifles (TR) na hivyo kuwaasa vijana wa TANU Youth League wajitokeze kuanzisha Jeshi jipya. Vijana wengi walijitokeza nchini kote na kuanza mafunzo yao tarehe 3 Machi, 1964, na kuhitimu tarehe 1 Septemba, 1964. Vijana hawa wakawa askari wa kwanza wa JWTZ, na Kapteni Mirisho Sarakikya akateuliwa kuwa Mkuu wa Majeshi na kupandishwa cheo kuwa Brigedia. Aidha, Luteni Elisha Kavana aliteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Majeshi, na kupandishwa cheo kuwa Meja. Tangu wakati huo JWTZ limeongozwa na Wakuu wa Majeshi wanane (8) ambao ni Jenerali Mirisho Sam Hagai Sarakikya (1964 - 1974), Jenerali Abdallah Twalipo (1974 - 1980), Jenerali David Bugozi Msuguri (1980 - 1988), Jenerali Ernest Mwita Kiaro (1988 - 1991), Jenerali Robert Philemon Mboma (1991 - 2001), Jenerali George Marwa Waitara (2001 - 2007), Jenerali Davis Adolf Mwamunyange (2007 - 2017) na Jenerali Venance Salvatory Mabeyo (2017 - hadi sasa).

Wakati Jeshi la Wananchi likianzishwa halikuwa na zana wala vifaa, kwani wakoloni hawakuacha kitu mbali na vitu vidogo vidogo. Serikali ilifanya kazi kubwa kuhakikisha kuwa Jeshi linakuwa na kanuni, wataalamu, zana na vifaa vinavyohitajika. Kazi hii ilifanyika kwa kujituma na weledi wa hali ya juu na kuiwezesha Tanzania kuwa na Jeshi makini na imara linaloheshimika ndani ya nchi, kikanda na kimataifa. Haya ni mafanikio makubwa na ya kujivunia kama Taifa.

Ubora, umahiri na uimara wa Jeshi letu, uliiwezesha Tanzania kupata ushindi wa kishindo katika vita vya Kagera vilivyoanza Oktoba, 1978. Vita hivyo vilitokana na Nduli Idd Amini aliyeamuru majeshi yake mwaka 1978 kuivamia Tanzania kwa madai kwamba eneo kuanzia Mutukula hadi Mto Kagera ni sehemu ya Uganda.

Kama mtakavyokumbuka baada ya uvamizi huo, tarehe 02 Novemba, 1978 aliyekuwa Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitangaza uamuzi wa kuyaondoa majeshi ya uvamizi kwa kusema “Sababu za Kumpiga Tunazo, Uwezo wa Kumpiga Tunao na Nia ya Kumpiga Tunayo…”. Hadi kufikia tarehe 25 Novemba, 1978 Majeshi ya Nduli Amin yalikuwa yamepigwa na kufukuzwa kutoka eneo la lote la Kagera. Majeshi yetu kwa kushirikiana na Jeshi la Ukombozi la Uganda yaliingia nchini Uganda na kuuteka Mji Mkuu Kampala tarehe 25 April, 1979 hali iliyosababisha Nduli Amin kuikimbia nchi yake.

Ndugu wanahabari, kutokana na ushindi uliopatikana, Majeshi yetu yalirejea kishujaa mwaka 1980 na kauli nzito kwa Watanzania kuwa “Kazi Mliyoyotutuma, Tumeimaliza”. Baada ya kukamilisha jukumu hilo, JWTZ lilipewa kazi ya kusaidia ulinzi wa nchi hiyo na kuwafundisha wanajeshi wa Uganda masuala ya Ulinzi na Usalama wa Taifa lao. Kazi hiyo ilitekelezwa na kuhitimishwa kwa mafanikio na uadilifu mkubwa.

**Kuanzishwa kwa Kamandi za Jeshi**

Jeshi liliendelea kuimarishwa kwa kuanzishwa kwa Kamandi tatu ambazo ni Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Kamandi ya Jeshi la Anga na Kamandi ya Jeshi la Wanamaji. Kuanzishwa kwa Kamandi hizi kumerahisisha utendaji na kuongeza ufanisi katika Jeshi letu kiutawala, kimafunzo na kivita na kulifanya kwenda na mahitaji ya wakati na kuwa Jeshi la kisasa.

**Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu**

Toka nchi yetu ilipopata Uhuru, Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu imekuwa ikitekeleza majukumu yake kama mhimili mkuu wa JWTZ. Kutokana na kukua kwa Jeshi letu, Kamandi hii iliundwa rasmi tarehe 25 Desemba, 2007 ili kuleta mageuzi ndani ya Jeshi kwa kuliweka katika muundo wenye ufanisi na tija zaidi katika Ulinzi na Usalama wa Taifa. Hii imesaidia kuyapunguzia majukumu Makao Makuu ya Jeshi ambayo yamebakiwa na majukumu ya mipango ya kimkakati.

**Kamandi ya Jeshi la Wanamaji**

Ndugu wanahabari, Kamandi ya Wanamaji ilianzishwa rasmi mnamo tarehe 06 Desemba 1971, baada ya nchi kuhitaji kuwa na ulinzi wa mipaka yake kwa upande wa bahari, maziwa na mito mikubwa. Uwepo wa Kamandi hii umesaidia kupunguza uvuvi haramu, maharamia, usafirishaji haramu wa binadamu, ugaidi, madawa ya kulevya na biashara haramu zinazoweza kupitishiwa baharini. Aidha, Jeshi hili lilishiriki kikamilifu katika uokoaji wa watu na mali katika kivuko cha MV Nyerere kilichozama tarehe 20 Septemba, 2018 katika Wilaya ya Ukerewe Mkoani, Mwanza.

**Kamandi ya Jeshi la Anga**

Ndugu wanahabari, Kamandi ya Jeshi la Anga ilianzishwa rasmi mwaka 1982. Kamandi hii inayo majukumu ya msingi katika wa Ulinzi wa Anga la Tanzania. Aidha, Kamandi hiyo husafirisha pia Maafisa na Askari wakati wa amani na dharura, na husaidia mamlaka za kiaraia katika kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na wakati wa maafa kama kusafirisha misaada ya kibinadamu.

**Ulinzi wa Mipaka**
Ndugu wanahabari, katika miaka 60 JWTZ limefanya mageuzi na kupata mafanikio makub

wa. Wizara kupitia JWTZ, imeendelea kutekeleza jukumu la kulinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhakikisha mipaka ya nchi yetu ambayo inajumuisha eneo la nchi kavu, anga na la maji imeendelea kuwa salama, kwa kipindi chote cha miaka 60 tangu tupate uhuru.

**Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika**

Mafanikio na mchango mkubwa wa Tanzania katika ukombozi wa kusini mwa Afrika ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje ya mwaka 1964. Sera hiyo ililenga kuhakikisha kuwa nchi zote za Afrika zilizokuwa hazijapata Uhuru wakati huo zinakuwa huru. Kufuatia kuundwa kwa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (OAU) mnamo mwaka 1963, Tanzania iliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ukombozi ya OAU na Makao Makuu ya Kamati hiyo kuwa Dar es Salaam. Jukumu hilo liliifanya Tanzania kuwa mstari wa mbele katika kuratibu shughuli zote za ukombozi pamoja na kushiriki mapambano ya kivita kuwang'oa mabeberu wa kibaguzi kusini mwa Afrika. Aidha, JWTZ lilitoa mchango mkubwa kwa kutoa mafunzo ya kijeshi kwa wapigania uhuru wa Vyama vya Ukombozi vya FRELIMO cha Msumbiji, MPLA cha Angola, ZANU PF cha Zimbabwe, SWAPO cha Namibia na PAC na ANC vyote vya Afrika Kusini. Pamoja na kushiriki katika kutoa mafunzo kwa wapigania uhuru, Wanajeshi wakishirikiana na Wananchi wa Tanzania walitoa mchango wa hali na mali, ikiwa ni pamoja na kujitolea kwa damu kwa lengo la kuunga mkono mapambano hayo.

Mchango huo mkubwa wa Tanzania uliwezesha nchi mbalimbali kujikomboa, na kuwang'oa makaburu huko Afrika ya Kusini. Baada ya mafanikio ya kuwang'oa mabeberu katika baadhi ya nchi, baadhi ya Maafisa wa JWTZ waliteuliwa kuwa washauri wa kijeshi, na wengine waliteuliwa kuongoza Kamati ya Ukombozi ya OAU. Miongoni mwao ni Hayati Brigedia Jenerali Hashimu Mbita ambaye aliteuliwa kuwa Katibu Mtendaji wa Kamati ya Ukombozi kuanzia mwaka 1972 hadi 1994 ilipomaliza kazi yake. Mchango wa Tanzania, hususan Hayati Brigedia Jenerali Hasjimu Mbita unaheshimika sana Kusini mwa Afrika, na hadi kupelekea Zimbabwe kumtunuku Nishani ya juu kabisa kama shujaa. Aidha, historia ya ukombozi na mchango wa Tanzania imechapishwa katika chapisho liitwalo, "Hashim Mbita Publication la SADC". Niwaombe watanzania wote kulisoma na kupata ufahamu zaidi na hivyo kujivunia mchango wa Tanzania.

Ni vema pia kufahamu kuwa shughuli mbalimbali katika harakati za ukombozi wa Kusini mwa Afrika, na mafunzo kwa wapigania uhuru yaliyotolewa na JWTZ zilifanyika kwa kutumia lugha ya kiswahili, na hivyo kudumisha udugu na umoja baina ya Tanzania na nchi hizo. Kwa sasa lugha ya kiswahili ni mojawapo ya lugha rasmi zinazotumika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Umoja wa Afrika, hii ni kutokana na kutambua mchango wa lugha ya kiswahili na mchango wa Tanzania katika harakati za ukombozi.
Mafunzo ya Kijeshi
25. Wizara kupitia JWTZ, imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi katika Shule na Vyuo vya kijeshi ndani na nje ya nchi. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa kiutendaji kivita Maafisa na Askari katika kutekeleza majukumu yao ya msingi ndani na nje ya nchi.

Aidha, tangu kupata uhuru Wizara kupitia JWTZ imeanzisha na imeendelea kuimarisha shule na vyuo vya kijeshi vya maafisa na askari katika kuboresha mafunzo. Baadhi ya vyuo na shule hizo ni Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC), Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC - Duluti), Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi – Monduli (TMA) na Shule ya Mafunzo ya Awali ya Kijeshi – RTS Kihangaiko.

**Mazoezi ya Kijeshi**
Wizara kupitia JWTZ imeendelea pia kuwajengea weledi maafisa na askari kwa kuwawezesha kushiriki katika mazoezi mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Wizara kupitia JWTZ imeshiriki katika mazoezi ya pamoja chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Mazoezi haya ya pamoja yamekuwa na manufaa katika maeneo mbalimbali ikiwemo kubadilishana uzoefu wa kiutendaji kivita, na kuimarisha umoja na ushirikiano katika operesheni za ulinzi wa amani. Aidha, mazoezi hayo yamewajengea wanajeshi wetu uwezo wa kiutendaji katika kukabiliana na matishio mbalimbali ikiwemo ugaidi, uharamia, uhamiaji haramu na maafa.

**Ushiriki Katika Shughuli za Ulinzi wa Amani**
Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika katika Operesheni za Ulinzi wa Amani katika nchi mbalimbali zenye migogoro kwa kupeleka vikosi, waangalizi wa kijeshi, wanadhimu na makamanda. Nchi ambazo JWTZ imewahi kushiriki katika ulinzi wa amani ni Liberia, Eritrea, Shelisheli, Ivory Coast (sasa Cote D'Ivoire), Comoros, Sierra Leone, na Sudan. Hivi sasa JWTZ linashiriki Ulinzi wa Amani katika nchi za Lebanon, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Msumbiji na Sudan Kusini.

**Kuanzishwa Mafunzo ya JKT kwa Vijana**
Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) lilianzishwa kufuatia Sheria ya JKT Na. 16 ya mwaka 1964 (The National Service Act No. 16 of 1964). Sheria hiyo imefanyiwa marekebisho mbalimbali hadi mabadiliko ya mwaka 2002. Sheria hiyo ilimpa Mkuu wa JKT dhamana ya kuandikisha vijana kwa ajili ya malezi, uzalishaji mali na ulinzi.

Wizara kupitia JKT imewapatia vijana wa kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa, uwezo wa kujitegemea na kuwa sehemu ya Jeshi la Akiba, kwa vijana wa Mujibu wa Sheria na wa kujitolea kwenye Kambi za JKT.

Tangu kuanzishwa kwake JKT iliendelea kutekeleza mafunzo ya vijana kwa ufanisi hadi mwaka 1994 mafunzo yalipositishwa. Hatua hiyo ilichukuliwa na Serikali kutokana na kuyumba kwa uchumi wa dunia miaka ya 1980 hadi 1990. Hivyo, Serikali ililazimika kusitisha mafunzo hayo kwa muda. Mafunzo hayo yalirejeshwa mwaka 2001 kwa vijana wa kujitolea na mwaka 2013 kwa vijana wa mujibu wa sheria. Mafunzo ya JKT yamekuwa na mafanikio kwa Taifa yakijumuisha; kuongezeka kwa uzalendo na uwajibikaji kwa vijana waliopitia mafunzo ya JKT; aidha, Vijana wa JKT wamekuwa sehemu ya Jeshi la akiba, na hivyo kuwa tayari kuilinda nchi pale inapohitajika; Vijana wa JKT huchangia pia katika ujenzi wa miradi ya kitaifa na ya kimkakati, mfano ujenzi wa uzio wa Mererani, na ujenzi wa Ikulu – Chamwino. Aidha, mafunzo yanayotolewa na JKT yamewajengea stadi vijana na kuwawezesha kujitegenea baada ya mafunzo. Aidha, SUMA-JKT inachangia pato la Taifa kwa kulipa kodi na kutoa gawio serikalini kama Shirika la Umma. Wizara imeendelea kuliimarisha JKT kwa kujenga miundombinu na kuanzisha makambi mapya na hivyo kuongeza uwezo wa kuchukua vijana wengi zaidi. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha vijana wote wanaohitimu kidato cha sita wanachukuliwa kuhudhuria mafunzo hayo kadri bajeti itakavyoruhusu.

**Mafunzo kwa Viongozi na makundi mbalimbali**

Wizara kupitia JKT imefanikiwa kutoa mafunzo maalum kwa makundi mbalimbali ya viongozi wa kitaifa, ikiwemo pia kutoka vyama vya siasa na watumishi wa Serikali. Baadhi yao ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watumishi wa serikali pamoja na watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mafunzo ya Jeshi la Akiba**

Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo kwa vijana katika mikoa yote ya Tanzania ambao ni sehemu ya Jeshi la Akiba. Jeshi hili limeendelea kushiriki katika shughuli za ulinzi ndani ya nchi, na liliweza kuongeza nguvu wakati wa Vita vya Kagera mwaka 1978 na 1979. Vile vile, JWTZ kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa, imeendelea kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi na usalama. Jeshi hili la Akiba limepata mafanikio makubwa katika kuwajengea wananchi uzalendo na kuwapatia ujuzi wa kulinda maeneo mbalimbali, na hivyo kujenga mshikamano wa Kitaifa.

**Viwanda vya Kijeshi**

Katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru, Serikali imeweza kuanzisha viwanda vya kijeshi ikiwemo pamoja na Tanzania Automotive Technology Centre (TATC), maarufu kama NYUMBU, Shirika la Mzinga na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT). Mashirika haya hufanya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia, uzalishaji wa vitendea kazi, na bidhaa na huduma mbalimbali kwa matumizi ya kijeshi na kiraia, uzalishaji mali na miradi ya Kimkakati.

Shirika la TATC maarufu kama NYUMBU linatambulika katika teknolojia ya magari.

Shirika hili limeendelea kufanya tafiti na kuhawilisha teknolojia za magari, zana na mitambo ili Taifa liweze kujitegemea kiteknolojia na kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kuhawilisha teknolojia za magari na mitambo ili kutanzua matatizo ya kiufundi katika sekta za ulinzi na usalama, usafirishaji, kilimo na viwanda; kusanifu na kuendeleza uzalishaji magari, mitambo na mashine zinazofaa kwa matumizi ya Tanzania; kutoa huduma ya ushauri kwenye sekta ya viwanda nchini katika uhandishi mitambo, usanifu na uzalishaji; kufanya tafiti kuhusu malighafi zinazotumika katika uhandisi mitambo na teknolojia ya juu ya kukalibu chuma; kuwa kituo cha kutoa mafunzo ya juu ya teknolojia; kukagua na kuthibitisha ubora wa vifaa na mashine zinazonunuliwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na kufanya shughuli nyingine maalum ya kihandisi.

Kwa upande mwingine, Shirika la Mzinga limeendelea kuzalisha vitendea kazi kwa ajili ya vyombo vya ulinzi na usalama na sekta ya madini pamoja na kuuza nje ya nchi, hivyo kuchangia pato la Taifa na kuokoa matumizi ya fedha za kigeni.

Aidha, SUMAJKT inaendelea kujenga na kuimarisha viwanda vyake vikiwemo:

(i) Kiwanda cha ushonaji Mgulani (National Service Garments Factory). Kiwanda hiki kimekuwa mkombozi mkubwa kwa Serikali, hususan katika vyombo vya ulinzi na usalama kwani kimeweza kushona sare mbalimbali za majeshi yetu na kupunguza gharama za ununuzi wa sare kutoka nje ya nchi. Vilevile, kiwanda hiki kinashona sare za taasisi zingine za Serikali pamoja na makampuni binafsi ya ulinzi.

(ii) Kiwanda cha Bidhaa za ngozi (SUMAJKT Leather Products) - Mlalakuwa JKT, ambacho huzalisha bidhaa zake kwa Maafisa na Askari wa JWTZ, Walinzi wa SUMAJKT Guard Ltd, Mgambo, na kampuni Binafsi za Ulinzi. Kiwanda hiki kimeokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kununua bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

(iii) Kiwanda cha Maji ya kunywa Mgulani (Dar es Salaam), SUMAJKT kinachozalisha maji safi na salama ya kunywa ya UHURU PEAK. Kiwanda hiki ni cha kwanza, kimesaidia kukuza uchumi na kutoa fursa za ajira, na kuhudumia Jeshi na Taasisi zingine za Serikali.

(iv) Kiwanda cha Kuchakata nafaka za mahindi – Mlale (Songea); kiwanda hiki kimekuwa kikihudumia baadhi ya Kambi za Jeshi na baadhi ya taasisi za Serikali. Pia, kimechangia katika kutoa ajira.

(v) Kiwanda cha Samani – Chang'ombe Dar es Salaam ambacho hutengeneza samani za aina mbalimbali za maofisini na majumbani. Hali hii imesaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa kuagiza samani hizo kutoka nje ya nchi.

(vi) Vile vile, shirika limekuwa likishiriki katika shughuli za ujenzi za kibiashara na pia ujenzi wa majengo na miundombinu ya Taasisi za Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na watu binafsi. Hali inayosaidia kuokoa fedha nyingi za Serikali, na kuongeza pato kwa ajili ya kuchangia uchumi wa nchi.

(vii) SUMAJKT imeweza pia kuanzisha Kampuni Tanzu ya Ulinzi (SUMAJKT Guard Ltd) ambayo imekuwa msaada katika kutoa ajira kwa vijana, kuchangia pato la Taifa na kuimarisha ulinzi katika Taasisi za Serikali, zisizo za kiserikali na watu binafsi.

Kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 SUMAJKT imeweza kutoa gawio kwa Serikali la jumla ya Shilingi billioni 3.78 kutokana na faida inayopatikana katika uzalishaji.

**Kilimo cha Kimkakati**

Ndugu wanahabari, Wizara kupitia JKT imeendelea pia kutekeleza Mkakati wa Kilimo (2019/2020 – 2024/25) wa kuliwezesha JKT kujitosheleza kwa Chakula. Mkakati huo unatekelezwa katika vikosi vya Chita – Morogoro, Milundikwa – Rukwa, Mlale – Ruvuma, Mgambo – Tanga na Oljoro - Arusha kwa kutumia vyanzo vya ndani vya JKT, na bajeti ya Serikali. Aidha, Wizara kupitia JKT inashiriki katika kilimo cha mazao ya kimkakati ya Taifa, ambayo ni Michikichi – Bulombora – Kigoma, Mkonge – Maramba na Mgambo Tanga, Korosho – Nachingwea na Manyoni Singida, Alizeti – Makutupora Dodoma, na Kahawa – Itende Mbeya na Tarime – Mara.

Ndugu wanahabari, katika kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi, Wizara kupitia JKT inaendelea na ujenzi wa mfumo wa umwagiliaji (irrigation scheme) katika shamba la Mpunga – Chita, ambalo ni shamba la mfano na limechangia kwa kiasi kikubwa katika kulisha vikosi vya Jeshi na kupunguza utegemezi.

**Ujenzi wa Miundombinu**

Katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu mbalimbali kwa kufanikisha ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi ya wanajeshi kote nchini. Mfano wa hivi karibuni, Wizara imetekeleza mradi wa nyumba 6,064 katika mikoa tisa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Kigoma, Morogoro, Kusini Pemba, Pwani na Tanga. Kujengwa kwa nyumba hizo kumeliwezesha Jeshi kupunguza uhaba wa nyumba za kuishi Wanajeshi na Watumishi wa Umma. Aidha, ukarabati wa baadhi ya nyumba za zamani pamoja na majengo ya huduma kama vile hospitali, mabwalo, mabweni ya kuishi askari, shule, vyuo na miundombinu mingine umeendelea kufanyika chini ya Wizara.

**Kusaidia Mamlaka za Kiraia**

Ndugu wanahabari, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na maafa na shughuli mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Baadhi ya maeneo ambayo JWTZ imeshirikiana na mamlaka za kiraia ni pamoja na, kushiriki katika uokozi, kuboresha huduma katika Taasisi za Serikali; kushiriki katika ujenzi wa miundombinu kama vile ujenzi wa Reli ya Kisasa ya Standard Gauge Railway (SGR), na mradi kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project - JNHPP); ulinzi wa maeneo ya kimkakati ikiwemo mgodi wa Tanzanite uliopo Mirerani Mkoani Manyara.

Kwa upande wa huduma za afya Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa huduma ya matibabu kwa wananchi waishio karibu na kambi za Jeshi. Takwimu zinaonyesha kuwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo ndiyo wanaopatiwa huduma kwa asilimia kubwa. Vile vile, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushiriki katika kutoa elimu katika ngazi ya sekondari na vyuo vya ufundi stadi.

**Upimaji wa Maeneo ya Jeshi**

Ndugu wanahabari, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linahitaji ardhi kwa ajili ya ujenzi wa makambi, makazi ya wanajeshi na maghala ya kuhifadhia silaha. Vile vile, Jeshi linahitaji ardhi kwa ajili ya kuendeshea mafunzo na mazoezi ya kijeshi. Kutopimwa kwa maeneo ya Jeshi hupelekea uvamizi na migogoro ya ardhi. Ili kuondoa migogoro katika njia ya kudumu kazi ya upimaji, uthamini na ulipaji fidia kwa maeneo yanayomilikiwa na Jeshi imeanza na itakuwa endelevu ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya Jeshi unaofanywa na wananchi. Kazi hii inafanyika kupitia mpango mkakati wa kupima na kutathimini maeneo ya Jeshi yenye migogoro kwa muda wa miaka mitatu 2020/21 -2022/23.

Katika kutekeleza mpango mkakati huu, Wizara imefanikiwa kupima maeneo 56, kazi iliyofanyika katika awamu mbili kwa maeneo ya Tanzania Bara. Wizara inaendelea kutekeleza awamu ya tatu inayojumuisha mikoa mingine ya Tanzania bara na Visiwani itakayojuisha maeneo 96.

**Michezo Jeshini**

Aidha, Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kushiriki katika michezo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Ushiriki huu pia unahusisha mashindano yanayoandaliwa na mashirikisho ya michezo ya Majeshi kutokana na Tanzania kuwa mwanachama wa Mashirikisho hayo. Hivyo, kupitia michezo ya Majeshi JWTZ imeshiriki michezo ya Kimataifa kwa nyakati tofauti ambapo timu zilifanikiwa kutwaa medali. Kama ilivyo kwa wanajeshi wa nchi nyingine, wanamichezo wa JWTZ wamechangia kwa kadri fursa zilivyokuwa zikipatikana katika kuliletea Taifa sifa njema ndani na nje ya Bara la Afrika. Katika hili tunawakumbuka na kuwaenzi wengi, ikiwa ni pamoja Kanali (Mstaafu) Abdalla Azizi, Kanali (Mstaafu) Juma Ikangaa, Meja (Mstaafu) Filbert Bayi, Sajini Restuta Joseph, Sajini Simbu, Koplo Bakari, waliyoliletea Taifa letu sifa njema na heshima kupitia michezo.

**HITIMISHO**

Ndugu Wanahabari, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itaendelea kuhakikisha kuwa mipaka ya nchi inaendelea kuwa salama. Wito wa Wizara kwa Wananchi ni kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa nchi kwa kujitoa kwa namna itakavyohitajika, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za viashiria vya matishio ya kiulinzi na kiusalama. Kama alivyowahi kusema mwasisi wa Taifa hili Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere nanukuu "Jukumu la Ulinzi wa Taifa ni Jukumu la Kila Mwananchi". Kwa muktadha huu, jukumu la ulinzi si la Wizara pekee bali ni la kila mtanzania mwenye mapenzi mema na nchi yetu, hivyo tuendelee kuwa pamoja kulilinda Taifa letu.

Aidha, naomba kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati watumishi wote wa Wizara, makamanda na askari wote wa JWTZ, vijana wa JKT kwa kazi kubwa na moyo wa kujituma, kulikowezesha mafanikio niliyoyaelezea tangu kuanzishwa kwa Wizara ya Ulinzi, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa.

Ndugu Wanahabari, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya ya kutangaza mafanikio ya serikali yetu kwa kipindi chote cha miaka 60 tangu nchi yetu ilipopata uhuru. Vile vile nitoe rai kwenu kuendelea kushiriki kikamilifu katika kulinda amani na utulivu uliopo kupitia tasnia yenu ya habari.

5Ndugu Wanahabari, baada ya kusema hayo, ninawaasa na kuwaomba Wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano katika ulinzi wa Taifa letu.



MAFANIKIO NA MAENDELEO YA SEKTA YA MALIASILI NA UTALII
KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

Ndugu wanahabari, Tanzania imejaaliwa kuwa na maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu na nyuki; na malikale yenye mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi. Mchango huo unatokana na uhifadhi wa mifumo ikolojia unaokidhi matakwa ya kimazingira, kijamii na kiutamaduni, kitaifa, kikanda na kimataifa. Aidha, maeneo ya maliasili yanatoa huduma za maji kwa matumizi mbalimbali; makazi ya wanyamapori na viumbe wengine, uchavushaji, uhifadhi wa udongo, ufyonzaji wa hewa ukaa (carbon) na hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kiuchumi, maliasili na malikale zimeendelea kuchangia katika kuingiza fedha za kigeni na Pato la Taifa (GDP) kupitia utalii, ajira, nishati, elimu, utafiti, utamaduni, burudani na tiba. Mfano sekta ya utalii huchangia takriban asilimia 25 ya fedha za kigeni na zaidi ya asilimia 17 katika Pato la Taifa. Aidha, ustawi wa sekta ndogo ya utalii unategemea pamoja na masuala mengine, uhifadhi mzuri wa maliasili, malikale, historia na utamaduni. Uhusiano bora kati ya uhifadhi na maendeleo unachangia katika ustawi wa maliasili, matumizi endelevu, ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi.

Kwa kuzingatia mgawanyo wa mamlaka nchini, Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia uhifadhi wa maliasili, malikale na maendeleo ya utalii. Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, mipango ya maendeleo na maelekezo mbalimbali ya Serikali.

## MAFANIKIO YA SEKTA YA MALIASILI NA UTALII KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

Ndugu Wanahabari, katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara, Serikali kupitia Sekta ya Maliasili, Malikale na Utalii imeliwezesha Taifa kupata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo:-

### 2.1 SEKTA YA UTALII

#### 2.1.1 Kukua na kuimarika kwa shughuli za utalii

Sekta ya utalii ina umuhimu mkubwa katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla katika nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania. Katika miaka 60 iliyopita Serikali iliimarisha utalii nchini kwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa mikakati ya kukuza vivutio mbalimbali vya utalii vikiwemo hifadhi za wanyamapori, maporomoko ya maji, milima, misitu ya mazingira asilia, utamaduni, fukwe na malikale.

**Kupitia uendelezaji wa vivutio hivyo, Tanzania imeweza kupata mafanikio mbalimbali yakiwemo:-**

#### 2.1.2 Kuongezeka kwa idadi ya Watalii na Mapato

Kutokana na juhudi za Serikali za kuendeleza na kuimarisha utangazaji wa vivutio vya utalii nchini, idadi ya Watalii wanaoingia nchini kutoka katika nchi mbalimbali Duniani imeongezeka kutoka 9,847 Mwaka 1960 hadi kufikia watalii 1,527,230 Mwaka 2019. Kadhalika, kumekuwepo na ongezeko la mapato yatokanayo na watalii, kwa mfano mwaka 1995 mapato yalikuwa Dola za Marekani milioni 259.44 ambapo yaliendelea kuongezeka hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019 kabla ya Ugonjwa wa UVIKO-19. Kutokana na jitihada za Serikali katika kukabliliana na ugonjwa wa UVIKO-19 idadi ya watalii imeanza kuongezeka kutoka watalii 620.867 mwaka 2020 hadi kufikia 716,169 mwezi Oktoba 2021.

#### 2.1.3 Kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi katika shughuli za utalii

Serikali imefanikiwa kuyafikia makundi mbalimbali katika jamii katika kutangaza na kuhamasisha utalii wakiwemo wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo, watu wenye mahitaji maalum, vikundi vya kidini, Madereva wa bodaboda na bajaji, mashirika binafsi na ya kiserikali. Aidha, wananchi wengi wemeendelea kushiriki kwenye shughuli za utalii ambapo ajira takriban milioni 1.6 za moja kwa moja na zile ambazo sio za moja zimepatikana.

Aidha, katika kuendelea kujenga mazingira bora ya kuwawezesha wananchi hususan vijana kuanzisha biashara za utalii nchini, Serikali imepunguza viwango vya ada ya leseni kutoka Shilingi za Tanzania sawa na Dola za Marekani 2000 hadi Shilingi za Tanzania sawa na Dola za Marekani 500 kwa magari kuanzia moja hadi matatu. Hatua hii imelenga kuongeza ushiriki wa wakala wa biashara za utalii ambao ni wazawa katika biashara za utalii. Kufuatia hatua hiyo, wakala wa biashara za utalii wazawa waliongezeka kutoka wakala 643 hadi kufikia 1,687 sawa na ongezeko la asilimia 162.4.

#### 2.1.4 Kuongezeka kwa juhudi za kutangaza utalii ndani na nje ya nchi

Katika kuimarisha utangazaji wa vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi,. Serikali imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuandaa na kushiriki kwenye makongamano, maonesho na ziara za utangazaji utalii (exhibition and road shows) katika masoko ya msingi (Uingereza, Marekani, Ujerumani, Ufaransa, Italia, Hispania na Australia) na masoko ya kimkakati (China, Urusi, India, Poland, Jamhuri ya Czech, Israeli, Uturuki, Falme za Kiarabu, Qatar, Kuwait na Saudi Arabia); kuimarisha matumizi ya TEHAMA; kuandaa ziara za mfunzo kwa waandishi wahabari wa kimataifa, mawakala wa ulii, na mawakala wa Usafirishaji kwa ajili ya kusaidia kutangaza Utalii wa Nchi yetu.
Aidha, Wizara imeendelea kutumia ofisi za Balozi za Tanzania nje ya nchi Kimkakati kutangaza na kuhamasisha utalii kikanda na kimataifa; kutumia mabalozi wa hiari (goodwill ambassadors) kutangaza Utalii; na kutumia vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi katika kutangaza na kuhamasisha utalii.

Kupitia juhudi hizi vivutio vya utalii vya Tanzania vimepata umaarufu mkubwa na Tuzo mbalimbali za Kimataifa. Mfano ni Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa hifadhi Bora zaidi barani Afrika katika kipindi cha miaka mitatu (3) mfululizo kuanzia 2019 hadi 2021. Pia imetambuliwa na Gazeti Maarufu la Forbes la nchini Marekani kama kivutio cha pili (2) duniani miongoni mwa vivutio bora 21 vya kutembelewa kwa mwaka 2021. Aidha, Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro, Serengeti na Tarangire zimeshinda tuzo ya kuwa hifadhi bora kati ya hifadhi bora 20 za kwanza Duniani 2021.

Pamoja na mafanikio hayo Tanzania kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) imetangazwa kuwa mshindi wa kundi la dhahabu miongoni mwa washindi 51 kutoka nchi 39 duniani wa tuzo ya huduma za viwango vya Kimataifa kwa mwaka 2020. Pia hifadhi tano (5) za Taifa ambazo ni Kilimanjaro, Serengeti, Mkomazi, Manyara na Arusha zimepata tuzo ya ubora wa huduma za viwango vya Kimataifa kwa mwaka 2020.

**2.1.5 Vivutio vya utalii vya Tanzania kuingizwa kwenye orodha ya Urithi wa Dunia**

Kufuatia juhudi za Serikali katika kulinda na kuhifadhi rasilimali za maliasili na malikale, maeneo saba (7) ya Tanzania yameorodheshwa kwenye orodha ya urithi wa dunia kutokana na umuhimu wake. Maeneo hayo ni Hifadhi ya Taifa Serengeti; Hifadhi ya Taifa Mlima Kilimanjaro; Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; Pori la Akiba Selous; Mji mkongwe wa Zanzibar; Michoro ya Miambani Kondoa; na Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Hatua hii imeiwezesha Tanzania kufahamika zaidi katika anga za kimataifa kutokana na maeneo hayo muhimu. Aidha, imeiwezesha Tanzania kuendelea kunufaika kupitia miradi mbalimbali inayofadhiliwa na Shirika la UNESCO na mashirika mengine duniani. Katika hatua nyingine, vivutio vitatu (3) vya Tanzania vimeingizwa kwenye maajabu saba (7) barani Afrika. Maeneo hayo ni Hifadhi ya Taifa Serengeti; Mlima Kilimanjaro na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

**2.1.6 Kuongezeka kwa mazao mapya ya utalii**

Katika kuvutia watalii wengi zaidi na kuongeza siku za mtalii kukaa nchini, Serikali imeendelea kuibua na kukuza mazao mapya ya utalii ambayo yameendelea kufanya vizuri yakiwemo; utalii wa michezo; utalii wa meli (Cruiseship Tourism); utalii wa fukwe; utalii wa mikutano na matukio; utalii wa nyuki (Api-Tourism); utalii wa kihistoria; utalii wa matibabu kwa kuanzia katika Hospitali za Umma za Muhimbili (MNH), Taasisi ya Mifupa (MOI), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI); utalii wa kilimo (Agrotourism) na Utalii wa Utamaduni. Mathalan, hadi sasa kuna miradi ya ujasiriamali wa utalii wa utamaduni zaidi ya 100 kwa nchi nzima.

**2.1.7 Kuboresha huduma za utalii wa uwindaji**

Ndugu wanahabari,

Katika kuimarisha shughuli za utalii wa uwindaji Serikali imeanzisha utaratibu wa kuuza vitalu vya uwindaji kwa njia ya mnada kupitia mfumo wa kielektroniki. Mathalan, katika awamu nne (4) za mnada wa kugawa vitalu kwa njia ya kielektroniki uliofanyika kati ya Juni 2019 na Mei 2021, asilimia 26 ya vitalu 46 vilivyoingizwa kwenye mnada viliuzwa. Mapato yaliyopatikana ni asilimia 84 ya mapato yote ambayo yangepatikana kwa kugawa vitalu vyote 46 bila mnada.

**2.1.8 Kuboresha utoaji wa huduma katika Sekta ya Utalii**

Katika kuboresha huduma kwenye Sekta ya Utalii, Serikali imeanzisha mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama AserT (Accommodation Services in Tanzania). Mfumo huo unawezesha wamiliki wa huduma za malazi kujitathmini kwa kutumia vigezo vya kupanga huduma za malazi katika ubora vilivyowekwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Serikali imeendelea kutoa mafunzo kwa watoa huduma za malazi kuhusu namna ya kusajili wageni kwa kutumia mfumo husika. Vilevile, Serikali imeendelea kuboresha Mfumo wa MNRT Portal ili kuwezesha ufuatiliaji wa watalii wanaoingia nchini kupitia malango mbalimbali, huduma za malazi, na vivutio vya utalii wanavyotembelea.

**2.1.9 Kuboresha miundombinu ya utalii**

Wizara imefanikiwa kuboresha miundombinu ya huduma za utalii kwa kujenga na kukarabati barabara, viwanja vya ndege, kambi za utalii na njia za utalii wa kutembea kwa miguu. Katika hatua hiyo, barabara zimeendelea kujengwa na kukarabatiwa ndani ya maeneo ya hifadhi za Taifa, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, hifadhi za misitu ya mazingira asilia, mashamba ya miti, mapori ya akiba, mapori tengefu pamoja na vituo vya malikale. Kwa mfano, Serikali imekarabati barabara zenye urefu wa kilomita 8,847 kati ya kilomita 12,000 katika hifadhi za Taifa; imejenga na kukarabati vivuko (drainage structures) 188; na kujenga viwanja vya ndege 27 vinavyotumika kuleta watalii katika hifadhi za Taifa. Aidha, kambi za kitalii na loji zimeendelea kujengwa katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa lengo la kuboresha huduma za malazi na kuhamasisha utalii wa ndani. Mathalan, Serikali imeendelea kujenga malazi ya kitalii ya gharama nafuu katika hifadhi za Taifa kwa lengo la kuhamasisha utalii wa ndani.

**2.1.10 Kuendeleza utalii ukanda wa Kusini**

Wizara inatekeleza Mradi wa Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth (REGROW), unaolenga kukuza utalii na uhifadhi wa maliasili na mazingira katika maeneo ya Hifadhi za Mikumi, Ruaha, Nyerere na Udzungwa. Mradi umejikita katika kuimarisha miundombinu ya vivutio vya utalii vilivyopo Ukanda wa Kusini hususan ujenzi wa barabara na viwanja vya ndege ndani ya Hifadhi pamoja na kutangaza ipasavyo eneo hili ili kuendeleza utalii katika Ukanda wa Kusini.

**2.1.11 Kuanzishwa kwa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)**

Ndugu wanahabari,

Bodi ya Utalii Tanzania ilianzishwa kwa Sheria Na. 25 ya mwaka 1962 na marekebisho yake ya mwaka 2002. Baada ya kuanzishwa bodi hii ilipewa jukumu la kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania ndani na nje ya nchi. Bodi imeendelea kuitangaza Tanzania kama kituo bora cha utalii kwa kutumia mbinu mbalimbali; kuendeleza mazao ya utalii ili kuifanya Tanzania iwavutie watalii; na kufanya tafiti mbalimbali ili kuboresha utalii; na kujenga uelewa wa faida za kiuchumi zitokanazo na utalii kwa watanzania. Uwepo wa bodi kwa kiasi kikubwa imewezesha Tanzania kufahamika zaidi katika anga za kimataifa na kutembelewa na idadi kubwa ya watalii kutoka nchi mbalimbali duniani.

**2.1.12 Kuanzishwa kwa Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT)**

Wakala ya Chuo cha Taifa cha Utalii ulianzishwa kwa Establishment Order Na. 7 ya mwaka 2003 na Sheria ya Wakala wa Serikali Sura 245. Wakala una ithibati ya NACTE kuanzia mwaka 2007. Kuanzishwa kwa Wakala huu, umewezesha mafunzo katika fani ya ukarimu, utalii, uratibu wa matukio na maeneo mengine yanayoingiliana; kufanyika utafiti katika sekta ya utalii na maeneo mengine; na kutoa ushauri wa kitaalamu kwenye sekta ndogo ya utalii.

**2.1.13 Kuandaliwa kwa Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 na kutungwa kwa Sheria ya Utalii ya Mwaka 2008**

Ndugu wanahabari, lengo kuu la Sera ya Utalii kwa ujumla ni kukuza uchumi na kuboresha maisha ya watanzania kwa kupunguza umaskini kupitia maendeleo endelevu ya utalii unaokubalika kijamii, kitamaduni, unaotunza mazingira na wenye maslahi kiuchumi. Katika kufanikisha jukumu hilo, Serikali imetunga Sera ya Utalii (1999) ambayo inatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Utalii Na. 29 ya mwaka 2008 ikiwa ni miongozo ya kuiendeleza sekta ya utalii. Sera na sheria hizo zinaendelea kufanyiwa mapitio ili kukidhi mahitaji ya siku hadi siku ya Sekta ya Utalii. Vilevile, Serikali imetunga kanuni tano (5) zinazotekeleza Sheria ya utalii ambazo kwa kiasi kikubwa zimewezesha kuboresha mazingira ya biashara ya utalii nchini.

**2.1.14 Kuanzishwa kwa miongozo ya viwango ya upangaji wa huduma za malazi na chakula katika daraja za ubora**

Serikali kwa kushirikiana na nchi nyingine za Afrika Mashariki imeanzisha na inaendelea kutekeleza miongozo ya viwango vya kupanga huduma za malazi na chakula katika daraja za ubora. Miongozo hiyo imewezesha kuboresha huduma zinazotolewa katika sekta ya Utalii hususan sehemu ya huduma za malazi. Kwa kuzingatia mwongozo hiyo jumla ya huduma za malazi 308 zimepangwa katika daraja za bora katika mikoa mitano (5) ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Manyara na Dodoma. Aidha, zoezi hili litaendelea kufanyika ili kufikia mikoa yote nchini.

**2.2 SEKTA YA WANYAMAPORI**

Ndugu wanahabari, katika kuhakikisha kuwa sekta ya maliasili inazidi kuimarika, Serikali imeendelea kutunza maliasili za nchi na kuyafanya mazao yatokanayo na maliasili, hususan wanyamapori, misitu na nyuki kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi; kuwaongezea wananchi kipato na fursa za ajira. Hatua hizo zimewezesha sekta ya maliasili kuongeza Pato la Taifa na fursa za ajira kwa wananchi na mafanikio mengine kama ifuatavyo:-

**2.2.1 Kuimarisha Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Maliasili**

Katika kudhibiti ujangili, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na uvamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa, Serikali imeendelea kuweka juhudi katika kulinda rasilimali hizi ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kikosikazi cha Taifa Dhidi ya Ujangili kinachojumuisha wadau wengine; kuanzisha Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu na kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili wa Wanyamapori ulioanza kutekelezwa tangu mwaka 2014. Aidha, operesheni za kiintelijensia zimeendelea kufanyika katika maeneo yaliyohifadhiwa ili kupunguza vitendo vya ujangili na uvunaji haramu wa rasilimali za wanyamapori na misitu. Mfano, kwa miaka ya hivi karibuni matukio ya vifo vya tembo kutokana na ujangili yameendelea kuwa chini kutoka tembo 18 mwaka 2016/17 hadi tembo watatu (3) mwaka 2020/21. Katika miaka ya karibuni hakukuwa na matukio makubwa ya ujangili wa faru kutokana na jitihada mbalimbali zikiwemo kuimarishwa kwa shughuli za doria, utoaji wa elimu ya uhifadhi kwa jamii na kuimarishwa kwa shughuli za intelijensia katika maeneo ya hifadhi na vijiji vinavyozunguka hifadhi za Taifa. Kupitia juhudi hizi, taarifa za ufuatiliaji wa matukio hayo zilizopo zinaonesha kuwa ujangili umepungua kwa takriban asilimia 90. Katika hatua nyingine, Serikali imeendeleza juhudi za kudhibiti maeneo yaliyohifadhiwa kwa shughuli za binadamu kama vile kilimo na mifugo.

**2.2.2 Kuimarisha mahusiano baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa**

Ndugu wanahabari, Serikali imeendelea kuimarisha mahusiano na jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi za wanyamapori kwa kuhakikisha kuwa wananchi wanapewa elimu ya kujiepusha na wanyama wakali na waharibifu. Aidha, Serikali imeendelea kutumia teknolojia ya ufuatiliaji wa wanyamapori hususan tembo na faru kwa kuwafunga vifaa maalum (VHF na GPS collar) kwa lengo la kuimairisha ulinzi na kuepusha migongano na wananchi wanaoishi kando ya hifadhi. Vilevile, Wizara imeandaa na kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Utatuzi wa Migogoro baina ya Wanyamapori na Binadamu wa mwaka 2020 hadi 2024. Mkakati huo unalenga kuweka njia bora na endelevu za kukabiliana na migongano baina ya binadamu na wanyamapori. Lengo la Serikali ni kujenga mahusiano mazuri kwa wananchi wanaoishi jirani na maeneo yaliyohifadhiwa kwa uhifadhi endelevu.

**2.2.3 Mikakati ya kuwanufaisha wananchi na rasilimali za maliasili**

Katika juhudi za kuwawezesha wananchi kunufaika na rasilimali za wanyamapori, Serikali imeanzisha rasmi utaratibu wa kuwaruhusu wananchi kufuga wanyamapori na kupata kitoweo kwa njia halali. Katika kutekeleza hilo, jumla ya leseni 46 za ufugaji wanyamapori na 33 za mabucha ya kuuza nyamapori zimetolewa ambapo Mabucha 14 yameanzishwa na tayari yanafanya kazi katika maeneo mbalimbali nchini. Hatua hii inalenga kuongeza wigo wa manufaa yatokanayo na rasilimali za wanyamapori kwa wananchi na hivyo kuimarisha ushiriki wao katika kulinda na kuhifadhi rasilimali hizo. Ili kuwezesha hatua hiyo, Serikali imefanya mapito ya Kanuni za Uuzaji wa Nyamapori (Game Meat Selling Regulations) za mwaka 2020 kupitia Tangazo la Serikali Na. 630 la tarehe 14 Agosti, 2020 kwa kupunguza bei ya usajili wa eneo la kuuzia nyamapori kutoka Shilingi 250,000 hadi 100,000 ili kuwawezesha wananchi wengi kufungua mabucha. Aidha, Serikali imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kuanzisha mashamba ya Wanyamapori ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa nyamapori na kufikiwa kwa malengo yaliyotarajiwa ambapo jumla ya mashamba 36 yameanzishwa na kuongeza idadi ya mashamba kufikia 69.

**2.2.4 Kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI)**

Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria Sura 260 na marekebisho yake ya mwaka 2002. Lengo la kuanzishwa taasisi hii ni kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti kuhusu wanyamapori. Kuanzishwa kwa taasisi imewezesha Serikali kupata mafanikio mbalimbali ikiwemo kufanya, kuratibu, kusimamia na kuendeleza tafiti za wanyamapori nchini; kufanya uchunguzi na ufuatiliaji wa mienendo ya magonjwa ya wanyamapori; kuidadi na kufuatilia mienendo ya wanyamapori nchini; kutoa elimu na mrejesho wa matokeo ya utafiti wa wanyamapori nchini; kushirikiana na taasisi mbalimbali zilizo ndani na nje ya nchi katika kufanya tafiti za wanyamapori; na kuwezesha uhifadhi endelevu wa wanyamapori.

**2.2.5 Kuanzisha kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA)**

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tanzania Wildlife Management Authority - TAWA) ilianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 na kutangazwa kwa amri (Order) iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 135 la tarehe 09 Mei 2014, pamoja na marekebisho yaliyochapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 20 la tarehe 23 Januari 2015. TAWA inatekeleza majukumu ya kiutendaji yaliyokuwa yakitekelezwa na Idara ya Wanyamapori ambayo ni usimamizi, uangalizi na uendelezaji wa rasilimali ya wanyamapori nje ya hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Kwa sasa Mamlaka inasimamia Mapori ya Akiba (29); Mapori Tengefu (27); na maeneo matatu (3) ya ardhioevu (Ramsar Sites). Aidha, Mamlaka ni msimamizi wa shughuli za ufugaji wa wanyamapori katika mashamba (6), Bustani za Wanyamapori (26), Ranchi (5); Breeding sites (30); na Sanctuaries na orphanage centre (1). Vilevile, Mamlaka ni mwangalizi wa shughuli za usimamizi wa wanyamapori kwenye maeneo 21 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMA).

**2.2.6 Kuwezesha Uwekezaji wa Kimkakati (Strategic Investment)**

Serikali inaendelea na juhudi za kuhamasisha uwekezaji wa kimkakati katika maeneo ya hifadhi kupitia Taasisi zake ikiwemo Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA). Mathalan, TAWA imetambua na kutangaza jumla ya maeneo maalum 12 ya uwekezaji "Special Wildlife Investment Concession Area (SWICA). Aidha, TAWA inaendelea na majadiliano na wawekezaji walioonesha nia ya kuwekeza , sambamba na kufanya mapitio ya Kanuni za SWICA. Aidha, katika kipindi hiki Serikali imetenga maeneo mapya ya uwekezaji wa kitalii katika hifadhi za Taifa Nyerere (35), Mto Ugalla (6) na Kigosi (4). Maeneo hayo mapya yana uwezo wa kujengwa hoteli zinazoweza kuchukua jumla ya vitanda 3,250.

**2.2.7 Kuongezeka kwa maeneo ya hifadhi za wanyamapori**

Katika kuimarisha uhifadhi, ulinzi na kuendeleza utalii, baada ya uhuru wa Tanzania Bara, Serikali imeandelea kuanzisha na kupandisha hadhi maeneo ya wanyamapori yaliyohifadhiwa ambayo yamewezesha Hifadhi za Taifa kuongezeka kutoka tatu (3) mwaka 1961 hadi 22 mwaka 2021. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori nje ya maeneo ya hifadhi za Taifa na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kwa kuanzisha mapori ya Akiba ambayo yameongezeka kutoka 0 hadi 27 mwaka 2021; mapori tengefu kutoka 0 hadi 26; maeneo ya ardhioevu kutoka 0 hadi matatu (3).

Aidha, hifadhi za Misitu zimeongezeka kutoka moja (1) hadi 363, Vituo vya Mambo ya Kale kutoka vitatu (3) mwaka 1961 hadi kufikia 133 pia kuongezeka kwa vituo vya Makumbusho ya Taifa kutoka kimoja kilichokuwepo mwaka 1961 hadi 7, Mapori ya Akiba ya Wanyamapori kutoka 9 hadi 22, Kuundwa kwa Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori 38 na kuanzishwa kwa Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia 20, Mapori Tengefu hayakuwepo na sasa yapo 27, Mashamba ya miti ya Serikali 23.

**2.2.8 Kuanzishwa kwa Vyuo vya Taaluma ya Uhifadhi wa Wanyamapori**

Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru, Serikali imeanzishwa vyuo vitatu (3) vya taaluma ya hifadhi wa wanyamapori amabvyo ni: Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka kilichoanzishwa mwaka 1963; Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi kilichoanzishwa mwaka 1966; na Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii (CBCTC) – Likuyu Sekamaganga kilichoanzisha mwaka 1995. Uwepo wa vyuo hivyo vimewezesha kupatikana kwa wataalam wa kutosha wenye taalamu ya uhifadhi wa wanyamapori ambao wameajiriwa katika taasisi mbalimbali za uhifadhi wa wanyamapori nchini.

**2.2.9 Kuanzishwa kwa Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania (TWPF)**

Mfuko ulianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 21 ya mwaka 1978 kwa lengo la kuongeza uwezo wa kifedha wa Sekta ya Wanyamapori kwa ajili ya kutekeleza kikamilifu shughuli za ulinzi wa wanyamapori na mazingira yake. Mfuko umeendelea kuwezesha shughuli mbalimbali za kuhifadhi wanyamapori ikiwemo uzuiaji ujangili; uendeshaji wa Kikosi cha ulinzi wa wanyamapori; kuchangia shughuli za maendeleo ya jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa; na kujenga uwezo katika masuala ya usimamizi wa wanyamapori.

**2.3 MISITU NA NYUKI**

Katika kuimarisha Sekta ya Misitu na Nyuki, Serikali imeendelea kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki na rasilimali hizo zimeendelea kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi na uhifadhi wa mazingira. Hatua hizo zimewezesha Taifa kupata mafanikio mbalimbali kupitia sekta hii ikiwemo:-

**2.3.1 Kuandaliwa kwa Sera ya Taifa ya Misitu na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki**

Kutungwa na kutekeleza kwa Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998 zimechangia kuimarisha uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki na hivyo kuongeza mchango wake katika uchumi.

### 2.3.2 Kutungwa kwa Sheria na Kanuni za Misitu na Ufugaji Nyuki

Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 na Sheria ya Ufugaji Nyuki Na.15 ya mwaka 2002, Kanuni za Misitu za mwaka 2004 na kanuni za ufugaji nyuki za mwaka 2005 zimeandaliwa ambazo zinaratibu Sekta ya Misitu na Ufugaji Nyuki nchini. Sheria na Kanuni hizi zimerahisisha pamoja na mambo mengine biashara na huduma za mazao ya misitu na nyuki.

### 2.3.3 Kuanzisha Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF)

Mfuko wa Misitu Tanzania umeanzishwa mwaka 2010 chini ya Sheria ya Misitu Sura Na. 323 kwa lengo la kukabiliana na changamoto za usimamizi wa rasilimali misitu hususan katika kuimarisha utekelezaji wa Sera na Sheria ya Misitu. Kuanzishwa kwa Mfuko huu kumesaidia katika kuwezesha na kugharamia miradi ya uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu, na miradi ya kuboresha kipato cha jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu ya hifadhi, kufanyika kwa tafiti mbalimbali za misitu, upandaji miti na kuhamasisha jamii kwa kupitia vipindi vya redio na televisheni kuhusu hifadhi ya misitu na vyanzo vya maji.

### 2.3.4 Kuanzishwa kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ulianzishwa kisheria kupitia Tangazo la Gazeti la Serikali (GN 269) la tarehe 30/7/2010 na kuzinduliwa rasmi tarehe 18/7/2011. Kuanzishwa kwa Wakala wa Huduma za Misitu ni kwa mujibu wa Sheria ya Wakala "the Executive Agencies Act Cap. 245 (Revised Edition 2009)", pamoja na Sera ya Misitu ya mwaka 1998, Sera ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998, Sheria za Misitu na Nyuki Sura 323 na Sura 224 za mwaka 2002. Taasisi hii ipo chini ya Idara ya misitu na Nyuki na inafanya shughuli zote za utendaji wa idara hii. Wakala umepanua wigo kibiashara na kuongeza maeneo ya uzalishaji miti na mazao ya nyuki ili kukidhi mahitaji halisi, shughuli za uwekezaji, kuboresha njia mbadala za mapato na uboreshaji wa hifadhi za misitu na nyuki kwa ujumla.

### 2.3.5 Kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI)

Taasisi hii ilianza kazi rasmi tarehe 1 Agosti 1980 na kupewa jukumu la kufanya, kusimamia na kuratibu shughuli za utafiti wa misitu nchini. Aidha, mwaka 2019 Taasisi iliongezewa jukumu la Utafiti wa Ufugaji Nyuki ambao awali ulikuwa unafanywa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI). Uwepo wa Taasisi hii umewezesha Serikali kupata mafanikio mbalimbali ikiwemo uchunguzi wa magonjwa na wadudu waharibifu wa miti na njia za kuyazuia; kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wadau mbalimbali juu ya matumizi ya teknolojia bora/mpya ya miti/misitu, hifadhi ya udongo, wanyama na mimea; na kuhamasisha uhifadhi wa misitu, kutoa ushauri wa kitaalamu na kuongeza uzalishaji, uuzaji, utumiaji na upasuaji wa mbao.

### 2.3.6 Kufanya tathmini ya kubaini Mchango wa Sekta ya Misitu katika Pato Ghafi la Taifa (GDP)

Tathmini ya kubaini Mchango wa Sekta ya Misitu katika Pato Ghafi la Taifa (GDP) ulifanyika kwa kushirikisha watalaam kutoka taasisi za Serikali za: Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Taifa ya Takwimu ( NBS) , Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) Matokeo ya awali yanaonyesha kuwa mchango halisi wa sekta katika pato la Taifa ni asilimia 3.3.

### 2.3.7 Kuanzishwa kwa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki na Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Misitu

Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki(A National Beekeeping Advisory Committee) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Ufugaji Nyuki Na. 15 ya mwaka 2002 kifungu cha 10 (1) na Kamati ya Ushauri wa Misitu (A National Forestry Advisory Committee) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002. Kamati hizi zina jukumu kubwa la kumshauri Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu masuala ya Ufugaji nyuki na Misitu.

### 2.3.8 Kuwezesha uanzishaji wa Jukwaa la Wafugaji Nyuki Tanzania (TABEDO)

Jukwaa la Wafugaji Nyuki Nchini (Tanzania Beekeeping Development Organization- TABEDO) lilianzishwa na kusajiliwa kwa Sheria ya makampuni "Companies act 2002 (cap 2012)" likiwa na cheti cha usajili namba 119226 cha tarehe 3 Agosti, 2015 na miongoni mwa majukumu ya chama hiki ni pamoja na kuwatambua wanachama wake na wafugaji wote waliopo kwenye mnyororo wa thamani ya mazao ya nyuki hapa nchini ambao ni vyama vya ushirika wa wafugaji nyuki, vikundi, mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na mfugaji mmoja mmoja.

### 2.3.9 Kutangaza hifadhi za misitu na nyuki kwenye Gazeti la Serikali

Mpaka sasa zipo hifadhi za Misitu ya asili 465 na hifadhi za nyuki tisa (9) ambazo zimetangazwa kisheria (Gazzetted Bee Reserve), hivyo kuongeza rasilimali za misitu na nyuki pamoja na kuimarisha uhifadhi wa mazingira.

### 2.3.10 Kuendeleza programu za upandaji miti

Katika kuimarisha uoto wa asili na kutunza mazingira, Serikali imeendelea kuzalisha mbegu bora za miti ambazo zinatumika katika mashamba ya Serikali na kuuzwa kwa wananchi, vikundi, taasisi na kampuni binafsi. Aidha, hadi sasa Serikali imeanzisha na inaendelea kuhudumia mashamba ya miti 23 katika maeneo mbalimbali nchini.

**2.3.11 Kuongeka kwa mnyororo wa thamani wa mazao ya ufugaji Nyuki**

Katika kuongeza thamani ya mazao ya ufugaji nyuki, Serikali imeendelea kuanzisha na kuendeleza viwanda vya kuchakata na kufungasha rasilimali za ufugaji nyuki. Hadi sasa vipo viwanda vitano na juhudi zinaendelea za kujenga viwanda vingi zaidi katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, elimu ya ufugaji nyuki pamoja na kuwezesha vikundi mbalimbali katika shughuli za ufugaji nyuki.

**2.3.12 Kuimairika kwa utoaji wa taaluma ya misitu na nyuki nchini**

Katika kutekeleza suala hili, suala imeendelea kuaimarisha vyuo vinavyotoa taalama ya misitu na ufugaji nyuki kwa kuboresha miundombinu na kuwezesha vitendea kazi na watumishi. Hatua hiyo imewezesha vyuo hivyo kuongeza udahili wa wanafunzi na hivyo kuongeza wataalam wa sekta ya misitu na nyuki ambao watoa huduma katika taasisi za umma na binafsi hapa nchini. Aidha, Tanzania ni nchi pekee Afrika ambayo inatota taalamu ya Shahada ya ufugaji nyuki ambayo inatolewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

**2.4 MAMBO YA KALE**

Ndugu wanahabari,
Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanzania bara, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kulinda na kuhifadhi maeneo ya malikale kama kumbukumbu za Taifa, vituo vya elimu na mafunzo; na vivutio vya utalii kwa maendeleo endelevu ya kizazi cha sasa na kijacho. Maeneo ya malikale yanatoa mchango mkubwa katika kukuza utalii wa ndani na Kimataifa. Aidha, maeneo ya malikale yameendelea kujenga uzalendo wa kitaifa kwa wananchi kwa kuwawezesha kutambua na kuenzi historia ya Taifa letu. Mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili ni pamoja na:-

**2.4.1 Kuanzishwa kwa Makumbusho ya Taifa sita (6)**

Katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru, Serikali imeanzisha Vituo sita (6) vya Makumbusho ambavyo ni Kijiji cha Makumbusho-1967, Makumbusho ya Elimu Viumbe-1987, Makumbusho ya Azimio la Arusha-1977, Makumbusho ya Mwl. Julius .K Nyerere – 1999, Makumbusho ya Kumbukizi ya Vita vya Maji Maji-2010 na Makumbusho ya Kumbukumbu za Dkt. Rashid Kawawa- 2017.

**2.4.2 Kufanyika kwa ukarabati wa Jengo la Soko la Watumwa katika Mji Mkongwe wa Mikindani**

Serikali imefanikiwa kufanya ukarabati wa Jengo la Soko la watumwa katika Mji Mkongwe wa Mikindani. Ukarabati wa jengo hilo ni mwanzo wa juhudi za kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya malikale 91 yaliyokasimishwa kwa Makumbusho ya Taifa kwa ajili ya usimamizi, ukarabati na uendelezaji.

**2.4.3 Kuanzishwa kwa Programu ya Siku ya Azimio la Arusha**

Serikali imewezesha programu ya Siku ya Azimio la Arusha-2021, Soko la kazi za Sanaa ya mikono (KijijiSoko)-2021, programu ya Museum Art Explotion (MAE)-2016, programu ya Ngoma za Asili -1997, Tamasha la Siku ya Mtanzania-1994, programu ya kuenzi tamaduni ya Jando na Unyago (Mkole)- 2018.

**2.4.4 Mafanikio mengine katika sekta ndogo ya mambo ya kale ni pamoja na:-**

i. Kutungwa kwa Sheria ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964 na kuandaliwa kwa Sera ya Malikale ya mwaka 2008;
ii. Mradi wa Uboreshaji wa Kituo cha Makumbusho ya Dar es Salaam (2003- 2011) uliozaa Kituo cha Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni ambacho kinatoa huduma mbalimbali zikiwemo huduma za Migahawa, Maabara, Maktaba, Kumbi za Maonesho, Studio, Theatre na Stoo za Uhifadhi wa mikusanyo;
iii. Kuboresha na kuanzisha Makumbusho ya Zamadamu ya Olduvai- Ngorongoro, Rashid Mfaume Kawawa mjini Songea, Mji wa Kihistoria wa Mikindani na Makumbusho ya Mkoa wa Iringa. Aidha, Nyumba ya Kumbukizi ya Makazi ya Mwl. Nyerere iliyopo Magomeni Dar es Salaam imekarabatiwa;
iv. Maeneo ya malikale katika mji wa Kihistoria wa Mikindani na eneo la Zamadamu la Laetoli-Ngorongoro yametangazwa kuwa maeneo ya Kihistoria na Kumbukumbu ya Urithi wa Utamaduni wa Taifa;
v. Kukarabati miundombinu ya vituo saba vya Malikale katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Lindi na Tanga. Vilevile, ukarabati wa majengo tisa ya kihistoria umefanyika katika mikoa hiyo;
vi. Katika kuhimiza urithi wa utamaduni wa mtanzania, Serikali imeanzisha matamasha mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kumbukumbu ya Vita vya Majimaji na Utalii wa Utamaduni, Songea; Tamsha la Kimondo cha Mbozi ambalo hufanyika sambamba na siku ya Vimondo Duniani kila mwaka. Pamoja na manufaa mengine, matamasha haya yamesaidia kupanua wigo wa mazao ya utalii nchini na kujenga umoja wa Kitaifa; na
vii. Katika kuboresha usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya malikale yaliyopo jirani na hifadhi za misitu na wanyamapori, vituo 18 vya Mambo ya Kale vimekasimishwa kwa taasisi za Wizara ili kuviendeleza na kuvitangaza kama vivutio vya utalii sambamba na maeneo ya hifadhi za asili.

**3. HITIMISHO**

Maliasili, malikale na utalii ni miongoni mwa sekta za uchumi nchini ambazo zinatoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa na kuendeleza ustawi wa maisha ya wananchi kupitia ajira, chakula, tiba na vifaa vya ujenzi. Aidha, sekta hii inatoa malighafi za viwanda vya kuchakata ngozi, kutengeneza mapambo na kusindika nyamapori na kujenga umoja wa Kitaifa. Hivyo, sekta hii ikisimamiwa ipasavyo itaoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi hususan katika miaka mengine ijayo.




MAFANIKIO NA MAENDELEO YA OFISI YA RAIS - TAMISEMI

KATIKA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA

## 1.0 UTANGULIZI

Ndugu Wanahabari Nchi yetu ilipata Uhuru Tarehe 09.12.1961 ambapo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyekuwa Waziri Mkuu wa kwanza aliunda Wizara ya Serikali za Mitaa na Kumteua Mheshimiwa Job Lusinde kuwa Waziri wa kwanza kuongoza Wizara hii. Akifuatiwa na Mawaziri 19 ikijumuisha wanawake wanne (4) akiwemo Waziri wa sasa Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu.

Tangu mwaka 1961 hadi sasa Ofisi ya Rais –TAMISEMI imekuwa ama inajitegemea yenyewe au kuwekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu au kwenye Ofisi ya Rais kama ilivyo sasa. Uamuzi wa wapi inawekwa umekuwa ukifanyika ili kuimarisha utendaji wa Ofisi hii.

Ofisi ya Rais TAMISEMI ni Wizara pekee ambayo Makao Makuu yake yalianzia Jijini Dodoma tangu mwaka 1973 pale Serikali ilipotangaza Makao Makuu ya Serikali kuwa ni Dodoma. Uwepo wa Makao Makuu Dodoma ulikua na lengo la kutoa fursa kwa wananchi na kwa wadau wake wakuu hususan Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufika Dodoma kwa urahisi wanapofuata huduma mbalimbali.

Madhumuni ya kuwepo kwa Serikali za Mitaa ni kupeleka Madaraka kwa Wananchi (D by D) ambapo chimbuko lake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika Sura ya 8, Ibara ya 145 na 146. Lengo ni kuimarisha madaraka kwa wananchi na kuwashirikisha katika kufanya maamuzi.

Wakati Nchi yetu inapata uhuru wake kulikuwa na majimbo nane ya Utawala ambayo yaliritihiwa toka utawala wa kikoloni wa Kiingereza mwaka 1966. Majimbo haya ni Jimbo la Kati, Jimbo la Mashariki, Jimbo la Ziwa, Jimbo la Kaskazini, Jimno la Nyanda za Juu Kusini, Jimbo la Tanga, Jimbo la Magharibi na Jimbo la Ziwa Magharibi. Rais wa kwanza Hayati Julius Kambarage Nyerere kwa Mamlaka aliyopewa aliunda Mikoa 15 na kuondoa utaratibu wa mgawanyo wa nchi katika Majimbo. Mikoa ya mwanzo ni Arusha, Pwani, Dodoma. Tanga, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga, Singida na Tabora.

Mnamo mwaka 1972 Serikali ilifuta Mamlaka hizi na kuanzisha mfumo wa Madaraka Mikoani. Mfumo huu ulizifanya Serikali za Mitaa kuitegemea Serikali Kuu kwa kila jambo kutokana na wananchi kutoshiriki katika maamuzi na pia katika shughuli za maendeleo. Kutokana na hali hii, Mamlaka za Miji zilirejeshwa mwaka 1978 na mamlaka za wilaya zilirejeshwa mwaka 1984.

## 2.0 MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Kwa sasa Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais - TAMISEMI) yapo kwa Hati ya Rais ya Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara iliyotolewa tarehe 07 Mei, 2021. Ofisi hii inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Hati ya Rais ya Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Ofisi ya Rais - TAMISEMI ina Idara kumi na moja (11) na Vitengo sita (6) na inasimamia Taasisi Saba (7) ambazo ni Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Shirika la Elimu Kibaha, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Shirika la Masoko ya Kariakoo na Tume ya Utumishi wa Walimu.

Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI inasimamia utekelezaji wa Sera mbalimbali za Kisekta na Sheria ya Tawala za Mikoa Sura 97, Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji Sura 288. Katika kutekeleza majukumu hayo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ina Mpango Mkakati unaoiongoza katika kutekeleza majukumu yake. Mpango huo una Dira na Dhima zifuatazo: -

### 2.1 Dira

Kuwa na Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye uwezo wa kuboresha huduma kwa wananchi.

### 2.2 Dhima

Kuratibu, kuwezesha na kusimamia Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi kwa kutoa Sera, Miongozo na maelekezo ili kuwepo na huduma zilizo boreshwa.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS TAMISEMI, MAFANIKIO YALIYOPATIKANA TOKA UHURU HADI SASA

Toka kuanzishwa kwake, Wizara hii inayosimamia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepata mafanikio mbalimbali. Katika muktadha huu nitajikita katika maeneo makubwa matano ambayo ni:-

- Kuimarisha utawala bora na kugatua madaraka kwa wananchi
- Kuimarisha Elimu Msingi na Sekondari
- Kuboresha utoaji wa Huduma za AfyaMsingi
- Kuimarisha Miundombinu ya Barabara na;
- Kuwawezesha wananchi kiuchumi

### 3.1 Utawala Bora na Ugatuaji wa madaraka kwa wananchi

i. Ongezeko la maeneo ya kiutawala

Katika kuimarisha ugatuaji wa madaraka kwa wananchi Serikali imekuwa ikiongeza maeneo ya kiutawala ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Hadi Sasa Nchi yetu ina Mikoa 26 kutoka Mikoa 15 iliyokuwepo baada ya uhuru, Baada ya uhuru Halmashauri zilikuwa 45 na hadi kufikia mwaka 2009 zilikuwa Halmashauri 129 na zimeendelea kuongezeka hadi kufikia 184 mwaka 2021.

Wakati wa Uhuru hakukuwa na Halmashauri za Majiji, hivi sasa kuna Halmashauri za Majiji 6, kulikuwa na Halmashauri ya Manispaa moja ya Dares Salaam na sasa kuna Halmashauri za Manispaa 20, Halmashauri za Miji zilikuwa 9 na sasa Halmashauri za Miji ni 21 na Halmashauri za Wilaya zilikuwa 10 na sasa zipo Halmashauri za Wilaya 137.

Aidha, hadi mwaka 2010 tulikuwa na Kata 3,952, Vijiji 10,351, Mitaa 2,650, Vitongoji 55,914. Hivi sasa kuna Tarafa 570, Kata 3,956, Vijiji 12,318, Vitongoji 64,361 na Mitaa 4,263.

Hatua hii inaimarisha utoaji wa huduma za kijamii na kiiutawala kwa wananchi.

ii. Ushamirishaji wa Demokrasia na ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo

Tangu Serikali za Mitaa zilivyorejeshwa mwaka 1982 chaguzi katika ngazi ya Kata, Vijiji na Mitaa na Vitongoji zimefanyika kuanzia mwaka 1983, 1988 na 1994. Kwa chaguzi zilizofanyika mwaka 1994, 1999, 2004, 2009, 2014, 2019 hazikujumuisha Chaguzi za Madiwani kwa kuwa kuanzia mwaka 1994 Chaguzi za Madiwani zilianza kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa sababu ya kuwepo kwa mfumo wa vyama vingi vilivyoanza mwaka 1992.

Aidha kumekuwa na Mwamko mkubwa wa Wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo ikiwemo kuibua miradi yao na hivyo wakati mwingine kuzidi kasi ya Serikali katika kukamilisha miradi katika maeneo mbalimbali. Mfano hadi kufikia June 2021, kuna maboma ya Zahanati 2,378 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Kwa upande wa sekta ya Elimu wananchi wameanzisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 10,300 katika Halmashauri mbalimbali na kati ya hayo Serikali ikatoa fedha ya tozo ya mawasiliano sh. bilioni 7 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 560.

iii. Uimarishaji wa Serikali za Mitaa

Kwa lengo la kuziimarisha Serikali za Mitaa na kuziwezesha kutoa huduma bora kwa wananchi, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali. Mojawapo ya hatua hizi ni kuanzishwa kwa Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ulioanzishwa mwaka 1998 ambao ulilenga katika kupeleka madaraka kwa Wananchi (D by D). Sambamba na hilo, Serikali ilitoa Tamko la Kisera la Ugatuaji wa Madaraka kama njia muafaka ya kufikisha na kuharakisha maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi na kuinua utoaji wa huduma kwa wananchi.

Dhana hii imejengwa kwa misingi ya kutoka kwenye mfumo wa Madaraka ya Serikali Kuu kuwa na maamuzi yote, na Serikali za Mitaa kuwa Mtekelezaji tu (yaani Mwagizaji na Mtekelezaji) kwenda katika mfumo wa Serikali za Mitaa wenye Mamlaka ya Kisheria ya kuamua mambo katika eneo lao na kuyatekeleza. Hivyo, kuwa na mfumo wa mahusiano ya majadiliano katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Ugatuaji wa Madaraka kwa wananchi unalenga kuzipatia Mamlaka za Mitaa uhuru wa kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu utoaji wa huduma kwa wananchi walio katika Mamlaka zao na kuwashirikisha katika kujiletea maendeleo na ustawi wao. Aidha, Tawala za Mikoa zimepewa mamlaka ya kusimamia na kuratibu shughuli mbalimbali za maendeleo ya kijamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora na endelevu kwa wananchi.

vi. Usimamizi wa Rasilimali Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru Halmashauri zimepiga hatua ya ongezeko la mapato ya ndani. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2010/11 makisio ya mapato ya ndani yalikuwa shilingi 175,084,789,727. Makusanyo halisi yalikuwa shilingi 158,279,374,601 sawa na asilimia 90.4. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Halmashauri zilikasimiwa kukusanya shilingi 814,960,990,077 na makusanyo halisi ni shilingi 757,054,979,113 sawa na asilimia 93. Katika kipindi cha miaka kumi makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani yaliongezeka kutoka shilingi 175,084,789,727 mwaka wa fedha 2010/11 hadi shilingi 814,960,990,077 kwa mwaka wa fedha 2020/21. Ongezeko hilo ni Shilingi 639,876,200,350 sawa na asilimia 365.46. Aidha, makusanyo ya mapato ya ndani katika kipindi hicho yaliongezeka kutoka shilingi 158,279,374,601 mwaka 2010/11 hadi shilingi 757,054,979,113 mwaka 2020/21. Ongezeko hilo ni shilingi 598,775,604,512 sawa na asilimia 378.30. Mafanikio ya makusanyo ya mapato ya ndani yametokana na Serikali kuimarisha usimamizi wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki.

.2 Sekta ya Elimumsingi

Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kipindi cha miaka sitini iliyopita imefanya maboresho mbalimbali katika Elimumsingi. Lengo mojawapo la maboresho hayo ni kuongeza upatikanaji, ubora na usawa katika elimu.

Elimu Kabla ya Uhuru hadi 1961

Katika kipindi hiki Elimu ilitolewa kwa watu wachache kwa lengo la kupata maafisa wachache ambao wanaweza kusaidia katika shughuli mbalimbali za utawala na kuandaa watu kwa ajili ya kushika uongozi wa nchi. Hadi mwaka 1961, kulikuwa na Shule za Msingi 3,270 zilizokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 450,626. Shule hizo ziligawanywa kwa matabaka ya rangi ambapo kati ya Waafrika 9,869,000 wanafunzi 431,056 walipata nafasi ya kusoma katika shule 3,115 na kati ya wananchi Wasio Wafrika 150,000 wanafunzi 19,570 walipata nafasi ya kusoma katika shule 155.

Kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuiwa na Serikali kuanzia Uhuru hadi sasa mafanikio makubwa yaliyopatikana ni pamoja na:-

i. Idadi ya shule za Msingi za Serikali zimeongezeka kutoka 3,270 mwaka 1961 hadi 16,656 mwaka 2021. Aidha, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi 486,470 mwaka 1961 hadi 10,687,593 mwaka 2021. Walimu wameongezeka kutoka 9,885 mwaka 1961 hadi 171,993 mwaka 2021.

ii. Shule za Sekondari zimeongezeka kutoka 39 mwaka 1961 hadi 4,002 za Serikali mwaka 2021. Aidha, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi kutoka 11,832 mwaka 1961 hadi 2,379,945 mwaka 2021. Walimu wameongezeka kutoka 764 mwaka 1961 hadi 87,992 mwaka 2021.

iii. Shule za Elimu Maalum zimeongezeka kutoka nne (4) za wamisionari (Tabora, Buigiri, Irente na Uhuru Mchanganyiko mwaka 1961 hadi kufikia 746 mwaka 2021. Aidha, kuna Elimu Jumuishi katika shule zote za msingi. Idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum imeongezeka kutoka 1,000 mwaka 1960 hadi 70,265 mwaka 2021.

iv. Utoaji wa Elimumsingi bila Malipo unazingatia Ibara ya 3.1.5. ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na Ibara ya 52(a) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

Kiasi cha shilingi bilioni 23.8 zinatolewa kila mwezi kuanzia mwezi Disemba, 2015 kwa ajili ya kugharamia utoaji wa Mpango wa Elimumsingi bila Ada na shilingi bilioni 3.0 zinapokelewa Baraza la Taifa la Mitihani kwa ajili ya shughuli za Mitihani. Aidha, kuanzia mwezi Oktoba 2021 Serikali imepeleka Shilingi bilioni 26.00 kwa ajili ya uendeshaji wa Shule za Msingi na Sekondari nchini.

Kuanzia Disemba, 2015 mpaka sasa Serikali imepeleka jumla ya Shilingi trilioni 1.43. kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Elimumsingi bila Malipo. Fedha hizi zimekuwa zikipelekwa katika shule moja kwa moja na kuwafikia wanufaika.

Mpango wa Elimumsingi bila malipo umesaidia kuongeza uandikishaji wa wanafunzi kutokana na kuondolewa kwa vikwazo. Katika mwaka 2016 jumla ya wananfunzi 3,335,637 waliandikishwa, kati ya hao wanafunzi 1,013,310 wa elimu ya awali, 1,896,584 wa darasa la kwanza na wanafunzi 425,743 wa kidato cha kwanza. Mwaka 2021 jumla ya wananfunzi 3,469,275 waliandikishwa, kati ya hao wanafunzi 1,198,564 wa elimu ya awali, 1,549,279 wa darasa la kwanza na wanafunzi 721,432 wa kidato cha kwanza.

### 3.3 Sekta ya Afya

Mwaka 1961, kulikuwa na Vituo vya kutolea huduma za Afya 1,343 vilivyokuwa na idadi ya vitanda 18,832 nchini. Serikali za Mitaa ilikuwa inamiliki Vituo vya Afya na Zahanati 737 pekee zenye vitanda 1,795. Watumishi wa kada mbalimbali za Afya walikuwa 3,172 kati yao Madaktari walikuwa 580, Madaktari wa Meno 30, Wasaidizi Madaktari wa Meno 19, Wafamasia 50,Wasaidizi Wafamasia 38, Tabibu 402, Wauguzi 1,999, Wateknolojia Maabara 3, Wasaidizi Maabara 49 na Wataalam wa Mionzi 2. Aidha mwaka 1961 watumishi waliofuzu Shahada ya Udaktari walikuwa 400 kati yao Watanzania wakiwa 20 pekee.

**Mafanikio**

i. Zahanati na vituo vya afya vimeongezeka kutoka 737 mwaka 1961 hadi 5,696 (Vituo vya afya 630 na zahanati 5,066) vya Serikali za Mitaa.

ii. Hospitali zinazotoa huduma zimefikia 142 mwaka 2021 wakati Serikali za Mitaa hazikuwa na hospitali mwaka 1961.

iii. Vituo vya Afya vinavyotoa huduma za upasuaji zimeongezeka kufikia 415 wakati hapakua na kituo kinachotoa huduma za upasuaji mwaka 1961.

### 3.4 Sekta ya Miundombinu ya Barabara

#### 3.4.1 Miundombinu ya Barabara zinazosimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Wakati wa Uhuru mtandao wa barabara ulikuwa na jumla ya kilometa 33,600 zilizojumuisha kilometa 16,000 zilizokuwa zikitambuliwa kama Barabara Kuu za Nchi na za Kawaida (Territorial Main and Local Main Roads) na kilometa 17,600 zikiwa ni Barabara za Wilaya (District Roads).

Hata hivyo mwaka 2006, kulifanyika zoezi la kuhakiki wa hali ya barabara nchini zilizochini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Local Government Roads Inventory and Condition Survey - LG-RICS). Katika zoezi hili barabara zilizoainishwa na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali na kuingizwa kwenye Sheria ya Barabara namba 13 ya 2007 zilikuwa na urefu wa kilomita 56,625. Mtandao huu ulihuishwa na kufikia barabara zenye urefu wa kilomita 108,946 ambazo zilihamishiwa chini ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijini (TARURA) pale ilipoanzishwa mwezi Julai, 2017.
Mwaka wa fedha 2019/20, zoezi la kuhakiki upya mtandao wa barabara zilizo chini ya TARURA lilifanyika na barabara zilizobainishwa na kuchapishwa kwenye gazeti la Serikali zina urefu wa kilomita 144,429.77 ambapo kati ya hizo barabara zenye hali nzuri na Wastani ni 53.37 na barabara zilizo katika hali mbaya ni wastani wa 46.63.

Mtandao wa barabara za wilaya umeongezeka kwa urefu wa kilomita 126,829.77 kutoka kilometa 17,600 zilizokuwepo mwaka 1961 hadi kufikia kilometa 144,429.77 mwaka 2021
Kulinganishwa na takwimu zilizochukuliwa 2006, mtandao wa barabara za lami umeongezeka kutoka kilomita 1,325 hadi kilomita 2,404.90 ikiwa ni ongezeko la kilometa 1,079.41 sawa na asilimia 81.47. na Mtandando wa barabara za changarawe Kumekuwepo na ongezeko la barabara za Changarawe kutoka kilometa 22,088.79 hadi kilometa 29,166.57 sawa na ongezeko la kilometa 7,077.78 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 32.04. Kuongezeka kwa urefu wa mtandao wa barabara na kuongezeka kwa barabara za lami na changarawe ni kiashiria cha maendeleo katika nchi kwani barabara ni kichocheo cha

maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Madaraja yameongezeka kutoka 2,960 mwaka 2006 hadi kufikia madaraja 3,191 na makalvati yameongezeka kutoka 67,992 hadi 69,317.

Kumekuwepo na ongezeko la bajeti ya ujenzi na matengenezo ya barabara kutoka Shilingi bilioni 94.020 katika mwaka wa fedha 2011/12 hadi Shilingi Bilioni 966.90 katika mwaka wa fedha wa 2021/22.

Serikali iliunda Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini – TARURA ulianzishwa na kuanza kazi rasmi tarehe 01 Julai, 2017. Maeneo mengine ni kuanzishwa kwa TARURA ambayo kazi yake mahususi ni kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara na madaraja, ambapo imejengewa uwezo kwa kupatiwa Wataalam na Vitendea Kazi ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2021/22, kila Halmashauri itakuwa na gari la usimamizi.

**3.4.2 Miundombinu ya Usafiri wa Umma Mijini**

Kabla ya kuwasilisha mafanikio ya sekta hii, naomba kufanya marejeo kwa ufupi sana kuhusu sekta ya usafiri wa umma mijini. Sekta hii ilianza kupewa kipaumbele hata kabla ya uhuru wetu, ambapo mwaka 1949 Serikali ya Mkoloni iliunda kampuni ya Dar es Salaam Motor Transport (DMT) kwa ajili ya kutoa usafiri wa umma katika Mkoa wa Dar es Salaam. Huduma hii iliendelea hivyo hata baada ya uhuru wetu wa mwaka 1961 chini ya Serikali ya Serikali yetu.

Aidha, kati ya mnamo mwaka 1967 hadi 1970, Serikali ilipanua zaidi wigo kwa kuweka kipaumbele na mpango kabambe kwa ajili ya kuboresha usafiri wa umma kwenye miji yote nchini ambapo awamu hii kampuni ya DMT iligawanywa na kuunda Kampuni mbili za Umma. Kwanza, ni Shrika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) kwa jili ya usafiri wa umma Mkoani Dar es Salaam. Pili, ni Kampuni ya Mabasi ya Taifa (KAMATA) kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri wa umma kutoka na kuingia Mkoani Dar es Salaam kwenda na kurudi Mikoa yote ya Tanzania. Juhudi hizi za Serikali zilichangia kuhakikisha kuna uwepo wa huduma ya usafiri wa mijini. Hata hivyo, kufuatia ongezeko la kasi la uhitaji wa huduma hii, hususani katika Mkoa wa Dar es Saalaam, hata baada ya kuishirikisha sekta binafsi katika ya kipindi cha mwaka 1983 hadi sasa, kwa kuanzia, Serikali ilianzisha Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) hapo mwaka 2007.
Mafanikio

**Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa mradi wa mabasi yaendayo haraka kupitia Wakala wa DART 2007 ni pamoja na:-**

(i) Ujenzi wa barabara maalum kwa ajili ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka kutoka kilomita sifuri (0 km) kipindi tunapata uhuru hadi kufikia kilomita 20.9 mwaka 2016 na ujenzi wa kilomita 23.6 unandelea ukiwa katika ufanisi wa asilimia 38.4 ambapo barabara hii itakamilishwa ifikapo Machi 2023. Aidha, ujenzi wa barabara nyingine za mradi zenye urefu wa kilomita 109.74 upo kweye hatua mbalimbali na ifikapo mwaka 2025 zitakuwa zimekalika kama Ilani ya Uchaguzi ya CCM inavyoelekeza.

(ii) Mradi umepunguza muda wa safari toka masaa matatu kabla ya kuanza mradi hadi wastni wa dakika arobaini na tano (45) kwa safari moja hivyo wananchi kuwezeshwa kuwahi katika shughuli zao za kijamii na kiuchumi zinazoongeza tija kwenye Pato la Taifa.

(iii) Aidha, kumekuwepo na ongezeko la watumiaji wa usafiri wa umma kupitia mradi wa DART ikiwa ni kutoka abiria 76,000 kwa siku wakati mradi ulivyoanza kutoa huduma Mei 2016 hadi kufikia abiria 200,000 kwa siku mwaka 2018 kabla ya kupata changamoto za kiundeshaji n idadi hiyo kushuka hadi wastani wa abira 100,000 kwa siku mwaka 2020 ambapo baada ya maboresho yanayoendelea, hivi sasa wastani wa abria wapatoa 160,000 wanatumia usafiri huu kwa siku.

(iv) Mradi umechochea matumizi ya teknolojia ya kisasa kwenye maendeleo ya sekta ya usafiri wa umma ambapo mradi umetoa fursa kwa Wataalam wetu wa ndani kusanifu na kuujenga Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi na Ukusanyaji Nauli (Automated Fare Collection System-AFCS) unaomilikiwa na Serikali na kwamba mfumo huu utafungamanishwa na Mfumo wa Kuongozea Magari (Intelligent Transport System-ITS) ikiwa ni sehemu ya maboresho endelevu ya huduma hii kwa wananchi waishio mijini.

(v) Kiasi cha Shilini milioni 127.57 kilikusanywa mwaka 2008/09 hadi kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 4.23 mwaka 2019/20 kabla ya kushuka hadi kufikia Shilingi bilioni 3.3 mwaka 2020/21 kama mapato ya yatokanayo na tozo ya kutumia miundombinu ya DART na vyanzo vyanzo vingine. Aidha, tangu mwenzi Agosti 2021, mapato ya Serikali yatokanayo na tozo hiyo yameongezeka kutoka Shilingi milioni 8.1 hadi Shilingi milioni 20.04 kwa siku (ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 147.35). Hivyo, Serikali inategemea kukusanya Shilingi bilioni 11.2 kutokana na tozo hiyo na vyanzo vingine. Vile vile, mradi umechangia mapato mengine ya Serikali kupitia kodi ya Serikali na iyotokana na huduma inayotolewa na kutengeneza ajira ya moja kwa moja kwa watu wapatao 1,051.

(vi) Kuchangia ujenzi wa taswira nzuri ya Tanzania katika duru za Kimataifa ambapo mradi ilitambuliwa na kupata tuzo mbili za Kimataifa. Tuzo ya kwanza ni ile ya Sustainable Transport Award na tuzo ya pili ni ile ya C40 Cities Bloomberg Philanthropies Award zilizotolewa mwaka 2018.

3.4.3 Ujenzi wa Miundombinu ya utoaji huduma kwa jamii

Aidha, kupitia miradi ya kimkakati Serikali imefan

ikiwa kujenga Stendi 19 za mabasi za kisasa, masoko 15, machinjio 5, madampo ya kisasa 8, maeneo ya kupumzikia 4 na maegesho ya malori 4.

**Kuwawezesha Wananchi kiuchumi**
Kwa kutambua umuhimu wa kuwawezesha wananchi kiuchumi hususani wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani zimekuwa zikitoa mikopo kwa vikundi mbalimbali vya kiuchumi. Mwaka 2015/16 jumla ya shilingi bilioni 6.69 zilitolewa kwa ajili ya mikopo kwa vikundi 4,037 vyenye jumla ya watu 40,657 kati yao wanawake ni 24,094, vijana 16,547 na watu wenye ulemavu 16. Mwaka 2020, kiasi cha shilingi bilioni 56.12 zilitolewa kwa ajili ya mikopo kwa vikundi 12,962 vyenye watu 150,477 kati ya hao wanawake ni 96,774, vijana 45,356 na watu wenye ulemavu 8,347. Hivyo kufanya jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 145.83 kutolewa kuanzia mwaka 2015 – 2020 na kunufaisha vikundi 47,309 vyenye watu 490,815 ambapo wanawake ni 318,616, vijana ni 155,781 na watu wenye ulemavu ni 16,418. Mikopo hiyo imechangia kukuza uwekezaji mdogo na mkubwa na kuongeza kipato cha wananchi. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2019/20, mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu inatolewa bila riba.

Kwa mwaka huu wa fedha 2021/22 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepanga kutoa jumla ya shilingi Bilioni 67.6 kama Mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu.

**3.6 Miundombinu ya TEHAMA**
Kuanzia mwaka 1961 mpaka 1999, hakukuwa na matumizi ya mifumo ndani ya Ofisi hii. Maboresho makubwa ya kimiundombinu yalifanyika na kuweza kuunganisha Mikoa yote 26 na Halmashauri zote 184 zilizokuwepo wakati huo kuja sehemu moja (kompyuta kuu). Maboresho haya ya miundombinu yaliongeza ufanisi wa kazi haswa katika mawasiliano na kupunguza gharama hasa za uwasilishajiwa taarifa

i. Kuanzishwa kwa mifumo ya TEHAMA, ambayo imeongeza udhibiti, usimamizi na ukusanyaji wa taarifa mbalimbali za kisekta.
ii. Kupunguza gharama za uendeshaji na muda wa kazi husika.
iii. Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani
iv. Kuongeza ufanisi katika mipango na bajeti za serikali.

**4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA**
Pamoja na mafanikio makubwa, zipo changamoto mbalimbali zilizojitokeza ikiwemo:-

4.1 Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi
i. Wananchi katika maeneo mengi kuhitaji kuongeza maeneo ya Utawala. Mfano uanzishwaji wa Vijiji, Kata, Mitaa na Halmashauri mpya, Wilaya na Mikoa
ii. Kufanyika kwa chaguzi kwa wakati tofauti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Madiwani, Vijiji, Mitaa na Vitongoji.

iii. Mamlaka za Serikali za Mitaa kutegemea fedha kutoka Serikali Kuu kwa zaidi ya wastani wa asilimia 88; na
iv. Ushirikwaji mdogo wa wananchi katika kupanga vipaumbele vyao vya , maendeleo.
v. Uwezo mdogo wa baadhi ya Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato
vi. Baadhi ya halmashauri kushindwa kuandaa maandiko ya miradi( mfano miradi ya kimkakati)
vii. Kuendelea kuajiri wataalam wa fani mbalimbali katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kuwajengea uwezo wataalam waliopo.
viii. Kuimarisha Tawala za Mikoa ili ziweze kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake
ix. Kukamilisha miundombinu ya maeneo mapya ya utawala.
x. Halmashauri kuhakikisha zinakusanya mapato ya kutosha ili ziweze kujitegemea
xi. Halmashauri zinazokusanya mapato ya ndani yasiyolindwa zaidi ya Shilingi bilioni 5 zihakikishe zinachangia asilimia 10 ya mapato hayo kwa ajili ya miundombinu ya barabara.
xii. Halmashauri zinazokusanya mapato ya ndani yasiyolindwa pungufu ya Shilingi bilioni 1 zihakikishe zinaongeza vyanzo vipya vya mapato ili kupunguza utegemezi na
xiii. Kuendelea kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza udhibiti wa matumizi na kuhakikisha matumizi yanafanywa kwenye shughuli zenye tija kwa wananchi

**Mwelekeo**
i. Serikali kuangalia uwezekano wa kufanya chaguzi wa Serikali za Mitaa kufanyika kwa wakati mmoja. Mwezi huu Novemba 2021 Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI walikutana kujadili namna bora ya kufanya ucjhaguzi huu kwa wakati mmoja.
ii. Serikali kuendelea kuratibu uanzishaji wa maeneo ya Utawala ili kufikia lengo la kusogeza huduma kwa Wananchi ikiwemo kufungua miundombinu ya barabara, umeme, maji na huduma nyignine;

iii. Kuimarisha ukusanyaji wa Mapato katika mamlaka za Serikali za Mitaa na kudhibiti Matumizi ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato. Aidha, Halmashauri zinasaidiwa na kujengewa uwezo ili kuongeza wigo na kubuni vyanzo vipya vya mapato; na

iv. Kuhakikisha Halmashauri ambazo zinakusanya zaidi ya bilioni 5 kwa mwaka wajitegemea katika kutoa huduma za jamii badala ya kusubiri Ruzuku ya Serikali kuu. Aidha kwa Halmashauri ambazo zinakusanya juu ya bilioni 1 na chini ya bilioni 4 zikusanye lengo la bilioni 4 na kuendelea ili kuweza kutoa

huduma za bora kwa wananchi. Vilevile Halmashauri zinazokusanya chini ya bilioni 1 kuongeza jitiahada ili kukusanya bilioni 1 hadi bilioni 4.

v. Serikali kuendelea kuunga mkono jitihada za wananchi katika miradi waliyoiibua. Mfano mwaka wa fedha 2020/21 tumetoa fedha kiasi cha shilingi milioni 50 kwa kila Zahanati iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi ambapo jumla ya 566 zinaendele kujengwa.

vi. Serikali imeandaa Miongozo ya Mfumo wa Fursa na Vikwazo ulioboreshwa ili kuwasaidia Wananchi kupanga na kuwa na vipaumbele vinavyotekelezeka pamoja na kupata rasilimali kutoka kwa wadau mbalimbali zilizo juu ya uwezo wao.

**4.2 Elimu Msingi**

i. Upungufu wa miundombinu katika baadhi ya shule za msingi na sekondari kutokana na ongezeko kubwa la uandikishwaji wa wanafunzi wa elimu ya awali,msingi na sekondari.
ii. Upungufu wa walimu wa elimu ya awali, maalum,msingi na sekondari hasa katika masomo ya sayansi, tehama na English
iii. Mtawanyo wa makazi ya wananchi unaosababisha wanafunzi kutembea umbali mrefu
iv. Upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
v. Kuibuka kwa tabia kwa baadhi ya shule za msingi na sekondari kulazimisha wanafunzi kuendelea na masomo ya muda wa ziada ikiwemo wakati wa likizo

**Mwelekeo**

i. Kujenga na kukarabati miundombinu ya shule kongwe za msingi na sekondari. Kipaumbele kitakuwa ni kuboresha miundombinu ya shule kongwe za Msingi zilizoazishwa kabla ya Uhuru.
ii. Kujenga shule mpya 1,000 za sekondari katika kata zisizokuwa na shule na ambazo zina msongamano mkubwa wa wanafunzi. Na katika hatua hii wiki iliyopita tumepeka kiasi cha shilingi bilioni 109.9 kujenga shule 234 za Kata katika Majimbo yote 214 na shule 20 kwenye Halmashauri ambazo zina shule zenye uwiano mkubwa wa wanafunzi darasani. Kila shule itagharimu shilingi milioni 600, ambapo awamu wa kwanza tumeleka shilingi milioni 470 kwa kila shule. Nitumie fursa kueleza kuwa fedha hizi zitumike kuanza ujenzio wa madarasa 8, vyumba vya maabara ya masomo ya sayansi 3 na matundu ya vyoo.
iii. Kujenga shule mpya 26 za wasichana kwa ajili ya masomo ya sayansi. Shule 1 katika kila Mkoa. Na katika hatua hii wiki iliyopita tumepeleka kiasi cha shilingi bilioni 30 kuanza kujenga shule 10 za wasichana za masomo ya sayansi katika mikoa 10 ya Dar es salaam, Kagera, Lindi, pwani, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Songwe, Tanga na Mwanza ambapo kila shule itagharimu shilingi milioni 600 , Ninaelekeza Wakuu wa Mikoa kuanza michakato ya ujenzi wa shule mara moja na kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizotolewa.
iv. Kuajiri Walimu wa elimu ya awali, msingi na sekondari ili kukidhi mahitaji yaliyopo.
v. Kujenga shule mpya za msingi ili kupunguza msongamano wa wanafunzi kwenye shule zenye wanafunzi Zaidi ya 2000 ili kuwa na wastani wa wanafunzi wasiozidi 1000 katika kila shule ya msingi.

vi. Kuboresha miundombinu ya madarasa ya elimu ya awali.
vii. Kujenga mabweni katika shule za msingi na sekondari ili kuwahudumia wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu na hatarishi na wenye mahitaji maalum.
viii. Kuratibu utendaji wa Walimu na kuhimiza mahudhurio ya wanafunzi ili kuweza kukamilisha Kalenda ya masomo kwaa mwaka.

**4.3 Huduma za Afya ya Msingi**

Pamoja kazi kubwa iliyofanyika ya kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za Afya ya Msingi, bado OR-TAMISEMI inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Kuwepo kwa Vituo vya Afya na Zahanati zenye miundombinu chakavu ya majengo.
ii. Uchache wa Zahanati na Vituo vya Afya katika Halmashauri mbalimbali.Kwa mfano kuna Zahanati 5,066 dhidi ya Vijiji 12,319 vilivyopo. Kwa upande wa vituo vya afya vilivyopo ni 630 dhidi ya kata 3,956 zilizopo
iii. Upungufu wa watumishi wa kada za afya kwa ngazi zote za Afya ya Msingi ambao unaathiri utoaji wa huduma bora za Afya kwa Wananchi.
iv. Uhaba wa nyumba za watumishi na miundombinu ya nishati na maji safi katika Vituo vya kutolea huduma za Afya.
v. Uhaba wa vifaa na vifaa tiba

**Mwelekeo**

i. Ujenzi na ukamilishaji wa zahanati kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma za afya. Na katika hili tutazingatia vigezo vinne ambayo ni Idadi ya watu, Jografia ya eneo husika, umbali kutoka kituo jirani na makao makuu ya halmshauri na mzigo wa magonjwa. Ujenzi wa vituo vya 481 unaendelea ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya 221 vilivyoanza kujengwa katika Tarafa na kata za kimkakati kwa kutumia fedha za miamala ya simu kiasi cha shilingi bilioni 55.2 zimeshapeleka katika Kata husika ambapo kila Kituo kimepelekewa milioni 250.
ii. Kuendelea kuboresha Miundombinu chakavu katika Vituo vya kutolea huduma za afya vya zamani.
iii. Ujenzi na ukamilishaji wa Hospitali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
iv. Kujenga nyumba za watumishi.
v. Serikali kuendelea kuajiri watumishi na kushirikiana na wadau katika kutoa ajira za Mikataba kwenye maeneo mahsusi ili kusaidia utoaji wa huduma za Afya
vi. Kuboresha upatikanaji wa vifaa tiba bora kwenye Vituo vyote vya kutolea huduma za Afya-

**4.4 Miundombinu ya barabara**

**Changamoto**

- Mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa

112,858.3 sawa na asilimia 78.14 ni barabara za udongo hivyo zinaharibika mara kwa mara hususan kipindi cha mvua

**Mwelekeo**

- Kuongeza mtandao wa barabara za udongo kuwa za changarawe. Serikali kwa kipindi cha 2021/22 hadi 2025/26 imepanga kuongeza barabara za changarawe kutoka kilometa 29,116.57 hadi kufikia kilometa 102,358.1. mpango huu unakadiriwa kutumia shilingi trillion 2.974 kwa kipindi cha miaka 5, na katika hatua hii tunamshukur Rais Samia kwa kuongeza bajeti ya Tarura kutoka shilingi bilioni 271 mwaka wa fehda 2020/21 hadi kufikia bilioni 966.9 mwaka wa fedha 2021/22.

Aidha Serikali kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021/22 hadi 2025/26 imepanga kuongeza madaraja toka 2,812 hadi 6,620 sawa 135% ambapo fedha zitakazotumika kwenye mpango huu zinakadiriwa kuwa Shilingi trilioni 2.974.

**Changamoto na Fursa Kuhusu Usafiri wa Umma Mijini**

(i) Kukosekana kwa mfumo thabiti wa kitaasisi wenye mamlaka ya kisheria ya kupanga, kusimamia, kuendesha, kuratibu, kutekeleza na kufuatilia usafiri wa umma mijini.

(ii) Kuchelewa kwa upatikanaji wa watoa huduma kamili kwenye mfumo wa DART awamu ya kwanza.

(iii) Kuchukua muda mrefu kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya barabara ya mabasi yaendayo haraka.

(iv) Fursa ya uwepo wa ongezeko kubwa la watumiaji wa huduma bora ya usafiri wa umma kwa Mkoa wa Dar es Salaam na hata miji mingine ya Tanzania, mfano mahitaji ya usafiri wa umma na miundombinu bora ya watembea kwa miguu ni asilimia 84 (Dar es Salaam), asilimia 80 (Dodoma), asilimia 90 (Mwanza), asilimia 70 (Arusha), asilimia 87 (Tanga), na asilimia 70 kwa Mkoa wa Mbeya. Pia, kuna fursa ya uhitaji wa maeneo nadhifu kwa ajili ya shuguli za biashara na huduma za jamii.

**Mwelekeo**

(i) Kutunga Sheria mahususi ya kuboresha usafiri wa umma kwenye miji yote ya Tanzania kupitia miundombinu na huduma zilizoratibiwa, na kufungamanishwa ili kuhakikisha kuwa miundombinu na huduma hizo ni zenye ufanisi na endelevu kwenye nyanja za kiuchumi, kijamii, na afya ya watu na mazingira.

(ii) Kuanzisha utaratibu wa kukuza na kutekeleza uratibu na ufungamanishi wa huduma bora ya usafiri wa umma mijini ikiwa ni pamona na kutenga na kueneleza maeneo maalum kwa ajiri ya wafanyabiashara, wakiwemo wafanyabishara wadogo, na maeneo ya wazi ya umma (public spaces).

(iii) Kuongeza mabasi idadi ya mbasi kwa awamu ya kwanza kutoka 210 yaliyopo sasa hadi 305 ifikapo Julai 2022 kwa awamu ya kwanza, na kuleta mabasi yapatayo 755 kwa ajili ya kutoa huduma kwenye awamu ya pili ifikapo Machi 2023. Aidha, kuanza maadalizi ya kuongeza mabasi kwenye awamu nyingine hadi kufikia kiasi cha mabasi yapatayo 3,650 yanayohitaji kwa awamu zote ifikapo mwaka 2025.

(iv) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya mradi yenye jumla ya kilometa 109.74 ifikapo mwaka 2025, hii ikiwa ni kwa awamu zote sita kwa Mkoa wa Dar es Salaam sambamba kuanza kwenda kwenye miji mara baada ya maboresho ya kufanyika kwa sheria.

(v) Kukamilisha ujenzi na usimikaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya Nauli ulifungamanishwa na Mfumo wa Kuongoza Magari (ITS) ifikapo Julai 2022, ikiwa ni sehemu endelevu ya maboresho ya huduma ya usafiri wa umma mijini.

(vi) Kuongeza wigo wa vyanzo wa mapato yasiyotokana na nauli kwa kuwekeza kwenye fursa fungamanishi na huduma za usafiri wa umma kwa lengo kuwa na huduma endelevu ya usafiri wa umma mijini.

**4.5 Uwezeshaji wananchi kiuchumi**

i. Baadhi ya vikundi kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati
ii. Uhitaji wa mikopo kutolewa katika vikundi vya kuanzia watu 5.
iii. Baadhi ya Halmashauri kushindwa kutenga fedha zinazotosheleza mahitaji ya mikopo ya vikundi
Mwelekeo
i. Kuweka utaratibu mzuri wa utakaowezesha vikundi vilivyokopeshwa kurejesha fedha kwa wakati.
ii. Kusimamia kanuni ya utoaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu ili kuruhusu hata mlemavu mmoja mmoja kupata mkopo.
iii. Kuweka utaratibu utakaowezesha idad ya wanakikundi kupungua kutoka watu watano hadi watatu, na kwa upande wa watu wenye ulemavu kuhakikisha mikopo inatolewa kwa mtu mmoja mmoja.
iv. Kuweka mifumo thabiti ya kuimarisha ukusanyaji na utoaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake,vijana na watu wenye ulemava

**4.6 Tehama**

Uchakavu na upungufu wa miundombinu ya TEHAMA katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Upungufu wa Wataalam na vitendea kazi vya TEHAMA.

Baadhi ya Halmashauri kutokuwa na mtandao imara wa intaneti.

Mwelekeo

i. Kuendelea kuajiri na kuwajengea uwezo watumishi waliopo katika fani za TEHAMA
ii. Ununuzi wa vifaa na vitendea kazi vya TEHAMA

iii. Kuhimiza na kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA

**5.0 HITIMISHO**

Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kutekeleza Sera na Mikakati ya kuwapatia huduma bora wananchi kupitia Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo 2021/22-2025/26 pamoja na kutekeleza Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020.

Mafanikio ya utekelezaji yametokana na kazi kubwa inayofanywa na viongozi wenzangu wa Ofisi ya Rais- TAMISEMI ambao ni mheshimiwa David Silinde (Mb) Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI na Festo Dugange (Mb) Naibu Waziri anayeshughulikia Afya. Napenda kutambua kazi kubwa inayofanywa na Katibu Mkuu Prof Riziki Shemdoe akisaidiwa na Naibu Makatibu Wakuu Gerald Mweli anayeshughulikia Elimu na Dkt. Grace Magembe anayeshughulikia Afya.

Vilevile, nawashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI, Wakurugenzi wa Halmashauri na watumishi wote kwa namna walivyotimiza wajibu wao katika kutekeleza majukumu yao.

Aidha, Ofisi ya Rais TAMISEMI inawashukuru wadau wanaowezesha utekelezaji wa miradi na program mbalimbali za maendeleo wakiwemo sekta binafsi, mashirika ya dini, wadau wa maendeleo na wananchi waliochangia nguvu kazi katika utekelezaji wa miradi.

Katika kipindi hiki Ofisi ya Rais TAMISEMI itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo, Wizara ya Kisekta Binafsi, mashirika ya dini na wananchi wote katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Napenda kusisitiza viongozi na watendaji kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ifikapo mwaka 2025.

**MWELEKEO**

i. Halmashauri zinazokusanya mapato ya ndani yasiyolindwa Zaidi ya shilingi bilioni 5 kutenga asilimia 10 kwa ajili ya miundombinu ya barabara. Aidha serikali itaendelea kutafuta vyanzo vingine vya mapato kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara
ii. Kuendelea kuajiri wahandisi wa miundombinu ya barabara
iii. Upungufu wa wataalam katika fani mbalimbali
iv. Kuwepo kwa maombi mengi ya uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala bila kukidhi vigezo.


COMPLETE
INDEPENDENCE
1961